# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA NA MASHIRIKA (LAAC) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**OCTOBER, 2023**

**YALIYOMO …………………………………………………………………………….…UKURASA**


**SEHEMU YA KWANZA……………………………………………………………….……..1**

**UTANGULIZI…………………………………………………………………………………..1**

**SEHEMU YA PILI…………………………………………………………………………...4**

**MAUDHUI YA RIPOTI…………………………………………………………….…….....4**

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI NA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021……………………………………………4**

**SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)……………………………………………….4**

**BENKI YA WATU WA ZANZIBAR……………………………………………………...…40**

**BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)……………………………………………..……66**

**MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)……………………………..….126**

**MFUKO WA BARABARA ZANZIBAR (ZRF)…………………………………….…….193**

**WIZARA YA UJENZI. MAWASILIANO NA UCHUKUZI ZANZIBAR…………….203**

**KAMPUNI YA UUNGANISHAJI NA USAMBAZAJI MAUDHUI (ZMUX)……..224**

**MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)…………………………………………… 231**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZAMAJI NA NISHATI (ZURA)…...289**

**MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA)………………………..301**

**MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI………………………………………………...316**

**MAMLAKA YA UHIFADHI WA MJI MKONGWE ZANZIBAR……………………337**

**MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR…..349**

**MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI…………………………..358**

**CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)……………………………….369**

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA)……………………………………………… 384

CHUO CHA KIISLAM ZANZIBAR……………………………………………………………393

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA
MADAWA YA KULEVYA…………………………………………………………………….401

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021……………………408

BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR…………………………………………………………….408

BARAZA LA MANISPAA MJINI…………………………………………………………...415

BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI "A"……………………………………………...446

BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI "B"…………………………………………475

BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE……………………………………………………...511

BARAZA LA MJI MKOANI………………………………………………………………...527

BARAZA LA MJI WETE…………………………………………………………………...539

BARAZA LA MJI WILAYA YA KASKAZINI 'A' UNGUJA……………………………550

BARAZA LA MJI WILAYA YA KASKAZINI "B"…………………………………………...566.

BARAZA LA MJI WILAYA YA KATI UNGUJA……………………………………….....580

HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA………………………………....594

HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI………………………………………601

UKAGUZI MAALUM WA MAPATO YATOKANAYO NA MINADA YA SAMAKI NA MAZAO YA BAHARINI "MADIKO" PEMBA…………………………………………...609

BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE……………………………………………………. 609

HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI……………………………………………614

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2022…………………………………………620**

**MRADI WA UJENZI WA DAHALIA YA WANAUME KATIKA SKULI YA SEKONDARI MOH'D JUMA PINDUA – PEMBA……………………………………………………………………………………………..…620**

**MRADI WA UJENZI WA UKUMBI WA MIKUTANO WA UMOJA NI NGUVU PEMBA……………………………………………………………………………………………….627**

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MIFUMO YA TEHAMA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021…………………………………………………………642**

**MFUMO WA ECONEX KATIKA BARAZA LA MANISPAA MJINI…………….………642**

**BODI YA MAPATO ZANZIBAR…….……………………………………………………...674**

**BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)……………..………………………..……………700**

**SHIRIKA LA UMEME (ZECO)……………………………………………………………..….722**

**SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR………………………………………………………………746**

**HITIMISHO…………………………………………………………………………..………………771**

# SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ni miongoni mwa Kamati za Kuduma za Baraza ambazo zimeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 85(1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 sambamba na Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020.

Kamati ya ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) ni moja kati ya Kamati za Baraza inayosimamia masuala ya fedha. Hivyo, Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika (LAAC) pamoja na masharti mengine ya yaliyopo Kikanuni hufuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwa kipindi hiki imefanikiwa kufanya ukaguzi wa Ripoti tano zilizowasilishwa katika vipindi tofauti katika Baraza, Ripoti zenyewe ni:

i. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

ii. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi Maalum kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

iii. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka wa fedha 2020/2021.

iv. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

v. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwakawa fedha 2020/2021.

## 1.1 MAJINA YA WAJUMBE NA SEKRETARIETI YA KAMATI

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali ya Mitaa na Mashirika, kwa mwaka huu wa uwasilishaji wa ripoti ya mwaka 2020/2021, inaundwa na Wajumbe 6 na Sekretarieti kama ifuatavyo:

1. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe - Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Bakar Hamad Bakar - Mjumbe
4. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Mjumbe
5. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Mjumbe
6. Mhe. Mohammed Ahmada Salum - Mjumbe

1.1.2 Sekretarieti ya Kamati hii iliongozwa na Makatibu wa Kamati kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi na Maafisa wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sekritarieti yenyewe ni:

1. Ndg. Nasra Awadh Salmin - Katibu
2. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
3. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu
4. Ndg. Rober Laurian Mweiro - Mkurugenzi wa TEHAMA Ofisi ya Mdhibiti
5. Ndg. Shekhe Abdallah Ali - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti
6. Ndg. Maryam Alhaj Juma - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti
7. Ndg. Abdallah Khamis Omar - Afisa wa Ofisi ya Mdhibiti
8. Ndg. Juma Moh’d Juma - Afisa TEHAMA Ofisi ya Mdhibiti.

## 1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Kamati imefanya kazi kwa mujibu wa masharti yaliyoelezwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020. Vile vile, Kamati hii ilizingatia matakwa ya Kanuni ya Kudumu inayoitaka Kamati kujipangia kazi zake baada ya kushauriana na Spika pamoja na kujipangia utaratibu mzuri wa kutekeleza

majukumu yake. Katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali Kamati ilijipangia kukutana na Watendaji wa Serikali za Mitaa, Mamlaka za Serikali na Mashirika yanayojitegemea yaliyopo Unguja, Pemba na kufanya ziara huko Dar - es – Salaam katika Eneo la Makurunge liliopo Bagamoyo pamoja na Kufanya ziara ya kimafunzo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Vile vile, Kamati ya LAAC ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kufanya ukaguzi ili kushuhudia uhalisia na usahihi wa maelezo yaliyowasilishwa na watendaji hao. Ukaguzi huo ulifanyika kwa mizunguko miwili tofauti kama ifuatavyo:

**Mzunguko wa Kwanza**: Tarehe 17 Julai, 2023 hadi tarehe 31 Julai, 2023.

**Mzunguko wa Pili:** Tarehe 07 Agosti, 2023 hadi tarehe 27 Agosti, 2023.

## SEHEMU YA PILI

## RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI NA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021

### 5.1.1 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)

Ukaguzi wa hesabu uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umebainisha taarifa ya michango ya vyanzo vya mapato vya Shirika la Umeme Zanzibar , utendaji wa mwaka kwa kila chanzo cha mapato katika Shirika la Umeme Zanzibar pamoja na kubainisha dosari za kiutendaji zilizojitokeza wakati wa ukaguzi na kubainisha njia za utatuzi wa dosari hizo.

**Ufanisi katika Uendeshaji wa Shirika (Operating Performance)**

Katika ukaguzi uliofanyika umeweza kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa shirika kwa kufanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2020/2021mambo yafuatayo yamebainika.

Ukaguzi umebaini mapato ya Shirika la Umeme Zanzibar yameongezeka kutoka shilingi 33,579,832,829 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia shilingi 34,344,039,918 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na ongezeko la shilingi 764,207,089 sawa na asilimia 2. Aidha, ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi kufikia shilingi 18,172,842,539 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukilinganisha na shilingi 13,716,567,850 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ni ongezeko la shilingi 4,456,274,689 sawa na asilimia 32.5.

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Shirika la Umeme limepata faida ya shilingi 16,171,197,379 ukilinganisha na faida iliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ni shilingi 19,863,264,979 kukiwa na upungufu wa shilingi 3,692,067,600 sawa na asilimia 19 , faida iliyoonekana hapo ilipatikana kabla ya kulipa ushuru.

Kwa upande wa faida baada ya tozo ya kodi imeonekana kupungua na kufikia shilingi 14,378,564,918 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukilinganisha na faida ya shilingi 16,950,977,857 iliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo imefanya upungufu wa shilingi 2,572,412,939 sawa naasilimia 15.

Ukaguzi umebaini kujitokeza kwa ongezeko kubwa la gharama za uendeshaji ikilinganishwa na mapato na gharama za uendeshaji katika mwaka unaomalizika.

Ukaguzi unapendekeza kwa uongozi wa Shirika la Umeme kufanya tathmini na upembuzi yakinifu wa kuvitambua na kuibua vyanzo vipya vya mapato, na iwapo vyanzo vya mapato havitashughulikiwa ipasavyo na matumizi kutodhibitiwa, shirika linaweza kupata matatizo katika kufikia malengo yakeya uanzishwaji.

**Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha (Financial Performance)**

Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlinganisho wamsimamo wa mtaji (Position of Working Capital) wa Shirika la Umeme kwa muda wa miaka miwiliambapo mambo yafuatayo yamebainika.

umebaini utendaji wa kifedha wa Shirika la Umeme umeimarika na kufikia uwiano wa mtajiwa 2.61:1 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukilinganisha na uwiano wa mtaji wa kifedha 2.27:1 kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kutokana na ongezeko hilo ukaguzi umebaini kuna ongezeko la mwenendo mzuri wa uwiano wa mtaji uliofikia vigezo vinavyotakiwa kiuhasibu wa 2:1 ambapo unaonesha uwezo mzuri wa kifedha wa Shirika kwa muda mfupi.

Kutokana na uchambuzi huo, ukaguzi umeweka alama ya msisitizo kwamba Shirika limefikia kiwangokinachotakiwa hata hivyo, mapitio zaidi yamebaini kuwa fedha nyingi za Shirika zipo mikononi mwa mapokezi hususani katika taasisi za Serikali na mawakala wake kutokana na kutolipwa ankara za umeme takribani asilimia 96 jambo ambalo lina uwezekano wa kuhatarisha kuendelea kwa huduma ya umeme.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuchukuwa jitihada za makusudi

kuhakikisha kuwa madeni ya muda mrefu ya umeme yanayodaiwa kutoka kwa ZAWA pamoja na taasisi/ mashirika mengine ya Serikali yanalipwa kwa nia ya kuboresha ukwasi na mwendelezo wa Shirika.

**5.1.1.1 Kukosekana kwa ushahidi wa mlinganisho kati ya matokeo ya zoezi la uhakiki mali za Shirika na kumbukumbu za vitabu za mali za kudumu za Shirika shilingi 318,866,791,672**

Kifungu cha 8.1(v) (a)-(b) cha kanuni za fedha za ZECO kinasema “Shirika litafanya uhakiki wa mali zinazohamishika mara moja kila mwaka.

Kutokana na zoezi la uhakiki wa mali za kudumu za Shirika uliofanyika mwishoni mwa mwaka ili kubaini pamoja na mambo mengine uwepo wa mali hiyo , hali halisi ya mali hiyo na usahihi wa thamani itakayoripotiwa katika taarifa za fedha kama ilivyoagizwa chini ya kifungu cha 8.1(v) (a)-(b)cha kanuni za fedha za Shirika. Ukaguzi umebaini zoezi la uhakiki wa mali za kudumu lililofanyikahalikuonesha usahihi wa taarifa kwa kukosekana mlinganisho wa matokeo yaliyobainika katika zoezi hilo na kumbukumbu za vitabu za mali za kudumu za Shirika.

Kushindwa Kuoanisha (reconciliation) matokeo halisi ya zoezi la kuhesabu mali za kudumu za Shirika dhidi ya vitabu vilivyorekodiwa mali hizo kunapelekea wakaguzi kushindwa kujiridhisha juu ya usahihi wa mali za Shirika pamoja na uwepo wa mali hizo zenye thamani ya shillingi za kitanzania 318,866,791,672 kama zilivyoripotiwa katika Hesabu za Shirika kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni,2021.

Ukaguzi unapendekeza uongozi wa Shirika la Umeme uhakikishe kwamba mara baada ya zoezi la uhakiki wa mali za Shirika kukamilika, matokeo ya mwisho yaoanishwe na kulinganishwa na rejista ya Mali na Vifaa ili kubaini uwepo wa mali hiyo , hali halisi ya mali hiyo na usahihi wa thamani itakayoripotiwa katika taarifa za fedha.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Shirika la Umeme kwa kufuata kanuni za fedha zilizopo hufanya uhakiki wa mali zake mara moja kila mwaka. Matokeo ya uhakiki huo ndio yanayotumika pamoja na mambo mengine kutayarisha mahesabu ya mwisho wa mwaka (financial statement-katika PPE schedule), Baada ya uhakiki, marekebisho (adjustments) yaliyofanyika katika mfumo wa uwekaji taarifa kwa mwaka 2020/2021 haukukamilika kama ilivyo katika kanuni za fedha. Hata hivyo katika mwaka wa fedha 2021/2022, kazi ya uhakiki wa mali za Shirika ilifanyika na taarifa za matokeo yake ziliwekwa kwa kuzingatia kanuni na taratibu zilizopo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Shirika limekiri kuwepo kwa dosari hii kuliko sabWabiswa na changamoto ya mfumo hata hivyo tayari dosari hiyo imesharekebiswa, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha sera ya mali za kudumu pamoja na mchakato wa uundaji wa vitengo vya kusimamia mali za kudumu za Serikali kwa mujibu wa Sheria ya msajili wa hazina kwa lengo la kusimamiwa ipasavyo mali hizo.

**5.1.1.2 Kasoro zilizobainishwa katika Rejesta ya Mali za Kudumu Katika Mfumowa SAP.W**

Katika ukaguzi wa mali za kudumu imebainika kuwa Shirika inatunza kumbukumbu za mali zake za kudumu (PPE) katika kifurushi cha programu cha SAP. Baada ya uhakiki wa daftari hilo, dosarimbalimbali zimebainika kama ifuatavyo ;

Rejesta haikuonyesha eneo la mali ili kutambulika kwa urahisi kuhusu idara/kitengo ambachomali hiyo ipo.

- Hali halisi ya mali haikuonyeshwa kwenye Daftari la Mali za kudumu kwa urahisi wa utambuzi wa baadhi ya mali zilizotengwa kwa ajili ya kuuzwa/kutupwa na kuondolewa kwenye Daftari.

- Mali zilizo na alama za utambuzi hazikuweza kuoanishwa na kulinganishwa kwenye Daftari. Hii ilisababishwa zaidi na ukosefu wa nambari za kipekee za utambulisho wa mali ili kutofautisha kundi moja la mali na jengine kama vile kompyuta na viti. Hii inaleta ugumu wa kuthibitisha kama mali zote za Shirika zimerekodiwa katika Daftari hilo.
- Kumekuwepo na mawasiliano duni kati ya kitengo kinachohusika na kutunza kumbukumbu za Mali za Kudumu za Shirika (Fixed Assets Section) na Kitengo Kikuu kinachohusika na Utoaji na Usomaji wa Mita kuhusu utambuzi wa vifaa ambavyo hutolewa ghalani kwa ajili ya kazi za ukarabati/matengenezo na vile vya Wateja wapya. Vifaa vya kazi za matengenezo ambavyo ni vya asili ya kudumu vinahitaji kuingizwa kama mali mpya na vya zamani kutolewa katika Daftari la Mali za Kudumu katika mfumo. Kwa hivyo, Daftari la Mali za Kudumu za Shirika katika mfumo wa SAP linaweza kuwa na malimbikizo ya taarifa isiyo sahihi kuhusu gharamahalisi ya mali za kudumu za Shirika.
- Mapitio ya zoezi la kuhesabu mali yalibaini baadhi ya mali ambazo zilitambuliwa kwa madhumuni ya kuzitupa/kuziuza kutokana na uharibifu usioweza kurekebishwa na sababu nyinginezo. Hata hivyo, kutokana na udhaifu wa kushindwa kuoanisha mali zilizo na alama za utambuzi kwenye daftari la Mali za kudumu katika mfumo wa SAP kuna uwezekano mkubwa wa kushindwa kuondoa mali hizo kwenye daftari kwa muda usiojulikana.
- Mfumo wa SAP haukuweza kurekodi wenyewe (automatically) mali za kudumu kutoka ghalani. Badala yake, mali za kudumu zilirekodiwa kwa mikono (manually) baada ya kurekodiwa kwanza katika programu ya excel, zoezi ambalo lilionekana kuwa la kuchosha, linalochukua muda na kuathiriwa na makosa.
- Mfumo wa SAP ulifanya kazi polepole sana wakati wa upakiaji wa faili kwa madhumuni ya kutazama na kusahihisha hifadhidata ya mali (asset database).

Kwa hivyo hutumia muda mwingi kuchapisha na kurejesha data. Baadhi ya taarifa za mali za kudumu hazikuweza kuthibitishwa kwa kuwa taarifa zake hazikufunguka hata kidogo kutokana na kasi ndogo yamfumo wa SAP.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro zilizobainishwa hapo juu taarifa za mali zinazoonyeshwa kwenye Daftari la Mali za kudumu katika mfumo SAP zinatia shaka hivyo basi thamani ya Mali za kudumu iliyoripotiwa katika taarifa za fedha kiasi cha shilingi 318,866,791,672 inatia shaka juu ya usahihi wake.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Shirika kuhakikisha kuwa Daftari la Mali za kudumu katika mfumo wa SAP linatunzwa likiwa na taarifa kamili na sahihi ili kuwezesha utayarishaji wa kumbukumbu sahihi na taarifa za kuaminika kuhusu thamani, uwepo na hali ya Mali.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Kutokana na Settings za sasa, Mfumo wa SAP hauoneshi moja kwa moja Thamani ya Mali na uwepo wa mali katika eneo moja la Daftari la Mali za kudumu badala yake taarifa hizo huonekana katika mfumo kwa kuangalia ripoti maalumu ya mali husika. Baada ya kugundua tatizo hilo, Tayari shirika limeunda kamati maalumu ambayo imeanza kufanyia kazi tatizo hilo na matarijio ni kukamilika kazi hiyo kabla ya Juni 2023. Hata hivyo utayarishaji wa hesabu za mwaka za Shirika unazingatia uhalisia na Shirika linaweka taarifa sahihi za thamani za mali za kudumu katika vitabu vya hesabu

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini ni kweli mfumo wa SAP ulikuwa na Changamoto kadhaa katika utoaji wa taarifa sahihi za mali za Shirika, hata hivyo Shirika limeshaanza kuufanyia marekebisho mfumo huo

Kamati inalishauri Shirika kuharakisha kufanya maboresho ya mfumo wa SAP aidha Shirika kuwa makini katika ununuzi wa Mifumo kwa kubaini uwezo wa mifumo katika

utendaji kazi kama unakidhi haja ya Shughuli zilikusudiwa kufanyika kabla ya kuingia katika mkataba wa manunuzi.

**5.1.1.3 Uchakavu wa Majengo ya Shirika katika vituo vya kuuzia Umeme**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa uchakavu wa Majengo yanayotumiwa kwa shughuli za Shirika katika vituo vya Makunduchi na Gamba, ukaguzi umebaini majengo hayo yalikuwa katika hali isiyoridhisha ambapo yanahitaji ukarabati mkubwa kama vile upakaji wa rangi , uwekaji wa AC, kuezekwa upya, vigae vya sakafuni, mbao za dari, grili za ulinzi kwa watunza fedha na kazi zinazohusiana ili kuyafanya yavutie kwa shughuli za kila siku kwa wafanyakazi.

Kwa upande wa Pemba imebainika kuwa majengo hayo yalikuwa katika hali mbaya sana kwani ni ya zamani na yanafanana na majengo chakavuambapo kwa upande wa Wesha Shirika linamiliki majengo kumi (10) ya makazi ya wafanyakazi wake yalionekana katika hali mbaya sana na chakavu. Maeneo ya dari, madirisha, milango na kadhalika yalikuwa zikining'inia karibu kuanguka. Nyumba nyingi zilikuwa zimeonyesha nyufa kali za ukuta na sehemu za paa zilikuwa karibu kuporomoka. Kwa ujumla, nyumba hizo hazifai kwa makazi ya watu.

Aidha,kwa upande wa Majengo ya kuhifadhia vifaa (ghala) Tibirinzi hayakuwa katika hali nzuri kwani imebainika Ghala kuu katika yadi ya nyuma lilikuwa karibu kuporomoka kutokana na nyufa kubwa za ukuta na kusababisha sehemu ya kuezekea ya jengo kuning'inia kwenye rafu za kuhifadhia vifaa.

Ghala jengine la lazamani la kuhifadhia vitu vilivyochakaa lililotengenezwa kwa bati lilionekana kuwa katika hali mbaya sana ambapo mabati hayo yanakaribia kuporomoka, sehemu ya kuhifadhi nayo ilikuwa haitoshelezi na kugeuzwa kuwa ni nyumba ya wadudu/wanyama hatari kama nyoka, nge n.k. zaidi ya hayo, usalama wa mita zilizopitwa na wakati na vitu vingine vinavyoweza kuuzwa vilivyomo ghalani humo viko hatarini kutumiwa vinginevyo na wafanyakazi wasio waaminifu au

kuibiwa na wahalifu.

Kutokana na kuchakaa kwa majengo hayo kunaweza kukapelekea Shirika kuhatarisha maisha ya watumiaji hasa nyumba za makazi zilizopo Wesha ambazo zinatumiwa na wafanyakazi na familia zao pamoja uwepo wa Mazingira ya ofisi yasiyoridhisha husababisha ufanyaji kazi mdogo na kupunguza ari ya kazi na kupelekea kushuka kwa mapato.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika kuchukua hatua za haraka kukarabati majengo hayo ili yawe katika hali nzuri hasa yale yanayokaliwa na wafanyakazi na familia zao kabla ya kuchelewa ili kuokoa maisha yao.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Shirika linakabiliwa na uchakavu wa baadhi ya majengo yake zikiwemo ofisi, nyumba za wafanyakazi na ghala za kuhifadhiya vifaa. Kwa kuzingatia hilo Shirika lina mpango wa kujenga jengo jipya la ofisi Pemba litakaloondoa tatizo la ofisi kwa wafanyakazi ili kuwa na mazingira mazuri katika kazi zao na kuwezesha kutoa huduma bora kwa wateja. Aidha, kwa upande wa Unguja matengenezo ya ofisi za Makunduchi na Gamba pamoja na nyumba mbili za Shirika yameshakamilika. Hata hivyo, Shirika limepanga kuendelea na kufanya matengenezo ya majengo kadri wa uwezo wa kibajeti utakavyoruhusu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limekiri kuwepo kwa dosari hiyo Kamati inalishauri Shirika kuongeza ufanisi katika makusanyo kwa lengo la kuongeza bajeti katika kushuhulikia majengo ya Shirika aidha kutafuta fursa za mikopo kupitia benki mbalimbali ili kukamilisha ujenzi wa majengo hayo na kurudisha mkopo kupita makusanyo yao ndani.

#### 5.1.1.4 Udhaifu wa udhibiti wa ndani katika Mali za Ghalani na Vifaa vinavyotumika

Ukaguzi umefanya mapitio ya udhibiti wa ndani juu ya mali zilizopo ghalani na zile zinazotumika kila siku ulibaini udhibiti hafifu wa ndani ambapo idara ya uhasibu ilitegemea zaidi kumbukumbu zilizowekwa na kitengo cha watunza ghala kuhusu masuala yote ya ununuzi na utoaji wa vifaa ghalani katika kipindi husika. Hakukuwa na kumbukumbu ambazo zilitunzwa na idara ya uhasibu katika leja kuu (general legder) ambazo zingerikodi manunuzi yote na utoaji wa vifaa ghalani katika mwaka husika kumbukumbu ambazo mwishowe zitahitaji kuoanishwa na kumbukumbu za ghala kwa nia ya kufichua tofauti yoyote baina ya kumbukumbu za idara ya uhasibu na zile za ghala zinazoweza kusababishwa na wizi, usambazaji hafifu, utunzaji mbaya wa kumbukumbu, ununuzi hewa wa vifaa na kadhalika.

Aidha, jukumu la kudhibiti na kulinda mali na vifaa vilivyonunuliwa na kutumika liliachwa chini ya usimamizi wa mtunza ghala na hakukuwa na udhibiti uliokwekwa kutoka upande wa uhasibu (finance department) katika kulinganisha na kuoanisha kumbukumbu za mtunza ghala na za mhasibu.

Kutokana na uwepo wa dosari hizo kunaweza kukapelekea kushindwa kubaini mapungufu ambayo yanaweza kusababishwa na wizi, udokozi, upokeaji wa vifaa hafifu, usambazaji duni, utunzaji mbaya wa kumbukumbu, ununuzi hewa na kadhalika, jambo ambalo ukaguzi umeshindwa kujiridhisha kwamba mali na vifaa vyote vilivyonunuliwa katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi vilipokelewa na kutumiwa kwa manufaa ya Shirika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika kuhakikisha kuwa manunuzi yote na matumizi ya vifaa vya ghalani vinakuwa na viambanisho vyote vya ununuzi na vya kutolea vifaa ghalani. Viambatanisho vyote vinatakiwa kuingizwa kila mwezi kwenye vitabu vya Shirika kwa pande zote za mtunza ghala na uhasibu ambapo ifikapo mwisho wa mwaka kufanyike mlinganisho baina ya kumbukumbu za uhasibu na ghalani na kama

kuna mapungufu yoyote yachunguzwe ili kuboresha udhibiti wa ndani kuhusu utumiaji wa vifaa vya ghalani.Hata hivyo,ni vyema matumizi ya mfumo wa SAP yanapendekezwa zaidi katika suala hili ili kuunganisha kumbukumbu za ghala na za uhasibu.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Shirika kwa sasa limeimarisha udhibiti wa ndani katika mali za ghalani na vifaa kwa kuhakikisha matumizi ya mfumo wa SAP yanaunganisha kumbukumbu za ghala na za uhasibu. Kwa upande wa ghalani kumbukumbu zote zinaendelea kuwekwa kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Shirika limekiri kuwepo kwa dosari hizo na tayari hatua zimeanza kuchukuliwa hata hivyo Kamati inaungana na ushauri uliotolewa na Mkaguzi wa kulitaka Shirika kuhakikisha kuwa manunuzi yote na matumizi ya vifaa vya ghalani vinakuwa na viambanisho vyote vya ununuzi na vya kutolea vifaa ghalani. Viambatanisho vyote vinatakiwa kuingizwa kila mwezi kwenye vitabu vya Shirika kwa pande zote za mtunza ghala na uhasibu.

**5.1.1.5 Kuongezeka kwa Mwenendo wa Madeni ya Umeme ya Serikali**

Katika uhakiki wa madeni ukaguzi umebaini mwenendo wa madeni yanayotokana na mauzo ya umeme yaliyoripotiwa katika kumbukumbu za Shirika katika mwaka unaoishia tarehe 30 Juni,2021 yalikuwa ni kiasi cha shilingi 50,090,055,315. Kati ya hizo madeni ya biashara yaliyoripotiwa ambayo Serikali inadaiwa ni shilingi 47,824,889,329 sawa na asilimia 95.6.
Katika deni hilo ZAWA amebeba kiasi kikubwa ambacho kimetokana na madeni pamoja na malimbikizo ya muda mrefu hadi kufikia kiasi cha shilingi 42,683,072,052 ambapo shilingi 18,154,141,399 ni deni la ZAWA Unguja na shilingi 24,528,930,653 ni deni ZAWA - Pemba, sawa na asilimia 90 ya deni lote la Serikali linalodaiwa na Shirika.

Aidha, katika kupitia kumbukumbu za malipo imebainika kwa muda mrefu Mamlaka ya Maji (ZAWA) haikufanya malipo ya bili zake za Umeme licha ya jitihada mbalimbali zinazofanywa na Shirika kuomba malipo hayo.

Kushindwa kufanya malipo ya bili za Umeme kwa Mamlaka ya Maji (ZAWA) kunaweza kukapelekea mambo yafuatayo kubainika:-

Kushindwa kulipa deni linalowakabili kutokana na deni hilo kuendelea kuwa kubwa siku hadi siku.

Shirika kuendelea kubeba mzigo mkubwa wa malipo ya kodi ya miundombinu ya asilimia 2 na malipo ya kodi ya VAT ya asilimia 15 ambapo malipo hayo yalipaswa kulipwa na Mamlaka ya Maji (ZAWA).

Kukosekana kwa tija ya Shirika kujiendesha kibiashara na hatimae kunaweza kukapelekea shirika hilo kujiendesha kwa huduma (Service Oriented).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kupitia Bodi ya Wakurugenzi kuchukuwa hatua za haraka kutokana na mwenendo usioridhisha wa madeni ya Serikali bila kuchelewa kwa kuwasiliana na Wizara ya Maji, Nishati na Madini ili iingilie kati kutafuta hatima ya madeni ya Serikali ya muda mrefu ambayo yanazidi kuongezeka.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Shirika la Umeme linaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha za matumizi ya umeme ya Taasisi za Serikali kwa kushirikiana na Bodi ya Wakurugenzi na Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Wizara ya Maji, Nishati na Madini iliwasilisha barua kwa kila Taasisi yenye deni kwa lengo la kuzitaka zisawazishe madeni yao.

Miongoni mwa juhudi zinazochukuliwa na Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Uongozi wa Shirika ni kuwasilisha barua kwa Taasisi zote zenye madeni, kufanya vikao na Taasisi hizo pamoja na kuzikatia umeme baadhi ya Taasisi ili kupata malipo ya madeni hayo.

Aidha, juhudi hizo zimepelekea baadhi ya Taasisi kufanya malipo ambapo kwa mwaka mpya wa fedha 2022/2023 Taaisi mbali mbali zimefanya malipo ya jumla ya TZS 2,500,788,794.27 (angalia Kiambatanisho Na. 5.1.1.5)

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini ni kweli Shirika linazidai Taasisi za Serikali Madeni makubwa na hatua za kufuatilia madeni hayo zinachukuliwa kwa kuwakumbusha kwa barua wadaiwa hao lakini bado jitihada zimeshindwa kutatua changamoto iliyopo.

Kamati inaishauri Serikali kutafuta muarubaini wa hili kwa vile madeni makubwa yanatokana na taasisi za Serikali ili waweze kulipa madeni yao na Shirika liweze kujiendesha kibiashara na kuweaa kutoa gawio kwa Serikali ipasavyo.

**5.1.1.6 Deni linalotokana na kuwaungia umeme wateja wapya kwa njia ya mkopo shilingi 1,218,418,442**

Katika ukaguzi uliofanyika Shirika la Umeme liliwasilisha madeni yenye thamani ya shilingi 1,218,418,442 yatokanayo na kuwaungia umeme wateja wapya kwa njia ya mkopo. Ukaguzi haukuweza kuthibitisha uhalali wa deni hilo kutokana na kutokupatiwa orodha halisi ya majina ya wanaodaiwa na kima cha fedha kwa kila mteja aliyeungiwa umeme kwa njia ya mkopo kwa ajili ya uthibitisho wa ukaguzi.

Kukosekana kwa orodha hiyo wakaguzi wameshindwa kujiridhisha juu ya kuwepo, usahihi na urejeshwaji wa mikopo mipya iliyoripotiwa kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.2 katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuunganisha mifumo yake ya kielektroniki (SAP na Suprima) inayotumika ili kuwezesha ufuatiliaji wa mikopo mipya ya wateja waliounganishiwa umeme pamoja na kusimamia mwenendo wa urejeshaji

wa fedha kwa lengo la kupatikana usahihi wa taarifa za madeni ya fedha zinazodaiwa.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Deni linalotokana na kuwaungia umeme wateja wapya kwa njia ya mkopo shilingi 1,218,418,422 tayari limeshalipwa kwa asilimia 55. Aidha, kwa wale ambao hawajakamilisha, madeni yao yamewekwa katika akaunti zao za umeme. Orodha ya wateja hao na madeni yao yaliobaki umeambatanishwa (angalia Kiambatanisho Na. 5.1.1.6).

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imeridhika na majibu ya Shirika hata hivyo Kamati inalishauri Shirika kuwa makini katika utoaji wa mikopo kwa wateja wapya na kufuatilia kwa karibu urejeshwaji wa madeni hayo ili kuepuka Shirika kupata hasara

**5.1.1.7 Kukosekana kwa uthibitisho wa usalama wa ukusanyaji wa Fedha**

Ukaguzi ulifanya ziara katika vituo mbali mbali vya kuuzia umeme na kubaini dosari mbali mbali za kiutendaji ambazo zinaweza zikapelekea upotevu wa fedha za umma kwani imebainika vituo vingi vinakuwa na makusanyo makubwa ya fedha bila ya kupelekwa benki.

Kwa mfano imebainika makusanyo ya fedha kwa siku katika kituo cha Makunduchi makusanyo zaidi ya shilingi milioni nne (Milioni 4), kituo cha Mkokotoni makusanyo zaidi ya shilingi milioni tatu (Milioni 3) na kituo cha Gamba makusanyo zaidi ya shilingi milioni mbili (Milioni 2) kwa siku. Hata hivyo, ushahidi wa kuthibitisha usalama wa kutosha juu ya ukusanyaji wa fedha ulikosekana.

Aidha, kwa upande wa kituo cha Makunduchi ukaguzi ulibaini kituo hicho kinakusanya mapato na kufanya miamala ya kibenki kwa kutumia watunza fedha wao wenyewe tofauti na kituo cha Gamba na Mkokotoni ambao walikuwa wakitumia huduma za wakala wa PBZ ambao walilazimika kutembelea vituo hivyo ili kurahisisha

huduma za kibenki. Hata hivyo, ilibainika kuwa kuna mazingira ambapo kituo cha kuuza umeme cha Makunduchi kinashikilia takriban milioni 10 ambazo zinaweza kuongezeka kutokana na siku za mapumziko ambapo huduma za benki hazipatikani.

Hata hivyo, pamoja na hali iliyobainika bado hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha miamala ya benki hiyo ilifanyika kwa kusindikizwa na polisi au gari badala yake wabeba fedha walitumia pikipiki wakati wa makusanyo ya kila siku ya benki. Ukaguzi ulibaini kwamba ingawa walinzi walipatikana katika kituo cha mauzo cha Makunduchi lakini walikuwa hawana bunduki kwa ajili ya ulinzi katika tukio la wizi au matukio yanayohusiana nayo.

Kutokuwepo kwa ulinzi wa kutosha katika vituo vya mauzo ya umeme kunaliweka Shirika katika hatari ya kupata hasara kutokana na wizi au matumizi mabaya ya fedha.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuhakikisha uwepo wa usalama wa kutosha katika vituo vya uuzaji umeme, kuweka ulinzi wa kutosha wakati wa kupeleka pesa za mauzo benki, pamoja kufunga mitambo maalum ya kubaini wahalifu (CCTV Camera). Hata hivyo ni vyema kwa watunza pesa wote wanaohusika moja kwa moja na ukusanyaji wa pesa taslimu na miamala ya benki wanapaswa kukatiwa bima.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Mpaka kufikia kipindi cha ukaguzi katika Vituo vya kuuzia umeme vya Gamba na Mkokotoni washika fedha wa shirika walikua wakienda kukusanya fedha kila baada ya siku mbili kwa vile fedha zenyewe hazikuwa nyingi. Kwa upande wa kituo cha Makunduchi, washika fedha wa kituo hicho walikuwa na utaratibu wa kuwasilisha makusanyo katika Tawi la PBZ Makunduchi, kutokana na kuwa kituo cha mauzo kiko karibu na Benki.

Hata hivyo, kwa sasa Shirika limeimarisha mfumo wa upelekaji fedha Benki kutoka kwenye vituo vya Gamba na Makunduchi kwa kuwatumia mawakala wa PBZ walioko kwenye maeneo hayo. Aidha, kutokana na mfumo wa malipo Serikalini kubadilika,

malipo yote yataanza kufanyika kwa mfumo wa ZAN Malipo kwa hiyo kadhia hiyo tunatarajia kuondoka karibuni.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Shirika limekiri kuwepo kwa dosari hiyo na hatua zimeshachukuliwa za kuongeza udhibiti na ulinzi katika vituo vya kuuzia umeme hivyo Kamati imeridhika na majibu yaliyotolewa na Shirika. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kukamilisha uwekaji wa mfumo wa Zan Malipo ili kuondoa kadhia hiyo.

**5.1.1.8 Ukosefu wa ushahidi wa kufanya uchambuzi wa faida na gharama kwenye Mauzo ya Umeme kupitia Wakala.**

Ukaguzi umebaini Shirika liliingia kwenye mikataba na watoa huduma watatu kwa ajili ya kuuza umeme kwa njia ya vituo na simu za mkononi kwa malipo ya ujira (commission basis).

Imebainika kwamba Shirika limeendelea na jitihada za kuongeza mauzo ya nishati na kuongeza kiwango cha kuridhisha wateja kupitia matumizi ya mawakala hata hivyo, hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha kuwa uchambuzi wa kina wa faida na gharama ulifanyika hapo awali, ili kujua faida na hasara itokanayo na uuzaji wa umeme kwa kupitia mawakala yaani kulinganisha mapato yanayopatikana dhidi ya malipo ya ujira ya mawakala kwa kulinganisha na gharama za uendeshaji zinazotokana na uuzaji wa umeme kupitia vituo vya Shirika vya mauzo.

Ilitarajiwa kwamba Shirika lingefanya uchambuzi wa gharama zake za uendeshaji wa vituo vya kuuzia umeme kama vile gharama ya mafuta, malipo ya posho ya saa za ziada kwa wafanyakazi wanaofanya kazi saa za usiku, wasindikizaji wa usalama, kodi ya pango kwa baadhi ya vituo vya mauzo na gharama zinazohusiana kwa kulinganisha na faida za kutumia mawakala ambao wataweza kupunguza gharama hizo kwa kiwango kikubwa (kama vile kufunga baadhi ya vituo vya kuuzia umeme au kufanya kazi wakati wa saa za kazi pekee) na kuamua ikiwa inafaa au la kushirikisha wakala.

Kukosekana kwa uchambuzi wa kina wa gharama zinazohusika dhidi ya mapato yatokanayo na matumizi ya mawakala kwa ajili ya uuzaji wa umeme kwa njia ya vituo na simu za mkononi, kama uwezekano wa Shirika kuongeza gharama zake za uendeshaji badala ya kupunguza kama inavyotarajiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika kufanya utafiti wa kina juu ya uchambuzi wa faida na gharama za kuwashirikisha mawakala katika mauzo ya umeme kupitia vituo vya mauzo na simu za mkononi kwa maamuzi zaidi ya Uongozi.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Shirika La Umeme liliamua kutumia wakala wa kuuza umeme kufuatia kuongezeka kwa watumiaji waliosambaa kila kona ya Zanzibar, jambo ambalo lingelilazimu Shirika kuwa na kituo cha kuuza umeme kila Kijiji/eneo ili kuwahudumia wananchi hao kwa ufanisi. Hivyo uamuzi huo ulilenga kutengeneza mazingira rahisi kwa wateja wake kupata huduma hii muhimu kwa vile idadi kubwa ya wananchi wanamiliki simu za mkononi, ambazo zinawawezesha kununua umeme wakati wanapohitaji. Kwa upande mwengine uwepo wa gharama kubwa za uwekezaji na uendeshaji wa vituo vya kuuzia umeme (vending stations) ungelifanya Shirika la Umeme kujenga au kukodi majengo mengi jambo ambalo ni gharama kubwa.

Hivyo, Shirika lilifikia maamuzi ya kuwatumia mawakala kwa kuzingtia zaidi faida zifuatazo:

- Kurahisisha ununuzi wa umeme kwa muda wote na hivyo kuongeza kiwango cha mauzo ya umeme.
- Kuhakikisha usalama wa ukusanyaji wa mapato ya Shirika.
- Kupunguza gharama za uendeshaji wa vituo vya kuuzia umeme.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa Shirika lina nia njema ya kutaka kurahisisha upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wakati na urahisi hasa ukizingatia

ongezeko kubwa la matumizi ya nishati ya umeme katika visiwa vya Zanzibar

Kamati inalishauri Shirika kupitia tena mkataba wake na mawakala hao ili kuuboresha Zaidi na tija iweze kupatika baina ya pande mbili za mkataba

Aidha kamati inaendelea kulishauri Shirika kuwasiliana na uongozi wa Wakala wa Serikali Mtanda E- Government kwa kuangalia namna ya bora kuuza Umeme kwa njia ya Mtandao ili kuepusha hasara kwa kuendelea kuwatumia mawakala hao.

Vile vile Kamati inaishauri Shirika kufanya uchambuzi wa kina ili kujua gharama za mauzo ya umeme na faida inayopatikana kabla ya kuingia katika uwakala.

**5.1.1.9 Ukosefu wa taarifa ya matumizi ya mafuta ya shilingi 173,645,231 ya Gari - Tawi la Pemba**

Katika ukaguzi uliofanyika Shirika liliripoti jumla ya shilingi 173,645,231 ikiwa ni gharama za matumizi ya mafuta kwa mujibu wa kumbukumbu zilizowasilishwa kwa ukaguzi katika tawi la Pemba kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021.

Aidha, ukaguzi haukupatiwa ripoti iliyoonyesha mwenendo wa masafa ya gari pamoja na kiasi cha mafuta kinachotumika kwa kila gari katika mwaka husika jambo ambalo limepelekea ugumu wa ufuatiliaji wa mwenendo wa matumizi ya mafuta kwa kila gari kwa ajili ya kusaidia uongozi wa Shirika kufanya maamuzi sahihi.

Hata hivyo, hakukuwa na kumbukumbu ambazo zilitolewa kwa ajili ya uthibitisho wa ukaguzi ili kuonyesha gharama za matengenezo kwa kila gari la tawi ambapo Ilitarajiwa kwamba kungekuwa na Daftari/kumbukumbu za gharama za matengenezo kwa kila gari la Shirika kuonyesha taarifa kama vile vipuri vilivyonunuliwa, huduma za vipindi (service), n.k. ili kurahisisha ufuatiliaji wa mwenendo wa gharama za matengenezo ya kila gari kwa ajili ya kusaidia maamuzi stahiki kwa uongozi wa Shirika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme katika tawi la Pemba kuhakikisha

unaweka utaratibu wa kuanzisha daftari maalum linalooneshia kumbukumbu za gharama za matengenezo ya gari pamoja na kuandaa ripoti za mara kwa mara za kila mwezi/robo mwaka kuhusiana na matumizi ya mafuta kwa kila gari ili kuweka usimamizi mzuri wa matumizi ya mafuta kwa lengo la kubaini gari yoyote ambayo itakuwa na muelekeo usioridhisha wa matumizi ya mafuta kuweza kuchukuliwa hatua stahiki.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Shirika la Umeme Zanzibar limekuwa na utaratibu wa kuweka kumbukumbu za matumizi ya mafuta na matengenezo ya magari kwa kila siku kupitia mfumo wa logbook. Aidha, mkusanyiko wa taarifa za mafuta zinawekwa pamoja kwenye mfumo wa excel sheet kwa kila mwezi. Vile vile, kwa sasa Shirika limeshaweka mfumo wa kutambua gharama za matumizi ya mafuta na matengenezo kwa kila gari kama ilivyoshauriwa katika kuboresha taarifa hizo kwa mara za kila mwezi/robo mwaka kuhusiana na matumizi ya mafuta kwa kila gari ili kuweka usimamizi mzuri wa matumizi ya mafuta

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na majibu yaliyotolewa na Shirika Kamati iliomba kupatiwa vielelezo hivyo ili kuthibitisha majibu yaliyotolewa mbele ya Kamati, Kamati haikupatiwa vielelezo hivyo.

Kamati inalishauri Shirika wakati inapowasilisha majibu ya hoja wawe na vielelezo vya kuthibitisha uhalali wa majibu wanayoyatoa

Aidha Kamati inaungana na ushauri ulitolewa na Mkaguzi wa kulitaka Shirika kufuata utaratibu kwa mujibu wa sheria katika matumizi ya mafuta pamoja na matengenezo ya gari.

### 5.1.1.10 Tofauti iliyobainika kati ya gharama halisi za matumizi na makadirio ya bajeti

Ukaguzi ulipitia bajeti iliyoandaliwa na Shirika la Umeme katika mwaka ulioshia tarehe 30 Juni 2021 na kubaini tofauti kubwa kati ya gharama halisi za matumizi na makadirio ya bajeti ambapo sababu za utofauti hiyo hazikuweza kupatikana kwa ukaguzi. Hali halisi ya utofauti huo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 13: Tofauti iliyobainika kati ya gharama halisi za matumizi na makadirio ya bajeti**

| Vifunguvya Bajeti | Aina ya Matumizi | Makadirio ya Matumizi 2020/21 (Tshs.) | Matumizi halisi 2020/21 (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) | ilimia(%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 61100 | Personnel | 19,241,045,420.00 | 14,346,911,305.00 | 4,894,134,115.00 | 25.44 |
| 61102 | ZSSF (13%) | 1,302,929,266.00 | 858,062,560.00 | 444,866,706.00 | 34 |
| 61103 | SDL 5% (Salary AndOvertime) | 1,967,114,087.00 | 533,867,221.00 | 1,433,246,866.00 | 73 |
| 61108 | Staff Training | 1,253,640,984.00 | 751,600,181.00 | 502,040,803.00 | 40 |
| 61200 | Utility And Services | 3,239,915,304.00 | 1,448,873,333.00 | 1,791,041,971.00 | 55 |
| 61201 | Grease And Transformer oil | 30,162,600.00 | 5,045,177.00 | 25,117,483.00 | 83 |
| 61202 | Water | 32,200,000.00 | 78,345,573.00 | (46,145,573.00) | (143) |
| 61203 | Electricity | 975,548,796.00 | 617,940,182.00 | 357,608,614.00 | 37 |
| 61205 | Postal | 1,560,000.00 | 2,847,222.00 | (1,287,222.00) | (83) |
| 61207 | News Paper | 8,448,000.00 | 3,521,990.00 | 4,926,010.00 | 58 |
| 61208 | Internet | 191,085,000.00 | 50,992,000.00 | 140,093,000.00 | 73 |
| 61209 | Stationery | 191,275,300.00 | 289,281,288.00 | (98,005,988.00) | (51) |
| 61210 | Sundry Items | 1,295,735,608.00 | - | 1,295,735,608.00 | 100 |
| 61212 | Security Guard | 270,720,000.00 | 148,205,000.00 | 122,515,000.00 | 45 |
| 61213 | Rent | 13,200,000.00 | 29,313,443.00 | (16,113,443.00) | (122) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 61401 | Advertisement | 109,663,000.00 | 71,328,730.50 | 38,334,269.50 | 35 |
| 61500 | Repair And Mainten ance | 10,824,404,533.0 0 | 3,704,474,744.00 | 7,119,929,789.00 | 66 |
| 61501 | Building Repair & Maintenance | 375,000,000.00 | 188,777,239.00 | 186,222,761.00 | 50 |
| 61502 | Furniture & Fitting Repair & Maintenance | 52,550,000.00 | 7,286,000.00 | 45,264,000.00 | 86 |
| 61503 | Plant & Machinery Repair & Maintenance | 290,409,704.00 | 2,740,860.00 | 287,668,844.00 | 99 |
| 61505 | HT & LT Line Repair &Maintenance | 5,815,925,329.00 | 3,507,670,645.00 | 2,308,254,684.00 | 40 |
| 61506 | Transformers & Substations Repair & Maintenance | 4,290,519,500.00 | - | 4,290,519,500.00 | 100 |
| 61600 | Offices Expenses | 1,114,630,000.00 | 742,070,370.00 | 372,559,630.00 | 33 |
| 61601 | Contingencies | 400,000,000.00 | 207,630,006.00 | 192,369,994.00 | 48 |
| 61602 | Insurance And Licences (BuildingAnd Others) | 72,000,000.00 | 35,979,381.60 | 36,020,618.40 | 50 |
| 61603 | "Donation, Sports &Gift " | 157,670,000.00 | 94,710,983.00 | 62,959,017.00 | 40 |
| 61700 | Motor Vehicle & Transport Expenses | 2,113,515,282.00 | 1,144,242,979.00 | 969,272,303.00 | 46 |
| 61703 | Petrol | 381,216,000.00 | 230,288,133.00 | 150,927,867.00 | 40 |
| 61704 | Diesel | 1,229,952,000.00 | 366,061,416.00 | 863,890,584.00 | 70 |
| 61900 | Customer Service Expenses | 3,454,300,000.00 | 1,035,494,859.00 | 2,418,805,141.00 | 70 |
| 61901 | Entertainment | 744,130,000.00 | 449,523,858.00 | 294,606,142.00 | 40 |

Kutokana na jadweli liliopo hapo juu linaonesha kuongezeka na kupungua kwa gharama za matumizi kinyume na makadirio ya bajeti yaliyopangwa na kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi jambo ambalo imebainika gharama za matumizi ya maji kuongezeka kwa asilimia 143, gharama za kodi kuongezeka kwa asilimia 122, gharama za Posta kuongezeka kwa asilimia 83 pamoja na gharama za vifaa vya kuandikia kuongezeka kwa asilimia 51 pamoja na gharama nyenginezo zimebainika kupungua kinyume na makadirio ya bajeti yaliyopangwa na kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi.

Aidha, ukaguzi haukuweza kupatiwa sababu za msingi zinazothibitisha kupanda/kushuka kwa matumizi ya bajeti iliyopangwa kwa lengo la kulishauri Shirika juu ya hatua za haraka za kuchukuwa ili kurekebisha hitilafu hiyo kwa mujibu wa kanuni nambari 2.3 ya Kanuni ya Fedha ya Shirika.

Kwa vile mipango ya matumizi ya bajeti inapopangwa hupitishwa na kukubaliwa na Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme, wakaguzi walitegemea kupatiwa idhini na ridhaa ya Bodi ya Wakurugenzi inayothibitisha matumizi ya ziada yaliyojitokeza kwa mujibu wa kifungu cha 22(2) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Shirika ya mwaka 2006 hadi ukaguzi unakamilika hatukuweza kupata idhini (kibali) kutoka kwa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Umeme iliyoridhia ziada ya matumizi hayo.

Uwepo wa tofauti kubwa ya gharama halisi za matumizi na makadirio ya bajeti iliyobainika kunatia shaka iwapo bajeti iliyotayarishwa ilizingatia takwimu halisi ili bajeti inayoandaliwa itumike kama zana ya kupima utendaji wa kazi za Shirika. Aidha kutokuwepo kwa ushahidi wa kuonyesha kwamba matumizi ya ziada ya bajeti yaliidhinishwa na Bodi kunatia shaka juu ya uhalali na kama matumizi hayo yalifanywa kwa manufaa ya Shirika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuhakikisha kuwa utayarishaji wa bajeti unatokana na takwimu halisi ili kufanya muonekano wa matumizi kuwa na uhalisia kwa manufaa ya Shirika, pindipo inapobainika kujitokeza kwa tofauti ya

matumizi hatua za haraka zichukuliwe ili kuweza kurekebisha dosari hiyo ambapo inapaswa kupata idhini ya matumizi kutoka kwa Bodi ya Wakurugenzi kabla ya kufanya matumizi yoyote.

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Shirika la Umeme lilifanya malipo ya ziada katika kifungu cha maji kutokana na malimbikizo ya madeni ya matumizi ya maji kutoka ZAWA. Aidha, kuhusu malipo ya ziada ya kodi (rent) Shirika lililipa fedha hizo kwa mujibu wa mahitaji ya kila mwaka ambapo bajeti iliyopangwa haikuzingatia vizuri uhalisia.

Kwa upande wa gharama za posta malipo yalihusisha malimbikizo ya fedha zilizolipwa na kushindwa kukamilisha malipo ya miaka mitatu iliyopita kwa sababu ya kufeli kwa control number.

Kwa upande wa kifungu cha vifaa vya kuandikia hii inatokana na matatizo ya Mtandao (SAP settings) kwa sababu matumizi yanajirikodi gharama za vifaa zinazotoka ghalani kwa njia ya good issue na sio yale yaliolipwa kwa muda ule, ambapo baada ya kugundulika kwa tatizo hilo, Shirika limeshafanya mabadiliko katika mfumo wa SAP ambapo kwasasa kila kifungu cha bajeti kimewekewa kikomo cha matumizi kuzuia uwezekano wa kuvuka kiwango kilichowekwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa mfumo wa SAP ulikuwa na dosari kwa kuwa ulishidwa kuweka limit ya matumizi ya vifungu na kupelekea baadhi ya vifungu kutumia Zaidi ya kilichopangwa na kuathiri vifungu vyengine ambavyo vimetumia fedha chache.

Hata hivyo Kamati imeridhika na majibu kwa vile Mfumo wa SAP tayari umeshafanyiwa maboresho na changamoto hiyo imetatuliwa.

#### 5.1.1.11 Kutokudhibiti matumizi ya zaidi ya kikomo cha bajeti kilichowekwa

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa mapitio ya vifungu vilivyowekwa kwenye bajeti na kubaini baadhi ya vifungu vimetumia kiasi chote cha fedha kilichopangwa, na baadhi ya vifungu kutumika zaidi ya makadirio yaliyowekwa, na baadhi ya vifungu kutumika kwa kiasi kidogo kulingana na makadirio yaliyopangwa.

Kwa mujibu wa utaratibu kama kifungu kimevuka kiwango cha bajeti kilichoidhinishwa ilihitajika kufanyika kwa mgawanyo mpya (reallocation) kwa lengo la kudhibiti matumizi zaidi ya kikomo cha bajeti kilichoidhinishwa.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini hapakuwa na udhibiti wowote kuhusu kuzuia mgawanyo mpya wa vifungu vya bajeti pale kifungu kimoja kinapokuwa kimeishiwa fedha kama ilivyobainishwa katika jaribio lililofanywa katika mfumo wa SAP.Aidha,ukaguzi ulibaini kuwa wafanyakazi wa idara ya fedha wanaweza kuhamisha kifungu kimoja cha matumizi kwenda kingine kinachofanana pale inapobainika kifungu kimoja kimemaliza kiwango cha bajeti kilichotengewa ili kutekeleza malipo bila ya idhini ya maofisa wenye dhamana hiyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 5.4.2 cha Muongozo wa Sera na Taratibu za Uhasibu na Fedha za Shirika la Umeme wa mwaka 2013 ambacho kinasema kuwa “matumizi ya ziada yasiyoidhinishwa hayaruhusiwi, hivyo matumizi yoyote ya kupita kiasi yanayotarajiwa lazima yaripotiwe kwa msimamizi husika kwa idhini ya kutumia zaidi kabla ya utekelezaji wa malipo hayo kufanywa”.

Kufanya matumizi kinyume na muongozo wa Sera na Taratibu za Uhasibu na Fedha za Shirika la Umeme kunaweza kusababisha matumizi ya zaidi ya ukomo wa bajeti kwa vifungu husika bila idhini kutoka kwa watu wanaohusika na hivyo kufanya bajeti kutokuwa na maana kama chombo cha kupima utendakazi wa Shirika na kupelekea kushindwa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti dhidi ya matumizi halisi kwa vifungu na hatimae kutoleta taswira sahihi kwa madhumuni ya kufanya maamuzi kwani baadhi ya vifungu vya matumizi vinaweza kuelemewa na matumizi yasiyo ya

tabaka hilo ili kuweka bajeti yenye uwiano.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuhakikisha kuwa uhamishaji/ugawaji mpya wa vifungu vya bajeti utakaofanywa unafuatiliwa na kuidhinishwa kupitia mfumo wa SAP ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa utekelezaji wa bajeti dhidi ya matumizi halisi.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Shirika limeimarisha udhibiti wa matumizi ya zaidi ya kikomo cha bajeti kilichowekwa na kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi.  Katika kuongeza msisitizo juu ya suala hilo, kwa kutumia mfumo wa SAP Shirika limeweka kizuwizi (limit) juu ya matumizi ya ziada ya bajeti kwa kila kifungu ambacho hakijapatiwa idhini.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa mfumo wa SAP ulikuwa na dosari kibajeti kwa vile ulishidwa kuzuia matumizi ya vifungu ambavyo vimeshafikia ukomo wa matumizi na kupelekea baadhi ya vifungu kutumia Zaidi ya kilicho idhinishwa bila ya ridhaa ya Bodi, hata hivyo Kamati imebaini hakukuwa na ongezo la Bajeti isipokuwa baadhi ya vifungu viliathirika kimatumizi kwa vile fedha zilizopangwa zimetumika katika vifungu ambavyo vilizidi bajeti ya matumizi yaliyopangiwa.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limesharekebisha dosari hiyo na sasa mfumo unaweka kuzuwizi (limit) juu ya matumizi ya ziada kwa kila kifungu Kamati inalishauri Shirika kuhakikisha linafuatilia  uwezo wa mifumo kiutendaji na kuifanyia majaribio kabla ya kukabidhiwa ili kubaini dosari na kuzichukulia hatua za haraka kabla ya mkandarasi kuondoka.

**5.1.1.12 Mchakato wa muda mrefu wa zabuni unaosababishwa na matatizo ya Idara ya Watumiaji**

Katika ukaguzi uliofanyika wa mapitio ya michakato ya zabuni kwa Shirika katika kipindi cha ukaguzi imebainika uwepo wa mwenendo wa ucheleweshwaji wa zabuni kwa baadhi ya zabuni kulikosababishwa na kurudiwa kwa mchakato wa zabuni/matangazo mapya ambapo baadhi ya zabuni hizo zilionekana kufutwa kutokana na mahitaji ya watumiaji yasiyofahamika yaliyowasilishwa na idara za watumiaji (users) kwenye kitengo kinachohusika na masuala ya ugavi kwa ajili ya kutekeleza mpango wa manunuzi wa mwaka.

Mahitaji ya mtumiaji ambayo yalionekana kuwa hayaeleweki ni pamoja na kushindwa kubainisha kiasi halisi, ubora na maelezo ya bidhaa/huduma inayohitajika katika kipindi fulani kitendo ambacho mwishowe kiliathiri kiasi cha fedha kilichopangwa awali kwa ajili ya utekelezaji wa manunuzi hayo kwa zaidi ya bei zisizo halisi na kusababisha kutangazwa tena au kufutwa kwa zabuni.Baadhi ya zabuni zilizotekelezwa na ambazo zilikuwa na hitilafu zinazohusika zimebainishwa katika jadweli lifuatalo:-

Kushindwa kufafanua mahitaji ya mtumiaji ipasavyo na idara za watumiaji wakati wa hatua za awali za utayarishaji wa mpango wa ununuzi wa kila mwaka husababisha utekelezaji usiofaa wa mpango kwa gharama kubwa (yaani, muda uliotumika kwenye zabuni, gharama za matangazo, posho kwa wajumbe wa bodi ya zabuni na wajumbe wa kamati ya tathmini, gharama za vifaa vya kuandikia na kadhalika).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuhakikisha kuwa idara za watumiaji zinawasiliana na kusaidia Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Uuzaji wakati wote wa mchakato wa manunuzi au uuzaji hadi kufikia hatua ya kuingia mikataba kwa kuandaa mahitaji yao mapema kabla ya kuingizwa katika mpango wa mwaka wa manunuzi ili kuepusha mchakato wa manunuzi ambao unaweza kuchukua muda mrefu na kupelekea upotevu wa fedha za Shirika kutokana na utangazaji upya wa zabuni na taratibu za tathmini zisizo za lazima.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Shirika limeboresha utaratibu wa matayarisho ya zabuni kwa kuwapatia mafunzo wakuu wa Idara zote na Vitengo ili kuhakikisha kwamba wakati wa utayarishaji wa mpango wa manununzi kila idara na vitengo vinawasilisha kwa ukamilifu na kwa wakati taarifa zote zinazohitajika kwa ajili ya manunuzi ya vifaa husika ikiwemo vigezo vya kiufundi (specifications), uhalisia wa bidhaa inayohitajika, muda wa upatikanaji, n.k.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imeelezwa kuwa sababu kuu ya kufanyika hayo ni ukosofu wa taaluma kwa watendaji wake katika kuaanda mchakato wa zabuni jambo ambalo limepelekea kutokea kwa dosari hizo hata hivyo kwa sasa Shirika limeshachukua hatua kwa kuwapatia mafunzo watendaji wake ili kuboresha utaratibu wa matayarisho ya zabuni.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Shirika kuwa makini wakati wa utayarishaji wa mchakato wa zabuni ili kukidhi vigezo ikiwemo vigezo vya kiufundi (specifications), uhalisia wa bidhaa inayohitajika na kuwasilisha mahitaji yao mapema kabla ya kuingizwa katika mpango wa mwaka wa manunuzi ili kuepusha mchakato wa manunuzi ambao unaweza kuchukua muda mrefu na kupelekea upotevu wa fedha za Shirika kutokana na utangazaji upya wa zabuni na taratibu za tathmini zisizo za lazima.

**5.1.1.13 Hatima isiyojulikana ya mchakato wa zabuni ya ujenzi wa Ofisi ya Shirika la Umeme Zanzibar itakayojengwa Chake Chake Pemba.**

Mchakato wa zabuni ya ujenzi wa ofisi ya ZECO Pemba (Chake Chake) ulianza tarehe 31 Agosti, 2020 (kupitishwa na bodi ya zabuni kwa kazi itakayofanyika) na ulikoma katika hatua ya utoaji wa tuzo tarehe 14 Mei, 2021 ambapo bodi ya zabuni ilimjulisha Afisa Masuuli juu ya uamuzi wake wa utoaji wa zabuni iliyoidhinishwa tarehe 29 Aprili, 2021 katika kikao cha 18 ambapo Mzabuni M/s Quality Building Contractors

(QBC) aliidhinishwa kwa ajili ya kazi hiyo kwa kiasi cha shilingi 5,489,662,486.

Ukaguzi umebaini kuwa taratibu zilizobaki za utoaji zabuni (hatua ya kusaini mkataba) hazikuendelea kwa takribani miezi 8 sasa na hakuna maelezo yakinifu yaliyotolewa kwa madhumuni ya ukaguzi ili kuhalalisha hali iliyobainika licha ya kwamba Ofisi ya Pemba kwa sasa imekuwa na nafasi ndogo ukilinganisha na idadi ya wafanyakazi wake na uchakavu wa majengo ya ghala ambayo yako katika hali mbaya.

Utekelezaji wa mchakato wa utoaji zabuni bila kumalizia matokeo yanayotarajiwa hufanya mchakato mzima kutokuwa na maana, unaotumia muda mwingi na kusababisha gharama kubwa, jambo ambalo huleta usumbufu kwa wazabuni walioshiriki katika zabuni na huenda wakaachwa gizani kuhusu matokeo ya zabuni na kuwapa mawazo hasi ambayo yanaweza kuathiri vibaya mtazamo wa ZECO mbele ya umma kuhusu mchakato wa utoaji zabuni.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuhakikisha kwamba shughuli zote za manunuzi zinatekelezwa ipasavyo kulingana na mpango uliowekwa ili kuepuka upotevu wa fedha za Shirika unaosababishwa na kusitishwa kwa zabuni pamoja na kulipa uzito tatizo la ubovu wa jengo la ofisi na mazingira mengine ya kazi ambayo yako katika hali mbaya katika tawi la Pemba na kuharakisha mchakato wa utoaji zabuni.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Shirika lilisitisha Mchakato wa zabuni ya ujenzi wa ofisi ya ZECO Pemba (Chake Chake) kutokana kutokuwa na fedha za kutosha za ujenzi wa jengo hilo katika bajeti ya mwaka 2020-2021. Hata hivyo, Shirika liliamua kutafuta mkopo kutoka benki za PBZ, CRDB na NBC ili kuwezesha ujenzi kufanyika kwakutumia fedha za mkopo kuliko kutumia fedha za ndani. Hivyo Shirika linaendelea na hatua mbali mbali za ujenzi katika mwaka wa Fedha 2023/2024. Kwa sasa, Shirika lipo katika hatua ya mazungumzo na mshauri elekezi (ZBA) kwa hatua za ujenzi wa jengo hilo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kuchunguza hoja hii imebaini kuwa Shirika lilipanga kutekeleza mradi huu kutoka vyanzo vyake vya mapato, hata hivyo maamuzi hayo yalitenguliwa baada kuongezeka mahitaji ya matumizi ya Shirika na kuamua mradi huo utekelezwe kwa fedha za mkopo kupitia Benki watakayokubaliana kukopa fedha hizo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Shirika kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi kujua chanzo cha uhakika cha upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa mradi huo ili kunusuru mradi kutotekelezeka kwa sababu ya ukosefu wa fedha na kusababisha gharama za mradi kuongezeka kutokana na kuchukua muda mrefu wa utekelezaji.

Aidha Kamati inakitanga Kitengo cha Mipango cha Shirika la Umeme kuhakikisha kinatoa mashirikiano makubwa katika upangaji na utekelezaji wa shughuli zote za Bajeti ya Shirika ili kuepuka kufanya kazi kwa mazoea.

**5.1.1.14 Ukosefu wa timu ya usimamizi wa mikataba kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Mikataba**

Kanuni ya 83 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2020 inaitaka "Taasisi ya Ununuzi na Usambazaji mali itawajibika kwa usimamizi bora wa mkataba wa manunuzi yoyote ya bidhaa, huduma na kazi".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika hapakuwa na ushahidi wa kuthibitisha kwamba Shirika liliunda timu ya usimamizi wa mikataba ili kusimamia utekelezaji bora wa kandarasi zote zilizotolewa katika mwaka wa ukaguzi. Hali hii imepelekea kukosekana kwa ushahidi wa utekelezaji wa ufanisi wa kandarasi zilizotolewa katika mwaka wa ukaguzi kama inavyobainika katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 15: Mikataba iliyokosa ripoti za utekelezaji**

| Aina ya Mkataba | Makubalianoya Alieingia Mkataba | Tarehe ya makubaliano | Thamani ya Mkataba (Tshs.) | Thamaniya Mkataba (USD) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa kituo cha Mauzio ya Umeme Mazizini | ZECO vs. ZENJI BUILDING | 12.04.2021 | 38,534,080 (VAT inclusive) | | Ripoti za utekelezaji kutoka kwa timu ya usimamizi wa kandarasi au idara ya watumiaji kuhusu kazi iliyotekelezwa pia zilikosekana. |
| Usambazaji wa Mita za umeme (lot 1, 4, 5 na 7) | ZECO vs. GENUS POWER INFRASTRUCTURELTD | 01.06.2020 | | (Lot 1, 580,470), (lot 4, 6,480), (lot 5,15,120) and (lot 7, 11,700) | Kwa mujibu wa mkataba bidhaa hizo zilipaswa kuwasilishwasi zaidi ya siku 90 tangu tarehe ya mkataba kuanza kutumika (01.06.2020). Haikuwa dhahiri kama bidhaa ziliwasilishwa ndani ya muda uliopangwa kama ilivyokubaliwa. |
| Supply of High Tension and Low Tension under Framework Lot 1, 2, 6 and 8 | ZECO vs. VISI-WANI GENERAL SUPPLIERS | 18.06.2021 | 2,476,864,150 | | Utekelezaji wa mkataba haukuonekana. |
| Supply of single phase split type AMR Compatible Meter – lot 2 | ZECO VS. WASION GROUP | 06.08.2020 | | 72,292.5 | Kwa mujibu wa mkataba bidhaa hizo zilipaswa kuwasilishwa si zaidi ya siku 90 tangu tarehe ya |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mkataba kuanza kutumika (01.06.2020). Utekelezaji wa mkataba haukuonekana. |
| construction of Trench Covers at Mtoni Old Switch Yard | ZECO vs. YASSIN & SONS | 22.04.2021 | 32,200,000 | | Ripoti za utekelezaji kutoka kwa timu ya usimamizi wa kandarasi au idara ya watumiaji kuhusu kazi iliyote- kelezwa zilikosekana. |
| Security Ser- vices at Mtoni | ZECO vs. KMKM | 01.01.2021 | 194,400,000 (kwa muda wa miaka mitatu) | | Kukosekana kwa Ripoti ya utendaji ya mtoa huduma. |

Kushindwa kufuatilia utekelezaji wa mikataba kunaweza kusababisha upotevu wa fedha za Shirika kutokana na kutofanya kazi vizuri kwa wazabuni kinyume na kanuni na masharti yaliyoainishwa kwenye mikataba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuhakikisha kwamba unafuatilia utekelezaji wa mikataba kwa ukaribu kupitia uundaji wa timu ya usimamizi wa mikataba ambayo itasimamia vigezo na masharti yote ya vipengele yaliyoainishwa ndani ya mikataba na kuchukua hatua za haraka endapo kutakuwa na utekelezaji mbaya wa mkandarasi.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Utaratibu wa Shirika juu ya kusimamia mikataba umeimarishwa kwa kuhakikisha kila mkataba unaosainiwa unawekewa msimamizi (contract manager) ili kuhakikisha ufuatiliaji wa uendeshaji wa mikataba hiyo unafanyika ili kuleta tija inayotarajiwa.

Aidha katika bajeti ya mwaka 2022/2023 Shirika limetenga bajeti na kuwapa mafunzo zaidi wasimamizi wa mikataba (contract managers) pamoja na wafanyakazi wa kitengo cha manunuzi wanaohusika na mikataba.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini Shirika halikuwa na timu ya usimamizi wa mikataba kwa mujibu wa Kanuni ya 83 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2020, kukosekana timu ya usimamizi wa mikataba huenda ikapelekea mradi kutekelezwa kwa viwango tofauti na makubaliano katika mkataba.

Kamati inalishauri Shirika kufuata kanuni ya 83 ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2020 ili mikataba ya miradi ya shirika isimamiwe vyema na iweze kutekelezwa ipasavyo ili thamani ya fedha ilingane na hali halisi ya matokeo ya mradi.

**5.1.1.15 Makosa yaliyoainishwa katika Mikataba ya Uuzaji wa Umeme kupitia Vituo ya Uuzaji na Simu za Mkononi.**

Ilibainika kuwa Shirika limeshirikisha watoa huduma watatu (3) kwa ajili ya uuzaji umeme kwa njia ya vituo vya mauzo na simu za mkononi ambapo taratibu zake za manunuzi zilianza mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo kukamilika na utekelezaji wa mikataba hiyo umefanyika katika mwaka 2021/2022 kama ilivyoonyeshwa hapa chini;

- ZECO na CRDB uliingiwa tarehe 10.09.2021 kwa muda wa miaka miwili unaoishia tarehe 10.09.2023 kwa ujira wa asilimia 2.
- ZECO na PBZ uliingiwa tarehe 11.08.2021 kwa muda wa miaka miwili unaoishia tarehe 11.08.2023 kwa ujira wa asilimia 2.
- ZECO na ZANTEL uliingiwa tarehe 01.09.2021 kwa muda wa miaka miwili unaoishia tarehe 01.09.2023 kwa ujira wa asilimia 2.
- Kutokana na mapitio ya mikataba hiyo dosari zifuatazo zimebainika:-
- Tofauti katika Msingi wa malipo ya Ujira (commission payments)

Ilibainika kuwa ingawa watoa huduma wote watatu waliotajwa hapo juu walikuwa

wakitoa huduma sawa hata hivyo misingi ya malipo ya ujira ilitofautiana. Ukaguzi umebaini kuwa PBZ na CRDB wana haki ya kupata asilimia 2 kutoka ZECO kwa kila muamala utakaokusanywa kutoka kwenye chaneli za PBZ/CRDB, yaani, kiwango cha ujira kitatozwa kwa makusanyo yaliyofanywa na PBZ/ CRDB. Wakati kamisheni ya asilimia 2 inayostahili ZANTEL kutoka ZECO ni kwa ajili ya kutekeleza kila ununuzi wa unit za TUKUZA (execution of each electronic TUKUZA recharge unit) yaani, kiwango cha ujira kitatozwa kwa manunuzi ya umeme yaliyofanywa na ZANTEL kutoka ZECO kwa ajili ya kuwauzia wateja

Misingi ya malipo ya ujira kwa ZANTEL ilionekana kuwa na hitilafu kwani taratibu za malipo ya ujira zinapaswa kuzingatia mauzo yaliyofanywa na mtoa huduma kwa niaba ya mkuu wake (principal). Kwa maana hiyo ZECO ilikuwa inalipa ujira ya ziada kwa ZANTEL kwa makusanyo/ mauzo ambayo hayajapokelewa na kusababisha kuengezeka gharama za uwendeshaji kutokana aina hii ya biashara.

- Malipo ya Ujira katika mauzo ya jumla

Kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha vigezo na masharti ya mkataba kati ya ZECO na CRDB pamoja na PBZ kinasema kuwa ZECO itamlipa CRDB/PBZ malipo ya ujira ya 2% ikijumuisha VAT kwa kila muamala utakaokusanywa kutoka katika chaneli za CRDB/PBZ. Kwa hiyo, kifungu kinatoa nafasi kwa watoa huduma kupokea malipo ya ujira yakijumuisha VAT na kodi nyinginezo ambazo hazijatajwa kwenye mkataba ikiwa ni pamoja na kodi ya miundombinu (2%) na kodi ya zuio ya 5% ambayo itakuwa mzigo mkubwa kwa ZECO.

Mikataba ya uuzaji wa umeme kwa njia ya vituo vya mauzo na simu za mkononi unaonekana kama biashara ya hasara inayoongeza gharama za uendeshaji badala ya kupunguza kama inavyotarajiwa kutokana na malipo ya ujira mkubwa kwa mawakala wanaohusika ikilinganishwa na gharama za uendeshaji zinazoweza kupatikana iwapo ZECO itaamua kuendesha vituo vyake vya kuuzia umeme.

**Ukaguzi unapendekeza mambo yafuatayo:-**

- Kufanya uchanganuzi wa faida na gharama ya uuzaji wa umeme kwa kushirikiana na mawakala ili kubaini mwenendo wa mauzo dhidi ya gharama za uendeshaji zinazohusiana na aina hii ya biashara kwa kulinganisha na gharama za uendeshaji endapo ZECO itaamua kufanya bishara yenyewe bila kutumia mawakala.
- Kupitia upya mikataba ya watoa huduma ya uwakala wa uuzaji wa umeme kwa njia ya vituo vya mauzo na simu za mkononi na kuondoa dosari zote zilizoainishwa hapo juu, mapitio hayo pia yazingatie kupunguza malipo ya ujira kwa mawakala wa kuhudumia Shirika kutokana na kupata hasara kubwa kutokana na malipo ya ujira ya ziada na mzigo wa ushuru.
- ZECO ifikirie kuanzisha mauzo ya umeme mtandaoni kupitia tovuti au kuwa na “code” wake wa USSD ambao utawaruhusu wateja kununua umeme kupitia simu za mkononi. Idara ya TEHAMA inapaswa kufanya upembuzi yakinifu wa kina katika eneo hili ili kusaidia Shirika kupunguza gharama za uendeshaji kwa kiasi kikubwa.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Mkataba wa PBZ na CRDB haujaanza utekelezaji wake. Hata hivyo, Serikali imelitaka Shirika la Umeme kutoa huduma ya uuzaji wa umeme kwa kupitia mfumo wa Serikali wa ZAN-MALIPO ambao utaondoa kabisa tatizo lililojitokeza katika mikataba hiyo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa mkataba wa PBZ na CRDB haujaanza utekelezeja wake hata hivyo imesikitishwa na Afisi ya mwanasheria mkuu ambayo ndio Serikali inaitegemea katika kuhakiki mikataba yote ya Serikali kwa vile mkataba huo imepitishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu licha ya kuwa na dosari mbalimbali ambazo zingeliweza kuliingiza hasara shirika endapo mkataba huu ungetekelezwa.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Shirika kuwa makini katika kufunga mikataba ya kibiashara na sekta binafsi katika uuzaji wa umeme kwa kuhakikisha tija inapatikana kupitia mikataba hiyo.

Aidha Kamati inalishauri Shirika kuufanyia kazi ushauri uliotolewa na Mkaguzi wa kufanya maboresho ya Mkataba baina Shirika na Zantel ili kasoro zilizoibuliwa na Mkaguzi kuweza kufanyiwa kazi.

Vile vile Kamati inalishauri Shirika la Umeme kabla kuanza kwa mchakato wa utoaji wa huduma zao kwa kishirikiana na Taasisi nyengine ni muhimu kufanya upembuzi yakinifu/Tafitii ndogo ili kupata kujua muelekeo mzuri wa huduma inayotaka kufanyika.

**5.1.1.16 Mabadiliko ya Muundo wa Mshahara - Changamoto zinazohusishwa kwenye Nafasi za Uongozi**

Kufuatia agizo lililotolewa na ofisi ya Rais-Tume ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora la tarehe 10 Juni,2020 lenye kumbukumbu namba CCB.174/234/02/31 Shirika lililazimika kurekebisha mfumo wake wa mishahara ili kuendana na agizo hilo kuanzia Juni, 2020. Hata hivyo, mapitio ya muundo mpya wa malipo ya nafasi za uongozi yalibaini kuwa muundo huo haukutoa uzito sawa wa malipo ya vitengo vingine muhimu ndani ya Shirika kama vile Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi, Kitengo cha Mahusiano ya Umma, Kitengo cha Sheria na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwani wasimamizi wa vitengo hivyo wana majukumu sawa na wale wanaoshikilia nyadhifa za usimamizi wa idara nyigine ndani ya Shirika.

Kwa hivyo, wao walichukuliwa kama wafanyakazi wengine wa kawaida katika viwango vya chini ambao hulipwa kulingana na kiwango chao cha elimu na uzoefu bila kujali majukumu mengine ya ziada wanayoyafanya katika majukumu yao ya kila siku.

Ushahidi wa kuthibitisha kwamba uongozi ulichukua hatua za kurekebisha hitilafu iliyobainishwa ili kuleta maelewano, usawa na motisha mahali pa kazi ulikosekana.

Uwepo wa pengo kubwa la mishahara kati ya ngazi ya uongozi na vitengo vingine linapunguza motisha kwa wafanyakazi ambapo mwenendo wa utendaji kazi unaweza kuzorota kwa kiwango kinachoongezeka ambacho kitaathiri vibaya malengo ya Shirika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kupitia kwa Bodi ya Wakurugenzi uchukue hatua za makusudi za kupitia upya muundo wa malipo ya mishahara kwa nafasi za uongozi kwa kuwasiliana na vyombo vinavyohusika ili kuhakikisha kuwa wakuu wa Vitengo nao wanapewa uzito sambamba na majukumu waliyonayo.

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Shirika limechukuwa juhudi mbali mbali katika kurekebisha changamoto zilizojitokeza katika ulipaji wa mishahara kwa baadhi ya viongozi kwa kurekebisha muundo na kupeleka katika ngazi husika kama ifuatavyo:

Tarehe 27/09/2022 Shirika liliwasilisha muundo wa Shirika la Umeme kwa Katibu Mkuu, (OR) Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora, kwa ajili ya mapitio na maoni.

Tarehe 21/10/2022, Shirika liliwasilisha muundo huo kwa katibu Mkuu Wizara ya Maji Nishati na Madini ili muundo huo upelekwe katika (OR) Kamisheni ya Utumishi wa Umma Zanzibar na

Tarehe 01/11/2022, Shirika lilipokea barua kutoka (OR)-Kamisheni ya Utumishi wa Umma Zanzibar, ikielekeza kwamba tarehe 29/11/2022 kutakuwa na kikao cha pamoja katika ukumbi wa Ofisi ya kamisheni, Mwanakwerekwe Zanzibar, ili kuendeleza mchakato wa muundo mpya wa ZECO, ambapo muundo huo umezingatia usawa wa Idara na Vitengo.Tumeambatanisha nakala ya barua zilizotajwa hapo juu kwa rejea (Kiambatanisho Na. 5.1.1.16). Kwa sasa muundo umekamilika na upo katika hatua ya utekelezaji.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa Shirika limeshachukua jitihada ya kuboresha muundo wake kwa lengo la kuleta uwiano wa mishahara kwa watumishi wake, licha muundo huo kukamilika Shirika limeonesha kutoridhika na muundo huo kwa vile kwa vile baadhi mapendekezo waliyoyatoa ya muundo huo hayajazingatiwa na baadhi ya idara kuondolewa kwa upande wa Pemba ambazo zinafanyakazi sawa na Idara za Unguja jambo ambalo litapelekea maslahi ya baadhi ya watumishi wa Shirika

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Shirika licha ya kuwa muundo huo kutokuwa na mgawanyo wa idara na vitengo kwa upande wa Pemba kama ulivyokuwa muundo wa awali kabla ya mabadiliko hata hivyo Shirika linaweza kuboresha maslahi ya watendaji wake kupitia muundo ulioyopendekezwa kwa kulinganisha majukumu wanayofanya watendaji wake katika afisi za Unguja na Pemba ili kuweka viwango sawa vya maslahi kwa kazi zinazofanana kwa kuonana uongozi wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala bora kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi suala hilo.

### 5.2.4 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR

**Taarifa ya Mapato na Matumizi**

**Kwa upande wa Kikund(Group)**

Chanzo kikuu cha fedha cha PBZ kwa upande wa Kikiundi katika mwaka wa fedha 2020/2021 ni amana kutoka kwa wateja ambayo huchangia wastani wa asilimia 76 ya jumla ya fedha zote zilizowekwa, asilimia 12 inatokana na mitaji iliyowekwa na asilimia 8 inatokana na mikopo iliyotolewa, aidha Hesabu ya Akiba huwakilisha wastani wa asilimia 87 ya jumla ya amana za wateja zilizowekwa.

**Kwa upande wa Benki (Bank)**

Chanzo kikuu cha fedha cha PBZ kwa upande wa Benki katika mwaka wa fedha 2020/2021 ni amana kutoka kwa wateja ambayo huchangia wastani wa asilimia 76 ya jumla ya fedha zote zilizowekwa, asilimia 12 inatokana na mitaji iliyowekwa na asilimia 8 inatokana na mikopo iliyotolewa. aidha Hesabu ya Akiba katika mwaka 2021 imewakilisha wastani wa asilimia 87 ya jumla ya amana za wateja zilizowekwa ukilinganisha na wastani wa asilimia 88 katika mwaka 2020.

Bakaa baina ya deni na mtaji kwa mwaka 2021

| | **KIKUNDI (GROUP)** | | **BANK (BENKI)** | |
|---|---|---|---|---|
| | **2021** | **2020** | **2021** | **2020** |
| | **Tshs '000'** | **Tshs '000'** | **Tshs '000'** | **Tshs '000'** |
| **Mikopo** | | | | |
| Amana za wateja | 774,721,080 | 593,562,822 | 759,633,561 | 578,363,644 |
| Mikopo iliyotolewa | 85,387,000 | 36,932,314 | 83,860,552 | 34,505,071 |
| Dhamana ya mikopo iliyotolewa | 15,678,513 | 15,642,205 | 15,678,513 | 15,642,205 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Madeni mengineyo | 16,301,641 | 16,221,052 | 15,330,363 | 14,647,373 |
| Jumla | 892,088,234 | 662,358,393 | 874,502,989 | 643,158,293 |
| Mtaji | | | | |
| Gawio la Mtaji | 31,000,000 | 36,000,000 | 31,000,000 | 31,000,000 |
| Ruzuku ya Serikali | 3,310,625 | 3,332,827 | 3,310,625 | 3,332,827 |
| Mapato yaliyobakishwa (Retained earnings) | 78,654,356 | 69,680,472 | 78,769,951 | 58,528,870 |
| Bakaa nyenginezo (Other re- serves) | 14,565,292 | 6,465,262 | 12,944,419 | 16,809,306 |
| **Jumla** | **127,530,273** | **115,478,561** | **126,024,995** | **109,671,003** |

**Ukopaji (Borrowings)**

Kikundi hakikuweka dhamana ya mikopo ya muda mrefu kwa mwaka 2020/2021 ambapo kilichangia wastani wa asilimia 16.53, kwa muda wa miaka 7 ya bondi ya iliyowekwa na ZSSF yenye wastani wa shilingi bilioni 5 iliyotarajiwa kufikia ukomo wa utolewaji mnamo mwezi wa Januari 2022, na dhamana ya asilimia 12 iliyowekwa kwa muda wa miaka 7 na ZSSF yenye jumla ya shilingi bilioni 10 bilioni inayotarajiwa kufikia ukomo wake mnamo mwezi wa Septemba 2025. Mchango wa mikopo kwa kikundi kwa mwaka ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Mikopo baina ya Benki na Benki (Interbank borrowing)**

| **Maelezo** | **Kikundi (Group)** | | **Benki (Bank)** | |
|---|---|---|---|---|
| | **2021** | **2020** | **2021** | **2020** |
| | **Tshs'000'** | **Tshs'000'** | **Tshs'000'** | **Tshs'000'** |
| | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mikopo kati ya benki na benki | 85,332,711 | 34,909,964 | 83,832,711 | 34,482,721 |
| Miaka 3, asilimia 11.5 mkopo kwa TMRC | - | - | - | - |
| Housing Microfinance Loan kwa Benk Kuu | - | 2,000,000 | - | - |
| Riba inayotokana na utowaji wa mikopo | 54,288 | 22,350 | 27,841 | 22,350 |
| **Jumla** | **85,387,000** | **36,932,314** | **83,860,552** | **34,505,071** |

**Dhamana kwa mikopo iliyotolewa (Debt securities in issue)**

| **Maelezo** | **Vikundi (Group)** | | **Benki** | |
|---|---|---|---|---|
| | **2021** | **2020** | **2021** | **2020** |
| | **TZS'000'** | **TZS'000'** | **TZS'000'** | **TZS'000'** |
| Mikopo ya miaka 7 ya asilimia 16.53 iliy-otolewa | 5,000,000 | 5,000,000 | 5,000,000 | 5,000,000 |
| Mikopo ya miaka 7 ya asilimia 12 ya dha-mana ya Kamapuni (Corporate bond) | 10,000,000 | 10,000,000 | 10,000,000 | 10,000,000 |
| Riba inayotokana na utowaji wa mikopo | 678,513 | 642,205 | 678,513 | 642,205 |
| **Jumla** | **15,678,513** | **15,642,205** | **15,678,513** | **15,642,205** |

**Uwekezaji (Investment)**

Mitaji iliyowekezwa na Kikundi hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2021

| **Uwekezaji** | **Idadi ya hisa (Tshs)** | **Gawio (Tshs)'000'** |
|---|---|---|
| Uwekezaji nje ya Afrika – Uwekezaji unaotoka nje ya nchi | 16 | 812,609 |
| TMRC | 625,000 | 1,013,750 |
| Umoja Switch Company Ltd | 39 | 60,769 |
| Uwekezaji wa Swift | 6 | 95,043 |
| | | **1,982,171** |

**Mitaji iliyowekezwa na Kikundi hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2021**

| **Uwekezaji** | **Idadi ya hisa (Tshs)** | **Gawio (Tshs)'000'** |
|---|---|---|
| Uwekezaji kwenda nchi nyengine ndani ya Afrika –Uwekezaji unaoingizwa ndani ya nchi | 16 | 812,609 |
| TMRC | 625,000 | 1,013,750 |
| Umoja Switch Company Ltd | 39 | 60,769 |
| MUCCOBA | 24,509,804 | 5,000,000 |
| Uwekezaji wa Swift | 6 | 95,043 |
| | | **6,982,171** |

## Matokeo ya Utekelezaji yaliyopitiwa (Review of Operating Results)

## Matokeo ya Utekelezaji (Operating Results)

### Kikundi (Group)

Benki ya Watu wa Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2021 kupitia vikundi ilipata faida kabla ya kodi yenye jumla ya shilingi milioni 23,591 ambapo vikundi viliingiza mapato ya riba yenye jumla ya shilingi milioni 75,572 na gharama za riba zenye jumla ya shilingi milioni 14,530 zilizotolewa na kupelekea kiwango cha riba kufikia wastani wa asilimia 81 mnamo mwaka 2021.

Katika mwaka 2021, Benki ya Watu wa Zanzibar iliingiza mapato yasiyo na riba ya vikundi yenye jumla ya shilingi milioni 24,212 ambapo gharama za uendeshaji zilizotumika ni shilingi 74,935 sawa na asilimia 74.44 ya mapato halisi na

### Benki

Banki hivyo iliingiza mapato yenye jumla ya shilingi milioni 22,691 mnamo mwaka 2021 ukilinganisha na shilingi milioni 18,101 zilizopatikana mnamo mwaka 2020 ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia 24.

Faida ya asilimia 17 ya mapato yenye jumla ya shilingi milioni 71,701 mnamo mwaka 2021 kutoka shilingi milioni 61,060 mnamo mwaka 2020. Gharama za riba kwenye mikopo (Interest expenses) iliongezeka kwa asilimia 33 hadi kufikia shilingi 13,866 mnamo mwaka 2021 kutoka shilingi milioni 10,432 zilizoripotiwa mnamo mwaka 2020,

### Mapato yasiyo na riba

Mapato yasiyo na riba yameengezeka kwa wastani wa shilingi milioni 4,115 sawa na asilimia 2 na kufikia jumla ya engezeko la shilingi milioni 23,381 mnamo mwaka 2021 ukilinganisha shilingi milioni 19,266 zilizoripotiwa mnamo mwaka 2020.

**Majibu ya Hoja**

Benki iliingiza faida kabla ya kodi jumla ya shilingi bilioni 22.69 mnamo mwaka 2021 ukilinganisha na shilingi bilioni 18.10 zilizopatikana mnamo mwaka 2020 ambapo ni sawa na ongezeko la silimia 25. Ongezeko hilo limechangiwa zaidi na faida iliyotokana na ukuaji wa utowaji wa mikopo hasa kwa wafanyakazi wa umma.

**Gharama za Uendeshaji (Operating Expenses)**

Jumla ya gharama za uendeshaji ziliongezeka kwa wastani wa shilingi 9,597 hadi kufikia jumla ya shilingi milioni 61,964 mnamo mwaka 2021 kutoka jumla ya shilingi milioni 71,561 zilizoripotiwa mnamo mwaka 2021

**Majibu ya Hoja**

Jumla ya gharama za uendeshaji ziliongezeka kwa wastani wa shilingi 9.597 hadi kufikia jumla ya shilingi bilioni 71.56 mnamo mwaka 2021 kutoka jumla ya shilingi bilioni 61.96 zilizoripotiwa mnamo mwaka 2020, lakini kihalisia matumizi ya taasisi yalipungua kwa kipindi hicho kutokana na usimamizi mzuri wa matumizi pamoja na kufanya matumizi yenye tija pekee kwa taasisi, ongezeko hilo sana limechangiwa na tengo (provision) kwa matarjio ya hasara kwa ajili ya bakaa ilisilosawazishika kwenye masahihisho ya akaunti za nje (NOSTRO) ambapo jumla ya bakaa hilo lilikuwa ni takriban shilingi bilioni 13.

**Uwezo wa kifedha wa PBZ (Financial Position)**

Benki ya Watu wa Zanzibar hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2021 ilikuwa na mali za Vikundi zenye jumla ya shilingi milioni 1,016,244, ambapo miongoni mwa mali hizo jumla ya shilingi 615,297 ni fedha taslimu za Wateja na shilingi milioni 192,941 ni salio la Benk Kuu ya Tanzania

Mali za PBZ zimeengezeka kwa asilimia 33 hadi kufikia jumla ya shilingi 996,368 mnamo mwaka 2021. Mikopo na kitangulizi cha fedha vimeengezeka kwa asilimia 27 kwa shilingi 128,798 hadi kufikia jumla ya shilingi 600,246 mnamo mwaka 2021 kutoka jumla ya shilingi 471,448 zilizoripotiwa mnamo mwaka 2020 na salio la Benki Kuu liliongezeka kwa asilimia 109 kutoka shilingi milioni 92,316 mnamo mwaka 2020 hadi kufikia shilingi milioni 193,338 mnamo mwaka 2021. Uwekezaji wa dhamana za wateja ulipungua kwa shilingi milioni 1,747 sawa na asilimia 4.24 kutoka shilingi milioni 41,174 mnamo mwaka 2020 hadi kufikia shilingi milioni 39,427 mnamo mwaka 2021.

**Mnyambuliko wa Kifedha (Cash Flows)**

Uwekezaji wa PBZ uliengezeka kwa jumla ya shilingi bilioni 1.8 ambapo kwaka 2020 ulifikia jumla ya shilingi bilioni 48.6 na Mikopo kwa wateja imeengezeka kwa wastani wa shilingi bilioni 129 mnamo mwaka 2021 ambapo mnamo mwaka 2020 ilipungua kwa wastani wa shilingi bilioni 93. Kwa upande mwengine uwekaji fedha uliofanywa na wateja uliengezeka kwa shilingi bilioni 182 mnamo mwaka 2021 ukilinganisha na ongezeko la bilioni 1 mnamo mwaka 2020

**Ulipaji wa Kodi (Taxes)**

Kwa mwaka 2021 PBZ ililipa kodi ya shirika (Cooperate Tax) yenye jumla ya shilingi milioni 9,608 na kodi kupitia mali (Deferred tax asset) yenye jumla ya shilingi milioni 8,526 mnmo mwaka 2021 ukilinganisha na jumla ya shilingi 3,913 zilizolipwa mnamo mwaka 2020.

PBZ kama Wakala wa ZRB na Malipo ya Kodi

PBZ kama wakala wa ZRB katika mwaka 2021 ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni 619 na kupelekea kuwepo makusanyo yenye jumla ya shilingi milioni 1,428 kutoka shilingi milioni 809 zilizokusanywa mnamo mwaka 2020.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kuifuatilia taarifa hii ya Mapato na Matumizi Kamati imebaini Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) inakabiliwa na changamoto wa uhaba wa mtaji katika uendeshaji wa shughuli za kibenki. Hivyo, na kuweza kuendesha biashara hii katika soko la ushindani.

Kamati inaishauri SerIkali pamoja na Wana HISA kuiongezea Mtaji benk hii ili iweze kutekeleza mipango yake pamoja na kuendesha biashara katika Soko la Ushindani.

Kwa upande wa matumizi Kamati pia imebaini uwepo wa dosari katika mipango ya uwekezaji wa Rasilimali majengo ya Ofisi katika maeneno mbali mbali wanayowekezwa na PBZ kwa ajili ya utoaji wa huduma za kibenki.

Kutokana na dosari hizo. Kamati inaushauri  Uongozi wa Benki kabla ya kufanya uwekezaji wowote wa Matawi ya Benki  ni vyema wakashirikiana na Idara ya Mipango Miji ili kujua Mipango ya Serikali kwa maeneo wanayohitaji kufanya uwekezaji ili kunusuru matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Mfano halisi, Tawi la PBZ makunduchi limejengwa kwa gharama kubwa ila kwa muda mfupi linavunjwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa utanuzi wa barabara.

Aidha, katika eneo la Nungwi Kamati imebaini kupitia Taarifa ya Hesabu ya Mwisho ya Mwaka “Financial Statement” kuwa PBZ ilifanya matumizi ya shilingi milioni 30,000,000 kukodi eneo kwa ajili ya kuanzisha tawi la PBZ ila eneo hilo halikuweza kuendeshwa shughuli za kibenki kutokana na kukosa vigezo kwa mujibu wa Kanuni na Miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania.

Hivyo, Kamati inaishauri Uongozi wa Benki kuwa makini wakati wanapotekeleza majukumu yao hususan katika suala la uwekezaji wa biashara za Kibenki kuhakikisha unafuata Sheria, Kanuni pamoja miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania.

Sambamba na hilo, katika kipengele cha “Government Grant” “Note 28” Kamati inaushauri Uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kabla ya kufanya matumizi ya uwekezaji huo ni vyema kuhakikisha uongozi unafanya tathmini ya kina kupitia wataalamu mbali mbali wa Serikali ili yasije kujitokeza tena yaliojitokeza nyuma.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

**5.2.4.1Kutokufuatwa kwa miongozo inayohusu mikato ya mikopo shilingi 6,214,000,000.**

Kwa mujibu wa kifungu cha 9 cha Kanuni ya Benki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2014 inazitaka "Benki au taasisi ya kifedha katika mapitio yanayofanywa katika kipindi cha kila robo mwaka kufanya makato katika mikopo, na hakiba ya fedha katika hesabu za wateja kwa muda wa robo nne mfululizo".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mikopo pamoja na akiba ya fedha katika hesabu za wateja zilizopitiwa na muda wa robo nne mfululizo bila ya kufanyiwa makato kinyume na miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania ambapo katika ukaguzi huo mambo yafuatayo yalibainika.

Kuwepo kwa mikopo pamoja na akiba ya fedha itokanayo na wateja katika kipindi cha 30/11/2021 ya shilingi 5,047,000,000 zitokanazo na PBZ na shilingi 1,660,000,000 zitokanazo na Benki ya Kiisalmu lakini hadi ukaguzi unakamilika mikopo hiyo haikuweza kukatwa.

Kuwepo kwa mikopo pamoja na akiba ya fedha itokanayo na wateja katika kipindi cha 30/12/2021 ya shilingi 2,700,000,000 zitokanazo na PBZ na shilingi 1,100,000,000 zitokanazo na Benki ya Kiisalmu lakini hadi ukaguzi unakamilika mikopo hiyo haikuweza kukatwa.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea hasara kwa Benki ya Watu wa Zanzibar itokanayo na adhabu na faini ya kutokufuata miongozo iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania inayozitaka Benki kufanya mikato katika mikopo ya fedha za akiba katika hesabu za wateja.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unafuata Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Benki Kuu ya Tanzania ili kuepusha uwezekano wa kupata adhabu na faini.

Majibu ya Hoja

Uongozi wa benki umeifanyia kazi dosari ya mikopo chechefu iliyopitiwa na muda wa robo nne mfululizo na hadi kufikia mwishoni mwa robo mwaka ya pili 2023, hakuna mikopo chechefu iliyokuwa kwenye orodha hii. Kwa sasa benki inafanya mapitio ya mikopo chechefu kwa kila robo mwaka kuendana na miongozo ya Benki Kuu.

Hapo awali sharia hii ilikua ikitekelezwa kila mwaka badala ya kila robo kutokana na uelewa kwamba robo nne katika mwaka ni sawa na mwaka kamili na hivyo uongozi ulikua unatekeleza sharia hii kila kipindi cha ufungaji wa hesabu za mwaka, tofauti na sasa ambapo uongozi hufanya makato ya mikopo iliyopitiwa na robo nne kila ikimalizika robo ya mwaka.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Uongozi wa Benki umekiri kuwepo kwa dosari hiyo hata hivyo juhudi zimeshachukuliwa za kufuata kifungu cha 9 cha Kanuni ya Benki na Taasisi za kifedha ya 2014 ambapo hadi kufika 2023 mikopo yote inakatwa kila robo mwaka.

Kamati inashauri uongozi wa Benki kufuata taratibu na miongozo mbalimbali inayotolewa na Benki na Taasisi za kifedha katika kutekeleza majukumu yao ili kuepusha uwezekano wa kupata adhabu na faini.

**5.2.4.2 Kuwepo kwa orodha ya muda mrefu ya mikopo iliyopitiwa na muda shilling 21,453,832,300.93**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mikopo pamoja na malipo ya awali yaliyotolewa kwa wateja yenye jumla ya shilingi 18,443,518,133.81 kwa idadi ya

mikopo 1772 iliyotolewa na PBZ na shilingi 3,010,314,167.12 kwa idadi ya mikopo 367 iliyotolewa na Benki ya Kiislamu ambayo muda wa kutolewa kwa mikopo hiyo umeshapita bila ya mikopo hiyo kutolewa ambapo ni kwenda kinyume na miongozo iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania. Mchanganuo wa mikopo pamoja na malipo ya awali ni kama inavyoonekana katika kiambatanisho nambari 2.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar unahakikisha unafuata Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Benki Kuu ya Tanzania ili kuepuka hasara itokanayo na adhabu na faini.

**Majibu ya Hoja**

Uongozi unaendelea na juhudi za kuhakikisha mikopo inayofikiwa na muda inafuata taratibu zote na inafanyiwa mapitio kila robo mwaka kwa mujibu wa miongozo ya Benki kuu na kuhakikisha marejesho ya mikopo yanakusanywa kwa mujibu wa taratibu.

Wakati huo huo TZS 8.0 billioni zimelipwa pamoja kuweka sawa mikopo yenye thamani ya TZS 1.98 bilioni pia TZS 0.905 bilioni ipo kwenye harakati za mnada pamoja na TZS 0.710 bilioni inasubiria taratibu kukamilika ili kuzifungua account hizi na pia TZS 4.808 bilion imefutwa na mikopo liyobakia tayari iko katika idara ya ufatiliaji madeni kwa hatua zaidi.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na majibu yaliyotolewa na Benki, Kamati imebaini bado kuna changamoto ya ucheleweshaji wa marejesho ya mikopo ya benki kinyume na taratibu na miongozo kutoka Benki Kuu.

Kamati ya LAAC inaishauri Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kufuatilia kwa karibu marejesho ya madeni yatokanayo na mikopo hiyo ili yaweze kulipwa kwa wakati.

Vile vile, Kamati inashauri uongozi wa Benki kufuata taratibu na miongozo mbalimbali inayotolewa na Benki na Taasisi za kifedha katika kutekeleza majukumu yao ili kuepusha uwezekano wa kupata adhabu na faini.

**5.2.4.3 Mkopo uliotolewa kwa mfanyakazi bila ya kuzingatia muda wa kustaafu shilingi 60,000,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 60,000,000 zimelipwa kwa ajili ya mkopo wa miaka 5 kwa Ndugu Rashid Salum Said ambaye anatarajiwa kufikia umri wa lazima wa kustaafu kazi baada ya miaka 3 kutoka tarehe ya uchukuaji mkopo. Katika kufanya ufuatiliaji imebainika kwamba mkopeshwaji ni mfanyakazi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania mwenye kitambulisho nambari 100990 ambaye baada ya miaka 3 hatoweza kufanya marejesho ya mkopo aliopatiwa kutokana na kutokuwa na mshahara kwa vile hatokuwa mtumishi tena wa Serikali.

Kufanya hivyo kunapelekea uwezekano wakutokupatikana kwa marejesho yanayotokana na mikato kwa kipindi cha miaka 2 ambayo mteja huyo atakuwa sio mtumishi tena wa Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo pamoja na kufanya uhakiki wa kina kwa mteja kabla yakutowa mikopo ili kuepusha kuitia hasara Benki kutokana na wateja hao kushindwa kuirejesha mikopo waliyopatiwa.

**Majibu ya Hoja**

Mteja ni daktari wa kitaalamu katika TPDF, na kuna utaratibu katika TPDF kuongeza muda wa kustaafu kwa wataalamu wote katika TPDF kwa miaka miwili zaidi baada ya muda wa kawaida wa kustaafu wa miaka sitini (miaka 60). Hadi kufikia mwezi wa saba deni safi la mkopo huo ni TZS 44,508,125.05 ambao amebakisha miezi 48 hadi kumaliza kwa mkopo huo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika ufuatiliaji wa hoja hii imebaini kuwepo kwa makubaliano maalum na Jeshi la Wananchi Tanzania katika kuwakopesha baadhi ya wanajeshi wenye sifa na ujuzi maalum kwa muda wa miaka miwili au zaidi wa muda wa kawaida wa kustaafu wa miaka 60 kwa kuamini kuwa watendaji hao wataongezewa muda zaidi wa kiutumishi kwa vile wanasifa na ujuzi maalum kama vile madaktari hivyo huweza wakaongezewa muda wa kiutumishi baada ya kustaafu.

**Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya kuwepo kwa makubaliano hayo baina ya Benki na Jeshi la Wananchi Tanzania katika utoaji wa mikopo kwa watumishi wa jeshi hilo, Kamati inashauri Benki kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo ya utoaji wa mikopo ili kunusuru kutokupatikana kwa marejesho yanayotokana na mikato kwa kipindi cha miaka 2 ambayo mteja huyo atakuwa sio mtumishi tena wa Serikali ikiwa hakupata kuongezwa muda wa utumishi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo za kiafya.

Aidha, Kamati inaitaka Serikali kupitia PBZ wahakikishe wanakaa na Uongozi wa JWTZ pamoja mdaiwa kupata njia sahihi ya kulipa Deni litakalosalia kabla muda wa kustaafu kwa mfanyakazi huyo.

**5.2.4.4 Kutokubadilika kwa kiwango cha makadirio ya hasara itokanayo na Benki ya Kiislamu**

Kwa mujibu wa viwango vya uwasilishaji wa taarifa za kifedha vya kimataifa nambari 9 (IFRS 9) inafafanua makadirio ya kiwango cha ubadhirifu kutokana na kiwango cha mikopo kilichotelewa ambapo makadirio hayo ni tofauti baina ya kiwango cha matarajio ya fedha na uhalisia wa makusanyo ya fedha yatokanayo na mikato inayohusu ulipaji wa kiwango cha mkopo kilichochukuliwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kiwango cha ubadhirifu kinachotokana na mikopo kwa Benki ya Kiislamu kipo katika hali ya kutokubadilika kwa kipindi cha muda mrefu jambo ambalo ni kinyume na IFRS 9 ambapo kiwango hicho kilipaswa kifanyiwe ukokotoaji wa asilimia 15 inayotokana na kiwango cha mkopo kilichotolewa.

Hali hii inaweza kuisababishia Benki hasara itokanayo na ukokotoaji wa kiwango cha ubadhirifu kisichoendana na uhalisia ambapo ni kwenda kinyume na viwango vya utayarishaji wa taarifa za fedha vya kimataifa kama ilivyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kufanya ukokotoaji wa kina kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha ya Kitaifa na Kimataifa ili kuepusha uwezekano wa upatikanaji wa hasara inayoweza kujitokeza kwa kutokufuata kikamilifu miongozo mbali mbali inayotolewa ulimwenguni.

**Majibu ya Hoja**

Uongozi umeifanyia kazi dosari ya makadirio ya asilimia ya ukokotoaji wa hasara tarajiwa (provision for Impairment loss) kwa mikopo yote na kwasasa kiwango cha ukokotoaji kinabadilika kwa mujibu wa taarifa sahihi za takwimu ya makadirio kinachokokotolewa kila robo mwaka.

Tatizo hili lilitatuliwa na washirika (wataalamu) wetu wa mfumo wa IFRS9 baadala ya kufanya maboresho yaliyomaliza tatizo hili mnamo mwaka 2022.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Benki imekiri kuwepo kwa dosari hiyo ambayo imetokana na changamato ya mfumo ya kutoweza kubadilisha asilimia hiyo kwa mujibu wa (IFRS9). Hata hivyo, juhudi zimeshachukuliwa  kwa kuboresha mfumo huo na wataalamu na kwasasa kiwango cha ukokotoaji kinabadilika kwa mujibu wa taarifa sahihi za takwimu ya makadirio kinachokokotolewa kila robo mwaka.

Kamati inaishauri uongozi wa Benki kuwa makini katika kutumia mifumo ambayo inakwenda sambamba na mabadiliko ya utendajikazi wa kibenki pamoja na kuweza kuifanyia mabadiliko kwa kutumia watendaji wake wa ndani pale inapohitaji mabadiliko badala ya kusubiri wataalamu kutoka nje ya nchi.

**5.2.4.5 Kutokufuatwa kwa sheria katika udhibiti wa hesabu za wateja zilizofungiwa**

Kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Kanuni za Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2019 inafafanua kwamba hesabu za wateja (akaunti) iliyofungiwa ni hesabu ambayo haitumiwi na mwenye hesabu hiyo kwa zaidi ya miezi mitano.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar inazifungia hesabu za wateja ambazo hazitumiwi kwa zaidi ya miezi 6 ambapo kunaweza kupelekea kuwepo kwa adhabu na faini kwa Benki husika, aidha ni kwenda kinyume na kanuni kama ilivyobainishwa katika kifungu kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kufanya ufuatiliaji wa hesabu za wateja ili kuenda sambamba na matakwa ya Sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha ya Kitaifa na Kimataifa ili kuepusha uwezekano wa upatikanaji wa hasara

inayoweza kujitokeza kwa kutokufuata kikamilifu miongozo mbali mbali inayotolewa ulimwenguni.

**Majibu ya Hoja**

Uongozi wa Benki umelifanyia kazi tatizo hili na kwasasa mfumo wa Benki unaizuia kutumika hesabu ya mteja ambayo imeachwa bila kutumia kwa Zaidi ya miezi mitano (5) badala ya miezi (6) kama ilivyokuwa hapo awali. ili kuendana na matakwa ya sheria za Benki kuu. Tatizo hili lilitatuliwa ndani ya mwezi wa Machi, 2022.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kwa kuwa Benki imekiri kuwepo kwa dosari hiyo ambayo imetokana na changamato ya mfumo ya kutoweza kubadilisha utaratibu wa kuzuia hesabu ya mteja ambayo imeachwa bila kutumia kwa zaidi ya miezi mitano (5) kama kanuni inavyoelekeza badala ya miezi (6) ambayo ilikuwa inatumika ndani ya mfumo wa Benki bila ya kubadilishwa ili kuendana na Kifungu cha 3 ya Kanuni ya 2019 ya Benki Kuu ya Tanzania.

Licha ya muda mrefu kupita kutokana na kusubiriwa kwa mtaalamu wa mfumo kutoka nje hata hivyo juhudi zimeshachukuliwa kwa kuboresha mfumo na kwa sasa mfumo wa Benki unaizuia kutumika hesabu ya mteja ambayo imeachwa bila kutumia kwa zaidi ya miezi mitano (5) badala ya miezi (6).

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri uongozi wa Benki kuwa makini katika kutumia mifumo ambayo inakwenda sambamba na mabadiliko ya utendajikazi wa kibenki pamoja na kuweza kuifanyia mabadiliko kwa kutumia watendaji wake wa ndani pale inapohitaji mabadiliko badala ya kusubiri wataalamu kutoka nje ya nchi.

**5.2.4.6 Utozaji wa ada ya huduma katika hesabu zilizofungiwa kinyume na miongozo**

Kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Kanuni ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2019 inafafanua kwamba kila mtoa huduma za kifedha au wakala wake hatatumia njia zisizo za haki za kibiashara kwa watumiaji wake. “Matendo yasiyo ya haki ni pamoja na kuendelea kutoza ada za haduma kwenye akaunti zilizofungiwa au akaunti yenye salio chini ya ada za huduma”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba hadi kufi kia tarehe 30/11/2021 Benki ya Watu wa Zanzibar imetoza ada ya huduma yenye thamani thamani ya shilingi 2,504,588,000 ambapo shilingi 2,234,689,150 ni ada ya huduma kabla ya tarehe

31/12/2020 na shilingi 269,898,850 ni ada ya huduma baada ya tarehe 31/12/2020 zitokanazo na hesabu za wateja zilizofungwa. Kufanya hivyo kunaweza kusababisha adhabu na faini kwa Benki ya Watu wa Zanzibar ambapo ni kwenda kinyume na miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unafuata kiukamilifu miongozo iliyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania ili kuepusha uwezekano wa upatikanaji wa hasara itokanayo na adhabu na faini.

**Majibu ya Hoja**

Maboresho ya mifumo yamefanyika ada za huduma hutozwa kwenye akaunti zinazostahiki tu, maboresho hayo yanawezesha kuendana na sharia za BOT. Kwa shilingi 269.898,850,00 zilizotolewa kama ada baada ya tarehe 31/12/2020 Uongozi unalifanyia kazi ili kuangalia uwezekano wa kuwarejeshea wateja kama ilivyoainishwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati baada ya mahojiano ya kina haikuridhika na majibu pamoja na utaratibu unaotumika na Benki hii juu ya suala zima linalohusiana na fedha inayokatwa kwa akaunti zilizofungiwa. Hivyo, Kamati inaitaka Benk ya watu wa Zanzibar kuzirudisha fedha hizo kwa wahusika wa akaunti hizo ndani ya mwezi mmoja na wahakikishe wanatoa taarifa za utekelezaji kwa kamati ya LAAC na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa ajili uhakiki wa utekelezaji huo

**5.2.4.7 Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 21,848,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 21,848,000 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa mbambali lakini bidhaa hizo hazikurikodiwa katika madaftari ya ghalani ili kuweza kuthibitisha juu ya uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya watu wa Zanzibar kuhakikisha kwamba bidhaa zote zinazo nunuliwa zinarikodiwa katika maftari ya ghalani kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo. Mchanganuo wa bidhaa zilizonunuliwa na kutumika bila ya kurikodiwa katika madaftari ya ghalani ni kama inavyoonekana hapo chini:

| ehe | Nambari ya mapol bidhaa | yelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipv (Tshs) | elezo |
|---|---|---|---|---|
| 8-No | 4 | ZAGPA | 7,000,00 | alipo kwa ajili ya ununuzi bidhaa mbalimbali |
| 8-No | 4 | | 1,600,00 | |
| 8-No | 4 | | 1,050,00 | |
| 8-No | 4 | | 780,00 | |
| 8-No | 4 | | 200,00 | |
| 8-No | 4 | | 180,00 | |
| 8-No | 4 | | 60,00 | |
| 8-No | 4 | | 54,00 | |
| 8-No | 4 | | 54,00 | |
| 24-No | 1 | Shamy Int. Ltd | 1,200,00 | |
| 24-No | 1 | | 1,500,00 | |
| 24-No | 1 | | 2,300,00 | |
| 24-No | | oja Switch | 3,150,00 | |
| 1-Se | | | 95,00 | |
| 23-Se | | | 2,625,00 | |
| **Jumla** | | | **21,848,00** | |

**Majibu ya Hoja**

Utaratibu uliotumika kununua kwa bidhaa zilizoainishwa ni kwa kwa njia ya "credit" ambapo mnunuzi alitakiwa kusambaza bidhaa kwanza na kupokelewa baada ya kufanyiwa uhakiki. Hivyo, bidhaa hizi zilipokelewa na kurekodiwa katika mfumo wa kumbukumbu wa mwenendo wa bidhaa za "store ledger card" na baadae msambazaji

alitakiwa kuwasilisha Ankara kwa ajili ya kuomba malipo ndani ya mwezi husika ambapo bidhaa zilipokelewa.

Kutokuwasilisha ankara kulipelekea kuonekana kwa ongezeko la thamani katika "ledger card" iliyooneshwa katika store reconciliation ya mwezi wa Novemba, 2021. Ambapo benki ilikuwa bado haijafanya malipo kwa wasambazaji hao.

Malipo ya bidhaa hizo yalilipwa baada ya wasambazaji kuwasilisha Ankara za malipo kwa bidhaa husika. Kwa tarehe zifuatazo:

**Uchunguzi wa Kamati**

Pamoja na majibu ya Uongozi wa Benki Kamati imebaini kuwa vifaa vilivyonunuliwa havikuambatanisha pamoja na "delivery note" na kushidwa kuingiza vifaa hivyo katika daftari la ghalani kinyume na sheria.

Kamati inashauri Benki licha ya kununua vifaa kwa njia ya mkopo ni vyema kufuata taratibu za  Sheria nambari 12 Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016 kwa kurikodi bidhaa zilizonunuliwa ili kuweza kuthibitisha juu ya uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo.

Aidha Kamati ya LAAC inaishauri Benki ya Watu wa Zanzibar inapofanya manunuzi ya vifaa vya Ofisi pamoja na "Stationary" kuhakikisha inatekeleza agizo la Serikali kwa kufanya manunuzi yay a vifaa vya Ofisi pamoja vifaa vya "Stationary" kupitia Wakala wa Uchapaji wa Serikali (ZAGPA).

**5.2.4.8 Kutokufutwa kwa bakaa ya fedha iliyodumu kwa muda mrefu katika hesabu ya mpito (suspense account) shilingi 233,929,931.95**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa hesabu za mpito zenye bakaa za fedha za muda mrefu ambazo hutumika kwa madhumuni tofauti lakini hesabu hizo hazijafanyiwa usuluhisho ili kuweza kufutwa ambapo hupelekea kuendelea kuwepo

kwa bakaa ya fedha kinyume na miongozo inayotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, aidha hadi ukaguzi unakamilika bakaa hizo hazikuweza kufanyiwa usuluhisho kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018 hali inayopelekea kushindwa kutofautisha baina ya hesabu ya muda pamoja na hesabu nyengine ambazo ni za kudumu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya watu wa Zanzibar kuhakikisha kwamba bakaa katika hesabu za marekebisho zinafutwa ili kuepusha hasara inayoweza kupatikana kutokana na adhabu na faini.

**Majibu ya Hoja**

Fedha hizi zinatokana na malipo ya mishahara iliyoshindikanwa kuingizwa kwenye akaunti za wateja kutokana na akaunti zao kukosewa fedha hizi zinautaratibu wa kuingiwa kwenye akauti za wateja baada ya kupokea masawazisho ya akaunti kutoka wizara ya fedha au kurejeshwa wizara ya fedha baada ya miezi mitatu (3) ikiwa hakujawasilishwa masawazisho ya akaunti za wateja. Utaratibu wa kuzirejesha baada ya miezi mitatu (3) kama hakuna masawazisho hili ni agizo kutoka Wizara ya Fedha. Hata hivyo fedha hizo zote tayari zimesharejeshwa Wizara ya Fedha.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imefuta hoja hii baada ya kupitia vielelezo husika na kujiridhisha kuwa fedha hizo kweli zimerudi Serikalini. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuwa makini katika kuhakiki Accounts za watendaji wa Serikali kabla ya kupeleka fedha za mishahara na Benki ili kuepusha uwepo wa fedha katika benki ambazo zimeshidwa kulipwa kwa wafayakazi kutokana na dosari mbalimbali ikiwemo kukosewa kwa akaunti zao.

#### 5.2.4.9 Kutokuifanyia mapitio ripoti za miamala ya ATM zinazowasilishwa na  BCX

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa makubaliano baina ya Benki ya watu wa Zanzibar na BCX kwa ajili ya utowaji wa huduma za miamala ya kibenki inayohusiana na ATM kwa kutumia VISA Cards baina ya benki hizo ambapo huduma hiyo hutolewa kwa wateja wa PBZ na kutumika kwa utoaji wa fedha katika ATM za Benki tofauti, pamoja na mawakala mbali mbali wanaotoa huduma hizo, lakini imebainika kwamba taarifa zitokanazo na miamala ya wateja katika matumizi ya ATM hazifanyiwi mapitio ili kuweza kujiridhisha uhalisia wa miamala iliyofanyika.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea uingizwaji wa miamala isiyo sahihi ambayo haiendani na miamala iliyofanyika katika Benki ya Watu wa Zanzibar.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha kwamba wanapitia ripoti za miamala inayofanyika kila siku inayotolewa na BCX ili kuendana na makubaliano yaliyofikiwa na Taasisi hizo.

**Majibu ya Hoja**

Uongozi unakubaliana na maelezo kwamba upatanishi wa hesabu za miamala ya VISA unafanywa kwa kutegemea ripoti kutoka BCX. Hii ni kwa sababu Benki haiwezi kupata ripoti moja kwa moja kutoka VISA kwa vile ni “Associate Member” na BCX ndie “Principle Member” wa VISA.

Hivyo benki hulinganisha ripoti mbili ya benki na ya BCX ili kubaini tofauti na kuweza kufanya “Settlement” ili kuweka hesabu sawa. Ni vigumu kuwa na uingizwaji wa miamala isiyo sahihi kwa sababu Benki ina mfumo wake ambao unarikodi miamala yote inayopita kwenye ATM na BCX hawana uwezo wa kuingia kwenye mfumo wa Benki.

Kutoka na maelezo hayo na uchunguzi uliofanywa na wakaguzi wa ndani na wa nje waliweza kuiondosha kasoro hii kwenye ripoti yao kwa mwaka uliofuata wa 2022.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja hii imeondolewa baada ya Kamati kujiridhisha kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) wao ni "Associate Members" wa BCX na sio "Principal Members" wa BCX. Hivyo ni vigumu kwa wao kupata ripoti moja kwa moja kutoka VISA. Hata hivyo, Benki imejipanga kwa kuwa na mfumo unarikodi miamala yote inayopita kwenye ATM na BCX hawana uwezo wa kuingia kwenye mfumo wa Benki.

**5.2.4.10 Kutokufanyika kwa mapitio ya sera za mikopo**

Kwa mujibu wa Kanuni ya Benki Kuu ya Tanzania chini ya Benki za kibiashara na Taaisi za kifedha ya mwaka 2014 inazitaka Bodi za Wakurugenzi za Benki au Taasisi za kifedha kufanya mapitio ya sera ya mikopo kila mwaka au mara kwa mara kadri inavyowezekana ili kuhakikisha upatikanaji wa usahihi wa mikopo inayotolewa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Benki ya Watu wa Zanzibar haikufanya mapitio ya sera za mikopo kwa mwaka 2021 hali ambayo inaweza kupelekea Benki ya Watu wa Zanzibar kupewa adhabu pamoja na kupigwa faini kutokana na kutokufanya mapitio hayo, aidha ni kuikosesha nguvu Benki ya Watu wa Zanzibar katika ushindani wa kibiashara wa mabenki pamoja na taasisi za kifedha ambapo ni kwenda kinyume na miongozo ya Benki Kuu ya Tanzania kama ilivyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha kwamba mapitio ya sera za mikopo zinafanywa kila mwaka ili kuendana na matakwa ya kisheria kwa lengo la kuepushia uwezekano wa Benki ya Watu wa Zanzibar kupata hasara itokanayo na adhabu na faini. Kukosekana kwa usahihi katika mgawanyo wa ziada ya fedha kwa hesabu za wateja

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(2) cha Kanuni za Kibenki na Taasisi za Kifedha ya mwaka 2014 inaelezea kuhusu kufanya malipo ya ziada au kutoa mikopo bila ya kuweka tarehe

maalumu ya ukomo wa malipo kwa mikopo hiyo kunaweza kupelekea mambo yafuatayo:-

- Utowaji wa mikopo kinyume na uwezo wa mkopaji
- umalizika kwa muda wa kurejesha mkopo
- Kutokutumika kwa hesabu ya mteja kwa muda wa siku sitini
- Salio katika hesabu ya mteja kutokukidhi malipo ya riba
- Mkopo kutokulipwa kutokana na uhaba wa fedha
- Madeni kutokulipwa kwa muda uliopangwa

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar haifanyi mgawanyo wa ziada ya fedha kwa usahihi katika katika hesabu za wateja, hali ambayo inaweza kupelekea uwepo wa adhabu na faini kama itakavyoamuliwa na Benki Kuu ya Tanzania kama ifuatavyo:-

- Kuzuiliwa kwa gawio la fedha,
- Kukosa fursa ya kupata mikopo au dhamana,
- Kuzuiwa kutoa mikopo,
- Kuzuiliwa matumizi ya mtaji,
- Kufutwa kwa leseni ya benki,

Kusimamishwa kazi mkurugenzi, afisa au mfanyakazi husika na kupelekea adhabu ya kuzuiliwa kushika nafasi yeyote katika benki au taasisi za kifedha inayohusu usimamizi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unafuata sheria, kanuni na miongozo inayotolewa na Benki Kuu ya Tanzania ili kuepusha Benki ya Watu wa Zanzibar kupata hasara itokanayo na adhabu na faini

**Majibu ya Hoja**

Hadi kufikia mwaka 2023, sera ya mikopo imepitiwa na tayari zinasubiria kuidhinishwa na bodi ili kupelekwa benki kuu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hiyo hata hivyo juhudi zimeshachukuliwa za kupitia sera ya mikopo katika mwaka 2023 ambapo sera hiyo inasubiri kuidhinishwa na Bodi.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri  Benki ya Watu Zanzibar kuharakisha udhinishaji wa Sera hiyo katika Bodi kwa lengo la kuanza utekeleza wa Sera hiyo ili kuepukana na hasara zitokanazo na adhabu na faini kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

**5.2.4.11 Ukokotoaji wa kiwango cha uchakavu kwa mali za kudumu kinyume na utaratibu**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar inaendelea kukokotoa kiwango cha uchakavu kwa mali za kudumu ambazo hazipaswi kukotolewa kutokana na mali hizo kutokuwa na thamani ambapo muda wa matumizi wa mali hizo umemalizika.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea Benki ya Watu wa Zanzibar hiyo kupewa adhabu na kupigwa faini, aidha ni kwenda kinyume na viwango vya kiuhasibu vilivyowekwa Kitaifa na Kimataifa

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unafanya mapitio ya mara kwa mara ya mali za kudumu ili kuepuka kuendelea kupunguza thamani mali zilizo na thamani ili kuendana na viwango vya kiuhasibu vya Kitaifa na Kimataifa.

**Majibu ya Hoja**

Uongozi umefanikiwa kuliweka sawa tatizo lililogunduliwa na mkaguzi na miamala sahihi ilipitishwa kama inavyohitajika na miongozo ya kiuhasibu ya kitaifa na kimataifa, tatizo lilisababishwa na kufanya mahesabu ya uchakavu wa mali kwa njia ya Excel, lakini kwa sasa uongozi umetafuta mtandao (system) maalum kwa ajili ya kuweka rekodi za mali za Benki na inayokokotoa kiwango cha uchakavu (depreciation) moja kwa moja kwenye mtandao.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile uongozi wa Benki umekiri kuwepo kwa dosari hiyo na kwa vile jitihada zimeshachukuliwa kwa kuanza kutumia mfumo (system) maalum wa kurikodi mali za kudumu za Benki Badala ya kuweka kuumbukumbu hizo kwa njia ya mkono kwa kutumia “EXCEL” ambao ulikuwa na dosari kadhaa.

Kamati inaishauri Benki ya Watu wa Zanzibar kuwa makini katika uhifadhi wa mali zake za kudumu kwa kuendelea kutumia mifumo ya kisasa ambayo itakayoleta ufanisi katika utendaji kazi kwa kutoa taarifa sahihi za mali za kudumu za Benki.

### 5.2.5 BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umebainisha taarifa ya michango ya vyanzo vya mapato vya Bodi ya Mapato Zanzibar , utendaji wa mwaka kwa kila chanzo cha mapato katika Bodi ya Mapato Zanzibar pamoja na kubainisha dosari za kiutendaji zilizojitokeza wakati wa ukaguzi na kubainisha njia za utatuzi wa dosari hizo. Hali halisi ni kama zitakavyoonekana hapo chini.

**Utendaji wa Bodi ya Mapato Zanzibar kwa kipindi cha Miaka Mitano**

Bodi ya Mapato Zanzibar imekuwa ikiongeza maboresho makubwa katika makusanyo ya mapato kutoka shilingi bilioni 297.18 katika mwaka wa fedha 2016/2017 hadi shilingi bilioni 404.54 kwa mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 107.36 ambapo ni sawa na asilimia 36.1 katika kipindi hicho.

**Jadweli lifuatalo linaonesha muhtasari wa utendaji wa Bodi ya Mapato Zanzibar kwa miaka mitano iliyopita (Tshs "Bilioni").**

| Item | indi cha mwaka wa fedha | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/2 | 2017/2 | 2018/2 | 2019/2 | 2020/2 |
| imates | 272 | 396 | 485 | 605 | 645 |
| ual | 297 | 410 | 439 | 463 | 404 |
| Performance | | 103 | 9 | 76 | 62 |
| GDP at Current P | 2,748 | 3,228 | 3,663 | 4,132 | 4,209 |
| GDP at Costant prices (20 | 2,491 | 2,684 | 2,874 | 3,078 | 3,116 |
| ctual Collections to GDP Ratio (Curr Pri | 10.8 | 12.7 | 11.9 | 11.7 | 9.6 |
| ctual Collections to GDP Ratio (Cost prices - 20 | 11.9 | 15.2 | 15.2 | 15.8 | 12.9 |

**Chanzo: ZRB na ripoti ya utafiti wa Kijamii na Kiuchumi Zanzibar 2020/2021**

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano ZRB ilikua ikifanya vizuri katika makusanyo ya mapato kwa kuzingatia vigezo mbali mbali vilivyowekwa isipokua kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Utendaji wa makusanyo kwa mwaka huo haukua mzuri sana ukilinganisha na matarajio yaliyowekwa na taasisi hiyo ambapo makusanyo hayo yalikuwa chini ya kiwango (asilimia 62.8) cha makadirio ya makusanyo yaliyowekwa.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini makusanyo hayo yameshuka kutokana na uwepo wa janga la maradhi ya UVIKO-19 lililoikumba dunia na kupelekea mapato ya nchi mbali mbali duniani kushuka.

Aidha, mbali na uwepo wa janga la maradhi ya UVIKO – 19 pato la taifa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 liliendelea kuongezeka licha ya kupanda kwa bei za mara kwa mara na kwa bei za sasa.

Uwiano wa mapato kwa Pato la Taifa kwa bei za sasa (current prices) ulipungua kutoka asilimia 11.78 kwa mwaka 2019/2020 hadi asilimia 9.61 kwa mwaka 2020/2021.

Hali hiyo inaonesha kwamba shilingi 9.61 zilipungua kwa kila shilingi 100 kutokana na kushuka kwa uchumi katika mwaka 2020/2021 ambazo fedha hizo ziliingia katika ofa za Serikali katika mfumo wa kodi ikilinganishwa na shilingi 11.78 kwa mwaka 2019/2020.

**Maelezo ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Makadirio ya makusanyo ya mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yalikuwa ni TZS 645.44 bilioni wakati makusanyo halisi ni TZS. 404.54 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 62.68 ya makadirio kukiwa na upungufu wa mapato ya jumla ya TZS. 240.90 bilioni ukilinganisha na mwaka 2019/2020 ambapo makusanyo yalikuwa ni TZS. 486.74 bilioni.

Ukaguzi uliofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, umebaini kwamba makusanyo hayo yameshuka kutokana na uwepo wa janga la maradhi ya UVIKO-19 lililoikumba dunia na kupelekea mapato ya nchi mbali mbali duniani kushuka.

Vianzio mbalimbali vya ZRA viliathirika na kushuka kwa mapato ya Serekali kulikosababishwa kupungua kwa:

a) Idadi ya wageni waliolala (bed night) katika hoteli za kitalii kinyume na matarajio.
b) Kampuni nyingi za watembeza wageni kufunga biashara kutokana na kukosa wageni wa kuwatembeza nchini.
c) Huduma na kufungwa kwa Mikahawa mikubwa kwa Wageni katika mahoteli.
d) Kupungua kwa matumizi ya simu na mtandao (internet) katika sekta ya utalii kutokana na baadhi hoteli kufungwa na idadi ndogo ya wageni waliolala.
e) Uingiaji wa bidhaa hasa za vinywaji vikali (pombe) na sigara kutoka Tanzania Bara kutokana na kupungua kwa mahitaji ya vinywaji katika hoteli zinazohudumia watalii.
f) Makusanyo ya Kodi ya Zuio kulikosababishwa na kupungua kwa matumizi ya Taasisi za Serikali katika miradi mikubwa ya maendeleo.

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hali ya makusanyo iliimarika ambapo makusanyo halisi yalifikia TZS. 374.295 bilioni sawa na asilimia 71.25 ya makadirio ya TZS. 525.305 bilioni.

**Uchunguzi na Mapendekezo**

Kamati imebaini ni kweli katika mwaka wa fedha 2020/2021 mripuko wa maradhi ya UVIKO 19 yalishika hatamu duniani kote na kusababisha kushuka kwa hali ya uchumi

duniani hali iliyopeleka kuathiri sekta mbalimbali za kiuchumi nchini kama vile Sekta ya utalii ambayo kwa kiasi kikubwa inachangia upatikanaji wa mapato ya Serikali.

Kamati inaishauri Mamlaka kwa vile janga hili la UVIKO 19 limepungua duniani na shughuli za kiuchumi na kijamii zimeanza kuimarika basi ni vyema Mamlaka kuanza kujipanga upya kwa kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato na kuweka mikakati imara ya kusimamia mapato hayo ikiwemo matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji mapato.

### 5.2.6 Utendaji wa mwaka kwa kila chanzo cha mapato katika Bodi ya Mapato Zanzibar.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, mchango wa vyanzo vya mapato unaonyesha kuwa, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ndiyo inaongoza kwa kuchangia asilimia 29.18 ya makusanyo yote ikifuatiwa na Makusanyo ya Mawizara mbalimbali yenye asilimia 26.43 na ya tatu ni Tozo ya Petroli (Petroleum levy) yenye asilimia 11.70 kama inavyoonyeshwa katika jadweli lifuatalo hapo chini:-

**Jadweli Nambari 37: Makusanyo ya Mapato kutoka katika vyanzo mbali mbali**

| Chanzo | Makadirio ya Makusany (Tshs) “Bilioni” | usanyo Halisi (Tshs) “ oni” | limia (%) |
|---|---|---|---|
| di ya Ongezeko la Thamani | 21 | 11 | 5 |
| uru wa Bidhaa | 3 | 2 | 7 |
| uru wa Hoteli | 4 | 1 | 3 |
| uru wa Migahawa | | | 2 |
| uru wa Waendesha Huduma za alii | 2 | ( | 2 |
| uru wa Stempu | 1 | | 5 |
| lipo ya Viwanja vya Ndege | 5 | 2 | 4 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| lipo ya Bandari | 3 | 1 | 58 |
| di ya Usafiri wa Baharini | 3 | 2 | 88 |
| uko wa Maendeleo ya Barabara | 15 | 13 | 82 |
| nuru wa Mafuta | 57 | 47 | 81 |
| kusanyo ya Wizara | 128 | 100 | 77 |
| di ya Ardhi | 9 | 6 | 70 |
| duma za vyombo vya moto | 2 | 1 | 68 |
| eni za Barabara | 6 | 4 | 81 |
| eni za Udereva | 2 | 1 | 74 |
| a ya usalama wa raia Uwanja wa ege | 12 | 5 | 45 |
| undombinu | 27 | 20 | 74 |
| **nla** | **.44** | **.54** | **68** |

**Chanzo: Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)**

**Maelezo ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

g) Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, baadhi ya vianzio vya mapato vinavosimamiwa na ZRA vimefanya vizuri ingawa havikuvuka malengo. Vianzio ambavyo vimefanya vizuri ni pamoja na:

h) Kodi ya usafiri Baharini ambayo ilifikia asilimia 88.99 kutokana na kuongezeka kwa usafirishaji wa mizigo na abiria wa ndani.

i) Mfuko wa Maendeleo ya Barabara ambao ulifikia asilimia 82.85 na Ushuru wa Mafuta ambao ulifikia asilimia 81.68 kutokana na ongezeko la kawaida la matumizi ya mafuta kwa shughuli zisizokuwa za kitalii.

j) Aidha kuna vianzio ambavyo havikufanya vizuri katika makusanyo vikiwemo ushuru wa Watembeza wageni ambao ulifikia 22.64, na ushuru wa Mikahawa ambao ulifikia asilimia 24.46 kutokana na kupungua kwa wageni ambao walitembelea Zanzibar kutokana na janga la Uviko-19.

### 5.2.7 Taarifa ya michango ya vyanzo vya mapato vya Bodi ya Mapato Zanzibar

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umebaini kuwa Bodi ya Mapato kupitia vyanzo vyake vya mapato unaonyesha kuwa, Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) imechangia asilimia 29.18 ya makusanyo yote ikifuatiwa na makusanyo ya Wizara iliyochangia kwa asilimia

26.43. Hali halisi ya makusanyo na michango hiyo kwa asilimia ni kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 38:Taarifa ya michango ya vyanzo vya mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021**

| anzo cha Mapato | kwa mwaka 2020/2021 | | pato Halisi kwa mwaka 2020/2021 | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | kisio (Tshs) | mia ya Mchan | kusanyo halisi hs) | Asilimia | |
| | "Bilioni" | (%) | "Bilioni" | Makusanyo(%) | Mchango (%) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| di ya Ongezeko la Thamar | 213.00 | 33.10 | 118.06 | 55.26 | 29.18 |
| uru wa Bidhaa | 38.90 | 6.03 | 28.85 | 74.16 | 7.13 |
| uru wa Hoteli | 43.60 | 6.76 | 15.75 | 36.12 | 3.89 |
| uru wa Mafuta | 57.95 | 8.97 | 47.33 | 81.68 | 11.70 |
| kusanyo ya Wizara | 138.21 | 21.41 | 106.93 | 77.37 | 26.43 |
| lipo ya huduma za Banda | 27.72 | 4.29 | 20.73 | 74.79 | 5.12 |
| ndombinu | 72.21 | 11.19 | 34.19 | 47.35 | 8.45 |
| nzo vyenginevyo | 53.19 | 8.24 | 32.69 | 61.46 | 8.08 |
| **Jumla** | **645.44** | **100.00** | **404.54** | **62.68** | **100.00** |

**Chanzo : Bodi ya Mapato Zanzibar**

**Maelezo ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) imechangia asilimia 55.26 ya mapato yote yaliyokusanywa na ZRA. Mchango huu mkubwa wa mapato unatokana na kodi ya VAT ina wigo mpana wa walipakodi ambao mauzo yao ni makubwa ambayo yanaanzia milioni 50 kwa mwaka kulinganisha na wafanyabiashara wengine.

Aidha, kianzio cha Mapato ya Mawizara kimechangia asilimia 77.84 ya mapato yote yaliyokusanywa na ZRA. Mchango huu mkubwa unatokana na usimamizi mzuri wa vianzio mbali mbali vya Mapato katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali uliofanywa na Maafisa Masuuli na pia ufuatiliaji wa karibu uliofanywa na ZRA. Aidha, taaluma ambayo ZRA inaitoa kwa maafisa mapato na Wahasibu wa Wizara, Idara na Taasisi za serikali umechangia kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato katika kianzio hiki.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini mchango mkubwa wa Kodi ya Ongezeko la Thamani ya (VAT) katika ukusanyaji mapato kwa kuchangia asilimia 55.26 ya mapato yote yaliyokusanywa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikufuatiwa Mapato ya Wizara ambayo yamechangia asilimia 77.84

Kamati inashauri Mamlaka kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa kuwafatilia kwa karibu wafanyabiashara ambao mauzo yao yanaanzia milioni 50 kwa vile wapo wafanya biasha ambao si waaminifu na wanajaribu kukwepa kodi hii kwa kutoa taarifa ambazo sio sahihi za mauzo ya biashara zao.

Aidha Mamlaka kuendelea kutoa elimu kwa Mawizara na Taasisi za Serikali juu ya namna ya kudhibiti na kusimamia vyema mapato ya Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na Mawizara na Taasisi za Serikali.

**5.2.8 Utendaji wa Kifedha**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021 Bodi ya Mapato Zanzibar ilijiendesha kwa hasara ya shilingi bilioni 2.2 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na upungufu wa shilingi milioni 625.22.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi ulibaini matumizi ya uendeshaji wa Bodi ya Mapato Zanzibar yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 13.9 mwaka wa fedha 2019/2020 hadi shilingi bilioni 15.6 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na ongezeko la shilingi bilioni 1.7 sawa na asilimia 11. Hali hiyo ilibainika kutokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji.

Aidha, ukaguzi umebaini mapato ya jumla katika kipindi hicho yaliongezeka kutoka shilingi milioni 13,346 kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2019/2020 hadi kufikia

shilingi milioni 13,361 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na ongezeko la shilingi milioni 15 sawa na asilimia 0.11 .

**Maelezo ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Mnamo mwaka 2020/2021 Mamlaka ya Mapato Zanzibar ilijiendesha kwa hasara ukilinganisha na mwaka 2019/2020 hii imetokana na kutoengezeka kwa ruzuku katika mwaka fedha 2020/2021.

Matumizi ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar yaliongezeka kutoka shilingi 13.9 bilioni hadi shilingi 15.6 bilioni mnamo mwaka 2019/2020 na 2020/2022, hali hii imetokana na kuengezeka kwa Mishahara na maposho katika ngazi ya Viongozi, pamoja na kuongezeka kwa michango wa Viongozi kwenda (ZSSF)

**5.2.9 Hali halisi ya Kifedha kwa mujibu wa mali za Bodi ya Mapato Zanzibar**

Katika mwaka wa ukaguzi unaoishia tarehe 30 Juni 2021 imebainika jumla ya mali za Bodi ya Mapato " total asset" ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 18.9 mwaka wa fedha 2019/20 hadi shilingi bilioni 27.6 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na ongezeko la shilingi bilioni 8.7.

Hali hii ilisababishwa zaidi na ongezeko la mali za muda mrefu "Non Current Asset" kwa shilingi bilioni 1.9 kutoka shilingi 18.9 mwaka 2019/2020 hadi shilingi bilioni 20.8 katika mwaka wa fedha 2020/2021 na kupungua kwa mali za muda mfupi "Current Asset" kwa shilingi bilioni 8.2 kutoka shilingi bilioni 9.8 mwaka 2019/2020 hadi shilingi bilioni 1.6 katika mwaka wa fedha 2020/2021. Kwa upande mwingine madeni yalipungua kwa shilingi milioni 0.62 kutoka shilingi bilioni 4.67 mwaka 2019/2020 hadi shilingi bilioni 4.05 katika mwaka wa fedha 2020/2021.

**Maelezo ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Mali za Mamlaka ya Mapato "total asset" ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 18.9 kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi shilingi bilioni 27.6 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na ongezeko la shilingi bilioni 8.7 hii imetokana na ulipaji wa gharama za ujenzi kwa mkandarasi wa jengo la Ofisi ya Gombani Pemba pamoja na kuingizwa thamani ya mifumo kwenye Vitabu vya Hesabu.

Madeni yalipungua kutokana na kumlipa Mkandarasi aliyejenga Ofisi ya ZRA Pemba.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imeridhika na maelezo yaliyotolewa kwa upande wa Mamlaka hata hivyo Kamati inatoa ushauri wa kumalizwa kwa madeni ya Mamlaka ambayo wanadaiwa kwa watoa huduma mbalimbali aidha Mamlaka kuendelea kuwa na usimamizi mzuri wa mali zake za kudumu ambazo zimeongezeka kutoka Tsh bilioni 18.9 2019/20 hadi Tsh bilioni 27.6 kwa mwaka wa fedha 2020/2021

**MATOKEO YA UKAGUZI**

**5.2.9.1 Kukosekana kwa ushahidi wa mlinganisho wa matokeo ya zoezi la uhakiki mali za Bodi ya Mapato Zanzibar na kumbukumbu za daftari la mali za kudumu za Bodi shilingi 20,830,164,946**

Kwa mujibu wa ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ilibainika kuwa uhakiki halisi wa mali za Bodi zinazohamishika ulifanyika mwishoni mwa mwaka (stock taking) ili kubaini pamoja na mambo mengine uwepo, hali na utumikaji wake kama ilivyoagizwa chini ya kifungu cha 41(4) cha kanuni za fedha za ZRB. Hata hivyo, zoezi hilo huwa na maana zaidi wakati matokeo halisi yanapolinganishwa na kuoanishwa na kumbukumbu za vitabu (Rejista ya PPE).

Ukaguzi umebaini kuwa hatua hiyo haikufanyika kutokana na ukweli kwamba Bodi

ilikuwa katika mchakato wa kuboresha Daftari lake la Mali za Kudumu na kuzipatia alama ya utambulisho kwa baadhi ya Mali hizo jambo ambalo ni ishara ya udhaifu wa usimamizi wa mali za Bodi. Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalisia wa shilingi 20,830,164,946 zilizobainishwa katika ufungaji wa hesabu kuwa ni thamani halisi ya mali za kudumu za Bodi ya Mapato.

Kushindwa Kuoanisha (reconciliation) matokeo halisi ya zoezi la kuhesabu mali za kudumu za Bodi dhidi ya vitabu vilivyorekodiwa mali hizo kunapelekea wakaguzi kushindwa kujiridhisha juu ya usahihi wa mali za bodi pamoja na uwepo wa mali hizo zenye thamani ya shillingi za kitanzania
20.8 bilioni kama zilivyoripotiwa katika Hesabu za Bodi kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB unapaswa kuharakisha mchakato wa kuboresha daftari la mali za kudumu kwa nia ya kuweka kumbukumbu sahihi za mali za Bodi.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Nii kweli kwa wakati huo, ZRA ilikosa Ushahidi wa mlinganisho kutokana na kasoro zilikuwemo kwenye mfumo wa mali unajulikana kama “ERP” ambao ulikuwa unatumiwa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar.

Hata hivyo, katika mwaka 2021/2022 ZRA ilipatiwa mfumo uitwao ‘Financial Management System’ (FMS), kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya kupata urahisi wa kuziingiza, kufanya marekebisho, kufanya mlinganisho pamoja na kuhifadhi kumbukumbu hizo.

Hadi kufikia Juni, 2022 ZRA ilikamilisha daftari hilo kwa usahihi wake na lipo tayari kwa ukaguzi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hiyo hata hivyo jitihada zimeshafanyika za kukamilisha mchakato wa kuboresha mali za kudumu kwa kupatiwa mfumo kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.Kamati inashauri Mamlaka kuwasiliana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kupatiwa mafunzo zaidi ya mfumo huo kwa watendaji wake ili uwekaji wa taarifa hizo uwe wa usahihi na wenye ufanisi

**5.2.9.2 Kushindwa kutenganisha thamani ya Ardhi na Majengo katika Hesabu shilingi 20,538,632,803.53**

Kwa mujibu wa viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAs 17) kifungu namba 74 kinasema: "Ardhi na majengo ni mali zinazoweza kutenganishwa na huhesabiwa tofauti,

hata kama zimenunuliwa pamoja. Hali hii inamaanisha kwamba Ardhi ni mali yenye maisha yasiyo na kikomo na kwa hivyo haipunguzwi thamani (not depreciated). Majengo yana maisha mafupi na kwa hiyo ni mali zinazoweza kushuka thamani".

Ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Mapato imekwenda kinyume na kifungu nilichokinakilii hapo juu kwa kuchanganya thamani ya ardhi na majengo katika jedwali la mali za kudumu za Bodi ya Mapato kwa ofisi za Unguja na Pemba kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni , 2021 kwa kubainisha thamani halisi ya kiasi cha shilingi 20,538,632,803.53 ambazo zinajumuisha shilingi 9,500,786,309 ikiwa ni thamani ya ardhi na jengo la ofisi kuu ya ZRB Unguja, shilingi 10,887,846,490,000 ikiwa ni thamani ya ardhi na jengo la ofisi ya ZRB Pemba na shilingi 150,000,000 ikiwa ni thamani ya Jengo la ZRB Pemba (Rest House).

Kutokana na kutokuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu katika Sekta ya Umma ya 17 kifungu namba 74 (IPSAS 17 Paragraph 74) kumepelekea kuishusha thamani ardhi kutokana na uchakavu wa majengo jambo ambalo si sahihi kwani ardhi hupanda thamani yake mwaka hadi mwaka, hivyo thamani ya mali za kudumu za Bodi (PPE) iliyoripotiwa katika hesabu za Bodi kipindi cha ukaguzi si sahihi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu katika kutoa taarifa kuhusu thamani ya mali, mitambo na vifaa vya Bodi.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

ZRA haikuweka thamani ya ardhi kwakuwa ilipewa ardhi hizo kutoka Serikalini zikiwa hazina thamani. Katika mwaka 2021/2022, ZRA imefanikiwa kufanya tathmini ya ardhi na kutenganisha thamani ya ardhi na majengo. Hivyo jumla ya TZS. 7,648,000,000.00 kuwa ni thamani ya ardhi pekee.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hiyo hata hivyo jitihada zimeshachukuliwa na Mamlaka kwa kufanya tathmini na kuweza kutenganisha thamani ya Majengo na thamani ya Ardhi ambapo hadi ukaguzi unakamilika thamani ya ardhi imeripotiwa kuwa ni TZS. 7,648,000,000.00

Aidha Kamati inaishauri ZRA kuwa na utaratibu wa kuzifanyia tathmini Mali, Ardhi zote wanakabidhiwa na Serikali ili kutimiza matakwa ya Sheria ya unanuzi na uondoshaji wa Mali za Umma namba 12/2016 ili pia zipate kuhifadhiwa kwenye Daftari la Mali za Kudumu (Fixed Asset Register) na kupata kuonekana kwenye hesabu za Mwisho wa Mwaka Kwa ukaguzi.

#### 5.2.9.3 Kutokufanyika tathmini ya Jengo la ZRB Mazizini shilingi 20,830,164,946

Kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya Uhasibu kwa sekta za umma namba 17 kifungu namba 49 (IPSAS 17 Paragraph 49) kinazitaka taasisi kutathmini Mali, Mitambo na vifaa vyake kila baada ya miaka mitatu au mitano ili kuripoti thamani halisi ya Mali inazozimiliki.

Aidha, kifungu nambari 51 (IPSAS 17) kimeweka sharti kwamba mali, mitambo na vifaa vitafanyiwa tathmini, kundi lote linalohusiana na mali, mitambo na vifaa ambalo litaangukia katika moja wapo ya hapo juu, yaani iwe katika kundi la mali,mitambo au vifaa ni lazima vifanyiwe tathmini.

Mapitio ya ripoti ya tathmini ya Mali za ZRB iliyotolewa Mei, 2021 yamebainisha kwamba jengo la ZRB (Ofisi Kuu) lililopo Mazizini limekosa ushahidi wa kuonyesha kwamba kulifanyika tathmini ya jengo hilo. Mapitio ya taarifa za fedha kwa zaidi ya miaka mitano (5) nyuma tokea mwaka 2014/2015 zinaonyesha kwamba jengo hilo lina thamani ya shilingi 9,500,786,309 jambo ambalo si sahihi kwa mujibu wa kifungu nilichokinakili hapo juu.

Kutokufanyika kwa tathmini ya jengo la ZRB kunapelekea ukaguzi kuwa na mashaka juu ya thamani ya mali, mitambo na vifaa vilivyooneshwa katika taarifa za fedha yenye thamani ya shilingi 20,830,164,946.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato kulifanyia tathmini Jengo lake ili kuendana na matakwa ya viwango vya kimataifa vya Uhasibu kwa sekta za umma namba 17 (IPSAS 17) ili kuweza kutoa taarifa sahihi za thamani ya jengo kwa wakati uliopo.

**Majibu ya Mamla ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Ni kweli ZRA haikufanya tathmini ya jengo la Mazizini kwa kipindi hicho. Hadi kufikia Juni, 2022 ZRA ilifanya tathmini ya jengo na kubaini thamani halisi ni TZS 9,332,900,000.00 kwa mujibu wa mtathmini kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hiyo hata hivyo tayari jitihada zimeshachukuliwa na Mamlaka kwa kufanya tathmini ya jengo hilo ambapo hadi kufikia juni, 2022 jengo hilo lina thamani ya Tsh 9,332,900,000.

Kamati inaendelea kusisitiza Mamlaka katika kufuata taratibu za kisheria na kuendana na matakwa ya viwango vya Kitaifa na Kimataifa vya Uhasibu kwa kufanya tathmini ya mali na vifaa vilivyomo kila baada ya miaka mitatu au mitano ili taarifa sahihi za thamani ya mali hizo ziweze kupatikana.

**5.2.9.4 Manunuzi ya vifaa yaliyofanyika na kuvitumia moja kwa moja bila ya kuzingatia utaratibu wa Kihasibu shilingi 525,278,370**

Katika ukaguzi uliofanyika tuliweza kupitia taarifa za fedha na kumbu kumbu za ghalani za ZRB zinazohusu vifaa vilivyonunuliwa katika kipindi cha ukaguzi na kubaini kuwa vifaa vyenye thamani ya shilingi 525,278,370 vilinunuliwa moja kwa moja bila kujali kama vilitumika au havikutumika.

Ukaguzi ulibaini kufanyika kwa malipo kwa ajli ya vifaa vya uchapishaji na fotokopi vyenye thamani ya shilingi 369,063,173 , vifaa vya kuandikia vyenye thamani ya shilingi 117,254,841 na vifaa vya kompyuta vyenye thamani ya shilingi 38,957,356. Hata hivyo katika ukaguzi huo ilibainika kuwa vifaa vyote vilivyopokelewa vilinunuliwa moja kwa moja bila ya kujali kama vilitumika au havikutumika jambo ambalo ni kinyume na

kanuni ya 29(k) ya Kanuni ya Fedha ya Bodi ya Mapato ya mwaka 2013.

Aidha, ukaguzi ulibaini jukumu la kudhibiti na kulinda hesabu za vifaa vilivyonunuliwa na kutumika liliachwa tu chini ya usimamizi wa mtunza ghala na kukosekana kwa udhibiti kutoka upande wa uhasibu (finance department) katika kulinganisha na kuoanisha kumbukumbu za mtunza ghala na za mhasibu na kukosekana kwa uhakiki wa vifaa vilivyonunuliwa.

Kwa kutozingatia matakwa ya kanuni ya 29(k) ya Kanuni ya Fedha ya Bodi ya Mapato ya mwaka 2013 kunaweza kupelekea kushindwa kubaini mapungufu ambayo yanaweza kusababishwa na wizi, udokozi, upokeaji wa vifaa hafifu, utunzaji mbaya wa kumbukumbu, ununuzi hewa na kadhalika. Kwa hivyo wakaguzi hawakujiridhisha kwamba ununuzi wote wa vifaa uliofanywa kipindi cha mwaka wa ukaguzi vilipokelewa na kutumiwa kwa manufaa ya Bodi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuhakikisha kuwa manunuzi yote na matumizi ya vifaa vya ghala vinakuwa na viambatanisho vyote vya ununuzi na kutolea vifaa ghalani. Viambatanisho vyote vinatakiwa kuingizwa kila mwezi kwenye vitabu vya Bodi kwa pande zote za mtunza ghala na mtu wa uhasibu. Mwisho wa mwaka kufanyike mlinganisho baina ya kumbukumbu za uhasibu na ghala na kama kuna mapungufu yoyote yachunguzwe ili kuboresha udhibiti wa ndani kuhusu utumiaji wa vifaa ghalani.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Ni kweli Mamlaka ilikuwa inarikodi matumizi ya vifaa wakati wa ulipaji badala ya wakati wa utumiaji hata hivyo, Mamlaka kwa kuzingatia ushauri kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) inaripoti matumizi katika hesabu zake wakati vifaa vinapotumika na sio vinaponunuliwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile mwaka 2013.Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hii na hatua stahiki zimeshachukuliwa. Hata hivyo, Kamati inaisisitiza Mamlaka kuwa makini katika utekelezaji wa shughuli zake kwa kufuata kanuni ya 29 (k) ya Kanuni ya Fedha ya Bodi ya Mapato ya Zanzibar.

**5.2.9.5 Utowaji wa Misamaha ya Kodi kinyume na Sheria ya kodi (Sheria ya Uanzishwaji wa ZRB)**

Kwa mujibu wa Kifungu 29(1) cha uanzishwaji wa ZRB sheria Na.7 ya mwaka 1996 (marekebisho ya mwaka 2021) kinawataka wakurugenzi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kumshauri Waziri anayehusika na masuala ya kodi, juu ya vigezo au sababu zinazopelekea uwepo wa misamaha ya kodi, kupunguza kodi, kuahirisha au kuondoa kodi.

Aidha, Kifungu cha 29(4) kinaelekeza kwamba Waziri mwenye dhamana (Fedha na Mipango) anaweza kutoa kibali cha misamaha baada ya mapendekezo ya Bodi ya Wakurugenzi ya ZRB.

Vile vile, kifungu namba 29A (1) kinabainisha kuwa Bodi ya Mapato italazimika, kwa mujibu wa sheria, Kutoa taarifa kwa Waziri mara kwa mara na pia kutoa taarifa ya mwaka na kuiwasilisha katika Baraza la Wawakilishi, miongoni mwa mambo mengine, taarifa itaonyesha kiwango cha kodi

kilichokusanywa au kusamehewa kwa mujibu wa vigezo maalum vilivyoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu 29.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na wahusika na kubaini kuwa tangu Novemba 2020

misamaha yote ilipitia moja kwa moja kwa Waziri (Fedha na Mipango) kinyume na taratibu za misamaha ya kodi iliyoelezwa kupitia kifungu 29 and 29A.

Kutokana na kitendo cha misamaha ya kodi kupitia moja kwa moja kwa Waziri mwenye dhamana na kufanyiwa maamuzi kinyume na kuzingatia matakwa ya kisheria ya kifungu 29 na 29A kumepelekea kukosekana kwa ushahidi wa kimaandishi wa kuthibitisha kwamba Bodi imezuiwa kujihusisha na misamaha ya kodi kwa mujibu wa sheria.

Aidha wakaguzi hawakupatiwa uthibitisho unaoonesha matakwa ya kisheria ya usimamizi wa misamaha kusimamiwa na Wizara ukizingatia kwamba kwa mujibu wa sheria na kanuni misahama hiyo husimamiwa na Bodi ya Mapato na utekelezaji wake hufanywa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Kutokana na kitendo cha ukiukwaji wa kifungu cha 29 na 29A kunaweza kukapelekea

Uwepo wa mapungufu yatakayopelekea kutoa mwanya wa matumizi mabaya ya misamaha ya kodi.

Bila kuwepo na ushahidi wa maandishi kuthibitisha kwamba Bodi haitakiwi kujihusisha na misamaha ya kodi, inaweza kuingizwa kwenye makosa ikiwa kwa bahati mbaya kutatokea makosa juu ya utolewaji wa misamaha ya kodi unaofanywa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB kuwasiliana na Wizara husika (Fedha na Mipango) kwa madhumuni ya kuweka sawa na kupata ufumbuzi wa kimaandishi, kwa lengo la kumjua ni nani mwenye jukumu la utoaji wa misamaha ya kodi.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar (ZRA)**

Kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) Nam. 7 ya 1996, ZRB ilitakiwa kumshauri Mh. Waziri anaeshughulikia Fedha juu ya misamaha ya kodi. Jukumu hili limefanyika tokea 1998 hadi 2020, ambapo Wizara ya Fedha ilianza kushughulikia misamaha ya kodi bila ya ushauri wa ZRA. Kwa kutambua hilo, ZRA ilihitaji ufafanuzi wa mabadiliko haya kwa barua yenye Kumbukumbu Nambari ZRB/F.4/VOL.IV/85 ya tarehe 26/6/2021 ambapo ZRA haikupata ufafanuzi juu ya suala hilo.

Hata hivyo, jukumu la kumshauri Mh. Waziri kuhusu misamaha ya kodi kwa sasa halipo tena kwa Kamishna Mkuu wa ZRA ambapo Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) Nam. 7 ya 1996, iliyokuwa imeainisha jukumu hilo imefutwa na kuanzishwa Sheria ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Nam. 11, ya 2022, ambayo haikuanisha jukumu la kumshauri Mh. Waziri wa Fedha kuhusu misamaha ya kodi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa ni kweli kuna misamaha ya kodi imetolewa bila idhini ya Bodi ya Mamlaka kinyume na utaratibu Kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) Nam. 7 ya 1996 kwa wakati huo.

Kamati imeshidwa kufanya kikao na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kupata ufafanuzi wa hoja hii kutokana kukosa muda uliosababishwa na ugumu wa ratiba za kazi za Kamati hata hivyo Kamati itaendelea kuifatilia hoja hii ili kubaini sababu zilizopelekea Mh Wazir kutoa kibali cha misamaha ya kodi kinyume na Kifungu cha 29(4).

Aidha Kamati itaendelea kufuatilia jambo hilo ili kubaini jukumu hili kwa sasa limebaki Ofisi ya Rais Fedha na Mipango au Vyenginevyo Kwa vile jukumu hili la kumshauri Mh.

Waziri kuhusu misamaha ya kodi kwa sasa halipo tena kwa Kamishna Mkuu wa ZRA baada ya Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) Nam. 7 ya 1996, iliyokuwa imeainisha jukumu hilo imefutwa na kuanzishwa Sheria ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Nam. 11, ya 2022, ambayo haikuanisha jukumu la kumshauri Mh. Waziri wa Fedha kuhusu misamaha ya kodi.

### 5.2.9.6 Madhara ya kisheria kwa kushindwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAPA NA.7 YA 2009 (R.E.2013)

Kitengo cha masuala ya huduma za kisheria na shughuli za Bodi kimesajili na kushughulikia kesi 9 katika hatua mbalimbali za Mahakama (Bodi ya Rufaa au Usuluhishi) katika kipindi cha ukaguzi. Ukaguzi wa kesi hizo ulibaini kuwa kesi nyingi zilizotokana na kushindwa kwa Maofisa wa ZRB Ukaguzi wa kesi hizo ulibaini kuwa kesi nyingi zilizotokana na kushindwa kwa Maofisa wa ZRB kufuata sheria na taratibu zilizoainishwa kwa mujibu wa sheria ya kodi TAPA Na.7 ya mwaka 2009 (R.E 2013) wakati wa kutekeleza majukumu yao. Hali hii imebainika katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 39: Baadhi ya kesi zilizotolewa maamuzi mbali mbali katika Mahkama**

| Namba | anaoshtakiana | bari ya Kesi | aelezo mafupi ya ju asili ya kesi | lisi ya Kesi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | mishna ZRB v/s Talib oud na Said Bakari A | 2021 ya ehe 3 Machi 21 iliyopo Iahakama Kuu Vuga ). | bainika kuwa agatim General pplier alidai fidia toka ZRB ya shiling lioni 758 kwa | B ililipa faini shilingi milioni 0 kama fidia hasara hiyo ada ya kubaini |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | sara iliyopatikana tokana na maofisa ZRB kushindwa shughulikia mali lizozikamata na pelekea uharibifu. | wa hasara hiyo ababishwa maofisa wa B wakati wa kamata mali o na kesi hiyo do inaendelea skilizwa. |
| 2 | gioma Ltd T/A New M ue Hotel v/s Kamishn B. | /2020 ya ehe 26 bruari 2021 opo (Bodi ya fani). | rufani anapinga muzi wa Kamishna kufuta usajili Biashara yake nyume na sheria. | si hiyo ilijadiliwa ya Mahkama nbapo mkata faa alisajiliwa ini ya kitengo a walipa kodi VAT. Kwa hivyo B ilishindwa tika kesi hii. |
| 3 | eid Mwinyi Mlenge V mishna ZRB V/s Khar ndu Haji | /2017 ya ehe 8 Julai 17 iliyopo Iahkama Kuu - ga.) | alamikaji anadai ia kutoka ZRB nye thamani ya ilingi milioni 92 kw badilisha umiliki w ajili wa gari kinyum | Mahakamani endelea sikilizwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kanuni na taratibu usajili. | |
| 4 | ıow Inn Hotel v/s mishna B | /2017 ya rehe 27 bruari 2017 il- ɔpo (Mahkama u – Vuga.) | alamikaji anadai ia kutoka ZRB ya ilingi milioni 120 hasara iliyotokana kufungwa kwa ashara yake ya teli kinyume na ratibu zilizowekwa ZRB. | ɔ Mahakamani aendelea sikilizwa. |
| 5 | ashallah Shipping .ltd V/s mishna ZRB | /2019 na /2021 ipo ɔdi ya Rufani) | alamikaji anadai ia kutoka ZRB ya ilingi milioni 200 ya hasara iliyotoka mauzo ya mafuta petroli kutoka kwa ananchi. | ɔ Mahakamani aendelea sikilizwa. |

**Chanzo: Daftari la kusajili kesi kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2021**

Ukaguzi umebaini kuwa ingawa Bodi ina kitengo imara cha sheria chenye uwezo wa kusimamia kesi mbalimbali, ushahidi wa kujiridhisha kwamba kitengo cha sheria kilihusika au kushauriwa ili kutoa ushauri wa kisheria wa namna ya kushughulikiwa

vyema hatua mbali mbali juu ya usimamizi mzuri wa utekelezaji wa TAPA kwa viongozi husika katika hatua za mwanzo za kesi hizo kwa lengo la kupunguza malalamiko kwa walipa kodi, kusimamia haki za walipa kodi na kuongeza mapato kwa Serikali Kuu haukupatikana.

Kutokana na kitendo cha kushindwa kutekeleza sheria za TAPA N.7 ya mwaka 2009 (R.E 2013) na taratibu nyinginezo mambo yafuatayo huenda yakajitokeza:-

- Bodi (ZRB) huenda ikaendelea kupata hasara kubwa ya fedha za Serikali kupitia fidia iliyosababishwa na uzembe uliotokana na ukiukwaji wa sheria hiyo.
- Haki za walipakodi zinaweza kuhujumiwa na wafanyakazi wasiowajibika wakati wa kuweka hatua za utekelezaji zinazochangia kuharibu sifa ya ZRB mbele ya umma na kukatisha tamaa utamaduni wa walipakodi wa kufuata kulipa kodi kwa hiari; hivyo kupoteza mapato ya Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB ihakikishe kuwa maafisa wa ZRB wanaohusika na hatua za utekelezaji wanatekeleza majukumu yao kwa uadilifu wa hali ya juu na uangalifu unaostahili kwa kuzingatia sheria na taratibu za TAPA NA.7 ya 2009 (R.E.2013). Utumiaji wa huduma za kisheria katika hatua za mwanzo za utekelezaji unapendekezwa zaidi ili kulinda Bodi dhidi ya hasara ya uzembe, kulinda haki za walipa kodi na sifa ya Bodi mbele ya umma. Zaidi ya hayo, watumishi watakaobainika kutumia madaraka yao vibaya kinyume na sheria na kanuni za kodi wanapaswa kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

## Majibu ya Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar (ZRA)

Ni kweli ZRA wakati wa kipindi cha ukaguzi kulikuwa na changamoto ya watendaji kutokufuata Sheria za Usimamizi wa Kodi. Kutokana na sababu hiyo ZRA inaelewea kuwa suala hili linatatuliwa na utoaji wa elimu ya usimamizi wa Sheria za Kodi kwa Watendaji wake na ni suala endelevu. Mamlaka inafanya kazi ya kutoa elimu kwa Watendaji wake kupitia mafunzo ya muda mfupi, mafunzo ya ndani pamoja na kupata uzoefu baina ya watendaji. ZRA ilikuwa ikitekeleza suala hilo na inaendelea kulitekeleza ili kuongeza weledi wa usimamizi wa Sheria za Kodi ikiwemo TAPA, Nam. 7 ya 2009, pamoja na kujenga uadilifu wa watumishi. Aidha, moja ya jukumu kubwa la ZRA ni kuwatendea haki walipakodi wakati wa usimamizi wa Sheria za TAPA ikiwemo kutokutoa maamuzi kinyume na Sheria ambapo hupelekea Serikali kutokupata hasara na kupunguza migogoro ya kikodi. Kwa sasa Weledi wa Usimamizi wa TAPA umeongezeka na unaendelea kuongezeka ili kutenda haki kwa walipakodi na kutoingiza hasara kwa Serikali.

**Jadweli namba 2**

**Hali ya sasa ya kesi zilizoorodheshwa katika jadweli namba 39**

| **am.** | **/anaoshtakiana** | **ambari ya esi** | **laelezo mafupi ya u ya asili ya kesi** | **ali halisi ya Kesi** | **ALI YA SASA** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | amishna ZRB v/s Ta boud na Said Bakari Ali. | /2021 rehe 3 Mac )21 iliyopo lahakama uu–Vuga. | bainika ku yagatim Gene upplier alidai fic utoka ZRB ya shilin ilioni 758 k asara iliyopatika utokana na maofi a ZRB kushind | RB ililipa faini ilingi milioni 1 va Kampuni yagatim Gene uppliers kama fic hasara hiyo baa kubaini kuv asara hi | esi hii imeshamaliza adaiwa wametakiv ulipa ZRA kiasi c ilingi )0,081,000/= kwa hasa yopatikana. Aidh /adaiwa hawa wameka |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | ushughulikia m alizozikamata upelekea uharibifu. | sababishwa aofisa wa Z akati wa kukama ali hizo na kesi hi ado inaendel uskilizwa. | ufaa katika Mahkama ufaa Tanzania kv tokukubaliana aamuzi ya Mahkar uu. |
| 2 | agioma Ltd T/A New N ue Hotel v/s Kamish RB. | 1/2020 rehe ebruari 20 yopo (Bodi ufani). | rufani anapin amuzi wa Kamishna a kufuta usajili v ashara yake nyume na sheria. | esi hiyo ilijadiliwa e ya Mahkar mbapo mkata ufaa alisajiliwa nini ya kitengo na walipa kodi a VAT. Kwa hivyo RB ilishindwa atika kesi hii. | esi hii ilijadiliwa nje ahkama ambapo Mka ufaa alikubalika kusajiliv atika wigo wa Kodi ngezeko la Thama VAT). |
| 3 | beid Mwinyi Mlenge V/s amishna ZRB V/s Khan andu Haji. | 3/2017 rehe 8 Jul 017 iliyo Mahkama Ku uga. | lalamikaji anad dia kutoka ZRB yen amani ya shilin ilioni 92 kv ubadilisha umiliki v sajili wa gari kinyun a kanuni na tarati a usajili. | o Mahakama aendelea usikilizwa. | o Mahakama aendelea kusikilizwa. |
| 4 | how Inn Hotel v amishna RB. | 7/2017 ya rehe 27 ebruari 20 opo | lalamikaji anadai dia kutoka ZRB ya hilingi milioni 120 a hasara iliyotokana a kufungwa kwa | o Mahakamani aendelea usikilizwa. | o Mahakama aendelea kusikilizwa. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mahkama uu – Vuga.) | ashara yake ya oteli kinyume na ratibu zilizowekwa a ZRB. | | |
| 5 | lashallah Shipping Co.ltd /s amishna ZRB | 2/2019 na 4/2021 ipo odi ya Rufan | llalamikaji anadai dia kutoka ZRB ya ilingi milioni 200 va hasa yotokana a mauzo ya mafuta a petroli kutoka kw ananchi. | o Mahakamani aendelea usikilizwa. | o Mahakama aendelea kusikilizwa. |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hioja hii imebaini kuwa Mamlaka ina uwezo mdogo kitaaluma katika kutekeleza Sheria ya TAPA Na.7 ya mwaka 2009 (R.E 2013) hali iliyopelekea kesi nyingi zilizotokana na kushindwa kwa Maofisa wa ZRB kufuata Sheria na taratibu zilizoainishwa kwa mujibu wa Sheria ya kodi TAPA Na.7 ya mwaka 2009 (R.E 2013) wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Hata hivyo, Mamlaka imeshachukua hatua ya kurekebisha dosari hiyo kwa kutoa mafunzo kwa watendaji wake ili kuongeza uwezo wa kusimamia vyema Sheria za Kodi ikiwemo TAPA, Nam. 7 ya 2009, pamoja na kujenga uadilifu wa watumishi ikiwemo kutokutoa maamuzi kinyume na Sheria ambapo kunapelekea Serikali kupata hasara na kuongeza migogoro ya kikodi.

**Mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na jitihada nzuri zilizochukuliwa na Mamlaka katika kutatua changamoto ya Utekelezaji wa Sheria ya TAPA Na.7 ya mwaka 2009 hata hivyo Kamati inaishauri Mamlaka kutimiza ahadi yake ya kutoa mafunzo kwa Watendaji wake kupitia mafunzo ya muda mfupi, mafunzo ya ndani pamoja na kupata uzoefu baina ya watendaji kuwa ni suala endelevu ili kuongeza weledi wa usimamizi wa Sheria za Kodi ikiwemo TAPA, Nam. 7 ya 2009 kwa lengo Serikali kutopata hasara inayotokana na Mamlaka kushidwa katika kesi za kodi Mahakamani.

Aidha, kwa kesi ambazo bado zinaendelea kusikilizwa Mahakamani Kamati inaishauri Mamlaka kufuatilia kwa karibu kesi hizo ili zipatiwe ufumbuzi ikiwa ni ndani ya Mahakama au usuluhishi nje ya Mahakama kwani kuendelea kuwepo kwa kesi hizo kutaendelea kupoteza rasilimali ya muda na fedha kwa upande wa Mamlaka katika kufuatilia kesi hizo.

**5.2.9.7 Madhara ya kisheria ya kukatishwa kwa Mkataba ulioingiwa kati ya ZRB dhidi ya Norway Rejesta Development and Associates USD 1,352,622 (Bila ya VAT)**

Katika mapitio ya utekelezaji wa mkataba ulioingiwa kati ya ZRB na DEVAS tarehe 24 Juni, 2019 (mkataba wa awali) kwa muda wa miezi 18 kuanzia tarehe 24 Juni 2019 hadi tarehe 23 Desemba 2020 (pamoja na kipindi cha dhima ya uharibifu cha miezi 12) kwa malipo USD 1,352,622 (Bila ya VAT) kwa huduma za ushauri kwa ajili ya maendeleo na utekelezaji wa EFD - Virtual Fiscal Devices Management System (VFDMS). Kutokana na ugonjwa wa janga la Corona kandarasi hiyo iliongezwa muda kuanzia tarehe 22 Januari , 2021 kwa miezi mingine 15 (pamoja na kipindi cha dhima ya uharibifu cha miezi 12) inayotarajiwa kukamilika Aprili, 2022.

Ukaguzi umebaini katika mapitio ya kumbukumbu (Muhtasari wa kumbukumbu za mkutano wa Bodi ya Wakurugenzi Na. 267 uliofanyika tarehe 27 Machi 2021, ripoti ya kamati iliyoundwa kupitia upya sheria na masharti ya mkataba na barua mbalimbali) yalibaini mwenendo usioridhisha wa utekelezaji wa mkataba kati ya pande hizo mbili uliopelekea ZRB kuamua kusitisha mkataba. Ilibainika kuwa ZRB inakusudia kusitisha mkataba huo kwa madai kuwa Mshauri huyo alikiuka mkataba kwa kushindwa kuutekeleza kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa (TOR). ZRB inadai kuwa mfumo ulioundwa ulikuwa kinyume kabisa na Masharti ya Mkataba (TOR).

Mapitio ya masharti ya mkataba yamebaini kuwa kusainiwa kwa Ripoti ya Uanzishwaji, Ripoti ya Tathmini ya Msingi na Ripoti ya Usanifu wa Mfumo ni maeneo ambayo yanaonekana ndio chanzo cha mgogoro unaotokana na ZRB kutokuwa makini wakati wa utekelezaji wa mkataba huo kuwa ndio wenye dosari kwenye mfumo ilibainishwa wakati wa hatua ya majaribio. Ushahidi kwamba kutiwa saini kwa hati hizo tatu muhimu kulihusisha wafanyakazi wa kiufundi (Idara ya ICT, timu iliyoteuliwa kuandaa TOR na watendaji wengine). Hata hivyo imebainika ushahidi wa watumiaji wa mfumo kushirikishwa kabla ya kusainiwa kwa hati hiyo ili kupata mapendekezo yao haukupatikana.

Aidha, mapitio ya mgongano huo unaoelekea kwenye kuvunjika kwa mkataba yameonesha kuwa jitihada mbalimbali zimefanywa na Bodi ya Mapato ikiwemo kuwasiliana na ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) kuomba kupatiwa ushauri wa kisheria juu ya njia nzuri na bora ya kuvunja mkataba kwa amani bila ya gharama au kwa gharama ndogo (barua yenye kumbukumbu namba ZRB/M.32/VOL.III/106 ya tarehe 19.07.2021 inahusika). Mwanasheria mkuu aliijibu barua hio kupitia (barua yenye kumbukumbu namba L.D 907/VOL.IV/74 ya tarehe 4 Agosti 2021). Ili kufuata

maagizo ya Mwanasheria mkuu Bodi ya Mapato iliandika barua kwa Katibu Mkuu ofisi ya Raisi Fedha na Mipango yenye kumbukumbu namba ZRB/M.45/2/VOL.III/41 ya tarehe19 Agosti, 2021. Mwanasheria alitegemea kukamilisha taratibu za uvunjwaji wa mkataba haraka iwezekanavyo mara atakapopokea majibu kutoka Wizarani ambapo bado hayajajibiwa.

Ukaguzi umebaini pia kwamba kukosekana kwa umakini kwa upande wa uongozi wa Bodi ya mapato katika hatua za mwanzo za utekelezaji wa mkataba huo ndiko kulikopelekea kuvunjika kwa mkataba.

Dhamira ya kutaka kuvunja mkataba huenda ikapelekea uwepo wa upotevu mkubwa wa fedha za Serikali endapo matokeo ya kuvunja mkataba yatageuka dhidi ya upande wa Bodi ya Mapato.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB kuwa makini katika kuhakikisha kwamba mchakato wa utekelezaji wa mkataba unakuwa shirikishi kuanzia mwanzo hadi mwisho (ukihusisha wafanyakazi wa kiufundi na watumiaji wa mfumo). Hali hii itarahisisha utekelezaji wa mikataba bila migogoro na kufikia thamani ya fedha zilizotumika kupata mfumo.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato ZRA**

ZRA inaona iko sahihi katika maamuzi yake ya kukatisha mkataba NRD kwa wao kushindwa kutekeleza mkataba kama tulivyokubaliana. Hata hivyo, ili kuepuka kuleta usumbufu kwa wawekezaji lakini hasara zinaweza kutokezea kwa kesi iliyopo (contingent liability), ZRA ipo katika hatua ya mazungumzo na Mshauri elekeze ili kutatua mgogoro uliopo, nje ya Mahakama.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati inakubaliana na hatua zilizochukuliwa na Mamlaka za kuvunja Mkataba huo kwa vile mkandarasi ameshindwa kutekeleza masharti yaliyowekwa ndani ya (TOR) na kupelekea kuundwa kwa mfumo wenye dosari kadhaa ambao hautaweza kukidhi haya matumuzi ya Mamlaka.

Hata hivyo Kamati inaishauri Mamlaka kuendelea kufanya mazungumzo ambayo yapo nje ya mahakama na Mkadarasi huyo ili suluhu na kwa vile Mamlaka tayari imeshapata ufumbuvi kwa kuunda mfumo mwengine ambao unafanya kazi zinazofanana na mfumo huo ambao umetengenezwa na wataalamu wa ndani wa ZRA.

**Mapendekezo ya Kamati**

Aidha Kamati inaisisitiza Mamlaka kuwa makini katika kufunga mikataba kwa kuunda timu ya kitaalamu kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao katika kusimamia mikataba ya Tehama. Kwa vile dosari zote zilizotekea katika mkataba huu zimetokana na Mamlaka kutokuwa makini katika kushiriki ipasavyo katika hatua za mwanzo za ujenzi wa mfumo hadi kufikia hatua ya makabidhiano hali iliyopelekea kujitokeza kwa mgogoro huu.

### 5.2.9.8 Kuongezeka kwa mwenendo wa Pingamizi zilizotolewa kwenye tathmini ya Kodi

Katika mapitio ya tathmini ya kodi iliyotolewa imebaini kuwa baadhi ya walipa kodi walikasirishwa na tathmini zilizotolewa na kuweka pingamizi. Ilibainika zaidi kuwa baadhi ya pingamizi zilizotolewa hazikuweza kutatuliwa kwa amani na wahusika walikimbilia mahakamani. Imebainika kuwa mapingamizi mengi yaliyotolewa yaliishia kwa walipakodi kushinda kwani kiasi cha tathmini ya kodi kinaweza kupunguzwa kwa

kiwango kikubwa baada ya mapitio na yale ya mashauri mahakamani mengine yalizingatiwa kujadiliwa nje ya mahakama ili kumaliza suala hilo kwa makubaliano.

Tathmini nyingi za kodi zilizobishaniwa zilionekana kutokana na tathmini zisizo sahihi kama ilivyobainishwa baada ya mahojiano na maafisa wanaowajibika na upitiaji wa baadhi ya mafaili ya walipa kodi zenye ripoti za ukaguzi wa kodi. Ushahidi wa iwapo taratibu za ukaguzi wa kodi ikiwa ni pamoja na kutuma barua za taarifa kuhusu kuanza ukaguzi, kufanya vikao na walipakodi (mikutano ya awali na ya mwisho) ili kuwasilisha matokeo ya ukaguzi wa kodi kabla ya kutoa tathmini za mwisho hazikuwepo katika kumbukumbu za walipakodi. Kesi chache zilizochaguliwa kwa madhumuni ya kielelezo zimeonyeshwa katika Jadweli hapo chini:-

Pamoja na ukweli kwamba pingamizi nyingi zilizotolewa ziliishia kuwapendelea walipakodi, hata hivyo, ushahidi wa kuthibitisha kwamba Bodi imefanya utafiti wa kina ili kujitathmini ni wapi ZRB imekosea ili kupata suluhu ya tatizo hilo ili kupunguza idadi ya mapingamizi na mashauri ya mahakama yanayotokana na tathmini ya kodi yenye mgogoro ulikosekana.

Kukosekana kwa umakini wa makisio ya tathmini ya ulipwaji wa kodi kwa walipa kodi unaweza ukapelekea:-

- Kuongezeka kwa mapingamizi ya kodi kutokana na ukiukwaji wa taratibu za ukaguzi kunasababisha kupungua kwa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa wakati.
- Iwapo wafanyakazi walikosa umahiri uliohitajika katika kutathmini kodi na au kutofuata sheria na kanuni za TAPA NO.7 ya 2009 (R.E. 2013) wakati wa tathmini ya kodi haikuweza kufahamika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB kutafuta sababu kuu za ongezeko la mapingamizi ya kodi kwa nia ya kuchukua hatua za kurekebisha ili kupunguza mwelekeo wa mapingamizi, kuimarisha uzingatiaji wa kulipa kodi kwa hiari na kuongeza mapato ya Serikali. Uzingatiaji wa sheria na taratibu za kodi wakati wa ukaguzi wa kodi unasisitizwa zaidi.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Mamlaka ilikuwa na pingamizi ya kodi kwa wafanyabiashara wawili tu, ambao ni Abdulsalam building contractors na Frasi co. Ltd ambao wameshalipa deni lote.

Aidha, kwa wafanyabiashara waliobakia waliorodheshwa na mkaguzi katika jadweli waliwasilisha pingamizi isipokuwa pingamizi zao hazikuwa halali kutokana na walipa kodi hao kutofata masharti ya kuwasilisha pingamizi ya kodi ndani ya siku thelathini baada ya hati ya makisio ya kodi kuwasilishwa na kuwasilisha moja ya tatu (1/3) ya kodi asiyoikubali kama Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya 2009 kifungu cha 21A (8) kinavyoeleza kama inavyoonekana katika jadweli namba 3.

**Jadweli namba 3.**

**Hali ya sasa kwa pingamizi mbali mbali zinazolalamikiwa na kutolewa na walipa kodi katika Jadweli namba 40.**

| **ngamizi za Walipa Kod** | **aelezo ya Tathmini** | **wango cha Ko lichopigwa** | **asi cha k yokubaliwa ılipwa baada kaguzi** | **asi cha k lichoondolev** | **li ya Sasa** |
|---|---|---|---|---|---|
| odul Salam uilding (Tz) ontract–Mwera | RB/N.3/VOL.1V/12 ssessment Of Vat No: 1 /08/2020 eriod: Jan 2019 - Febr | Tshs.13,611,459. | hs. 11,439,400 | hs.2,172,072 | ngamizi iliwasilishwa na ameli oja ya tatu ya deni. Kwa barua rehe 31/10/2020 na ameom ısamehewa adhabu na ri |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | )20 | | | | nbapo alisamehewa adhabu h. 2,172,072.69 na kutaki lipa riba na kodi halisi. De neshalipwa kwa risiti nam 859289, E:832523, E:8722 089607, E:283024 |
| awaii Clearing Forwading - swandui | RB/N.3/VOL.1V/16 ssessment Of Vat No: 1 /09/2020 eriod: Jan 2018 - Dec )19 | Tshs.19,212,744. | hs. 16,771,000 | hs.2,441,722 | eni la Tshs. 16,771,000. nemaliza kulipwa kwa ri amba: E:854050, E:8450 833414, E:0896608 na T 441,722.40 zimesamehewa. |
| uality Building ontractors - ombasa | RB/N.3/VOL.1V/17 ssessment Of Vat No: 1 /09/2020 eriod: Oct 2018 – Ju )19 | Tshs.53,301,557. | hs. 44,454,254 | hs.8,956,171 | eni la Tsh. 44,454,254. nemaliza kulipwa kwa ri amba: E:837366, E:842974, 58003. Mlipakodi amesamehe dhabu na riba kwa barua yen umbukumbu N RB/CON/Q.1/VOL.I/58 ya tare 7.01.2021. |
| arajani General res. - Darajani | RB/N.3/VOL.IV/28 ssessment Of Vat No. 2 )/11/2020 eriod: July 2017 – Jur )20 | Tshs.28,076,698. | hs. 21,836,800 | hs.6,239,849 | lipakodi aliomba kusamehe dhabu na riba kwa barua rehe 5/03/2021 amba isamehewa adhabu yote na ri va asilimia hamsini kwa bar enye kumbukumbu RB/TR/D.2/VOL.I/15 ya tare 3/03/2021. Deni limeshalipwa k siti no: E:049536, E:8823 882373, E:068909, E:08050 859677, E:0902697. |
| ergreen (Z) | RB/N.3/VOL.IV/62 | Tshs.98,916,868. | hs. 77,419,626 | hs.21,497,17 | lipakodi aliomba kusamehe |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| aders - Malan-<br>ege | ssessment Of Vat No: 6<br>/03/2021<br>eriod; Aug 2018 – Dec,<br>)20 | | | ) | lhabu na riba kwa barua<br>rehe 21/04/2021 amba<br>isamehewa adhabu yote na ri<br>va asilimia hamsini kwa bar<br>enye kumbukumbu N<br>RB/TR/E.21/VOL. I/23. De<br>neshalipwa kwa risiti r<br>0904434, E:0910103. |
| vergreen (Z)<br>mited - Malan-<br>ege | RB/N.3/VOL.IV/61<br>ssessment Of Vat No: 6<br>/03/2021<br>eriod; Aug 2018 - Dec<br>)20 | Tshs.166,776,780. | hs 130,657,365 | hs<br>5,119,415.21 | lipakodi aliomba kusamehev<br>lhabu na riba kwa barua<br>rehe 21/04/2021 amba<br>isamehewa adhabu yote na ri<br>va asilimia hamsini kwa bar<br>enye kumbukumbu N<br>RB/TR/E.20/VOL.I/37. De<br>neshalipwa kwa risiti r<br>0904433, E:0919348. |
| asi Com.Ltd | RB/N.3/VOL.1V/74<br>ssessment Of Vat No. 7<br>/04/2021<br>eriod: Jan 2019 - Nov<br>)20 | T<br>69,697,506. | shs 52,273,129.83 | hs<br>7,424,376.61 | lipakodi aliwasilisha pingamizi<br>aada ya hapo alikata rufaa kut<br>odi ya Rufaa za Kodi amba<br>ahkama iliamua ZRA na Fr<br>akubaliane nje ya Mahkama.Z<br>msamehe adhabu yote na asilim<br>) ya riba kwa barua yen<br>umbukumbu nam<br>RB/TR/F.19/VOL.II/18.Hata hiv<br>lipakodi amemaliza malipo yo<br>va risiti namba<br>0987996, E:103449<br>0992489, E:0983997, E09738<br>0967709, E:1048988, E:10625 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 221883 |
| ddy Co. Ltd | | USD 482,046. | | | lipakodi ameanza kulipa U ),191.16 kwa risiti no: E:109008 1078791 baada ya kuchukuliv atua za ugomboaji kwa kupi tu wa tatu (third party). Bak yobaki ni USD 401,855.39 amba aendelea kufuatiliwa. |
| ıllah Motors d | | Ts 32,787,4 | | | lipakodi ameahidi kulipa deni la dani ya mwaka 2022/2023. |
| ıwiya Tanzania aders | | Ts 439,730,311. | | | RA ilimtaka alipe deni lake lo va barua yenye kumbukumbu N RB/TR/Z.1/VOL.I/50 ya tare /07/2022. |
| ecol Corpora- on | | U 3,018,770. | | | RA inaendelea kufuatilia deni h va barua zenye kumbukum am. ZRB/CON/S.25/ VOL.II RB/CON/S.25/ VOL.II/9 RB/CON/S.25/ VOL.II/10. |
| hudi Holding d, - Mkoani emba | RB/N.3/VOL.1V/72 ssessment Of Vat No. 7 5/04/2021 eriod: Jan 2018 – Aug, )20 | Tshs. 923,100,6 | | | RA ilipokea pingamizi amba aikukidhi vigezo kwa kuv lipakodi hakutimiza masharti ılipa moja ya tatu (1/3). Ha vyo, ZRA inaendelea kuwasilia a mlipakodi huyu ili kufil uafaka wa deni hili. |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa Mamlaka imeshachukua jitihada ya Kufuatilia pingamizi hizo ambapo Kamati imearifiwa kuwa Pingamizi zilikuwa ni za wafanya biashara wawili tu ndio waliokidhi vigezo vya pingamizi na wameshalipa madeni yao yote na kwa wale ambao wameorodheshwa na Mkaguzi yalikuwa ni madeni ambayo yametokana wafanyabiashara kuwa kiwango duni cha elimu kwa walipa kodi jambo ambalo linapelekea kuongezeka kwa kesi nyingi za pingamizi za kodi hata hivyo wameshidwa kutekeleza masharti ya pingamizi ya kodi na hatimae kukubaliana na Mamlaka kulipa madeni yao na kwa kiasi kikubwa wameshamaliza kulipa madeni hayo

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Mamlaka kuchukua hatua za haraka kwa kuweka mfumo mzuri ambao hautokua na dosari katika kukadiria kodi ambapo pande zote mbili zitaridhika na kiwango cha kodi kitakachokadiriwa.

Aidha Kamati inaishauri Mamlaka kutoa elimu zaidi kwa walipa kodi kwa vile walipakodi hao huwa hawana uelewa wa kutosha juu ya masuala ya kodi na hupelekea kuweka pingamizi zisizokuwa na msingi na hatimae kushidwa kukidhi vigezo pingamizi na kupelekea Mamlaka kukosa mapato yake kwa wakati husika.

**5.2.9.9 Kutokufanyika kwa Ukaguzi wa Kodi kwa muda mrefu**

Ukaguzi wa kodi unaweza kuwa na jukumu kubwa katika kuboresha usimamizi wa kodi na kuzingatia walipa kodi kwa ujumla kwa kuhusisha tabia zao. Hata hivyo, mapitio yanaonesha kuwa kaguzi nyingi zilizofanywa zilihusisha vipindi virefu vya ukaguzi vya zaidi ya miaka mitatu nyuma na kupelekea tathmini kubwa za kodi. Sababu za kufanya

kaguzi za vipindi virefu badala ya vipindi vifupi (mwaka mmoja) hazikuweza kuthibitishwa. Baadhi ya kesi zenye tathmini kubwa za kodi zimeoneshwa katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 41: Baadhi ya kesi zenye tathmini kubwa za kodi ambazo bado hazijalipwa**

| a la Mlipa Koc | Nambari ya Kumbukumbu ya Tathmini | Muda uliofanyiwa ukaguzi | athmni iliyotolew (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| nset Beach ngalow - Kend ngwi | 3/N.3/VOL.V/07 sessment Of Hotel Le : 07 01/07/2020 | 2017 - Dec 2020 | 661,128.01 | aka 3 na miezi 6. |
| uslim Nurdin nailjee – andege | 3/N.3/VOL.1V/11 sessment Of VAT No: /08/2020 | 2017 - Jun 2020 | 897,500.00 | aka 3 na miezi 6. |
| pha General nders - Kinazin | 3/N.3/VOL.V/09 sessment Of VAT No /06/2021 | 2016 -Nov 20 | 871,655.46 | aka 5 |
| rumaru Hotel l - Forodhani | 3/N.3/VOL.V/12 sessment Of VAT No. /06/2021 | y 2015 - Nov 202 | ,964,307.21 | aka 5 |
| mi Ali Makam andege | 3/N.3/VOL.1V/14 sessment S/Duty No: /09/2020 | 2017 - Jun 2020 | 492,400.24 | aka 3 na miezi 6 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| con Traders - andege | B/N.3/VOL.IV/49 sessment Of VAT No: /01/2021 | 2016 - Nov 2020 | 098,086.19 | Miaka 5. Aidha ripoti ya aguzi wa kodi onesha kuwa ukaguzi wa visho kabla ukaguzi wa sasa ulifanyika uari 2009 di disemba 2012 years. Kukosekana kwa ushah kufanya tathmini ya ulipaj kodi katika kipindi cha vaka 2013 hadi 15. |
| ribu Glocery - kunazini | B/N.3/VOL.IV/54 sessment Of VAT No: /01/2021 | 2016 - Nov 2020 | 417,099.22 | aka 5 |
| ergreen (Z) nders Malandege | B/N.3/VOL.IV/62 sessment Of VAT No: /03/2021 | g 2018 - Dec 2020 | 916,868.86 | aka 2 na miezi 6. |
| ergreen (Z) nited Malandege | B/N.3/VOL.IV/61 sessment Of VAT No: /03/2021 | g 2018 - Dec 2020 | 5,776,780.21 | aka 2 na miezi 6. |
| rahman Ismai ai M/Ladu | B/N.3/VOL.IV/56 sessment Of VAT No: /03/2021 | 2016 - Nov 2020 | 907,198.04 | aka 5. |

Kutokufanyika kwa ukaguzi wa ulipaji wa kodi kwa kipindi kirefu kwa wakati mmoja kunaweza kusababisha mzigo mkubwa wa kodi kwa walipa kodi na kusababisha hasara ya fedha za Serikali, kwani walipakodi wengi wanaweza kushindwa kulipa kodi

iliyotathminiwa na baadhi wanaweza kuamua kufunga biashara zao au kukimbia nchini na kupelekea mambo yafuatayo kubainika:-

- Ugunduzi wa mapema wa maeneo ambayo walipakodi wameshindwa kufuata sheria utashindikana.
- Mzigo mkubwa wa kodi husababisha kuongezeka kwa mizozo ya kodi ambayo inaweza kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.
- Kuongeza usumbufu kwa walipa kodi kutokana na upekuzi wa nyaraka za ukaguzi kuwa wa miaka mingi iliyopita ambapo baadhi ya taarifa hizo haziwezi kupatikana kwa mara moja.

Kwa vile lengo la ukaguzi wa kodi ni kuongeza ulipaji wa hiari kwa walipa kodi na kuongeza mapato kwa Serikali ukaguzi unashauri ni muhimu kwa Bodi kuhakikisha kuwa ukaguzi unafanyika kwa wakati ikiwezekana ndani ya mwaka, kwa walipa kodi wakubwa na wa Kati.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Ni kweli kaguzi zimekua zikichukua muda mrefu, katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, ZRA ilikuwa na jumla ya wakaguzi wanane (8) ambao walitakiwa kufanya ukaguzi kwa walipakodi zaidi ya 4,000. Uwepo wa wakaguzi wanane (8) ambao ni wachache umechangia kiasi kikubwa kutofanyika kwa kesi nyingi za ukaguzi ambapo jumla ya kaguzi 96 tu zilifanyika. Aidha, kwa mwaka 2022/2023, ZRA imeongeza wakaguzi ishirini na nne (24) na kufanya idadi ya wakaguzi kuwa thelathini na mbili (32) ambapo idadi ya kaguzi zinazotarajiwa kufanywa zimeongezeka na kufikia mia tano (500), ambapo zilizokamilika zimefikia mia mbili na thelathini na tatu (233) hadi kufikia mwezi Machi, 2023.

## Jadweli Nambari 4

## Hali ya sasa ya baadhi ya kesi zenye tathmini kubwa za kodi zilizo orodheshwa katika jadweli nambari 41

| a la Ml odi | mbari mbukumbu thmini | uda uliofanyi aguzi | thmni iliyotole shs) | ekelezaji | li ya sasa |
|---|---|---|---|---|---|
| nset Bea ngalow ndwa ngwi | B/N.3/VOL.V/07 sessment Of Ho vy No: /07/2020 | l 2017 - Dec 2020 | ,661,128.01 | dha hizi zililipwa kwa risiti nam 0979700, E:042128, E:003537 0017576 zenye jumla ya T ,772,700.00 na bakaa ya adhabu a ya S. 3,888,470.60 zilisamehewa k ujibu wa barua nam B/HT/S.3/VOL.1/71 ya tare /12/2021. | emaliza deni. |
| uslim Nur mailjee landege | B/N.3/VOL.1V/1 sessment Of V : 11 27/08/2020 | n 2017 - Jun 2020 | ,897,500.00 | dha hizi zililipwa kwa risiti nam 864539, E:865915, E:09961 879051, E:816933, E:8321 638310 na E:828298 zenye jumla S. 15,897,500.00. | emaliza deni. |
| pha Gene aders nazini | B/N.3/VOL.V/09 sessment Of V . 09 08/06/2021 | n 2016 -Nov 20 | ,871,655.46 | dha hizi zililipwa kwa risiti nam 0907741, E:981735, E:09508 0892887, E:0949021 na E:09679 nye jumla ya TZS. 23,871,655.46 | emaliza deni. |
| arumaru otel Ltd rodhani | B/N.3/VOL.V/12 sessment Of V . 12 25/06/2021 | ay 2015 - Nov 2020 | 1,964,307.21 | dha hizi zililipwa kwa risiti nam 0964289, E:0965909, E:09720 0982743, E:0992105, E:09878 1000870, E:1011934, E:10220 1034088 zenye jumla ya T 5,084,369.10 na bakaa ya adhabu a ya TZS. 56,880,118. isamehewa kwa mujibu wa bar mba ZRB/HT/M.2/VOL.1/87 | emaliza deni. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | rehe 11/10/2021. | |
| imi Ali akame - landege | B/N.3/VOL.1V/1 sessment S/Duty : 14 09/09/2020 | n 2017 - Jun 2020 | ,492,400.24 | dha hizi zililipwa kwa risiti nam 942754, E:836309, E:8505 870838, E:586444, E:08926 0893268, E:942754, E:09109 0955262 na E:0965901 zenye jum TZS. 21,166,000.00 na bakaa lhabu ya TZS. 3,326,394. isamehewa kwa mujibu wa bar mba ZRB/TR/M.507/VOL.1/3 rehe 16/09/2021. | emaliza deni. |
| lcon Trade landege | B/N.3/VOL.IV/49 sessment Of V : 49 25/01/2021 | n 2016 - Nov 2020 | ,098,086.19 | dha hizi zililipwa kwa risiti nam 0987780, E:0982473, E:09737 868307, E:0896733, E:09067 918117, E:843460, E:09507 0964448, E:0836043, E:0934687, X130090 zenye jumla ya T ,763,900.00 na bakaa ya adhabu a ya TZS. 6,334,326.47 zilisamehe va mujibu wa barua nam B/TR/F.3/VOL.1/31 ya tare /01/2022. | emaliza deni. |
| ribu Gloc Mkunazini | B/N.3/VOL.IV/54 sessment Of V : 54 27/01/2021 | n 2016 - Nov 2020 | ,417,099.22 | dha hizi zililipwa kwa risiti nam 0902613, E:0906860, E:09948 934535, E:0934875, E:09922 0987527, E:1004487, E:10128 1033110, E:1058657, E:10402 1046619, E:1058398, E:10810 1087889, E:1081261 na E:011905 nye jumla ya TZS. 19,519,000.00 | tua za ugomboaji kaa ya T ,952,099.22 zinaende chukuliwa. |
| ergreen (Z) aders Malandege | B/N.3/VOL.IV/62 sessment Of VAT : 62 17/03/2021 | g 2018 - Dec 2020 | ,916,868.86 | dha hizi zililipwa kwa risiti nam 0904434 na E:0910103 zenye jum TZS. 77,419,626.00 na bakaa lhabu ya TZS. 21,497,175. | emaliza deni. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | isamehewa kwa mujibu wa bar mba ZRB/TR/E.21/VOL.I/23 ya tare )/05/2021. | |
| ergreen nited Malandege | .B/N.3/VOL.IV/61 sessment Of V o: 61 17/03/2021 | ug 2018 - Dec 2020 | 6,776,780.21 | dha hizi zililipwa kwa risiti nam 0904433 na E:0910348 zenye jun TZS. 130,657,365.00 na bakaa dhabu ya TZS. 36,121,416. isamehewa kwa mujibu wa bar mba ZRB/TR/E.20/VOL.I/37 ya tare )/05/2021. | emaliza deni. |
| prahman mail Vuai M/Ladu | .B/N.3/VOL.IV/56 sessment Of V o: 56 05/03/2021 | n 2016 - Nov 2020 | ),907,198.04 | dha hizi zililipwa kwa risiti nam 0902646, E:918259, E:09149 932186, E:940225, E:09504 099495, na H205605 zenye jumla S. 21,175,683.45 na T 772,057.30 za adhabu na ri isamehewa kwa mujibu wa bar mba ZRB/TR/A.4/VOL.1/24 ya tare )/09/2021. | tua za ugomboaji kaa ya TZS. 2,959,457. naendelea kuchukuliwa |

**Uchunguzi wa Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kutofanya kaguzi za kodi kwa muda mrefu kutokana na uhaba wa wafanyakazi wa ukaguzi, hata hivyo Mamlaka imeweza kuchuchukua hatua kwa kuongeza wafanyakazi hao kutoka wanane (8) na kuwa thelathini na mbili (32) kwa lengo kuongeza kasi ya ukaguzi wa kodi.

Ongezeko hilo la wafanyakazi katika kitengo cha kaguzi za kodi zimeleta tija kwa kuwa kasi ya ukaguzi wa kodi imeongezeka kufikia mia tano (500), ambapo zilizokamilika zimefikia mia mbili na thelathini na tatu (233) hadi kufikia mwezi Machi, 2023.

Aidha Kamati imebaini kuwa walipakodi ambao wameorodheshwa na Mkaguzi tayari wameshafanyiwa ukaguzi na kufanyiwa tathmini ya madeni yao ambapo kwa sasa

wengi wao wameshamaliza madeni na hatua zaidi zinachukuliwa na Mamlaka za kugomboa madeni kwa walipakodi waliobaki ambao wameshafanyiwa ukaguzi wa kodi kama ilivyoonekana katika jadweli la majibu ya Mamlaka.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inishauri Mamlaka kuendelea kuchukua jitihada Zaidi ya kuendelea kuajiri wafanyakazi hao ili kukidhi haja ya kufanya kaguzi hizo kila mwaka badala ya hali ya sasa ya kufanya kaguzi za kodi baada ya miaka mitatu au zaidi hali inayopelekea changamoto kwa walipakodi kuwaongezea mzigo wa kodi ambao mwisho wa siku wanashidwa kulipa na kuisababishia hasara Serikali.

### 5.2.9.10 Mapitio ya pingamizi yaliyokosa ushahidi wa kukamilishwa kwa kesi

Mapitio ya ripoti za madeni ya kodi kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 ambayo yalipatikana kwa ajili ya ukaguzi yalibaini kuwa baadhi ya madeni ya kodi yaliyotokana na tathmini ya kodi ambayo ufuatiliaji wake wa urejeshaji ulidaiwa kuwa katika mchakato wa uhakiki kwa vile tathmini za kodi zilizotolewa zilikuwa na mzozo.

Hata hivyo, mchakato wa mapitio hayo ulionekana kuchukua muda mrefu zaidi kinyume na sheria ya usimamizi wa kodi TAPA namba 7 ya mwaka 2009 (R.E 2013) kwa kuwa hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha kuwa mapitio hayo yalikamilika na kwamba kodi iliyotakiwa ilikusanywa.

Kesi chache zilizobainishwa zimeonyeshwa kwenye jedwali hapo chini ambapo ukaguzi haukuweza kuthibitisha usahihi wa ulipaji wa madeni hayo ya kodi yaliyo katika mchakato wa mapitio.

**Jadweli Nambari 42: Mapitio ya pingamizi yaliyokosa ushahidi wa kukamilishwa kwa kesi**

| Mlipa Kodi | elezo ya tathmini | iasi kili- chokadiriw (Tshs) | si kilichowe l (Tshs) | Malipo yan- ay daiwa (Tshs) | elezo |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| C Eletrical<br>l Plumbing<br>Ltd - Mweni | /N.3/VOL.V/15<br>essment Of VAT No: 06<br>/2020<br>iod: Jan 2016 - May<br>0 | 11,502,777.45 | 0 | 11,502,777.45 | guzi<br>kodi<br>endelea. |
| sim Bakari Ali<br>ete Pemba | /N.3/VOL.IV/22<br>essment Of VAT No:22<br>10/2020<br>iod: 06/10/2020 | 119,716,441.33 | 0 | 119,716,441.33 | atiliaji<br>anyika<br>i ya ZRB<br>nba |
| sim Daud<br>man. -<br>ndege | /N.3/VOL.IV/37<br>essment Of S/<br>y No: 37<br>12/2020<br>iod: Oct 2017 - Oct<br>0 | 414,885.51 | 0 | 50,414,885.51 | guzi<br>kodi<br>endelea. |
| udi Holding<br>- Mkoani<br>nba | /N.3/VOL.1V/72<br>essment<br>/AT No. 72<br>04/2021<br>iod: Jan 2018 - Aug<br>0 | 923,100,607.69 | 0 | 923,100,607.69 | Ukaguzi<br>wa kodi<br>unaendelea. |
| v Jambiani<br>ch Hotel - Jambiani<br>w<br>dy) - Paje | /N.3/VOL.VI/09<br>essment Of Ho- tel Levy No: 09<br>07/2020<br>iod: Nov 2018 - Nov<br>9 | 92,286.16 | 0 | 92,286.16 | Ukaguzi<br>Va Kodi Unaendele |
| dys Place Ltd<br>je | /N.3/VOL.VI/08<br>essment Of Ho-<br>Levy No: 08<br>07/2020<br>iod: Jan 2014 - Dec<br>9 | 482,046.55 | 0 | 482,046.55 | Ukaguzi<br>Wa Kodi<br>Unaendelea. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| C Eletrical<br>l Plumbing<br>Ltd - Mweni | ;/N.3/VOL.V/15<br>essment Of VAT No:<br>06<br>/2020<br>iod: Jan 2016 - May<br>.0 | 247,904.64 | 0 | 247,904.64 | Ukaguzi Wa Kodi Unaendelea. |

Ukaguzi unashauri kutokana na uwepo wa mapitio ya pingamizi yaliyokosa ushahidi wa kukamilishwa kwa kesi ili kuthibitisha kuwepo, usahihi na kutekeleza hatua za ulipaji au kuzifuta ikiwa imethibitishwa kuwa zimetokana na kumbukumbu ambazo si sahihi baada ya kuzingatia taratibu zote zinazofaa za kufuta madeni.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Mamlaka ilikuwa na pingamizi ya kodi kwa wafanyabiashara watatu tu ambao ni Juhudi holding, New Jambiani beach hotel na Teddy place Ltd ambao hawakufuata masharti ya kuwasilisha malipo ya moja ya tatu (1/3) kwa mujibu wa Sheria ya usimamizi wa kodi namba 7 ya mwaka 2009 kifungu cha 21A(8).

Wafanyabiashara walioredheshwa katika jadweli nambari 42 hawakuwasilisha pingamizi na walikukuwa na madeni wanayostahiki kuyalipa. Kama inavyoonekana katika jadweli namba 5.

**Jadweli namba 5**

**Hali ya sasa ya pingamizi yaliyokosa ushahidi wa kukamilishwa kwa kesi yaliyo ainishwa katika jadweli namba 42**

| na la Mli odi | aelezo ya tathmin | asi k iokadiriwa ſshs) | asi kilicho wa (Tshs) | alipo yana aiwa (Tshs) | tekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| & C Eletrical nd Plumbing o. Ltd - Mwen | RB/N.3/VOL.V/15 ssessment Of V/ o:15 06 /10/202 eriod: Jan 2016-M 020 | 1,502,777.45 | | 1,502,777.45 | RA imechukua hatua ufuatilia deni hili kw arua yen umbukumbu Na RB/CON/J.6/VOL.I/12, RB/CON/J.6/VOL.I/17, RB/CON/J.6/VOL.I/21 |
| assim Bakari Vete Pemba | RB/N.3/VOL.IV/22 ssessment Of V/ o:22 06/10/2020 eriod: 06/10/2020 | 19,716,441.3 | | 19,716,441.33 | akuna pingam yowasilishwa ZRA lipakodi. Hatua gomboaji zinaendel uchukuliwa. |
| assim Daud thman- landege | RB/N.3/VOL.IV/37 ssessment Of S/Du o: 37 7/12/2020 Peric ct 2017 – Oct 2020 | 0,414,885.51 | | 0,414,885.51 | akuna pingam yowasilishwa ZRA lipakodi alitakiv ulipa deni lake lote. Ha madai za kumta ulipa deni h mewasilishwa kwa enye kumbukuml am. RB/TR/K.177/VOL.I/8, RB/TR/K.177/VOL.I/11 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| hudi Holding<br>d, - Mkoani<br>emba | RB/N.3/VOL.1V/72<br>ssessment Of V<br>o. 72 15/04/2021<br>eriod: Jan 2018 – A<br>020 | 23,100,607.( | | 23,100,607.69 | RA ilipokea pingam<br>mbayo haikukidhi vige<br>va kuwa mlipako<br>akutimiza masharti<br>ulipa moja ya tatu (1/<br>ata hivyo, Z<br>aendelea kuwasilia<br>a mlipakodi huyu<br>ufikia muafaka wa de<br>li. |
| ew Jambiani<br>each Hotel<br>mbiani (New<br>eddy) - Paje | RB/N.3/VOL.VI/09<br>ssessment Of Ho<br>evy No:<br>3/07/2020<br>eriod: Nov 2018<br>ov 2019 | 2,286.16 | | 2,286.16 | RA ilipokea pingam<br>mbayo haikukidhi vige<br>va kuwa mlipako<br>akutimiza masharti<br>ulipa moja ya tatu.<br>namo tare<br>1/12/2020 mlipako<br>ikata rufaa ya kodi k<br>odi ya Rufaa za Ko<br>anzibar. Hivyo, hoja<br>lipakodi ziliweke<br>ngamizi na ZRA<br>utakiwa kulipa deni<br>odi.<br>arehe 21/11/20<br>lipakodi amewasilis<br>arifa ya kukata rufaa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | odi, hivyo kesi yake i tika Baraza la Rufaa odi. |
| eddys Place L Paje | RB/N.3/VOL.VI/08 ssessment Of Ho- l Levy No: 08 3/07/2020 eriod: Jan 2014 – D 019 | 32,046.55 | | 32,046.55 | RA ilipokea pingam mbayo haikukidhi vige va kuwa mlipako akutimiza masharti ulipa moja ya tatu. arehe 9/9/20 lipakodi aliwasilis arifa ya kukata rufaa odi, hivyo kesi ya kuwa katika Mahakan a Rufaa. Aidh neamuliwa alipe deni odi. aada ya kuchukuliv atua za ugomboaji v eni kupitia mtu wa ta hird party) Mlipako meanza kulipa U 0,191.16 kwa risiti n 1090088, E:1078791. |
| & C Eletrical nd Plumbing o. Ltd - Mwen | RB/N.3/VOL.V/15 ssessment Of V o:15 06/10/202 | 47,904.64 | | 47,904.64 | RA imechukua hatua ufuatilia deni hili kv arua yen umbukumbu Na |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | eriod: Jan 2016 ay 2020 | | | | RB/CON/J.6/VOL.I/12, RB/CON/J.6/VOL.I/17, RB/CON/J.6/VOL.I/21 |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Mamlaka imekiri kuwepo kwa kesi za pingamizi za madeni kwa walipakodi wake ambapo pingamizi hizo ziliondolewa kwa kuwa hawakufuata masharti ya kuwasilisha malipo ya moja ya tatu (1/3) kwa mujibu wa Sheria ya usimamizi wa kodi namba 7 ya mwaka 2009 kifungu cha 21A(8).

Hata hivyo Mamlaka imeonesha jitihada ya kufatilia madeni hayo katika ngazi mbalimbali za Mahakama na baadhi ya kuwaandikia barua ya kulipa madeni yao hata hivyo bado muitikio wa kulipa madeni hao hauridhishi.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Mamlaka kuendelea kufanya jitihada ya kufuatilia madeni yake kwa ukaribu zaidi ili madeni hayo yaweze kulipwa kwa wale wote walioshidwa kukidhi masharti ya pingamizi na kuweka utaratibu mzuri wa kukadiria kodi ambazo hazitokuwa na migogoro baina ya pande mbili ili Mamlaka iweze kukusanya mapato yake kwa wakati bila ya usumbufu wowote.

**5.2.9.11 Madeni ya kodi ya muda mrefu yanayodaiwa na yasiyoweza kukusanywa chini ya Msamaha wa kodi (Tax Debts under Amnesty)**

Katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitangaza msamaha wa asilimia mia moja (100%) ya riba na adhabu kuhusiana na madeni ya kodi ya miaka ya nyuma kwa makundi yote ya kodi yaliyokuwepo hadi 31 Disemba 2019.

Kutokana na hali hiyo kipindi cha kutuma maombi na kulipa kodi chini ya msamaha kilipangwa kati ya tarehe 1 Julai, 2019 hadi 31 Desemba, 2019 na kuongezwa hadi tarehe 30 Septemba, 2020 kutokana na ugonjwa wa UVIKO

-19 ulioathiri uchumi duniani kote. Lengo la msamaha huo wa kodi lilikuwa ni kuongeza ukusanyaji wa mapato na ulipaji wa madeni ya muda mrefu ya kodi na kuwasaidia walipa kodi kulipa ada zao za kodi kwa wakati na kuongeza tija ya ulipaji kodi kwa hiari.

Hata hivyo, mapitio ya ripoti ya tathmini kuhusu athari za msamaha wa kodi katika ukusanyaji wa mapato iliyotayarishwa na Bodi ya Mapato katika mwaka wa ukaguzi unaoishia tarehe tarehe 30 Juni 2021 ulionyesha athari mbaya ya kutokulipwa kwa kodi za madeni ambapo ilibainika kuwa pamoja na jitihada zilizofanywa na Bodi ya Mapato kuwaondolea riba na adhabu walipakodi wenye madeni ya muda mrefu ya kodi kwa njia ya msamaha, wengi wa walipakodi walikuwa bado hawajalipa madeni yao hadi ukaguzi unakamilika.

Ukaguzi uliweza kufanya mahojiano na maofisa wanaohusika na ukusanyaji wa madeni na kubaini walipakodi waliomba msamaha lakini wakashindwa kujitokeza kulipa madeni yao walionekana kuwa yametokana na makosa ya mfumo na baadhi yalisababishwa na tathmini zisizo sahihi.

Madeni ya muda mrefu ya kodi ambayo walipa kodi walipewa idhini ya msamaha lakini wakashindwa kulipwa.

Aidha, ukaguzi umebaini kesi za madeni ya walipa kodi chini ya msamaha ambao walishindwa kulipa kutokana na makosa ya mfumo au na tathmini zisizo sahihi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 44: Walipa kodi chini ya msamaha ambao walipinga madeni yao kutokana na hitilafu za mfumo au tathmini zisizo sahihi**

| Namba | Mlipa Kodi | Kiasi cha fedha kinachodaiwa (Tshs | Kiasi cha fedha inachodaiwa (USD | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | RENA INN OURISM PROMOTIO | | 16,413 | ni lililoingizwa kimakosa katika mfumo wa ZI bapo mlipa kodi ewasilisha hati husika ili kufuta hitilafu. |
| 2. | HAA COMPANY | 3,861,493 | 6,829 | a mujibu wa kumbu kumbu za mlipa kodi onesha madeni ya kodi ya shilingi 2,912,528 D 1,598. |
| 3. | PHIA KAYOM- BO DENGE | 6,346, | | a mujibu wa rikodi za walipa kodi zina- ones ni halisi ni shilingi 696,350.98 wakati rikodi za umo wa ZITAS zinaone- sha deni ni shilingi 49,999.02 |
| 4. | RADISE BEACH BUN W(NUNGWI | | 42, | a mujibu wa kumbu kumbu za mlipa kodi aonesha USD 8,429 wakati mfumo wa ZITAS aonesha USD 42,080. |
| 5. | RICAN HOTEL | | 533, | a mujibu wa rikodi za mlipa kodi zinaonesha D 5,306.93 lakini mfumo wa ZITAS unaoenes ni hilo ni USD 508,121. |
| 6. | MTE BEACH | 402, | | pa kodi analalamika kuwa amepewa deni wa. |
| 7. | LLAH MOTOR LTS | 25,631, | | pa kodi alikadiriwa chini ya VAT wakati uhali kuwa amesajiliwa kwa kodi ya ushuru na amua kukimbia. |

Kutokana na majadweli niliyoyabainisha hapo juu yanaonesha utunzaji wa kumbu kumbu usioridhisha na tathmini zisizo sahihi zinapelekea mambo yafuatayo kubainika:-

- Kuna uwezekano mkubwa wa madeni yaliyo chini ya msamaha kuwa madeni hewa ambayo hayataweza kulipika.
- Uwepo wa madeni hewa hutoa taswira isiyo sahihi kwa Serikali na watumiaji wengine wa ripoti za mapato yanayotarajiwa ambayo hayatakusanywa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB kuhakikisha kunakuwepo na usahihi wa madeni ya kodi yaliyotokana na msamaha ili kurahisisha urejeshwaji wake na kutoa taswira ya madeni ya kodi iliyo sahihi kwa Serikali na umma kwa ujumla.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato (ZRA)**

Ni kweli kuna madeni ya muda mrefu ya wafanyabiashara ambayo yaliombewa msamaha wa kodi na hayakuweza kulipwa hadi ukaguzi ulipokamilika.

Hata hivyo, ZRA imeendelea kufanya ufuatiliaji wa usahihi wa madeni ya walipakodi na kuchukua jitihada ya kufuatilia madeni hayo ambapo kwa sasa yameshaanza kulipwa kama yanavyoonekana katika jedweli hapo chini.

Vile vile wapo baadhi ya walipakodi ambao wamekoma kuwasilisha ritani tokea mwaka 2018, 2019 na 2020 ambapo baadhi yao wamewasilisha barua za kufunga biashara.

Aidha kwa madeni ambayo yameshindwa kugombolewa, hatua za kisheria za kufuta madeni hayo zitachukuliwa kama inavyoonekana katika jadweli namba 6 na 7

**Jadweli namba 6**

**Hali ya sasa kwa madeni ya muda mrefu yenye Msamaha wa Kodi yaliyokuwa hayakulipwa nakuoredheshwa katika jadweli namba 43**

**Jadweli namba 7**

**Hali ya sasa ya Walipakodi chini ya msamaha ambao walipinga madeni yao kutokana na hitilafu za mfumo au tathmini zisizo sahihi nakuoredheshwa katika jadweli namba 44**

| mba | a la Mlipa Kodi | ısi cha fedha achodaiwa (Tshs) | ısi cha fedha achodaiwa (USD) | aelezo | li ya sasa |
|---|---|---|---|---|---|
| | RENA INN, TOURISM OMOTION | | 16,413 | ni lililoingizwa kimakosa katika mfumo wa TAS ambapo mlipa kodi ewasilisha hati husika ili kufuta hitilafu. | kweli deni hili liliingizwa katika mfumo kimakosa, kw a ZRA imeshasawazisha deni hili kupitia dokezo la ehe 18/09/2020. |
| | HAA COMPANY | 3,861,493 | 6,829 | a mujibu wa kumbu kumbu za mlipa kodi onesha madeni ya kodi ya shilingi 2,912,52 USD 1,598. | ni hili limetokana na malipo yake ya ritani ambalo ba ijalipwa, mlipakodi amepelekewa barua ya ukaguzi anza 05/05/2023 ambao utahusisha kukagua Usahil si cha deni ambacho hakijalipwa. |
| | PHIA KAYOM-BO DENGE | 6,346, | | a mujibu wa rikodi za walipa kodi zina-esha deni halisi ni shilingi 696,350.98 waka odi za mfumo wa ZITAS zinaone-sha deni ni lingi 5,649,999.02 | kweli mlipakodi ana deni halisi la kiasi cha 696,350.9 bapo hatua za ugomboaji zinaendelea pamoja na amba mlipakodi huyu aliwasilisha barua ya kufunga shara tarehe 1/09/2022 na kwa sasa biashara hio endeshwa na mfanya biashara mwengine. Hata hivy ongeza ya deni la makosa litafutwa kisheria. |
| | RADISE BEACH BUN W(NUNGWI | | 42, | a mujibu wa kumbu kumbu za mlipa kodi aonesha USD 8,429 wakati mfumowa ZITA aonesha USD 42,080 | tua za urekebishaji wa deni hilo pamoja na ugomboa aendelea. |
| | RICAN HOTEL | | 533, | a mujibu wa rikodi za mlipa kodi zinaonesh D 5,306.93 lakini mfumowa ZITAS aoenesha deni hilo ni USD 508,121. | pakodi huyu aliwasilisha ritani yenye kodi ya jumla y D 5,306.93, yakatokea makosa ya uingizaji wa ritani ngizwa jumla ya kodi USD 508,121.Aidha marekebis kosa yamefanywa kwa mujibu wa sheria na taratibu zopo. |
| | ITE BEACH | 402, | | ipa kodi analalamika kuwa amepewadeni wa. | ni la USD 216 limegombolewa tarehe 15/01/2021 k ti namba FK 137785, aidha deni lililoongezwa akosa la TZS 402,024 limerekebishwa kwa sawazishwa katika mfumo baada ya kubainika makos |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | iyojitokeza. |
| | LLAH MOTORLTS | 25,631,( | | ipa kodi alikadiriwa chini ya VAT wakati alisia alikuwa amesajiliwa kwa kodi ya ushu kuamua kukimbia. | thmini ya mlipakodi ilifanywa kwa wigo wa ushuru w mpu na sio VAT kupitia tathmini namba 36 ya tarehe /05/2019. Ugomboaji wa deni unaendelea ingawaje ethibitika mlipakodi ameamua kukimbia Zanzibar na funga biashara taratibu za ugomboaji zinaendelea. |

**Uchunguzi wa Kamati**

Mamlaka imekiri kuwepo kwa madeni ya muda yanayodaiwa na mengine ni vigumu kuyakusanya kutokana na Baadhi ya wafanyabiashara kufunga biashara na kukimbia nje ya Zanzibar na baadhi ya Madeni yametokana na hitilafu za mfumo kwa kutoa taarifa zisizo sahihi za madeni kama inavyoonekana katika jadweli la majibu ya hoja ya Mamlaka katika jadweli la 6 na 7.

Hata hivyo Mamlaka imeanza kuchukua jitihada ya kufuatilia madeni hayo na yapo baadhi yameshaanza kugombolewa jadweli na 6 linahusika na kufatilia madeni mengine hususan ya wafanyabiashara ambao wamefunga biashara zao **na kukimbilia nje ya Zanzibar jadweli namba 7 linahusika.**

**Mapendekezo ya Kamati**

Kwa Mamlaka imeshaanza kuchukua jitihada ya kurekebisha dosari hiyo hata hivyo Kamati inaishauri Mamlaka katika kuzingatia uwekaji mzuri wa kumbukumbu za madeni kwa wateja wake ili taarifa za madeni ziweze kupatikana kwa usahihi.

Aidha Kamati inaishauri Mamlaka kuwa na mifumo imara itakaoweza kutoa taarifa za madeni ya kodi kwa usahihi na ufanisi wa hali ya juu ili madeni hayo yaweze kulipika bila ya kuwa na mgogoro wowote kwa walipa kodi, na kwa yale madeni ambayo yameshindikana kulipwa basi ni vyema kufuata taratibu za kuyaondoa madeni hayo kwa mujibu wa Sheria na kanuni zilizopo.

**5.2.9.12 Tathmini ya kodi zenye migogoro iliyochelewa kutatuliwa kwa muda mrefu.**

Katika mapitio ya madeni yaliyoripotiwa na kitengo cha usimamizi wa madeni ya kodi yalibaini tathmini za muda mrefu za kodi ambazo hazijatatuliwa kwa kipindi kirefu tangu

mwaka 2014 hadi ukaguzi unamalizika. Aidha, ukaguzi ulifanya mahojiano na maafisa wanaohusika na kubaini ya kwamba hakuna hatua zozote za kulipwa kwa madeni haya kwani juhudi za ufuatiliaji hazikuzaa matunda.

Hatima ya tathmini za kodi zenye mgogoro wa muda mrefu hazikuweza kubainishwa na uongozi wa Bodi ya Mapato ambapo ushahidi wa kuwasilishwa kwa madeni hayo kwenye Bodi ya wakurugenzi pamoja na vielelezo vya uthibitisho wa kushindwa kuyakusanya kwa hatua zaidi haukupatikana. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato (ZRA)**

Ni kweli zilikuwepo tathmini za muda mrefu za kodi ambazo hazijatatuliwa kwa kipindi kirefu tangu mwaka 2014.

ZRA imekuwa ikichukuwa hatua mbalimbali za ugombozi wa madeni ikiwa ni pamoja na kujadiliana na walipakodi kuona njia bora ya kuweza kulipa madeni hayo. Hata hivyo, kwa sasa ZRA inaendelea kufuatilia ugomboaji wa madeni na yatayobainika hayana uwezo wa kugomboleka yatapendekezwa kufutwa kwa utaratibu wa Sheria.

**Jedweli namba 8**

**Hali ya sasa ya madeni yanayodaiwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014**

| Jina la Mlipa Kodi | si cha Deni Halisi | lipo ya Thuluthi oja | | amaha Kodi | | si cha Deni kilichobaki | | Hali halisi | | Hali ya sasa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | n. | D | n. | D | n. | D | n. | D | | |
| ep Two Co.Ltd (Pa ght Hotel) | ,044,527 | | .49,999 | | | | .894,527 | | kimbia nchi | ipakodi aliwasilisha barua ya kutoridhika ni tarehe 14/02/2014 ambayo alidai: - vango cha bei ya chumba kilowek kitumiki Hotelini kwake juwi mauzo yalowekwa kwenye ukag mepatikana wapi ya vyumba, mkahawa r |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | ırehe 14/3/2014 alitumiwa barua takiwa kufika Mamlaka ya Mapato Zanzi a ajili ya maongezi ya ukaguzi pia alitak wsilisha malipo ya 1/3 ili pingamizi y ilizwe kulingana na matakwa ya sha ehe 28/03/2014<br><br>ırehe 13/9/2016 alitumiwa ukumbusho visho juu ya deni hili na kutakiwa ku ıra moja.<br><br>rehe 27/9/2016 aliwasilisha barua ıgamizi kwenye ZANZIBAR TAX APP ARD<br><br>rehe 09/02/2022 alitakiwa kufika Maml Mapato Zanzibar kwa barua ya w B/HT/S.18/VOL.1/56 kwa ajili ya kuja ni. Kutokana na ufuatiliaji wa muda mr deni hili takriban miaka tisa iliyop ebainika kuwa deni hili halikusanyiki, atibu ya kulifuta deni hilo zitachukuliwa. |
| im RashidNassor | .893,008 | | | | | | .893,008 | | thmini ya Kodi yofanyiwa ina ata. | 014 Ripoti ya ukaguzi yenye deni la .893,008.11 I ilitolewa<br>di alitumiwa barua ya deni tar /04/2014 na<br>sha barua ya ufafanuzi wa pingamizi wasilisha vielelezo tarehe 21/04/2014.<br>5/3/2017 alitakiwa kuwasilisha thuluthi m malipo ili pingamizi yake ipitiwe amb ijalipwa.<br>rehe 09/02/2022 alitakiwa kufika Maml Mapato Zanzibar kwa barua ya w B/HT/S. I/VOL.1/1 kwa ajili ya kujadili den<br><br>ipakodi huyu amedai kuwa hana deni tokana na kwamba walikubaliana na Z wa hakukuwa na deni la aina yoyote ıwasilisha vielelezo vya madai hayo amba di sasa hajawasilisha. |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | tokana na ufuatiliaji wa muda mrefu wa d takriban miaka tisa iliyopita, imebain wa deni hili halikusanyiki, na taratibu toa mapendekezo ya kulifuta deni l achukuliwa. |
| b total | 5,937,535 | | 49,999 | | | | 787,535 | | | |

## Hali ya sasa ya madeni yanayodaiwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015

| Jina la Mlipa Kodi | si cha Deni Halisi | | alipo ya Thuluthi oja | | amaha Kodi | | si cha Deni kilichobaki | | Hali halisi | Hali ya sasa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | h. | D | h. | D | h. | D | h. | D | | |
| nzibar Tea Packers .Ltd | 55,509,4 | | | | | | 55,509,4 | | fungaBiashara | A ilichukua hatua mbalimbali za ugomb deni hili ambapo tarehe 09/02/20 takiwa kufika Bodi ya Mapato Zanzibar k rua ya wito ZRB/TR/Z.4/VOL.1/33 kwa kujadili deni.<br>rua ya Wito imerudi Bodi ya Map nzibar kutokana na kubainika kwan mpuni hiyo imeuzwa tangu 2019, hi wezekano wa kulikusanya deni hau atibu ya kutoa mapendekezo ya kulif ni hilo zitachukuliwa. |
| tepa FoodCo.Ltd | 652,378 | | | | | | 652,378 | | fungaBiashara | ipakodi amesita kuwasilisha ritani to wezi wa Disemba 2018, ZRA imechu hata za kumtafuta mfanya biashara h a kipindi hicho bila ya mafanikio, hi wezekano wa kulikusanya deni hili haupo atibu ya kutoa mapendekezo ya kulif ni hilo zitachukuliwa. |
| batna Build-ing C | 4,169,112 | | | | | | 4,169,112 | | fungaBiashara | A ilichukua hatua mbalimbali za ugomb |

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | deni hili ambapo tarehe 10/02/2( takiwa kufika Mamlaka ya Mapato Zanzi a barua ya wito ZRB/TO/G.4/VOL.1/65 k i ya kujadiliana deni, hata hivyo mlipak kuitikia wito vilevile ZRA inaende chukua hatua za kugomboa deni hili. |
| stal ResortLtd | .669,585 | 98,. | | | | | .669,585 | 98,. | ipa kodi kakimb Hoteli inamiliki uongozi vengine. | A inaendelea na utaratibu wa kukamili lelezo vya mlipakodi huyu kwa lengo toa mapendekezo ya kulifuta deni hilo. |
| mubeenG.Group | .951,129 | | | | | | .951,129 | | ipa kodi katoro hi. | ipa kodi amesita kuwasilisha ritani zake uzo ZRA tokea mwaka 2015, juhudi za npata mlipa kodi huyu zimeshindikana, A ipo katika hatua za kutoa mapendekez a lengo la kulifuta deni hili. |
| **b total** | **9,951,703** | **98,.** | | | | | **9,951,703** | **98,.** | | |

**Hali ya sasa ya madeni yanayodaiwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016**

| **Jina la Mlipa Kodi** | **ısi cha Deni Halisi** | | **alipo ya Thuluthi ɔja** | | **samaha ı Kodi** | | **ısi cha Deni kilichobaki** | | **Hali halisi** | **Hali ya sasa** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **h.** | **D** | **h.** | **D** | **h.** | **D** | **h.** | **D** | | |
| SHA BOU-TIQU | | 75,868 | | | | | | 75,868 | ipa kodi kakimbia n teli inamilikiwa na ngozi vengine. | A ilichukua hatua mbalimbali za ugomboaji ni hili ambapo tarehe 14/03/2022 alitak fika Bodi ya Mapato Zanzibar kwa barua to ZRB/HT/K.22/VOL.1/36 kwa ajili jadiliana deni, mlipakodi huyo hakuitikia v o, hata hivyo ZRA inaendelea kuchukua ha mapendekezo ya kufuta deni hilo. |
| **b total** | | | | | | | | **75,868** | | |
| **and total** | **)75,889,2** | **174,383** | **8,149,.** | | | | **)67,739,23** | **174,383** | | |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hiyo licha ya Mamlaka kuchukua jitihada mbambali za katika kuyakomboa madeni hayo lakini bado hakuna matumaini ya mafanikio katika jitihada hizo kwa vile wadaiwa hao kutoonesha dalili ya kulipa madeni hayo kwa vile yameshachukua muda mrefu kama inavyoonekana katika jadweli namba 8 la majibu ya hoja ya Mamlaka.

Kamati inaishauri Mamlaka kufuata utaratibu wa kisheria wa kufuta madeni ambayo yamedumu kwa muda mrefu licha ya Mamlaka kufuatilia madeni hayo kwa karibu lakini jitihada hizo hazikuzaa matunda kwani kuwepo kwa madeni hayo yasiyogomboleka kunaisababishia mzigo mkubwa wa madeni katika vitabu vya hesabu vya Mamlaka.

### 5.2.10 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)

**Sera na Mikakati ya Uwekezaji**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2021 ukaguzi uliweza kupima uwezo wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kwa kuangalia Sera na Mkakati wa uwekezaji iliyoidhinishwa na Bodi ya Wadhamini na kubaini imeweka mipaka katika maeneo yanayoruhusiwa ya uwekezaji kwa kuzingatia hitaji la kudumisha ukwasi wa kutosha, kwa lengo la kuongeza faida na kupunguza hatari (minimum risk) kwa kufanya mgawanyiko wa uwekezaji (diversifi cation of investment) na kuhakikisha usalama kamili wa rasilimali za Mfuko (security of the Fund's resources).

**Majibu ya Mfuko**

Mfuko umekuwa ukiendelea kuwekeza katika miradi yenye tija kwa lengo la kupata faida na kukuza rasilimali za Mfuko huku ukizingatia ukwasi wa Mfuko ili kuendelea kuwalipa wanachama wake bila kusita, kwa kipindi husika rasilimali za uwekezaji zimeongezeka kutoka TZS495 bilioni hadi kufikia TZS 555 bilioni sawa na ongezeko la asilimia kumi na mbili (12%), na kuendelea kuufanya Mfuko kuwa himilivu.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imeushauri Mfuko kuwa makini wakati unaandaa Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka. Hii ni kutokana na kuwa Taarifa hiyo ina upungufu ikiwemo:

i. Kwenye ukurasa wa 13 kuna 150,000 hazikujumlishwa ingawa zimeoneshwa;
ii. "Note" 8 haina maelezo ya uchambuzi ingawa haikupaswa kuandikwa kwenye Taarifa hiyo;

iii. Ukurasa wa 31 “Beginning of year” ni Tsh. 534,253,767,402 kwa tarehe 30 Juni, 2021 wakati katika mwaka wa 2020 hesabu imefungwa tarehe 30 Juni, 2020 kukiwa na Tsh. 534,251,136,545.

**Uchambuzi wa taarifa za mabadiliko ya mali halisi zinazopatikana na kwa faida**

Kama inavyoonekana katika taarifa ya mabadiliko ya mali zote zinazopatikana kwa faida, ukaguzi umebaini michango ya wanachama imeongezeka katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021 na kufikia shilingi bilioni 80.9 ukilinganisha na mwaka wa fedha wa fedha 2019/2020 ambapo michango ya wanachama ilikuwa shilingi bilioni 75.9 ikiwa ni ongezeko la kila mwaka la asilimia 6.18 ( kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kulikuwa na ongezeko la asilimia 0.77. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa wanachama wanaochangia kutoka wanachama 104,837 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia wanachama 106,982 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na kuingiza wanachama wapya kutoka sekta binafsi.

Aidha, imebainika gharama za mafao zilizolipwa kwa wastaafu zilifikia jumla ya shilingi bilioni 38.04 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 sawa na asilimia 32 ya ongezeko ukilinganisha na mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ongezeko la shilingi bilioni 28.75 ni sawa na asilimia 18.31. Ongezeko hilo la malipo ya mafao limechangiwa na ongezeko la mishahara ya walengwa hasa kutoka sekta ya Serikali.

Takriban asilimia 48 ya matumizi ya faida yanahusiana na malipo ya viinua mgongo na asilimia 41 ya pensheni ya kila mwezi ambayo pensheni iliongezeka wakati malipo ya viinua mgongo yakipungua.

**Majibu ya Mfuko**

Ongezeko hilo la malipo ya mafao limetokana na ongezeko la mishahara ya wanachama waliolipwa mafao kutoka sekta ya Serikali.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imeushauri Mfuko kuweka taarifa za uchambuzi na kwa upande wa Pemba ili uonekane uhalisia wa utendaji.

Vile vile, Kamati ya LAAC iliushauri Mfuko kutokuweka taarifa za Pemba kwenye Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa mwaka kwa kuwa fedha zote za michango zinalipwa Makao Makuu ya Taasisi hutika.

**Uwiano wa faida kwa michango**

Imebainika ongezeko halisi la shughuli na wanachama, ambalo linakokotolewa kama michango kidogo ya mafao, lilionekana kupungua kutoka shilingi bilioni 44 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi shilingi bilioni 38.5 mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na upungufu wa shilingi bilioni 5.5 sawa na asilimia 12.5 ya upungufu. Uwiano wa faida kwa michango uliongezeka kutoka shilingi bilioni 38.7 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia shilingi bilioni 44 mwaka kwa mwaka wa fedha 2020/2021, hali hii inaonesha kupungua kwa mzunguko wa fedha kwenye Mfuko kutokana na ongezeko la madai.

**Majibu ya Mfuko**

Uwiano wa Michango na Mafao ulipungua kwa mwaka 2020/21 ukilinganisha na mwaka 2019/20 kwa sababu ya kuongezeka kwa ulipwaji wa mafao kwa wanachama wanaostaafu. Mwaka 2021 wafanyakazi wengi wa serikali walistaafu hasa ikizingatiwa hakukuwa ajira mpya nyingi na wafanyakazi wengi hawakuongeza mikataba.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inakubaliana na maelezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya uwepo wa upungufu wa mzunguuko wa fedha za Mfuko kutokana na Ongezeko la Madai, Kamati inashauri, Uongozi wa Mfuko kuweka Mikakati madhubuti

ya kuhakikisha Madai yote yanafuatiliwa na kulipwa ili kuongeza mzunguuko wa Fedha za Mfuko

**Mapato yatokanayo na uwekezaji**

Ukaguzi umebaini mapato ya Mfuko yatokanayo na uwekezaji katika mwaka wa fedha 2020/2021 yalifikia shilingi bilioni 39.45 ukilinganisha na shilingi bilioni 36.58 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.3. Ongezeko hilo kwa ujumla linatokana na mapato yatokanayo na uthamini wa mali za uwekezaji, gawio na mapato ya viwanja vya burudani. Chanzo kikuu cha mapato ya uwekezaji kwenye Mfuko ni mapato ya riba (treasury bonds) inayochangia asilimia 66.

**Majibu ya Mfuko**

Ongezeko la faida ya uwekezaji limeongezeka kutokana na Mfuko unaendelea kusimamia vizuri uwekezaji wake. Pia, Mfuko unaendelea kutekeleza na kuwekeza kwenye Miradi yenye tija zaidi ili kuufanya uwe endelevu na uweze kulipa mafao kwa wanachama wake kwa wakati na ufanisi.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC iliushauri Mfuko kuwa makini na maamuzi ya uwekezaji unaotarajiwa kuwekezwa katika kiwanja cha Gombani ili uwekezaji huo ulete tija iliyokusudiwa.

**Mabadiliko ya Thamani ya Fedha (Fair Value Change)**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi ulibaini Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ulipata faida yenye thamani (fair value gain) ya shilingi bilioni 3.2 ukilinganisha kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo Mfuko ulipata hasara yenye thamani (fair value loss) ya shilingi bilioni 2.85

**Majibu ya Mfuko**

Hakukuwa na hasara iliyopatikana kwenye ongezeko la thamani (Fair Value Change) kama ilivyoripotiwa. Kutokana na Jadweli hapo juu thamani iliongezeka kutoka TZS 2.8 Bilioni mwaka 2019/20 hadi kufikia TZS 3.2 Bilioni kwa mwaka 2020/21. Kuongezeka kwa thamani ya fedha kwa Mfuko kunatokana na kuongezeka kwa thamani ya soko ya rasilimali za uwekezaji.

**Mapato mengineyo**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021 ukaguzi umebaini mapato mengineyo (other income) yaliongezeka na kufikia jumla ya shilingi milioni 68 ukilinganisha na kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo mapato hayo yalikuwa shilingi milioni 53. Ukaguzi uliweza kubaini kwamba ongezeko la mapato hayo limetokana na kuongezeka kwa vyanzo vya mapato ikiwemo utayarishaji wa vitambulisho vya ZSSF, mauzo ya hati ya Zabuni, Ada pamoja na Fomu za maombi ya ukodishwaji.

**Majibu ya Mfuko**

Ni kweli mapato mengineyo yaliongezeka kutokana na kuongezeka kwa baadhiya vyanzo vya mapato ikiwemo utayarishaji wa vitambulisho vya ZSSF, Mauzo ya hati za Zabuni, Ada pamoja na Fomu za maombi ya ukodishwaji wa miradi ya ZSSF.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati inaishauri Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kuendelea kubuni miradi yenye kuleta tija na kuuwezesha mfuko kuendelea kuwahudumia wanachama wake.

**Uchambuzi wa taarifa za mali za mfuko wa hifadhi ya jamii**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ulibaini mali zinazomilikiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ziliongezeka na kufikia jumla ya shilingi

bilioni 610 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo mali hizo zilikuwa na thamani ya jumla ya shilingi bilioni 537 kukiwa na ongezeko la shilingi bilioni 73 sawa na asilimia 14. Aidha ukaguzi umebaini ongezeko hilo kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii limetokana na uwekezaji mpya wa Bidhaa za Makumbusho ya Mapinduzi, Uwekezaji katika hisa, Uwekezaji katika Usalama wa Serikali (Investment of Government Security) na biashara zinazoendelea kufanyika katika maduka ya Michenzani mall, Thabiti Kombo na jengo la Hifadhi.

**Majibu ya Mfuko**

Mali za Mfuko zimeongezeka kutokana na uwekezaji mpya wa maeneo mbalimbali ya kiwemo Majengo, Masoko ya Fedha na Mitaji.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii inaushauri Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar katika kuendelea na uwekezaji wenye tija pamoja na kutunza mali zake za kudumu kwa kuzifanyia maboresho ya mara kwa mara kama vile majengo na miradi mbalimbali ya uwekezaji inayomilikiwa na Mfuko.

**Taarifa ya Uwekezaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii**

Katika ukaguzi uliofanyika wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa kipindi cha mwaka kilichoishia tarehe 30 Juni 2021, imebainika kwamba uwekezaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii uliongezeka kutoka thamani ya shilingi 497 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia thamani ya shilingi bilioni 555 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na ongezeko la shilingi 58 sawa na asilimia 12. Ongezeko hilo limejumuisha Dhamana za Serikali, Hati fungani za Kampuni, Amana za kudumu, Hisa, Mali za Uwekezaji na Hisa za uwekezaji ambapo hali hiyo imetokana na uwekezaji wa ziada uliofanywa katika

kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na kuongezeka kwa michango na mapato ya uwekezaji.

**Maelezo ya Mfuko**

Ni kweli uwekezaji wa Mfuko umekuwa kwa mwaka 2020/21, ongezeko hilo limechangiwa na uwekezaji uliofanywa kwenye Dhamana za Serikali, Hati fungani za Makampuni, Hisa, Mali za Uwekezaji zisizohamishika ambapo hali hiyo imetokana na uwekezaji wa ziada uliofanywa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na kuongezeka kwa michango na mapato ya uwekezaji.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mfuko wa Hifadhi inaendelea na kuendesha Miradi Kwa kufuata Sera na Mikakati iliyojiwekea, Kamati inaushauri Uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kuendelea na mikakati wa kutekeleza miradi yenye Tija, kuhakikisha kunakuwa na usalama wa rasilimali za mfuko Na pia kupunguza hatari za Mfuko katika Uwekezaji.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

**5.2.10.1 Kukosekana kwa Ushahidi wa mlinganisho wa matokeo ya zoezi uhakiki mali za Mfuko wa Hifadhi ya jamii Zanzibar na kumbukumbu za daftari la mali za kudumu za Mfuko shilingi 3,260,948,760.**

Kwa mujibu wa ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ilibainika kuwa uhakiki halisi wa mali za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii zinazohamishika ulifanyika mwishoni mwa mwaka (stock taking) ili kubaini pamoja na mambo mengine uwepo, hali na utumikaji wake kama ilivyoagizwa chini ya kifungu cha 13.11 cha kanuni za fedha za ZSSF. Hata hivyo, zoezi hilo huwa na maana Zaidi wakati matokeo halisi yanapolinganishwa na kuoanishwa na kumbukumbu za vitabu (Rejista ya PPE). Hatua hii ilikosa ushahidi wa kufanywa na Mfuko kinyume na kanuni ya 13.14 ya kanuni za fedha za Mfuko na

Mwongozo wa Uhasibu na hivyo mantiki ya kufanya zoezi hilo kukosa manufaa yaliyotarajiwa.

Ukaguzi umebaini kuwa hatua hiyo haikufanyika kutokana na ukweli kwamba Mfuko ulikuwa katika mchakato wa kuboresha Daftari lake la Mali za Kudumu na kuzipatia alama ya utambulisho kwa baadhi ya Mali hizo jambo ambalo ni ishara ya udhaifu wa usimamizi wa mali za Mfuko. Hata hivyo, ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalisia wa shilingi 3,260,948,760 zilizobainishwa katika ufungaji wa hesabu kuwa ni thamani halisi ya mali za kudumu za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Kushindwa kuoanisha (reconciliation) matokeo halisi ya zoezi la kuhesabu mali za kudumu za Mfuko dhidi ya vitabu vilivyorekodiwa mali hizo kunapelekea wakaguzi kushindwa kujiridhisha juu ya usahihi wa mali za Mfuko pamoja na uwepo wa mali hizo zenye thamani ya shilingi 3,260,948,760 kama zilivyoripotiwa katika Hesabu za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2021.

**Majibu ya Mfuko**

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar huandaa zoezi la uhakiki wa mali za Mfuko kwa mujibu wa sheria ambapo kila mwisho wa mwaka Mfuko ulikuwa unatumia utaratibu usiotumia mfumo wa kieletroniki, wakati ukaguzi ulipofanyika Mfuko ulikuwa kwenye kipindi cha mpito cha kuhamisha taarifa za kumbukumbu za mali za Mfuko kupeleka kwenye mfumo wa kieletroniki, ukaguzi ulivyobaini hakukuwa na mlinganisho wa matokeo ya zoezi la uhakiki wa mali za Mfuko wa Hifadhi ya jamii Zanzibar na kumbukumbu za daftari la mali za kudumu kwa sababu wakati wa ukaguzi zoezi la kuhamisha taarifa lilikuwa linaendelea.

Kwa sasa dosari hizo zimesharekebishwa na taarifa husika zimeshaanza kuwekwa katika Mfumo unaoweka daftari la kudumu la mali za Mfuko na hadi kufikia mwishoni mwa mwaka ulioshia Juni 30, 2022 utekelezaji umefikia wastani wa asilimia 90 na

taarifa ya mlinganisho itaandaliwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2022/23 baada ya zoezi la uhakiki mali kukamilika.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja imebaki kama ilivyo, kwa kuwa zoezi hilo lilifanyika baada ya ukaguzi. Hivyo, Kamati ya LAAC inaushauri Mfuko kuhakikisha kuwa unatekeleza shughuli zake kama taratibu zinavyoelekeza ili iweze kujulikana hesabu au thamani halisi ya mali za Mfuko.

**5.2.10.2 Daftari la Mali za kudumu ambalo halijakamilika**

Kutokana na Kanuni ya Daftari la Mali za Kudumu kifungu cha 16(j) cha kanuni za fedha za Mfuko (kama ilivyorekebishwa) inayosema "Daftari la Mali za Kudumu lazima litoe maelezo ya mali kama eneo, gharama halisi ya ununuzi wa mali, tarehe ya ununuzi, viwango vya uchakavu, aina ya mali, alama za utambulisho n.k.". Katika ukaguzi uliofanyika kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika daftari la Mali za kudumu la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii lililoandaliwa kupitia mfumo wa Navision limebainika kuwa na dosari mbali mbali kama zifuatazo:

1. Daftari halikuonyesha eneo ambalo mali ilipo ili kutambulika kwa urahisi katika Idara/kitengo ambacho mali hiyo ipo.
2. Hali halisi ya mali haikuonyeshwa kwenye Daftari la Mali za kudumu ili kuweza kutambuliwa kwa urahisi kwa baadhi ya mali zilizotengwa kwa ajili ya kuuzwa/kutupwa na kuondolewa kwenye Daftari.
3. Mali zilizo na alama za utambuzi hazikuweza kuoanishwa na kulinganishwa kwenye Daftari kwa kuwa haikuwekwa nafasi katika Daftari la Mali za kudumu na Vifaa kwa dhumuni hilo. Hii inaleta ugumu wa kuthibitisha kama mali zote za Mfuko zimerekodiwa katika Daftari hilo.

Kutokana na dosari zilizobainika hapo juu inapelekea thamani ya Mali na Vifaa vilivyoripotiwa katika taarifa za hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 zenye thamani ya shilingi 3,260,948,760 kutia shaka juu ya usahihi wa taarifa hizo ambapo ni kinyume na matakwa ya kifungu nambari 16(j) cha kanuni za fedha za Mfuko.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuhakikisha kuwa Daftari la Mali za kudumu lenye maelezo muhimu ya kujitosheleza linatunzwa na kuboreshwa mara kwa mara ili kuwezesha utoaji wa takwimu sahihi na za kuaminika za mali zinazomilikiwa na Mfuko.

**Majibu ya Mfuko**

Ukaguzi wa Mwaka wa fedha 2020/21 ulibaini kutokuboreshwa kwa Daftari la Kudumu (Fixed Asset Register), kwa kutoonesha mahali ilipo mali pamoja na nambari ya utambuzi. Kwa sasa Mfuko ulishaboresha Daftari hilo na umeshakamilisha kwa kiasi kikubwa na kuweka sawa kumbukumbu za mali katika daftari la mali za kudumu hadi mwaka fedha 2021/22 ambapo daftari limeboreshwa na kuweza kuonesha mahali ilipo mali nambari ya utambulisho na hali ya mali, hadi kufikia mwaka wa fedha 2022/23 Mfuko utakuwa umeshakamilisha kabisa.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja hii imebaki kama ilivyo, pamoja na hayo, Kamati ya LAAC inaushauri Mfuko kuhakikisha kuwa inazisajili mali zake zote kama tararibu zinavyoelekeza ili kuepusha upotevu wa mali za umma.

**5.2.10.3 Mali za kudumu ambazo hazikurekodiwa kwa jina la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar**

Katika uhakiki wa hati miliki/cheti cha umiliki wa ardhi na mali zinazomilikiwa na Mfuko ukaguzi ulibaini baadhi ya mali zinazomilikiwa na Mfuko hazikusajiliwa kwa jina la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambapo linathibitisha uhalali wa kisheria wa mali

inayomilikiwa na Mfuko. Baadhi ya mali hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

**Majibu ya Mfuko**

Mfuko wa Hifadhi Jamii Zanzibar Tayari umeshakamilisha mchakato wa kuhamisha majina ya utambulisho wa Hati miliki kutoka kwa Ndugu Said Salim Awadh iliyopo kilimani na viwanja vilivyopo Kariakoo kutoka kwa Kondo Ibrahim kondo, Omar Mwinyiduchi na Khamis Machano na kusomeka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar.

Kwa upande wa Mkataba wa Ndugu Abubakar Haji Bobea eneo lake halikununuliwa na Mfuko kwani hatukufikiana makubaliano.

Kwa upande wa Ndugu Said Salim Awadh tayari Mfuko umeshapatiwa cheti cha uhaulishaji Ardhi (Certificate of Land Transfer), Hatua inayofuata ni kupatiwa Hati kamili ya umiliki.

Kwa upande wa ndugu Kondo Ibrahim kondo, Omar Mwinyiduchi na Khamis Machano, Mfuko tayari umeshawasilisha maombi Kamisheni ya Ardhi ya kupatiwa Hati za umiliki

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Baada ya majadiliano ya kina sambamba na kuzikagua nyaraka husika, Kamati ya LAAC imeridhika na maelezo yaliyotolewa na Mfuko, hivyo, hoja hii imefutwa.

**5.2.10.4: Kuazimwa gari la Mfuko kwa Kipindi kisichojulikana**

Katika ukaguzi wa rasilimali za Mfuko uliofanyika imebainika gari moja yenye usajili nambari SLS 251A iliyoko Makao Makuu Mnarani iliazimwa na Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuanzia tarehe 15 Aprili, 2021 kwa ajili ya kazi maalum kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba AR/IKL/M.30/I.VOL.XV/133 ya tarehe 12 Aprili, 2021 kutoka Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwenda kwa Mkurugenzi Mkuu wa ZSSF ikiomba idhini ya kuazimwa gari hiyo. Hata hivyo, ukaguzi haukuweza

kupatiwa vielelezo vinavyobainisha makubaliano ya muda wa matumizi ya gari hilo pamoja na gharama za matengenezo pindipo ikitokea gari hilo limepata ajali au kuharibika.

Kwa mujibu wa kumbukumbu ya kikao cha bodi ya zabuni Na.6 (kikao cha dharura) kilichofanyika tarehe 8 disemba, 2020 ukaguzi ulibaini gari moja la ZSSF lenye usajili namba SLS 245A lilipata ajali eneo la Machomane Pemba tarehe 26 disemba, 2020 likiwa mikononi mwa Ofisi ya Rais, Kazi ,Uchumi na Uwekezaji ambapo gharama zote za matengenezo ya uharibifu uliojitokeza zilighar amiwa na ZSSF kwa kulipa fedha za ziada ambazo hazikuweza kulipwa na Shirika la Bima la Zanzibar jambo ambalo fedha hizo zilipaswa kulipwa na Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa vile gari hilo lilipata ajali katika mikono yao.

Hadi ukaguzi unakamilika gari lenye namba ya usajili SLS 251A bado halijarejeshwa kwa muda usiopungua mwaka mmoja jambo ambalo lilitilia shaka mahali lilipo na hali yake kutokana na kukosekana kwa maelezo ya kurejeshwa kwake.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango kwa lengo la kutafuta hatima ya gari hilo ambalo haliko tena mikononi mwa ZSSF ili kubaini uwepo na umiliki wake katika vitabu vya ZSSF.

**Majibu ya Mfuko**

Ni kweli gari namba SLS 251A mali ya Mfuko iliazimwa na Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji tarehe 15 Aprili 2021 kwa ajili ya kazi maalum, Mfuko ulifanya jitihada mbalimbali za kuandika barua kuomba gari hilo lirudishwe lakini hadi leo bado halijarudishwa.

Pia, gari namba SLS 245A mali ya Mfuko iliazimwa na Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji na kupata ajali eneo la Machomane Pemba, baada ya kupata ajali matengenezo yake yaligharamiwa na Mfuko kwa sababu Mfuko ulifuatilia matengenezo hayo yafanywe na Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji lakini hakuna jitihada zozote zilizochukuliwa na Ofisi hiyo baada ya kutokezea ajali.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC kupitia barua ya tarehe 2 Oktoba, 2023 yenye kumbukumbu Namba AC.169/191/01/3 iliyotoka kwa Mkurigenzi wa Mfuko huo ilieleza kuwa Mfuko umekubaliana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango juu ya gari hiyo ambapo Wizara imekubali kuufidia Mfuko gari nyengine kutokana na kuchukuliwa kwa gari hiyo kwa muda mrefu.

Kamati ya LAAC haina pingamizi na suala hilo, hata hivyo, inautaka Mfuko kuhakikisha kuwa gari hiyo inapatikana kama ulivyoahidiwa.

**5.2.10.5: Fedha zilizowekwa benki kwa muda mrefu katika Akaunti ya ZSSF bila ya taarifa zake kuoneshwa katika daftari la fedha (Cash book)**

Ukaguzi ulipitia taarifa za usuluhishi wa kibenki pamoja na hesabu zilizoandaliwa na Mfuko kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na kubaini uwepo wa kiasi kikubwa cha fedha ambacho bado hakijatambulika kwani kiasi hicho kililimbikizwa katika hesabu ya Amana ya benki tangu mwaka 2019 ambazo taarifa zake hazikuweza kupatikana katika vitabu vya fedha vya Mfuko kutokana na kuwa taarifa za uwepo wa fedha hizo Mfuko haikuweza kuzitambua.

Aidha, ukaguzi ulifanya mahojiano na uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na kubaini sababu zilizopelekea uwepo wa fedha hizo ni kushindwa kutumia namba za udhibiti (control number) wakati wa kupokea michango ya wanachama kwenye akaunti ya benki ya ZSSF kwa wale waliopewa namba za udhibiti na vile vile wachangiaji wenyenye kupuuza kutumia namba za udhibiti na badala yake hupendelea kuwasilisha michango yao kutumia mfumo wa zamani (manual system).

Hata hivyo, ukaguzi ulibaini jukumu la kufuatilia amana zisizojulikana ni la idara ya fedha na kitengo cha ufuatiliaji (compliance unit). Aidha ukaguzi ulibaini vitengo hivyo havikuwa vikifanya kazi kwa mashirikiano ili kuhakikisha kwamba mwelekeo wa muda mrefu wa amana zisizojulikana umepunguzwa au kuondolewa.

Uwepo wa Amana za muda mrefu ambazo hazijajulikana chanzo chake zinafanya kiasi cha pesa kilichoripotiwa katika vitabu vya mfuko kukosa uhalisia ukilinganisha na kiasi kilichopo benki.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuimarisha juhudi zake katika kufuatilia chanzo cha fedha yoyote ambayo haitambuliki ili kuweka kumbukumbu sahihi za mfuko kuhusu miamala ya kifedha. Aidha matumizi ya nambari za udhibiti kwa stakabadhi zote za Mfuko (michango, uwekezaji na mapato mengine) inapendekezwa zaidi. Vikao vya uhamasishaji juu ya umuhimu wa kutumia/ rejea namba za udhibiti wakati wa kuweka amana mbalimbali za Mfuko vifanyike kwa wadau wote (mabenki na wateja wa Mfuko) ili kupunguza/kuondoa mwenendo wa amana zisizojulikana.

**Majibu ya Mfuko**

Utaratibu wa wanachama kuweka fedha za michango/Miradi moja kwa moja kwenye akaunti za Mfuko bila kufuata utaratibu uliowekwa inapelekea uwepo wa fedha usiotambulika kwenye akaunti za Mfuko. Baada ya Serikali kuanzisha mfumo maalum

wa malipo kwa kutumia nambari ya utambulisho (Control Number) sasa fedha zote zinazoingia kwenye akaunti za Mfuko zinatambulika.

Fedha zilizobainika wakati wa ukaguzi tayari Mfuko ulishachukua jitihada za kuwasiliana na Mabenki ili kufahamu chanzo cha fedha hizo na tayari fedha hizo zilizoripotiwa zimeshafanyiwa kazi na kuripotiwa katika vitabu vya Mfuko.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inakubaliana na hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo, kwa kuwa Mfuko umechukua hatua mbali mbali dhidi ya hoja hii, Kamati ya LAAC imeridhika na hatua hizo, hivyo, imefuta hoja hii.

**5.2.10.6 Udhaifu katika usimamizi wa mikataba**

Ukaguzi uliofanyika katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021 ulibaini uwepo wa uzembe uliosababishwa na uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa kutokuchukuwa hatua kutokana na ukiukwaji wa vipengele muhimu vilivyobainishwa katika mikataba mbalimbali iliyoingiwa kati ya Mfuko na wadau wengine kwa mikataba inayohusiana na uuzaji wa nyumba, mikataba ya upangishaji na mikopo iliyotolewa kwa taasisi mbalimbali ikiwamo Serikali na wakala wake pindipo inapobainika muhusika anapokiuka masharti ya mikataba hiyo. Vifungu vilivyotajwa vya mikataba ambayo uongozi wa Mfuko ulishindwa kuzifanyia kazi ni kama ilivyoonyeshwa hapa chini: -

1. Kutokutozwa kwa riba ya asilimia 15 kutokana na ucheleweshwaji wa malipo ya uuzwaji wa nyumba (House Sale Agreements) kwa mujibu wa kifungu 3.3.1 cha Mkataba. Aidha kwa mujibu wa kifungu 3.3.2 kinaeleza ikiwa kosa la kuchelewa kulipa litaendelea kwa muda wa miezi miwili mfululizo, mkodishaji atakuwa na

haki ya kughairi au kusitisha makubaliano hayo jambo ambalo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umeshindwa kutekeleza matakwa ya kifungu hicho.

2. Kutotozwa faini kwa kushindwa kulipa kodi kwa mujibu wa tarehe zilizoainishwa katika mkataba kwa mujibu wa kifungu 1.5 cha mkataba cha ukodishwaji wa ardhi (Lease Agreements). Aidha kwa mujibu wa kifungu 2.5 kinaeleza kwamba Mkodishwaji anatakiwa kulipa kodi inayostahiki kwa wakati na ikiwa atachelewa Mkodishaji atakuwa na haki ya kutoza faini ya asilimia 5 jambo ambalo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umeshindwa kutekeleza matakwa ya kifungu hicho. Hata hivyo, imebainika kutokufanyiwa kazi kwa kifungu 2.6 ambacho Mkodishwaji akishindwa kulipa kodi kwa muda wa miezi mitatu mfululizo Mkodishaji atalazimika kutoa notisi ya siku kumi na nne (14) kwa mpangaji jambo ambalo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umeshindwa kutekeleza matakwa ya kifungu hicho.
3. Mikataba ya Mikopo (Loan Contracts) Vifungu mbalimbali vya mikopo iliyotolewa kwa Serikali, Wakala na Taasisi nyinginezo vinaeleza kuwa "Ikiwa deni litatoweka kwa muda wa siku 15 kuanzia tarehe ya kulipwa, jumla ya malimbikizo haya ya madeni yatatozwa ziada ya riba kuanzia tarehe ya malipo halisi Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umeshindwa kutekeleza agizo hilo la kutoza riba ya ziada kwa kushindwa kulipa mkopo kwa tarehe husika.

Kutokutekelezwa kwa vipengele vilivyoainishwa katika mikataba kunapelekea kusababisha hasara isiyoweza kurejeshwa ya fedha zilizowekezwa na wanachama ambazo zingeweza kuwekezwa tena katika miradi mingine yenye faida kama vile dhamana za hazina (treasury bonds) na amana za muda maalum (Fixed Deposits).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kufuatilia utekelezaji wa mikataba kwa ukaribu kwa kuunda timu ya usimamizi wa mikataba ambayo

itasimamia vigezo na masharti yote kama yalivyoainishwa katika mikataba hiyo na kuchukua hatua za haraka endapo utekelezaji utakiukwa.

**Majibu ya hoja**

Kutokana na wimbi la mripuko wa ugonjwa wa Uviko 19 ambalo liliathiri hali za uchumi wa nchi na mwananchi mmoja mmoja pia lilipekea washirika wetu wa biashara wakiwemo tuliowakodisha na kuwauzia maeneo ya miradi yetu ya uwekezaji, Mfuko ulipokea maombi mbalimbali ya wadau wetu hao kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi pamoja na kuwapa unafuu katika ulipaji wa kodi kwa maeneo yetu ya biashara.

Kwa mahusiano mazuri ya biashara (Business relationship), Mfuko ulizingatia na ulikubali maombi yao. Hivyo kupelekea malipo yao kwenda tofauti na maelekezo ya mkataba.

Kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 baada ya wimbi la mripuko wa ugonjwa wa Uviko 19 kutengemaa Mfuko unaendelea kusimamia masharti ya mkataba.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inakubaliana na hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutokana na majibu yaliyotolewa kwenye “Management Letter”, hata hivyo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hii baada ya kuridhika na maelezo mapya yaliyotolewa na Mfuko.

Pamoja na kuifuta hoja hiyo, Kamati ya LAAC inazishauri Taasisi za Umma kuwa makini na kuwa na kauli moja wakati wa kujibu hoja za Mkaguzi Mkuu ili kuepusha kuwa na hoja zisizo na msingi.

**5.2.10.7 Mapato ya muda mrefu yatokanayo na Mikopo kwa Serikali na Taasisi, Uuzwaji wa Nyumba, Kodi na Michango ya Wanachama ambayo bado hayajalipwa TZS 97,585,698,701.**

**i Mikopo iliyotolewa kwa Taasisi za Serikali TZS 8,882,689,160**

Katika kipindi cha ukaguzi uliofanyika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika uwepo wa baadhi ya mali za uwekezaji zinazohusiana na mikopo iliyotolewa kwa taasisi mbalimbali zenye jumla ya shilingi 8,882,689,160. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 7,197,706,045 sawa na asilimia 81.03 zilikuwa ni marejesho ya mkopo kutoka ZSTC.

Aidha, ukaguzi ulipitia mwenendo mzima wa urejeshaji wa mikopo hiyo na kubaini mwenendo mbaya wa urejeshaji ambapo baadhi ya wakopaji walionekana kulipa fedha zote za malipo wanayodaiwa na kukwepa kulipa malipo ya riba ya shilingi 2,347,607,737 na baadhi yao walishindwa kulipa kabisa mikopo hiyo yenye jumla ya shilingi 6,535,081,421 na wengine walikuwa wakilipa bila ya kuzingatia makubaliano ya ulipaji jambo ambalo limepelekea uwepo wa malimbikizo ya mikopo ya muda mrefu ambayo hayajarejeshwa kwa zaidi ya miaka mitatu (3), fedha ambazo zingeliweza kutumika katika uwekezaji mwingine.

Hata hivyo ukaguzi haukuweza kupata ushahidi wa juhudi zinazochukuliwa na uongozi wa Mfuko kuhakikisha kiasi cha mkopo na riba kutoka kwa taasisi hizo unarejeshwa.

**Majibu ya Mfuko**

Ni kweli kunatatizo la marejesho ya mikopo ya Taasisi za Serikali. Mfuko umefuatilia madeni hayo kwa taasisi za Serikali kama ifuatavyo: -

1. ZSTC hadi sasa wameshalipa deni lao lote la mkopo na imebakia riba.
2. ZIFA / SUZA wanaendele kulipa kwa kusuasua na deni limebaki shilingi
3. ZATUC wameshamaliza deni lao hilo na hawadaiwi

4. Admira Investment Company anaedelea kulipa na deni limebakia shilingi 26, 337,452.04
5. Nalasa anaendelea kulipa na deni limebakia shilingi 7,049,246
6. Baraza la Manispa Mjini deni lao limehamishiwa Hazina ambalo wamelikubali ila hawajaanza kulipa hadi sasa.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kuhakikisha kuwa madeni hayo yanalipwa katika kipindi kifupi kijacho ili katika miaka ijayo hoja hii isijirudie tena.

**ii. Mikopo ya Serikali (Wizara ya Fedha na Mipango) TZS 58,669,100,673**

Ukaguzi ulipitia mfumo mzima wa mwenendo wa ulipaji wa mikopo iliyotolewa kwa Serikali kama sehemu ya rasilimali za uwekezaji katika kumbukumbu za Mfuko na kubaini mwelekeo wa kuongezeka kutoka kiasi cha shilingi 48,672,786,435 hadi kufi kia shilingi 58,669,100,673. Aidha, ukaguzi ulibaini mwenendo usioridhisha wa ulipaji wa deni la mkopo na kukwepa ulipaji wa riba kwa baadhi ya mikopo iliyotolewa. Hata hivyo imebainika kuwa baadhi ya mikopo iliyotolewa haikulipwa kabisa tangu ilipotolewa kwa zaidi ya miaka mitatu (3) na kutokuzingatia makubaliano ya urejeshaji wa mikopo hiyo.

**Majibu ya Mfuko**

Serikali imekuwa inaendelea kulipa madeni yake kwa mujibu wa makubaliano na muda wa ulipwaji wa madeni hayo. Hadi mwezi Machi, 2023 Serikali inatakiwa ililipe deni lililoiva la **TZS 3,674,083,332.35 na TZS 1,380,000,000** ambapo tayari Mfuko umeshakumbushia deni hilo.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kuhakikisha kuwa madeni hayo yanalipwa katika kipindi kifupi kijacho ili katika miaka ijayo hoja hii isijirudie tena.

**iii. Madeni ya muda mrefu ya Uuzaji wa Nyumba TZ 27,452,313,659**

Ukaguzi umebaini uwepo wa madeni yaliyoripotiwa katika taarifa za fedha za Mfuko ni kiasi cha shilingi 27,452,313,659 kinachohusiana na madeni ya uuzaji wa nyumba. Kiasi hicho cha deni kimejumuisha wanunuzi ambao hawakulipa kabisa kwa mwaka mzima na wengine wamekuwa wakilipa taratibu sana kinyume na makubaliano ya mauzo.

Aidha, ukaguzi umebaini hakukuwa na jitihada kubwa katika ufuatiliaji wa fedha zilizochukuliwa na uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuona fedha hizo zinarejeshwa kutokana na uuzwaji wa nyumba. Aidha, ukaguzi umebaini Benki Kuu ya Tanzania (BOT) inachangia sehemu kubwa ya deni kiasi cha shilingi 1,624,430,080 linalotokana na uingiaji wa mkataba wa mauzo na Mfuko tarehe 30 Julai, 2018 kununua nyumba 14 (vyumba) kwa fedha taslimu tofauti na wanunuzi wengine wanaolipa kwa mkopo. Vigezo na masharti ya mauzo hayo yaliitaka BOT kulipa asilimia 40 sawa na shilingi 1,047,329,920 za jumla ya fedha za mkataba ambazo ni shilingi 2,618,324,800 na bakaa ya asilimia 60 sawa na shilingi 1,570,994,880 ilipaswa kulipwa ndani ya miezi mitano (5) kuanzia tarehe ya kusainiwa mkataba 31 disemba, 2018 ambayo iliashiria kumaliza muda wa mkataba. Hata hivyo mapungufu yafuatayo yamebainika kama ifuatavyo: -

1. BOT imeshindwa kuzingatia makubaliano ya mauzo na hakukuwa na riba inayotozwa kwa malipo yaliyocheleweshwa kwani hakukuwa na kifungu hicho katika mkataba wa mauzo tofauti na mikataba ya wanunuzi wengine ambayo ilikuwa inatozwa riba.

2. Makubaliano ya mauzo kati ya BOT na ZSSF yalimpendelea mnunuzi na kuathiri ZSSF kwa kuwa hakukuwa na kipengele kinachoonyesha madhara ya kushindwa kuzingatia makubaliano ya mauzo.

Wanunuzi wafuatao hawajalipa fedha yoyote ya ununuzi wa Nyumba za Mbweni:

1. Nassoro Abdallah Hemed,
2. The Bank of Tanzania (BOT),
3. Ghalib Hamdoun Mansour (9B6),
4. Mussa Saleh Abdalla,
5. Munawar Semi Ally,
6. Said Gharib Bilal
7. Ahmada Yahya Abdulwakil
8. Carolyne Mkony Paul
9. Nabil Karim Virani
10. Daud Abdallah Ramadhan

**Majibu ya Mfuko**

Benki Kuu ya Tanzania (BOT) tayari wameshalipa deni lao lote. Madeni yaliyobaki yanatonakana na utaratibu wa uuzwaji nyumba ambazo marejesho yake yanalipwa kidogo kidogo kwa mujibu wa makubaliano. Hata hivyo, katika kusimamia utekelezaji wa mikataba ya mauziano Mfuko umeshafanya na unaendelea kufanya uhakiki na kuwaondosha wadaiwa wote kwa mujibu wa mkataba ulivyo.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini kuwa kati ya Wanunuzi kumi walioripotiwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu kuwa hawalipa fedha yoyote ya

ununuzi wa nyumba hizo, Wanunuzi watano wametolewa kwenye nyumba hizo. Wanunuzi wenyewe ni kama wafuatao:

1. Ghalib Hamdoun Mansour (9B6),
2. Mussa Saleh Abdalla,
3. Munawar Semi Ally,
4. Carolyne Mkony Paul
5. Nabil Karim Virani

Hoja imebaki kama ilivyo, pamoja na hayo, Kamati inautaka Mfuko kufuatilia kwa karibu madeni yaliyobakia ili hoja hii isijirudie tena.

**iv. Madeni ya muda mrefu ya ukodishaji wa nyumba TZS 1,499,716,016**

Ukaguzi ulipitia taarifa za fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 na kubaini uwepo wa madeni ya shilingi 1,499,716,016 yanayohusiana na ukodishwaji wa nyumba ambapo deni hilo limeongezeka kwa shilingi 727,495,746 sawa na asilimia 94.21 kutoka shilingi 772,220,270 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Ukaguzi umebaini ongezeko la deni hilo linaonesha kwamba kuna mifumo dhaifu ya kukusanya kodi za nyumba kwa wakati licha ya kuwepo kwa mtoa huduma anayesimamia ukusanyaji na upangishaji wa nyumba za ZSSF.

Kwa mujibu wa makubaliano ya mikataba ya ukodishwaji wa nyumba za ZSSF, wapangaji wanatakiwa kulipa kodi za nyumba kila mwaka mapema kabla ya kipindi cha kodi kuanza na kutokana na utaratibu huo hakutarajiwi kuwepo kwa madeni

yatokanayo na ukodishaji wa nyumba. Mifano ya kesi za wapangaji na ada za kukodisha ni kama zinavyoonekana katika jadweli lifuatalo: -

**Majibu ya Mfuko**

Mfuko unaendelea kufuatilia madeni ya pango kwa wapangaji wake ila hawa baadhi ya wapangaji wameshaondoka na hawapo nchini na wengine hawapatikani.

**iv. Madeni ya muda mrefu ya michango ya wanachama TZS 1,081,879,193**

Ukaguzi ulipita taarifa za madeni ya michango ya wanachama wa Mfuko na kubaini kati ya madeni ya michango ya shilingi 3,416,153,752 yaliyoripotiwa, shilingi 1,081,879,193 ilionekana kuwa bado haijalipwa kwa kipindi cha muda mrefu kuanzia mwaka 2002 hadi 2019 kiasi ambacho kinatia shaka urejeshaji wa madeni hayo.

Aidha, ukaguzi ulibaini baadhi ya waajiri waliochangia walisimamisha shughuli zao hali ambayo ilitia shaka juu ya kurejeshwa kwa michango hiyo. Uwepo wa madeni ya muda mrefu ambayo hayajalipwa kunapelekea kutokuwepo kwa usahihi wa taarifa za madeni hayo ambapo kunaweza kukapelekea upotevu wa fedha za wanachama ambazo zingeweza kuwekezwa katika uwekezaji wenye tija kama vile dhamana za Hazina (Treasury Bonds), amana za muda maalum (FDR) n.k.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuhakikisha kuwa, Mfuko unawekeza katika hati fungani za Hazina na bili ambazo hazina hatari na hazina gharama za riba.

Vile vile, Mfuko unapaswa kuunda kamati ya ufuatiliaji ambayo itafuatilia kwa karibu uwekezaji wa fedha zote kwa kuhakikisha kuwa sheria na masharti ya mkataba/makubaliano yanafuatwa, endapo uwekezaji wowote unaoonyesha dalili za kutofanya vizuri hatua za haraka lazima zichukuliwe pamoja na kuongeza juhudi za kurejesha fedha za wanachama ambazo zimeshikiliwa mikononi mwa wadaiwa bila kupata riba yoyote.

**Majibu ya Hoja**

Madeni haya yaliyoanzia mwaka 2002 hadi 2019 yametokana na baadhi ya waajiri pamoja na waajiriwa kutokuleta taarifa zao pale ambapo iwe waajiri wamefunga biashara au waajiriwa wameacha kazi, wamefariki au wamefikwa na dharura yeyote ambayo imewapelekea kuacha kazi. Sababu hizo ndizo zinazopelekea michango kusita na kulimbikiza madeni kwa sababu Mfuko unakosa taarifa sahihi za waajiri na waajiriwa hao.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inautaka Mfuko kutekeleza shughuli zake kama Sheria inavyowaelekeza kwa upande wa Mwajiri ambae hamlipii mwajiriwa wake.

**5.2.10.8 Utoaji wa mikopo ziada kwa wafanyakazi kabla ya kurejeshwa kikamilifu mikopo ya awali TZS 741,642,520**

Ukaguzi ulipitia Sera ya mikopo kama ilivyoainishwa katika Muongozo wa Rasilimali Watu wa mwaka 2017 kifungu cha 3.11 ambacho kinaweka vikwazo juu ya suala la mikopo ya ziada kwa wafanyakazi kabla ya kurejesha mikopo ya awali. Hata hivyo ukaguzi umebaini baadhi ya watumishi walikuwa na mikopo mikubwa kwenye akaunti zao kiasi ambacho kimeleta wasiwasi kwamba mwenendo wa Mfuko unaweza kuwa hatarini kutokana na kutoa mikopo ya ziada kabla ya kurejesha mikopo ya awali kinyume na kanuni hiyo. Mifano ya kesi zilizotajwa kwa madhumuni ya kielelezo ni kama inavyoonyeshwa katika jadweli lifuatalo: -

Utoaji wa mikopo ya ziada kwa wafanyakazi kabla ya kurejesha mikopo iliyotangulia unaweza kusababisha upotevu wa fedha za wanachama kwa kuwa fedha hizo zimeshikiliwa mikononi mwa wadaiwa kwa muda mrefu bila ya kutozwa riba ambayo

ingeweza kuekezwa kwenye miradi mingine yenye faida na kuleta tija kubwa ndani ya muda mfupi kwa maendeleo ya Mfuko.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko kuweka sera imara za utoaji wa mikopo na kuhakikisha sera hizo zinazingatiwa, zinasimamiwa na kufuatwa kikamilifu.

**Majibu ya Mfuko**

Mfuko ulikuwa unatoa mikopo kama motisha kwa wafanyakazi wake ili kuboresha mazingira na ufanisi kwenye utendaji kazi. Hivyo, Mfuko ulizingatia zaidi marejesho kutoka kwenye mshahara wa mfanyakazi.

Kuanzia mwaka 2021/22 Mfuko umeshaweka sera imara za utoaji wa mikopo na kuhakikisha sera hizo zinazingatiwa, zinasimamiwa na kufuatwa kikamilifu.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja hii imebaki kama ilivyo na hasa ikizingatiwa kuwa sera husika imeandaliwa baada ya hoja hii kuibuliwa.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inautaka Mfuko kutekeleza shughuli zake kama taratibu zinavyoelekeza.

**5.2.10.9 Uwekezaji usio na ufanisi TZS 10,957,582,160**

Ukaguzi ulipitia jalada la uwekezaji wa Mfuko na kubaini vitega uchumi vingi vya Mfuko upatikanaji wake wa faida hauridhishi. Hali hiyo imetokana na uwepo wa fedha nyingi zitokanazo na michango ya wanachama wa Mfuko kuekezwa kwenye vitega uchumi mbali mbali visivyokuwa na tija na ufanisi kwani fedha hizo zingeweza kuekezwa kwenye mali zinazobadilishwa kwa urahisi.

Kutokana na uhalisia wa uwekezaji uliobainika ukaguzi haukuweza kuona jitihada za uwekezaji wa faida zinazoendelea kuchukuliwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ili kunusuru kuendelea kwa Mfuko kujiekeza kwa hasara. Kuendelea na uwekezaji usio

na tija kunapelekea upotevu wa fedha za wanachama ambazo zingeweza kuwekezwa katika rasilimali nyingine zinazozalisha faida kwa muda mfupi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kupitia Idara ya Uwekezaji kuwa makini katika kuchagua vitega uchumi vyenye kuleta faida, kwa vile vitega uchumi vinavyotokana na maagizo ya Serikali ni vyema Mfuko kupendekeza michango midogo itolewe badala ya kuwekeza fedha nyingi za wanachama kwenye maeneo ambayo hayana tija jambo ambalo linaweza kusababisha ZSSF kushindwa kutimiza wajibu wake wa msingi (malipo ya mafao ya wanachama) pamoja na kuzingatia muongozo wa uwekezaji wakati wa kuandaa ripoti za uwekezaji za kila mwezi ili kusaidia ubainifu wa mapema wa mwenendo usiokuwa na tija kwa kila aina ya uwekezaji kwa hatua zinazohitajika.

**Majibu ya Mfuko**

Uwekezaji wa Mfuko unatizama zaidi kwenye mapato ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Miradi iliyorodheshwa hapo juu ni miradi ambayo Mfuko umeiweka kwenye mgawanyo wa miradi itakayodumu na kulipa kwa muda mrefu ambapo faida yake haionekani katika kipindi kifupi hasa ikizingatiwa kuwa ni miradi inayosaidia na kuinua uchumi wa nchi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na majibu ya Mfuko kutokana na uhalisia wa miradi hiyo, hivyo, imeifuta hoja hiyo.

### 5.2.10.10 Mapendekezo ya Ripoti ya Tathmini ya hali halisi ya Mfuko ambayo hayajatekelezwa kama ilivyoelekezwa na Bodi ya Wadhamini

Kutokana na ukaguzi wa ripoti ya uthamini wa takwimu uliofanywa na African Risk and Insurance Services mwaka 2018 iliyotolewa tarehe 18 Septemba, 2019 ulibaini udhaifu unaohitaji mikakati ya kuchukuliwa na ZSSF ili kuongeza uendelevu na ukwasi.

Ripoti hiyo ilibainisha vihatarishi ikiwa ni pamoja na uwekezaji usio na tija na usioainishwa, mapato yasiyotosheleza kutokana na uwekezaji, muundo wa uwekezaji na kutokuwafi kia wachangiaji wa mfuko kwa kiasi kikubwa. Aidha ripoti inaeleza kuwa mapato ya ZSSF yatazidiwa na malipo kwa wanachama katika vipindi vya kuanzia mwaka 2039 hadi 2050 iwapo hatua za kurekebisha hazitachukuliwa kufanya ZSSF kuwa na ukwasi mzuri.

Bodi ya Wadhamini, ilipopokea ripoti hiyo, iliagiza uongozi wa ZSSF kuyafanyia kazi mapendekezo ya ripoti ya takwimu ambayo ni pamoja na kupitia upya muundo wa uwekezaji, kuwekeza katika vitega uchumi vyenye mapato ya kutosha, uwekezaji kwenye miradi yenye faida na kupunguza uwekezaji wa mali zisizozalisha haraka (real estate) na kuwa na uainishaji sahihi wa mali za Mfuko. Ilipendekezwa wakati wa ukaguzi wa mwaka uliopita kwamba uongozi unapaswa kutekeleza agizo la Bodi kwa kupitia upya muundo wa uwekezaji na kuelekeza rasilimali zaidi kwenye uwekezaji wa miradi yenye faida kubwa zaidi.

Wakati wa ukaguzi wa sasa haikuonekana kama uongozi wa ZSSF uliyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa badala yake ilibainika kuwa Menejimenti iliendelea kuwekeza kwenye mali zisizohamishika (real estate) ambazo zilionekana kuwa na muda mrefu wa malipo na marejesho yatokanayo na uwekezaji usioridhisha ambapo fedha nyingi zimebaki mikononi mwa wadaiwa mapato ambayo uwezekano wa kurejesha ulikuwa hauridhishi na pia kulikuwa na matarajio ya kuwekeza kwenye miundombinu (yaani uwekezaji katika ujenzi wa kituo cha daladala na bustani) unaotarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Ukaguzi ulipitia mpango wa uwekezaji wa miaka mitatu (3) na kubaini kuwa Mfuko umetenga shilingi bilioni 169.44 kwa ajili ya uwekezaji wa majengo ambayo kwa maoni ya mkaguzi uwekezaji wa aina hiyo hauna tija kwani utazalisha kiasi kidogo cha

mapato kwa miaka mingi. Kwa hali hii mtiririko wa fedha na uwekezaji huenda usitoshe kulipa mafao ya wanachama katika siku zijazo.
Ukaguzi unapendekeza uongozi wa ZSSF kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na kupitia upya muundo wa uwekezaji na kuelekeza rasilimali zaidi kwa uwekezaji wenye tija ili kuokoa Mfuko kufilisika.

**Majibu ya Hoja**

Menejimenti ya Mfuko imeyafanyia kazi mapendekezo ya Bodi ya Wadhamini kwa kubadilisha Sera za Uwekezaji kama ilivyoshauriwa kwenye Ripoti ya Tathmini. Ubadilishaji huo umesaidia Mfuko kuwekeza zaidi kwenye miradi yenye faida kubwa na kupunguza uwekezaji kwenye miradi yenye faida ya wastani. Wakati ukaguzi unafanyika Mpango wa uwekezaji ulikuwa unaelekea kumalizika muda wake na hivyo kupelekea kutokubadilishwa, mabadiliko yalifanyika katika mpango wa uwekezaji mpya uliotengenezwa ambao ulizingatia agizo hili. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2021/22 Mfuko haukufanya uwekezaji wowote katika miradi ya majengo.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imeridhika na majibu ya Mfuko kutokana na uhalisia uliokuwepo, hivyo, imeifuta hoja hiyo.

### 5.2.10.11 Majengo ambayo ni Vitega Uchumi vya Mfuko vinavyohitaji ukarabati mkubwa

Ukaguzi ulitembelea majengo ya ZSSF tarehe 24 Novemba, 2021 na kubaini baadhi ya majengo yanahitaji ukarabati mkubwa ili kuyaboresha kwa kuyaweka katika mazingira mazuri. Majengo yaliyoainishwa ambayo yanahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa ni pamoja na yafuatayo: -

1. Majengo ya zamani yaliyopo Mbweni ambayo ni majengo chakavu yenye nyasi nyingi zinazozunguka majengo na rangi hafifu. Majengo yanahitaji ukarabati mkubwa ili kurekebisha madirisha, milango, upakaji rangi ukuta na sehemu nyingine za jengo ili kurejesha hali ya majengo.
2. Hakuna ukarabati na matengenezo ya eneo la Biashara katika jengo la Mwanakwerekwe (shopping centre) yaliyofanyika. Mahojiano na viongozi waliohusika yalibaini kuwa jengo hilo halifai kufanya biashara wakati wa mvua kutokana na kuvuja na kusababisha usumbufu kwa wapangaji kutokana na kuingia maji vyumbani. Upakaji rangi wa kuta za nje na za ndani na matengenezo pamoja na uwekwaji wa lifti mpya unahitaji kujumuishwa kama ni sehemu ya ukarabati.

Ukaguzi umebaini kuwa Mfuko wa Hifadhi ya jamii umekuwa ukijikita katika kuanzia mipango ya kuendeleza miradi mipya ya uwekezaji katika majengo na kupuuza kuchukua hatua za matengenezo katika majengo yake ya zamani ambayo yataweza kusaidia mipango ya muda mfupi ili kunusuru majengo hayo kuharibika na kupelekea Mfuko kupata hasara kutokana na kufanya ukarabati kwa kutumia gharama kubwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuweka mipango ya ukarabati wa majengo yake yote ambayo inaweza kusaidia mipango ya muda mfupi kwa ajili ya kufanya matengenezo ya mara kwa mara ili kuyaweka katika mtazamo mzuri wa kuwavutia wafanyabiashara/wapangaji kwa lengo la kuongeza mapato ya uwekezaji kabla majengo hayo hayajafi kia kwenye uharibifu mkubwa kama ilivyo sasa na kupelekea gharama kubwa za ukarabati.

**Majibu ya Hoja**

Mfuko wa Hifadhi ya jamii Zanzibar umekuwa ukiyafanyia matengenezo majengo yake ya uwekezaji kila ambapo majengo hayo yanahitaji matengenezo.

Kwa upande wa Jengo la Mwanakwerekwe na Mbweni ya zamani (old) kwa sasa Mfuko unaendelea na taratibu za zabuni na inategemewa ukarabati utafanyika mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2023/24.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imeridhika na majibu ya Mfuko kutokana na uhalisia uliokuwepo, hivyo, imeifuta hoja hiyo.

**5.2.10.12 Kukosekana kwa makubaliano ya matumizi ya nyumba za ZSSF katika umiliki wa Taasisi nyengine za Serikali**

i. **Nyumba za ZSSF zilizochukuliwa na Serikali TZS 700,000,000**

Ukaguzi ulifanya mapitio ya nyaraka mbali mbali za majengo yanayomilikiwa na ZSSF kwa ajili ya uwekezaji (Mbweni Mpya) na kubaini hadi kufikia tarehe 24 Novemba 2021, majengo hayo bado hayajauzwa na yamechukuliwa na Serikali. Miongoni mwa majengo hayo ni nyumba yenye namba 10A1, 10B1, 11B1 na 14B1.

Kutokana na kumbukumbu na mahojiano yaliyofanywa na viongozi wenye dhamana yalibaini kuwa hakukuwa na makubaliano ya kimaandishi kati ya ZSSF na Serikali yanayoainisha vigezo na masharti ya matumizi ya majengo hayo. Katika ukaguzi wetu tulibaini kila nyumba moja itauzwa kwa gharama ya shilingi 175,000,000 hivyo kwa nyumba zilizochukuliwa zitagharimu jumla ya shilingi 700,000,000 kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba AB.199/246/01 ya tarehe 16 Machi, 2021 iliyopelekwa kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Wizara ya Fedha na Mipango.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba FJ: 7/539/02/03/55 ya tarehe 18 Machi, 2021 iliyotumwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa ZSSF ilibainisha Serikali kupitia Ofi si ya Rais Fedha na Mipango imekubaliana na vigezo na masharti yaliyotolewa na kuthibitisha kununua nyumba hizo kwa mujibu wa maelekezo tuliyopatiwa kutoka ZSSF. Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu nambari

ZSSF/AB.199/246/04/02/193 ya tarehe 17 Septemba, 2021 iliyoandikwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwenda kwa Katibu Mkuu Ofi si ya Rais Fedha na Mipango iliyodai kuomba malipo ya nyumba hizo pamoja na kujaza fomu ya maombi kama sehemu ya nyaraka za mkataba wa mauzo ya nyumba hizo.

Hata hivyo, ilibainika Serikali kupitia Katibu Mkuu - Fedha na Mipango kutokuonesha nia ya kununua nyumba hizo kwa ajili ya matumizi ya Serikali baada ya kupelekewa hati za mauzo kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba CAB.2/199/01/05 ya tarehe 01 Oktoba, 2021 aliyotumiwa Mkurugenzi Mkuu wa ZSSF inahusika. Kwa mujibu wa barua nyenye kumbukumbu namba ZSSF/AB.199/246/04/02/194 ya tarehe 22 Oktoba,2021 ZSSF ilimuandikia barua Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango kuomba ufafanuzi wa malipo ya ghorofa 4 katika kipindi cha umiliki wa nyumba hizo, kipindi cha kukabidhi nyumba hizo kwa ZSSF na kurudisha funguo za nyumba hizo kwani kwa kuendelea kukaa ndani ya nyumba hizo inasababisha ugumu kwa ZSSF kuuza nyumba zilizotajwa kama ilivyokusudia.

Katika kujibu hoja zilizojitokeza katika barua ya ZSSF hapo juu ya tarehe 22 Oktoba, 2021 Katibu Mkuu Wizara ya Fedha alimuandikia barua Mkurugenzi Mkuu wa ZSSF barua yenye kumbukumbu namba CA.2/199/01/10 ya tarehe 2 Novemba, 2021 akiuagiza Mfuko huo kuwasiliana na Katibu Mkuu-Ikulu ili kupata hatma ya nyumba hizo kuhusiana na kodi ya pango na tarehe ya kukabidhiwa nyumba hizo kwa madai kuwa viongozi wanaokaa kwenye nyumba hizo ni wa Ikulu.

Hadi tunakamilisha ukaguzi tarehe 28 Disemba,2021 ukaguzi umeshindwa kujua hatma ya upatikanaji wa kodi kwa kipindi chote nyumba hizo zilivyokaliwa pamoja na urejeshwaji wa funguo za nyumba hizo kwa mmiliki (ZSSF) kwa ajili ya kuziuza au vyenginevyo.

**Majibu ya Mfuko**

Serikali ilionyesha nia kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar wa kuzinunua nyumba tajwa hapo juu, baada ya Mfuko kufuatilia nyumba hizo Serikali iliamua kutozinunua tena na kuzirudisha kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar. Kwa sasa nyumba hizo zote zimesharudishwa kwa Mfuko na kuuzwa kwa wanunuzi wengine.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imebaini kuwa Serikali ilizizuia nyumba hizo kwa muda wa mwaka mmoja bila ya kulipa fedha yoyote, hata hivyo, Mfuko haukupata hasara kwani bei iliyouzwa ililingana na ile bei ambayo nyumba hizo zingekodishwa, hivyo, hoja hii imeifuta.

ii. **Nyumba ya ZSSF Inayokaliwa na ZBA**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii unamiliki ardhi na jengo iliyopo Kilimani ijulikanayo kwa jina la ZSSF Kilimani Annex (zamani ikiitwa Old Bakhresa). Ukaguzi umebaini pamoja na Mfuko huo kuwa na mpango wa kulitumia jengo hilo kwa shughuli zake za uwekezaji, jengo hilo lilionekana kutumiwa na ZBA. Baada ya mahojiano na maafisa wanaohusika kutaka kujua kuhusu ada ya ukodishwaji au sababu ya ukaaji ilibainika kuwa hapakuwa na mapato yoyote ya fedha ambazo Mfuko ulikuwa ukipata licha ya kwamba Mfuko umeweka jengo hilo katika kundi la Mali ya uwekezaji. Aidha ilibainika kuwa mhusika alitakiwa kukaa ndani ya nyumba hiyo kwa muda usiozidi miezi minne (4) kama ilivyoonyeshwa kwenye barua yenye kumbukumbu namba ZSSF.36/KEY/VOL.III/46 ya tarehe 29 Machi, 2021 (barua imeandikwa na ZSSF kwa Waziri wa Fedha na Mipango ikiomba hatima ya nyumba inayokaliwa na ZBA tangu mwaka 2017) iliyoambatanishwa na barua yenye

kumbukumbu namba MOICT/M.120/C.8/VOL.I/92 ya tarehe 30 Agosti, 2017 iliyoandikwa na Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar kwa Mkurugenzi Mtendaji ZBA ikimuomba Mkurugenzi Mwendeshaji kuwasilisha mara moja mipango mbadala ya muda mfupi na mrefu ya mahali pa kukaa baada ya kipindi cha miezi 4 kilichotolewa na ZSSF kupita.

Tangu wakati huo (29 Machi, 2021) ZSSF bado haijapokea barua yoyote kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Mipango kuhusu suala hilo. Ushahidi wa juhudi za ufuatiliaji zilizofanywa kuikumbusha Wizara pia haukupatikana.

Kutokana na hali hiyo ukaguzi ulishindwa kubainisha sababu za msingi zinazopelekea ZBA kuendelea kukalia nyumba hiyo licha ya muda waliotakiwa kuhama kuisha na hakuna tija inayopatikana ya kuiwezesha ZSSF kutekeleza mipango yake ya uwekezaji.

Uwepo wa dosari hiyo unapelekea kuusababishia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii upotevu wa fedha za wanachama ambazo zingeweza kupatikana katika kipindi cha kukaliwa na ZBA au kuwekeza katika rasilimali nyingine za kuzalisha mapato.

**Majibu ya Mfuko**

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar uliwaazima jengo chakavu ZBA kwa matumizi ya Ofisi yao, ZBA walichukua jengo hilo na kulikarabati hivyo iliwalazimu kulitumia muda mrefu hadi hapo walipopata ofisi yao, ZSSF haikuwa na pingamizi kwa muda waliotumia ZBA kwenye jengo hilo.

Kwa vile ZBA wamehamia eneo jengine kwa shughuli za ofisi zao tayari jengo hilo wamesharejesha kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imeridhika na majibu ya Mfuko kutokana na uhalisia uliokuwepo, hivyo, imeifuta hoja hiyo.

**5.2.10.13 Uwepo wa kiasi kikubwa cha michango ya wanachama ambayo haijaingizwa katika akaunti za wanachama husika shilingi bilioni 15**

Katika ukaguzi uliofanyika kuhusiana na mapitio ya taarifa ya michango ya wanachama ukaguzi umebaini uwepo wa shilingi bilioni 15 ambazo zinatokana na michango ya wanachama ambayo haijangizwa katika akaunti za wanachama husika hadi kufi kia tarehe 1 Disemba 2021.

Aidha, katika kupitia kumbu kumbu za wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ilibainika mapitio hayo ilibainika tatizo hilo lilianza kuwepo tangu mwaka 2012/2013 kwa kiasi cha shilingi 513,665,063 ambacho kwa sasa kimeongezeka hadi kufi kia shilingi 15,005,211,569. Kutokana na uwepo wa changamoto hiyo ukaguzi umebaini sababu kubwa iliyochangia kuongezeka kwa michango ya wanachama ambayo haijaingizwa katika akaunti za wanachama husika ni ukosefu wa namba za usajili kwa wafanyakazi wengi wanaochangia ili itambulike kwa urahisi katika mfumo unaotumika (FUMIS) katika akaunti husika.

Mahojiano yaliyofanywa na viongozi wenye dhamana yalibaini kuwa hakukuwa na ufuatiliaji wa kutosha wa wanachama waliochangia (wafanyakazi) ili kuhakikisha wanakuwa na namba za usajili mara tu baada ya kusajiliwa na Mfuko (ZSSF). Hata hivyo, jukumu la kufuatilia suala hilo halikuelezwa bayana kati ya kitengo cha

ufuatiliaji (compliance unit) na usajili kwani kila kitengo kinaonyesha kwamba hakijakabidhiwa jukumu hilo.

Vile vile, hakukuwa na ushahidi kwamba Mfuko uliweka udhibiti mzuri kama vile kutoa adhabu kwa kila mwanachama mwajiri baada ya muda fulani ikiwa wafanyakazi wote walio chini ya waajiri hao watakuwa hawana namba za usajili kama njia mbadala ya kuhimiza usajili wa lazima ili kuzuia suala la ongezeko la kiasi cha michango isiyoingizwa katika akaunti za wanachama husika badala ya kuwasubiri waje kwa hiari.

Kushindwa Kushindwa kutatua tatizo hili kunaweza kusababisha usumbufu na ucheleweshaji usio wa lazima wakati wa malipo ya mafao kwa wanachama.
Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kufanya mambo yafuatayo:-

1. Kufuatilia watumishi wote waliosajiliwa bila kutumia namba za wanachama kwa lengo la kuondosha dosari iliyobainika.
2. Kitengo chenye jukumu la kufuatilia usajili wa wanachama kihakikishe usajili kamili wa wanachama ambao wanaweza kutambuliwa kwa uwazi kwa namba zao za usajili.
3. Udhibiti mkali unapaswa kuwekwa kwa waajiri wanaochangia kama njia mbadala ya kuzuia mwelekeo wenye mashaka.

**Majibu ya Mfuko**

Waajiri na Waajiriwa wa Sekta zote za Umma na Binafsi hawafuatilii kwa kina taarifa sahihi zikiwemo nambari za wanachama (Waajiriwa). Hivyo, inapelekea wakati wa

uwasilishaji wa michango yao kukosewa nambari na kupelekea michango yao kuingizwa katika hesabu ya pamoja (Suspense).

Mfuko unaendelea kuchukua jitihada za kuhakikisha suala hili linamalizika kwa kuendela kutoa elimu kwa waajiri na wachangiaji pia kuendelea kufanya uhakiki wa mara kwa mara kwa wanachama wake wote wa Serikali na Binafsi ili kurekebisha taarifa (Data Clearance) ikiwemo nambari za uanachama.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inaunga mkono hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo, kutokana na hatua mbali mbali zilizochukuliwa na Mfuko dhidi ya hoja husika, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hiyo.

**5.2.10.14 Ufuatiliaji wa Wanachama Waajiri Wanaokiuka Sheria ya ZSSF (Malimbikizo ya Michango) kufanywa kwa njia mkono**

Katika ukaguzi uliofanyika tulifanya mahojiano na maafisa wenye dhamana chini ya Kitengo cha ufuatiliaji (compliance unit) na kubainika ufuatiliaji wa wanachama waajiri waliokiuka (malimbikizo ya michango ya wanachama) ulifanyika kwa mkono jambo ambalo ilitarajiwa mfumo wa Taarifa za Wanachama (FUMIS) ungetoa muhtasari wa ripoti kwa kila mwanachama inayoonyesha kiasi kilichochangiwa katika mwezi fulani na malimbikizo ambayo mwajiri hajatuma kwenye Mfuko. Sababu za kutoa taarifa za malimbikizo nje ya mfumo (manually) hazikuweza kufahamika.

Aidha, ukaguzi ulibaini idadi ya waajiri hai na wasiofanya kazi wanaochangia ZSSF haikuweza kubainishwa kwa kuwa mfumo (FUMIS) haukuweza kutoa ripoti kama hiyo.

Kushindwa kwa mfumo wa FuMIS kutoa taarifa za wanachama hai na wasiochangia kunaweza kupelekea kushindwa kujua mwenendo wa idadi ya wanachama wanao kiuka sheria ya ZSSF.

Ufuatiliaji wa wanachama wanaokiuka Sheria ya Mfuko (kulimikiza madeni ya wanachama) nje ya mfumo wa FuMIS (manually) ni kazi inayochosha, inachukua muda mwingi na haileti tija na ufanisi unaotarajiwa kwani waliokiuka wote wanaweza wasijulikane kwa ufuatiliaji wa haraka na hivyo kupunguza ukusanyaji wa michango ya wanachama.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuangalia upya mfumo wa FuMIS ili kuhakikisha unafanya zoezi hili muhimu pamoja na kutoa mafunzo ya kutosha kwa watumiaji wa mfumo ili kuhakikisha kuwa malimbikizo ya michango yanatolewa kwenye mfumo wa kieletroniki (FuMIS) ili kuongeza kiwango cha utii wa Sheria ya Mfuko na kuongeza ukusanyaji wa michango ya wanachama.

**Majibu ya Mfuko**

Mfumo wa kieletroniki wa FUMIS haujajumuisha taarifa za wanachama wanaolimbikiza michango isipokuwa Mfuko unatumia tovuti ya uwasilishaji wa michango (Employer Portal) kupata taarifa ya wanachama wanaolimbikiza michango yao.

Mfuko ulichukua ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kwa sasa Mfuko umeboresha Mfumo wa taarifa za wachangiaji (Employer Portal) ambapo taarifa za wanachama wanaolimbikiza michango zinapatikana.

Vile vile, Mfuko unaendelea na hatua za kujumuisha kipengele cha kufuatilia malimbikizo ya michango ya wanachama kwa kutumia mfumo wa taarifa za wanachama (FUMIS) kama ilivyoshauriwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inaunga mkono hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo, kutokana na hatua mbali mbali zilizochukuliwa na Mfuko dhidi ya hoja husika, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hiyo.

**5.2.10.15 Utendaji wa Mfuko wa Hiari (VSS- Voluntary Social Scheme)**

Kwa mujibu wa kanuni ya 3(1) na (2) ya kanuni za Mfuko wa Hiari wa -VSS G.N 49/2015 inaitaka ZSSF (Mfuko Mkuu) kuanzisha uendeshaji wa mpango wa uchangiaji wa hiari ambao utakuwa unafanya kazi chini ya mwamvuli wa Mfuko Mkuu. Kwa kuzingatia kanuni zilizotajwa, ZSSF ilianzisha uendeshaji wa mfuko huo wa hiari (VSS) tangu mwaka 2015. Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika katika eneo hili kuhusu uendeshaji wa mfuko wa hiari tangu kuanzishwa kwake ulibaini kasoro zifuatazo;-

1. **Kutokuwepo kwa mpango mkakati**

Haikujulikana dhahiri kama Mfuko Mkuu una mpango mkakati wa uendeshaji wa mfuko wa hiari ambao unaweza kuwa kama dira kuu inayobainisha dira na dhamira kuu itakayofikiwa katika kipindi fulani (yaani taswira ya wapi Mfuko wa hiari unatakiwa kuwa katika siku zijazo kwa mfano baada ya miaka 3 hadi 5).

2. **Kutokufanyika kwa Tathmini ya Utendaji kazi wa Mfuko wa Hiari Tangu kuanzishwa Kwake**

Haikufahamika dhahiri kama Mfuko umewahi kufanya uchambuzi wa jinsi mfuko umekuwa ukifanya kazi tangu kuanzishwa kwake na kuweka hatua za kuboresha pamoja na kusitisha mfuko huo.

Ukaguzi umebaini kuwa gharama zote za kiutawala za uendeshaji wa mfuko wa hiari kama vile gharama za mafuta zinazohusiana na shughuli za uhamasishaji, mishahara na posho zinazohusiana na kazi hiyo kwa watumishi wanaosimamia shughuli za mfuko, gharama za vifaa vya kuandikia na kadhalika zilionekana kumezwa na Mfuko Mkuu.

Hata hivyo, imebainika vyanzo vya kufadhili mfuko mdogo (wa hiari) ili kuimarisha uendelevu wa mfuko havikutambuliwa vyema na kuchambuliwa. Kanuni ya 4(d) ya Mfuko wa hiari (VSS) GN 49/2015 inataka fedha zilizopatikana kutoka kwenye mfuko huo ziwekezwe katika miradi inayowezekana ambayo si hatarishi (risk free investment). Hata hivyo, ukaguzi haukubaini kama kiasi cha fedha kilichokusanywa kutoka kwenye mfuko huo tangu kuanzishwa kwake kiliwekezwa kutokana na kutokupatiwa orodha ya vitega uchumi vilivyotokana na fedha za mfuko wa hiari (VSS) na kupata riba hadi tunakamilisha ukaguzi wetu.

Kushindwa kufuatilia ipasavyo maendeleo ya Mfuko wa hiari ili kubaini jinsi unavyofanya kazi kunaweza kusababisha kumeza fedha zote zinazopatikana kutoka katika Mfuko wa lazima (Mfuko Mkuu) hali ambayo itapelekea Mfuko wa lazima kushindwa kufanya kazi yake ya msingi ambayo ni kulipa mafao ya wanachama.

Vile vile, kufanya kazi bila mpango mkakati wa Mfuko wa hiari (VSS) ni kama kufanya kazi bila muongozo hali ambayo inaweza kusababisha kudhoofika kwa Mfuko huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kufanya tathmini ya uendeshaji wa Mfuko wa hiari tangu kuanzishwa kwake na kuweka mikakati (mipango mkakati) ili kuhakikisha utendaji bora kutokana na kuwepo kwa mwenendo mbaya wa utendaji. Njia moja ya kuhakikisha uendelevu wa Mfuko huo ni kuwekeza fedha zinazopatikana katika vitega uchumi vyenye tija na ufanisi.

**Majibu ya Hoja**

Mpango Mkakati mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umejumuisha shuhuli za utekelezaji za Mfuko wa Hiari ambao umeeleza malengo na kazi za Mfuko huo, kwa kuzingatia ushauri uliotolewa Mfuko tayari unaendelea kuufanyia kazi ushauri huo na tunategemea mwaka wa fedha 2023/2024 kufanya maboresho ya Mpango Mkakati Mkuu ikiwemo kuzitenganisha dira na dhamira.

Vile vile, Mfuko utaendelea kufanya tathmini ya kina ya Mfuko wa Hiari kama inavyofanyika kwa Mfuko Mkuu.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inaunga mkono hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo, kutokana na hatua mbali mbali zilizochukuliwa na Mfuko dhidi ya hoja husika, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hiyo.

### 5.2.10.16 Kuchelewa kutekeleza mchakato wa utoaji wa Zabuni kwa baadhi ya Zabuni

Ukaguzi ulifanya mapitio ya michakato ya zabuni iliyofanywa na Mfuko katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021 na kubaini mwenendo wa ucheleweshwaji wa zabuni kwa baadhi ya zabuni kulikosababishwa na kurudiwa kwa

mchakato wa zabuni/matangazo mapya ambapo baadhi ya zabuni hizo zilionekana kufutwa mwishoni.

Aidha, kutokana na uwepo wa changamoto hiyo ukaguzi umebaini uwepo wa dosari ya kushindwa kubainisha kiasi halisi, ubora na maelezo ya bidhaa/huduma inayohitajika katika kipindi fulani kitendo ambacho mwishowe kiliathiri kiasi cha fedha kilichopangwa awali kwa ajili ya utekelezaji wa manunuzi hayo kwa zaidi ya bei zisizo halisi na kusababisha kutangazwa tena au kufutwa kwa zabuni.

Kushindwa kufafanua mahitaji ya mtumiaji ipasavyo na idara za watumiaji wakati wa hatua za awali za utayarishaji wa mpango wa ununuzi wa kila mwaka husababisha utekelezaji usiofaa wa mpango kwa gharama kubwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuhakikisha kuwa idara za watumiaji zinawasiliana na kusaidia Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Uuzaji wakati wote wa mchakato wa manunuzi au uuzaji hadi kufi kia hatua ya kuingia mikataba kwa kuandaa mahitaji yao mapema kabla ya kuingizwa katika mpango wa mwaka wa manunuzi ili kuepusha mchakato wa manunuzi ambao unaweza kuchukua muda mrefu na kupelekea upotevu wa fedha za wanachama kutokana na utangazaji upya wa zabuni na taratibu za tathmini zisizo za lazima.

**Majibu ya Mfuko**

Ucheleweshwaji wa kutekelezwa mchakato wa utoaji wa zabuni hutokea kutokana na aidha Mfuko kughairisha manunuzi, kutoendelea na mpango wa manunuzi kwa wakati husika, kubadilisha mipango ya utekelezaji wa majukumu ya Idara husika au kupanda gharama za bidhaa au huduma ukilinganisha na makisio yaliyopangwa.

Mipango ya manunuzi huwa ni makisio ya mahitaji kwa Mfuko hivyo hakuna athari ikiwa manunuzi hayo hayakuhitajika na hayakutumika.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC iliukata Mfuko kutoa maelezo kwa kila kipengele kama inavyoonekana kwenye Kiambatanisho Namba 3 cha Ripoti ya Mkaguzi Mkuu, hata hivyo, Mfuko haukuwasilisha maelezo hayo kwa Kamati kama ulivyoelekezwa.

Kutokana na dosari iliyobainika na Mkaguzi Mkuu, Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kuweka idadi ndogo ya ununuzi na kwa kuzingatia kipaombele ili hoja kama hiyo isijitokeze tena.

**5.2.10.17 Kuchelewa Kusaini Mkataba Baada ya uamuzi wa tuzo za Zabuni**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 139 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2021 inataka ndani ya siku ishirini na nane (28) za kalenda baada ya kutimiza masharti yote Afisa Masuuli na mzabuni wataingia mkataba rasmi wa usambazaji wa bidhaa, utoaji wa huduma au kufanya kazi za ujenzi/ ukarabati kabla ya kuanza kazi hizo.

Hata hivyo, mapitio ya mchakato wa kusaini mkataba baada ya uamuzi wa tuzo za zabuni kwa wazabuni mbalimbali ilionekana kuchukua muda mrefu.

Kucheleweshwa kwa utiaji saini wa mkataba husababisha kucheleweshwa kwa utekelezaji wa kazi, huduma au bidhaa ndani ya tarehe zilizolengwa za kukamilisha kazi hizo na zinaweza kusababisha usumbufu kwa watumiaji na athari za gharama kubwa za manunuzi kwa taasisi ikiwa itatumia njia mbadala kama vile manunuzi ya dharura ili kupata huduma, kazi au bidhaa.

Ukaguzi unashauri ongozi wa ZSSF kuhakikisha michakato yote ya ununuzi inatekelezwa kulingana na mpango wa manunuzi na hatua yoyote ya hitilafu iliyobainishwa au itakayobainishwa katika mchakato wa zabuni inapaswa kushughulikiwa ipasavyo ili kuepusha athari za gharama kwa Mfuko zinazosababishwa na mchakato wa manunuzi kuchukua muda mrefu.

**Majibu ya Hoja**

Mfuko huwa unautaratibu wa kutayarisha mikataba na kuiwasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mamlaka nyengine za Serikali (ZBA, ZICTIA, EGov n.k), mara tu baada ya uamuzi ya tuzo ya zabuni kutolewa.

Hivyo, ucheleweshwaji wa kusaini huwa unasababishwa na mchakato mzima wa uwasilishwaji wa mikataba hiyo na kupokea ushauri kutoka kwenye Mamlaka hizo.

Katika kuhakikisha utekelezaji wa ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Mfuko ulifanya mawasiliano na Mamlaka hizo kwa ajili ya kukubaliana njia nzuri ya muda wa uwasilishwaji na upokewaji wa ushauri wao.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inaunga mkono hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo, kwa kuwa suala linalodaiwa lipo nje ya uwezo wa Mfuko, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hiyo.

### 5.2.10.18 Mpango wa Manunuzi ambao haujatelezwa kwa Mwaka wa fedha 2020/21

Kwa mujibu wa kikao cha Bodi ya Zabuni cha 7 (kikao cha kawaida) kilichofanyika tarehe 05 Machi, 2021 ukaguzi ulibaini kuwa Bodi ya Zabuni ilikiagiza kitengo cha

Manunuzi na Ugavi kupitia upya mpango wa manunuzi ya mwaka na kubainisha manunuzi yote ambayo hayakuweza kufanyika katika mwaka huo kwa ajili ya kuidhinishwa tena kwenye mpango wa manunuzi katika mwaka unaofuata. Orodha ya manunuzi yaliyopangwa lakini yameshindwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Mapitio ya utekelezaji wa jumla wa shughuli za manunuzi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umebaini kuwa kati ya shughuli 32 zilizopangwa, shughuli 18 hazikutekelezwa sawa na asilimia 56.25 na shughuli 14 zilitekelezwa sawa na aslimia 43.75. Kwa ujumla hali ya utekelezaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2020/2021 ilionekana kutoridhisha.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na maofisa wanaohusika na kubaini mambo yafuatayo: -

1. Ukosefu wa utayari (commitment) kwa idara ya watumiaji (user departent) katika kubainisha mahitaji na vipaumbele vinavyopaswa kufanywa katika kipindi fulani.

2. Idara za Watumiaji kushindwa kutathmini uwezo wake wa kutekeleza shughuli zilizoratibiwa ambayo ni pamoja na kuzingatia masuala kama vile uandaaji wa bajeti inayofaa kupitia shughuli za utafiti wa soko mapema, kuandaa vipimo vya kiufundi na kiasi kinachohitajika.

Kushindwa kwa Idara za watumiaji kuainisha misingi ya zabuni na kufanya utafiti wa soko mapema juu ya bei za zabuni zilizolengwa kulisababisha kupangwa kwa shughuli nyingi zisizo za uhalisia ambazo nyingi ziliishia kufutwa pamoja na kughairishwa

kutokana na bei kuwa juu zaidi maradufu ya kiasi kilichopangwa hapo awali kitendo ambacho kililazimu kujumuishwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka uliofuata.

Kuwepo kwa utekelezaji hafifu wa mpango wa manunuzi wa mwaka unapelekea mpango uliondaliwa kuwa si wa uhalisia hivyo kuwa vigumu kutekelezwa au kutekelezwa kwa gharama kubwa ambayo ni upotevu wa fedha za wanachama ambazo zingeweza kuwekezwa ili kupata riba kutokana na uwekezaji wenye tija. Upo uwezekano kwamba Idara za watumiaji hazifahamu kikamilifu jukumu lao muhimu wakati wa kupanga mpango wa ununuzi wa kila mwaka.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF uhakikishe kuwa utayarishaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka uwe wa kushirikishwa. Kila idara ya watumiaji inapaswa kubainisha kwa uwazi mahitaji na uwezo wake katika kufanya shughuli zilizopangwa kabla ya kupeleka mipango kwa kitengo cha ununuzi na ugavi kwa ajili ya utekelezaji ili kuimarisha utekelezaji mzuri wa mpango huo.

**Majibu ya Hoja**

Mfuko huwa una utaratibu wa kuupitia Mpango wa Manunuzi kila baada ya miezi mitatu (Quarterly basis). Vile vile, Mfuko hutathmini tena (Evaluate) miradi yake ya uwekezaji kabla ya kutekelezwa na endapo Mfuko umebaini Mpango wa Manunuzi au mradi wa Uwekezaji hautoleta tija kabla ya kutekelezwa Mfuko huacha kwa kutekeleza mradi huo. Hivyo, miradi hiyo ilionekana haina tija kwa kipindi hicho ndio maana haikutekelezwa na ni jambo ambalo lililopelekea kutokutekelezwa kwa Mpango wa Manunuzi.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja imebaki kama ilivyo, hasa ikizingatiwa kuwa vitu vilivyopangwa ni vingi.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inaushauri Mfuko kufanya uchambuzi yakinifu mapema ili kuweza kujua shughuli gani inaweza kutekelezeka katika mwaka husika kwa lengo la kuwa na shughuli chache ambazo zitatekelezeka.

**5.2.10.19 Dosari zilizobainika katika baadhi ya Vipengele vya Mikataba**

Ukaguzi ulifanya mapitio ya mikataba mbalimbali iliyoingiwa kati ya ZSSF na Wakandarasi mbalimbali wa bidhaa, kazi, huduma na ushauri na kubaini dosari mbalimbali kama ilivyobainishwa katika kila mkataba uliopitiwa kama inavyoonyeshwa hapo chini: -

1. **Mkataba kati ya ZSSF dhidi ya KNIGHT FRANK TZ LTD na TERRANOVA wa utoaji wa huduma za ukodishaji na usimamizi wa Majengo ya ZSSF yaliyopo Zanzibar**

Katika kipengele cha makubaliano ya mkataba huu dosari zifuatazo: -

a. **Malipo ya kamisheni kwa jumla ya takwimu za makusanyo ya kodi (Payment of Commisionon gross figure)**

Mkataba ulioingiwa kati ya ZSSF na NIGHT FRANK TZ LTD ulisainiwa tarehe 11 Mei, 2020 kwa muda wa miaka miwili (2) ambao unamalizika tarehe 10 Mei, 2022 huku mkataba kati ya ZSSF na TERRANOVA ulitiwa saini tarehe 05 Agosti, 2019 kwa miaka miwili (2) muda uliomalizika tarehe 05 Agosti, 2021.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya bei ya mkataba ya utoaji wa huduma za usimamizi wa mali kwa kukodisha na usimamizi wa Majengo ya ZSSF yanayosimamiwa na Knight Frank TZ Ltd na Terranova ilibaini kuwa Knight Frank alilipwa kamisheni ya asilimia 4.5 kwenye mapato ya jumla ya kukodisha yaliyokusanywa kwa mwezi vivyo hivyo na Terranova ililipwa asilimia 5 ya mapato ya kila mwezi ya kukodisha.

Ukaguzi umebaini malipo kulingana na takwimu za jumla yanaonekana kuwa ni makubwa kwa ZSSF kwa kuzingatia kwamba asilimia 15 ya kodi ya VAT na asilimia 10 ya Kodi ya zuio ya kodi ya kukodisha na gharama zingine zinazohusiana za matengenezo hulipwa na Mfuko. Hivyo ada zinazolipwa kwa watoa huduma kwa mujibu wa mikataba na masharti hayakuwa ya kiuchumi kwa Mfuko.

**Majibu ya Hoja**

Mfuko uliingia makubaliano na Kampuni zilizotajwa hapo juu kwa ajili ya kusimamia na kuendesha miradi yake inayohusiana na majengo (Real Estate).

Kutokana na mapungufu ya makubaliano ya kimkataba yaliyojitokeza awali kama ilivyoripotiwa kwenye taarifa hii, Mfuko uliamua kutoendelea tena na Kampuni ya KNIGHT FRANK baada ya Mkataba wa awali kumalizika. Hivyo, Mfuko uliingia Mkataba kwa njia ya zabuni na Kampuni ya TERRANOVA kwa ajili ya kusimamia na kuendesha miradi yake inayohusiana na majengo (Real Estate) kulingana na ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa maslahi ya pande zote mbili.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu yaliyotolewa na Mfuko, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kuwa makini wakati inafunga mikataba ili kuepuka kupata hasara, sambamba na kupata hoja zisizo na msingi.

**b. Malipo ya gharama za Huduma zilizolipwa awali (Mkataba kati ya ZSSF na TERRANOVA)**

Kwa mujibu wa kifungu cha sita (6) cha kanuni na masharti ya mkataba kinaeleza kuwa "mtoa huduma atasimamia mali zilizotajwa humu kwa niaba ya mwajiri kwa mujibu wa kanuni za usimamizi bora wa mali zisizohamishika na mwajiri atawasilisha kwenye akaunti ya mtoa huduma kiasi cha shilingi 15,484,780 kwa mwezi ambazo zitatumika awali kwa gharama za huduma na matengenezo.

Ukaguzi umebaini kwamba uwekaji wa shilingi 15,484,780 kwa mwezi awali kwa ajili ya gharama za huduma na matengenezo kama ilivyoelezwa katika kifungu cha sita (6) kunatoa mwanya kwa mtoa huduma kupokea kiasi hicho bila gharama kubainishwa kwa matumizi ya huduma hiyo ambayo haina ushahidi wa kufuatiliwa na fedha iliyobaki baada ya kulipa gharama zilizotolewa kwa ajili ya malipo ya huduma na kazi za matengenezo (ndogo) ikiwa zitafanywa.

Aidha, ukaguzi umebaini kifungu cha sita (6) kinatofautiana na kifungu cha nane (8) cha kanuni na masharti ya mkataba ambapo kinaeleza ya kwamba "Mtoa Huduma

atadai na kukusanya na kupokea tozo za huduma kutoka kwa mpangaji kwa ajili ya usimamizi wa mali na malipo hayo yatatumika kwa ajili ya uendeshaji wa mali hizo kwa mujibu wa kanuni na masharti ya mkataba".

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha sita (6) bila ya kuathiri utekelezaji wa kifungu cha nane (8) ukaguzi umebaini kukinzana kwa utekelezaji wa vifungu hivyo kumetoa mwanya kwa mtoa huduma kupata malipo mara mbili baada ya kukusanya malipo ya huduma kutoka kwa wapangaji na sio kama ilivyoainishwa katika kifungu namba sita (6).

**Majibu ya Mfuko**

Mkataba baina ya ZSSF na TERRANOVA uliruhusu kufungua akaunti ya pamoja baina ya pande mbili zetu, akaunti ambayo inawekwa fedha kwa ajili ya kugharamia huduma zote za usimamizi wa majengo yetu. Matumizi ya fedha hizo huratibiwa na kusimamiwa kwa pamoja kulingana na gharama za huduma zinazopatikana pamoja na matengenezo madogo madogo. Fedha inayobaki baada ya kutolewa gharama zote husalia kwenye akaunti ambayo inasimamiwa na pande zote mbili.

Licha ya mapungufu ya vifungu vilivyoainishwa hapo juu Mtoa huduma hakuweza kupokea tozo au ada yoyote, Mkataba mpya baina ya Mtoa huduma na Mfuko umesharekebishwa pamoja na kuweka sawa vifungu vilivyoainishwa hapo juu ambapo sasa Mtoa huduma hawezi kupokea tozo au ada yeyote kwa kipindi chote cha mkataba kwa vile tozo hizo zimeshakusanywa na Mfuko kwenye kodi za mwezi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inaunga mkono uchunguzi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hata hivyo, Kamati imeifuta hoja hii kwa kuwa hakuna athari yoyote iliyopatikana licha ya kuwepo kwa dosari hiyo.

Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kuwa makini wakati inafunga mikataba ili kuepuka kupata hasara.

2. **Ukiukwaji uliobainishwa katika ufuatiliaji wa utendaji Watoa huduma na matokeo ya kazi wanazozifanya**

a. **Kutokuwepo kwa Kipengele katika Mikataba ya kusaidia ZSSF kupima utendaji wa Watoa Huduma (ZSSF Vs KNIGHT FRANK na TERRANOVA)**

Katika mapitio ya mikataba ya huduma za wasimamizi wa majengo kati ya ZSSF VS. KNIGHT FRANK TZ LTD na TERRANOVA ukaguzi umebaini dosari katika ufuatiliaji wa utendaji wa watoa huduma kwa kukosekana vifungu katika mikataba yao ambavyo vingeweza kutumika kama nyenzo ya kuangalia jinsi watoa huduma wanavyofanya kazi vizuri na kuweka hatua za kuboresha utendaji kazi pamoja na kubainisha madhara yatokanayo na mikataba hiyo kwa kutofanya kazi kwa mtoa huduma. Mikataba hiyo ilionekana kuwa inawanufaisha watoa huduma kwa kutaka kulipwa fidia baada ya kucheleweshwa kwa malipo ya kamisheni ya watoa huduma huku Mfuko ukiathirika kwa vile madhara ya kutofanya kazi vizuri yanaweza kusababisha Mfuko kupata hasara ya fedha za wanachama kwa kukodishwa kwa muda mrefu.

Ukaguzi ulitarajiwa kuwa watoa huduma wangekuwa wameekewa lengo la kufikia katika kukusanya kwao kwa mfano kukusanya na kufi kia makusanyo ya asilimia 70

kila robo mwaka au kila mwezi na kama wakishindwa kufikia lengo la makusanyo hayo, kungeliwekwa kipengele cha kupunguzwa kwa kamisheni n.k. Hata hivyo, pamoja na kukosekana kwa vigezo vya msingi katika kutathmini watoa huduma kitengo cha uwekezaji hakikuweza kutoa taarifa za utendaji wa watoa huduma hadi kumalizika kwa mkataba wa mtoa huduma (TERRANOVA) ambae mkataba wake umemaliza tangu tarehe 05 Agosti,2021.

**Majibu ya Mfuko**

Mfuko ulibaini mapungufu hayo kwenye mkataba wa awali kwa vile Mfuko haukuwa na uzoefu wa kuingia kwenye makubaliano ya kuendesha na kusimamia majengo yake. Baada ya mkataba wa awali kumalizika pamoja na kupokea ushauri wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mikataba yote mipya Mfuko umeweka masharti ya kupima utendaji kazi kwa watoa huduma na Mfuko umekuwa unawafuatilia ipasavyo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa licha ya kuwa mkataba huo ulipelekewa Afisi ya Mwanasheria Mkuu lakini bado mkataba huo ulikuwa na upungufu, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kuwa makini wakati inafunga mikataba ili kuepuka kupata hasara, sambamba na kupata hoja zisizo na msingi.

Vile vile, Kamati ya LAAC inaishauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuwa makini wakati inapitia mikataba ili kuepusha lawama kwani Afisi hii ndio tegemeo la kutoa ushauri kwa kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 56 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984.

**b. Kifungu kinachohimiza Utendaji duni wa Watoa Huduma (ZSSF vs KNIGHT FRANK LTD)**

Kifungu cha 6 cha sheria na masharti ya mkataba kinasema kuwa "Mtoa Huduma ataruhusiwa na kusimamia mali zilizotajwa humu kwa niaba ya Mwajiri kwa mujibu wa kanuni za usimamizi bora wa mali zisizohamishika na Mwajiri atabeba gharama za awali za upandishaji vyeo na utangazaji wa majengo, umeme, usafi shaji na ulinzi hadi majengo yawe ya kutosha na wapangaji".

Kifungu hiki kina uwezekano wa kuhimiza mtoa huduma kupunguza juhudi za kuhakikisha kuwa majengo yanakaliwa kikamilifu kama ilivyoainishwa chini ya SCC 1.1 (GCC 1) kwani gharama zote za nafasi zilizo wazi zitagharamiwa na Mfuko kwa muda usiojulikana. Kifungu hicho hakikuweka muda wa kumkemea mtoa huduma kutoa umiliki kamili na madhara ya kutowasilisha kwa ZSSF kutokana na gharama zilizoainishwa katika kipindi cha nafasi hiyo pia hayakutajwa.

**Majibu ya Hoja**

Jengo la biashara alilopatiwa Msimamizi na Mtoa huduma huyo lilikuwa ni jipya na biashara ngeni kwa hapa Zanzibar. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa kipindi kile cha mkataba wa awali haukuona umuhimu wa kuweka muda maalum kwa vile ulikuwa na lengo la kuvutia wafanyabiashara, lakini pia, kumtumia mtoa huduma huyo kwa ajili ya kutuletea wafanyabiashara kwa kipindi chote cha mkataba wake wa awali.
Kwa sasa Mfuko umetoa kipengele hicho cha Mtoa huduma kwa vile tayari jengo hilo limeshapata wapangaji na halihitaji tena kutangazwa tofauti na awali

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Mfuko, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kufanya utafiti wa kina kabla ya kufanya kitu chochote ili kuepuka kupata hasara, sambamba na kupata hoja zisizo na msingi.

3. **Ukiukwaji uliobainishwa katika upeo wa kazi uliofanywa**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika mikataba iliyoingiwa na ZSSF pamoja na watoa huduma mbali mbali imebainika baadhi ya vifungu vya mikataba vilikuwa vikipingana kuhusu upeo/aina ya kazi iliyofanyika na kusababisha mkanganyiko kwa wahusika wa mikataba au msomaji mwingine yeyote wa nyaraka za mkataba. Baadhi ya mikataba iliyobainishwa kuwa na utata wa wigo wa kifungu cha kazi ni kama inavyoonyeshwa hapa chini: -

**a. Mkataba kati ya ZSSF dhidi ya KNIGHT FRANK TZ LTD na ZSSF Dhidi ya TERRANOVA wa utoaji wa huduma za ukodishaji na usimamizi wa Majengo ya ZSSF yaliyopo Zanzibar**

Mkataba ulioingiwa kati ya ZSSF na NIGHT FRANK TZ LTD ulisainiwa tarehe 11 Mei, 2020 kwa muda wa miaka miwili (2) ambao unamalizika tarehe 10 Mei, 2022 huku mkataba kati ya ZSSF na TERRANOVA ulitiwa saini tarehe 05 Agosti, 2019 kwa miaka miwili (2) muda uliomalizika tarehe 05 Agosti, 2021.

Ukaguzi umebaini upeo wa kazi kwa NIGHT FRANK TZ LTD haukuwekwa bayana kwani hati ya mkataba inaeleza kuwa Mtoa huduma alipaswa kutoa huduma ya usimamizi wa mali kwa ZSSF Michenzani Mall huku barua ya tuzo ya kazi hiyo yenye kumbu

kumbu nambari ZSSF/ BA.183/474/02/135 ya tarehe 29 Januari, 2020 kwa mujibu wa vifungu GCC na SCC vya kanuni na masharti ya mkataba vinaeleza kuwa mtoa huduma atazingatiwa kwa mujibu wa huduma aliyoitoa katika mali zisizohamishika kwa ajili ya kuipatia na kuisimamia ZSSF.

Upeo wa kazi pamoja na mgawanyiko wa kazi kwa mtoa huduma (Night Frank) ulibainika zaidi juu ya nyongeza iliyoingia kati ya ZSSF na NIGHT FRANK tarehe 24 Disemba, 2020 kwa ajili ya kutoa huduma na kusimamia Jengo la ZSSF "Sheikh Thabit Kombo" lililopo Kisonge.

Upeo huu wa mgongano wa kazi unaleta ugumu kwa upande wa tatu kuelewa ni majengo gani mtoa huduma alipaswa kufanya kazi ya usimamizi na huduma anazozitoa na ikiwa ni majengo yote ya Zanzibar basi hapakuwa na haja ya kuingia katika nyongeza ya kusimamia majengo ya Kisonge.

Hata hivyo, imebainika pia mkataba kati ya ZSSF na TERRANOVA ulikuwa na upungufu mkubwa katika upeo wa kufanya kazi kwani ulishindwa kufafanua kabisa ni jengo lipi mtoa huduma alipaswa kulifanyia usimamizi na huduma za kukodisha kama barua ya tuzo yenye kumbukumbu namba ZSSF/BA.183/474/02/376 ya tarehe 05 Julai, 2019 ilivyobainisha ambapo hati ya mkataba aliyopewa haikubainisha upeo wa kazi anazozifanya badala yake nyaraka zote zinaonyesha kuwa mtoa huduma alipaswa kusimamia na kukodisha mali zote za ZSSF za Majengo zilizopo Zanzibar

**Majibu ya Mfuko**

Zabuni iliyotolewa ilikuwa ni ya usimamizi na uendeshaji wa majengo mapya ya Michenzani Mall na Thabiti Kombo ambapo Kampuni ya KNIGHT FRANK ndio iliyoshinda zabuni hiyo. Baada ya kumalizika Michenzani Mall Mfuko ulimzawadia mshindi huyo na baadae ulimzawadia na jengo la Thabiti Kombo.

Mkataba ambao uliainisha majengo yote ya ZSSF Zanzibar ulikuwa na nia ya kutaja majengo ya biashara ya Michenzani Mall na Thabiti Kombo kama msimamizi alivyokabidhiwa. Kwa sasa mkataba umeshaisha na wasimamizi wamepatiwa mkataba mpya ambao umeainisha kwa uwazi majengo yaliyokusudiwa.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Baada ya majadiliano ya kina juu ya hoja hii, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa barua ya tuzo ndio iliyokuwa na upungufu na mkataba ulikuwa upo sahihi.

Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC inaitaka Mfuko kuwa makini wakati inaandaa nyaraka mbali mbali ili kuepusha hasara hapo baadae.

**b. Mkataba baina ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar na ZSSF kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya kuandikia**

Mkataba uliingiwa tarehe 14 Disemba, 2020 wenye thamani ya shilingi 74,180,000 bila VAT. Upeo wa kazi kwa mujibu wa masharti ya mkataba yalikuwa ni kusambaza vifaa vya ofisi. Kwa mujibu wa kifungu cha 13 cha sheria na masharti ya mkataba kinasema; "Ikiwa muuzaji atashindwa kutengeneza na kuufunga mlango wa kuteleza wa kiotomatiki ndani ya muda ulioainishwa chini ya mkataba huu, mteja anaweza, bila

kuathiri masuluhisho mengine yote chini ya mkataba huu, kupunguza thamani ya fedha kutoka katika bei ya mkataba kwa mujibu wa uharibifu utakaojitokeza hadi kufikia asilimia 0.1 kwa siku na haitazidi asilimia 10 ya mkataba".

Kutokana na hali hiyo ukaguzi umebaini uwepo wa utekelezaji wa kifungu cha 13 kinakinzana na upeo wa kazi ya mtoa huduma ikiwa ni kusambaza vifaa vya kuandikia au kutengeneza na kuufunga mlango wa kuteleza wa kiotomatiki.

**Majibu ya Hoja**

Mfuko ulibaini hilo lilikuwa tatizo la kiuandishi ambalo lilifanya marejeo ya kazi ambayo haikuwa katika mkataba huo. Hata hivyo, mkataba huu ulishamalizika na hakukujitokeza tatizo la kutozwa hiyo adhabu iliyotajwa katika kifungu tajwa hapo juu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Mfuko, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.
Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kuwa makini wakati inafunga mikataba ili kuepuka kupata hasara, sambamba na kupata hoja zisizo na msingi.

**c. Mkataba kati ya ZSSF hidi ya SANTECH TRADERS SMC PRIVATE LTD kwa ajili ya kusambaza sare za wafanyakazi waZSSF**

Mkataba uliingiwa tarehe 16 Machi, 2021 kwa thamani ya shilingi 119,071,440 kwa muda wa kipindi cha wiki kumi na mbili (12). Ukaguzi umebaini upeo wa kazi kwa mujibu wa masharti ya mkataba ulikuwa ni kusambaza sare za wafanyakazi wa ZSSF.

Hata hivyo, kwa mujibu wa kifungu cha tatu (3) cha kanuni na masharti ya mkataba kinaeleza kuwa "mteja anafanya makubaliano ya kumlipa mzabuni kwa kuzingatia kusambaza, ufungaji na uagizaji wa samani kwa kuzingatia mahitaji ya mteja kwa thamani ya shilingi 119,440,000 pamoja na VAT".

Kutokana na hali hiyo ukaguzi umebaini kifungu cha 3 kinapingana na upeo wa kazi ya msambazaji ikiwa ni kusambaza Sare za wafanyakazi wa ZSSF au kusambaza, kufunga na kuagiza samani.

**Majibu ya Mfuko**

Mfuko ulibaini hilo lilikuwa tatizo la kiuandishi ambalo lilifanya marejeo ya kazi ambayo haikuwa katika mkataba huo. Hata hivyo, mkataba huu ulishamalizika na hakukujitokeza tatizo la kiutekelezaji.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja imebaki kama ilivyo, pamoja na hayo, Kamati ya LAAC iliutaka Mfuko kuzingatia uchunguzi na maoni ya Mkaguzi wa Ndani kwani suala hili alilibaini, isipokuwa kwamba, Mfuko haukuchukua hatua yoyote.

**d. Mkataba baina ya ZSSF dhidi ya TRIP CONSTRUCTION CO. LTD na ZSSF dhidi ya WAKANDARASI WA KUJENGA UASHI kwa ajili ya Matengenezo ya Ofisi kuu ya ZSSF Kilimani, Ofisi ya ZSSF Pemba, Uhuru na Viwanja vya Burudani vya Umoja (Lot I na II)**

Mkataba kati ya ZSSF na TRIP CONSTRUCTION CO.LTD uliingiwa tarehe 08 Oktoba, 2020 kwa muda wa miezi kumi na mbili (12) unaoishia tarehe 08 Oktoba, 2021 kwa ajili ya matengenezo ya majengo ya ZSSF (Lot II -Electrical and AC Works). Upeo wa kazi ya matengenezo ulikuwa unakinzana kati ya taarifa ya barua ya tuzo, hati ya Mkataba, na muhtasari wa mazungumzo ya tuzo kati ya ZSSF na mkandarasi.

Taarifa ya barua ya tuzo yenye kumbukumbu namba ZSSF/BA.183/474/01/201 ya tarehe 07/09/2020 ilitoa fursa kwa mtoa huduma kufanya matengenezo ya Majengo ya ZSSF ofisi kuu Kilimani, Ofisi ya ZSSF Pemba, Uhuru Amusement. Park Unguja, na Umoja Amusement Park Tibirinzi Pemba.

Muhtasari wa mazungumzo ya kikao kilichofanyika kati ya ZSSF na Mkandarasi (TRIP) tarehe 04 Septemba, 2020 kifungu cha 2.3 kilibaini kuwa mkandarasi huyo alikuwa afanye matengenezo ya jengo la ZSSF Kilimani, Bustani ya Burudani Kariakoo (Unguja), Bustani ya Burudani iliyopo Tibirinzi. Pemba, Ofisi ya ZSSF Pemba na majengo yote ya Mfuko.

Hati ya mkataba chini ya vifungu SCC (1) na GCC (1.1) inaeleza jina na namba ya utambulisho wa mkataba ni: Matengenezo ya Majengo ya ZSSF makao makuu Kilimani, Kituo cha Manunuzi cha ZSSF Mwanakwerekwe, Uhuru Amusement Park, ZSSF Real Estate Mbweni, na Hifadhi ya Umoja Amusement Tibirinzi Chake Chake Pemba.
Ukaguzi umebaini dosari zilizobainishwa hapo juu kwenye upeo wa kazi za matengenezo pia zilizingatiwa katika mkataba ulioingiwa kati ya WAKANDARASI WA

UJENZI WA UASHI WA ZSSF VS tarehe 08 Oktoba, 2021 kwa muda wa miezi kumi na mbili kwa LOT I (Mechanical and Civil works).

Kwa mazingira yaliyoonyeshwa hapo juu ukaguzi ulishindwa kuelewa ukubwa wa upeo wa kazi iliyokabidhiwa kwa watoa huduma wa TRIP CONSTRUCTION LTD na WAKANDARASI WA UJENZI WA UASHI.

**Majibu ya Hoja**

Mfuko uliingia mikataba ya huduma na kampuni mbili tajwa hapo juu kwa kazi mbili tofauti ambapo LOT 1 (Mechanical and Civil works) ambapo ni huduma za matengenezo ya mashine na ujenzi wakati LOT II (Eletrical and AC Works) ilikuwa kwa huduma za Umeme na Vipoza hewa. Kutokana na maelezo hayo, hakukuwa na muingiliano wa kazi na upeo wa kazi hizo kwa watoa huduma hao.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini kuwa hoja hii imejitokeza kutokana na majibu ya Mfuko iliyoyatoa kupitia “Management Letter”, hata hivyo, maelezo ya hoja ya Mkaguzi Mkuu kwenye Ripoti husika yanatofautiana na maelezo ya hoja kwenye “Management Letter”.

Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kuwa makini wakati inajibu hoja za Mkaguzi ili kuepuka kupata hoja zisizo na msingi.

**e. Mkataba kati ya ZSSF dhidi ya TERA TECHNOLOGIES AND ENGINEERING Ltd kwa ajili ya Ugavi, Uwekaji wa Rafu za Kielektroniki kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar.**

Mkataba kati ya wahusika ulisainiwa tarehe 24 Septemba, 2020 (mkataba wa awali) kwa thamani ya shilingi 609,517,776 Pamoja na VAT kwa muda wa miezi sita unaoishia tarehe 24 Machi 2021. Mkataba wa awali uliongezwa kwa miezi mitatu (3) kutoka tarehe 24 Machi, 2021 hadi 30 Julai, 2021 kwa gharama ya ziada ya shilingi 90,770,000 pamoja na VAT.

Ukaguzi ulibaini uwepo wa utofauti wa upeo wa kazi baina ya mkataba na barua ya tuzo kama inavyoonekana hapo chini:- Upeo namba 1 (hati ya mkataba) inaeleza kuwa mkataba ulikuwa wa kusambaza, ufungaji na uwekaji wa rafu za kielektroniki ambapo upeo namba 2 (barua ya tuzo ya tarehe 20.05.2020 yenye kumbukumbu namba ZSSF/AB.199/306/03/239) inaeleza kuwa mkataba ulikuwa kwa ajili ya kusambaza, ufungaji na kuwaagiza rafu za kielektroniki na uanzishaji wa hati za kielektroniki katika mfumo wa Taarifa za Usimamizi (eDMIS).

**Majibu ya Hoja**

Zabuni kwa ajili ya kazi hii ilitolewa moja kwa ajili ya usambazaji na ufungaji wa rafu za kieletroniki na utengenezaji wa mfumo wa usimamizi wa majalada ya kieletroniki. Baada ya mchakato wa zabuni, Mzabuni TERA TECHNOLOGIES alipewa tuzo ya kufanya kazi kama ilivyotangazwa. Hata hivyo maoni yaliyotolewa na Mwanasheria Mkuu yalielekeza kutayarishwa mikataba miwili ili kutenganisha kazi mbili ambazo ni:

1. Usambazaji na ufungaji wa rafu za kieletroniki.
2. Utengenezaji wa mfumo wa usimamizi wa majalada ya kieletroniki.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikujadili hoja zilizosalia kwa kuwa hoja majibu ya hoja hizo yanafanana, hivyo, hoja hizo zimebaki kama zilivyo.

## 4. Ukiukwaji uliobainishwa wakati wa kuanza na kukamilika kwa Mikataba (Muda wa Mikataba)

Baadhi ya mikataba iliyoingiwa na kutekelezwa katika mwaka wa ukaguzi ilionekana kutokuwa na uhakika katika muda wa kuanza na kukamilika kwa mikataba hiyo (muda wa mikataba). Baadhi ya dosari zilizobainika katika mikataba mbali mbali ni kama zifuatazo: -

### a. Nyongeza kati ya ZSSF dhidi ya KNIGHT FRANK TZ LTD (Nyongeza ya Mkataba wa utoaji huduma za Letting and Property Management wa ZSSF Michenzani Mall situated Michenzani Zanzibar

Pamoja na kusimamia jengo la ZSSF Michenzani Mall, Mfuko uliingia katika makubaliano na mtoa huduma ya kuendeleza usimamizi wa mali na kutoa huduma kwa jengo jingine jirani la ZSSF - Sheikh Thabit Kombo maarufu kwa jina la Jengo la Kisonge lililopo Kisonge.

Nyongeza hiyo ilitiwa saini tarehe 24 Disemba 2020 na kuanza kutumika kuanzia tarehe 01 Januari, 2021. Ukaguzi umebaini kutokuainishwa kwa tarehe ya kukamilika kwa mkataba kwenye nyongeza na hivyo kusababisha ugumu wa kuamua muda maalum wa kukamilisha huduma walizokubaliana.

**Majibu ya Mfuko**

Mtoa huduma tayari alishapatiwa mkataba wa kusimamia jengo la Michenzani Mall ambao muda wake ulikuwa wa miaka miwili. Ongezeko la kazi (Adendum) kwa kutumia Mkataba wa awali haubadilishi muda wa makubaliano ya awali katika Mkataba mkuu. Hata hivyo, Mtoa huduma huyo ameshamaliza muda wake kwa sasa hana mkataba wowote na Mfuko.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikujadili hoja zilizosalia kwa kuwa hoja majibu ya hoja hizo yanafanana, hivyo, hoja hizo zimebaki kama zilivyo.

**b. Mkataba baina ya ZSSF dhidi ya BUDDA AUTOWORKS wa utaoji huduma za magari kwa ZSSF.**

Mapitio ya muda wa mkataba kama ilivyoelezwa chini ya sehemu za SCC 2 & 3 (GCC 19) kwa sheria na masharti ya mkataba yalidhihirisha utata wakati wa kuanza na kukamilika kwa mkataba ambapo SCC 2 inasema "tarehe ya kuanza kwa mkataba itakuwa miezi 12 baada ya tarehe ya kusainiwa. mkataba" wakati SCC 3 inasema kwamba" muda wa kukamilika ni mwaka 1 kutoka tarehe ya kuanza kwa mkataba" yaani kuanzia tarehe 18 Agosti, 2020.

Iwapo vifungu hivyo viwili vitafasiriwa vyema na tarehe ya kuanza kwa mkataba itakuwa miezi kumi na mbili baadaye baada ya kusainiwa kwa mkataba yaani tarehe 18 Agosti, 2021 na itafikia mwisho baada ya miezi kumi na miwili (12) mingine yaani 18 Agosti, 2022. Katika suala hili, tarehe za kuanza na kukamilika zilikuwa zinapingana. Hata hivyo, mkataba huo ulidhaniwa ulianza tarehe 18 Agosti, 2020 na kukamilika tarehe 18 Agosti, 2021. Katika suala hili, mkataba ulionekana kuwa umeisha bila ushahidi wa kuongezwa.

**Majibu ya Hoja**

Mfuko ulibaini hilo lilikuwa tatizo la kiuandishi ambapo SCC 2 ya mkataba ilipaswa itumie neno "from" badala ya neno "after". Hata hivyo, mkataba huu ulishamalizika na hakukujitokeza tatizo kutokana na mgongano wa neno hilo.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikujadili hoja zilizosalia kwa kuwa hoja majibu ya hoja hizo yanafanana, hivyo, hoja hizo zimebaki kama zilivyo.

c. **Mkataba baina ya ZSSF dhidi ya MELISHA Media Production kwa ajili ya usambazaji wa Vifaa vya utangazaji wa ZSSF**

Mkataba kati ya wahusika ulitiwa saini tarehe 16 Machi, 2021 kwa thamani ya shilingi 47,725,000 (pamoja na kodi zote). Hata hivyo, muda wa utoaji wa mkataba (muda wa mkataba) uliotajwa chini ya kifungu cha 3 na 6 cha kanuni na masharti ya mkataba ulikuwa unakinzana. Kifungu cha tatu (3) kinasema wiki 3 kama kipindi cha uwasilishaji ambapo kifungu cha sita (6) kinasema wiki 8 kutoka tarehe ya kusainiwa. Kutokana na hali hiyo ukaguzi umebaini vifungu hivyo vinapingana.

**Majibu ya Hoja**

Vifungu hivyo vilipingana kutokana na kosa la kiuandishi. Hata hivyo, mkataba huo umeshamalizika muda wake sambamba na hilo, kwa sasa Mtoa huduma huo hana mkataba wowote na ZSSF.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikujadili hoja zilizosalia kwa kuwa hoja majibu ya hoja hizo yanafanana, hivyo, hoja hizo zimebaki kama zilivyo.

d. **Mkataba baina ya ZSSF dhidi ya WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR kuhusu usanifu na usimamizi wa ujenzi wa Jengo la Wizara ya Kilimo la FUFUNI Pemba (Kazi ya ushauri)**

Mkataba kati ya wahusika ulitiwa saini tarehe 09 Aprili, 2021 kwa thamani ya shilingi 20,000,000 pamoja na VAT. Kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha masharti ya mkataba yaliyotajwa kama "makubaliano haya yataanza kutumika tangu tarehe ya kusainiwa

na yataendelea kuwa halali hadi utimilifu wa pande mbili za majukumu yao chini ya makubaliano".

Ukaguzi umebaini mkataba huo haukuonesha tarehe ya makubaliano yao, kutokana na dosari hiyo itapelekea mkataba utaendelea kutumika kwa muda usiojulikana. Kushindwa kufafanua kwa uwazi na kupitia vigezo na masharti ya mkataba kunaweza kusababisha kutoelewana baina ya pande mbili za mkataba wakati wa utekelezaji wa mkataba hali ambayo inaweza kusababisha upotevu wa fedha za wanachama.

Aidha, malipo ya usimamizi na ada za upangishaji wa majengo ya vitega uchumi kwa watoa huduma bila ya kuwakata tozo na kodi mbalimbali za Serikali hali inayoweza kusababisha Mfuko kuweza kuwa kulipa ada kubwa ya watoa huduma ikilinganishwa na thamani ya huduma zinazotolewa na washauri pamoja na kukosekana thamani ya fedha kwenye mikataba iliyoingiwa (value for money on the contracts entered).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kuhakikisha yanafanyika mambo yafuatayo;

1. Uandaaji wa vigezo na masharti ya wakandarasi kutoka kwa idara za watumiaji unapaswa kuangaliwa na kitengo cha sheria pamoja na uongozi wa Mfuko ili kufi chua makosa na ukiukwaji wowote kabla ya kutekeleza mikataba ili kuimarisha haki kwa pande zote mbili kwenye kazi hizo.
2. Kupitia upya vipengele vya mikataba ya usimamizi na ukodishaji wa majengo ya uwekezaji ikiwemo kipengele cha ulipaji ujira na vigezo na masharti mengine ili kuhakikisha kunakuwepo wa utekelezaji na uwajibikaji mzuri wa mikataba.
3. Kuunda timu ya usimamizi na ufuatiliaji wa mikataba ili kusimamia utekelezaji sahihi wa kanuni na masharti ya mkataba.

**Majibu ya Mfuko**

Mkataba huo haukuwa na tarehe ya muda wa kukamilika kutokana na taratibu ambazo walipaswa kuchukua Wizara ya Kilimo za kuwatafutia watendaji wake ofisi mbadala jambo ambalo muda wake wa kukamilika haukujulikana. Kwa sasa mkataba huo umeshaisha na hakukuwa na athari yoyote.

Pia, Mfuko huwa unawatoza kodi zote za Serikali watoa huduma wote wanaofanya biashara na Mfuko.

Vile vile, Kitengo cha Sheria kime Kitengo cha Sheria kimaimarishwa kwa kuongezewa nyenzo za utendaji kazi ili kufanya kazi kwa umakini na uweledi, hivyo Kitengo kwa sasa kinasinamamia na kufuatilia mikataba yote ya Mfuko na Watoa huduma pia kinasimamia utekelezaji sahihi wa kanuni na masharti ya mikataba hiyo. imarishwa kwa kuongezewa nyenzo za utendaji kazi ili kufanya kazi kwa umakini na uweledi, hivyo Kitengo kwa sasa kinasinamamia na kufuatilia mikataba yote ya Mfuko na Watoa huduma pia kinasimamia utekelezaji sahihi wa kanuni na masharti ya mikataba hiyo.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikujadili hoja zilizosalia kwa kuwa hoja majibu ya hoja hizo yanafanana, hivyo, hoja hizo zimebaki kama zilivyo.

**5.2.10.20 Mapungufu yaliyobainishwa katika Ugavi uliofanywa na ZAGPA**

Ukaguzi ulipitia kumbukumbu za Bodi ya Zabuni katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na kubaini uwepo wa dosari katika uletaji wa bidhaa na utoaji wa huduma zinazofanywa na ZAGPA ambapo mzabuni alionekana kuwa na dosari zifuatazo: -

1. Mara nyingi Mzabuni alilaumiwa kuishiwa vifaa wakati mnunuzi (ZSSF) anapoagiza.

2. Kuchelewa au kushindwa kabisa kuleta vifaa alivyoagizwa. Kuwa na bei kubwa ya vifaa ikilinganishwa na viwango vya bei ya soko.
3. Kudai kiasi kikubwa kama malipo ya awali ili kutekeleza mkataba.
4. Kutokuwa na uwezo wa kifedha za kuendesha huduma anazotakiwa kuzitoa.

Kwa mujibu wa mapitio ya kumbukumbu za bodi ya zabuni na mikataba ukaguzi ulibaini kuendelea kuwepo kwa dosari nilizozibainisha hapo juu kumepelekea Bodi ya Zabuni kufanya maamuzi ya kununua kutoka vyanzo vingine ili kuondokana na usumbufu wa shughuli za Mfuko za kila siku kama vile kucheleweshwa kwa malipo ya mafao.

Kutokana na dosari zilizobainika kwa Mzabuni (ZAGPA) kumepelekea kujitokeza kwa dosari za kiutendaji katika shughuli zinazofanywa na kusimamiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa mujibu wa mpango wa manunuzi na kupelekea kufanya manunuzi kinyume na mpango wa manunuzi na kwa kuingia gharama kubwa ya manunuzi kinyume na bajeti ya matumizi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kutafuta ushauri kutoka kwa Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali chakavu Zanzibar (ZPPDA) kuhusu matatizo yanayohusiana na vifaa vinavyotolewa na wakala wa Uchapaji wa Serikali. Ikiwa itashindikana kwa pendekezo la kwanza, Mfuko unapaswa kutafuta ushauri zaidi kutoka kwa mamlaka za juu za Serikali ili kutatua suala hilo ili kuepusha usumbufu na ucheleweshaji wa shughuli za Mfuko kwa kutegemea vifaa kutoka ZAGPA kwa kuzingatia vifaa vinavyotolewa kuwa na bei kubwa kulingana na bei halisi ya sokoni.

**Majibu ya Hoja**

Mapungufu makubwa yanayotokana na upatikanaji wa bidhaa au utoaji wa huduma za usambazaji wa bidhaa husababishwa na Taasisi tajwa hapo juu, katika kuondoa mapungufu hayo uongozi wa Mfuko ulifanya mazungumzo na uongozi wa Taasisi hiyo ili kuondoa changamoto zilizojitokeza na kukubaliana njia bora ya utendaji wa kazi. Baada ya mazungumzo na kukubaliana njia bora ya utendaji kazi, kwa sasa ZAGPA wamekuwa wakituandikia barua mapema kwa vifaa vyote ambavyo hawana uwezo navyo na kutupa ruhusa tutumie njia ya zabuni ya kawaida kwa Kampuni nyengine kulingana na mahitaji yetu.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja hii imebaki kama ilivyo, kutokana na majibu ya Mfuko. Pamoja na hayo Kamati ya LAAC imeutaka Mfuko kuwa makini wakati unatekeleza shughuli zake

### 5.2.11 MFUKO WA BARABARA ZANZIBAR (ZRF)

**Taarifa ya Mapato**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mfuko wa Barabara una vyanzo vikuu viwili vya mapato ambavyo ni Mfuko wa Maendeleo ya Barabara na Ushuru wa Magari, ambao ni shilingi 100 kwa lita moja ya petroli na dizeli inayoagizwa kutoka nje ya nchi ya Zanzibar ambapo ndio chanzo kikuu cha mapato ya Mfuko unaochangia asilimia 77 ya mapato yote.

Ushuru wa Magari hutozwa shilingi 100,000 kwa kuagiza magari kutoka nje ya nchi na hii inafanya takribani asilimia 23 ya mapato yote.

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Sheria ya Fedha ya Umma nambari 12 ya mwaka 2016 makusanyo ya kila mwezi yanawasilishwa Hazina kwa madhumuni ya kurekodiwa. Uhaulishaji wa fedha kutoka Hazina kwenda Mfuko wa Barabara Zanzibar mara nyingi hufanyika kila mwezi.

Aidha, imebainika kujitokeza kwa ongezeko la makusanyo ya Ushuru wa Maendeleo ya Barabara na Ushuru wa Magari. Makusanyo ya Mfuko wa Maendeleo ya Barabara yameongezeka kwa asilimia 7 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikilinganishwa na 2019/2020. Ushuru wa Magari kwa upande mwingine uliongezeka kwa asilimia 152 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2019/2020.

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021, Mfuko ulikusanya Tozo ya Maendeleo ya Barabara ya jumla ya shilingi bilioni 12.550 ikilinganishwa na mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 ambapo ni shilingi bilioni 11.948 . Makusanyo ya Ushuru wa Magari yalikuwa shilingi bilioni 3.758 ikilinganishwa na mwaka uliopita na shilingi bilioni 1.490.

Mfuko wa Barabara ulipokea jumla ya shilingi bilioni 10.322 kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango zinazohusiana na Tozo. Hata hivyo, imebainika Kiasi cha fedha ambacho hakijapokewa mwishoni mwa mwaka kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kilikuwa shilingi bilioni 8.329. Kati ya hizo, shilingi bilioni 5.057 zilikuwa za mwaka wa fedha 2020/2021.

Ukaguzi umebaini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 mapato mengineyo yameshuka na kufikia shilingi milioni 1.190 ikilinganishwa na mwaka uliopita wa 2019/2020 na kufikia shilingi milioni 71.040. Kupungua kwa kiasi kikubwa cha fedha kumetokana na kukosekana kwa kodi ya ukodishwaji wa Ofisi uliokuwa ukifanyika hapo awali.

Kiujumla kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukusanyaji wa mapato yameongezeka na kufikia jumla ya shlingi bilioni 14.17 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo jumla ya shilingi bilioni 13.53 zilikusanywa.

Kwa upande wa matumizi imebainika Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imetumia jumla ya shilingi bilioni 8.928 kwa kazi za matengenezo ya barabara ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo matumizi ya matengenezo ya barabara yalikua shilingi bilioni 14.55 na kiasi hiko kinajumuisha na matumizi ya ziada. Hata hivyo matumizi ya jumla yamebainika kupungua na kuwa shilingi bilioni 10.123 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo yalifikia bilioni 15.88.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imeushauri Uongozi wa Mfuko wa Barabara Zanzibar kuboresha vyanzo vyake vya mapato ili kuzidisha ufanisi wa utendaji kazi wa taasisi hiyo.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

**5.2.11.1: Matumizi ambayo hayajaidhinishwa kwenye bajeti shilingi 85,470,373**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilibainika Mfuko wa Barabara kufanya matumizi yenye thamani ya shilingi 85,470,373 sawa na Dola za Kimarekani 34,700 kwa ajili ya ununuzi wa gari ambapo matumizi hayo hayakujumuishwa kwenye bajeti iliyoidhinishwa ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2021.

Kufanya matumizi nje ya bajeti iliyoidhinishwa kunaweza kusababisha matumizi ambayo hayana tija na kupelekea kuingiza hasara kwa Mfuko wa Barabara Zanzibar.

Ukaguzi ulishauri Uongozi wa Mfuko wa Barabara Zanzibar (ZRF) kusimamia utekelezaji wa bajeti iliyoidhinishwa na Bodi ili kuondoa changamoto za matumizi yasiyo na tija kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa.

**Majibu ya Mfuko**

Ni kweli, kama ukaguzi ulivyobaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ZRF ilitumia jumla ya TZS 85,470,373 sawa na Dola za Kimarekani 34,700 kwa ajili ya ununuzi wa gari aina ya Toyota Pickup Double Cabin.

Fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa gari hiyo zilifanyiwa uhaulishaji kutoka kifungu cha "Provision" kilichokuwepo kwa fedha zilizobaki katika hesabu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kutengewa matengenezo ya Msikiti uliopo pembezoni ya Barabara ya Fuoni ambayo ilitengenezwa kupitia fedha za ZRF. Baada ya Mkandarasi aliyejenga Barabara hiyo ambaye ni MECCO kuamua kuchukua jukumu la kutengeneza

Msikiti huo, Menejimenti ya ZRF ilipendekeza kwa Bodi kuzitumia fedha zilizotengwa kwa matumizi ya Msikiti zitumike kwa ununuzi wa gari baada ya kujitokeza kwa mahitaji hayo.

Menejimenti ya ZRF iliwasilisha ombi la uhaulishaji kwenye Kikao cha Bodi cha 30 lilichofanyika tarehe 19 Septemba 2020 na kuidhinishwa.

Kwa upande mwengine, tunakiri kwamba, kutokana na viwango na taratibu za ufungaji wa hesabu, haikuwa sahihi kutumia kifungu cha "provision" kufanya uhaulishaji, licha ya fedha hizo kuwepo kwenye hesabu. Kumbukumbu za Kikao cha Bodi za ruhusa ya kuhaulisha zinaambatanishwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:-

- Mfuko wa Barabara Zanzibar ulifata taratibu zote za kihasibu pamoja na Sheria za Kimataifa IPSAS.
- Uongozi wa Mfuko wa Barabara Zanzibar ulizingatia na kuchukua hatua zote stahili za ndani (internal policy) ili kuweza kuhalalisha matumizi hayo.
- Kwenye viambatanisho vilivyowasilishwa nyaraka zote stahiki kutoka bodi ya Mfuko wa Barabara ziliwasilishwa.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC baada ya kufuatilia kwa kina imeridhishwa na taratibu zilizochukuliwa na Uongozi wa Mfuko wa Barabara katika suala la uhaulishaji wa fedha za ujenzi wa msikiti na badala yake fedha hiyo kutumika kwa ununuzi wa gari kwa ajili ya shughuli za Ofisi. Hivyo hoja hii imeondolewa.

### 5.2.11.2: Fedhaza Ukarabati wa Jengo ambazo hazikutumika Shilingi 522,955,500

Kwa mujibu wa mpango wa ununuzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini Mfuko wa Barabara ulitenga jumla ya shilingi 522,955,500 kwa ajili ya matengenezo mbali mbali ikiwemo mifumo ya maji, mifumo ya umeme, ukarabati wa milango, upakaji wa rangi katika sehemu ambayo iliyokuwa ikitumiwa na ZURA katika jengo la Mfuko wa Barabara. Aidha, hadi ukaguzi unakamilika ukarabati huo haukuweza kufanyika badala yake ukarabati huo umehamishiwa katika mpango wa ununuzi kwa mwaka unaofuata wa 2021/2022.

Kutokutekeleza kwa mpango wa ununuzi kwa mujibu wa sheria na taratibu kunapelekea kuathiri mipango ya utekelezaji ya Taasisi husika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Barabara Zanzibar kuhakikisha unatekeleza ipasavyo mipango iliyojipangia kwa mujibu wa sheria na taratibu za ununuzi zilizopangwa kwa mwaka husika.

**Majibu ya Mfuko wa Barabara**

Ni kweli, kama ukaguzi ulivyobaini kuwa TZS 522,955,500 zilitengwa na kuingizwa kwenye mpango wa ununuzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya matengenezo ya Jengo lote. Fedha hizi hazikutumika kwa kima kilichopangwa na badala yake zilitumika TZS 10,927,000 tu kutokana na kutokukamilika kwa taratibu za zabuni na kupelekea kufutwa kwa zabuni hiyo kulikosababishwa na changamoto zifuatazo:

- Kuchelewa kupata ruhusa ya Ripoti ya Tathmini ya Matengenezo ya Jengo kutoka Mamlaka ya Ununuzi (ZPPDA).
- Kumalizika kwa muda wa uhalali wa Zabuni husika ambayo ilisababishwa na kuchelewa kupatiwa muongozo wa ZPPDA juu ya ufumbuzi wa kuendelea na zabuni husika ambapo mjumbe mmoja wa Kamati ya Tathmini alikuwa hakuweka saini katika ripoti hiyo.
- Kutowasilishwa kwa michoro ya Jengo la ZRF kutoka kwa Mshauri Elekezi changamoto ambayo ilichangiwa zaidi na kutokuwepo kwa "as built drawings" kutoka kwa Mkandarasi wa jengo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:-

- Licha ya jengo kutumika kwa zaidi ya miaka kumi sasa ila bado Uongozi wa Mfuko wa Barabara haujapatiwa mchoro wa "as built drawings"
- Jiatihada za kupatiwa mchoro huo bado hazijaleta matokeo mazuri ya mchakato huo.
- Uongozi wa Mfuko wa Barabara unashindwa kufanyia ukarabati wa miundombinu ya Ofisi kwa kukosa michoro hiyo jambo amabalo linaweza kusababisha kutokea kwa hoja hii kwa miaka ijayo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya Uongozi wa Mfuko wa Barabara kukiri kuwepo kwa dosari ya ucheleweshaji wa utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi. Kamati ya LAAC haikuridhishwa na mwenendo wa mchakato wa kuipata michozo ya "as built drawings", kwani

kukosekana kwa mchoro huo wa awali unaukosesha Uongozi wa Mfuko wa Barabara kulifanyia ukarabati jengo pamoja na miundombinu yake.

Kutokana na kasoro hizo Kamati ya LAAC imeitaka Mfuko wa Barabara Zanzibar kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa taratibu zilizopo Kisheria na Kikanuni ili kuepuka hoja zisizo za lazima.

**5.2.11.3: Kukosekana kwa mapato yatokanayo na makusanyo ya kodi shilingi milioni 74**

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika Mfuko wa Barabara Zanzibar umeshindwa kukusanya shilingi milioni 74 kwa mwaka zinazotokana na kodi ya kukodisha sehemu ya jengo la Ofisi katika ghorofa ya chini na ghorofa ya tatu ambapo hapo awali sehemu hiyo iliweza kukodishwa kwa taasisi mbali mbali zilizokuwa zikifanya shughuli zao katika eneo hilo na kupelekea sehemu hiyo kuwa tupu na haitumiki baada ya taasisi hizo kuhama na hapakuwepo na jitihada zinazochukuliwa kuhakikisha sehemu hizo zinakodishwa na kurejesha hali ya kipato kilichokuwa kinapatikana awali hali ambayo inaweza kujitokeza kuchakaa au kuharibika kwa miundombinu iliyokuwepo awali na kupelekea hasara kubwa kwa Mfuko.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa jengo hilo lina Ofisi zilizokuwa wazi katika ghorofa ya pili ambazo zingeliweza kukodishwa kwa taasisi nyengine na kuingiza kipato kwa Mfuko wa Barabara.

Aidha, imebainika Mfuko wa Barabara una kumbi mbili za mikutano ambazo zina uwezo wa kukodishwa kwa taasisi mbali mbali kwa ajili ya kufanya mikutano yao kwa lengo la kupata mapato jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika imebainika hakuna

shughuli yoyote inayofanywa ambayo ingeliweza kuingiza kipato kwa Mfuko wa Barabara Zanzibar.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Barabara kuchukuwa jitihada za makusudi za kuhakikisha wanatafuta wapangaji katika sehemu zilizotupu kwa lengo la kuongeza mapato.

**Majibu ya Mfuko wa Barabara**

Ni kweli, kama ukaguzi ulivyobaini, kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kulikuwa hakuna pato lolote lililoingia kwa ajili ya kodi ya Jengo kwa ajili ya Ofisi

ziliokuwa wazi ambapo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 fedha zilizokusanywa kama kodi ya ofisi zilikuwa ni TZS milioni 74 ambazo zilikusanywa kutokana na kukodishwa ofisi katika ghorofa ya chini (ground floor) na ghorofa ya Pili.

Kushindikana kukodisha ghorofa ya Chini na ya Pili kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kulitokana na sababu zifuatazo:

i.Dhamira ya ZRF ya kufanya matengenezo makubwa ya jengo kwa hivyo Menejimenti iliamua kutokodisha kwa sababu wakati wa matengenezo uwezekano wa kuhama hama baina ya ofisi kupisha matengenezo ungekuwa mkubwa na ofisi za juu zingetumika na ZRF wakati wa matengenezo hayo

ii.Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango (ambayo ni Wizara Mama) ilikuwa ishaonesha dhamira kwa maadishi ya kutaka kukodi baadhi ya ofisi hizo kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani.

iii.Kutokana na kuongezeka kwa wafanyakazi wa ZRF vyumba viwili ambavyo awali viliwahi kukodishwa kwenye ghorofa ya chini vimekuwa vikitumika na wafanyakazi wa ZRF.

Kuhusiana na matumizi ya ukumbi, umekuwa ukikodishwa kwa ajili ya matumizi ya mikutano au kazi maalum. Utaratibu uliowekwa awali na kuidhinishwa na Bodi ilikuwa kwa wakodishwaji kuchangia umeme kwa kima cha TZS 50,000 kwa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na TZS 100,000 kwa Taasisi nyengine ambazo zinawasilishwa kwa njia ya kununua coupon ya umeme moja kwa moja.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:-

1. Mfuko wa Barabara Zanzibar hauna ufanisi wa hali ya juu katika mchakato wa ufuatiliaji wa madeni wanapotoa huduma za ukodishaji wa sehemu zilizopo katika jengo lao.

2. Uongozi wa Mfuko wa Barabara umekosa mpango mzuri wa ukodishaji wa Ofisi zilizo wazi.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro hizo Kamati imeutaka uongozi kuhakikisha inatumia vizuri rasilimali zake kwa kuziekea mikakati madhubuti ili kuepusha upotevu wa fedha pamoja na mali za Serikali.

### 5.2.11.4: Kukosekana kwa udhibiti mzuri wa matumizi ya mafuta yenye thamani ya shilingi 53,909,923

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini mapungufu yatokanayo na udhibiti wa matumizi ya mafuta yenye thamani ya TZS 53,909,923 kwa mujibu wa madaftari ya kutunzia taarifa za mafuta ambapo imepelekea kukosekana kwa kumbukumbu zinazorikodiwa katika daftari maalum linalooneshа kiwango cha mafuta kilichotumika pamoja na masafa yanayotumiwa na gari kwa mujibu wa kilomita.

Kukosekana kwa daftari la kumbukumbu linalooneshа mwenendo wa gari, kiwango cha mafuta na masafa yaliyotumika kunaweza kupelekea matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Barabara kuweka udhibiti mzuri wa usimamizi wa mafuta ili kuepusha matumizi yasiyokuwa na tija.

**Majibu ya Mfuko wa Barabara**

Kama ukaguzi ulivyobaini, TZS 53,909,923 ni kiwango cha fedha ambazo zilitumika kwa matumizi ya mafuta kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Mafuta haya yanajumuisha mafuta ambayo yanawekwa kwenye gari za ZRF ambazo kwa kipindi hicho zilikuwa ni nne. Aidha, yalijumuisha coupon za mafuta ambazo hupewa wafanyakazi wa ZRF. Mafuta ambayo yalitumika kwa gari za ZRF yalikuwa na kiwango cha TZS 8,902,528, Utaratibu unaotumika kwa sasa wa kudhibiti mafuta kwa gari za ZRF ni kuhakikisha kuwa log book zinatumika ipasavyo na zinajazwa kikamilifu, hapo nyuma kulikuwepo na changamoto ya ujazaji wa log book lakini kwa sasa imeshapatiwa ufumbuzi.

Kwa upande mwengine, utoaji wa mafuta kwa gari za ZRF hutolewa kwa kiwango maalum kwa wiki, ambazo haziongezeki, isipokuwa kwa sababu maalum ambayo inaripotiwa na kuombewa idhini.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro hizo Kamati imeutaka Uongozi wa Mfuko wa Barabara Zanzibar kuhakikisha kufuata utaratibu wa matumizi wa rasilimali zake ili kuepusha hoja zisizo za lazima.

Vile vile, Kamati inaushauri Uongozi wa Mfuko Barabara kuandaa utaratibu mzuri wa udhibiti wa mafuta pamoja na uwekaji wa daftari la kumbukumbu linaloonesha mwenendo wa gari, kiwango cha mafuta na masafa yaliyotumika ili kuepusha matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

**WIZARA YA UJENZI. MAWASILIANO NA UCHUKUZI ZANZIBAR – UNGUJA**

**5.2.11.5 Kukosekana kwa udhibiti mzuri wa matumizi ya mafuta yenye thamani ya shilingi milioni 352**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini mapungufu yatokanayo na udhibiti wa matumizi ya mafuta yenye thamani ya shilingi milioni 352 kwa mujibu wa madaftari ya kutunzia taarifa za mafuta yaliopo Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar ambapo imebainika kuna jumla ya vitendea kazi 27 vilivyowekwa kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyopangwa na Mfuko wa Barabara Zanzibar. Ukaguzi haukupatiwa kitabu cha kumbukumbu kinachooonesha mwenendo wa mafuta (log book) kwa vitendea kazi 10 tulivyovichangua kwa ajili ya ukaguzi, hata hivyo imebainika vitabu saba (7) vya kurikodia kumbukumbu za mafuta vilivyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi vilibainika kuwa na mapungufu ya kurikodia kumbukumbu kwa mujibu wa utaratibu ambapo imepelekea

kukosekana kiwango cha mafuta kilichotumika pamoja na masafa yanayotumiwa na gari kwa mujibu wa kilomita.

Kukosekana kwa daftari la kumbukumbu linalooonesha mwenendo wa gari, kiwango cha mafuta na masafa yaliyotumika kunaweza kupelekea matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Barabara kuweka udhibiti mzuri wa Usimamizi wa mafuta ili kuepusha matumizi yasiokuwa na tija.

**Majibu ya Wizara**

Ni kweli kwamba mpaka anafika Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi, kulikuwa na mapungufu ya kukosekana daftari la kumbukumbu linalooonesha mwenendo wa gari, kiwango cha mafuta na masafa yaliyotumika (log book).

Uongozi wa Wizara umepokea ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya udhibiti mzuri wa usimamizi wa mafuta ili kuepusha matumizi yasiyo na tija.

Kwa sasa Wizara kupitia Wakala wa Barabara wanatumia (log book) vizuri kwa kurekodi matumizi ya mafuta kila gari kwa mujibu wa taratibu. Vyombo vyote vya kazi vimepewa daftari za kumbukumbu zinazooonesha mwenendo wa kila gari, kiwango cha mafuta na masafa yaliyotumika. Log book hizo hujazwa na dereva husika kwa kutiwa sahihi na msimamizi mkuu wa kazi husika au baadae kuthibitishwa na mkuu wa magari

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC, imebaini yafuatayo:

1. Kutokuwepo kwa vielelezo vya matumizi ya mafuta ya shilingi milioni 352 ambayo hajafuata utaratibu wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nambari 11 ya mwaka 2016.
2. ‘Log book’ zilikuwepo ila zilikuwa hazitumiki ipasavyo.

3. Watendaji Wanaohusika na utoaji wa mafuta walikuwa hawafuatilii magari baada ya kupatiwa mafuta suala la urejeshaji wa risiti kama utaratibu unavyoelekeza.
4. Kutokuwepo kwa uhifadhi mzuri wa kumbukumbu za Ofisi.

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hizi zisijitokeza tena Kamati ya LAAC, imependekeza yafuatavyo:

1. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ihakikishe inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo ili kuepusha matumizi makubwa ya mafuta yenye kuitia hasara Serikali.
2. Uongozi wa Wizara kuandaa utaratibu mzuri katika kufuatilia suala la utoaji na uchukuaji wa mafuta katika vyombo vya Serikali pamoja na Binafsi zinavyotumika kwa kazi za Serikali ikiwemo za ujenzi wa miradi ya Barabara.
3. Wizara kuhakikisha vyombo vyote vinavyopatiwa mafuta kwa ajili ya shughuli za Serikali ni lazima vyombo hivyo virikodiwe katika 'log book' ili kuepusha matumizi mabaya na upotevu wa fedha za Serikali.
4. Wizara kuandaa utaratibu mzuri wa uhifadhi wa nyaraka za Serikali ili kuepusha hoja zisizo kuwa za lazima.

**5.2.11.6 Kutokufanya kazi kwa vifaa vya kutengenezea Barabara**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika uwepo wa vifaa vingi ambavyo havifanyi kazi kwa muda mrefu ambapo vinahitaji matengenezo makubwa na vyenginevyo vinahitaji matengenezo ya kawaida jambo ambalo linapelekea kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba. Hali halisi ya vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

**Jadweli Nambari 65: Vifaa vya matengenezo ya Barabara ambavyo havifanyi kazi kwa muda mrefu - Unguja**

| amba | ina ya Gari | amba ya Usajili | lodel | liaka Iiyotumik | laelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| | USA | MZ 278 B | C3 | 3 | ack Heo Loader |
| | lerced benz | MZ 288 B | | 1 | rane Truck |
| | ino | MZ 204 B | S 271 KD | 9 | ump Truck |
| | ino | MZ 280 B | S 271 KD | 9 | ump Truck |
| | ino | MZ 206 B | S271KD | 9 | ump Truck |
| | omatsu | MZ 122 D | C 200 - 7 | 1 | xcavator |
| | eyland daff | MZ 273 B | | 9 | ow bed truck |
| | issan | MZ 265 B | | 7 | ick up |
| | aver | MZ 400 B | ynapac F7W | 1 | oller finisher |
| | omatsu | MZ 291 B | VA-380-1 | 0 | Wheel loader |

Aidha, uwepo wa dosari hiyo kwa upande wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi - Pemba uwepo wa vifaa vingi ambavyo havifanyi kazi kwa muda mrefu ambapo vinahitaji matengenezo makubwa na vyenginevyo vinahitaji matengenezo ya kawaida kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 66: Vifaa vya matengenezo vya Barabara ambavyo havifanyi kazi kwa muda mrefu – Pemba**

| amba | ina ya Gari | amba ya Usajili | ina ya Kifaa | lodel | lahali ilipo |
|---|---|---|---|---|---|
| | VECO | MZ 6710 | ump Truck | 80 | lakao Makuu |
| | VECO | MZ 6711 | ump Truck | 80 | lakao Makuu |
| | ISSAN | MZ 129 B | ick up | | lakao Makuu |
| | OYOTA | MZ159 B | ick up | .2 | lakao Makuu |
| | EGSON | | rusher Plant | | wareni Vitongoji |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | ARKER | | sphalt Mix Plan | | wareni Vitongoji |
| | OMATSU | | uldozer | 85 EX - 15 | wareni Vitongoji |
| | AT | | xcavator | 29 | le |
| | AT | MZ 5615 | lotor Grader | 40G | lakao Makuu |
| | AT | MZ 167 B | lotor Grader | 40H | lakao Makuu |
| | ATALIS | | Vheel loader | | wareni Vitongoji |
| | OMAG | VBO 2 | ibrating Roll Work behind) | AYATA BW75H | lakao Makuu |
| | OMAG | | ibrating | AYATA BW75H | lakao Makuu |
| | OMAG | | ibrating Roller | | lakao Makuu |
| | LOWKNOX | | aver | K90 | lakao Makuu |
| | STERPETTER | | oncrete Mixer | M27 | lakao Makuu |
| | STERPETTER | | oncrete Mixer | M27 | lakao Makuu |
| | STERPETTER | | oncrete Mixer | M27 | lakao Makuu |

Kuwepo kwa vifaa visivyofanya kazi kwa muda mrefu kunapelekea ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo imepelekea Wizara kukodi vitendea kazi kwa taasisi binafsi jambo ambalo linapelekea kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kusimamia ipasavyo matengenezo ya vifaa ambavyo vinaweza kurekebishwa na kufanya kazi na vile visivyoweza kufanya kazi kuondoshwa katika Daftari la Kudumu.

**Majibu ya Wizara**

Ni kweli kwamba mpaka anafika Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi, kulikuwa na vifaa visivyofanya kazi kwa muda mrefu kunapelekea ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo imepelekea Wizara kukodi vitendea kazi kwa taasisi binafsi jambo ambalo linapelekea kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Uongozi wa Wizara umepokea ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya kusimamia ipasavyo matengenezo ya vifaa ambavyo vinaweza kurekebishwa na kufanya kazi na vile visivyoweza kufanya kazi kuweza kuondoshwa katika daftari la kudumu.

Wakala wa Barabara imefanya ununuzi wa vipuri na kuvifanyia matengenezo ya baadhi ya vifaa na kuanza kutumika. Aidha, vifaa ambavyo vilikuwa havitengenezeki kutokana na uchakavu wake vimeuzwa na vyengine vipo kwenye utaratibu wa kutaka kuuzwa. Vifaa hivyo vinaonekana katika.

**Jadweli lifuatalo:Unguja: Vifaa vinavyotaka kuondolewa (Kuuzwa)**

| | ina ya Gari | amba ya Usajili | lodel | liaka Iiyotumika | laelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 19. | USA | MZ278 B | C3 | 3 | ack Heo Loader |
| 20. | lerced benz | MZ288 B | | 1 | rane Truck |
| 21. | ino | MZ280 B | 5 271 KD | 9 | ump Truck |
| 22. | ino | MZ206 B | 5 271 KD | 9 | ump Truck |
| 23. | aver | MZ400 B | ynapac F7W | 1 | oller finisher |
| 24. | omatsu | MZ291 B | /A – 380 - 1 | 0 | /heel loader |
| 25. | eyland daff | MZ273 B | | 9 | ow bed truck |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya Wizara kukiri mapungufu yaliobainika katika hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati ya LAAC inapendekeza kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuharakisha uuzwaji wa vifaa vya ujenzi pamoja na magari yasiofanyika matengenezo ili kuondokana na mzigo wa vifaa chakavu na yasiotumika ambayo yanaonekana katika “Assert Register Book”.

Vile vile, Kamati ya LAAC inaishauri Wizara kushirikiana na Mfuko wa Barabara kwa vifaa ambayo vinaweza kutengenezeka kuvifanyia matengenezo ya haraka iwezekanavyo ili kuepusha ucheleweshwaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuingia gharama za utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa kukodi vifaa hivyo.

**5.2.11.7 Kutokukamilika kwa miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi 1,177,805,523**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ilipokea fedha kutoka Mfuko wa Barabara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbali mbali ya ujenzi wa Barabara Kisiwani Pemba. Ziara ya ukaguzi zilizofanyika wakati wa ukaguzi zilibani kuwa miradi yenye thamani ya shilingi 1,177,805,523 ilikuwa haijakamilika ingawa tarehe za mikataba hiyo zilikuwa tayari imeshapita.

Miradi iliyochelewa kukamilika kwa wakati ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 67: Miradi ya maendeleo ambayo haikukamilika**

| latengenezo ya Baraba 'wango cha lami | refu (km) | harama (TZS) | atua iliyofikia |
|---|---|---|---|
| )31 Chake Chake - Wete | 6 | .450,000 | azi inaendelea |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 163 Bogoa - Michenzani | | 37,500 | azi inaendelea |
| ımla Ndogo | | 0,237,500 | |
| karabati wa Barabara (uzibaji wa viraka) | | | |
| UR Njia za Mjini (Urban Road) | ,000 | 6,000,000 | Iradi haukutekelezeka |
| Njia za Vijijini (Rural Road) | ,600 | 5,600,000 | Iradi haukutekelezeka |
| ımla Ndogo | | 1,600,000 | |
| latengenezo ya mara kwa mara kwa Barabara za ndani zisizo na lami | | | |
| MW Kipapo – Mgelem /ambaa road(9.30km) to grav :andard – Phase | | 00,000,000 | Iradi umetekelezwa kv silimia 70 |
| ımla Ndogo | | 00,000,000 | |
| tengenezaji wa michirizi | | | |
| OK Barabara ya Ole - Kengeja | | 57,130,000 | Iradi umetekelezeka kv wango hafifu chini silimia 50 |
| IWG Mangwena road section | | 8,838,023 | |
| ımla Ndogo | | 25,968,023 | |
| ımla Kuu | | .177,805,523 | |

Aidha, ukaguzi umebaini miradi yenye thamani ya shilingi 41,600,000 haikuweza kutekelezeka kama ilivyobainishwa katika jadweli hapo juu, hata hivyo imebainika miradi yenye thamani ya shilingi 225,968,023 imetekelezwa kwa kiwango hafifu cha chini ya asilimia 50. Pamoja na uwepo wa dosari za utekelezaji wa miradi hiyo imebainika mradi wa ukarabati wa Barabara za ndani umetekelezwa kwa kiwango cha asilimia 70 jambo ambalo ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa hatua zilizochukuliwa dhidi ya Wakandarasi waliopewa

miradi hiyo na kushindwa kuikamilisha kwa mujibu wa makubaliano kama inavyoonekana katika jadweli hapo juu.

Kuchelewa kukamilika kwa miradi kunatokana na ucheleweshwaji wa upatikanaji wa fedha kwa wakati na uwepo wa zana duni za kufanyia kazi jambo ambalo linaweza kupelekea miradi hiyo kutokukamilika kwa wakati na kupanda gharama za vifaa na hatimae kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Barabara Zanzibar kuhakikisha wanaingizwa fedha kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza miradi yake iliyojipangia kwa ufanisi ili kuweza kuleta tija kwa jamii.

**Majibu ya Wizara**

Uongozi wa Wizara unakiri kwamba mpaka anafika Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kukagua kwamba baadhi ya miradi haijakamilika utekelezaji wake na baadhi ilikuwa inaendelea na hatua ya utekelezaji. Hata hivyo, kuna baadhi ya taarifa hazijaripotiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hazipo kwenye uhalisia.

Taarifa hizo ni pamoja:

- Barabara ya Chake Chake – Wete na Bogoa – Michenzani, Barabara hizi hazikuwa kwenye mpango wa matengenezo ya kiwango cha lami bali ilikuwa ni matengenezo ya kawaida ambayo yanajumuisha; ukataji wa majani, usafishaji wa misingi ya maji ya mvua na kazi ndogo ndogo.
- Hakukuwa na Mpango kazi wa uzibaji viraka vya Barabara kwa Km 1000 kwa njia za mjini na Km 1600 njia za vijijini badala yake ulikuwa ni uzibaji wa viraka kwa njia za mjini kwa mita za mraba 1000 na njia za vijijini mita za mraba1600.
- Kazi zote ambazo zimeorodheshwa katika Jadweli No. 67 zimetekelezwa na wafanyakazi wa ndani wa Wakala wa Barabara (Force Account) na sio Wakandarasi.

Hata hivyo, Uongozi wa Wizara umepokea ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu uongozi wa Mfuko wa Barabara kuhakikisha wanaingiza fedha kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza miradi yake iliyojipangia kwa ufanisi ili iweze kuleta tija kwa jamani.

**Sambamba na hilo,** hatua mbalimbali zimechukuliwa na Wizara kuhakikisha kuwa kazi hizo zilimalizika kwa mujibu wa bajeti iliyowekwa kama ifuatavyo:

**Chake Chake - Wete na Bogoa – Michenzani**

Barabara hizi zilikamilishwa kwa kutumia fedha zile zile zilizoingizwa katika kipindi husika cha mwaka wa fedha 2020/2021 na sio kuombewa fedha nyengine.

**Barabara ya Ole – Kengeja na Mangwena**

Ujenzi wa Kalavati na misingi ya maji ya mvua ya barabara ya Ole – Kengeja na ujenzi wa misingi ya maji ya mvua na gabion kwa barabara ya Mangwena zote zilifanywa na Wakala wa Barabara. Hata hivyo, fedha za utekelezaji wa kazi za ujenzi huo zilipatikana mwisho wa robo ya nne (30 Juni, 2021). Kwa sababu ya kuchelewa huko kwa fedha za utekelezaji kulisababisha pia kuchelewa kwa kazi hiyo na kutokamilika ndani ya mwaka wa fedha husika (2020/2021). **Uzibaji wa viraka kwa barabara za Mjini na Vijijini**

Kazi hizi zilijumuisha matengenezo ya kawaida ya mara kwa mara ya uzibaji wa mashimo kwa barabara za Mjini na Barabara za Vijijini. Wakala wa Barabara ilielekeza nguvu zaidi kwenye uzibaji wa viraka kwenye barabara kuu na barabara za Mjini ambazo zilikuwa zinahitaji matengenzo ya dharura. Barabara zilizozibwa viraka vya dharura ni Machomanne - Vitongoji, Chanjaani - U/Ndege na Wete - Gando. Baada ya kukamilika barabara za dharura tuliendelea na utaratibu uliowekwa wa kukamilisha barabara zilizobakia.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini mambo yafuatayo:

i) Ni kweli kuwa utekelezaji wa miradi ujenzi wa barabara kwa upande wa Pemba umechukua muda mkubwa na kushidwa kutekelezwa kwa wakati.

ii) Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi hazikuwa sahihi kwa upande wa takwimu za masafa ya uzibaji wa viraka katika Barabara za Mjini na Vijijini.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Wizara kwa upande wa Pemba kuhakikisha wanakamilisha utekelezaji wa miradi ya barabara kama ilivyopangwa katika bajeti husika ili kuepuka kuingiza hasara Serikali kwa kchelewesha utekelezaji wa miradi hiyo.

Aidha, Kamati inashauri Afisi ya Mdhibiti NA Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kazi za ukaguzi kwa ufanisi ili kutoa taarifa zilizosahihi za ukaguzi kwa wakaguliwa na kuepusha kuweka taarifa katika hoja ambazo sio sahihi.

**5.2.11.8 Kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi ya mafuta yenye thamani ya shilingi 803,711,500**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kupitia hati za kumbukumbu za ununuzi wa mafuta, vitabu vya kumbukumbu za kurikodia mafuta na kubaini hakukuwa na uthibitisho wa nyaraka kwamba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi – Pemba imepokea mafuta kutoka kwa Kampuni ya Mafuta ya GAPCO LTD Zanzibar yenye thamani ya shilingi 803,711,500.

Kukosekana vielelezo vinavyothibitisha kupokelewa kwa mafuta hayo kunapelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo ya mafuta hayo na matumizi yaliyofanyika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi – Pemba kuhakikisha inaweka udhibiti mzuri wa kumbukumbu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Manunuzi.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Pemba imepokea hoja inayohusiana na kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi ya mafuta yenye thamani ya Tshs 803,711,500 pia imeelezwa kuwa kwa ujumla Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi – Pemba kupitia Wakala wa Barabara ina jumla ya vyombo 10 ambavyo vinapaswa kupatiwa mafuta, Wizara kupitia Wakala kwa wakati huo wa ukaguzi ilikuwa inamiliki vyombo 20 zikiwemo Zana nzito, Magari na Mitambo na zilikuwa zinatumika kwa kazi za ujenzi pamoja na matengenezo ya barabara yaani 'Routine Maitanance.' vyombo kumi vilivyochaguliwa na Mkaguzi takriban vyombo hivyo vilikuwa havitumiki mara kwa mara na vingine havijatumika kabisa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 mfano mashine ya kupikia lami ya viraka (U-MIX) na Buldozer New Holand, aidha Piki piki Nne zilizoorodheshwa zinafanya kazi ya usimamizi wa kazi za matengenezo ya kawaida (Routine maintenance) kwa kawaida huwa wanapatiwa lita tano za Petrol kwa mzunguko wa kazi wa wiki moja. Hata hivyo utaratibu wa utoaji wa mafuta ulikuwa unafanyika kwa kutumia stores ledger, reguisition note pamoja na log book kwa magari yaliyokuwa yanatumika kwa wakati huo.

Kuhusu suala hili la matumizi ya mafuta kwa Wakala wa barabara ni ukweli usiofichika vipo vyombo ambavyo vilikuwa vinatumika bila ya kuwepo kwa log book kwa sababu ya kuto kusoma kwa mwenendo wa Magari yetu tuliyokuwa tunatumia yaani (mailage) hata hivyo utaratibu mwengine wa kuweka kumbu kumbu nzuri za mafuta zilikuwepo kama vile reguisition note pamoja stores ledger katika kuongeza uthibiti kwa magari ya kubebea kifusi pia tumeweka fomu maalum ambazo huonyesha mafuta yaliyoingizwa kwenye gari,

aina ya malighafi aliyobeba, muda aliopakiliwa malighafi hio, muda alioshusha pamoja na 'mileage' zake na fomu hizo husainiwa na Mkuu wa kware ambaye alimpakilia pamoja na 'Trip checker' ambaye kwa kawaida huwepo eneo la kazi. Fomu hizi huwasilishwa kwa Muhandisi dhamana kila siku na kuhifadhiwa katika faili maalum la kumbukumbu.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa Mdhibiti ameshidwa kutoa maelezo ya kielelezo kipi kinahitajika katika kuthibitisha mapokezi ya mafuta kwa upande wa Wizara Pemba kwa vile Mkaguzi alipewa kielelezo cha upokeaji wa mafuta kutoka Kampuni ya GAPCO hata hivyo mdhibiti hakuridhika na kielelezo hicho kwa vile alihitaji delivery note.

Hata hivyo Kamati imeifuta hoja hii kwa vile vielelezo vya upokeaji wa mafuta kutoka kampuni ya GAPCO viliwasilishwa mbele ya Kamati na kuridhiwa.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi MKuu wa Hesabu za Serikali kutokulazimisha kupatiwa kielelezo anachokita yeye tu kwa ajili ya kuthibitisha uhalali wa jambo fulani wakati vipo vielelezo ambavyo vinatosha kujiridhisha katika ukaguzi wa hoja husika.

**5.2.11.9 Kukosekana kwa udhibiti mzuri wa matumizi ya mafuta yenye thamani ya shilingi 1,293,203,250**

Kwa ujumla Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi – Pemba ina jumla ya vitendea kazi 10 ambavyo vinapaswa kupatiwa mafuta. Ili kuweza kuweka udhibiti mzuri wa mafuta ilipaswa kuwepo kwa uwekaji mzuri wa kumbukumbu kwa mujibu wa vitabu vya kurikodia mwenendo na masafa ya vyombo vya moto (log book).

Aidha, ukaguzi haukuweza kupatiwa stakabadhi za manunuzi (receipts) na mapokezi (Delivery Note) ya lita 574,757 yenye thamani ya shilingi 1,293,203,250 kutoka kwa msambazaji wa mafuta ambae ni Kampuni ya CAPCO LTD Zanzibar. Hata hivyo, imebainika utoaji wa mafuta haukuwa na utaratibu mzuri wa uwekaji kumbukumbu za mafuta

kutokana na kukosekana kwa makabidhiano ya mapokezi ya mafuta hayo. Vile vile, hakukuwa na uthibitisho kwamba vyombo 10 vilikuwa vikifanya kazi katika kipindi hicho ambapo imepelekea kutumika kwa mafuta hayo.

**Jadweli Nambari 68: Idadi ya Vyombo vya moto vilivyokadiriwa kutumia mafuta**

| **amba** | **laelezo** | **mabari sajili** | **lwaka lionunuliwa** | **ampuni iliyotengeneza** |
|---|---|---|---|---|
| | lotor Cycle | MZ 6747 | 008 | NGKEN |
| | lotor Cycle | MZ 6749 | 008 | NGKEN |
| | lotor Cycle | MZ 6750 | 008 | NGKEN |
| | lotor Cycle | MZ 433C | 010 | ONDA |
| | rusher | | 977 | ARKER |
| | sphalt | | 008 | -MIX |
| | uldozer | | 014 | EW HOLAND |
| | omb Roller | MZ 4569 | 994 | YNAPACK |
| | ib Roller | MZ 4568 | 994 | YNAPACK |
| | ump Truck | MZ 519B | 019 | ATA |

Kukosekana kwa daftari la kumbukumbu linalooonesha mwenendo wa gari, kiwango cha mafuta na masafa yaliyotumika kunaweza kupelekea matumizi mabaya ya rasilimali za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi – Pemba kuweka udhibiti mzuri wa usimamizi wa mafuta ili kuepusha matumizi yasiyokuwa na tija.

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Pemba imepokea hoja inayohusiana na Kukosekana kwa udhibiti nzuri wa matumizi ya mafuta yenye thamani ya Tshs 1,293,203,250, pia katika hoja hiyo imeelezwa Wizara inamiliki vitendea kazi 10 kwa wakati huo, Wizara kupitia Wakala wa Barabara ilikuwa inamiliki vitendea kazi 20 zikiwemo Zana, Magari na Mitambo, kuhusu utaratibu wa kutoa mafuta pamoja na log book pia kuna stores ledger book' na 'requesition book' zote zinatumika kwa ajili ya kuweka kumbu kumbu nzuri za mafuta.

Kuhusu stakabadhi za manunuzi (receipts) na mapokezi (delivery Note) ya lita 574,757 yenye thamani ya Tshs 1,293,203,250 kutoka kwa msambazaji wa mafuta ambae ni Kampuni ya GAPCO LTD Zanzibar Wakala wa Barabara inatumia fomu maalum za kukabidhiana mafuta yanayonunuliwa, fomu hiyo inawekwa sahihi na Afisa kutoka Wakala wa Barabara ambae ni mnunuzi na Afisa kutoka Kampuni GAPCO ambae ni muuzaji, hata hivyo Kampuni hiyo haitowi delivery note kwa sababu Tasisi ndio zinakwenda kununua wenyewe mafuta, kwa upande wa receipts zote zipo na zipo tayari kwa ajili ya ukaguzi, vile vile vielelzo vyengine vinavyohusiana na mapokezi ya mafuta ni pamoja na stores ledger book na reguisition form ambayo inatumika kwa ajili ya kutolea mafuta. Vyombo kumi vilivyochaguliwa na Mkaguzi takriban vyombo hivyo vilikuwa havitumiki mara kwa mara na vingine havijatumika kabisa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 mfano mashine ya kupikia lami ya viraka (U-MIX) na Buldozer New Holand, aidha Piki piki Nne zilizoorodheshwa zinafanya kazi ya usimamizi wa kazi za matengenezo ya kawaida (Routine maintenance) kwa kawaida huwa wanapatiwa lita tano za Petrol kwa mzunguko wa kazi wa wiki moja.

- **Combination Roller SMZ 4569 Dynapark.** Kifaa hiki kinatumika kwa kushindilia lami, hivyo matumizi yake ni ya chini sana na katika miaka mingine haitumiki kabisa. Kwa

mwaka 2020/2021 ilitumika kwa siku kumi na moja tu (Gombani Pagali siku nne. Mangwena siku mbili, Wete Konde siku moja na ZRB na Bohari siku nne.

- **Vibrating Roller:** Kifaa hiki hakifanyi kazi na kwa sasa kimeshauzwa kiliharibika tangu mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2020/2021 katika sehemu ya Mangwena.

Hivyo kwa mujibu wa vyombo vilivyochaguliwa ni Gari SMZ 519B tu ambayo inafanya kazi mara kwa mara na ina kumbukumbu nzuri za log book pamoja na kufuata taratibu nyengine za uwekaji wa kumbukumbu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa wakati wa ukaguzi hakukuwa na maelewano baina ya Mkaguzi na Mkaguliwa hali iliyosabibisha kushidwa kuelewana juu ya majibu ya hoja yaliyotolewa na Wizara kwani dosari hii ingeweza kupata usuluhishi kama wangelifahamiana ni vielelezo vipi vinahitajika katika kujibu hoja hiyo.

**5.2.11.10 Kutokukatwa kwa ushuru wa bidhaa shilingi milioni 29**

Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2019 Kifungu namba 4 (c)(iv) kinabainisha ya kwamba malipo ya wasambazaji wa bidhaa yanapaswa kutozwa kodi ya asilimia mbili (2%). Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi – Pemba imeshindwa kukata kodi kwa wasambazaji mbali mbali wa bidhaa na kupelekea kuikosesha mapato Serikali.

Hali halisi kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 69: Orodha ya wasambazaji wa bidhaa ambao hawajakatozwa kodi ya ushuru wa bidhaa**

| amba | arehe | ati Namba | ielipwa | asi cha Fed licholipwa | odi ya ushu yotakiwa kukatw |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 5/01/2021 | 40/1 | asoud Abrahman Masoud | 100,625,0 | 2,012,5 |
| 2 | 5/01/2021 | - | apco Zanzibar Limited | 64,790,0 | 1,295,8 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | /24/2020 | 7/32 | asoud Abrahman Masoud | 56,637,5 | 1,132,7 |
| 4 | /24/2020 | 7/31 | asoud Abrahman Masoud | 56,637,5 | 1,132,7 |
| 5 | /29/2021 | 36/4 | apco Zanzibar Limited | 38,171,0 | 763,4 |
| 6 | /17/2020 | 7/26 | shmoh Contractors Ltd | 37,524,0 | 750,4 |
| 7 | /11/2021 | 21/3 | alipo ya Ununuzi wa Mafuta | 36,594,0 | 731,8 |
| 8 | /06/2021 | 4/4 | apco Zanzibar Limited | 36,594,0 | 731,8 |
| 9 | /04/2021 | 14/2 | im Transporter Limited | 35,650,0 | 713,0 |
| 10 | /18/2020 | 19/11 | alfan Mohammed Khalfan | 35,592,5 | 711,8 |
| 11 | /15/2021 | 25/2 | apco Zanzibar Limited | 35,055,0 | 701,1 |
| 12 | /01/2021 | 1/3 | apco Zanzibar Limited | 35,055,0 | 701,1 |
| 13 | /11/2020 | 8/11 | apco Zanzibar Limited | 34,390,0 | 687,8 |
| 14 | /04/2021 | 12/10 | alfan Mohamed Khalfan | 34,040,0 | 687,8 |
| 15 | /22/2020 | 21/10 | apco Zanzibar Limited | 33,934,0 | 678,6 |
| 16 | /11/2021 | 12/5 | apco Zanzibar Limited | 33,544,5 | 670,8 |
| 17 | /30/2020 | 28/11 | apco Zanzibar Limited | 33,269,0 | 665,3 |
| 18 | /26/20202 | 22/11 | alipo ya Ununuzi wa Mafuta | 33,269,0 | 665,3 |
| 19 | /21/2020 | 7/27 | apco Zanzibar limited | 33,079,0 | 661,5 |
| 20 | /27/2021 | 63/1 | apco Zanzibar Limited | 32,566,0 | 651,3 |
| 21 | /08/2020 | 12/12 | apco Zanzibar Limited | 32,395,0 | 647,9 |
| 22 | /21/2020 | 27/12 | apco Zanzibar Limited | 32,395,0 | 647,9 |
| 23 | /29/2020 | 34/12 | apco Zanzibar Limited | 32,395,0 | 647,9 |
| 24 | 29/2021 | 94/6 | asoud Abrahman Masoud | 29,411,5 | 588,2 |
| 25 | /28/2021 | 83/6 | asoud Abrahman Masoud | 29,170,0 | 583,4 |
| 26 | /24/2020 | 7/33 | asoud Abrahman Masoud | 28,750,0 | 575,0 |
| 27 | /28/2021 | 84/6 | alfan Mohammed Khalfan | 26,275,2 | 525,5 |
| 28 | /08/2020 | 11/12 | apco Zanzibar limited | 25,575,0 | 511,5 |
| 29 | /07/2020 | 8/1 | im Transporters Ltd | 23,805,0 | 476,1 |
| 30 | /29/2020 | 7/38 | im Transporters Ltd | 23,805,0 | 476,1 |
| 31 | 15/2020 | 22/12 | alfan Mohammed Khalfan | 22,885,0 | 457,7 |
| 32 | /17/2021 | 38/3 | alfan Mohammed Khalfan | 22,080,0 | 441,6 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 33 | /06/2020 | 7/1 | zim Transporters Ltd | 21,240,0 | 424,8 |
| 34 | /15/2020 | 7/23 | zim Transporters Ltd | 21,240,0 | 424,8 |
| 35 | /18/2021 | 26/4 | apco Zanzibar limited | 19,085,5 | 381,7 |
| 36 | /25/2021 | 30/2 | asoud Abrahman Masoud | 18,975,0 | 379,5 |
| 37 | /09/2021 | 59/3 | apco Zanzibar limited | 18,297,0 | 365,9 |
| 38 | /01/2021 | 14/4 | apco Zanzibar limited | 18,297,0 | 365,9 |
| 39 | /09/2020 | 2/3 | apco Zanzibar limited | 17,527,5 | 350,5 |
| 40 | /28/2021 | 1/10 | apco Zanzibar limited | 17,252,0 | 345,0 |
| 41 | /22/2021 | 85/6 | saa Kheri Asaa | 16,344,7 | 326,8 |
| 42 | /27/2021 | 50/1 | apco Zanzibar limited | 16,283,0 | 325,6 |
| 43 | /04/2021 | 64/1 | apco Zanzibar limited | 16,283,0 | 325,6 |
| 44 | /04/2021 | 13/2 | apco Zanzibar limited | 16,283,0 | 325,6 |
| 45 | /05/2021 | 6/1 | apco Zanzibar limited | 16,197,5 | 323,9 |
| 46 | /29/2020 | 35/12 | apco Zanzibar limited | 16,197,5 | 323,9 |
| 47 | /30/2021 | 37/4 | halfan Mohammed Khalfan | 14,720,0 | 294,4 |
| 48 | /29/2021 | 95/6 | apco Zanzibar limited | 14,469,0 | 289,3 |
| 49 | /22/2021 | 62/6 | apco Zanzibar limited | 14,469,0 | 289,3 |
| 50 | /24/2021 | 37/2 | saa Kheri Asaa | 11,005,5 | 220,1 |
| 51 | /19/2021 | 29/4 | saa Kheri Asaa | 10,876,3 | 217,5 |
| **Jumla** | | | **1481,001,035** | | **29,620,0** |

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Pemba inakiri kupokea hoja inayohusiana na kutokukatwa kwa ushuru wa bidhaa ya Tshs 29,620,020, Wizara inapenda kutoa ufafanuzi juu ya ukatwaji wa kodi ya zuio pamoja na kodi nyengine kwa wasambazaji mbali mbali wa bidhaa kama walivyoorodheshwa na Mkaguzi.

Wasambazaji wote walioorodheshwa katika kiambatanisho nambari 69 wamekatwa kodi ya zuio (withholding Tax) ya asilimia 2 au asilimia 5 kwa upande wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na asilimia 15 ya VAT au asilimia 3 Stamp Duty kwa upande wa Bodi ya

Mapato Zanzibar (ZRB) ambayo kwa sasa inajulikana kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kodi hizo zote zilizokatwa kwa wakati na kwa mujibu wa sheria No. 7 mwaka 2009 Tax Administration Procedure Act (TAPA) kifungu No 50. Pamoja na Income Tax Act ya mwaka 2004 kifungu No 83.

Kodi ya zuio la mafuta kwa kampuni ya GAPCO kwa mujibu wa sheria ipo muongozo wa sheria ya mafuta , hata hivyo kodi hiyo inazuiwa moja kwa moja wakati wa uingizaji kwenye kituo kikuu cha kupokelea huko Wesha kwa upande wa Pemba kodi zinazotozwa ni pamoja na Petroleum Levy, Road Development Fund, Infrastructure Tax na Road Liecence, hakuna kiwango chengine kinachozuiwa wakati wa ununuzi wa mafuta.

Risiti za makato yote hayo kama zilivyoorodheshwa na Mkaguzi na kuwasilishwa kwa Taasisi yetu zipo tayari kwa ajili ya ukaguzi ukiondoa kodi ya mafuta kwa Kampuni ya GAPCO.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

i) Afisa aliyefanya ukaguzi wa hesabu ya makato ya kodi kwa wasambazaji wa bidhaa kwa asilimia 2 haikuwa sahihi kwa vile asilimia hiyo imekatwa katika fedha halisi ya malipo bidhaa kabla ya kukatwa kwa asilima ya 15 ya VAT na hatimae kutoa kiwango ambacho sio sahihi cha kodi kinachostahiki kukatwa.

ii) Aidha, kutokana na mapungufu hayo Kamati ya LAAC imejiridhisha kwa kupitia vielelezo vilivyowasilishwa mbele ya Kamati na kuthibitisha kuwa wasambazaji hao walikatwa kodi ya ushuru wa bidhaa, hivyo Kamati inaifuta hoja hiyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inaishauri Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wanapofanya ukaguzi kutumia wataalam wa fani husika katika kazi zao za ukaguzi ili kuondokana na uwepo wa hoja zisizohitajika kuwepo katika ripoti.

**5.2.11.11 Kukosekana kwa Ushahidi wa ushindani wa upatikanaji wa watoa huduma shilingi 221,105,170**

Kwa mujibu wa jadweli la tano la Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 linaitaka kuwepo kwa "quotation" za ushindani wa bei kwa wasambazaji mbali mbali kwa kuanzia manunuzi ya shilingi milioni 15 na chini ya milioni 50.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi – Pemba haikupata "quotation" za ushindani wa bei moja kwa moja kutoka kwa wasambazaji wa bidhaa za vifaa vya ujenzi. Orodha ya wasambazaji wa bidhaa na kiasi kilicholipwa yanaonyeshwa kwenye jadweli lifuatalo:

**Jadweli Nambari 70: Malipo yaliyolipwa bila ya kuwepo kwa ushindani wa bei**

| amba | arehe | ati Namba | lielipwa | iasi cha Fedh ilicholipwa |
|---|---|---|---|---|
| | 7/17/2020 | /26 | ashmoh Contractors Ltd | 7,524,000 |
| | 2/04/2021 | 4/2 | zim Transporter Limited | 5,650,000 |
| | 2/04/2021 | 2/4 | halfan Mohamed Khalfan | 4,040,000 |
| | 6/29/2021 | 4/6 | lassoud Abrahma lassoud | 9,411,250 |
| | 6/28/2021 | 4/6 | halfan Mohamed Khalfan | 6,275,200 |
| | 2/15/2020 | 2/12 | halfan Mohamed Khalfan | 2,885,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2/18/2021 | 0/2 | lassoud Abrahma lassoud | 8,975,000 |
| | 6/28/2021 | 5/6 | saa Kheri Assa | 6,344,720 |
| **ımla** | | | | **21,105,170** |

**Majibu ya Wizara**

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kupitia Wakala wa Barabara Pemba imepokea hoja inayohusiana na kukosekana kwa ushahidi wa ushindani wa upatikanaji wa watoa huduma wenye thamani ya Tshs 221,105,170 ikiwa ni Wasambazaji wa bidhaa na vifaa vya ujenzi kama walivyoorodheshwa na Mkaguzi.

Naomba kutoa maelezo kuwa vitabu vyote vinavyohusiana na watoa huduma mbali mbali kwa mujibu wa jadweli la tano la Sheria ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 linalotaka kuwepo kwa "quotation" za ushindani wa bei kwa wasambazaji mbali mbali kwa kuanzia manunuzi ya Tshs 15 na chini ya milioni 50 vitabu vyote vipo tayari kwa ajili ya ukaguzi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC baada ya kuvipitia kwa kina vielelezo vyote vilivyowasilishwa mbele ya Kamati imeondoa hoja hii. Kwa kuwa utaratibu uliotumika katika ushindani wa upatikanaji wa watoa huduma unakubalika kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya Mwaka 2016 wa "Framework Contract".

### 5.2.15 KAMPUNI YA UUNGANISHAJI NA USAMBAZAJI MAUDHUI (ZMUX)

**Taarifa ya Mapato**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Ripoti yake ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika na Taasisi Zinazojitegemea za SMZ kwa mwaka wa fedha 2020/2021 haikuonesha Taarifa ya Mapato ya Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui.

**Uchambuzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia suala hilo Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Kampuni hiyo katika mwaka huo wa fedha ilikadiriwa kukusanya jumla ya Tsh. 1,357,800,000 na hadi kufikia Juni, 2021 ilifanikiwa kukusanya Tsh. 1,363,236,903 kukiwa na ongezeko la Tsh. 5,436,903.

Kutokana na mapungufu hayo yaliyojitokeza kwenye Ripoti hiyo, Kamati ya LAAC inaishauri Afisi ya Mkaguzi Mkuu kuwa makini wakati inaandaa Ripoti zake ili kuepusha usumbufu kwa watumiaji wa Ripoti hizo.

**Majibu ya Kampuni**

Katika mwaka huo wa fedha Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui ililazimika kutumia fedha za ziada kutokana na sababu zifuatazo:

1. **Kutokubajeti maswala ya kodi**

Kampuni ilitakiwa kulipa kodi ya bidhaa zinazotoka nje (STB's) ambapo hapo awali ilikuwa inapewa msamaha wa kodi kupitia Wizara ya Fedha lakini kwa mwaka 20/21 ilitakiwa bidhaa hizo kuzilipia kodi, hali ambayo ilipelekea kupanda kwa matumizi hayo.

2. **Ving'amuzi vya ziada vya dharura**

Kutokana na uhitaji mkubwa wa STB’s Kampuni iliomba ruhusa ya kununuwa STB’s elfu moja (1000) ambavyo vilisafirishwa kwa njia ya ndege kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya wateja na kuzuwia soko la biashara hali hio ilipelekea kuongezeka kwa matumizi haya.

3. **Kuongezeka kwa ‘exchange rate’**

Ununuzi wa STB’s malipo yake yaliongezeka kutokana na kupanda kwa Dola.

4. **Malipo ya mkonga wa Serikali.**

Hapo awali Kampuni haikuwa ikilipa gharama za huduma ya mkonga wa Serikali lakini kwa mwaka 2020/2021 ZMUX ilitakiwa kuchangia gharama za uendeshaji na matengenezo (operation and maintenance) kwa shilingi milioni kumi kwa mwezi (Tsh. 10,000,000) jambo ambalo lilipelekea kupanda kwa matumizi.

5. **Kuongezeka kwa matumizi ya Umeme.**

Awali Kampuni ilikuwa ikirusha matangazo yake kwa transimiter moja tu, lakini mara baada ya uhitaji wa content za ziada Kampuni ilipaswa kuongeza transmitter ya ziada jambo ambalo lipelekea kuongezeka kwa matumizi ya umeme katika vituo.

**Uchanguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilitaka kujua kiwango cha fedha kilicholipwa kwa upande wa kodi ambapo ilielezwa kuwa jumla ya Tsh. 42,427,606 zililipwa kwa mwaka huo.

Vile vile, Kamati ilitaka kujukua kiwango cha fedha kilicholipwa kwa ajili ya matumizi ya mkonga ambapo ilielezwa kuwa jumla ya Tsh. 60,000,000 zililipwa kwa matumizi hayo.

Kamati ya LAAC iliridhika na majibu ya Kampuni hivyo haikuwa na maelezo zaidi.

**5.2.15.1 Dosari katika Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu za ZMUX**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kampuni ya ZMUX haikuingiza taarifa za hesabu za mwaka uliopita ili kuweza kulinganisha taarifa za hesabu za miaka miwili tofauti hali ambayo inaweza kupelekea taarifa za hesabu kutokuwa sahihi ambapo ni kwenda kinyume na muongozo wa kimataifa wa utayarishaji na uwasilishaji wa taarifa za hesabu (IPSAS1).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kampuni kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya utayarishaji na uwasilishaji wa tarifa za hesabu za kitaifa na kimataifa.

**Majibu ya Kampuni**

Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui (ZMUX) wakati wa uandaaji wa hesabu za mwaka 2020/2021 haikuweka hesabu ya mwaka uliopita (2019/2020) kwa lengo la kupata mlinganisho wa hesabu “ comparabililty” hata hivyo, masawazisho yalishafanyika na mlinganisho huo ulishawasilishwa Wizara ya Nchi, (AR), Fedha na Mipango kwa ajili ya masawazisho.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haikuwajibika ipasavyo wakati Kampuni ya ZMUX ilivyowasilisha Taarifa ya Hesabu ya Fedha ya Mwaka. Hivyo, kwa namna moja au nyengine Kamati ya LAAC inadiriki kutamka kuwa Afisi ya Mkaguzi Mkuu imechangia kwa kiasi kikubwa kutokea kwa dosari hiyo.

Kamati ya LAAC inatamka hivyo kwa kuwa Afisi ya Mkaguzi Mkuu huzipitia Taarifa za Hesabu za Fedha za Mwaka za kila Taasisi na endapo itabaini mapungufu basi Taasisi hiyo hutakiwa kufanya marekebisho, hata hivyo, kwa upande wa Kampuni hii jambo hilo halikufanyika na dosari hiyo ilibanika na Wizara ya Nchi, (AR), Fedha na Mipango.

Kwa kuwa nyaraka hiyo iliwasilishwa zaidi ya sehemu moja, na kwa kuwa jambo hili limeshafanyika, hivyo basi, Kamati ya LAAC inaishauri Kampuni endapo itatokea jambo lolote ambalo imehusisha zaidi ya Taasisi moja ni vyema marekebisho yoyote yatakayofanyika kuhusiana na jambo hilo yakawasilishwa kwa Taasisi zote ili kila Taasisi iweze kujua kilichofanyika dhidi ya jambo hilo.

**5.2.15.2 Matumizi Yaliyofanywa Nje ya Vifungu vya Bajeti**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba ZMUX imefanya matumizi nje ya vifungu bila ya kuwepo kwa idhini kutoka kwa Katibu Mkuu anayehusika hali inayoweza kupelekea uhalali wa malipo hayo kutokuthibitika kisheria ambapo ni kwenda na kinyume na sharia nambari 12 ya usimamizi wa fedha za umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZMUX kuhakikisha unazingatia Sheria, Kanuni na Miongozo wakati wa kufanya malipo ili kuepuka kufanya malipo nje ya Bajeti iliyoidhinishwa.

Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jaduweli hapo chini:-

| Jina Na Kifungu | Bajeti Iliyoidhinishwa | Kiasi Cha Fedha Kilichotumika | Kiasi Cha Fedha Kilichotumika Nje Ya Bajeti | Asilimia Iliyotumika Nje Ya Bajeti |
|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa Decoder | 400,000,000 | 488,547,000 | 88,547,000 | 22.14 |
| Ununuzi wa Antena | 100,000,000 | 127,109,988 | 27,109,988 | 27.11 |

**Majibu ya Kampuni**

Kampuni ya ZMUX kwa mwaka wa fedha 2020/2021 uliopita baadhi ya matumizi yake katika kifungu cha ununuzi wa ving'amuzi na antena yamezidi makadirio, hii imesababishwa na malipo ya kodi za utowaji wa bidhaa hizo katika bandari ya Zanzibar, hata hivyo, ruhusa ya matumizi hayo yalitolewa na Katibu Mkuu.

Aidha, ikumbukwe kuwa Kampuni ilikuwa inapata msamaha wa kodi (exemption) katika uingizaji wa ving'amuzi kwa miaka yote iliyopita, ila kwa ving'amuzi vya mwaka 2020/2021 Serikali iliitaka Kampuni kulipa kodi zote zinazohusiana na uingizaji wa bidhaa zao nchini hali ambayo ilipelekea kuongezeka kwa matumizi kulinganisha na bajeti iliyopangwa katika vifungu hivyo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kujiridhisha na majibu ya Kampuni, Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa barua iliyoruhusu matumizi hayo ambapo Kampuni ya ZMUX iliwasilisha nakala ya barua ya terehe 15 Septemba, 2020 yenye kumbukumbu Namba WHUMK/H.10/22/VOL.II/167.

Vile vile, katika kufuatilia hoja hii Kamati ilibaini kuwa Kampuni inatumia baadhi ya Watendaji na Vitengo vya Wizara katika kufanikisha shughuli zake. Kwa mfano; Mkaguzi wa Hesabu za Ndani, Bodi ya Zabuni na kadhalika.

Kutokana na hilo, Kamati ya LAAC imeishauri Kampuni kuhakikisha kuwa inakuwa na Watendaji na Vitengo vyake ili Kampuni hiyo ijitegemee kiutendaji.

Kwa msingi huo, Kamati inaishauri Kampuni kuukamilisha muundo wa Afisi haraka iwezekanavyo ili kasoro hiyo iondoke.

**5.2.15.3 Kukosekana Ripoti ya Uchunguzi wa Ubora wa Vifaa**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kampuni ya ZMUX haikuandaa ripoti ya ukaguzi wa ubora wa bidhaa mbalimbali (Inspection Report) vinavyonunuliwa hali ambayo inaweza kupelekea kupokea na kutumika kwa bidhaa zisizo na viwango ambapo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa ZMUX kuhakikisha unafanya uchunguzi wa bidhaa inazonunua pamoja na kuandaa ripoti ya uchunguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa viwango vya bidhaa hizo.

**Majibu ya Kampuni**

Kampuni ya ZMUX kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliingiza nchini vin'gamuzi na antena kutoka nchini China, ripoti za uchunguzi (Inspection reports) kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na ile ya Zanzibar (ZBS) zilifanyika na tunaimbatanisha katika ripoti hii.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hizo Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Takribani vifaa vingi vinavyotumiwa na Kampuni ni vya muda mrefu kwani vipo ambavyo vina miaka 10.

   Kutokana na hilo Kamati ya LAAC inaishauri Kampuni kununua vifaa vya kisasa ili kwenda na wakati.

2. Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 huwakwaza baadhi ya Taasisi za Umma, ikiwemo Kampuni ya ZMUX kwa upande wa kufanya biashara na Wafanyabiashara ambao wamesajiliwa.

   Hii ni kutokana na kuwa Kampuni hii hufanya sana biashara na Kampuni za nje ya nchi hususan China, hivyo, ni vigumu kwa Kampuni hizo kufanya usajili Zanzibar.

   Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuifanyia marekebisho Sheria hiyo ili kila Taasisi itumie Sheria hiyo bila usumbufu wowote.

3. Bei za bidhaa mbali mbali zilizowekwa kwenye mfumo hazilingani na uhalisia wake, hivyo, Kamati ya LAAC inaishauri Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kulifanyia kazi suala hilo ili kuwa na bei inayoendana na uhalisia.

## 5.2.16 MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)

**Taarifa ya Mapato**

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 24,545,220,914. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ilikusanya jumla ya shilingi 8,380,692,230.37 sawa na asilimia 34 ya makadirio.

**Majibu ya Mamlaka ya maji Zanzibar (ZAWA)**

Kwa mwaka wa Fedha 2020/21 Mamlaka ya Maji Imepangiwa kukusanya Tsh 10,452,500,914 kutoka vyanzo vya ndani na Tsh 14,092,720,000 kutoka serikali kuu kwa shughuli mbali mbali za maendeleo.

Ni kweli Mamlaka kwa kwaka wa fedha 2020/21 ulifanikiwa kukusanya Tsh7,799,887,593.93 sawa na asilimia 32 ya makadirio. Makusanyo ya ndani yalikuwa ni Tsh 3,002,792,136 ambapo Tsh 5,377,900,095 zilipatikana kutoka serikali kuu kwa shughuli za maendeleo. Hii imetoka na sababu mbali mbali:

- Kuharibika kwa pampu mara kwa mara kunokotokana na kupanda na kushuka kwa umeme.
- Mwamko mdogo wa wateja juu ya ulipiaji wa huduma ya Maji.
- Kukosekana kwa huduma ya maji kwa sehemu kubwa ya maeneo ya uwekezaji.
- Idadi ndogo ya wateja waliofungiwa mita.
- Kwa upande wa fedha kutoka serikali kuu, mamlaka imepatiwa Tshs 5,377,900,095 sawa na asilimia 38 ya makadirio. Hii imetokana na ufinyu wa Bajeti.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Baada ya kupitia kwa kina taarifa ya Mapato Kamati imeona ipo haja ya Mamlaka kuchukua hatua zifuatazo ili kuongeza ukusanyaji wa mapato.

- Mamlaka kuboresha miundombinu ya maji katika maeneo mbali mbali ya Mji wa Zanzibar.
- Kuongeza idadi ya ufungaji mita kwa wanaopata huduma ya maji kwa uhakika.
- Kuongeza visima vipya vya maji pamoja na kuweka pampu za kisasa ikiwemo pampu zinazotumia nishati ya jua "solar energy".
- Kutoa elimu kwa jamii juu ya utunzaji wa maji pamoja na ushajihishaji wa kulipa kwa hiari huduma ya maji.

**Taarifa ya Matumizi**

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 24,545,222,914 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 kiasi cha shilingi 7,799,887,593.93 kimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ni sawa na asilimia 32 ya makadirio

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2021, Mamlaka ilitarajia kutumia Tsh 24,545,220,914 kwa kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Ambapo Tshs 7,799,887,593.93 zilitumika kwa mwaka huo wa fedha. Mamlaka ilipokea Tshs 3,626,499,991 ikiwa kama ruzuku ya mishahara na Tsh 1,751,400,103.80 kwa kazi mbali mbali za maendeleo ikiwemo ununuzi wa Pampu, malipo ya fidia kwa

waathirika wa miradi,Gharama za kuunganishiwa umeme, ujenzi wa vibanda vya kuhifadhia mitambo na kadhalika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kupitia taarifa ya matumizi imebaini kuwa Mamlaka imepokea kiwango kidogo cha ruzuku kutoka Serikalini ikiwa ni sawa na asilimia 32 ya makadario, hivyo ni wazi kuwa shughuli nyingi zilizopangwa za kuboresha huduma za upatikanaji wa maji hazikuweza kutekelezeka ipasavyo.

Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka kujikita zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kama kuna upungufu wa ruzuku kutoka Serikali nakisi hiyo itaweza kufidiwa na mapato hayo na kuweza kukamilisha shughuli zilizopangwa kwa mwaka husika wa Bajeti.

**5.2.16.1 Kuwepo kwa ukusanyaji pungufu wa mapato.**

Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kufanya makusanyo ya shilingi 10,452,500,914 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 makusanyo halisi yalikuwa ni shilingi 3,002,792,136 sawa na asilimia 28.73 ya makadirio kukiwa na upungufu wa jumla ya shilingi 7,449,708,778 sawa na asilimia 71.27 za makadirio.

Hali hii inaweza kupelekea kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa jambo ambali litarudisha nyuma maendeleo ya Serikali.

Uongozi wa Mamlaka ya Maji unashauriwa kusimamia ukusanyaji wa mapato kiukamilifu, pamoja na kuangalia changamoto zote zilizokwamisha ukusanyaji wa mapato ili kwenye mwaka wa fedha unaofata kuzisawazisha na kufikia malengo yaliyopangwa. Hali halisi ya

mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 72 : Kuwepo kwa ukusanyaji pungufu wa mapato**

| Namba | Maelezo | Kiasi cha Fedha zilizokusanywa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | akadirio ya mapato kwa mwaka 2020/2021 | 10,452,500,9 |
| 2 | apato halisi yaliyokusanywa kwa mwaka 2020/2021 | 3,002,792,1 |
| 3 | fauti ya makadirio na makusanyo (mapato liyokosekana) | 7,449,708,7 |
| 4 | ilimia ya mapato yaliyokosekana | 71 |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji ZAWA**

Ni kweli malengo ya makusanyo hayakufikiwa kwa mwaka 2020/2021 kulikosababishwa na kukosekana kwa maji sehemu kubwa ya wateja pamoja na idadi ndogo ya wateja wenye mita. Kwa sasa Menejimenti imepanga kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kuboresha upatikanaji wa maji kupitia miradi ya Maji inayotekelezwa. (Uhuishaji na Uimarishaji wa huduma ya Maji-Benkiya Exim India na mradi wa Ahueni ya UVIKO 19) na kuwafungia mita za maji kwa wateja wake.

Aidha Mamlaka imeanza kufunga mita kwa wateja wake ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023.Ambapo tunatarajia kuendelea kufunga mita hizo kwa wateja wa mahoteli na Taasisi za Serikali na wateja binafsi kwa mwaka fedha 2023/2024

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kulichunguza hili imebaini kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) haikuwa na uwezo wa kusambaza maji kwa wateja wake wote kutokana na kuwa na visima vichache vinavyozalisha maji na kuwa na miundombinu chakavu inayoathiri usambazaji maji kwa wananchi wa Zanzibar, jambo ambalo linapelekea wananchi hao kutolipia huduma za maji kwa sababu ya kukosa huduma hiyo

Vile vile Kamati imebaini upotevu wa Mapato kwa Mamlaka kutokana na kutumia mifumo ya kizamani ya kukadiria bili na kutoa risiti kwa wateja hali inayopelekea ukwasi katika kufuatilia bili hizo kwa wateja na wakati mwengine bili hizo huwa na makisio ambayo si sahihi.

Aidha, Kamati imearifiwa kuwa Mamlaka inatekeleza miradi miwili ambayo inalenga kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji na kufunga mita za kisasa (Smart meter na Prepaid meter) kwa ajili kudhibiti matumizi mabaya ya maji na kuongeza mapato kwa Mamlaka,

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Mamlaka kusimamia vyema miradi hiyo ili kuweza kutekelezwa kwa wakati uliopangwa na wananchi waweze kupatiwa huduma ya maji kwa uhakika ili kuepusha kutolipa huduma ya maji kunakosababishwa na kutopata huduma hiyo kwa wakati na kwa uhakika,

Aidha, Kamati inashauri Mamlaka inalisimamia vyema zoezi la ufungaji mita za maji katika makaazi ya watu na sehemuu za biashara na kuhakikisha kuwa ufungaji wa mita hizo unakwenda sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya upatikanaji wa maji katika maeneo hayo kwa lengo la kuongeza wigo wa makusanyo ya mapato ya Mamlaka.

### 5.2.16.2 Dosari iliyobainika katika malipo ya wateja wa Mahoteli

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Maji inatumia mfumo wa malipo kwa watenja wake mbalimbali, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuendana kwa taarifa za mapato na kupelekea kushindwa kutofautisha aina za wateja wa Mahoteli waliosajiliwa katika mfumo huo hali inayopelekea kukosekana kwa tija ya ukusanyaji kwa kutokufikiwa kwa malengo yaliyopangwa ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya Maji namba 4 ya mwaka 2006 kifungu cha 31 (1).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka kufanya jitihada za makusudi za kuiwezesha Mamlaka ya Maji ili iweze kurekebisha mifumo yake ya mapato ikiwa ni pamoja na kuweza kufanya utambuzi wa aina ya wateja walionao pamoja na hadhi za Mahoteli yanayopatiwa huduma ya maji.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji ZAWA**

Kutokana na Sheria ya Maji Namba 4 ya Mwaka 2006 ambayo imepelekea kuwepo kwa kanuni ya Ada ya Maji 2013 maalum wa bei za maji “tariff”, tariff ya huduma ya maji imegawika sehemu kuu 2. Wateja wenye matumizi ya mita na wateja wa bei za makisio ambao hawana mita.

Kutokana na bei hizo mahoteli ambayo yameshafungwa mita yanaondoka kwenye bei za makisio ambazo zilibainishwa kwa madaraja na hivyo kulipia kwa mujibu wa matumizi, aidha Mamlaka inaendelea na mpango wakuimarisha taarifa za wateja kwa kubadilisha mfumo wa taarifa za wateja kutoka kwenye SBM2 na kuingia kwenye mfumo wa UNIFIED BILLING SYSTEM unaotumika na Mamlaka zote za maji Tanzania.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hii Kamati inaendelea kushauri katika kuweka mifumo bora ya Udhibiti wa mapato ya Mamlaka, kwa vile utaratibu wa kufunga

mita mpya umeshaanza basi ni vyema kuharakisha ufungaji huo hasa katika maeneo ya Hoteli za Kitalii kwa vile maeneo hayo yanatumia kiwango kikubwa cha maji hivyo kukosa bili sahihi za utumiaji wa maji katika mahoteli kwa kutokuwa na mita za maji ni kuipotezea Mamlaka mapato na hatimae shughuli za Mamlaka kuzorota.

**5.2.16.3 Mapato yanayodaiwa na Mamlaka kwa ajili ya utoaji huduma kwa mahoteli 139,573,446.27**

Katika ukaguzi uliofanyika imebaina kwamba kuna wateja wa mahoteli wa daraja mbali mbali ambao hawakulipa bili zao za kila mwezi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hali iliyopelekea upungufu wa makusanyo na hivyo kuikosesha Serikali mapato ambayo yangeweza kutumika kwa jaili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali za maendeleo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume kifungu cha 31 (1) cha sheria ya maji nambari 4 ya mwaka 2006. Hali halisi ya mahoteli ambayo hayakulipa bili za maji ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 73 : Mahoteli ambayo hayakulipa bili za Maji**

| Namba | a la Hoteli | mbari ya ta | ambao haikulipiwa huduma maji | Kiasi cha fedha kinachodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ntain Garden lage | one | /06/2013 hadi 30/06/ 2021 | 5,200,000. |
| 2 | lele Villa | 54466 | /06/2013 hadi 30/0/6 2021 | 1,420,162. |
| 3 | nani Kendwa | Non | /06/2013 hadi 30/06/ 2021 | 9,500,0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ach Bangalows | | | |
| 4 | Rosa Dei Vent | on | /06/2013 hadi 30/06/ 2021 | 4,480,000. |
| 5 | ame Tree Cotta | on | /06/2013 hadi 30/06/ 2021 | 56,020,000. |
| 6 | galawa Lodge | 95747 | /01/2019 hadi 30/06/2021 | 2,400,000. |
| 7 | llardin Compan D | 86261 | /01/2021 hadi 30/06 2021 | 28,000. |
| 8 | conut Beach In | on | /06/2013 hadi 30/06/2021 | 2,880,000. |
| 9 | ghland Bungalo | on | /02/2021 hadi 30/06/2021 | 19,000. |
| 10 | otel Executive | on | /06/2013 hadi 30/06/ 2021 | 3,858,800. |
| 11 | aruhubi Beach la | 95763 | June 2013-30 June 2021 | 5,570,000. |
| 12 | anch Lodge | on | /06/2013 hadi 30/06 2021 | 5,900,000. |
| 13 | na Beach Hotel | 95765 | /04/2019 hadi 30/06/2021 | 27,332,484. |
| 14 | nazi Upepo | on | /06/2013 hadi 30/06/2021 | 3,240,000. |
| 15 | occo Beach Vill | on | /06/2013 hadi 30/06/2021 | 6,840,000. |
| 16 | zimkazi Beach llage | on | /06/2013 hadi 30/06/2021 | 1,827,000. |
| 17 | oni Lodge nzibar | on | 09/2013 hadi 30/06/2021 | 28,000. |
| 18 | nex 11 Imani ach Lodge | on | /06/2013 hadi 30/06/2021 | 3,030,000. |
| Jumla | | | | 139,573,446. |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji ZAWA**

Jumla ya hoteli 18 zimekosekana mapato yake kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 kutokana na sababu zifuatazo

Baadhi ya hoteli kukosa maji kwa kipindi kirefu ila bili zao kuingia katika mfumo wa malipo kila mwezi kutokana na kutumia bei za makisio.

Baadhi ya mahoteli kufungwa kabisa kutokana na kuwepo kwa maradhi ya uviko-19 Aidha ZAWA inatarajia kufanya uhakiki maalum kwa mahoteli yote ili kutambua vyanzo halisi vya huduma ya maji, utafiti huo utashirikisha watendaji wa ZAWA na watendaji wa chuo cha maji. Uhakiki umeshaanza kwa hotel zote za mkoa wa Mjini Magharibi na Mikoa mengine inategemewa kumalizika ndani ya mwaka huu wa fedha 2022/2023.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kwamba baadhi ya madeni ambayo Mamlaka inadai kwa wateja wake wa Mahotelini sio sahihi kwa vile Mfumo wanaotumia wa kutoa bili za huduma ya maji kwa wateja unatoa bili hata kama mteja hapati maji kabisa au hatumii huduma ya maji pindi akifunga hoteli kwa sababu mbalimbali kama vile kutokea kwa mripuko wa maradhi ya UVIKO 19, hali hii inapelekea kuwasababisha madeni makubwa wateja wao ambao mwisho wa siku wanashidwa kulipa madeni hayo

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya inaishauri Mamlaka ya Maji (ZAWA) kusimamia vyema utekelezaji wa mradi wa ufungaji mita za maji majumbani na sehemu za biashara ili ukamilike kwa wakati na kuondoa changamoto hizo za kuwalimbikizia madeni wateja wake kutokana na kuwafanyia makisio ambayo sio sahii kwa kutumia mfumo wa SBM2 ambao una kasoro kadhaa. Aidha, Kamati inasisitiza juu ya uharakishaji wa ufanyaji wa uhakiki wa madeni hayo kama walivyopangwa kukamilika mchakato huo katika mwaka wa fedha 2022/2023 ili wadaiwa hao waweze kulipa madeni sahihi yanayodaiwa na Mamlaka iweze kupata mapato yake

wanayodai kutoka kwa wateja wake hao.

**5.2.16.4 Mifumo ya kukusanyia mapato SBM2, POS, Zantel na Tigo kumilikiwa na Kampuni binafsi**

Ukaguzi uliofanywa umebaini kwamba Mamlaka ya Maji ZAWA inatumia mifumo ya aina tatu katika kutekeleza majukumu yake ya ukusanyaji wa mapato mifumo yenyewe ni SBM2, POS (Point of sales), mtandao wa Zantel na mtandao wa Tigo.

Ukaguzi umebaini kuwa mifumo yote mitatu inayotumika ndani ya Ofisi za Mamlaka ya maji kwa ajili ya kukusanyia mapato inamilikiwa na Kampuni za watu binafsi hali ianyoweza kupelekea kushindwa kupata ufanisi katika makusanyo yatokanayo na makusanyo ya mapato.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kufanya juhudi za ziada ili kuweza kuwa na udhibiti mzuri katika ukusanyaji wa mapato na kupelekea utoaji wa huduma bora zilizokusudiwa.

Aidha kuendelea kutumia mifumo ya Kampuni binafsi kwa ajili ya makusanyo ya mapato kwa Serikali kunaweza kupelekea Serikali kutopatiwa taarifa sahihi za makusanyo ya mapato kutoka kwa Kampuni binafsi jambo ambalo linaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma na kuingiza hasara Serikali.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji ZAWA**

ZAWA inakiri kutumia mifumo ya aina tatu kama ilivyoainishwa katika hoja ya mkaguzi kwa lengo la kukusanya mapato kwa urahisi na kuweza kupunguza malipo ya fedha taslim pia kuepuka kutumia risiti za mkono (Manual receipt), Hata hivyo kwa wakati huo Serikali ilikuwa bado haijaanza kutoa huduma hiyo. ZAWA kwa sasa imeacha kutumia huduma hizo na inakusanya mapato yake kupitia

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Malaka imekiri kuwepo kwa dosari hii na tayari wameshachukua hatua ya kuachana na matumizi ya mifumo hii na kutumia mfumo wa malipo wa Serikali wa Zan Malipo na mfumo wa taarifa za wateja uitwao **UNIFIED BILLING SYSTEM** ambao unamilikiwa na Mamlaka. Kamati haikuona haja ya kuendelea na hoja hii, aidha Kamati imeendelea kuzishauri Mamlaka za Serikali kwa kuzibiti mianya ya upotevu wa mapato kwa kutumia mifumo ya ukusanyaji mapato inayomilikiwa na Mamlaka badala ya mtu binafsi ambayo huenda ikafanyiwa hujuma kwa kutoa taarifa zisizo sahihi za ukusanyaji wa mapato ikiwa mtu huyo si muaminifu.

**5.2.16.5 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na utoaji wa huduma ya maji shilingi 406,093,121.881**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 406,093,121.881 ni kiasi cha fedha kinacho daiwa na Mamlaka ya Maji kwa ajili ya utoaji wa huduma ya maji kwa taaasisi mbali mbali zilizoweza kupatiwa huduma ya maji lakini wameshindwa kufanya malipo yao na kupelekea uwepo wa malimbikizo ya madeni ambayo yanaweza kupelekea kukosekana kwa ufanisi katika utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Zanzibar ambapo ni kwenda kinyume na kifungu namba. 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kufanya juhudi za ziada ili kuweza kuwa na ufuatiliaji mzuri katika ukusanyaji wa mapato na kupelekea utoaji wa huduma bora zilizokusudiwa. Hali halisi ya madeni yatokanayo na utoaji wa huduma ya maji ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 74 : Madeni yatokanayo na utoaji wa huduma ya maji**

| Namba | Jina la taasisi | ha kinachodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | ɔspitali ya Mnazi Mmoja | 194,702,127. |
| 2 | irika la Utangazaji ZBC TV na Radio | 5,784,041. |
| 3 | irika la Umeme | 37,096,386. |
| 4 | akao Makuu J.W.T.Z Kambi 14 | 28,431,424. |
| 5 | raza la Wawakilishi | 9,616,068. |
| 6 | isi ya Raisi | 9,760,049. |
| 7 | ara ya Maendeleo ya Uvuvi | 1,881,000. |
| 8 | izara ya Afya | 106,666. |
| 9 | irika la Bandari | 275,013. |
| 10 | amlaka ya Udhibiti Maji na Nishati | 758,867. |
| 11 | TC Maisara | 404,781. |
| 12 | uli ya Sekondari ya Dr Abeid Amani Karume | 18,469,684. |
| 13 | uli ya Sekondari ya Dr Ali Mohammed Shein | 3,712,647. |
| 14 | uli ya Sekondari Mikindani Dole | 2,706,713. |
| 15 | uli ya Sekondari Aboud Jumbe Mwinyi Fuoni | 2,818,855. |
| 16 | uli ya Sekondari ya Dr John P Magufuli | 1,203,099. |
| 17 | uli ya Sekondari Lumumba | 964,000. |
| 18 | uli ya Sekondari Ben Bella | 3,948,113. |
| 19 | izara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 27,962,610. |
| 20 | uli ya Sekondari Ya Haile Selas | 1,710,000. |

| | | |
|---|---|---|
| 21 | amlaka ya Udhibiti Maji na Nishati (ZURA) | 2,505,135. |
| 22 | uli ya Miwaleni | 926,417. |
| 23 | nzania Revenue Authority | 1,781,918. |
| 24 | TC Building | 975,757. |
| 25 | raza la Manispa Magharibi | 9,014,112. |
| 26 | vanja wa MaoTsetung | 1,991,861. |
| 27 | izara ya Kilimo Maliasili na Mifugo na Uvuvi | 1,483,194. |
| 28 | SF | 4,020,493. |
| 29 | yumba ya Makamo wa Kwanza | 962,822. |
| 30 | yumba ya Mkamo wa Pili wa Rais | 983,360. |
| 31 | ara ya Utabibu Mifugo | 2,433,315. |
| 32 | spital ya KMKM | 2,668.321. |
| 33 | rume Institute | 809,679. |
| 34 | izara ya Habari | 275,013. |
| 35 | tuo cha Polisi Madema | 24,846,000. |
| | mla | 406,093,121.8 |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji (ZAWA)**

Mamlaka inaendelea na ufuatiliaji wa madeni kwa wadaiwa hao, sambamba na kutoa Ankara za malipo (Monthly Bill) pamoja na barua za ukumbusho kwa wadaiwa. Aidha mpango wa Mamlaka kwa sasa ni kuanza kuwafungia SMART WATER METER Pamoja na PREPAID WATER METER wateja wote wa Taasisi ili kuepusha usumbufu wa kudai bili mwisho wa mwezi, zoezi ambalo linatarajiwa kuanza ndani ya mwezi wa mei 2023 kwaupande wa taasisi za Serikali.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja imesikitishwa sana na kuongezeka kwa madeni hayo kila mwaka licha ya Kamati hii kufanya jitihada mbali mbali za kuhakikisha madeni haya yanalipwa kwa kukutana na Uongozi wa Ofisi ya Rais fedha na Mipango na kutafuta njia mbadala ikiwemo taasisi zinazodaiwa kukwata fedha za OC kwa kila mwaka wa fedha ili fedha hizo zilipwe katika madeni ya Maji wanayodaiwa ila hadi sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada za Mamlaka hii katika kuwapatia huduma za maji wananchi wa Zanzibar.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile utaratibu huu wa kupunguza madeni kwa taasisi kupitia kukatwa OC zao na Ofisi ya Rais fedha na Mipango kushindikana, Kamati inashauri Serikali kutafuta njia mbadala au suluhisho la kuduma ili kila taasisi za Serikali zilipe madeni ya huduma mbalimbali wanazopatiwa na taasisi nyengine.

Aidha, Kamati inaisisitiza  Mamlaka kukamilisha kwa wakati mpango wake wa kuwafungia SMART WATER METER Pamoja na PREPAID WATER METER zoezi ambalo linatarajiwa kuanza ndani ya mwezi wa mei 2023 kwa upande wa taasisi za Serikali.

**5.2.16.6 Kukiukwa kwa taratibu za Mpango wa Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kwa Walinzi wa ZAWA shilingi 196,200,000**

Ukaguzi uliofanywa umebaini kwamba Mamlaka ya Maji ZAWA imegawa manunuzi kwa ajili ya kupata huduma za ulinzi kutoka katika Kampuni tano (5) tofauti ambapo kunapelekea kufanyika kwa kazi zinazolingana kwa kutumia watoa huduma tofauti jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha 42(c) cha sheria nambari 11ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka, kufanya kazi za manunuzi kwa kuzingatia sheria

kanuni pamoja na miongozo mbali mbali inavyoelekeza ikiwa ni pamoja kutofanya mgawanyo wa kazi unaopelekea kukwepa uitishaji wa zabuni kutokana na kazi zilizopangwa.

**Jadweli Nambari 75 : Kampuni zilizotumika katika utoaji wa huduma**

| **Namba** | **a la Kampuni** | **Tarehe ya kufung mkataba** | **a wa malip** | **mla ya malipo kv mwezi (Tshs)** | **Jumla ya malipo kwa kipindi cha mkataba (Tshs)** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ınd Mash Company Ltc | /07/2020 | vaka 1 | 1,800,( | 21,600,( |
| 2 | ınd Mash Company Ltc | /07/2020- /06/2021 | vaka 1 | 900,( | 10,800,( |
| 3 | ı SGA | /12/2020 | ezi 7 | 3,600,( | 25,200,( |
| 4 | ı SGA | /12/2019- /11/2020 | ezi 7 | 3,600,( | 25,200,( |
| 5 | IKM | /06/2020- /6/2022 | vaka 1 | 3,000,( | 36,000,( |
| 6 | ı Cheju | /11/2020- /11/2022 | ezi 7 | 1,800,( | 12,600,( |
| 7 | A Security Services | /10/2020- | ezi 9 | 7,200,( | 64,800,( |
| **Jumla** | | | | | **196,200,(** |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji (ZAWA)**

Upatikanaji wa ulinzi huu haukua na mchakato isipokua Serikali hutoa agizo la vikosi kwenda kulinda pindi ikitokea dharua kama uchaguzi au hujuma. Mfano ni wa agizo la Mh Rais Mwinyi la kuvitaka Vikosi hivyo kwenda kulinda Bumbwisudi mwishoni mwa mwaka

2022 baada ya kutokea hujuma. Hata hivyo ZAWA inaendelea na kufuata taratibu za kimanunuzi kwa kampuni chache za kibinafsi inazofanya nazo kazi ikiwa ni pamoja na Zabuni ya ulinzi kwa vituo vya Mamlaka ya Maji Zanzibar visima vya Kiashange kwa kutoa Kotesheni kwa wazabuni watatu (3). Kiambatanisho D. NB: KMKM wameshaiarifu ZAWA kuwa kuwa kuanzia mwaka 2023 malipo yao yatakua 9,000,000/= kwa mwezi badala ya 3,000,000/= Deni la KMKM hadi sasa limefikia 351,000,000/= Deni la JKU hadi sasa limefikia shilingi kuanzia mwaka 2023 malipo yao yatakua 9,000,000/= kwa mwezi badala ya 3,000,000/= Deni la KMKM hadi sasa limefikia 351,000,000/= Deni la JKU hadi sasa limefikia shilingi 113,400,000

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kwamba ni kweli taratibu za kimanunuzi zimekiukwa kutokana na agizo lilitolewa na Serikali la kutaka maeneo ya vituo vya Mamlaka kulidwa na Vikosi vya SMZ kutokana na hujuma zilizokuwa zinafanyika katika maeneo hayo. Hata hivyo, Kamati imeshidwa kupatiwa kwa maandishi agizo hilo kwa ajili ya kujiridhisha zaidi,

Aidha, Kamati imebaini vituo hivyo vinalidwa na vikosi tofauti vinavyofanya kazi moja ya ulinzi kwa gharama tofauti ya kila kikosi kinacholipwa kwa mwezi jambo ambalo linapelekea hasara kwa Mamlaka kwa vile kulikuwa na uwezekano wa kuchagua kikosi kimoja tu kwa kulinda vituo vyote kwa makubaliano ya gharama sawa kwa vituo vyote kwa kila mwezi.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati haipingani na maagizo yanatolewa na Serikali kwa vile yanalenga kuleta maslahi kwa nchi. Hata hivyo, maagizo hayo wanapaswa pia kuambatanishwa kwa njia ya maandishi kama ni ushahidi wa utekelezaji wa husika kwa vile baadhi ya taasisi hutukeleza

jambo fulani kwa kukiuka taratibu mbalimbali za kisheria kwa kisingizio cha kuagizwa na viongozi wa Serikali.

Vile vile, Kamati inaishauri Mamlaka kutumia njia ya 'Single Source' kama ni agizo kwa Serikali kwa kutumia kikosi kimoja tu kwa ajili ya ulinzi wa vituo vyote vya Mamlaka tofauti na hali ya sasa ya kila kituo kinalidwa na kikosi tofauti na kila kikosi kinalipwa gharama tofauti kwa kazi zinazofanana za ulinzi kwa kila mwezi

### 5.2.16.7 Vifaa ambavyo havikuingizwa katika Daftari la Ghalani USD 224,100

Ukaguzi uliofanywa umebaini kwamba Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilinunua vifaa mbali mbali kutoka kwa Kampuni ya Rahisi Solution Limited lakini vifaa hivyo havikuweza kurikodiwa katika daftari la kuhifadhia vifaa vya ghalani ambapo kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma namba 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka, kufanya kazi za manunuzi kwa kuzingatia sheria kanuni pamoja na miongozo mbali mbali inavyoelekeza ikiwa ni pamoja kuweka kumbukumbu za vifaa mbali mbali vinavyonunuliwa. Vifaa ambavyo havikurekodiwa katika daftari la ghalani ni kama vifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 76 : Vifaa ambavyo havikurekodiwa katika daftari la ghalani**

| Namba | Vifaa | adi | i Cha Fedha SD) | la Ya Fedha SD) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | s Devices | | 6 | 31,2 |
| 2 | esktop Pos | | 7 | 7,6 |
| 3 | ell Server | | 14,7 | 29,4 |
| 4 | s Application (Client App) | | 42,0 | 42,0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | ckend Application (Billing) | | 65,0 | 65,0 |
| 6 | osk Pos Controller App (5 Years Lincence) | | 3 | 21,6 |
| 7 | wer Backup | | 12,4 | 12,4 |
| 8 | s Protection Covers | | | 9 |
| 9 | rver Cabinet 42u | | 1,2 | 1,2 |
| 10 | stem Initial Setup | | 5,6 | 5,6 |
| 11 | stem Users | | 3,5 | 7,0 |
| **Jumla** | | | | **224,1** |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

ZAWA inakiri kwamba vifaa vilivyoletwa na kampuni ya Rahisi Solution kwa ajili yaukusanyaji wa mapato havikuingizwa katika Daftari la Ghalani kwa sababu ya uharaka wamatumizi. Hata hivyo, ZAWA hivi sasa inasimamia kuingizwa katika Daftari la Ghalani vifaa vyote vinavyonunuliwa

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kutokea kwa dosari hiyo, Kamati inaungana na ushauri wa Mkaguzi wa kuitaka Mamlaka kufanya kazi za manunuzi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni pamoja na Miongozo mbali mbali inavyoelekeza ikiwa ni pamoja kuweka kumbukumbu za vifaa mbali mbali vinavyonunuliwa katika daftari la ghalani.

**5.2.16.8 Kuwepo kwa wafanyakazi walioajiriwa bila ya kibali kutoka Utumishi**

Ukaguzi uliofanywa umebaini kwamba Mamlaka ya Maji ZAWA iliajiri wafanyakazi wapya 22 kuanzia mwezi wa 3,4,5,8 na mwezi wa 9 kuanzia mwaka wa fedha 2019-2020 na 2020/2021 na kulipwa mshahara jumla ya shilingi 125,608,830 bila ya kupata kibali cha uajiri huo kutoka Utumishi mabapo ni kwenda kinyume na kifungu namba 7(4) cha kanuni

ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka, kufanya kazi kwa kuzingatia sheria kanuni pamoja na miongozo mbali mbali inavyoelekeza ikiwa ni pamoja kufuata utaratibu ulioelekezwa katika kufanya uajiri wa wafanyakazi wapya ili kuepusha uwezekano wa kuwepo kwa mgongano wa kimaslahi. Orodha ya wafanyakazi walio ajiriwa bila ya kibali ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 77 : Orodha ya wafanyakazi walio ajiriwa bila ya kibali**

| Jina | ehe ya kuajiriwa | Nafasi aliyoajiriwa | shahara Uliolip (Tshs) | zi ya malipo | Kiasi cha fedha zilizolipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| aha Yussuf Twaha | /08/2020 | uhandisi rasilimali ji | 593,( | 11 | 6,523,( |
| mada Nassor Juma | /08/2020 | sa mdhibiti mader | 501,! | 11 | 5,516,! |
| ma Rajab Mbarouk | /08/2020 | sa manunuzi | 593,( | 11 | 6,523,( |
| amis Nassor Moh'D | /09/2020 | ndi mchundo ume | 484,7 | 10 | 4,847,8 |
| assoud Ramadhan mada | /05,2020 | sa manunuzi na avi | 593,( | 14 | 8,302,( |
| med Juma Haji | /03/2020 | sa mdhibiti mader aidizi | 501,! | 16 | 8,024,( |
| di Haroub Moh'D | /03/2020 | sa mdhibiti mader aidizi | 501,! | 16 | 8,024,( |
| ur Shaaban Ameir | /03/2020 | sa mdhibiti mader aidizi | 501,! | 16 | 8,024,( |
| hura Hashim Salum | /03/2020 | tib mukhtasi | 593,( | 16 | 9,488,( |
| sra Rajab Salum | /03/2020 | sa mtabibu maji | 501,! | 16 | 8,024,( |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | aidizi | | | |
| kungu Handu Haji | /03/2020 | sa mtabibu maji aidizi | 501,5 | 16 | 8,024,0 |
| eid Mussa Suleiman | /03/2020 | sa buhusian 0 | 593,0 | 16 | 9,488,0 |
| tma Tahir Hussein | /03/2020 | sa manunuzi na gavi | 593,0 | 16 | 9,488,0 |
| ania Salum Nassor | /04/2020 | sa mtibabu maji | 593,0 | 15 | 8,895,0 |
| ey Ali Aley | /03/2020 | ndi mchundo imamizi maji | | | Hakuoneka |
| yyana Seif Mansor | /03/2020 | uhandisi usambaza ji | | | Hakuoneka |
| Moh'D Hamad | /03/2020 | ndi mchundo ambazaji maji | | | Hakuoneka |
| dulkarim Ali Faki | /03/2020 | ndi mchundo ume | | | Hakuoneka |
| am Nassor Ali | /03/2020 | sa mipango | | | Hakuoneka |
| san Ali Suleiman | /04/2020 | sa uhusiano | 593,0 | 15 | 8,895,0 |
| fidhi Abdalla Ali | /04/2020 | ndi mchundo kenika | 501,5 | 15 | 7,522,5 |
| ula Haji Haji | /04/2020 | uhandisi rasilimali ji | 593,0 | 15 | 8,895,0 |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Hadi mkaguzi anamaliza ukaguzi ni kweli bado mjadala wa taratibu za uajiri wa wafanyakazi hao 22 ulikua ukiendelea Serikalini ingawa kwa sasa tayari waajiriwa hao wameshapata kibali cha ajira zao kutoka Wizara ya Utumishi. Kiambatanisho cha barua CCB.213/08/01/09. Angalia pia. Kiambatanisho cha mikataba ya ajira hizo

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati haikuona haja ya kuendelea na hoja hii kwa vile taratibu zote zimeshakamilishwa za uajiri wa watumishi hao ikiwa ni pamoja na kupatiwa kibali kutoka kwa Wizara ya Nchi, (AR), Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Hata hivyo, Kamati inaishauri Mamlaka kuhakikisha wanakamilisha taratibu zote za kiutumishi kabla ya kuajiri watumishi wapya ili kuepusha dosari kama hizi kujitokeza tena.

**5.2.16.9 Malipo ya posho la mafuta kwa Wakurugenzi 6 wasiostahiki jumla ya 102,672,000**

Kwa mujibu wa toleo la malipo ya Wakurugenzi wa nafasi za uteuzi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi linaloeleza kwamba Wakurugenzi wanaoteuliwa na Mh. Rais wanapaswa kulipwa kiwango cha malipo ya posho la mafuta.

Ukaguzi uliofanywa umebaini kwamba Mamlaka ya Maji ZAWA imewalipa posho la mafuta jumla ya Tzs 8,555,000 kwa mwezi Wakurugenzi wake 6 wa ndani ambao sio wateuliwa wa nafasi za Mh.Rais.

Kuwalipa posho la mafuta Wakurugenzi ambao sio wateuliwa wa nafasi za Mh. Rais ni kwenda kinyume na toleo la malipo ya Wakurugenzi. Orodha ya Wakurugenzi waliolipwa posho la mafuta kinyume na sheria ni kama wafuatao:-

**Jadweli Nambari 78 : Malipo ya posho la mafuta kwa Wakurugenzi 6 wasiostahiki**

| Namba | Jina | Cheo | ɿo ya posho | Miezi aliyolipw | ıla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ssan Juma Ali | ɩurugenzi wa ndani | 1,426,( | 12 | 17,112,( |
| 2 | ıar Bakari Mshindo | ɩurugenzi wa ndani | 1,426,( | 12 | 17,112,( |
| 3 | ɀija Mussa Mshibe | ɩurugenzi wa ndani | 1,426,( | 12 | 17,112,( |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | ıulid Hassan Khamis | ɾurugenzi wa ndani | 1,426,( | 12 | 17,112,( |
| 5 | ssan Khamis Hassan | ɾurugenzi wa ndani | 1,426,( | 12 | 17,112,( |
| 6 | ›hamed ILyasa Moham | ɾurugenzi wa ndani | 1,426,( | 12 | 17,112,( |
| **Jumla** | | | | | **102,672,(** |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji ZAWA**

Wakurugenzi wa Mamlaka ya maji ZAWA walikuwa wanalipwa posho la mafuta katika mshahara wa kila mwezi ambayo posho hiyo ilitokana na Maamuzi ya BODI ya Wakurugenzi ya ZAWA kupitia kikao chake cha Disemba 2013 huko hoteli ya Tibirinzi Pemba ambapo pamoja na mambo mengine ilipitisha posho ya mafuta kwa wakurugenzi wake wa ndani. Msingi wa kufanya hayo ilikuwa ni kifungu cha 14(f) cha Sheria ya Maji ya Mwaka 2006 kilichoipa Bodi hiyo Mamlaka ya kuidhinisha posho na mishahara ya wafanyakazi wa ZAWA. Aidha, toleo ililonukuliwa katika katika hoja halikukataza Bodi kutoamuru kulipwa

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kujadili hoja hii inaona ni vyema kuishauri Serikali kuandaa muongozo maalum utakasaidia kutoa maalekezo mahsusi kwa baadhi ya matumizi ya fedha yanayoidhinishwa na Bodi ili bodi ziweze kutekeleza shughuli zake kwa uwazi na ufanisi mkubwa bila ya kukuika taratibu na masharti ya matumizi ya fedha za Serikali.

**5.2.61.10 Kulipwa mshahara kwa mfanyakazi alieacha kazi kwa hiari**

Mnamo tarehe 28/09/2020 Mamlaka ya Maji ZAWA ilipokea barua kutoka kwa mfanyakazi wake Nd. Seif Said Juma yenye kichwa cha habari kuacha kazi kwa hiari.

Kumbukumbu zinaonyesha kwamba mtumishi huyo alirejesha mshahara wa mwezi huo kupitia risiti namba BJK280920200044 ya 28/09/2020 yenye jumla ya shilingi 428,000 kwa mujibu wa sheria na kanuni za Utumishi.

Ukaguzi uliofanywa umebaini kwamba licha ya mtumishi huyo kuacha kazi, mwezi uliofuata wa Oktoba alilipwa mshahara wake kamili. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni ya Utumishi wa Uma nambari 11 ya mwaka 2011.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji  Zanzibar (ZAWA)**

Wakurugenzi wa Mamlaka ya maji ZAWA walikuwa wanalipwa posho la mafuta katika mshahara wa kila mwezi ambayo posho hiyo ilitokana na Maamuzi ya BODI ya Wakurugenzi ya ZAWA kupitia kikao chake cha Disemba 2013 huko hoteli ya Tibirinzi Pemba ambapo pamoja na mambo mengine ilipitisha posho ya mafuta kwa wakurugenzi wake wa ndani. Msingi wa kufanya hayo ilikuwa ni kifungu cha 14(f) cha Sheria ya Maji ya Mwaka 2006 kilichoipa BODI hiyo Mamlaka ya kuidhinisha posho na mishahara ya wafanyakazi wa ZAWA. Aidha, toleo lililonukuliwa katika katika hoja halikukataza Bodi kutoamuru kulipwa

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa ni kweli mtumishi huyo ameshaurejesha mshahara huo na Kamati imeridhika kwa kupatiwa risiti inayoonesha kurudishwa kwa mshahara huo.

Hata hivyo Kamati inaishauri Mamlaka kuwa makini katika kutekeleza majukumu yake kwa kufuata Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo

**2.2.16.11 Kukosekana kwa ukaguzi wa magari 15 yanayomilikiwa na Mamlaka ya Maji**

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna jumla ya gari 15 zinazomilikiwa na Mamlaka ya Maji lakini hadi ukaguzi unakamilika gari hizo hazikuonekana kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka, kufanya kazi kwa kuzingatia sheria kanuni pamoja na miongozo mbali mbali inavyoelekeza ikiwa ni pamoja na kufuata utaratibu ulioelekezwa

katika uwasilishwaji wa taarifa na mali zinazomilikiwa na Mamlaka kwa ajili ya ukaguzi.

**Jadweli Nambari 79 : Gari ambazo hazikuonekana wakati wa ukaguzi**

| mba | na ya Chombo | mba ya Gari | bila ya Gari | ara inayopatikana |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ri | S 198 B | yota Town Ace | undi |
| 2 | ri | S 202 A | yota Town Ace | undi |
| 3 | ri | S 190 B | yota Hilux | undi |
| 4 | ri | S 225 B | yota Hilux | undi |
| 5 | ri | S 166 B | ssan Hard Bod | undi |
| 6 | ri | IZ 5362 | yota Land Cruiser | undi |
| 7 | ekcta | IZ 5319 | lment 604 | undi |
| 8 | di | P | ssan Hard Bod | undi |
| 9 | ri | S 159 A | ado | dha |
| 10 | ri | S 176 A | zuki Scudo | dha |
| 11 | ri | S 160 A | ssan Caravan Min Bus | ashara |
| 12 | ri | S 169 B | ssan Hard Bod | ashara |
| 13 | ri | S 151 B | ssan Hard Bod | Maji |
| 14 | ri | S 175 A | V Honda | Maji |
| 15 | ri | S 158 A | zuki Vitara | Maji |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Magari hayo yalichukuliwa na Afisi ya Rais Ikulu na kuwekwa Katika Afisi ya ZAECA ambapo

hatimae yaliuzwa na fedha iliingia mfuko mkuu wa Serikali na mengine kugawiwa katika Idara nyengine za Serikali. Kiambatanisho kinafafanua.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kukosekana kwa utaratibu wa kisheria wa kuhamisha mali za Serikali kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyengine bila ya idhini ya wahusika wenyewe ambao ni Mamlaka ya Maji

Kamati inashauri taasisi za Serikali kufuata taratibu, kanuni na miongozo iliyopo ya kuhamisha mali kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyengine kwa lengo la kutambua msimamizi halali wa mali hizo kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi wa mali wakati wa ukaguzi unapofika, aidha Kamati inaishauri Mamlaka kuonana na uongozi wa Wizara ya Fedha kupitia Msajili wa hazina kwa kuziondoa gari hizo katika mali za Mamlaka kwa mujibu taratibu za kisheria kwa vile hawana tena umiliki wa mali hizo.

### 5.2.16.12 Kutokuripotiwa kwa matumizi sahihi ya bajeti ya ofisi ya Pemba kwenye hesabu ya mwisho wa mwaka shilingi 3,741,805,000

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021, imebainika kujitokeza kwa tofauti ya shilingi 3,741,805,000 kwenye hesabu ya mwisho wa mwaka wa fedha 2020/2021 iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Ukaguzi umebaini Mamlaka ya Maji (ZAWA) – Pemba ilipangiwa kutumia jumla ya shilingi 2,237,764,246, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuripotiwa matumizi yenye jumla ya shilingi 5,979,569,246 kwenye bajeti ya matumizi ya Pemba jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa tofauti ya shilingi 3,741,805,000 na kupelekea hesabu ya mwisho wa mwaka ya ZAWA kutokuonesha sura halisi na sahihi.

Kuwasilishwa kwa hesabu zilizofungwa ambazo hazikuakisi vigezo vya ufungwaji wa hesabu

ni kwenda kinyume na miongozo ya utayarishaji na ufungaji wa hesabu ya kitaifa na kimaitafa pamoja na kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Maji (ZAWA) kufanya usuluhishi wa hesabu zake kabla ya kufunga hesabu na kuziwasilisha kwa ajili ya ukaguzi. Aidha, ukaguzi unashauri kuweza kufanyika kwa marekebisho ya taarifa za hesabu pale inapobainika kujitokeza kwa tofauti ya miamala ya fedha iliyoripotiwa ili hesabu hiyo iweze kuakisi vigezo vya ufungaji wa hesabu vilivyowekwa na kukubalika kitaifa na kimataifa na hatimae kuiwasilisha hesabu hiyo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kukaguliwa na kutolewa maoni ya ukaguzi.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji  Zanzibar (ZAWA)**

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imefuatilia tatizo hilo la kuripotiwa kwa Fedha za Bajeti ya Matumizi tu. Jumla TZS 2,237,764 264 na Pia walitakiwa Pembawaripoti fedha zote za bajeti zilopangwa zikiwa bajeti ya umeme na bajeti ya Maendeleo ya Miundo mbinu. Jumla ya TZS 3,741,805,000. Hata hivyo tumerekebisha tatizo hilo na kwa sasa Idara ya Fedha inafanya uhakiki wa bajeti

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imeelezwa kwamba maelezo aliyopewa Mkaguzi kwa upande wa Pemba hayakuwa sahihi kutokana na hesabu hiyo kutojumuishwa na mapato ya ruzuku pamoja na mapato ya umeme kwa upande wa Pemba kulikosababishwa na mtoa maelezo hayo hakuwa mtu sahihi na si mwenye jukumu hilo, Kamati ilijumuisha hesabu hizo na kujirizisha kuwa kulikuwa na makoseo ambapo bajeti ya miundombinu pomoja na umeme yenye thamani ya Jumla ya Tsh 3,741,805,000 hazikuingizwa kwenye hesabu ya matumizi alizopewa mkaguzi kwa upande wa Pemba.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Mamlaka kuwa makini wakati wanapotoa majibu ya hoja kwa mkaguzi kwa kutoa majibu yenye uhalisia, aidha uongozi wa Mamlaka ichukue jitihada ya kuyapitia majibua yote ya hoja kabla ya kuwasiliswa kwa mkaguzi kwa lengo la kujiridhisha usahihi wa majibu wanayotoa.

**5.2.16.13 Dosari iliyobainika katika manunuzi ya POS na vifaa vyengine vya kielektroniki vyenye thamani ya USD 224,110**

Katika ukaguzi uliofanyika imebanika kwamba Mamlaka ya Maji ZAWA ilinunua mashine za kukusanyia mapato POS (Point of sales) na vifaa vyengine vya kielektroniki kutoka kwa Kampuni ya Rahisi Solution Limited kwa thamani ya USD 224,110 na kupelekea uwepo wa dosari zifuatazo:-

- Kukosekana kwa kumbukumbu za muhtasari wa kikao cha bodi ya Zabuni kilichopitisha manunuzi hayo.
- Kutokuwepo kwa tangazo la zabuni lililofanyika kwa ajili ya manunuzi hayo
- Kukosekana kwa ripoti ya kamati ya tathmini.
- Kukosekana kupatiwa taarifa ya idhini ya matumizi ya mkataba huo pamoja na maelekezo kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa kifungu 27(3) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma ya mwaka 2016.

Kukosekana kwa taarifa hizo kumetia shaka juu ya uhalali wa manunuzi yaliyofanyika kama yameakisi kanuni, miongozo na sheria zilizopo, kufanya hivyo kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar, kufanya kazi kwa kuzingatia sheria kanuni pamoja na miongozo mabli mabli ikiwa ni pamoja na kufuata kikamilifu sheria ya Ununuzi na uondoaji wa mali za Umma.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Mamlakaya Maji (ZAWA) haikununua vifaa hivyo moja kwa moja isipokuwa mwaka

2018, ZAWA ilitaka kuingia mkataba wa ushirikiano na kampuniya ZANZIBAR CONNECTIONS COMPANY LIMITED (Comnet) katika kazi ya kukusanya ada za malipo ya maji. Aidha, ZAWA ilikopa vifaa kutoka kampuni ya ZANZIBAR CONNECTIONS COMPANY LIMITED (Comnet) ambayo tayari ilikuwa na vifaa hivyo vya kukusanyia mapato. ZAWA iliwataka iwapatie vifaa hivyo kwa njia ya mkopo kwa ajili ya kuendelea na mradi huo wa kukusanya mapato na baadae ZAWA kulipa kidogo kidogo kwa kadri ya upatikanaji wa makusanyo ya malipo ya maji kupitia vifaa hivyo kama ilivyoainishwa katika Mkatabawa mkopo huo wa vifaa na huduma. Katika kusaini mkataba huo wa mkopo wa vifaa hivyo, ZAWA iliingia mkataba na Kampuni ya RAHISI SOLUTION LTD kwa sababu kampuni hiyo ya ZANZIBAR CONNECTIONS COMPANY LIMITED (Comnet)iliitarifu ZAWA kuwa kutokana na majukumu makubwa ya kazi katika Kampuni hiyo ya ZANZIBAR CONNECTIONS COMPANY LIMITED (Comnet),tayari wameunda kampuni nyengine inayojulikana kwa jina la RAHISI SOLUTION LTD inayoshughulikiamasuala ya “software development” peke yake ambayo ndio itakayokuwa na wajibu wakuingia mkataba waulipaji wadeni hilo badala yakuingia mkataba na Kampuniya ZANZIBAR CONNECTIONS COMPANY LIMITED (Comnet) ambapo kwa wakati huoilikuwa imepewa jukumu la kushughulikia “internet service provider. Hatahivyo, ZAW Ailiendelea kukusanya mapato kwa ufanisi kulinganisha wakatiwa kabla ya matumizi ya vifaa hivyo na mapato yaliongezeka baada ya wananchi kupata mwamko mkubwa wakulipia

maji na wakati huohuo kupata risiti ya elektroniki na kuthibitisha malipo ya majina madeni yaliosalia kwa upande wa Watumiaji. Pia kwaUongoziulikua n wasaa mzuri kuona mwenendo wa mapato kupitia mtandao wakati huo huo unapofanyika miamala ya fedha zinazokusanywa Zoezi hilo lilendelea na njia mbadala waukusanyaji wa mapatowa ZAN Malipo. ZAWA inaendelea kufanyamanunuzi kwa kuzingatia kanunina hadi pale Serikali Kuu ilipokuja Sheria.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na majibu hayo, Kamati imebaini kikuikwa kwa taratibu za kisheria katika ununuzi wa vifaa hivyo, Kamati inaungana na ushauri ulitolewa na Mkaguzi wa kuitaka Mamlaka ya Maji Zanzibar, kufanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni pamoja na Miongozo mabli mabli ikiwa ni pamoja na kufuata kikamilifu Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma.

**5.2.16.14 Ucheleweshwaji wa mapokezi ya vifaa vya kusambazia maji shilingi 392,101,020**

Mamlaka ya Maji Zanzibar imefunga makubaliano ya mkataba mdogo (Addendum) na kampuni ya African Power Machinery Tz. Ltd ya Dar es Salaam uliosainiwa tarehe 16/04/2021 wenye thamani ya shilingi 392,101,020 kwa ajili ya kupatiwa vifaa mbali mbali vya kusambazia maji kwa njia ya mkopo ambavyo vilitegemewa kupokewa ndani ya wiki kumi (10) kwa mujibu wa mkataba.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kuchelewa kuwasilishwa na kupokelewa kwa vifaa hivyo ikiwemo pampu za maji 12, Mota 3 na Compressor 2 kwa wastani wa muda wa miezi minne (4) na kuendelea jambo ambalo limepelekea kuathiri malengo ya Mamlaka waliyojipangia kuweza kuwapatia huduma za maji safi na salama wananchi wa Zanzibar kwa wakati na kupelekea uwepo wa malalamiko na changamoto kutoka kwa wananchi wa

Zanzibar.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka, kufanya juhudi ili kuhakikisha kwamba kila kifaa kinachonunuliwa kinapokelewa na kinasambazwa katika eneo husika kwa muda sahihi uliopangwa ili kuepusha athari ya kukosekana kwa huduma ya maji safi na salama katika eneo husika kwa lengo la kupunguza malalamiko kwa wananchi.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

ZAWA ilifanya kikao na Kampuni ya African Power Machinery Ltd kujadili ucheleweshaji wa vifaa hivyo ikiwemo utaratibu wa makato kwa vifaa vilivyocheleweshwa na kufikia makubaliano ya makato kama inavyojieleza kwenye Kiambatanisho B.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imeelezwa vifaa hivyo vilitakiwa kusafirishwa kwa njia ya meli badala yake wakafanya 'addendum' kwa ajili ya kusafirisha vifaa hivyo kwa njia ya ndege jambo ambalo lilichukua muda wa kuwasili kwa vifaa hivyo ila hadi Kamati ilipofanya ukaguzi wake vifaa hivyo tayari vimeshawasili.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Mamlaka kuwa makini katika ufungaji wa mikataba na makampuni mbalimbali ya usambazaji wa vifaa kwa kujirizisha ufanisi na utendaji kazi wao Aidha kusimamia vyema mikataba hiyo kwa kutoza faini husika iliyomo ndani ya mkataba iwapo masharti ya mkataba yatakiukwa kama vile ucheleweshaji wa vifaa kwa muda uliopangwa ndani ya mkataba husika

**5.2.16.15 Kutokulipwa kwa malipo ya fidia shilingi 98,809,457.04**

Ukaguzi uliofanywa umebaini kwamba Mamlaka ya Maji ZAWA ilipaswa kulipwa fidia kutoka Kampuni ya African Power Machinery Tz Ltd yenye jumla ya shilingi 98,809,457.04 kutokana na Kampuni hio kushindwa kuwasilisha Compressor mbili zilizonunuliwa kwa

wakati na kupelekea ucheleweshwaji wa siku 126 ambapo kwa mujibu wa makubaliano yaliomo kwenye General Condition of Contract gharama kwa siku iliyocheleweshwa ni 0.2 kutoka thamani halisi ya vifaa vilivyonunuliwa ambayo ni shilingi 392,101,020.

Kushindwa kudai malipo ya fidia kwa mzabuni huyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na tozo ya adhabu ya kuchelewa kuwasilisha vifaa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa zabuni jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu 25.1 cha General Condition of Contract.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka, kufanya juhudi katika kufuatilia malipo yatokanayo na fidia ili kuongeza kiwango cha mapato ya mamlaka kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wote wa zanzibar.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Mamlaka ya Maji Zanzibar baada ya ucheleweshwaji wa vifaa hivyo ilipeleka barua kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata muongozo na ushauri juu ya kadhia hiyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilitutaka kufanya Kikao cha pamoja baina ya ZAWA na Kampuni ya African Power Machinery ili kutatua jambo hilo. Kiambatanisho A kinahusika. ZAWA ilifanya mawasiliano na Kampuni ya African Power Machinery Ltd na kuwataarifu juu ya kuchelewesha vifaa hivyo na makato ambayo ZAWA wanatakiwa kuyakata kwa Kampuni hiyo juu ya ucheleweshaji huo. Baada ya kikao kilichofanyika baina ya ZAWA na Kampuni ya African Power Machinery kampuni hiyo licha ya kutoa sababu zilizopelekea ucheleweshaji wa vifaa hivyo pia ilikubali kukatwa kiasi cha shilingi 35,260,612.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati iliomba kupatiwa barua iliyowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa lengo la kujiridhisha na barua hiyo iliwasilishwa mbele ya Kamati yenye Kumb kumb LD/901/Vol.III/35 ya kuomba kupatiwa ushauri kwa Mwanasheria Mkuu.

Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka kuwa makini katika kutafuta wasambazi wazuri wa vifaa wenye weledi na ufanisi wa kazi zao ili dosari kama hizo zisiweze kujitokeza tena kwani ucheleweshaji huo unaviza jitihada za Mamlaka katika kuwapatia huduma bora wananchi za upatikanaji wa maji safi na salama.

**5.2.16.16 Kukiukwa kwa taratibu za manunuzi za mashine (Mota) nane (8) zenye thamani ya shilingi 107,163,900**

Mamlaka ya Maji ZAWA ilifanya manunuzi ya Mota nane zenye thamani ya shilingi 17,043,478.26 zilizolipwa kwa mujibu wa hati ya malipo namba 7/3 ya tarehe 25/3/2021 kwa mzabuni DJN KIRENGA GENERAL SUPPLY CO. LTD.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi ikiwemo kujitokeza kwa dosari zifuatazo:-

Kukosekana kwa kumbukumbu za muhtasari wa kikao cha bodi ya Zabuni kilichopitisha manunuzi hayo.

Kutokuwepo kwa tangazo la zabuni lililofanyika kwa ajili ya manunuzi hayo

Kukosekana kwa ripoti ya kamati ya tathmini.

Kukosekana kupatiwa taarifa ya idhini ya matumizi ya mkataba huo pamoja na maelekezo kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mujibu wa kifungu 27(3) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma ya mwaka 2016.

Kukosekana kwa taarifa hizo kumetia shaka juu ya uhalali wa manunuzi yaliyofanyika kama yameakisi kanuni, miongozo na sheria zilizopo, kufanya hivyo kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar, kufanya kazi kwa kuzingatia

sheria kanuni pamoja na miongozo mabli mabli ikiwa ni pamoja na kufuata kikamilifu sheria ya Ununuzi na uondoaji wa mali za Umma.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji  Zanzibar (ZAWA)**

Mamlakaya Maji ilifanya manunuzi ya mota nane (8) kwa njia ya “Emergency Procurement” ilikuharakisha upatikanaji wa maji katika maeneo ambayo yalionekana na uhaba mkubwa wa maji, Mamlaka ilipeleka barua Kwenda Ofisiya nRais Fedha na Mipango kuomba ruhusa ya kutumia njia hiyo. Kiambatanisho E kinaeleza. Hata hivyo kwa kutambua umuhimuwa huduma na hali ya kifedha kwa ZAWA ilikua mbaya sana na mahitaji yalikua makubwa yaliyotokana na ukoesefu mkubwa kwa baadhi ya watumiaji huduma kwa maeneo yaliyopelekea ZAWA kwa kushaurianana Mh Waziri wakati huo kuomba kupata machine hizo kwa njia ya mkopo kwa wale walokua tayari kuikopesha ZAWA wakati huo na ambae alikua na machine hizo katika ghala yake kwa wakati huo ni kampuni moja pekee ambayo ilikubali kuikopesha ZAWA machine zenye thamani hio ambazo hadi Leo hajapatiwa malipo yake na machine zikiendelea kutoa huduma maeneo mbali mbali kama yalivyoainishwa katika Invoice ya machine hizo ndani ya mkataba husika wa mkopo huo. ZAWA imeyapokea mapendekezo naushauri juu ya kufuata kanuni na sharia za manunuzi za nchi katika kutekeleza majukumu yake yakila siku.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini kutokamilishwa kwa baadhi ya taratibu za manunuzi zilizotumika kwa njia ya “Emergency Procurement” ilikuharakisha upatikanaji wa huduma ya  maji katika maeneo mbali mbali. Hata hivyo, Kamati inashauri kulipwa fedha zote za mtoa huduma ambae ametoa mashine hizo kwa mkopo ili haki iweze kutendeka kwa vile Mamlaka imekiri kupokea na kutumia mashine hizo.

### 5.2.16.17 Kuwepo kwa Visima 33 vilivyoshindwa kutoa huduma ya maji

Mamlaka ya Maji Zanzibar ina jukumu la kuhakikisha linatoa huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar wakati wote. Ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya Maji inamliki visima 172 kwa upande wa Unguja ambapo kati ya visima hivyo jumla ya visima 139 vinafanya kazi na kutoa huduma ya usambazaji wa maji safi na salama wa wananchi mbali mbali wa maeneo ya Unguja.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni uwepo wa visima 33 ambavyo vimekabiliwa na changamoto mbali mbali na kupelekea kutokufanya kazi kwa muda mrefu jambo ambalo limeongeza uwepo wa malalamiko kwa baadhi ya maeneo ya Zanzibar kutokupata maji kikamilifu na baadhi ya maeneo mengine kuwa na mgao wa maji au kutokupata maji kabisa jambo ambalo limepelekea wananchi wa Zanzibar kupaza sauti zao kwenye vyombo vya habari na kutoa malalamiko ya kutokupatikana kwa huduma ya maji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji kuongeza jitihada za kupambana na kupunguza changamoto zinazojitokeza mara kwa mara kwa baadhi ya maeneo ya Zanzibar ikiwemo kuwa na Mfuko wa Dharura wa kukabiliana na maafa yatokanayo na vitendo vya hujuma ya mifumo ya maji ili kuhakikisha huduma hiyo haisiti kwa wananchi. Mchanganuo wa visima 33 vilivyokuwa havifanyi kazi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 80 : Visima 33 vilivyoshindwa kutoa huduma ya maji kwa upande wa Unguja**

| Namba | laya | Visima vyote | Idadi ya Visima ambavyo vifanyi kazi | eneo ya Visima |
|---|---|---|---|---|
| 1 | skazinii A | 25 | | ADB NO.4<br>Chaani Tassaf<br>ADB 3 Kiashange |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | skazini B | 21 | | Donge Mbiji ndani<br>Kinduni<br>Donge Mbiji nje |
| 3 | ti | 26 | | Kwambani<br>Miwani<br>ADB Kinyongo<br>Bambi Mpapa |
| 4 | Kusin | 18 | 5 | Makunduchi Kilimo<br>Bwejuu<br>Kizimkazi Pangoni<br>Mfumbwi<br>Kivuli #2 |
| 5 | Magh<br>A | 38 | 10 | Chemani N9-2<br>Machui N8<br>Welezo 66<br>Welezo 64<br>Kizimbani N4<br>Kizimbani RAK- 2ADB<br>Bumbwisudi NB 1<br>Bumbwisudi NB 6<br>Bumbwisudi Ghana<br>Bumbwisudi N 8 |
| 6 | Magh<br>B | 26 | 3 | Chunga 26<br>Dimani<br>Mbweni Matrekta |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7 | Mjini | 17 | 5 | Sebleni SEMUSO<br>Sebleni kwa wazee -1<br>Chumbuni Solar<br>Chumbuni RAK<br>Turkey |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Kutokana na kuharibika kwa pampu maeneo mbali mbali ya visima vyenye kuwahudumia wananchi wa Unguja na Pemba. ZAWA inaendeleza juhudi za kupatikana kwa pampu ili kurudisha huduma ya maji safi na salama kwa Wananchi. Miongoni mwa juhudi hizo, ZAWA imenunuwa pampu kupitia fedha za Uviko-19 kwa lengo la kurudisha huduma

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hiyo inayotokana na kuharibika kwa pampu za maji katika maeneo mbalimbali ya visima vinavyohudumia watu, Kamati inaishauri Mamlaka kuendelea kukchukua jitihada za kufunga pampu mpya katika visima hivyo ili hudma ya maji iendelee kupatikana katika maeneo mbalimbali ya mji wa Zanzibar

**5.2.16.18 Kuwepo kwa Matenki ambayo hayatumiki (Mabovu)**

Ukaguzi uliofanywa umebaini kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo yamewekwa matenki ya kuhifadhia maji kwa ajili ya kuwasambazia Wananchi lakini matenki hayo hayafanyi kazi kwa muda mrefu jambo ambalo ni kinyume na malengo ya mamlaka ya maji katika utoaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wote wa Zanzibar na kujitokeza uwepo wa malalamiko kwa wananchi.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kujitokeza kwa malalamiko kwa wananchi kutokana na

kukosa kwa huduma ya maji kwa muda mrefu ama kwa kutokuwepo kwa matenki ya kuhifadhia maji katika maeneo yao au kutofaidika na huduma ya maji kutokana na kwamba matenki yaliyowekwa katika maeneo yao yanatumika kusambazia maji katika maeneo mengine ya jirani.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji kuhakikisha inakuwa na miundombinu imara ya kusambaza maji na kukabiliana na majanga yoyote yanayoweza kutokezea ili kuhakikisha huduma hiyo inaendelea kupatikana kwa wakati wote.

**Jadweli Nambari 81: Matenki ambayo hayafanyi kazi iliyokusudiwa**

| Namba | eo liliopo Tanki | Vifaa | a ya Tanki | | o wa tenki | fadhili |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | elezo | ground | eel | | 450m3 | Z |
| 2 | uso- 1 | derground | ncrete | | 50m3 | Z |
| 3 | le Old | derground | ncrete | | 100m3 | Z |
| 4 | imbani Old | ground | ncrete | | | Z |
| 5 | mbwisudi | ground | P | | 250 | DB |
| 6 | fenesini | m ST. Tower | eel | | 225 | RA |
| 7 | fenesini Old | m ST. Tower | eel | | 225 | Z |
| 8 | ngwi | m Con. Tower | p | | 250 | Z |
| 9 | zari | derground | ncrete | | 150 | Z |
| 10 | kwajuni | m ST.Tower | eel | | 225 | Z |
| 11 | aani- 1 | m ST. Tower | eel | | 22 | INA |
| 12 | ahonda Booster | derground | ncrete | | 20 | Z |
| 13 | ope | ground | eel | | 50 | Z |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 14 | akunduchi | m ST. Tower | eel | | 22 | IINA |
| 15 | timkazi | m ST. Tower | eel | | 150 | 1Z |
| 16 | uyuni B | m ST. Tower | eel | | 225 | 1Z |
| 17 | inga | m ST.Tower | eel | | 225 | 1Z |
| 18 | genihaji | m Con. Tower | RP | | 48 | 1Z |
| 19 | achui | m ST. Tower | eel | | 22 | IINA |
| 20 | twachani | m Con Tower | RP | | 75 | 1Z |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Kutokana na uchakavu wa Matangi ya kuhifadhia maji maeneo mbali mbali, ZAWA imeyafanyia uchunguzi matangi hayo na kuona ya kwamba hayafai kutumika kutokana na muda wa "Material" yaliyotumika yamepita muda wake [Life time Expired]. Hata hivyo; ZAWA imeshawasilisha matangi hayo Wizara ya Fedha kwa lengo la kufanyika tathmini na kuuzwa, hatua ambayo imeshakamilika na tayari matangi hayo yameshauzwa

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati haikuona haja ya kuendelea na hoja hii kwa vile hatua zimeshachukuliwa za kuyauza matangi hayo. Hata hivyo, Kamati imeelezwa kuwa Mamlaka imeshajenga matangi mapya 25 kwa upande wa Unguja na Pemba hivyo Kamati inaishauri Mamlaka kuendelea kukamilisha ujenzi wa matangi hayo katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar kwa lengo la kuboresha usambazi wa maji kwa wananchi.

**5.2.16.19 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na tozo ya malipo ya visima binafsi shilingi 63,650,000**

Kwa mujibu wa kifungu cha 31 (1) cha Sheria Nambari 4 ya Mamlaka ya Maji Zanzibar ya mwaka 2006 kimeipa uweza wa kukusanya mapato yatokanayo na huduma ya maji kwa

wateja wa aina mbali mbali kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya Visima 1646 vimesajiliwa katika mfumo wa mapato wa Mamlaka ya Maji kupitia Idara ya Rasilimali Maji ambapo kwa kipindi cha mwaka wa fedha

2020/2021 imebainika jumla ya visima 373 vimefanya malipo yatokanayo na huduma za maji yenye thamani ya shilingi 18,620,000 sawa na asilimia 23.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa mapato yenye thamani ya shilingi 63,650,000 yanayotokana na kushindwa kukusanywa kutoka katika visima 1273 jambo ambalo limepelekea baadhi ya huduma kutotekelezeka kwa wakati kutokana na uchache wa fedha za makusanyo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha unachukuwa jitihada za makusudi katika kusimamia vyanzo vyake vya mapato kwa lengo la kuongeza kiwango cha makusanyo na kuendelea kutoa huduma bora kwa jamii.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

**1.** Ni kweli kwamba lipo tatizo la kukusanya mapato kupitia visima kwa sasa Idara ya Rasilimali Maji imeandaa mkakati kwa kupeleka bili za visima kama inavyofanyika kwa wanaotumia huduma ya maji ya ZAWA ili mwananchi aweze kujua deni lake na kuweza kulipa, ambapo bili hizo zitatolewa kwa kupitia mfumo wa malipo.

2. Kupitia 'survey' inayofanywa kwa kushirikiana na Shirika la UNICEF ambayo Idara ya Rasilimali Maji ikishirikiana na Idara ya Biashara imeandaa ziara ya kupitia maeneo ambayo watu wanatumia visima (waliosajiliwa na wasiosajiliwa) na kuweza kuwashajihisha juu ya ulipaji wa visima

3. Kuendelea na zoezi la utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya dhana ya kufuata taratibu za

uchimbaji wa visima, kupitia zoezi hili wananchi wamehamasika kuja kujisajili na mpaka kufika 30 Septemba 2022 idadi ya wamiliki wa visima wapatao 1800 wamesajiliwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kuwep kwa dosari hii na kuna juhudi zinaendelea kuchukuliwa na Mamlaka ili kuvisajili visima binafsi na viweze kutoa tozo ulipangwa kwa mujibu wa sheria, Kamati inaishauri Mamlaka kuongeza kasi ya kufanya Survey na kusajili visima vyote binafsi na kuanza kukusanya tozo katika visima hizo kwa lengo la kuongeza mapato ya Mamlaka.

**5.2.16.20 Upotevu wa fedha za makusanyo shilingi 927,682,692.71**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Maji (ZAWA) imefanya makusanyo ya fedha yenye thamani ya shilingi 2,274,407,813.76 kupitia mfumo wa SBM2 na mashine za POS (Point of sales) kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo kati ya fedha zilizokusanywa baada ya kupitia hesabu ya benki imebainika jumla ya shilingi 1,346,725,121.05 ndio fedha halisi zilizowasilishwa benki na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 927,682,692.71 ambazo hazikuwasilishwa benki na hazikuonekana matumizi yake hadi ukaguzi unakamilika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa makusanyo hayo ambayo hayakuwasilishwa benki ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 82 : Fedha za makusanyo ambazo hazikuwasilishwa benki**

| **Mw** | **M2 (Tshs)** | **ifa za hesabu za benki (Bank tement (Tshs)** | **auti (Tshs)** |
|---|---|---|---|
| ai, 2020 | 104,826,998 | 59,520,450 | 45,306,548 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| osti, 2020 | 151,916,357 | 65,510,900 | 86,405,457 |
| ptemba, 2020 | 213,556,251 | 116,882,520 | 96,673,731 |
| toba,2020 | 162,377,888 | 72,269,250 | 90,108,638 |
| vemba, 2020 | 142,846,102 | 314,178,120 | (171,332,017. |
| cemba, 2020 | 247,204,975 | 120,557,300 | 126,647,675 |
| uari, 2021 | 305,836,780 | 100,153,050 | 205,683,730 |
| oruari, 2021 | 233,556,090 | 127,576,722 | 105,979,367 |
| chi, 2021 | 181,033,387 | 97,710,121 | 83,323,266 |
| rili, 2021 | 147,669,109 | 69,760,987 | 77,908,122 |
| i, 2021 | 175,551,885 | 90,512,000 | 85,039,885 |
| i, 2021 | 208,031,985 | 112,093,700 | 95,938,285 |
| **Ju** | **2,274,407,813** | **1,346,725,121** | **927,682,692** |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Menejimenti kutokubaliana na hoja ya mkaguzi kwa sababu jadueli alilioonesha,

fedha zilizokuwepo benki hazikuwa sahihi, Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Serikali

alichukua fedha Taslim tu wakati statement imekusanya fedha zinazotokana na hundi, na fedha za Miamala ya benki na Benki (TT) na fedha Taslm. Hata hivyo menjimenti inakiri

kuwepo kwa Tofauti ndogo ya SBM2 na Bank statement kwa kila mwezi ambayo inasababishwa na Mambo yafuatayo: -

i) Kuna Miamala iliyofanyika benki ambayo kwa bahati mbaya inakosekana katika

SBM2 kwa wakati husika kutokana na kutojulikana nani kafanya muamala huo na

kupelekea kutoingizwa kwenye SBM2 kwa mwezi husika na inapojulikana aliyefanya

muamala huo huingizwa kwenye SBM2 na kwa wakati huo huwa haionekani tena

benki.

ii) Kutokana na kutumia mitandao ya simu katika ukusanyaji mapato inapelekea fedha

kuingia kwenye SBM2 siku husika lakini benki zinaingia mwezi mara mbili tu.

iii)Kutokana na Commission ya easy pesa na bank charges zote huleta tofauti

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa dosari za mfumo za SMB2 na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 927,682,692.71 ambazo hazikuwasilishwa benki

Kamati baada ya kujadiliana na mkaguzi juu ya uwepo wa hoja hii, Kamati imebaini kuwa Mamlaka wakati inajibu hoja kupitia Management letter imeshidwa kuwasilisha vielelezo hivyo vya TT na hundi kwa ajili ya kuthibitishwa na Mkaguzi ili kuondelewa kwa hoja au kupunguzwa kwa kiasi cha fedha kilichokosekana benki katika taarifa ya mkaguzi

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Mamlaka kuwa makini wakati wa kujibu hoja za Mkaguzi kwa kujibu hoja kwa usahihi na ukamilifu wake pamoja na kuambatisha vielelezo husika vya hoja hiyo ili mkaguzi atoe taarifa yake kama ilivyo bila ya kumuone mtu au taasisi kwa kupitia majibu aliyopatiwa na taasisi husika.

**5.2.16.21 Malipo yaliyokosa vielelezo shilingi 11,860,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 11,860,000 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya huduma mbali mbali zilizotumika na Mamlaka ya Maji (ZAWA), dosari iliyobainika ni kutokuambatanishwa kwa vielelezo vya hati za malipo ili kuweza kujiridhisha na kuthibitisha juu ya uhalali wa malipo hayo.

Kukosekana kwa vielelezo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 83 : Malipo yaliyokosa vielelezo**

| **ti Namba** | **Maelezo** | **Anaelipwa** | **mani (Tshs)** | **ichokosekana** |
|---|---|---|---|---|
| **1000907 1001079 toba 2020** | lipo kwa ajili ya kikosi kazi cha mlaka ya maji | ZAWA | 1,000, | oti ya utekelezaji wa kazi liyoifanya |
| **1001093 /11/2020** | lipo kwa ajili ya kikosi kazi cha mlaka ya maji | ZAWA | 1,000, | oti ya utekelezaji wa kazi liyoifanya |
| **1001316 /12/2020** | lipo kwa ajili ya siku ya pumziko kwa wafanyakazi wa tibu maji | ZAWA | 560, | oti ya utekelezaji wa kazi liyoifanya |
| **1001321 /12/2020** | lipo kwa ajili ya wafanyakazi u ya mradi wa riwssz na swss aofadhiliwa na bank ya Exim lia | ZAWA | 1,425, | oti ya utekelezaji wa kazi liyoifanya |
| **1001322 /12/2020** | lipo kwa ajili ya wafanya lioshiriki kazi siku za mapumzik | ZAWA | 720, | oti ya utekelezaji wa kazi liyoifanya |
| **1001325 /12/2020** | lipo kwa ajili ya wafanyakazi ra fedha kwa siku za mapumzi | ZAWA | 1,830, | oti ya utekelezaji wa kazi liyoifanya |
| **1001408 /12/2020** | lipo kwa ajili ya siku ya pumziko kwa wafanyakazi wa tibu maji | ZAWA | 700, | oti ya utekelezaji wa kazi liyoifanya |
| **1001409** | lipo kwa ajili ya siku za pumziko kwa wafanyakazi wa | ZAWA | 700, | rifa ya utekelezaji kazi za |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| /12/2020 | ra ya ufundi | | | vujo walioziba |
| 1001415 /12/2020 | lipo kwa ajili ya wafanyakazi w u ya mradiwa swssssz aofadhiliwa na bank ya Exim ya lia | ZAWA | 1,425,0 | oti ya utekelezaji wa kazi liyoifanya |
| 1001417 /12/2020 | lipo kwa ajili ya wafanyakazi w u ya mradi wa swssssz aofadhiliwa na bnk ya Exim ya lia. | ZAWA | 1,250,0 | oti ya utekelezaji wa kazi liyoifanya |
| 1001419 /12/2020 | lipo kwa ajili ya wafanyakazi w u ya mradi wa swssssz aofadhiliwa na bank ya Exim ya lia. | ZAWA | 1,250,0 | oti ya utekelezaji wa kazi liyoifanya |
| **Jumla** | | | **11,860,0** | |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Menejiment kupitia idara ya Fedha na Mipango tayari imeshafuatilia ripoti hizo na tayari zimeshawasilishwa kwa uongozi utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Serikali tayari yameshakuliwa hatua.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Mamlaka. imekiri kuwepo kwa dosari hiyo na wameshaanza kuchukua hatua ya kukamilisha vielelezo vilivyokosekana. Hata hivyo, Kamati inaishauri Mamlaka kufuata Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016 kifungu namba 34(1) katika utekelezaji wa majukumu yake.

### 5.2.16.22 Kutokupelekwa kwa Pampu nne (4) pamoja na vifaa vyake Pemba

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Maji Zanzibar imenunua pampu 12 na vifaa vyake kutoka kwa Kampuni ya African Power Machinery Tz Ltd kwa jumla ya shilingi 773,980,422 ambapo pampu na vifaa hivyo vimenunuliwa kutokana na agizo lililotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati alipofanya ziara ya kutembelea katika Mamlaka ya Maji Zanzibar ambapo kati ya pampu na vifaa vilivyonunuliwa viliagizwa pampu nne (4) pamoja na vifaa vyake vipelekwe Mamlaka ya Maji Pemba kwa ajili ya kutatua changamoto za ukosefu wa maji zinazowakabili wananchi.

Dosari iliyobainika ni kwamba hadi ukaguzi unakamilika pampu nne (4) pamoja na vifaa vyake hazikupelekwa Pemba, jambo ambalo limepelekea kuendelea kujitokeza kwa changamoto za kukosekana kwa huduma za maji kwa baadhi ya maeneo kunakotokana na tatizo la kukosekana kwa pampu za maji.

Kutokuziwasilisha Pampu nne (4) na vifaa vyake kwa Mamlaka ya Maji Pemba ni kwenda kinyume na utekelezaji wa Agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alilolitowa wakati wa ziara yake.Mchanganuo wa Pampu ambazo hazikupelekwa Pemba na badala yake zinatumika katika maeneo mengine ni kama zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 84 : Pampu na vifaa ambavyo havikupelekwa Pemba**

| Namba | ɔta (KW) | mpu (m3/h) | mpuni | aa | Idadi | eo/Kisima |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 5 | 46-126”<br>(18.5KW) | UNDFOS | ɔle&<br>ntrol<br>nel | 1 | ongani /Kitongani<br>K |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | | 30-136" (9.2KW) | UNDFOS | ble &Con- l Panel | 1 | guja Ukuu Skuli |
| 3 | | 46-156" (22KW) | UNDFOS | ble & ntrol nel | 1 | ejuu/Bwejuu |
| 4 | 5 | 30-216" (18.5KW) | UNDFOS | ble & ntrol nel | 1 | nge/ Donge ange |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Idara ya Operesheni za Kiufundi inajukumula kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inapatikana kwa Wananchi wa Unguja na Pemba. Kutumika kwa Pampu hizo maeneo ya kisima cha Kitogani RAK, Unguja Ukuu Skuli, Bwejuu na Donge Kipange ni maeneo ambayo Mh. Rais alitoa maagizo ya kuitaka ZAWA kurudisha huduma maeneo hayo pamoja na maeneomengine yenye ukosefu wa huduma ya maji.

Agizo ambalo alilitoa katika ziara yake aliyoifanya tarehe 03 Julai 2021 Mkoa wa Kusini. Kupitia agizo hilo ZAWA ililizingatia na baada ya kupata pampu hizo ZAWA ilitekeleza agizo hilo kwa kurudisha huduma maeneo hayo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Mamlaka imekiri kutowasilisha pampu hizo kisiwani Pemba kwa wakati huo ila kwa sasa tayari zimeshawasili kwa mnasaba huo Kamati inaishauri Mamlaka kufanya kazi zake kwa ufanisi ili kupunguza malalamiko yasiyokuwa ya lazima kwa wananchi wetu. Aidha,

kuharakisha upatikanaji wa maji safi na salama visiwani Zanzibar kwa vile malalamiko hayo yameshakua ya muda mrefu.

**Mamlaka ya Maji Zanzibar (Zawa) - Pemba**

**5.2.16.23 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 311,616,969**

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Maji (ZAWA) - Pemba imeripoti uwepo wa deni la shilingi 311,616,969 wanalodaiwa kwa muda mrefu kutokana na kupatiwa huduma ya ulinzi, ujenzi pamoja na uwepo wa deni la stahiki za watumishi.

Pamoja na uwepo wa juhudi zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha inafanya ukaguzi wa madeni yote na kuchukuwa jitihada za kuwalilpa wale wote wanaoidai Serikali,dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa za uwasilishwaji wa deni hilo ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya kuliandikia ili kukaguliwa na ofisi ya Mdhbiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na hatimae kulitoleya maoni na mapendekezo kwa Serikali kwa lengo la kuchukuwa juhudi za kulipwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuchukuwa juhudi za makusudi kuliandikia na kuliwasilisha deni hilo kwenye mamlaka husika ili taratibu za haraka za kuweza kulipwa zichukuliwe kwa lengo la kutimiza ahadi za viongozi wakuu walizozitoa ikiwemo kulipa madeni yote ya wazabuni kwa lengo la kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi wa Zanzibar.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Ni kweli kwamba Mamlaka ya Maji Tawi la Pemba ina kiasi kikubwa cha madeni ya watoa huduma pamoja na wafanyakazi ambayo yanafanya jumla ya shilingi za kitanzania shilingi 311,616,969 ambayo hayakuwasilishwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Aidha, Zawa Pemba tayari ilichukua hatua za kuliwasilisha deni hilo Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji tarehe 02/08/2021 na deni hilo liliwasiliswa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji Nishati na

Madini Zanzibar kwa barua yenye nambari kumbu kumbu ZAWA/A.10/10/VOL.II/67 yenye jumla Tzs 46,316,440,865.18 ( kiasi hiki kinajumuisha deni ambalo ZAWA Pemba inadaiwa TZS 311,616,969). Pamoja na hivyo, tarehe 13/1/2023 Mamlaka ya Maji Makao Makuu iliwasilisha tena deni hilo kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa barua ya tarehe 13/1/2023 yenye nambari za kumbukumbu ZAWA/A.10/3/VOL.V/30 yenye jumla ya TZS 190,766,954.

Vile vile, ZAWA Pemba imejitayarisha kuyalipa madeni ambayo itakua yanadaiwa kwa kutayarisha bajeti kwa kila Mwaka wa Fedha pamoja na kuweka mikakati ya kutokuongezeka kwa madeni kila unapomalizika Mwaka wa Fedha. Aidha, Mamlaka ya Maji Tawi la Pemba imefanikiwa kuyalipa madeni yote ya wafanyakazi yenye jumla ya Tzs 55,147,800 sawa na asilimia 100 na baadhi ya madeni ya watoa huduma kutoka nje (Suppliers) kwa jumla ya Shilingi 65,702,215 sawa na asilimia 25.6 ya deni lote hadi sasa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imebaini Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) - Pemba imechelewa kuwasilisha madeni yake Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango badala yake imewasilisha deni hilo Makao Makuu ya Mamlaka ya Maji na Makao makuu kuwasilisha deni hilo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji Nishati na Madini Zanzibar kwa barua tarehe 02/08/2021 yenye nambari kumbu kumbu ZAWA/A.10/10/VOL.II/67 jambo ambalo limecheleweshа barua hizo kufika kwa wakati katika Ofisi ya Rais fedha na Mipango.

Licha ya Ucheleweshaji huo Kamati imerizika na majibu yaliyotolewa na Mamlaka inaamua kuifuta hoja hii kutokana jitihada ambazo Mamlaka imezichukua za kulipa madeni yote ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Maji Pemba kwa asilimia 100. Aidha kuendelea kulipa madeni ya watoa huduma kutoka nje yenye jumla ya Tzs 65,702,215 sawa na asilimia 25.6

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kuwasilisha madeni yake moja kwa moja katika Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kuliandikia ili kukaguliwa na ofisi ya Mdhbiti na Mkaguzi Mkuu na Nakala iende kwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji Nishati na Madini Zanzibar kwa lengo kuepusha ucheleweshaji wa uwasilishaji wa barua za madeni kutoka kwa Mamlaka.

Kamati inaishauri Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) - Pemba kuendelea na mikakati ya kumaliza deni la watoa huduma (Supplies) na kudhibiti ongezeko la madeni mapya miaka ijayo ili Mamlaka iweze kuboresha huduma zake za upatikanaji wa maji safi na salama katika Visiwa vya Pemba.

**5.2.16.24 Kutokutenganishwa kwa Ofisi ya masjala ya siri na bayana**

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Maji Pemba haijatenganisha masjala ya siri na ya bayana hali ambayo inaweza kupelekea kuvuja kwa taarifa za siri za Serikali pamoja na kupelekea kuwepo kwa mchanganyiko wa majalada ya nyaraka, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 52(1) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar ya mwaka 2014.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Ni kweli kwamba ZAWA Pemba haina nafasi ya peke yake ya Masjala ya Siri. Kwa hivi sasa Masjala hio imetenganishwa ndani ya Masjala ya Bayana kwa kuekewa kabati la peke yake linalosimamiwa na muhusika maalumu. Changamoto ya kuzichanganya Masjala hizo mbili katika chumba kimoja kunatokana na ufinyu mkubwa wa nafasi unao ikabili Ofisi ya ZAWA Pemba.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imearifiwa kuwa Ofisi ya Mamlaka Maji Zanzibar (ZAWA) - Pemba inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa nafasi inayopelekea kushidwa kutenganisha masjala bayana na siri. Katika kutatua changamoto hii Mamlaka imeiambia Kamati inasubiri kumalizika kwa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mamlaka kwa upande wa Unguja ambapo mradi huo pia unategemea kujenga Jengo la Mamlaka kwa upande wa Pemba na Changamoto hiyo ya ufinyu wa nafasi itaondoka.

Kamati inaishauri Mamlaka kuharakisha utekelezaji wa mradi wa jengo jipya kwa upande wa Pemba kwa lengo la kuongeza ukubwa wa Ofisi ili shughuli za Mamlaka zifanyike kwa ufanisi mkubwa.

**5.2.16.25 Uwepo wa uchakavu wa mali za kudumu kwa muda mrefu**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya maji-Pemba inamiliki mali za aina mbali mbali ambazo zimekaa kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo au kuchukuliwa hatua za kuuzwa mali chakavu jambo ambalo linapelekea kuendelea kuchakaa kwa mali hizo na huwenda ikapelekea kukosekana kwa mapato ya Serikali pale itakapochukuwa jitihada za kuondoa mali chakavu kutokana na kuchelewa kuchukuwa maamuzi hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya maji – Pemba kuchukuwa jitihada za makusudi katika kuzifanyia matengenezo mali hizo au kuziuza kwa lengo la upatikanaji wa mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mali hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 85 : Udhibiti usioridhisha wa Mali za Kudumu**

| Namba | ıa ya Mali | Idadi | ıhala Ilipo |
|---|---|---|---|
| 1 | ri (SLS 242 B) | 1 | WA – Machomane |
| 2 | ri (SMZ 6173) | 1 | WA – Machomane |
| 3 | ri (SLS 125 B) | 1 | WA – Machomane |
| 4 | ri (DFP 3979) | 1 | WA – Machomane |
| 5 | ri (SLS 226 B) | 1 | WA – Machomane |
| 6 | nereta | 1 | WA – Machomane |
| 7 | Compressor | 1 | WA – Machomane |
| 8 | ri (SMZ 6174) | 1 | se Camp Sharif Ali |
| 9 | nereta | 1 | se Camp Sharif Ali |
| 10 | lling Machine | 1 | se Camp Sharif Ali |
| 11 | mputer Desktop | 7 | WA – Machomane |
| 12 | ıshine ya kudurufu (Photocopy Machine) | 1 | WA – Machomane |
| 13 | ıshine za kukusanyia mapato (POS Machine) | 9 | WA – Machomane |
| 14 | oyozi (Air Condition) | 5 | WA – Machomane |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

Ni kweli ZAWA inazo mali zilizochakaa. Aidha, jitihada zimefanyika ili kupembua katika mali hizo kuona ipi itaweza kufanyiwa marekebisho na matengenezo. ZAWA Pemba iliwasilisha barua yenye kumbukumbu ZAWA/MP/A.10/3/97 yatarehe 7/10/2022 kwahatua za kuomba kuondoshwa mali hizo zilizochakaa na kujibiwa kwamba ombi hilo lilipaswa kufanywa na Makao Makuu ya ZAWA ilikupatakibali.

Kwa sasa, mali zote zilizoombewa kuondolewa zimeshafanyiwa utaratibu wa kuuzwa

kupitia barua yenye nambari za kumbukumbu BC.246/406/01/144 ya tarehe 13/1/2023 na siku ya tarehe 15/1/2023 mnada wa kuuza vifaa hivyo ulifanyika ZAWA Pemba.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imeelezwa gari mbili za Mamlaka hazijafanyiwa mnada na zimechukuliwa na Mamlaka kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo kwa vile hazikuwa zimechakaa sana na zinauwezo mkubwa wa kufanya kazi ikiwa zitapatiwa matengenezo. Vile vile, gari moja imeshidwa kuuzwa kutokana na Serikali kushidwa kupata bei ambayo imejipangia katika mnada na Gari zilibagia zote zimuzwa kwa njia ya mnada

Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi mkuu, kwa vile Mamlaka imechukua jitihada za kuziuza mali zake na kwa sasa mali hizo zote zimeshafanyiwa utaratibu kuondolewa kwa njia ya mnada hivyo Kamati inaamua kuifuta hoja hii.

Kamati inaishauri Serikali kupita Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kukamilisha utaratibu wa kulifanyia mnada mwengine gari lenye namba za usajili SLS 242 (B) ambalo halikuuzwa kutokana na wateja kutofikia bei iliyopangwa kwani kuendelea kubaki hapo kutapelekea kuchakaa na kupoteza thamani na hatimae kuuzwa kwa bei ndogo kabisa na kuikosesha Serikali mapato.

**5.2.16.26 Kutokuripoti kazi kwa muda mrefu**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Nd. Nassor Juma Kombo mwenye nambari ya uajiri 15950 ambae amechukua likizo tangia 30/06/2008, dosari iliyobainika ni kuendelea kulipwa stahiki zake za mshahara na maposho hali ya kuwa hajaripoti kazi kwa muda wote bila ya uwepo wa hatua yoyote ya kiutumishi iliyochukuliwa dhidi yake jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma zinazotokana na kulipa mshahara kwa watumishi waliokuwa hawapo kazini.

Aidha, mtumishi wa umma kutokuripoti kazi kwa muda mrefu ni kwenda kinyume na kifungu nambari 82(1) cha Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha unachukuwa jitihada za makusudi za kusimamisha malipo ya mtumishi huyo pamoja na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) - PEMBA**

Ni kweli yupo mfanyakazi wa Mamlaka ya Maji Tawi la Pemba mwenye nambari ya uajiri 15950 ambae yupo likizo bila ya malipo kuanzia tarehe 30/6/2008 kutokana na mfanya kazi huyo kapata uteuzi wa kuwa Sheha wa Shehia ya Mbuyuni, Wilaya ya Mkoani Pemba, kuanzia tarehe 11/6/2008 hadi hivi sasa.

Vile vile, kumbukumbu zote za mfanyakazi huyo zipo na kilichokosekana ni barua ya majibu ya ruhusa ya kwenda katika likizo hilo. Aidha, suala hili limewasilishwa Makao Makuu kwa barua yenye nambari za kumbukumbu ZAWA/MP/W.10/21/VOL.III/80 ya tarehe 8/12/2022 ilitaratibu za kiutumishi ziweze kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kupewa barua yake ya majibu ya likizo bila malipo.

Aidha, mfanyakazi huyo hajawahi kulipwa mshahara wala stahiki nyengine yoyote kwa kipindi chote ambacho yupo likizo bila ya malipo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati kufuatilia hoja hii imeomba kupatiwa vielelezo vya malipo ya mshahara kwa mwaka 2020/2021 na kubaini kuwa mfanyakazi huyo hakuwepo kwenye orodha ya malipo tokea alipo andika barua ya kuacha kazi tarehe 30/06/2008.

Aidha, Kamati imebaini Mkaguzi ameshidwa kupatiwa barua kutoka Mamlaka iliyomruhu mtendaji huyo kuacha kazi na kendelea na majukumu yake ya uteuzi kwa mujibu wa Sheria

utumishi ili kuthibitisha kuwa mtendaji huyo hayupo tena kwenye Mamlaka na hakuna mshahara wala Stahiki zozote zinazotolewa kwake.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Uongozi wa Mamlaka ya Maji ZAWA kufuata Sheria za Utumishi ambazo zinatutaka endapo Mtendaji anapoondoka sehemu ya kazi kwa njia mbali mbali kama vile kuacha kazi, likizo, au uhamisho ni lazima Uongozi wa Mamlaka itoe Barua ya kuruhusu kuondoka kwa Mtendaji huyo ili Uthibitisho wa mtendaji huyo kuwa hayupo kazini uweze kupatikana.

**5.2.16.27 Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 55,750,898.88**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Maji imefanya manunuzi na Simba Pipe Industries Limited kwa hati namba 8/7 ya tarehe 17/7/2020 kwa ajili ya Ununuzi wa bomba za HDPE za inchi sita kwa jumla ya shilingi 55,750,898.88 lakini mfanyabiashara huyo hakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato, ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) - PEMBA**

Ni kweli kwamba Mamlaka ya Maji Ofisi ya Tawi Pemba ilifanya malipo ya mfanya biashara Simba Pipe Industries Limited ambaye hakuwa na usajili kutoka kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Hatahivyo, tayari mfanyabiashara huyo alifanya usajili tarehe 8 Januari 2021 wenye nambari za usajili ZPPDA/G/047/2021 na kwasasa wafanyabiashara wanaotumika ni wale ambao wameshajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inakubaliana na hoja ya Mkaguzi hata hivyo Kamati inaifuta hoja hii kwa vile Mamlaka kwa sasa inapokea huduma kwa wafanya biashara mbali mbali ambao tayari wameshasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, kwa mfano mfanyabiashara Simba Pipe Industries Limited ambaye hapo awali alikuwa hajasajiliwa na sasa tayari ameshasajiliwa.Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka kuendelea kufuata sheria ya manunuzi kwa kupokea huduma kwa wafanya biashara ambao wamesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

**5.2.16.28 Madeni ya maji ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu shilingi 18,071,075,899.38**

Jumla ya shilingi 18,071,075,899.38 ni madeni ya maji ambayo hayajalipwa kutoka kwa baadhi ya wateja wakiwemo Taasisi za Serikali, wafanyabiashara na watu binafsi kwa muda mrefu sasa. Ukaguzi umebani kwamba idadi kubwa ya wateja wanaodaiwa hawako makini katika ulipaji wa madeni yao, aidha uongozi wa Mamlaka ya Maji - Pemba umeshindwa kuchukua hatua zinazostahiki.

Hadi ukaguzi unakamilika idadi kubwa ya wateja hao wameshindwa kulipa madeni yao.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar namba 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama ufuatavyo:-

**Jadweli Nambari 86 : Madeni ya muda mrefu**

| **mba** | **laya** | **di ya Wanaodai- wa** | **ni Halisi (Tshs.)** |
|---|---|---|---|
| | ake Chake | 918 | 23,225,955.82 |
| | te | 612 | 41,214,441.89 |
| | oani | 032 | 82,543,356.81 |
| | cheweni | 18 | 24,092,144.86 |
| **nla** | | **280** | **071,075,899.38** |

**Majibu ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) - PEMBA**

Ni kweli Mamlaka ya Maji Pemba inadai kiasi kikubwa cha fedha ambacho ni madeni ya muda mrefu yatokanayo na utumiaji wa huduma ya maji kwa wateja wake.

Miongoni mwa jitihada ambazo Mamlaka inachukua ni pamoja na kutoa Ankara kwa wateja wake wote kwa kila mwezi, kupeleka barua za madeni kwaTaasisi, kutuma ujumbe mfupi kupitia simu za wateja, kuondoa huduma ya maji ikibidi kwa mteja husika. Vile vile, Mamlaka hutumia njia ya mazumgumzo na matangazo kuwahamsisha wateja kuweza kusawazisha madeni yao ya huduma ya maji. Pamoja na jitihada hizo Mamlaka bado inabakia kuwa na jukumu la kutoa huduma ya maji safi na salama kama ambavyo sera ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyoelekeza.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imeelezwa kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) inaendelea na mpango wake kufunga mita za maji kwa wateja wake wa Zanzibar, hivyo ufungaji huu wa mita utasaidia kuondoa changamoto ya ukusanyaji wa mapato kwa mfumo wa zamani uliokuwa unatumiwa na Mamlaka, ambao unasababisha wateja wengi wanaopatiwa huduma ya maji kutolipa bili ya maji kwa muda mrefu kutokana na sababu mbalimbali, vilevile Mamlaka hukubwa na changamoto kadhaa katika kufuatilia bili za maji kwa wateja wake ambao hawakufungiwa mita.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inatoa ushauri kwa Mamlaka kuendelea kuchukua jitihada za kudai madeni kwa wateja wake kwa lengo kuongeza mapato, kwa vile Mamlaka bado ina kazi kubwa ya kuhakikisha inatoa huduma ya maji kwa wananchi wa Zanzibar,

Aidha, Kamati inaishauri Mamlaka ya Maji ZAWA kukamilisha mpango wake wa kufunga mita za maji kwa wateja wake kwa lengo kuleta ufanisi wa utoaji huduma za maji na ukusanyaji wa mapato jambo ambalo litapelekea Mamlaka kuondokana na madeni ya muda mrefu kwa wateja wake.

**5.2.16.29 Kutokuwepo kwa muhasibu wa mapato**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Maji Pemba inakusanya mapato kupitia vianzio vyake mbali mbali lakini haina Muhasibu maalum kwa ajili ya kusimamia mapato hayo hali ambayo inaweza kupelekea kupungua kwa ufanisi katika suala zima la ukusanyaji wa mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016.

**Majibu ya Mamlaka ya Maji  Zanzibar (ZAWA) - Pemba**

Ni kweli kwamba Mamlaka ilikosa muhasibu wa mapato kwa kipindi kirefu jambo ambalo lilileta msongomano wa kazi kwa Muhasibu aliyepo. Hata hivyo, jitihada zimechukuliwa ili kuziba pengo hilo ikiwa ni pamoja na kumpangia kazi mfanyakazi wa ndani katika nafasi hiyo. Mfanyakazi huyo mwenye Stashahada ya Uhasibu na alipangiwa kazi hiyo tarehe 10/11/2022 kwa barua yenye nambari ya kumbukumbuOPF/A.88/88.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii Mamlaka imesema imeomba kibali cha Uajiri Serikalini kwa lengo la kutoa nafasi za ajira ikiwemo nafasi ya uhasibu, Kamati imeomba kupatiwa barua hiyo na imeweza kuwasilishwa mbele ya Kamati.

Hata hivyo, Kamati inaipongeza Mamlaka kwa hatua walizozichukua za kumteua mtendaji wa ndani mwenye Stashahada ya Uhasibu ili kuboresha huduma za Ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka kwa upande wa Pemba.

Pia, Kamati inaishauri Mamlaka kuendelea kufuatilia suala la kibali cha uajiri ili kumpata Muhasibu Mapato mwenye sifa zinazostahiki, aidha kumuendeleza kitaaluma muhasibu mapato ambaye ameteuliwa ili kuboresha utendaji kazi wa Mamlaka katika ukusanyaji wa mapato.

### 5.2.17 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZAMAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)

**Taarifa ya Mapato**

Ukaguzi umebaini kuwa mapato ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar yamepungua kutoka shilingi 16,473,560,512 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia shilingi 15,505,069,856 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na upungufu wa shilingi 968,490,656 sawa asilimia 5.9 ya upungufu.

**Majibu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati(ZURA)**

Mamlaka inathibitisha kupungua kwa mapato kutokana na Mazingira ya kupungua kwa uingizaji wa mafuta nchini hali iliyotokana na mripuko wa maradhi ya Uviko-19. Kwa kawaida ni kuwa mapato ya Taasisi yanaenda sambamba na uingizwaji wa mafuta yanayotokana Zaidi na shughuli za lkiuchumi ambapo ziliteteereka kipindi cha maradhi hayo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Ni kweli Mapato hayakuweza kufikia lengo kutokana na uwepo wa maradhi ya UVIKO – 19. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza Mamlaka kusimamia vyema vyanzo vyake vya ndali ili kwa mwaka unaofuata kufikia lengo lililokusudiwa la makusanyo.

**Taarifa ya Matumizi**

Ukaguzi umebaini kuwa matumizi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar yamepungua kutoka shilingi 14,008,586,980 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia shilingi 13,646,466,307 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na upungufu wa shilingi 362,120,673 sawa na asilimia 2.6 ya upungufu.

**Majibu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati(ZURA)**

Matumizi ya Mamlaka yalipungua kutokana na athari zilizojitokeza za kiuchumi zilizosababishwa na Uviko – 19 pamoja na kuimarika kwa mfumo wa udhibiti wa ndani (Internal Control System)

Ufanisi katika Uendeshaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini kwamba utendaji wa kifedha wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar umeendelea kuimarika kutokana na kuwepo kwa ufanisi katika utendaji wa shughuli za Mamlaka. Kwa mujibu wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka 2020/2021 ukaguzi umebaini kuwa

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar imeendelea kupata faida ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Mamlaka imepata faida ya shilingi 1,858,603,549.

Hata hivyo, faida ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar imeonekana kuendelea kupungua kutoka shilingi 2,869,816,964 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia shilingi 1,858,603,549 ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 35.2. Upungufu huo wa faida unatokana na kupungua kwa mapato ya Mamlaka kulikofuatiwa na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji.

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati kuendelea kuchukua jitihada za kuongeza mapato ya Mamlaka pamoja na kwenda sambamba na kupunguza gharama za uendeshaji za Mamlaka.

**Majibu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati(ZURA)**

Katika Mwaka 2020/2021, Mamlaka iliimarisha Mazingira ya kazi kwa wafanyakazi wake kwa kuwahamisha kutoka ofisi ambayo Mamlaka ilikodi kuhamia katika ofisi yake mpya. Katika mchakato huo Mamlaka ililazimika kukamilisha mahitaji ya majengo hayo ikiwemo kufanya "partition", ununuzi wa baadhji ya thamani pamoja na vitendea kazi vilivyopungua kutokana na ukubwa wa ofisi. Zaidi ya jukumu hilo Mamlaka ilipaswa kwa Mwaka wa kwanza kuhudumia majengo yote mawili ikiwemo Huduma za maji, Umeme na usafi ambazo zilipandisha kwa kasi gharama za uendeleshaji.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imeridhishwa na majibu yalivyokuwa yakijibiwa wakati wa majadiliano ya hoja hii. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati kuusimamia na kuutekeleza kikamilifu ushauri walipatiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kuhakikisha kupunguza gharama za uendeshaji za Mamlaka.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

**5.2.17.1 Kukosekana kwa kumbukumbu za mapokezi ya Mafuta yaliyonunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka**

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar ilinunua mafuta kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka na kwa ajili ya posho la usafiri kwa wafanyakazi wa Mamlaka.

Ukaguzi umepitia kumbukumbu za ghalani za mafuta na kubaini kuwa kumbukumbu zilizowekwa na Mamlaka zinaonyesha kiasi tu cha mafuta yaliyotolewa kwa ajili ya matumizi pasi na kuonyesha kiasi cha mafuta yaliyonunuliwa kabla ya kutumika.

Mchanganuo wa mafuta yaliyonunuliwa na Mamlaka ambayo kumbukumbu zake hazikupatikana kwa ukaguzi ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 87: Kukosekana kwa kumbukumbu za mapokezi ya Mafuta**

| **Hati Namba** | **Ankara Namba** | **Kiasi cha fedha kilicholipwa** (Tshs) | **Aliyelipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|
| 2/9/2020 ya 1/9/2020 | 317<br>9 / 05322 | 7,200,000 | | |
| 54/09 ya 10/9/2020 | 320<br>3 / 05610 | 2,730,000 | | |
| 1/10 ya 2/10/2020 | 327<br>2 / 06036 | 7,276,000 | | |
| 15/11 ya 5/11/2020 | 333<br>6 / 06852 | 7,638,000 | | |
| 28/11 ya 7/1/2020 | 344<br>0 / 422 | 2,064,000 | United Group Ltd. | Malipo ya fedha kwa |
| 61/02 ya 15/02/2021 | 353 / 1066 | 7,388,000 | | ajili ya ununuzi wa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2 | | | |
| 71/3 ya 9/3/2021 | 358<br>3 / 1662 | 7,336,000 | | mafuta ya Ofisi. |
| 88/5 ya 19/5/2021 | 377<br>1 / | 9,385,600 | | |
| 40/6 ya 23/6/2021 | 385<br>3 / 3914 | 9,730,560 | | |
| 3/6 ya 7/6/2021 | 379<br>8 | 6,191,000 | | |
| 1/5 ya 3/5/2021 | 445 /59257 | 1,385,600 | Zanzibar Petroleum Ltd. | |
| 38/6 ya 23/6/2021 | 757 / 59859 | 1,544,960 | | |
| **Jumla** | | **69,869,720** | | |

Kukosekana kwa kumbukumbu za mapokezi ya mafuta yaliyonunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka kunaweza kupelekea upotevu wa mafuta ya Mamlaka.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar kuhakikisha kuwa kumbukumbu za ununuzi wa mafuta yanayonunuliwa kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka zinaweka vizuri na kufanyiwa usuluhisho kwa kila mwezi.

**Majibu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati(ZURA)**

Mamlaka ilipokea hoja hiyo na kuifanyia kazi kwa mujibu wa matakwa yaliyohitajika ya kumbukumbu hizo na kwa hivi sasa kumbukumbu zote za mapokezi ya mafuta na matumizi zinaonekana katika mifumo iliyoboreshwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja hii imeondolewa baada ya Kamati ya LAAC kuvipitia vielelezo vyote vinavyohusiana na upokeaji wa mafuta pamoja na matumizi ya mafuta katika "Store Ledger Book" pamoja na "Payment Voucher" zote na kubaini vielelezo vyote vilikuwepo na vipo sahihi.

Hivyo, Kamati inawashauri wakaguzi kutoka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapofanya ukaguzi kuvipitia vielelezo vyote wanavyokabidhiwa wakati wa ukaguzi ipasavyo ili kuepusha uwepo wa hoja zisizo na mashiko.

**5.2.17.2 Kukosekana kwa Mpango wa Dharura wa Vituo vya Mafuta**

Kwa mujibu wa kanuni nambari 42(b) cha Kanuni za Vituo vya Mafuta za mwaka 2019, vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuwa Mpango wa Dharura (Management Emergency Plan). Mpango huo unatoa mungozo wa namna ya kukabiliana na hali za dharura kama vile hatua za kuchukua wakati wa kukabiliana na majanga ya moto n.kUkaguzi umebaini kuwa bado Mpango huo wa dharura haupo.

Kukosekana kwa Mpango wa Dharura kwa vituo vya mafuta ni kuwenda kinyume na Kanuni za Vituo vya Mafuta za mwaka 2019 na kunaweza kupelekea vituo hivyo kushindwa kukabiliana na hali za dharura.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar kuwa wanaandaa mkakati maalum wa kuhakikisha kuwa vituo vyote vya mafuta vinakuwa na Mpango wa Dharura (Management Emergency Plan) na kwamba wafanyakazi wote wa vituo hivyo wanauelewa.

**Majibu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati(ZURA)**

Mamlaka inakiri kuwa wakati wa ukaguzi Mpango wa dharura wa vituo vya mafuta (Management Emergency Plan) Kwa mujibu wa kanuni nambari 42(b) cha Kanuni za Vituo vya Mafuta za mwaka 2019, haukuwepo na kuwasilishiwa wakaguzi kutokana na kutokamilika uandaaji wake (Rasimu ya awali) kwa ajili ya matumizi , hii inatokana na kuwepo na upungufu wa wataalamu kwa wakati huo na mahitaji makubwa ya kuandaa kanuni na nyenzo mbali mbali za kusimamia Huduma za Maji na Nishati Zanzibar. Hata hivyo Mpango wa Dharura (Management Emergency Plan) umeshaandaliwa na umeanza kutumika kwa Mwaka wa fedha 2021/2022.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya kukiri kwa hoja hii pamoja na kukamilika na kuanza kutumika kwa Mpango wa Dharura wa Vituo vya Mafuta. Kamati ya LAAC inaishauri Mamlaka husika kuharakisha utoaji wa elimu kwa watendaji pamoja na wahusika wa vituo vya mafuta kuhusiana na Mpango huo wa Dharura ilioandaliwa.

### 5.2.17.3 Uidhinishaji wa Vituo vya Mafuta kinyume na Kanuni Vituo vya Kujaza Mafuta

Kwa mujibu wa kifungu nambari 20(1) cha Kanuni za Vituo vya kujaza mafuta ya mwaka 2019 inaeleza kwamba vituo vya kujaza mafuta vinatakiwa viwepo katika umbali wa masafa yasiyopungua kilo mita moja (1,000 Meters) baina ya kituo kimoja na chengine. Aidha kwa mujibu wa kifungu nambari 11(2) cha kanuni hiyo kinaeleza ya kwamba eneo la kituo cha Mafuta lisipungue mita za mraba 900.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa mbali mbali za uongozi pamoja na kutembelea vituo mbali mbali na kubaini ya kwamba baadhi ya vituo vya uuzwaji wa mafuta (Petrol Stations) vinafanya kazi bila ya kufuata na kuzingatia matakwa ya kanuni nilizozitaja hapo juu kwa kubainika kuwepo na vituo zaidi ya kimoja katika umbali wa masafa mafupi. Mchanganuo wa vituo vilivyoruhusiwa kufanya kazi bila ya kufuata misingi ya kisheria ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 88: Vituo vilivyoruhusiwa kufanya kazi bila ya kufuata misingi ya kisheria**

| Namba | Jina la Eneo | Idadi ya vituo vilivyopo | Umbali wa masafa baina ya vituo na ukubwa wa eneo (Meters) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Fuoni Jitimai | 2 | 1,000 | Kutokukidhi kwa umbali wa vigezo na vilivyotakiwa pamoja na ukubwa wa eneo la kituo |
| 2 | Mchina Mwisho | 2 | 1,000 | |
| 3 | Amani area | 2 | 1,000 | |
| 4 | Chasasa | 1 | 1,000 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Limbani | 1 | 1,000 | |
| 6 | Kengeja | 1 | 196.56 | |
| 7 | Mwanakwerekwe | 2 | 1,000 | |

Kuwepo kwa vituo vingi vya kuuzia mafuta katika masafa madogo au kuwa na eneo dogo la kituo kunapelekea kujitokeza kwa uwepo wa foleni wa vyombo vya moto ambavyo vinapelekea kufunga njia na kusababisha kero kwa wananchi jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 20(1) pamoja na 11(2) vya Kanuni za Vituo vya kujaza mafuta ya mwaka 2019.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Maji na Nishati kuhakikisha unasimamia usalama wa vituo vya kuuzia mafuta kwa kuzingatia umbali,ukubwa wa eneo,pamoja na uwezo wa kituo kuhimili wingi wa vifaa vya moto ili kunusuru majanga hatarishi yanayoweza kujitokeza.

Aidha, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati inashauriwa kufanya mapitio ya sheria yao ili iweze kuendana na hali halisi ya mazingira ya vituo vya mafuta vilivyopo.

**Majibu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati(ZURA)**

Mamlaka inakiri uwepo vituo vya mafuta visivyotimia umbali wa masafa ya kilomita moja kama ilivyoainishwa na kanuni ya vituo vya mafuta ya mwaka 2019, hii inatokana na vituo vingi kati ya vilivyoainshwa kuwa vimejengwa kabla ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za maji na Nishati (ZURA), isipokuwa vituo viwili ambavyo ni Fuoni Jitimai kwa Unguja na Limbani kwa Pemba, Mamlaka iliridhia kujengwa kwa vituo hivyo viwili kutokana na mahitaji kwa wakati huo, Hata hivyo kuepusha kukeukwa kwa kanuni inapotokezea haja ya kujenga kituo chini ya masafa

ya kilomita moja Mamlaka imeifanyia mapitio Kanuni ya mwaka 2019 ya Usimamizi wa vituo vya mafuta na kuwa na kanuni ya 2022, ambayo inaruhusu ujenzi wa vituo vya mafuta kwa maeneo yaliyochini ya umbali wa kilomita moja inapotokezea haja ya kufanya hivyo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inaitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) kwa vituo vyote vinavyoendelea kujengwa baada ya kuwepo kwa Kanuni mpya ya inayoruhusu ujenzi wa vituo vya mafuta katika maeneo yaliyochini ya umbali wa kilomita moja wahakikishe wanafanya uchunguzi wa kutosha ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza baadae.

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI - PEMBA**

**5.2.17.4 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 1,285,000**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 1,285,000 zimetumika kwa malipo mbali mbali ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Pemba lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya usimamizi wa Fedha za umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo yenye vielelezo pungufu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 89: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Nambari ya Hati | Nambari ya | Kiasi cha | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| ya Malipo | Hundi | Fedha | | |

| | | kilicholipwa (Tshs.) | | |
|---|---|---|---|---|
| 16/8<br>9/7/2020 | 000199 | 560,000 | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati. | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari kikazi. |
| 10/10<br>16/9/2020 | 000202 | 725,000 | | |
| **Jumla** | | **1,285,000** | | |

## Majibu ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati(ZURA)

Mamlaka imechukua hatua za kuhakikisha kuwa vielelezo vyote hivyo vimepatikana na vimeshaambatanishwa kwenye hati husika za malipo. Nakla za vielelezo hivyo zipo kwa ajili ya hatua muafaka

## Uchunguzi wa Kamati

Kamati imebaini kitengo cha uhasibu kutokuwa makini katika utendaji wake wa kazi kwa kushidwa kuweka vielelezo husika katika hati za malipo kwa wakati kinyume na Sheria.

Aidha Kamati ya LAAC imebaini kwa kutokuwepo kwa uhifadhi mzuri wa kumbukumbu za Ofisi kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (ZURA).

## Mapendekezo ya Kamati

Kamati inashauri kitengo cha uhasibu cha Mamlaka kufuata taratibu za kisheria na miongozo mbalimbali katika matumizi ya fedha za Serikali ikiwemo vielelezo vyote vya matumizi kuambatanishwa katika hati husika ya malipo.

Aidha Kamati inaishauri Mamlaka pamoja na watendaji wake kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa uwekaji na uhifadhi wa kumbukumbu za matumizi ya fedha za Serikali.

### 5.3.2 MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA)

**Taarifa ya Mapato**

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,811,300,200 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 2,208,011,671 kutoka vyanzo vyake vya ndani vya mapato sawa na asilimia 121.9 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati**

**Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini** kuna Fedha hii shilingi 125,388,153 inaonekana katika kipengele cha "Receipts' ukurasa wa 17 katika "Note' 2. Katika "Financial Statement" Fedha hii haikupaswa kuonekana katika taarifa ya Mwisho wa Hesabu ya Mwaka kutokana na Mamlaka kutoingiziwa fedha hizo katika akaunti ya Mamlaka isipokuwa Mamlaka walinufaika kwa wafunzo ya watendaji tu yanayohusiana na African Development Bank.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Mamlaka ya Kukuza Vitenga Uchumi Zanzibar (ZIPA kuandaa mpango wa kuwapatia mafunzo Wahasibu wake wa ndani ili kuwepa kuandaa Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka katika viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,678,292,950 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 2,708,126,280 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ya

Kukuza Uwekezaji Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 2,131,389,790 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 79.58 ya makadirio na kutumia jumla ya shilingi 648,782,500 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 23.96 ya makadirio.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kufanya matumizi kwa kuzingatia bajetia husika ili kuepusha matumizi ya fedha yaliopo katika vifungu vyengine kinyume na malengo yaliopangwa.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

**5.3.2.1 Kutokuboreshwa kwa mfumo wa kuhifadhia taarifa za Miradi**

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar inatumia mfumo maalum wa kuhifadhia taarifa za miradi za wawekezaji iliyopitishwa na Mamlaka kwa ajili ya kurahisisha ufuatiliaji na Usimamizi wa miradi hiyo. Mfumo huo unasaidia Mamlaka kupata taarifa muhimu za kila mradi tangu ulipoanza kusajiliwa hadi kufika tarehe husika au tarehe ya unapomalizika kwake.

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwazi katika miradi iliyopitishwa na Mamlaka. Aidha kunaweza kupelekea upotevu wa taarifa za miradi na hatimae kupelekea upotevu wa fedha za Umma.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka uhakikishe kwamba wanauboresha mfumo wa kuhifadhia taarifa za miradi za wawekezaji iliyopitishwa na Mamlaka ili uweze kuendana na wakati na uwezekutoa taarifa zote muhimu ambazo zitasaida Mamlaka kutekeleza kazi zake kwa uwazi na ufanisi zaidi.

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar inakiri kuwa mfumo uliokuwa ukitumika wakati wa ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 haukuwa na uwezo wa kuhifadhi taarifa

za Miradi na dhamira (intension) ya uwekezaji zilizokubaliwa au kukataliwa pamoja na maombia ya msamaha wa kodi kwa miradi iliyosajiliwa ZIPA. Mfumo wa awali wa kuhifadhia takwimu ambao unatumia program Excess ulikuwa na uwezo wa kuhifadhi takwimu za uwekezaji pale tu muekezaji anapopatiwa cheti cha uwekezaji takwimu hizo zikijumuisha, jina la mradi, kiwango cha uwekezaji, taarifa binafsi za muekezaji, eneo la uwekezaji, ajira pamoja na kiwango halisi kilichoekezwa.

Hata hivyo, kwa kuzingatia ushauri wa Serikali na kutatuwa changamoto za kuwa na taarifa kamili za uwekezaji kuanzia hatua ya kuwasilisha dhamira, ZIPA kupitia mfumo wake wa kuhudumia wawekezaji mtandaoni (http://ziew.zipa.go.tz) uliozinduliwa rasmi na Mhe. Dr. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imezingatia ukusanyaji wa taarifa hizo.

Kwa hatua ya sasa, muekezaji anapatiwa cheti cha uwekezaji kupitia mtandao, taarifa za dhamira zilizopokelewa, zilizokubaliwa na kukataliwa zote zinapatikana katika database ambayo imo katika mfumo huo.

Aidha, kwa upande wa taarifa za misamaha, uundaji wa mfumo unaendelea kwa kuunganisha mifumo ya taasisi nyengine (IMMIGRATION, PBRA, TRA, ZRA, NIDA na Vitambulisho vya Mzanzibar Mkaazi) kwa taasisi ambazo zipo katika kituo cha pamoja cha huduma (One Stop Centre) na hazina mifumo yake ya taarifa, ZIPA itaunda mifumo yao kwa mujibu wa Sheria, taratibu na takwimu ambazo zitatumika baina ya taasisi za kituo kimoja cha uwekezaji.

Kadhalika, kwa kuwa suala la utoaji misamaha ya kodi za miradi ya uwekezaji iliosajiliwa, ZIPA linahusisha taasisi nne kuu ZIPA, ZRA, TRA na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, ZIPA itunda mfumo wa kupokea na kujadili mambo hayo na baadae kufanya muunganiko (intergration) na mfumo wa utoaji misamaha kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ambao kwa sasa upo katika hatua za awali za uundaji.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imeridhika na hatua zilizochukuliwa katika kulitatua suala la uwekaji wa takwimu za wawekezaji katika mfumo ili kuhakikisha dhamira ya Serikali ya kuwa na taarifa sahihi za wawekezaji wote waliopo nchini inafikiwa.

Sambamba na hilo, kupitia hoja hii Kamati ya LAAC inaendelea kuishauri Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kuharakisha ukamilishaji wa uundwaji wa mfumo wa pamoja unaohusiana na taarifa za msamaha kwa taasisi zote zinazohusika kwa lengo la kuepusha upotefu wa fedha za Serikali.

**5.3.2.2 Dosari zilizobainika katika Matumizi ya Maeneo Huru ya Vitega Uchumi Maruhubi na Amani**

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa maeneo huru ya Vitega Uchumi Amani na Maruhubi hayatumiki vizuri kama ilivyokusudiwa kutokana na kubainika kuwepo kwa dosari mbali mbali zinazoashiria uwepo wa hali ya matumizi yasiyoridhisha hambapo dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

- Baadhi ya miradi ya uwekezaji kukosa sifa ya kuwepo katika maeneo hayo iwemo kukosekana kwa uchakataji wa bidhaa kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi.
- Kusokekana kwa udhibiti madhubuti wa uingiaji na utokaji katika maeneo hayo
- Baadhi ya miradi kutokufuata mipango yao ya asili iliyokubaliwa na Mamlaka.
- Hali hiyo inaweza kupelekea maeneo hayo kushindwa kufikia lengo la uanzishwaji wake.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka kuongeza bidii katika kuhakikisha kuwa maeneo huru ya uchumi yanasimamiwa, yanatunzwa na kuendelezwa ili lengo la kuanzishwa kwake

liweze kufikiwa kwa maslahi ya taifa.

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka imechukua hatua mbali mbali za udhibiti wa uingiaji na utokaji katika maeneo huru ya Vitega Uchumi ya Amani na Maruhubi kwa kuchukua hatua mbali mbali zikiwemo:

- Mamlaka imewataka wafanyakazi na Makampuni (Wawekezaji) wote waingie Maeneo hayo kwa kutumia Vitambulisho. Kwa wale ambao sio wafanyakazi wamewekewa daftari maalum la uingiaji na utokaji.
- Mamlaka imejenga uzio katika eneo la Amani na kukarabati eneo la Maruhubi kwa lengo la kudhibiti maeneo hayo.
- Mamlaka imefunga CCTV Camera kwa ajili ya uangalizi madhubuti wa Maeneo hayo.

**Miradi isiyofuata Mipango ya asili iliyokubaliwa na Mamlaka**

Kwa kipindi hiki, Mamlaka imeshaanza zoezi la kutoa barua kwa Miradi yote iliyobainika inayokwenda kinyume na makubaliano ya mikataba, na kuwataka Wawekezaji waendane na azma na malengo ya mikataba yao ya asili.

Mamlaka imewahakikishia Wawekezaji pamoja ba kuwaonya kuwa wote watakaokwenda kinyume na makubaliano ya asili miradi yao itafutwa,

Kwa kuongezea zaidi, Mamlaka inajitahidi kusajili miradi inayokwenda sambamba na azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Gari zilizopo eneo huru la Maruhubi.**

Taratibu za kuondoshwa magari hayo zimefanyika kwa kuuzwa gari hizo kupitia Mamlaka ya

Mapato Tanzania (TRA) kwa njia ya Mnada.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na hatua nzuri zilizochukuliwa na Mamlaka katika kudhibiti matumizi mabaya ya maeneo huru ya vitega uchumi kinyume na malengo yaliyokusudiwa, Kamati inashauri Mamlaka kuendelea kuyadhibiti maeneyo hayo ili yatumike kwa matumizi ya uwekezaji kama yalivyokusudiwa.

Aidha Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kumalizia mnada wa gari iliyobaki ili eneo hilo litumike katika uwekezaji wenye tija.

**5.3.2.3 Dosari zilizobainika katika matumizi ya vitabu vya risiti**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021 ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji inatumia vitabu vya risiti za zamani kwa ajili ya malipo ya 'gate pass' bila ya kufuata utaratibu wa kisheria ambapo katika ukaguzi huo dosari zifuatazo ziliweza kubainika

- Kutokupatikana kwa kumbukumbu za mapokezi ya vitabu hivyo ikiwemo idadi pamoja na sehemu vilipopelekwa kwa ajili ya matumizi.
- 'Logo' ya Mamlaka iliyomo katika risiti hizo ni ya zamani na tayari ishabadilika

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea upotevu wa mapato ya Mamlaka ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamaizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka kuhakikisha wanavifuatilia vitabu hivyo vya zamani ambavyo bado vinatumika kukusanyia mapato na kuanzisha utaratibu wa kutumia vitabu vya mapato vya kisasa vinavyotumika katika kukusanya mapato mengine ya Mamlaka.

Mchanganuo wa Vitabu vya Risiti hizo zilizobainika kubakia ghalani ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 103: Vitabu vya risiti vya zamani vya gate pass vilivyobakia ghalani**

| **mba** | **mbari za Risiti** | **di ya Vitabu** |
|---|---|---|
| | 251-26300 | |
| | 351-26400 | |
| | 401-26450 | |
| | 801- 27850 | |
| | 001-29950 | |
| | 001-30950 | |
| | 001-32950 | |
| | 001-33950 | |
| | 501- 34950 | |
| | 001-35950 | |
| | 001-36950 | |
| **nla** | | **7** |

## Majibu ya Mamlaka

Mamlaka inakiri kutumia vitabu vya kukusanyia mapato ya "Gate pass" vya zamani ambavyo ni vya muda mrefu ambavyo hata kumbukumbu za uingiaji vitabu hivyo hazipo pamoja na idadi ya vitabu hivyo kutokupatikana. Aidha, vitabu hivyo vina "Logo" ya zamani

katika risiti zake.

Mamlaka iliweza kuchukua hatua kwa kufuata ushauri wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kutakiwa kuvibadilisha vitabu hivyo na kwenda na wakati kisheria na kuangalia muundo pamoja na mfumo mpya wa Mamlaka.

Ingawa Mamlaka ilichelewa kuanza mchakato wa kuchapisha vitabu hivyo kutokana na kutokaa sawa kwa mfumo wa Manunuzi wa Serikali (e – pro) kwa upande wa ZIPA, lakini hivi sasa Mamlaka inatumia vitabu vipya vya "Gate pass" vinavyokwenda sambamba na muundo mpya vinavyotumia "Logo" mpya ya Mamlaka.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hiyo hata hivyo hatua zimeshachukuliwa na kwa sasa Mamlaka inatumia vitabu vipya vya "Gate pass" vinavyokwenda sambamba na muundo mpya vinavyotumia "Logo" mpya ya Mamlaka.

Kamati inasisitiza Mamlaka kuwa makini katika usimamizi wa mapato ya Serikali na kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamaizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**5.3.2.4 Kutokuonyeshwa kwa Wadaiwa wa miradi ya uwekezaji katika hesabu za mwisho wa mwaka, USD. 387,308**

Ukaguzi umebaini kuwa taarifa za fedha za Mamlaka kwa mwaka 2020/2021 hazikuonyesha madeni ya miradi ya wawekezaji yenye jumla ya Dola za Kimarekani 387,308 hali iliyopelekea taarifa za Hesabu za mamlaka kutokuonyesha uhalisia ambapo ni kwenda kinyume na viwango vya ufungaji wa hesabu vya kitaifa na Kimataifa.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka kufunga hesabu zao kwa kufuata miongozo ya kiuhasibu iliyopo Kitaifa na Kimataifa ili kuepusha kutokuonyesha uhalisia wa hesabu za

mwisho wa mwaka. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 104 : Miradi ya wawekezaji ambayo haikuonyeshwa katika hesabu za mwisho wa mwaka**

| Namba | a la Mradi | alizia Kulipa Deni | Deni Analodaiwa (USD) hadi 30 Juni, 2021 |
|---|---|---|---|
| 1 | oni Motor Co | 2017 | 15,8 |
| 2 | abi Motor | 2013 | 8, |
| 3 | ccess Motor | 2013 | 13,8 |
| 4 | kuna Matata Used Car | 2013 | 5,4 |
| 5 | ) Motor Used Car | 2013 | 3, |
| 6 | to Zone Tanzania | 2018 | 10,5 |
| 7 | mingo | 2013 | 7,( |
| 8 | y Motor | 2016 | 2,8 |
| 9 | eik Motors | 2018 | 10,7 |
| 10 | iwani Motors | - | 15, |
| 11 | e Horizon | 2017 | 172,5 |
| 12 | nahra | 2016 | 48, |
| 13 | REC | 2014 | 29,( |
| 14 | per Shine | 2014 | 3, |
| 15 | vannah Shed Rent | 2020 | 25,7 |
| 16 | ZAI Motor | 2018 | 11, |
| 17 | l Motors | 2016 | 2,5 |
| **Jumla** | | | **USD 387,** |

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka inakiri kuwa madeni ya miradi yenye thamani ya USD 387,30 hayakuonyeshwa kwenye hesabu za mwisho wa mwaka 2020/2021 na kupelekea hesabu hizo kutokuonyesha uhalisia wa hesabu za Mamlaka.

Sababu kuu ya kutofanya hivyo ni kuwa Mamlaka imeomba kufutwa kwa Deni hili ambalo ni la muda mredu wadaiwa wake ni wadaiwa sugu wanaotokana na sababu mbali mbali.

Hata hivyo, kwa hatua ya sasa deni hili linafanyiwa uhakiki na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya kuthibitisha kuwa ni deni sugu na linalostahiki kufutwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imebaini kuwa Mamlaka imewasilisha deni hilo Kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya uhakiki na kufutwa kwa deni, kwa kuamini kuwa wao ndio wenye Mamlaka ya kufuta deni bila ya kuwasilisha barua ya kufuta madeni hayo sugu kwa Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kama sheria inavyoelekeza.

**Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya Mamlaka ya kuwasilisha deni hilo kwa ajili ya uhakiki kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Kamati inashauri Mamlaka kuharakisha uwasilishwaji wa barua kwa Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kufutwa kwa madeni hayo.

Aidha Kamati inaishauri Mamlaka inapoandaa taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka ni vyema taarifa za madeni ya muda mrefu yaonekane katika taarifa hiyo kwa mujibu viwango vya ufungaji wa mahesabu wa kitaifa na kimataifa na kuondolewa kwake mpaka madeni hayo yafutwe kwa mujibu wa Sheria.

### 5.3.2.5 Kukokesakana kwa vielelezo vya mapato na matumizi ya fedha za Maendeleo shilingi 125,388,153

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Taarifa za fedha za Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 zimeonyesha kuwa Mamlaka imepokea mapato yenye jumla ya shilingi 125,388,153 kutoka kwa washirika wa maendeleo lakini vielelezo vinavyothibitisha mapato na matumizi ya fedha hizo havikuweza kupatikana kwa ajili ya ukaguzi.

Kufanya hivyo kunapelekea taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kutokuonyesha usahihi wa taarifa ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mamlaka kuhakikisha kuwa unafanya kazi zake kwa kuzingatia matakwa ya Sheria kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na kufanya utunzaji wa vielelezo vyote vinavyohusiana na masuala ya fedha ili viweze kupatikana wakati wa ukaguzi.

**Majibu ya Mamlaka**

Ni kweli kwamba katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mamlaka ilionyesha imepokea Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo yenye jumla ya shilingi 125,388,153. Ukaguzi ulibaini kuwa vielelezo vinavyothibitisha kupokea kwa Mapato haya na Matumizi yake havikupatikana kwa ajili ya ukaguzi hii ilitokana na Mamlaka haikupokea fedha hizi kwa njia ya fedha taslim wala katika hesabu (Account) yake yoyote, bali fedha hizi zilitokana na Mradi wenye jina ISPGG III ulikuwepo Wizara ya Fedha na Mamlaka iliweza kufaidika na sehemu ya mradi huo kwa watendaji wake kuweza kuhudhuria mafunzo yaliyoratibiwa na Wizara ya Fedha yaliyotokana na Mradi huo.

Aidha, malipo haya ya shilingi 125,388,153 yalilipwa na Wizara ya Fedha na waliohusika na kusimamia Mradi huo.

Mamlaka imeweza kufuatilia vielelezo vya malipo hayo na kupata vivuli vya hati za malipo na kuziweka kwa ajili ya kuthibitisha uhalali wa malipo hayo pamoja na kuziweka kama ni kumbukumbu kwa Mamlaka.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kuifuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC imegundua yafuatayo:

1. Fedha hii shilingi 125,388,153 inaonekana katika kipengele cha “Receipts’ ukurasa wa 17 katika “Note’ 2. Katika “Financial Statement”

2. Fedha hii haikupaswa kuonekana katika taarifa ya Mwisho wa Hesabu ya Mwaka kutokana na Mamlaka kutoingiziwa fedha hizo katika akaunti ya Mamlaka isipokuwa Mamlaka walinufaika kwa wafunzo ya watendaji tu yanayohusiana na African Development Bank.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Serikali ili kasoro kama hizi zisjitokeze tena Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuandaa mpango madhubuti wa kuwapatia mafunzo wahasibu wetu wa ndani ya taasisi kwa lengo la kuwasilishwa taarifa za Hesabu ya Mwisho wa Mwaka kwa mujibu viwango vinavyokubalika.

**5.3.2.6 Gari zilizowekwa katika Eneo Huru la Uchumi Maruhubi kwa muda mrefu pasi na kuingiza mapato kwa Mamlaka.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa katika eneo Huru la Uchumi Maruhubi zipo gari ambazo zimekaa kwa muda mrefu bila ya kuchukuliwa kwa hatua zinazofaa ikiwa ni pamoja

na kuuzwa au kufanyiwa matengenezo.Kufanya hivyo kunaweza kuikosesha Serikali mapato ambapo kunaongeza gharama za uhifadhi wa gari hizo

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka kufuatilia uwezekano wa kuzihamisha gari hizo kwenda eneo jengine nje ya Eneo Huru la Uchumi kwa vile haziingizi mapato yoyote kwa Mamlaka. Mchanganuo wa gari hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 105 : Gari zilizowekwa katika Eneo Huru la Uchumi Maruhubi Tangu miaka ya 2000**

| Namba | na la Kampun | ehe Ya KuingiaEn Huru la Uchumi | a Ya Gari | mba Ya Chasis | **ngi** |
|---|---|---|---|---|---|
| ROYAL MOTOR CO. LTD | | | | | |
| 1 | | P, 2012 | YOTA EMINA LUCIDA | R10-049351 | |
| 2 | | AY, 2014 | EWOOD | ATA486EY852624 | een |
| 3 | | AY, 2015 | IHHATSU YRV | LGM201931513821 | ite |
| 4 | | P, 2014 | SSAN PRIMERA | NBAAP120045227 | ver |
| 5 | | G, 2015 | SSAN PREMERA | NFEAP12U0132122 | ver |
| 6 | | R, 2014 | UXHALL FRONTERA | D5JMWL4SV703433 | een |
| 7 | | AY, 2017 | STUBISHI CANTER | 52EE560219 | ite |
| MTONI MOTOR CO LTD | | | | | |
| | | | | | |
| 8 | | 00 | RCEDES BENZ BRABAS | DD2193751A014449 | ck |
| 9 | | P, 2014 | IW | BAGH83451DP29820 | ck |
| ZENJI MOTORS CO LTD | | | | | |
| 10 | | AY, 2016 | XHOLLMOVANO | NFEAP11U0387299 | ite |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 11 | | C, 2012 | NZ BUS | DB6683222NO98005 | ver |
| 12 | | 16 | YOTA HIACE | 721LHB300097492 | d |
| 13 | | 12 | SSAN PREMERA | | ver |
| 14 | | 17 | SSAN MARCH | 12074557 | ange |
| 15 | | DV, 2019 | YOTA HIACE | H10-6009055 | hite |
| 16 | | DV, 2019 | YOTA PASSO | IC10-0045737 | hite |
| ISSZAH MOTORS CO LTD | | | | | |
| 17 | | B, 2014 | MW | BACS120X0AP76945 | ue |
| BREIK MOTORS CO LTD | | | | | |
| 18 | | N, 2015 | ECO | | |
| 19 | | N, 2015 | AZDA | ZDW192200308224 | |
| VISIWANI MOTORS CO LTD | | | | | |
| 20 | | | IWWOO | A4M11CE2C709074 | |
| **21** | | | **SSAN TERANO** | | |

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka inakiri kwamba katika mwaka 2020/2021 kulikuwa na gari ambazo zimekaa kwa muda mrefu katika eneo la Maruhubi bila ya kuchukuliwa hatua, kama jadweli linavyoonyesha hapo juu.

Kwa kufuata ushauri wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa kuzitaka kuzihamisha gari hizo na kuzipeleka eneo jengine kwa kuwa haziingizi mapato ya aina yoyote. Mamlaka ya Kukuza Vitenga Uchumi Zanzibar (ZIPA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wamefanikisha kuziondoa gari hizo kwa kuziuza kwa njia ya Mnada, isipokuwa gari moja tu aina ya IVECO ambayo bado haijapata mteja hadi muda huu na inaendelea kuwemo kwenye system ya Mnada ya TRA.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Mamlaka imeshachukua jitihada kubwa ya kuziondoa gari hizo kwa njia ya mnada hata hivyo Kamati imearifiwa kuwa imebaki gari moja tu ambayo ipo katika mchakato wa kuondolewa kwa mujibu wa sheria

Kamati inashauri Mamlaka kuharakisha ukamilishaji wa zoezi hilo ili kuokoa fedha za Serikali na kuwezesha maeneo hayo kutumika katika uwekezaji ulikusudiwa.

### 5.4.3 MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI

**Taarifa ya mapato**

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imekadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 525,367,200.Hadi kufi kia tarehe 30, Juni 2021 Mamlaka imekusanya jumla ya shilingi 1,066,062,658.56 sawa na asilimia 202.9 ya makadirio.

**Majibu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar**

Ni kweli katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mamlaka ilikusanya Jumla ya shilingi 1,066,062,658.56 kutokana na vyanzo vyake vya ndani ambazo ni sawa na asilimia 202.9 ya makadirio ya makusanyo kwa mwaka ya shilingi 525,367,200. Ongezeko la makusanyo halisi limetokana na sababu ifuatayo:-

Kuongezeka kwa vyanzo vya mapato ambavyo awali vilikuwa havijaingizwa katika bajeti ya mwaka 2020/2021. Kwa mwaka huo wa fedha, Mamlaka ilishinda zabuni ya kutengeneza vitanda vya Daya na Makunduchi na ulishaji wa chakula kutoka Baraza la Mitihani Zanzibar kwa ajili ya kuwaengezea mafunzo ya vitendo wanafunzi wa vyuo vya Mamlaka. Makadirio ya makusanyo ya vyanzo hivi vilikuwa havijaingizwa katika makadirio ya makusanyo katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/ 2021.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imebaini Mamlaka ya Mafunzo Amali Zanzibar kutojiamini katika ukusanyaji wa mapato katika baadhi ya vifungu vyake kama vile kifungu cha mapato mengineyo wamekisia kiwango kidogo cha mapato yatokanayo na Zabuni kwa kuamini kwamba huenda wakashindwa kupata zabuni mbalimbali zinazotolewa na baadhi ya taasisi za

Serikali kama vile zabuni ya utoaji huduma za chakula kwa walimu wanaosimamia mitihani ya taifa.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka katika kujiimarisha zaidi katika utoaji wa huduma mbalimbali ili waweze kuwa na ushindani mkubwa katika soko la zabuni zinatolewa na Tasisi mbalimbali za Serikali kwa madhumuni ya kuongeza mapato ya Mamlaka.

Aidha, Kamati inaishauri Mamlaka kuweka makadirio ya mapato yenye uhalisia kulingana na chanzo chenyewe na kuweka mikakati maalum ya kufikia makadirio waliojiwekea.

Vile vile, Kamati inaishauri Mamlaka katika kuongeza mapato ya ndani ni vyema kuongeza juhudi za uzalishaji mali zenye kiwango na ubora na kuweza kuleta ushindani katika soko, vilevile kubuni miradi mengine mipya ya uzalishaji kwa lengo la kuongeza fani mbalimbali ambazo hutolewa na vyuo hivyo ili kukidhi mahitaji ya soko kwa wakati huu na ujao.

**Taarifa ya Matumizi**

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,847,667,200 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 101,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufi kia tarehe 30, juni 2021 jumla ya shilingi 3,046,437,515 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 34.4 ya makadirio na shilingi 87,347,250 ziliingizwa na kutumika kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 86.5 ya makadirio

**Majibu ya Mamlaka ya Maunzo ya Amali Zanzibar**

Ni kweli Mamlaka katika kipindi cha mwaka wa fedha ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh 8,847,667,200/- kwa ajili ya utekelezaji shughuli zake mbali mbali na hadi unamalizika mwaka wa fedha 2020/2021, Mamlaka imeweza kutumia Jumla ya Tsh 3,919,910,015.82/-

(ikijumuisha mishahara, kazi za kawaida na miradi) katika shughuli zake mbali mbali ambazo ni sawa na asilimia 44.

Makadirio ya makusanyo yatokanayo na ruzuku ya matumizi mengineyo (Other Charge-O/C) kutoka Serikali Kuu yamepungua kulinganisha na Makadirio kwa mwaka na ndiko kulikopelekea Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya matumizi ambayo yalipangwa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Sababu kubwa ni kuwa mwaka wa fedha 2020/2021 ungonjwa wa UVIKO 19 bado ulikuwa unaendelea na umeathiri shughuli za kiuchumi katika Taasisi mbali mbali.

Kwa upande wa shughuli za maendeleo fedha zilitoka kwa wahisani wa maendeleo ambao ni FAWE ZANZIBAR kwa Mradi wa kilimo cha Mwani ambapo hadi kufikia 30 june 2021 walichangia sh 14,040,000.0 sawa na asilimia 28 ya makadirio na UNESCO walichangia sh 73,307,250 sawa na asilimia 143.74 ya makadirio.

Lengo kuu la mradi wa mwani kuwasidia vijana wa kike kuweza kupata taaluma ya uchumi wa buluu kwa upande wa ukulima na usarifishaji wa mwani. Na mradi wa UNESCO ni kuwasaidia walimu na vijana katika upande wa kilimo biashara na maendeleo ya ubunifu wa Viwanda.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini Mamlaka haikufikia malengo ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa kufanya matumizi ya asilimia 44 tu ya makadirio ya matumizi kutoka na uhaba wa upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo OC kutoka Serikalini kutokana na mripuko wa maradhi ya COVID 19 ambapo mamlaka ilikadiria kupokea Tzs 6,536,000,000 na kupokea Tzs 982,255,432 sawa na asilimia 15% ya makadirio na kupelekea shughuli nyingi za mamlaka kutekelezwa kwa kiwango cha chini na kutofikia malengo ambayo wamejiwekea.

Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuzipatia fedha za matumizi mengineyo OC/ kwa taasisi za Serikali kama zilivyopitishwa katika bajeti za mwaka husika kutokana na kupungua kwa mripuko wa maradhi ya COVID 19 duniani na hali za uchumi kuanza kuimarika ulimwenguni, aidha upatikanaji wa hafifu wa fedha za matumizi mengineo OC kunarejesha nyuma juhudi za Mamlaka katika kufikia malengo yake mbalimbali waliojiwekea.

**5.4.3.1 Malipo ya mishahara ambayo haikukatwa kodi shilingi 50,302,500.**

Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2014, mwajiri anapaswa kuzuia kodi (withholding tax) kwa malipo yote yatokanayo na ajira na kuwazilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 50,302,500 zimelipwa kwa watumishi (walimu) wa kutwa walioajiriwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa ajili ya kufundisha wa fani mbali mbali katika vyuo vya Amali, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokukatwa kwa kadi ya zuio katika mishahara ya walimu hao. Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na matakwa ya Sheria ya Kodi ya Mapato. Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali uhakikishe kuwa unasimamia na kutekeleza taratibu za kukata kodi kwa watumishi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo.

**Jadweli Nambari 112 : Malipo ya mishahara ambayo haikukatwa kodi**

| S/N | jina | Mahala | Mshahara | Muda Wa Mkataba | Kiasi cha mishahara |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ısoud Ali Salim | Mkokotoni | 717,000.00 | 6 | 4,302,( |
| 2 | amis Juma Khamis | | 509,000.00 | 6 | 3,054,( |
| 3 | na Moh’d Khamis | | 717,000.00 | 6 | 4,302,( |
| 4 | nifa A. Makame | | 717,000.00 | 3 | 2,151,( |
| 5 | a Abdalla Khamis | | 509,000.00 | 2 | 1,018,( |
| 6 | eman M Suleman | | 377,000.00 | 7 | 2,639,( |
| 7 | dall Khamis Ali | | 509,000.00 | 6 | 3,054,( |
| 8 | Bashir M.Moh’d | | 446,000.00 | 6 | 2,676,( |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 9 | Bakar Ali | Mwanakwerekwe | 399,500.00 | 6 | 2,397,( |
| 10 | um Sulema Seif | | 509,000.00 | 6 | 3,054,( |
| 11 | med Abdallah | | 399,500.00 | 5 | 1,997,! |
| 12 | tuni Suleman Ali | Vitongoji | 386,000.00 | 2 | 772,( |
| 13 | dhili Moh'd Haji | | 377,000.00 | 7 | 2,639,( |
| 14 | mza Moh'd Salim | | 717,000.00 | 5 | 3,585,( |
| 15 | M. Ali | | 717,000.00 | 6 | 4,302,( |
| 16 | na S. Ali | | 446,000.00 | 5 | 2,230,( |
| 17 | ade A. Masoud | | 509,000.00 | 5 | 2,545,( |
| 18 | sra A.Simai | | 717,000.00 | 5 | 3,585,( |
| | | | | | 50,302,! |

**Majibu ya Mamlaka ya Maunzo ya Amali Zanzibar**

Ni kweli kufuatia uhaba wa walimu katika vyuo vya mafunzo ya Amali, Mamlaka ya mafunzo ya ililazimika kuchukua walimu wa kutwa kwa lengo la kuwapatia vijana mafunzo kwa muda uliopangwa. Katika zoezi hili Mamlaka ya Mafunzo ya Amali inakiri kwamba iliwalipa mishahara walimu 18 waliokuwa wakifundisha katika vyuo vitatu vya MMA navyo ni:-Mwanakwerekwe, Mkokotoni na Vitongoji bila ya kuwakata kodi yenye thamani 2,726,640. Ushauri umefanyiwa kazi na kwasasa tatizo limesharekebishwa na walimu wote wa kutwa wanakatwa kodi kama sharia inavyoelekeza.Mfano ni Vocha ya malipo namba PV11/9 ya malipo ya walimu wa muda inathibitisha utekelezaji wa shauri lililotolewa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati.**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa walimu hao wameshamaliza mikataba yao na kwa sasa hawapo tena katika mikono ya mamlaka, hivyo basi itakua ngumu kuwapata walimu hao kwa lengo la kurudisha kiwango cha pesa kwa kila mmoja ambae alistahiki kukatwa kodi ya zuio (With holding tax)

Hata hivyo, Kamati inaishauri mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa vile wao ndio wamepewa mamlaka kwa mujibu ya sheria ya kodi Sheria ya mwaka 2014 kufanya zuio la

kodi kwa muajiri wake na hawakufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria. hivyo ni vyema Mamlaka kuwajibika kwa kuonana na uongozi wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania TRA kwa ajili ya kulipa deni hilo la Tsh 2,726,640 ili dosari hii isiweza kujitokeza tena kwa mara nyengine tena.

**5.4.3.2 Uhaba wa Walimu na Watendaji Muhimu katika Ofi si na Vyuo vya Mamlaka.**

Katika kufanikisha malengo ya Mamlaka ya kukuza na kushajiisha mafunzo ya amali kwa vijana, Mamlaka ilipatiwa vyuo viwili (Chuo cha Mafunzo ya Amali Makunduchi na Chuo cha Mafunzo ya Amali Daya Mtambwe) vya mafunzo ya Amali kutoka Serikali Kuu. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mamlaka inakabiliwa na uhaba wa walimu na watendaji wengine muhimu katika Ofisi zake ukilinganishana na mahitaji ya huduma inayopaswa kutolewa katika vituo hivyo.

Kuwepo kwa uhaba wa walimu na watendaji muhimu kunapelekea Mamlaka kushindwa kufikia malengo yake kwa ufanisi ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya Utumushi wa Umma Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kuchukua hatua za haraka za kupatikana kwa wafanyakazi wanaohitajika ili kuweza kuendana na mipango ya Mamlaka iliyopo kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuzingatia Sheria pamoja na miongozo ambapo itapelekea kuondokana na athari zinazoendelea kupatikana.

Mchanganuo wa taarifa za uhaba wa baadhi ya walimu na watendaji muhimu katika Ofi si za Mamlaka ni kama inaivyoonekana katika jadweli hapo chini:

JadweliNambari 113: Mchanganuo wa uhaba wa watendaji katika Mamlaka

| mba | dara | dadi ya Wafanyal liohitajika | di ya Wafanyal liopatikana | ungufu |
|---|---|---|---|---|

| mba | dara | dadi ya Wafanyak liohitajika | di ya Wafanyak liopatikana | ungufu |
|---|---|---|---|---|
| | sa | | | |
| | lezi wa Dakhalia(Matron) | | | |
| | reva | | | |
| | vangalizi wa Ofisi | | | |
| | sa Mitihani | | | |
| | hauri Nasaha | | | |
| | valimu wa Electronics | | | |
| | valimu wa Userem rpentry) | | | |
| | valimu wa Magari | | | |
| | utubi | | | |
| | valimu wa Kiingereza | | | |
| | valimu wa Dini | | | |
| | valimu wa Hesabu | | | |
| | valimu wa Ufundi Bomba | | | |
| | valimu wa Komputer | | | |
| | aidizi Mhasibu | | | |

**Majibu ya Mamlaka ya Maunzo ya Amali Zanzibar**

Ni kweli Mamlaka inakabiliwa na uhaba wa walimu na watendaji muhimu katika Taasisi kama ukaguzi ulivyobainisha. Hii ni kutokana na kuzuiwa kwa ajira za wafanyakazi 95 waliopangwa kufundisha katika vyuo vipya vya Mafunzo ya Amali Makunduchi na Daya. Ajira ambayo iliidhinishwa na Ofisi ya Raisi Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa barua ya tarehe 10 Ogasti 2020 yenye kumbukumbu Na. AB.80/234/01/52. Lengo likiwa ni kuhakiki Wafanyakazi halisi wa Serikali katika Wizara na Taasisi zote za Serikali.

Uongozi wa Mamlaka umetekeleza Ushauri uliotolewa na Wakaguzi ambapo Juhudi mbali mbali zilifanyika ili kuhakikisha vyuo vinapatiwa walimu ikiwemo pamoja na kufuata maelekezo yaliyotolewa na Baraza la Mapinduzi (BLM) la kuitaka Ofisi ya Raisi Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuisaidia Mamlaka kupata watumishi kupitia Wizara na Taasisi tofauti za Serikali. Maelekezo hayo ya BLM yanafuatia barua ya maombi kutoka Mamlaka kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya kuomba kupatiwa kwa dharua Wafanyakazi 95 kama ilivyokubaliwa kabla.

Zoezi la kuhamisha baadhi ya Wafanyakazi kutoka Taasisi nyengine lilifanyika na lilisaidia kidogo kwa kupata wafanyakazi wa kawaida kama walezi wa dahalia, Walimu wa Kiengereza na Dini. Walimu wa fani za ufundi na Ujasiriamali hawakupatikana. Katika mwaka wa Fedha 2021/2022 Mamlaka imepatiwa nafasi 20 tu za ajira mpya ambapo mchakato wa ajira umeshafanyika na Wanatarajiwa kuajiriwa baada ya kukamilisha upekuzi wa Kiusalama kutoka GOS. Nafasi hizo 20 ziliidhinishiwa kupitia barua yenye kumbukumbu Na. DB.117/157/01/30 ya tarehe 26th Julai 2022.

Hata hivyo, tatizo la uhaba wa Wafanyakazi hasa walimu wa fani za Ufundi bado halijamalizika. Zipo baadhi ya fani zitakuwa na mwalimu mmoja tu ambae anasifa ya

kufundisha fani husika. Mfano fani ya ufugaji, uvuvi na Ufundi wa zana za kilimo katika chuo cha Amali Makunduchi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kupata ufanunuzi zaidi wa hoja hii imeelezwa kuwa kwa mwaka huu wa fedha 2020/2021 Wizara imeomba kibali cha uajiri wa watumishi 4,000 na kupatiwa watumishi 2,000 na pia wanatarajia kupatiwa walimu wengine zaidi wakati Serikali ikiendelea na taratibu zake za kiutumishi hivyo basi mamlaka nayo haitokuwa nyuma katika kuongezewa idadi ya walimu wapya katika fani mbalimbali.

Hata hivyo, Kamati inaiomba Mamlaka kulifuatilia kwa karibu jambo hilo kwani uwepo walimu wa kutosha ndio msingi wa upatikanaji wa mafunzo hayo amali, bila uwepo wa walimu wa kutosha na wenye fani ni wazi kuwa wanafunzi wetu wanaweza kuhitimu bila ya kuwa na ustadi uliokomaa na kukosa ushindani katika soko la bidhaa na huduma watakazo toa kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Kwa ujumla.

**5.4.3.3 Dosari zilizobainika katika usimamizi na ufuatiliaji wa Mikopo.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kutekeleza jukumu la kuwahamasisha vijana kujiunga na Mafunzo ya Amali na kuwajenga katika maadili ya ujasirimali, kujiajiri na kujitegemea ambapo Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imetenga fedha ambazo zinatumika kuwapatia mikopo nafuu wahitimu wa Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa lengo la kuanzisha miradi yao mara tu baada ya kumaliza mafunzo yao. Dosari zilizobainika katika usimamizi na ufuatiliaji wa mikopo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukosekana kwa makabidhiano ya risiti zote za vifaa vilivyonunuliwa na Mkopaji kwa ajili ya mradi aliouombea mkopo kama inavyotakiwa katika kifungu cha 6 cha Mkataba wa Mkopo.

(ii) Mkopeshaji (Mamlaka) kutokutowa 'notisi' ya mwezi ya maandishi kwa Mkopaji aliyeshindwa kulipa deni kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 7, kifungu cha 8 na Kifungu cha 9 cha Mkataba wa Mkopo.

(iii) Mkopeshaji (Mamlaka) kushindwa kutoza faini ya asilimia 2% ya ziada ya kiasi cha mkopo kilichocheleweshwa kulipwa na Mkopaji kinyume na kifungu cha 13(b) cha Mkataba wa Mkopo.

(iv) Kukosekana kwa ufuatiliaji wa maendeleo ya mradi kila baada ya miezi mitatu kama ambavyo Mkopaji anavyopaswa kuripoti maendeleo ya mradi wake. Uwepo wa kasoro zilizobainishwa hapo juu zinaashiria udhaifu katika usimamizi na ufuatiliaji wa mikopo ya wahitimu na jambo linaloweza kupelekea kutokufikiwa kwa malengo ya mikopo hiyo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba unachukua hatua madhubuti katika kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mikopo ya wahitimu ili kuhakikisha kuwa malengo ya utoaji wa mikopo hiyo yanafikiwa. Mchanganuo wa vikundi vilivyokuwa na mkopo ndani ya mwaka fedha 2020/2021 ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 114 : Dosari zilizobainika katika usimamizi na ufuatiliaji wa Mikopo**

| Namba | a la Kikundi | lakilip | yaMradi | reheYa Mkc | Kiasi Cha Mkopo Kilichotolewa | asi cha Mkopo K cholipwa | Kiasi chaMkopo Kilichobaki | ilimia yaMarejes (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | veni Electronic rkshop | anyanya | ndi Elecctronik | 3/16 | 5,000 | 2,700 | 2,300 | 54 |
| 2 | Iuka rkshop | ıonda | remala | 3/16 | 3,500 | 1,725 | 1,774 | 49.3 |
| 3 | haraskaa perative | gwiPemba | a Vya Umeme luma | '20 | 8,649 | 450 | 8,199 | 5.2 |
| 4 | ga vices | ga | ndi gari | 3/16 | 7,445 | 3,035 | 4,409 | 40.8 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5 | hakarike pring | ke- ke | oni | 10/16 | 7,741 | 1,480 | 6,260 | 19.1 |
| 6 | ki Ni veli | ge Pale | oraji Na pambo | 2/17 | 5,000 | 2,970 | 2,030 | 59.4 |
| 7 | v eration | era ofaani | ndi tronic | 2/17 | 5,000 | 1,870 | 3,130 | 37.4 |
| 8 | olution perative | Kwere- e | ndi nputer | /17 | 5,000 | 1,330 | 3,670 | 26.6 |
| 9 | hekucha | Pemba | tufali | /18 | 9,180 | | 9,180 | 0 |
| **Jumla** | | | | | **56,515** | **15,561** | **40,953** | **27.5** |

**Majibu ya Mamlaka ya Maunzo ya Amali Zanzibar**

Uongozi wa Mamlaka umetekeleza ushauri uliotolewa na Mkaguzi kwa kuhakikisha kwamba hatua madhubuti zinachukuliwa katika kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa mikopo ya wahitimu ili kuhakikisha kuwa malengo ya utoaji wa mikopo hiyo yanafikiwa. Hatua hizo ni kama ifuatavyo:

(i) Moja ya masharti ya vikundi inavotakiwa kufanya baada ya kupatiwa mkopo ni kuwasilisha risiti za vifaa baada ya kununua vifaa watavyotumia katika miradi yao wanayoanzisha. Uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali umesimamia na kuchukua hatua katika suala zima la kudai risiti za wanavikundi zilizonunuliwa vifaa, vifaaa na risiti zao wanaziwasilisha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali katika suala hili wanavikundi wote wanapopewa mkopo wa Mamlaka.

(ii) Kwa mwaka wa 2021 kuna baadhi ya vikundi vilichelewesha kurejesha marejesho ya mikopo kwa utaratibu ambao walitakiwa kuufuta. Katika kuhakikisha vikundi vinarejesha mikopo yao kwa wakati Mamalaka ya mafunzo ya Mamlaka ilifanya juhudi mbalimbali za kuwajuilisha na kuwataka kulipata madeni yao. Miongoni mwa njia zilizotumika katika kudai madeni hayo ni pamoja na :- Kuwaandikia barua ya kuwakumbusha na kuwataka

walipe madeni yao kwa wakati Barua ya tarehe 14/07/20202,yenye kumbukumbu Na. P33/MMA/3/V0LII/03 inahusika. Pia, kufanyika vikao mbali mbali, Unguja na Pemba baina ya vikundi vya Wahitimu, masheha na maafisa wa Mikopo wa Mamlaka kwa lengo la kusisitiza malipo hayo.

(iii) Mamlaka ya mafunzo ya Amali hadi sasa haijatoza faini ya asilimia 2 kwa vikundi vilivyochelewa kufanya marejesho ya mikopo yao. Hii ni kutokana na lengo kuu la Mkopo husika ni kushajihisha na kuendeleza fani za ufundi ambazo wamejifunza katika vyuo vya Amali na waweze kujiajiri. Kifungu hicho kiliwekwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka kwa lengo la kuwafanya vikundi vilipe mikopo kuweza kurejesha mikopo yao kwa wakati na si kukifanyia kazi kama kinavyoonekana katika Mkataba. Msisitizo huo pia umetolewa zaidi na kikao cha 49 cha Bodi ya Wakurugenzi.

(iv) Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ina seksheni maalum ya Mikopo na Uzalishaji ambapo maofisa wake wanafanya ziara kwa kila baada ya miezi mitatu ya kuvitembelea vikundi vyote Unguja na Pemba vilivyopatiwa mikopo na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa lengo la kuangalia maendeleo na changamoto zinazowakabili katika miradi yao na ripoti za ufuatiliaji huo kwa kila robo mwaka huwa zinawasilishwa katika vikao vya Bodi kwa ajili ya kujadiliwa. Pia Maafisa wa mikopo wanafanya ziara maalum kwa vikundi husika na kuwafanyia mikutano pale haja inapojitokeza.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini mambo yafuatayo;

Baadhi ya miradi ya vikundi kushidwa kufanya kazi kabisa kutokana na kutofanyiwa uchunguzi wa awali na kubaini iwapo mradi unaweza kutekelezeka kwa hali halisi ya eneo ambalo linatariwa kufanyika kwa mradi kwa mfano kikundi cha Kumekucha cha Ole Pemba Kilichojikita katika shughuli za utengenezaji wa matofali kimeshindwa kurejesha mkopo

hata kwa asilimia moja kutokana na kushindwa kuendelea na mradi baada ya kukosa nishati ya Umeme ya (three phase) ambayo ndio iliyokuwa inahitajika kwa mujibu ya vifaa hivyo ambavyo wamevinunua kwa mkopo waliopatiwa na Mamlaka.

Vilevile Kamati imebaini Mamlaka Kutosimamia vyema vifungu vya masharti mkataba kama vile kutoza faini ya asilimia 2% ya ziada ya kiasi cha mkopo kilichocheleweshwa kulipwa na Mkopaji kinyume na kifungu cha 13(b) cha Mkataba wa Mkopo

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Mamlaka kufanya ufuatiliaji wa karibu wa aina mradi na vifaa vitakavyotumika katika eneo la mradi ili kubaini halisi ya mazingira kama inaendana na utekelezaji wa mradi unaotarajiwa kufanyika, ili kama kuna changamoto zozote katika eneo la mradi waweze kuzipatia ufumbuzi mapema kabla ya kuekeza mradi husika kwa lengo la kuepusha mradi kushidwa kufanya kazi na kusababisha kutorejeshwa kwa mikopo hiyo.

Kwa vile Mamlaka ina lengo zuri kwa wanafunzi wanahitimu mafunzo hayo kwa kuwawezesha kuwapatia mikopo kwa lengo la kujiendeleza katika fani ambazo wamepatiwa. Kamati inaishauri Mamlaka kuweka usimamizi mzuri wa urejeshaji wa mikopo hiyo ili iweze kuleta tija kwa wanavikundi na kuweza kurejeshwa kwa wakati ili kuendelea kuwahudumia wahitimu wengine ambao watahitaji mikopo hiyo

Aidha kamati inaishauri Mamlaka kufuata masharti ya vipengele vya mkataba kama ilivyojiwekea na kama kuna kipengele kinaleta ukwasi katika utekelezaji wake ni vyema kukiondoa kwa kufanya marekebisho ya mkataba na kuweka kipengele ambacho kitaweza kutekelezeka na si vyenginevyo.

**MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI PEMBA**

**5.4.3.4 Kukosekana kwa mapato ya utowaji wa huduma shilingi 57,406,000.**

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba inawadai jumla ya shilingi 57,406,000 kwa ajili ya utowaji wa huduma kwa baraza la mitihani Zanzibar hali ambayo imepelekea kutopatikana kwa mapato yalikusudiwa na hivyo kushindwa kutowa huduma mbali mbali zinazohitaji matumizi ya fedha yaliyokusanywa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya mafunzo ya Amali - Pemba kufanya juhudi za ufuatiliaji wa mapato yaliyokosekana kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo kuhusu umuhimu wa upatikanaji wa mapato hayo. Mchanganuo wa mapato yaliyokosekana kutokana na utowaji wa huduma ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

| Mwaka wa fedha | Jina la Mdaiwa | (iasi cha fedha kinachodaiw (Tshs) |
|---|---|---|
| )18/2019 | Baraza la Mitihani | 29,200,000 |
| )20/2021 | | 28,206,000 |
| **Jumla** | | **47,406,000** |

**Majibu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba**

Mwaka 2018/2019 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar kupitia Chuo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni ilipata kazi ya usambazaji wa chakula cha wanaosainisha mitihani ya darasa la nne (4) la sita (6) na form (2). Aidha Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji kiliwekwa kama kisaidizi cha Chuo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni kwa usambazaji wa

chakula kwa upande wa Pemba katika kituo cha FIDEL CASTRO. Deni lililokuwepo lilikuwa ni la Addendum lenye kiwango cha shilingi 39,100,000/- . Na kwa sasa deni hilo limelipwa na tayari fedha hizo zimeshahaulishwa kupitia akaunti ya Chuo cha Amali Vitongoji.

Kwa mwaka 2020/2021 Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kupitia vyuo vyake ilifanikiwa kupata zabuni ya usambazaji wa chakula kutoka Baraza la Mitihani Zanzibarambapo zabuni iliotangazwa yenye kumbukumbu namba SMZ/K01/NC/NRT/2020-2021/21 & 22 na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kufanikiwa kupata loti tatu (3) katika loti zilizotangazwa zenye uchambuzi ufuatao.

I. Loti namba tatu (3) na loti namba (4) zilisimamiwa na Chuo cha Amali Mkokotoni
II. Loti namba tano (5) ilisimamiwa na Chuo cha Amali Vitongoji.

Hivyo basi, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kupitia zabuni iliotajwa hapo juu, Mamalaka ya Mafunzo ya Amali kupitia Chuo cha Amali Vitongoji ambayo ilishinda loti namba tano (5) yenye thamani ya shilingi 80,586,000/- na mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha unaoishia JUNI 30, 2021, Chuo Cha Amali Vitongoji kilikuwa kimeshalipwa jumla ya Shilingi 52,380,900 na Jumla ya shilingi 28,205,100/- bado hazijalipwa mpaka sasa.

Tunakubalina na ushauri ya Mkaguzi kufanya juhudi za ufatiliaji wa mapato yaliokosekana, hata hivyo juhudi zilimechukuliwa kwa kuandikia barua yenye kumb. No P33/MMA/1/VOL.IV/20 ya tarehe 17/2/2021 inayoelezea kukutana na wahusika na kufanya ukaguzi wa kina kwa waliosimamia chakula cha walimu waliosahihisha mitihani na barua yenye kumb. No P33/MMA/PDMU/VOL.I/07 ya terehe 22/1/2021 inaelezea kukumbushia madeni yote lakini mpaka muda huu hawajalipa.

Hata hivyo baraza la Mitihani limeenda kinyume na mkataba wa makubaliano wenye No. SMZ/KO1/NC/NRT/2020-2021/21&22 yenye jumla ya sh 80,586,000/- kilicholipwa ni sh 52,380,900/- na kilichobaki sh 28,205,100/- hadi sasa fedha hizi hazijapatikana.

**Uchunguzi wa Kamati.**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kwamba kiwango cha deni ambalo Mamlaka inadai kutoka Baraza la Mitihani la taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ni la Addendum lenye jumla ya Tzs 39,100,000 na sio kiwango cha fedha cha Tzs 29,200,000 ambacho kimeripotiwa na Mkaguzi hata hivyo deni hilo tayari limeshwalipwa lote

Aidha Mamlaka imethibitisha kuwa kiwango cha deni walichokuwa wanadai kutoka Baraza la Mitihani la Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni Tzs 80,586,000 na sio deni la Tzs 28,206,000 kama ilivyoripotiwa na Mkaguzi ambapo hadi kufikia 30 Juni 2021 kiasi cha deni la Tzs 52,380,900 limelipwa na Kwa sasa Mamlaka inadai deni lenye jumla ya Tzs 28,205,100 tu na sio deni la Tzs 47,406,000 kama alivyoripoti Mkaguzi katika kitabu chake.

Hata hivyo kamati imeendelea kuhoji juu ya sababu ya utofauti huo wa uwasilishaji wa deni baina ya Mamlaka na Mkaguzi na kamati kubaini kuwa Mamlaka ya Mafunzo Amali Pemba imewasilisha barua za majibu ya hoja za Mkaguzi yani 'Management letter' na katika barua hiyo Mamlaka kwa upande wa Pemba imekiri kuwa inadai kiwango hicho cha deni ambacho mkaguzi amekiripoti bila kufanya mawaliano na Uongozi wa Mamlaka Makao makuu Unguja ambao wao ndio wenye taarifa sahihi za deni hilo.

**Mapendekezo wa Kamati**

Kamati inazishauri taasisi za Serikali ambazo Makao Makuu yake yapo Unguja kufanya kazi kwa pamoja na kuimarisha mawasiliano ya ndani wakati wanapojibu hoja za mkaguzi ili kuepusha upande mmoja kutoa taarifa ambazo zinatofautiana na taarifa za upande mwengine.

Aidha kamati inasisitiza endapo taasisi kutoka Pemba zinapofanya uwasilishaji wa hoja za mdhibiti ni vyema kuwasilisha majibu hayo katika uongozi wa juu wa Mamlaka au taasisi ili kujiridhisha iwapo taarifa zilizotolewa ni sahihi au sio sahihi ili waweze kufanya marekebisho kabla ya kuwasilishwa kwa mdhibiti na mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali ili kuepusha dosari kama hizo kutokea.

Kwa upande mwengine kamati inashauri uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa vile taasisi hizi mbili ziko chini yake ni vyema kuitisha kikao baina Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Baraza la Mitihani Zanzibar kulipatia ufumbuzi kiwango cha deni kilichobakia ambacho hakijalipwa hadi sasa licha ya kuwa jitihada za kulifuatilia deni hilo zinaendelea upande wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar.

**5.4.3.5 Ucheleweshwaji wa upelekaji wa mapato benki shilingi 2,420,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 2,420,000 zimakusanywa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba kupitia katika vianzio vyake mbali mbali vya mapato lakini mapato hayo yamecheleweshwa kupelekwa benki hali ambayo inaweza kupelekea matumizi ya fedha hizo kinyume na utaratibu pamoja uwepo wa uwezekano wa upotevu wa fedha zilizokusanywa na kushindwa kutoa huduma bora zilizokusudiwa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 56(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa

Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato yaliyocheleweshwa kupelekwa benki ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 116 : Mapato yaliyocheleweshwa kupelekwa Benki.**

| a Maku- sanyo | mba ya fomu | Kiasi cha Fedha kilichokusanywa (Tshs | arehe iliy- elekwa benki | elezo |
|---|---|---|---|---|
| /12/2020 – /1/2021 | 1971-002110 | 600,( | /2021 | dha kwa ajili ya zaji wa fomu za iunga. |
| 2/2021-5/2/2021 | 0360-000400 | ),000 | /2/2021 | |
| 2/2021- /2/2021 | 0401-000703 | 1,620,( | /2021 | |
| /1/2021 | 2111-002130 | 100,( | /2021 | |
| **Jumla** | | **2,420,(** | | |

## Majibu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali inakiri kukusanya fedha zenye thamani ya shilingi 2,420,000.00 ambazo zilitokana na mauzo ya fomu za kujiunga na Chuo kipya cha Mafunzo ya Amali Daya. Ucheleweshwaji wa upelekaji wa mapato benki yaliyotokana na uuzaji wa fomu ulisababishwa na;-

Kukosekana kwa mshika fedha wa Chuo na kupelekea kazi ya uuzaji wa fomu kufanywa na uongozi wa chuo ambao ulikuwa mpya katika masuala ya uongozi na usimamizi wa fedha.

Kwa sasa tatizo hilo limeshapatiwa ufumbuzi kwa kufuta malipo kwa utaratibu wa fedha kwa njia ya mkononi (cash) na kuanzisha utaratibu wa malipo kupitia nambari za hesabu za

benki moja kwa moja barua ya tarehe 15/07/2022 yenye kumbukumbu namba MMA/P/OUT/Vol.I/21/01 na ya tarehe 23/11/2022 yenye kumbu kumbu namba MMA/P/OUT/15/Vol.IV/97 zinahusika.

Aidha uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ulifanya juhudi za ziada na za kutafuta mshika fdha kupitia barua ya tarehe 09/04/2021 yenye kumbukumbu namba VTA/P/OUT.15/VOL.III/88 na kufanikiwa kupatiwa nd. Zuwena Said Soud, barua ya tarehe 15/4/2021 yenye kumbukumbu namba CAB.450/485/01/A/14, kutoka OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO inahusika. Pia chuo kilifanikiwa kupata account yake.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inakubalina na hoja ya Mkaguzi hata hivyo kamati inaifuta hoja hii kwa vile Mamlaka tayari imeshachukua jitihada za kumtafuta mshika fedha na kufanikiwa kumpata nd. Zuwena Said Soud ambae kwa sasa anaendelea na kazi zake na tunategemea changamoto zilizojitokeza kutokana na ukosefu wa Mshika fedha wa Chuo zitaondoka.

Sambamba na hayo Kamati inaishauri Mamlaka na taasisi za Serikali kutofanya kazi kwa mazoeza bali wafanye kazi kwa mujibu wa sheria zilizowekwa serikali aidha kama kutakuwa na changamoto ya ukosefu wa mfanyakazi mwenye taaluma Fulani basi ni vyema mamlaka iwasiliane na uongozi wa juu ili kulipatia ufumbuzi suala hilo badala ya kuteua mtu au kikundi cha watu kufanya kazi ambazo hawana taaluma nazo ambazo hupelekea kuvunja sheria na kupelekea dosari kama hizi kutokea

**5.4.3.6 Kukosekana kwa mkataba wa mkopo shilingi 24,776,750.**

**Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali** Zanzibar imetoa mkopo wa kiasi cha shilingi 24,776,750 kwa ajili ya kuanzisha mradi wa matufali katika Chuo cha Amali Vitongoji Pemba lakini Mamlaka haina mkataba wa mkopo huo hali

ambayo imepelekea hadi ukaguzi unakamilika jumla ya shilingi 16,337,192 ni bakaa ya fedha ambazo hazijalipwa ikiwa ni sawa na asilimia 65.94 ya fedha iliyokopeshwa.

Dosari iliyobainika ni kutokuwepo kwa mkataba ulioingiwa baina ya mamlaka ya Mafunzo ya Amali na chuo cha mafunzo ya Amali Vitongoji na kupelekea kutokuwepo kwa nguvu za kisheria katika uwasilishwaji wa madai ili kuweza kupata kiasi cha fedha kilichokopeshwa kwa ajili ya uwendelezaji na utekelezaji wa shughuli nyengine za Mamlaka. kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar**

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ina mikakati ya kuendeleza vyuo vyake viwe vinafanya shughuli za Uzalishajimali kupitia miradi yake inayoanzisha na pia kuengeza fursa ya mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa fani husika. Ili kufikia adhma hiyo Chuo cha Vitongoji kupitia fedha za ALSD I kilipatiwa TSH 24,776,750 kama revolving fund kwa ajili ya kuanzisha mradi wa matofali.Utaratibu mzima wa kuendesha shughuli za Uzalishajimali za vyuo vya Mamlaka ya Mafunzo ya Amalina jinsi ya kurejesha fedha hizo umeelezwa na Muongozo wa Uzalishajimali wa vyuo vya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji ni sehemu ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ambayo inaongozwa na Miongozo iliyopitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, hivyo Mamlaka ya Mafunzo ya Amali haikuona haja ya kujifungisha Mkataba.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatila hoja hii imebaini kuwa Mamlaka hutoa fedha yani 'revolving fund' na sio mkopo kama ulivyoripotiwa na Mkaguzi fedha hizo hutolewa na Mamlka kwa lengo la kuviwezesha vyuo vyake katika kuendeleza shughuli za uzalishaji na kuongeza makusanyo

ya mapato ya Mamlaka na kunakuwa na utaratibu wa kurudisha fedha hizo kwa mujibu wa muongozo wa Mamlaka kifungu namba 7

Hata hivyo Mamlaka haipingani na hoja ya Mkaguzi lakini inaifuta hoja hii kwa vile Mamlaka haitoi mkopo kwa vyuo vyake na hutoa 'revoving fund' kilochosababisha uwepo wa hoja hii ni Mamlaka kushindwa kuzipatia jina sahihi fedha hizi na kuziita mkopo ambapo Mkaguzi alipobaini Mamlaka imetoa mkopo alihitaji kupatiwa mkataba wa mkopo baina ya Mamlaka na vyuo vyake na kushidwa kupatiwa hivyo basi hoja hii imeweza kuandikwa katika kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mapendekezo ya kamati**

Kamati inashuri uongozi wa Mamlaka kurekebisha neno mkopo na kutafuta lugha nzuri ya kuita fedha hizi ambazo huzitoa kwa vyuo vyake kwa lengo la kuviwezesha, ili mkaguzi anapokuja kukagua na kuelezwa fedha hizi ni mkopo atahitaji kuona mkataba wa mkopo na taratibu zake na anaposhidwa kupatiwa mkataba huo itapelekea dosari hii kujitokeza tena. Aidha, marekebisho hayo yaende sambamba na marekebisho ya neno mkopo ambalo lipo katika muongozo Mamlaka unaotoa ufafanuzi wa utolewaji na urejeshwaji wa fedha hizo.

Vile vile Kamati inaishauri Mamlaka na Taasisi za Serikali katika kutoa mashirikiano mazuri baina yao na wakaguzi wakati wa kujibu hoja za mkaguzi kwani kamati inaamini kuwa mashirikiano hayo yataleta tija kwa kupatikana ufafanuzi mzuri wa kila hoja na kwa zile hoja ambazo zitakuwa na mapungufu ya kibinaadamu zitaweza kupatiwa ufumbuzi katika vikao vya mkaguzi na mkaguliwa na hoja pekee zitakazoripotiwa ni zile ambazo zimekosa majibu ya kuridhisha kwa Mkaguzi.

### 5.4.4 MAMLAKA YA UHIFADHI WA MJI MKONGWE ZANZIBAR

**Taarifa za Mapato**

Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 920,100,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi za kawaida. Aidha Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 30,000,000 kutoka vyanzo vyake vya ndani vya mapato.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi 587,316,746 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 63.81 ya makadirio. Aidha Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 53,760,000 kutoka vyanzo vyake vya ndani ikiwa ni sawa na asilimia

179.2 ya makadirio na ilikusanya jumla ya shilingi 111,952,015 ikiwa ni mapato mengineyo.

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka haikuandaa taarifa ya moja kwa moja kuhusiana na Taarifa ya Mapato, hata hivyo, Mamlaka ilitoa ufafanuzi juu ya maswali mbali mbali yaliyoulizwa na Kamati kwenye masuala ya mapato.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia Taarifa hii Kamati iliomba kupatiwa sababu zilizopelekea Mamlaka hii kukusanya mapato zaidi ya asilimia mia, ambapo ilielezwa kuwa mapato ya Mamlaka yaliongezeka kutokana na kuongezeka kwa vibali vya biashara, ujenzi, ukarabati wa

majengo na kutozwa faini kwa vyombo vya moto vilivyoingia katika eneo la Mji Mkongwe kinyume na utaratibu.

Vile vile, Kikao kilibaini kuwa mapato ya Mamlaka huingizwa kwenye hesabu ya benki yenye jina la Katibu Mkuu wa Wizara husika, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu. Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC imeitaka Mamlaka kuingiza fedha hizo kwenye hesabu ya benki ya Mamlaka kwa kuwa Mamlaka ina hesabu ya benki inayohusiana na mapato.

**Taarifa za Matumizi**

Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 920,100,000 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 762,067,691 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 82.82 ya makadirio.

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka haikuandaa moja kwa moja Taarifa ya Matumizi, hata hivyo, Mamlaka ilitoa ufafanuzi juu ya maswali mbali mbali yaliyoulizwa na Kamati.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia Taarifa ya Matumizi, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ina makosa kadhaa ikiwemo; "Note" moja kuwa na zaidi ya jina moja kwa mfano "Note 10" inasomeka kuwa ni Óther Payment na "Routine Maintenance and Repair", jambo ambalo ni kinyume na taratibu za ufungaji wa hesabu.

Kutokana na dosari hiyo, Kamati ya LAAC inaitaka Mamlaka kuwa makini wakati inaandaa Taarifa hiyo ili Taarifa hizo zikidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

Aidha, Kamati ya LAAC inazidi kuiomba Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwapatia mafunzo mara kwa mara Wahasibu ili waendane na wakati.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 5.4.4.1 Majengo ndani ya Eneo la Hifadhi la Mji Mkongwe ambayo yapo katika Hali Mbaya

Mji Mkongwe ni moja wapo ya miji mikongwe zaidi ya Afrika Mashariki, wenye sura ya kipekee ikiwemo vichochoro vyembamba na majengo mazuri ya asili na ndio kitovu cha utamaduni wa Zanzibar. Kwa mujibu wa kifungu nambari 7(f) cha Sheria Nambari 4 ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ya mwaka 2010, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar ina jukumu la kuhakikisha matumizi bora ya majengo ya Mji Mkongwe pamoja na matengenezo ya majengo yaliyomo katika eneo la hifadhi.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa majengo mengi ndani ya eneo la hifadhi ya Mji Mkongwe ambayo yapo katika hali mbaya na yamekosa matumizi yaliyo bora na salama ili kuilinda hadhi na haiba ya mji huo. Majengo hayo yanamilikiwa na taasisi za aina tatu ambazo ni Watu Binafsi, Shirika la Nyumba Zanzibar na Kamisheni ya Wakfu.

Kuwepo kwa majengo yaliyo katika hali mbaya ndani ya eneo la hifadhi la Mji Mkongwe kunaweza kupelekea kuanguka kwa majengo hayo na hatimae kupoteza haiba na sura nzima ya mji huo wa urithi wa utamaduni.

**Orodha ya majengo ndani ya Eneo la Hifadhi la Mji Mkongwe ambayo yapo katika hali mbaya**

| Nam. | Namba ya Nyumba | Eneo iliyopo | Mmiliki | Matumizi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 542 | Shangani (Tausi hotel) | Binafsi | Haitumiki |
| 2. | 539 | Shangani (Tausi hotel) | Binafsi | Haitumiki |
| 3. | 341 | Shangani (Minara miwili) | Binafsi | Inatumika |
| 4. | 300-302 | Shangani | ZHC | Inatumika |
| 5. | 353 | Gizenga (Sheha Shangani) | ZHC | Inatumika |
| 6. | 2410 | Vuga | Binafsi | Inatumika |
| 7. | 4402 | Mkunazini | ZHC | Inatumika |
| 8. | 1724 | Mkunazini (Kanisani) | ZHC | Inatumika |
| 9. | 1822B | Mkunazini | ZHC | Inatumika |
| 10. | 1572 | Mchambawima | ZHC | Haitumiki |
| 11. | 1956/57 | Kiponda | Wakfu | Inatumika |
| 12. | 1472/1473 | Kiponda | Wakfu | Inatumika |
| 13. | 807 | Kiponda | Shia | Haitumiki |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14. | 1455 | Kiponda | Binafsi | Haitumiki |
| 15. | 1228 | Kokoni | ZHC | Inatumika |
| 16. | 712/717 | Malindi (Jumba la Washihiri) | Wakfu | Inatumika |
| 17. | 1193 | Malindi (Karibu na Zanzibar cable) | Binafsi | Inatumika |
| 18. | 1198/99/1200 | Malindi | Binafsi | Inatumika |
| 19. | 1188/90 | Malindi | ZHC | Haitumiki |
| 20. | 681 | Malindi | ZHC | Inatumika |
| 21. | 890 | Malindi | Binafsi | Haitumiki |
| 22. | 2515 | Mtendeni | ZHC | Inatumika |
| 23. | 2801/2811 | Mtendeni (Jumba Maro) | Wakfu | Inatumika |

**Majibu ya Mamlaka**

Ni kweli baadhi Majengo ndani ya Mji Mkongwe yapo katika hali mbaya kiasi cha kuweza kuhatarisha maisha ya watu na samani za Mji Mkongwe. Mji Mkongwe una majengo yanayomilikiwa na taasisi tofauti zikiwemo Taasisi za Serikali, kama Shirika la Nyumba, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na watu binafsi, jukumu la ukarabati wa majengo ndani ya eneo hili ni la wamiliki wenyewe. Mamlaka ya Mji Mkongwe ina jukumu la kusimamia na kutoa ushauri wa kitaalamu katika ujenzi au ukarabati wa majengo hayo.

Katika kupambana na hali ya majengo yaliyopo katika hali mbaya, Mamlaka imepanga Mikakati ifuatayo;-

1. Kutangaza fursa kwa wawekezaji kuchukua baadhi ya majengo na kuyaimarisha kwa lengo la kuyaendeleza kwa matumizi kama Mpango Mkuu wa Uhifadhi na Urithi unavyoelekeza.
2. Kuanzisha kwa Mfuko wa Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe 2021 ili kutumia fedha za Mfuko huo kuimarisha eneo la Hifadhi ya Mji Mkongwe.
3. Kuwasiliana na wamiliki wa majengo hayo kwa ajili ya kuchukua hatua mbali mbali za kuyahami.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Mamlaka imetumia fedha zilizobakia katika mwaka wa fedha uliopita (2019/2020) bila ya kupata ruhusa ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kama taratibu zinavyoelekeza.
2. Mamlaka imefanya matumizi kwa kufanya ukarabati mkubwa jengo la Skuli ya Hurumzi lililogharimu Tsh. 11,626,540, jengo linalotumiwa na Bodi ya Kondominium lililogharimu Tsh. 35,397,026 na kufanya ukarabati mdogo jengo la Mahakama Kuu Vuga lililogharimu Tsh. 3,135,800 fedha ambazo hazionekani kwenye Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka kama Mamlaka imepokea fedha hizo kwa ajili hiyo.
3. Endapo mmiliki wa jengo hana uwezo wa kufanya ukarabati Mamlaka hutoa baadhi ya huduma bure ili zoezi la ukarabati lifanyike, kwa mfano Mamlaka hutoa majukwaa, kibali, hupaka rangi na kadhalika.

4. Ukarabati umefayika kwa majengo matano tu kati ya majengo 23 yaliyotajwa na Mkaguzi Mkuu. Majengo yenyewe ni kama yafuatayo:
    a. Nyumba namba – 542
    b. Nyumba namba – 539
    c. Nyumba namba – 807
    d. Nyumba namba – 1188/90
    e. Nyumba namba – 890

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hizo zisijitokeza tena katika siku zijazo Kamati ya LAAC imependekeza yafuatayo:

1. Mamlaka iendelee na jitihada ya kuyafanyia ukarabati majengo yake na kuwataka wamiliki wa majengo yaliyopo katika eneo la Mji Mkongwe kuyafanyia ukarabati majengo yao ili kulinda hadhi ya mji huo kama kanuni ya 19(1) ya Kanuni za Jumla za Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ya mwaka 2023 inavyoelekeza.
2. Mamlaka itoe muda maalum kwa watu binafsi wenye majengo katika Mji Mkongwe kuyafanyia ukarabati majengo yao ili kuepusha mvutano usio wa lazima kanuni ya 19(2) na (3) za Kanuni za Jumla za Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ya mwaka 2023 zinavyoelekeza.
3. Mamlaka ihakikishe kuwa inafanya matumizi yake kwa kufuata taratibu za fedha zilizopo ili kuepusha kupata hoja zisizo na msingi.

### 5.4.4.2 Manunuzi/huduma zilizolipwa kwa Taasisi zisizosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, shilingi 12,225,000

Kwa mujibu wa Kifungu nambari 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinazitaka taasisi zenye kutoa huduma au uuzaji wa bidhaa kusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ili ziweze kushiriki katika manunuzi ya umma. Vile vile kifungu nambari 23(2), kinakataza manunuzi kufanywa kwa watoa huduma au wauzaji bidhaa ambao hawajasajiliwa.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar imefanya malipo kadhaa kwa mafundi ambazo hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar.

Kufanya malipo kwa wauzaji bidhaa au watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 na kunaweza kupelekea kupoteza mapato ya Serikali.

**Manunuzi yaliyofanywa kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma**

| Hati Nam. | Aliyelipwa | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tsh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| D8/10 | Salum Ali Yussuf | 3,700,000 | Malipo ya ununuzi wa honda |
| 9/10 | Ali Juma Hamad | 3,825,000 | Malipo ya upakaji rangi |
| 9/9 | | 3,500,000 | Malipo ya ujenzi wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Moh'd Abeid Juma | | banda |
| 5/9 | | 1,200,000 | Malipo ya utengenezaji wa mifereji |
| **Jumla** | | **12,225,000** | |

**Majibu ya Mamlaka**

Ni kweli kwamba vocha namba D8/10 aliyelipwa Bwana Salim Ali Yussuf yenye jumla ya Shilingi 3,700,000 kwa ajili ya ununuzi wa honda "click" haisajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma.

Kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha hili ilikuwa ndio duka peke yake linalouza "Click" na kwa bahati mbaya muuzaji huyu alikuwa hajasajili duka lake. Mamlaka itahakikisha tatizo hili halitojitokeza tena hasa kwa uwepo wa mfumo wa manunuzi wa kielectroniki.

Aidha, Vocha namba 9/10 aliyolipwa Bwana Ali Juma Hamad yenye jumla ya Shilingi 3,825,000, vocha namba 9/9 yenye kiasi cha Shilingi 3,500,000 na vocha namba 5/9 yenye Shilingi 1,200,000 zilizolipwa kwa Bwana Mohammed Abeid Juma hazijasajiliwa. Hii ni kwa sababu hawa ni mafundi ambao walipewa mafunzo na Mamlaka kwa ajili ya kuongeza nguvu kazi na walitumiwa katika kazi za matengenezo, upakaji rangi na utengenezaji wa mifereji. Hata hivyo, Mamlaka itahakikisha mafundi kama hawa wanajisajili kwa ajili kuwapa kazi za ukarabati.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na maelezo ya Mkaguzi Mkuu na hasa ikizingatiwa kuwa Mamlaka imekiri dosari hii, kwa msingi huo, Hoja hii imebaki kama ilivyo.

Kutokana na hali hiyo, na ili hoja kama hii isijitokeze tena, Kamati ya LAAC inaitaka Mamlaka kufanya ununuzi na watoa huduma ambao wamesajiliwa na Mamlaka.

### 5.4.4.3 Kutokukatwa kodi ya zuio kwa malipo ya watoa huduma, shilingi 426,250

Kwa mujibu wa kifungu nambari 81 na 83 cha Sheria ya Kodi ya Mapato Tanzania ya mwaka 2004, taasisi za Serikali zinatakiwa kuzuia asilimia fulani kutoka katika malipo ya mtoa huduma (2% kwa bidhaa na 5% kwa huduma) na kuwasilisha kodi hizo katika Mamlaka ya Mapato ndani ya siku 7 baada ya kumalizika kwa mwezi husika.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar haikukata kodi ya zuio kutoka katika malipo ya watoa huduma mbali mbali kama inavyotakiwa na sheria.

Kutokuwakata kodi ya zuio kwa wauza bidhaa na watoa huduma ni kwenda kinyume na sheria za kodi na kunaweza kupelekea kuikosesha Serikali mapato.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kuhakikisha kuwa wanazuia kodi ya zuio kutoka katika malipo ya watoa huduma wa Mamlaka na kuwasilisha kwa Mamlaka husika ndani ya muda unaotakiwa kisheria.

**Watoa huduma ambao hawakukatwa kodi ya zuio**

| Hati Nam. | Aliyelipwa | Kiasi cha Fedha (Tsh.) | Kiasi cha Kodi ya Zuio 5% (Tsh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 9/10 | Ali Juma Hamad | 3,825,000 | 191,250 | Malipo ya upakaji rangi |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9/9 | Moh'd Abeid Juma | 3,500,000 | 175,000 | Malipo kwa ujenzi wa banda |
| 5/9 | | 1,200,000 | 60,000 | Malipo kwa ajili ya utengenezaji wa mifereji |
| **Jumla** | | **8,525,000** | **426,250** | |

**Majibu ya Mamlaka**

Ni kweli Mamlaka haikuzuia kodi kwa watoa huduma ambao walikuwa hawajasajiliwa. Hata hivyo, Mamlaka itahakikisha inafanyakazi na watoa huduma waliosajiliwa na kuzuia kodi hizo kwa mujibu wa Sheria.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja hii imebaki kama ilivyo, na ili kasoro kama hiyo isijitokeze tena katika siku zijazo, Kamati ya LAAC inaitaka Mamlaka kabla ya kufanya maamuzi kwa yale masuala ambayo haina utaalamu nayo kupata ushauri katika Taasisi husika ili kuheshimu Sheria za nchi pamoja na kuepuka kupata hoja zisizo na msingi.

### 5.4.4.4 Kutokuonyeshwa kwa mapato yanayotokana na Bustani ya Forodhani

Mapato ya Bustani ya Forodhani yanasimamiwa na Kamati ya pamoja ya usimamizi wa Bustani ya Forodhani inayoundwa Taasisi ya Serikali na Taasisi ya sekta binafsi. Matumizi yanayotokana na mapato ya Bustani hiyo yanaidhinishwa na Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar.

Ukaguzi umebaini kuwa Taarifa ya Fedha ya mwisho wa mwaka 2020/2021 ya Mamlaka haionyeshi kiasi cha fedha kilichokusanywa na kutumika kutokana na mapato ya bustani ya Forodhani.

Kutokuonyeshwa taarifa za mapato yanayotokana na bustani ya Forodhani kunapunguza uwazi katika usimamizi wa mapato hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar kuhakikisha kuwa unaonyesha mapato na matumizi yanayotokana na bustani ya Forodhani ili kuongeza uwazi katika usimamizi wa mapato hayo.

**Majibu ya Mamlaka**

Ni kweli mapato yanayotokana na Bustani ya Forodhani hayaonekani katika taarifa ya fedha ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. Hii ni kutokana na mapato haya kuwa yanakusanywa na Meneja wa Bustani ya Forodhani na yanasimamiwa na Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ya Mjini pamoja na Mhasibu wa Manispaa hiyo. Hata hivyo, Mamlaka imepokea ushauri na utaufanyia kazi ili kuhakikisha fedha hizi zinaonekana katika vitabu vya Mamlaka.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imekubaliana na maelezo ya Mkaguzi Mkuu, hivyo basi, Hoja hii imebaki kama ilivyo. Pamoja na hayo, Kamati inaitaka Mamlaka kuyasimamia mapato hayo kwani hadi sasa mapato ya bustani hii yanayumba.

### 5.4.5 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)

**Taarifa ya Mapato**

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 2,108,400,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi 1,678,906,355 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi za kawaida, sawa na asilimia 79.63 ya makadirio.

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar haikuandaa maelezo maalum kuhusiana na Taarifa ya Mapato, isipokuwa kwamba, ilitoa ufafanuzi kwa mujibu wa maswali ya Kamati.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia taarifa hii, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Mamlaka haina kianzio cha mapato cha moja kwa moja, isipokuwa kwamba, mapato ya Mamlaka yanatokana na Matumizi Mengineyo (Other Charge) na endapo Mamlaka itapata mapato wakati inatekeleza shughuli zake basi mapato hayo huyawasilisha Serikali.

Kamati ya LAAC, imeishauri Mamlaka kuzidisha juhudi katika kutekeleza shughuli zake ili kuzinusuru rasilimali za umma kwa maendeleo ya nchi hii.

**Taarifa ya Matumizi**

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,108,400,000 kwa ajili ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 1,678,906,355 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 79.63 ya makadirio.

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar haikuandaa maelezo maalum kuhusiana na Taarifa ya Matumizi, isipokuwa kwamba, ilitoa ufafanuzi kwa mujibu wa maswali ya Kamati.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini na kupendekeza yafuatayo:

i). Mamlaka haikuingiziwa fedha za kutosha, jambo linaloweza kupelekea Mamlaka hii kushindwa kutekeleza majukumu yake iliyojipangia.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuipatia fedha za kutosha Mamlaka hii ili iweze kutekeleza shughuli zake bila ya usumbufu wowote.

ii). Mamlaka haikuwasilisha Taarifa ya mwaka ya Mkaguzi wa Ndani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika mwaka husika kama kifungu cha 117(6) cha Sheriakmk ya Usimamizi wa Fedha inavyoelekeza.

Kutokana na hilo, Kamati ya LAAC inaitaka Mamlaka kutekeleza majukumu yake kama Sheria za nchi zinavyoelekeza ili kuepusha dosari zisizo na msingi.

iii). Mamlaka haikuwa na Kamati ya Ukaguzi (Audit Committee) katika mwaka husika kama Sheria ya Usimamizi wa Fedha inavyoelekeza.

Kutokana na dosari hiyo, Kamati ya LAAC inaitaka Mamlaka kutekeleza majukumu yake kama Sheria za nchi zinavyoelekeza ili kuepusha dosari zisizo na msingi.

iv). Taarifa ya Fedha ya Mwisho wa Mwaka ina mapungufu ikiwemo;

i. Kutokuwekewa “code” kifungu kinachohusiana na “Operation”;
ii. “Code” ya Kasma ya “Special Allowance” ambayo ni 2111009 imetumika kwenye zaidi ya “Note” moja. “Note” zenyewe ni “Note” 7 inayohusiana na “Personal Emolument” na “Note” 9 inayohusiana na “Suppliers and Consumables”.
iii.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

**5.4.5.1 Kutokutayarisha ripoti ya mwaka inayohusu kazi zilizofanywa na Mamlaka**

Kifungu nambari 12 cha Sheria Nambari 1 ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ya mwaka 2012 kinamtaka Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka atayarishe au aagize kutayarishwa kwa ripoti ya mwaka inayohusiana na kazi zilizofanywa na Mamlaka pamoja na maelezo ya hesabu za Mamlaka kwa kila mwaka wa fedha na kuiwasilisha ripoti hiyo kwa Waziri ndani ya kipindi cha miezi minne baada ya mwisho wa mwaka wa fedha husika na kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka haitoi ripoti hiyo kama ilivyotakiwa katika kifungu nambari 12 cha Sheria Nambari 1 ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ya mwaka 2012.

Kutokutayarisha ripoti ya mwaka na kutokuchapisha katika Gazeti Rasmi la Serikali kunainyima jamii taarifa muhimu kuhusiana na shughuli za Mamlaka.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka usimamie kikamilifu utoaji wa ripoti kwa kila mwaka wa fedha ili kuipatia jamii taarifa muhimu kuhusiana na shughuli za Mamlaka.

**Majibu ya Mamlaka**

Ripoti ya mwaka inayohusiana na kazi zilizofanywa na Mamlaka iliyotajwa kwenye kifungu cha 12 cha Sheria nambari 1/2012 inalingana na ile iliyotajwa kwenye kifungu cha 33 cha Sheria hiyo ripoti ambayo iliandaliwa na kuwasilishwa.

ZAECA inaamini kuiwasilisha ripoti hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi kuwa tayari imeshaifanya kuwa au imeshasababisha kuwa ni ripoti ya wazi inayoweza kufikiwa na jamii, kama haifanyiki hivyo basi ZAECA inaahidi itachukua bidii zaidi kuanzia sasa ili kuhakikisha ripoti hiyo inachapishwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

Aidha, ZAECA inaahidi kuwa wakati wa utayarishaji wa ripoti hiyo kuanzia sasa itahusisha na kutaja vifungu vyote viwili kile cha 12 na cha 33 vya Sheria nambari 1 ya mwaka 2012 ili kuonesha kwa urahisi utekelezaji wa Sheria.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Ripoti iliyoelezwa katika vifungu viwili tofauti vya Sheria husika ni Ripoti ambayo ina maudhui moja, hivyo, Mamlaka ilikuwa sahihi kuandaa Ripoti moja.

Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC imeifuta hoja inayohusiana na uandaaji wa Ripoti, isipokuwa kwamba, Kamati imeibakisha hoja inayohusiana na kutokutangazwa kwa Ripoti hiyo kwenye Gazeti rasmi la Serikali. Hivyo, Kamati ya LAAC inaitaka Mamlaka kuitangaza Ripoti hiyo kama Sheria inavyoelekeza.

**5.4.5.2 Kutokufanyika kwa Tathmini ya Utendaji kazi**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 17 cha Sheria Nambari 1 ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ya 2012, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar anatakiwa angalau mara moja kila baada ya miaka

miwili kuteua mtu au taasisi yenye sifa kufanya tathmini ya utendaji kazi ili kujua kama viwango vya utendaji kazi ambavyo kila mchunguzi anapaswa kuwa navyo vimefikiwa na kama viwango hivyo vinatosheleza.

Mtu au Taasisi iliyoteuliwa kufanya tathmini ya utendaji kazi inatakiwa kuandaa ripoti ya tathmini ya utendaji kazi na kuiwasilisha kwa Waziri ambapo Waziri nae ataiwasilisha ripoti hiyo kwa Rais na baadae kuiwasilisha Baraza la Wawakilishi.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar haifanyi tathmini ya utendaji kazi na haiwasilishi ripoti ya tathmini ya utendaji kazi ili kujua kama viwango vya utendaji kazi ambavyo kila mchunguzi au mtu aliyeteuliwa kufanya uchunguzi vimefikiwa na kama viwango hivyo vinatosheleza.

Kutokufanywa kwa tathmini ya utendaji kazi kunapelekea Mamlaka na Serikali kwa ujumla kushindwa kufahamu kama viwango vya utendaji kazi ambavyo kila mchunguzi anapaswa kuwa navyo vimefikiwa na kama viwango hivyo vinatosheleza.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kufanya tathmini ya utendaji kazi kwa wachunguzi wake na kuandaa ripoti kama inavyotakiwa na Sheria.

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka inayo utaratibu uliojiwekea wa kufanya tathmini sio tu kwa wachunguzi bali kwa watumishi wake wote.

Hata hivyo, takwa la Sheria la kifungu tajwa cha 17 cha Sheria namba 1/2012 limekuwa gumu kutekelezeka kutokana na ukweli kuwa kulitekeleza takwa hilo lina athari kubwa kiutendaji kwa Mamlaka na linaweza kuleta athari hasi ambayo inaweza kuongeza wigo wa watendaji wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.

Kutangaza udhaifu wa wachunguzi na mapungufu walionayo maana yake ni kuwaambia wahalifu kutumia udhaifu wa wachunguzi wetu kutekeleza uhalifu wao.

Kutokana na hilo Serikali kupitia Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar katika Mswaada wa Kubadilisha Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Sheria nambari 1/2012 imeondoa takwa hili la Sheria. Hivyo, matarajio ni kuwa takwa hili litakoma mara tu baada ya Sheria mpya kupitishwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inakubaliana na hoja ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuwa katika wakati huo jambo hilo lilikuwa ni takwa la kisheria. Isipokuwa kwamba, Kamati ya LAAC imeifuta hoja hiyo kwa kuwa takwa hilo limeshafutwa kufuatia kutungwa wa Sheria mpya ya mwaka 2023.

### 5.4.5.3 Kutokutangazwa kwa waliopatikana na hatia za Rushwa na Uhujumu Uchumi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 77 cha Sheria Nambari 1 ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ya mwaka 2012 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi inatakiwa angalau mara moja kwa kila mwaka kuchapisha katika Gazeti Rasmi la Serikali majina ya watu wote waliopatikana na hatia kwa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar haichapishi majina ya waliopatikana na hatia ya makosa ya rushwa na uhujumu uchumi katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Kutokutangazwa kwa majina ya waliopatikana na hatia za Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kunapunguza uwazi wa mapambano dhidi ya rushwa na kunaweza kupelekea kutokwa na hofu kwa wahujumu wa uchumi wengine.

**Majibu ya Mamlaka**

Ni kweli kwa mwaka 2020/2021 Mamlaka ilipata kuwatia hatiani wahalifu Mahakamani (conviction), hata hivyo, wahalifu hao hawakuwahi kutangazwa kwenye Gazeti Rasmi la Serikali, hivyo, Mamlaka inaahidi kulifanyia kazi suala hilo ili kuhakikisha takwa la Sheria linatekelezwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja hii imebaki kama ilivyo, pamoja na hilo, Kamati ya LAAC inaitaka Mamlaka kulifanyia kazi suala hilo kama kifungu cha 97 cha Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar inavyoelekeza.

### 5.4.5.4 Mamlaka kukosa wataalam wa fani tofauti

Kwa mujibu wa Sheria Nambari 1 ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ya mwaka 2012, Mamlaka Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar imepewa uwezo wa kupambana na rushwa na uhujumu uchumi katika sekta na mazingira tofauti ikiwemo rushwa na ubadhirifu katika masuala ya ujenzi, ukwepaji kodi, manunuzi ya umma na utakatishaji fedha.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka haina wataalamu wa fani muhimu ambazo wanapaswa kuwa nazo katika utekelezaji wa kazi zake za kawaida kama vile wahandisi, wataalamu wa kodi, wataalamu wa manunuzi, wataalamu wa mifumo ya TEHAMA, wataalamu wa uhalifu mitandaoni n.k.

Kuendelea kuazima wataalamu kutoka sekta binafsi au za Serikali kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa vitendo vya uvujaji wa taarifa za Serikali na upoteaji wa nyaraka muhimu za Serikali kabla ya uchunguzi kumalizika jambo ambalo linaweza kupelekea kupoteza ushahidi wa tuhuma inayofanyiwa kazi kwa kuzingatia zaidi wataalamu hao wanaweza kukosa maadili ya kazi za upelelezi.

Aidha, kukosekana kwa wataalamu wa fani muhimu ambazo Mamlaka inazihitaji kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake kunapelekea Mamlaka kushindwa kufanikisha majukumu yake kwa ufanisi na hatimae kuweza kukodi au kuazima wataalamu kutoka nje ya taasisi yao jambo ambalo linapelekea kuingiza hasara Serikali kutokana na kiasi kikubwa cha fedha kinachoweza kutumika kwa ajili ya kuwalipa wataalamu ada ya kufanya kazi ya upelelezi husika.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka kuajiri wataalamu wa fani muhimu ambazo Mamlaka inazihitaji kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa uhuru na kwa ufanisi zaidi kwani kwa kufanya hivyo kutaweza kuisaidia Mamlaka na taifa kwa ujumla katika kuongeza mapambano ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi katika Taasisi za Serikali na taifa kwa ujumla.

**Majibu ya Mamlaka**

Ni kweli Mamlaka ina upungufu wa wataalamu wa kada mbali mbali hasa ukizingatia kipindi hicho cha ukaguzi 2020/21 upungufu ulikuwa mkubwa.

ZAECA tokea wakati huo imekuwa ikilifanyia kazi suala hilo na hatimae mwaka huu 2023 Mamlaka imepata kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi Serikalini cha kuajiri baadhi ya wataalamu hao.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na majibu ya Mamlaka, Kamati ya LAAC ilitaka kujua idadi halisi ya Watumishi ambayo inahitajika, ambapo, Kamati ilielezwa kuwa Mamlaka kwa wakati ule (tarehe 30 Machi, 2023) ilikuwa imemuajiri Mshauri Elekezi kwa ajili ya kufanya tathmini hiyo, hivyo, Kamati ya LAAC haikupata idadi halisi kutokana na sababu hiyo.

Isipokuwa kwamba, Mamlaka iliomba Wizara inayohusiana na ajira kuajiri Watendaji 50 na badala yake wameruhusiwa kuajiri Watendaji 12 tu.

Kwa kuwa Mamlaka hii utendaji wake unahusiana na haki za watu, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kuipatia Watendaji wa kutosha Mamlaka ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa wepesi na kwa weledi.

## 5.4.6 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI

### TAARIFA YA MAPATO

Mamlaka ya Usafiri Barabarani kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Mamlaka ilikadiriwa kupokea Jumla ya shillingi 1,344,200,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kazi za kawaida. Aidha Mamlaka ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 3,400,585,000 kutoka vynanzo vyake vya ndani vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 June, 2021, Mamlaka ya Usafiri na usalama Barabarani ilipokea jumla ya 755,527,331.23 kwa matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia 56.21 ya makadirio. Aidha Mamlaka ilikusanya jumla ya shilingi 2,782,077,700 kutoka vyanzo vya vyake vya ndani sawa na asilimia 81.81 ya makadirio

### Majibu ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Mamlaka ilikusanya fedha kutoka katika vyanzo vyake vya ndani vya mapato na kupata fedha za matumizi kama ilivyo elezwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Fedha hizo zilikusanywa na kupatikana kama ifuatavyo:

| **ems** | **lakadirio 2020/2021** | **alisi 2020/2021** | **silimia** |
|---|---|---|---|
| ızuku ya Mshahara | 57,700,000.00 | 37,025,415.00 | 7.9 |
| ızuku ya Matumizi ya Kawaida | 76,500,000.00 | 51,501,000.00 | 1.0 |
| akusanyo kutoka Vyanzo vya Ndani | 400,585,000.00 | 782,077,700.00 | 1.81 |
| **ımla** | **744,785,000.00** | **530,604,115.00** | **4** |

Mamla ya usafiri na usalama barabarani kwa mwaka wa fedha 2020/202i ilikusanya fedha hizo kupitia vyanzo vinane (8) vya mapato ya ndani. Vyanzo hivyo ikiwemo ukaguzi wa vyombo vya moto, mitihani ya madereva wanafunzi, utowaji wa ruhusa za njia, utowaji wa

vibali vya madereva wakigeni, utowaji wa lena, utoaji wa beji kwa madereva na makonda, utoaji wa leseni za magari ya biasahara na usajili wa vyuo na walimu. Sababu kuu za kutofikia lengo kwa silimia mia moja ni:

a. Kupungua kwa maombi ya mitihani ya madereva wanafunzi kwa asilimia asilimia hamsini (50%) ya madereva wanafunzi waliokadiriwa na wengine kutoakmilisha kufanya mitihani ya Vitendo.

b. Kupungua kwa maombi ya upasishaji wa Vyombo vya moto kwa asilimia kumi na tatu (13%) ya makadio ya mwaka 2020/2021

c. Kupungua kwa maombi ya leseni za madereva wanafunzi (Leaner) kutoka 13,596 zilizokadiriwa hadi 8,933 Zilizotolewa kwa mwaka 2020/2021

d. Kupungua kwa maomba ya ruhusa za njia kutoka 27,204 zilizokadiriwa hadi 17,955 Zilizotolewa sawa na asilimia 66 ya makadirio

e. Kupungua kwa maombi ya leseni za Magari yanayofanya biashara kwa asilimia 13

f. Upungufu wa zana za kufanyia kazi katika usimamizi wa usalama barabarani

Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati imeomba kupatiwa ufafanuzi juu ya mamlaka kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya kutoka vyanzo vyake vya ndani katika mwaka wa fedha 2020/2021 na kuelezwa kuwa sababu ya mripuko wa maradhi COVID 19 ambapo Serikali imepiga marufuku mikusanyiko mbalimbali jambo ambalo limeweza kuathiri shughuli mbalimbali za mamlaka katika ukusanyaji wa mapato kama vile uchache wa wanafunzi katika vyuo vya udereva wanaotarajia kufanya maombi leseni, Uchache wa watalii wanaomba vibali vya kuendesha

vyombo vya moto ‘Permit’ , na sababu nyenginezo ambazo zimeanishwa hapo juu ambazo ndizo zimepelekea mamlaka kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato.

Kamati inaishauri mamlaka ya usafiri na usalama barabarani kwa vile maradhi ya Covid 19 yamepungua duniani na Shughuli za kiuchumi na kijamii hivyo ni vyema kusimamia vyanzo vyao vya mapato na kuboresha mianya ya upotevu wa mapato na kutumia mifumo mbalimbali ya Tehama katika ukusanyaji ili waweze kufikia malengo waliojiwekea na kuweza kutekeleza shughuli zao walizojipangia kwa asilimi mia (100).

Kamati imebaini katika taarifa ya mwisho ya mahesabu ya Mamlaka ya mwaka 2020/2021 kifungu cha mapato mengineyo hakina makisio ya mapato ila wameweza kupokea jumla Tzs 6,000,916.23 ambapo kamati imeelezwa fedha hizo mamlaka imezipokea kutoka Serikalini kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya madeni kwa wafanyakazi ambao walikua wanafanya kazi muda wa ziada na siku za mapumziko kwa ajili ya kuwadumia wageni ambao wanahitaji kupatiwa vibali vya kuendesha vyombo vya moto.

Kamati inaishauri Mamlaka kuweka makisio ya bajeti katika vifungu vyake vya mapato kwa mujibu wa sheria ili vifungu hivyo viweze kuleta sura sahihi ya makusanyo yake na viweze kufanyiwa tathmini ya mapato yaliyokadiriwa na mapato halisi yaliyokusanywa kwa mwaka wa fedha husika.

Kamati imehoji juu ya kiwango kikubwa cha makusanyo ya mapato ya ‘permit’ ya Tzs 197,130,000 ukilingamisha na makadirio ya Tzs 48,718,000 na kuelezwa kuwa hali hiyo imetokana na kuchukua jitihada za makusudi katika kuimarisha chanzo hicho kwa kuanza kutoa huduma siku za mapunziko na skuku ili waweze kuwahudumia wateja wao ambao ni wageni wa kitalii siku zote bila ya usumbufu wowote na kupelekea chanzo hicho kuvunga malengo waliyojiwekea.

Kamati inaipongeza Mamlaka kwa jitihada zake katika kuongeza mapato hasa mapato yatokanayo na ‘permit’ kwa kuamua kutoa huduma hii mpaka siku za mapunziko , Kamati inaishauri mamlaka kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato yake mengineyo na kuendelea kudhibiti uvujaji wa mapato kwa watu ambao wanaghushi nyaraka na vibali mbalimbali ambavyo vinatolewa na Mamlaka.

**Taarifa ya Matumizi**

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla shillingi 4,744,785,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia June 30, 2021 Mamlaka ilitumia jumla ya shillingi 3,537,505,255 kwa kazi za kwaiada sawa na asilimia 74.56 ya makadirio.

**Majibu ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani**

Ni kweli Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla shillingi 4,744,785,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia June 30, 2021 Mamlaka ilitumia jumla ya shillingi 3,537,505,255 kwa kazi za kwaiada sawa na asilimia 74.56 ya makadirio, hali hii imetokana na kupatikana kwa kiwango kidogo cha ruzuku za matumizi wa kawaida kutoka Serikalini aidha kutofika malengo ya Ukusanyaji wa mapato kutoka na mripuko wa maradhi ya Covid 19.

**Uchunguzi na Mapendekezo Kamati ya LAAC**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini ni kweli mamlaka imekadiria kupokea jumla ya Tzs 676,500,000 ambazo ni ruzuku ya matumizi mengineyo kutoka serikalini na imepokea jumla ya Tzs 161,500,000 sawa na asilimia 24.0, hivyo basi Mamlaka imeshidwa kutekeleza shughuli zake mbalimbali ambazo imejipangia kwa asilimia mia moja (100) na baadhi ya Shughuli kushidwa kutekelezwa kabisa kutokana kutofikia malengo ya ukusanyaji wa

mapato na uhaba wa fedha za ruzuku kutoka Serikalini kwa mfano matumizi ya ununuzi wa fanicha na gari ya Mamlaka yameshidwa kufanyika kabisa licha ya mamlaka kutenga bajeti kwa ajili ya manunuzi hayo ambayo yanalenga kuimarisha mazingira ya utendaji kazi wa mamlaka kwa vile bado mamlaka hii ni changa na inahitaji gari kwa ajili shughuli za Mamlaka na fanicha mbalimbali kwa ajili matumizi ya Ofisi.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inatoa ruzuku kama ilivyopangwa katika bajeti ya mamlaka ili shughuli za mamlaka ziweze kutekelezwa kwa uhakika na kwa muda uliopangwa.

Aidha Kamati imebaini uwepo wa matumizi ya Tzs 2,314,520.20 katika kifungu cha huduma za Benki (Bank service charges) ambacho hakikupangiwa bajeti ambapo ni kunyume na Sheria kwani vifungu vyote vya matumizi vinatakiwa kuwekwa makisio yake ya bajeti wakati wa uandaaji wa bajeti. Hivyo basi, Kamati inashauri Mamlaka kuwa na umakini katika uandaaji wa bajeti ili kuepusha dosari kama hizi kujitokeza mara nyengine tena.

**5.4.6.1 Matumizi yaliyozidi bajeti iliyo idhinishwa shilingi 27,591,790.**

Kwamujibu wa vifungu nambari 46(6)na 47(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, Afisa Mhasibu anapaswa kufanya matumizi ya bajeti kwa mujibu wa mipaka iliyowekwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali na hatolipa deni ambalo fedha zake hazikuidhinishwa. Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar imefanya matumizi ya kifungu cha malipo ya muda wa ziada pasina kuzingatia bajeti iliyotengwa katika kifungu hicho. Kufanya matumizi zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016 na kunaweza kupelekea Mamlaka kutofikia malengo yaliyopangwa katika mwaka wa fedha ujao kwa kulipa madeni ya mwaka wa fedha uliopita. Ukaguzi unashauri

uongozi wa Mamlaka uhakikishe unafanya matumizi ya fedha kwa kuzingatia bajeti iliyo pangwa ili iweze kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 120: Matumizi yaliyozidi bajeti iliyoidhinishwa.**

| fungu | asi cha baj yoidhinishwa (Tshs) | asi cha matum aliyolipwa (Tshs) | asi cha matum anayo dai (shs) | mla ya matum shs) | ofauti kati ajeti na Jumla atumizi (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| alipo uda v ada | 5,850,000 | 7,290,388 | 6,151,402 | 3,441,790 | 7,591,790 |

**Majibu ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama barabarani**

Mamlaka ilitenga Jumla ya shilingi 55,850,000.00 kwa ajili ya kulipa watendaji wao wanaofanya kazi kwa masaa ya ziada na imewalipa watendaji wake jumla ya shilingi 47,290,388.00 sawa na asilimia 84.67 ya makadirio katika kifungu cha malipo ya muda wa ziada kama ilivyo oneshwa na taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Aidha Mamlaka ilifanyakazi kwa muda wa ziada baada ya kupata agizo la kuendelea kutoka huduma za Permit kwa madereva wageni katika siku za mapumziko na siku za sikukuu. Hali hiyo ilipelekea Mamlaka kuwa na deni la shilingi 36,151,402.00 kwa watendaji wake.

Deni hilo lilihakikiwa na Afisi ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya Mh. Rais kutoa agizo la kulipwa madeni yote ya Wakandarasi na wafanyakazi. Mamlaka iliingiziwa fedha maalum za kulipa madeni yote baada ya kuhakikiwa ikiwemo deni la malipo ya muda wa ziada. Kwa kuwa taarifa ya fedha imeandaliwa kwa msingi wa CASH BASE. Kiasi kinachohesabiwa kuwa ni matumizi ni Tzs.42,290,388/= na siyo

TZS.83,441,7790/=. Hivyo kwa msingi uliotumika kuandaa Taarifa ya fedha, matumizi hayo hayakukiuka bajeti iliyopangwa.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati**

Kamati inakubaliana na hoja ya mkaguzi hata hivyo kamati inaifuta hoja hii kwa vile Mamlaka inafunga hesabu zake za mwaka kwa kutumia mfumo wa Cash Base na sio Acrual Base. Kwa hali hiyo Mamlaka haikutumia fedha zaidi za malipo ya madeni yaliozinishwa katika bajeti na kiwango hicho kilichozidi cha deni cha Tzs 36,151,402.00 ambacho kimelipwa na Serikali wakiwezi kuingizwa kama ni matumizi ya Mamlaka kwa vile deni hilo limelipwa na Serikali kwa maagizo ya Mh. Rais

**5.4.6.2 Kutokuwepo kwa vifaa vya kuzimia moto (fire extinguisher)**

Mamlaka ya Uasafiri na usalama barabrani inaendesha shughuli zake za kiutendaji za kila siku kwa kutumia majengo yake yaliyopo mtaa wa Mwanakwerekwe Zanzibar. Ukaguzi umebaini kwamba jengo la zamani la Mamlaka lilopo Ofisi Kuu ya Mwanakwerekwe ambalo hutumiwa kwa ajili ya kutoa huduma za moja kwa moja kwa wananchi haliko katika hali ya usalama kwa kutokuwepo kwa vifaa vya kuzimia moto.

Aidha ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka haijatoa mafunzo kwa watendaji wake juu ya utumiaji wa vifaa hivyo vya kuzimia moto. Kutokuwepo kwa vifaa vya kuzimia moto (fire extinguisher) ktika jengo kuu la Mamlaka ni Kwenda kinyume na sheria Namba 8 ya mwaka 2005 ya Afya na Usalama Kazini na kupelekea kukosekana kwa usalama wa watu na majengo pindi Janga la moto linapotokea. Ukaguzi unashauri kwamba, uongozi uhakikishe kuwa wanaweka vifaa vya kuzimia moto katika majengo yote ya Mamlaka Pamoja na kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake juu ya utumiaji wa vifaa hivyo

**Majibu ya Mamlaka ya usafiri na Usalama barabarani**

Mamlaka imepokea na kufanyia kazi ushauri wa ukaguzi wa kuweka vifaa vya 8 kuzimia moto katika majengo yote ya Mamlaka. Kwa sasa Mamlaka inajumla ya Chupa za kuzimia moto tatu (3) ambapo moja ipo katika eneo la kutolea huduma kwa wananchi, moja ipo katika eneo la ofisi ya Uendeshaji na moja ipo katika ofisi za upasishaji Karakana. Katika kutekeleza Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005, Mamlaka imejipangia kuongeza vifaa vya kuzimia moto katika kila eneo hatarishi ili kuwa na uhakika wa usalama kwa watendaji wa wananchi wanaokuja kupatiwa huduma ndani ya offisi za Mamlaka.

Katika bajeti ya Mwaka 2023/2024 Mamlaka imejipangia kununua mitungi mitano ili kukidhi maeneno yote ambayo yanahudumia watu wengi ndani ya ofisi za Mamlaka. Maeneo hayo ikiwemo ukumbi wa mitihani, ukumbi wa mikutano, eneo la kutolea Control namba na risit Ofisi za Mwanakwerekwe na Ofisi zilizokuwepo Karakana. Aidha Mamlaka imetoa elimu ya matumizi ya vifaa vya kuzimia moto kwa watendaji wake katika eneo la Ofisi kuu na Karakana. Hata hivyo elimu hiyo itaendelea kutolewa kila mara Mamlaka watakapo ongeza vifaa vya aina tofauti vya kuzimia moto kutoka na Ushauri wa Jeshi la Kuzima Moto Zanziba

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati**

Kamati inakubaliana na hoja ya mkaguzi hata hivyo kamati inaifuta hoja hii kwa vile mamlaka imechukua juhudi ya kununua vifaa vya kuzimia moto, kwa sasa mamlaka imenunua chupa za kuzimia moto tatu (3) (fire extinguisher) na inaendelea na mpango wa kukamilisha vifaa hivyo katika bajeti zijazo.

Kamati inaishauri mamlaka kuhakikisha inakamalisha vifaa vya zimamoto kwa vile mamlaka inatoa huduma katika eneo la mwanakwerekwe ambapo kunakua na mkusanyiko wa

wateja ambao wanapatiwa huduma, hivyo uwepo wa vifaa hivyo vitasaidia kudhibiti kwa haraka majanga ya moto pindi yatakapotokea.

**5.4.6.3 Kutokutumia mifumo katika utoaji wa huduma za Mamlaka**

Kwa mujbu wa Sheria Nambari 7 ya Usalama Barabarani ya mwaka 2003 kama ilivyorekebishwa katika Sheria Nambari 10 ya mwaka 2019, Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabrani imepewa jukumu la kisheria la kuhakikisha kuwa huduma za usafiri na usalama barabarani zilizo salama zenye kuaminika na zilizo bora. Miongoni kwa kazi za Mamlaka hii ni Pamoja na usimamizi wa mitihani kwa madereva, utoaji wa leseni za Udereva, vibali vya udereva kwa wageni ukaguzi wa vyombo vya moto, ruhusa za njia, usajili wa skuli za mafunzo ya udereva na utoaji wa beji.

Ukaguzi umebaini kwamba, Mamlaka haina mifumo ya Kielectroniki inayosaidia utowaji wa huduma zake za msingi kwa ukamilifu na inayoweka udhibiti ulio Madhubuti katika huduma za Mamlaka, badala yake ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka bado inaendelea kutumia mifumo ya kizamani (manual system) kwa ajili ya kutoa huduma zake.

Aidha ukaguzi umebaini kuwa kwa sasa Mamlaka inamifumo miwili ambayo ni Private Motor Vehicle Registration (PMR) na Commercial Motor Vehicle Registration (CMVR) inayotumika kwa ajili ya upasishaji wa vyombo vya moto na kuweka kumbukumbu za vyombo vilivyopasishwa pasina kuweza kutoa leseni za vyombo vilivyopasishwa jambo ambalo linapelekea Mamlaka kutegemea mifumo ya Taasisi Nyengine (ZRB) ambayo kimsingi Mamlaka haina udhibiti wa Mifumo hiyo.

Kutokutumia mifumo ya kielectoroniki katika utoaji wa huduma za msingi za Mamlaka kunaweza kupelekea kuwepo kwa nyaraka zisizo halali katika sekta ya Usafiri Barabarani, na kunaweza kupelekea uvujaji wa mapato ya Mamlaka kwani baadhi ya nyaraka zinaweza

kughushiwa kirahisi katika mifumo ya kizamani (Manual System) Ukaguzi unashauri kwamba, uongozi wa Mamlaka kutumia mifumo ya kisasa ya kielectroniki katika utoaji wa huduma zake kwa ukamilifu ili kupunguza uwezekano wa kuwepo kwa nyaraka zisizo halali katika sekta ya usafiri barabarani.

**Majibu ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani**

Mamlaka imepokea na kufanyia kazi ushauri wa Ukaguzi katika kuboresha utoaji wa huduma zake za msingi. Mamlaka kwa sasa inajumla ya mifumo minne (4) inayotumika katika kutoa huduma za msingi, mifumo hiyo ikiwemo Mfumo wa:

1. Private Motor Vehicle Registration (PMVR),

2. Commercial Motor Vehicle registration (CMVR),

3. Zanzibar Online Drining Lences Application Portal (ZODLAP),

4. Mfumo wa adhabu za papokwapapo kwa makosa ya Usalama Barabarani.

Mamlaka inendelea kutayarisha mifumo mengine ambayo itatumika katika huduma nyengine kama vile utoaji wa vibali vya madereva wa kigeni, beji, na leseni za njia. Mifumo ipo katika hatua za maandlizi chini ya Kampuni ya UBX ambayo inasimamiwa na wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati**

Kamati inakubaliana na hoja ya mkaguzi hata hivyo kamati inaifuta hoja hii kwa vile mamlaka imechukua jitihada ya kuongeza mifumo miwili na kuwa na jumla ya mifumo minne ya utendaji kazi ambayo imeanishwa katika majibu yao.

Kamati inaipongeza mamlaka katika jitahada zake za kuboresha ufanisi na utendaji kazi kwa kuongeza matumizi mifumo ya Tehama katika kutoa huduma mbalimbali, aidha kamati

inaishauri Mamlaka kukamilisha kwa haraka mifumo mengine ya utoaji huduma ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato na utoaji wa huduma kwa haraka ili kupunguza msongamano wa wateja katika eneo la mamlaka.

### 5.4.7 CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umebainisha taarifa ya michango ya vyanzo vya mapato vya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar , utendaji wa mwaka kwa kila chanzo cha mapato katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar pamoja na kubainisha dosari za kiutendaji zilizojitokeza wakati wa ukaguzi na kubainisha njia za utatuzi wa dosari hizo.

**Taarifa ya Mapato**

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 26,136,378,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 . Kati ya fedha hizo shilingi 11,236,378,000 ni kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato na shilingi 14,900,000,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 jumla ya shilingi 23,102,485,830 zilikusanywa ambapo shilingi 8,792,990,441 ni kutokana na vyanzo vya ndani vya mapato ambapo ni sawa na asilimia 78.3 ya makadirio na shilingi 14,309,495,389 ya ruzuku ilipokelewa kutoka Serikalini sawa na asilimia 96 ya makadirio.

**Majibu ya Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA)**

Ni kweli Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar hakikufikia lengo la kukusanya mapato ya ndani kama ilivyokadiriwa. Hali hii ilisababishwa na kuchelewa kwa Bodi ya Mikopo ya Zanzibar kulipa ada za wanafunzi kwa wakati uliotarajiwa. Mpaka kufikia tarehe 30 Juni 2021, Chuo kilikuwa kinadai bodi ya Mikopo ya Zanzibar kiasi cha shilingi 1,131,960,375. Hata hivyo, Bodi ya Mikopo ya Zanzibar imelipa deni lake lote katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021-22.

Vile vile, upungufu huo ulichangiwa na idadi ndogo ya wanafunzi wa kigeni waliodahiliwa mwaka huo kutokana na janga la korona. Chuo kilikadiria kukusanya jumla ya shilingi

160,000,000 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, chuo kiliweza kukusanya kiasi cha shilingi 26,453,116 tu kwenye chanzo hicho. Aidha, idadi ya wanafunzi wa kigeni katika idara ya Kiswahili na lugha za kigeni imeendelea kuongezeka kutokana na kupungua kwa janga la korona.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Ni kweli janga la UVIKO 19 limeleta athari kiuchumi na kijamii katika sehemu mbalimbali duniani hata hivyo Kamati inashauri uongozi wa chuo kuweka mikakati imara ya kuhakikisha kuwa mapato yanaongezeka kwa vile maradhi ya UVIKO 19 yamengua kwa asilimia kubwa na kupelekea shughuli za kiuchumi na kijamii kuendelea duniani kote.

**Taarifa ya matumizi**

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 26,091,618,250 kwa matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021, hadi kufikia 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 24,895,462,246.07 zilitumika ambazo ni sawa na asilimia 95.4 ya makadirio.

**Majibu ya Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA)**

Ni kweli, Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar hakikuweza kutekeleza shughuli zake zote ilizojipangia kufikia asimilia 100%. Hii imetokana na chuo kutokamilisha hatua za ununuzi wa vifaa mbali mbali ambapo jumla ya shilingi 2,002,539,350 zilitengwa. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, Jumla ya shilingi 404,821,647 zilitumika. Hali hiyo imetokana na Chuo kutofikia lengo la ukusanyaji lililojipangia.

**Uchunguzi na mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii inashauri uongozi wa Chuo kutekeleza shughuli mbalimbali walizojipangia kwa kufuata mpango wa manunuzi na Bajet katika mwaka husika ili kuepuka kufanya shughuli ambazo zipo nje ya bajeti na mpango wa manunuzi.

Aidha Kamati inashauri uongozi wa Chuo kuhakikisha wanatekeleza miradi ya waliyojipangia kwa ufanisi mkubwa kama vile miradi ya majengo ya vyuo kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kujisomea katika vyuo vyake.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

**5.4.7.1 Manunuzi yaliyofanyika nje ya mpango wa manunuzi Shilingi 1,191,359,462**

Kifungu cha 42(7) cha sheria ya ununuzi na uondoaji wa mali za Umma kinaeleza kwamba ununuzi hautofanyika kinyume na mpango wa manunuzi na uondoshaji wa mali za umma isipokuwa kwa hali ya haraka na dharura.

Aidha kifungu cha 42(4) cha sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma inaeleza kuwa taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma kila baada ya miezi mitatu na kwa namna yoyote itakavyo jitokeza itafanya mapitio na kuboresha mpango wa ununuzina uondoshaji wa mali za Umma.

Mapitio ya mpango wa manunuzi wa mwaka 2020/21 wa Chuo kikuu chs Taifa Zanzibar (SUZA) yalibaini kwamba Chuo kilifanya manunuzi mbalimbali yenye thamani ya Shilingi 1,191,359,462 nje ya mpango wa manunuzi kinyume na kifungu cha 42(7) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma namba 11 ya mwaka 2016.

Aidha ukaguzi haukupatiwa mpango wa manunuzi uliofanyyiwa mapitio na kuboreshwa ambao ulipaswa kuwasilishwa mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Uchambuzi wa manunuzi yaliyofanyika njeya mpango yanaonekana katika jadweli hapo

chini:-

Manunuzi nje mpango wa manunuzi yanaweza kupelekea kutotekelezwa kwa mipango mingine na kunaweza kukwamisha shughuli stahiki zilizopangwa kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Chuo kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kufuata matakwa ya sheria ya ununuzi na Uondoshaji wa mali za umman kuhakikisha kwamba inafanya mapitio y mpangona kuboresha mpangongo wa ununuzi kwa kuingiza shughuli zote muhimu katika bajeti na mpango wa manunuzi wa kila mwaka ili kuepuka kufanya manunuzi nje ya mpango ambayo yanaweza kusababisha gharama za ziada au zisizo za lazima kwa Shirika.

**Majibu ya Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar (SUZA)**

Uongozi wa Chuo unakiri kufanya ununuzi nje ya Mpango wa Ununuzi uliopitishwa mwazo. Hii ilitokana na udharura wa shughuli zilizojitokeza kutokana na uhitaji wa kupunguza gharama za ununuzi wa vitabu vya kujibia mitihani, ukarabati wa miundombinu ya Skuli mpya ya Meno na Kilimo pamoja na ujenzi wa ukuta katika Taasisi ya Utalii , Maruhubi. Hata hivyo Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kilifanya maboreho ya Mpango wake wa Ununuzi wa mwaka wa fedha 2020 – 21 ili kukidhi haja hiyo na kuwasilisha Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Tarehe 6/07/2021 kumbukumbu Namb SUZA/ODVCA/CON.4/301. Hivyo kazi zote zilizotajwa kwenye jaduweli ziliingizwa kwenye mpango wa ununuzi ulioboreshwa.

Ununuzi wa mashine ya kuchapisha vitabu vya kujibia mitihani “booklet” ulifanyika kwa ajili ya kupunguza gharama na ununuzi vitabu hivyo. Mfano chuo kilikuwa kinatumia zaidi ya milioni 80 kwa mwaka kwa ajili ya ununuzi wa booklet. Pia uamuzi huu pia umeimarisha usalama wa vitabu vya kujibia mitihani.

Ujenzi wa dahalia skuli ya kilimo, matengenezo katika skuli ya meno pamoja na ujenzi wa madarasa skuli ya Kizimbani yalifanyika kutoka changamoto ya ubora wa miundombinu hio baada ya tishio ya kufutwa kwa udahili wa Skuli hizo kutokana na uchakavu wa miundombinu yake ambayo iliilazimu Serekali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoa fedha za marekebisho ya miundombinu hiyo.

SUZA ililazimika kujenga ukuta kwa ajili ya kuimarisha usalama katika Taasisi ya Utalii, maruhubi ambalo lilitumika kama kituo cha cha kufanyia majumuisho ya matokeo ya uchaguzi kitaifa oktoba 2020.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile uongozi wa Chuo umekiri kuwepo kwa dosari hiyo Kamati inashauri uongozi wa Chuo kufuata taratibu za kisheria katika kutekeleza majukumu yake ikiwemo kufanya matumizi yaliyokuwemo ndani ya mpango wa manunuzi katika mwaka husika.

Kamati haipingani na dharura katika kutekeleza mpango wa manunuzi kwa vile dharura zinakubalika kisheria Kamati inashauri ikiwa kuna jambo la dharura na uharaka wa kufanya manunuzi nje ya mpango basi ni vyema Uongozi wa Chuo kufuata taratibu za kisheria kwa kuupita tena (Review) mpango wa manunuzi na kurekebisha ikiwa kuna haja ya kufanya manunuzi ya lazima kwa vifaa au huduma ambazo hazikuwapo ndani ya mpango wa manunuzi.

**5.4.7.2 Mapokezi ya vifaa visivyofanyiwa ukaguzi vyenye thamani ya shilingi 283,740,000**

Katika ukaguzi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), imebainika kwamba Chuo kilifanya manunuzi ya vifaa vya maabara na mashine za kuchapisha mitihani vyenye thamani ya shilingi 283,740,000 bila ya kukaguliwa wakati wa kupokelewa kinyume na taratibu za manunuzi ambazo zinaelekeza kuwa manunuzi yote yanayofanywa na taasisi za Umma

yanapaswa kukaguliwa ili kuweza kubaini kama yamefikia vigezo vilivyoainishwa kwenye mkataba.

Aidha miongozo bora ya manunuzi “best practice” inamtaka Mkuu wa Taasisi kuteua Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi ya vifaa ambayo itawajibika kukagua, kuthibitisha ubora wa vifaa au huduma na kupokea pindi vinaponunuliwa. Baadhi ya vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila ya kukaguliwa ni kama vinavyoonekana katika jadweli hao chini:-

**Jadweli Nambari 122 : Vifaa vilivyopokewa ambavyo havijafanyiwa ukaguzi**

| Namba | a la Msambazaji | a fedha (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | 'S Lab equipment Limited | 164,740,( | unuzi na ufungaji wa vifaa vya ıabara |
| 2 | 'Equator traders | 119,000,( | unuzi wa mashine za kuchapi- sh tihani SUZA |
| **Jumla** | | **283,740,(** | |

kupokea bidhaa, vifaa bila kukaguliwa na kukubaliwa na kamati ya ukaguzi na mapokezi ya vifaa na huduma kunaweza kukatoa fursa kwa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar kununua vifaa na huduma zisizokuwa na viwango vya ubora au zisizofuata mahitaji muhimu ya manunuzi.

**Majibu ya Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar (SUZA)**

Uongozi Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) unakiri haukufanya tathmini kwa wakati wa vifaa vya maabara vilivyonunuliwa kwenye mwaka wa fedha 2020-21. Hata hivyo Chuo kilifanya tathmini ya vifaa hivyo katika mwaka wa fedha 2021-22. Ripoti ya tathmini ya vifaa vya Maabara ilifanyika Tarehe 02/12/2021. Kwa upande wa ununuzi wa mashine ya kuchapisha vitabu vya mitihani ilifanyiwa tathmini tarehe 14/12/2020. Vielelezo vya tathmini vimeambatanishwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa ni kweli wakati mkaguzi alipofanya ukaguzi wake hakukuwa na ripoti ya Tathmini ya vifaa hivyo vilivyonunuliwa hata hivyo Uongozi wa Chuo umeshachukua jitihada kwa kukamilisha tathmini ya vifaa hivyo.

Kamati inashauri uongozi wa Chuo kuwa makini katika kufuata Sheria na miongozo kwa kuhakikisha kuwa tathmini hufanywa baada ya vifaa kununuliwa tu na si vyenginevyo kwa lengo la kupata fursa ya kuvirejesha vifaa hivyo kwa mtoa huduma ikiwa havijakidhi vigevo kwa mujibu wa makubaliano katika mkataba husika.

### 5.4.7.3 Upungufu wa watumishi Katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA)

Katika ukaguzi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar katika kipengele cha rasilimali watu ukaguzi umebaini Chuo kinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali watu . Changamoto hii imebainika katika Shule ya Biashara Chwaka, Shule ya Afya Mbweni , Shule ya kilimo Kizimbani na baadhi ya Vitengo katika Makao makuu ya Chuo Tunguu.

Katika Shule ya Biashara Chwaka hususan katika idara ya Ununuzi na usambazai wa vifaa kuna mkufunzi mmoja tu anaesimamia kada ya manunuzi. Aidha katika Shule ya Afya Mbweni changamoto hii imejitokeza kwa kiwango kikubwa katika kila kada inayosomeshwa kwa mujibu wa takwimu za idadi ya wakufunzi wanaohitajika na hali halisi iliyopo ya walimu kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 123 : Upungufu wa watumishi SUZA**

| Kada | Kiwango cha chini ya wakufunzi naohitajika | shi walio- po sasa | Tofauti |
|---|---|---|---|
| gree in Medicine | 19 | 12 | 7 |
| gree in Dental Surgery | 10 | 3 | 7 |

| PLOMA PROGRAMMES | | | |
|---|---|---|---|
| armacy | 5 | 2 | 3 |
| nical Dentistry | 5 | 1 | 4 |
| ysiotherapy | 5 | 1 | 4 |

Upungufu wa watumishi katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar unasababisha kiwango cha utendaji kazi kuwa chini katika baadhi ya idara au vitengo na kupelekea kushindwa kutekeleza malengo yaliyopangwa. Pia, unasababisha watumishi waliopo kuelemewa na kazi na hivyo kupunguza ufanisi wa kazi.

Ukaguzi unapendekeza kupitia Ofisi ya Rais, Katiba ,Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuharakisha upatikanaji wa vibali vya ajira kwa mujibu wa uhitaji wa watumishi ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa watumisi katika Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar.

**Majibu ya Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar (SUZA)**

Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinakiri kukabiliwa na tatizo la upungufu wa watumishi hasa wanataaluma. Hii ni changamoto ya muda mrefu ambayo imesababishwa na sababu zifuatazo:

a. Zuio la ajira za watumishi kutoka katika Serikali Kuu lilitolewa kwa barua namba CAB.40/158/01/5 ya tarehe 08 Disemba, 2020.

Kwa lengo la kupunguza uhaba wa watumishi hasa wanataaluma kufuatia zuio la ajira, Uongozi wa Chuo uliomba kibali cha ajira 37 kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kujaza nafasi zilizotokana na wanataaluma waliostaafu, waliopata uteuzi na waliofariki. Barua zenye namba SUZA/BLM/70/19/VOL. I/67 ya tarehe 07 June, 2021 na BLM/138/U/C.1/ ya tarehe 16 June, 2021 zinahusika.

b. Uhaba wa waombaji wenye sifa zinazohitajika katika soko la ajira la ndani kwa nafasi za

wanataaluma. Uongozi wa Chuo unakabiliwa na changamoto ya kukosa waombaji wenye sifa zinapotangazwa ajira kujaza nafasi za wanataaluma. Hali hii imejitokeza katika mchakato wa ajira uliyofanyika mnamo tarehe 27/10/2021. Katika mchakato huu nafasi 16 kati ya nafasi 38 zilizotangazwa zilikosa waombaji wenye sifa. Jadueli namba 4 linahusika. Vile vile mnamo tarehe 23/10/2022, Uongozi pia ulitangaza tena nafasi 16 zilokosa waombaji wenye sifa zinazohitajika na kujitokeza tena nafasi 5 zilokosa waombaji wenye sifa zinazohitajika. Jadueli namba 6 linahusika.

Ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa waombaji wenye sifa zinazohitajika, Uongozi ulichukua hatua zifuatazo:

- Uongozi uliomba kibali cha kuajiri wanataaluma waliostaafu ambao bado wana uwezo wa kuendelea na kazi za kufundisha, barua namba SUZA/BLM/70/19/VOL.II/21 ya tarehe 29/7/2022 na BLM/98/UM/C.13/74 ya tarehe 25/08/2022 zinahusika.
- Kuomba vibali vya kuajiri wanataaluma wa kigeni, barua namba P33/2/23/CON/VOL.V/82 ya tarehe 26/01/2022 na BLM/98/UM/C/13/53 ya terehe 13/01/2023 zinahusika. Mpaka sasa Chuo kina jumla ya wanataaluma 11 wa kigeni Jadueli namba 3 linaonesha taarifa za wanataaluma waliyosaidia kupunguza uhaba kwa njia ya mkataba.
- Uongozi umewasilisha Ofisi ya Rais (Ikulu) pendekezo la kuongezewa muda wa utumishi kwa wanataaluma. Ilipendekezwa miaka ya kustaafu kwa lazima kwa mhadhiri/mhadhiri mwandamizi iwe 65 na kwa profesa mshiriki na profesa iwe 70 badala ya 60. Pendekezo hili lina lengo la kuwabakisha wanataaluma wazoefu wenye uwezo wa kiafya, kufundisha, kufanya tafiti na kutoa huduma za ushauri elekezi ili kusaidia kuwajenga wanataaluma wachanga na kupunguza uhaba wa wanataaluma uliopo. Barua zenye namb. SUZA/70/20/VOL.III/61 ya tarehe 24 Agosti, 2021 na CCB.51/196/01/33 ya tarehe 18 Agosti, 2021 ziliyoambatanishwa zinahusika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini ni kweli Chuo kikuu cha Taifa SUZA kinakabiliwa na uhaba wa walimu katika fani mbalimbali hata hivyo uongozi wa Chuo umechukua juhudi mbalimbali za kuhakikisha changamoto hiyo inapungua kwa kuomba kibali cha ajira Serikalini lakini juhudi hizo hazikufua dafu kwa vile baadhi ya nafasi hazikupata wataalamu wenye sifa zinazotakiwa kwa waombaji wa nafasi hizo.

Kamati inashauri Serikali kuyakubali Mapendekezo yaliyotolewa na Uongozi wa Chuo kwa kuruhisiwa kupata kibali cha ajira kwa kuajiri walimu wa nje kwa fani ambazo zimekosa wataalamu wa ndani ya nchi na mapendekezo mengine yaliyombwa na uongozi wa Chuo kenda Serikali kupitia barua mbalimbali kwa lengo la kukiimarisha Chuo hicho kitaalamu na Kwenda sambamba na ushindani wa vyuo vilivyopo ndani na nje ya Zanzibar katika kutoa mafunzo bora na yenye weledi.

**5.4.7.4 Changamoto za Miundombinu katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA)**

Miundombinu ya elimu ni nyenzo muhimu katika mazingira ya kufundishia na kujifunza katika vyuo vikuu na taasisi zingine za elimu. Miundombinu bora huwezesha ufundishaji bora, huboresha matokeo ya wanafunzi, na hupunguza idadi ya ukatishaji masomo na faida zingine.

Ukaguzi umebaini kuwa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kinakabiliwa na uhaba wa rasilimali ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa. Udahili wa wanafunzi umekuwa ukiongezeka wakati vitendea kazi na miundombinu ya elimu ikiendelea kubaki vilevile kama ilivyobainika katika Shule ya Afya Mbweni

Kwa mfano, katika Shule ya Afya Mbweni, ukaguzi umebaini kuwa idadi ya wanafunzi imekuwa ikiongezeka wakati rasilimali za chuo zimebaki vilevile. Upungufu ulibainika

kwenye vyumba vya madarasa na kumbi za mihadhara, dahalia, wafanyakazi (idadi ya wahadhiri), magari, na vifaa vingine vya mafunzo ya vitendo. Idadi ya wanafunzi wenye sifa za kujiunga na chuo katika mwaka 2020/2021 ilikuwa imeongezeka kwa kiwango kikubwa ukilinganisha na uwezo wa chuo wa kudahili wanafunzi.

**Kielelezo Na. 1 kinaonesha wanafunzi wa kada za Afya wenye sifa walioomba kujiunga na chuo na idadi ya wanafunzi waliodahiliwa kwa mwaka wa 2020/2021.**

**Jadweli Nambari 124 : Changamoto za Miundombinu katika Chuo cha SUZA**

| **Aina ya Fani** | **a kuda- hili** | **adi ya waliomba** | **Tofauti** |
|---|---|---|---|
| ctor of Medicine | 35 | 2 | 261 |
| ctor of dental Surgery | 10 | | 33 |
| chelor of Science in Nursing | 50 | | 37 |
| chelor of Science in Environmental Health | 55 | | -10 |
| loma in Clinical medicine | 65 | 2 | -173 |
| loma in Clinical Dentistry | 25 | | -63 |
| loma in Nursing and Midwifery | 50 | 1 | -80 |
| loma in Pharmacy | 65 | 2 | -162 |
| loma in Environmental Health | 50 | 1 | -54 |

Aidha katika Shule ya Afya mbweni ukaguzi umebaini hali isiyoridhisha ya hosteli za chuo na nyumba za makazi. Vyoo na miundombinu ya majitaka ndani ya baadhi ya dahalia imechakaa

Changamoto katika miundombinu ya elimu husababishwa na bajeti ndogo na fedha chache zinazoelekezwa kwenye uboreshaji wa miundombinu ya elimu na vifaa vingine vya kujifunzia. Ikiwa hatua za kurekebisha hazitachukuliwa, hali hii itaendelea kuathiri ubora na

viwango vya elimu yetu.

**Ukaguzi unapendekeza:-**

Serikali iongeze bajeti ya kuboresha Chuo Kikuu cha TaifaZanzibar katika miundombinu ya elimu na vifaa vya kujifunzia.

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar kianzishe mpango wa uwekezaji katika miundombinu ya elimu na zana za kujifunzia, ambapo asilimia fulani ya mapato ya ndani itumike katika utekelezaji wa mpango wa uboreshaji wa miundombinu na vifaa vya kujifunzia.

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar kinashauriwa kubuni miradi mingi inayohusiana na uhitaji na uimarishaji wa miundombinu pamoja na vifaa ya kujifunzia na kutafuta wahisani wa maendeleo kwa ajili ya ufadhili.

**Majibu ya Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar (SUZA)**

Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinakiri kukabiliwa na changamoto kubwa ufinyu na uchakavu wa miundombinu yake.

Katika kukabiliana na suala hili , Chuo kimeendelea na jitihada mbalimbali za kutenga fedha zake kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu hiyo pamoja na kutafuta wahisani wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mipya. Mfano wa juhudi hizo ni kama ifuatavyo;

Katika mwaka wa fedha 2023-24 ,Chuo kimetenga jumla ya shilingi bilioni 2.2 kupitia skuli husika kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu.

SUZA inakamilisha mpango mkuu wa ujenzi wa miundombinu katika kampasi zake. Kazi imefanywa kwa mashirikano ya karibu na Chuo kikuu cha Ardhi na Mpango huu unatarajiwa kuidhinishwa hivi karibuni.

SUZA kwa kushirikiana na SMT na SMZ imeendelea na jitihada za kutafuta wafadhili mbali mbali kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa miundombinu ya Chuo. kwa mfano, Chuo kinatekeleza mradi wa HEET unaotarajiwa kujenga majengo manne katika Kampasi ya Tunguu.

Pia Chuo kinatarajiwa kutekeleza mradi mwengine wa utanuzi wa miundombinu kupitia ufadhili wa BADEA ambapo mradi huo unatarajiwa kujenga majengo mengine manne katika Kampasi ya Tunguu kuanzia mwaka wa fedha 2023/24.

SUZA imeendelea na jitihada ya kutenga baadhi ya makusanyo yake kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, katika mwaka wa fedha 2023/24 Chuo kinatarajiwa kutumia kiasi cha TZS billion 4 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Skuli ya Meno ambalo pia litatumiwa kufundishia wanafunzi wa Skuli ya Afya na Sayansi za Tiba .

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na Maelezo yaliyotolewa na Uongozi wa Chuo katika kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha miundombinu ya vyuo vyake kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ya SMT katika kutafuta wafadhili mbalimbali.

Kamati inashauri uongozi wa Chuo kuongeza jitihada ya ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vya ndani kwa lengo la kuboresha mazingira na miundombinu ya vyuo vyake.

Aidha kuharakisha utekelezaji wa Mradi wa BADEA unatarajiwa kujenga majengo mengine manne katika Kampasi ya Tunguu kuanzia mwaka wa fedha 2023/24 na mradi wa HEET unaotarajiwa kujenga majengo manne katika Kampasi ya Tunguu.

**5.4.7.5 Kutokufanya Tathimini na Kupima Utendaji wa Watumishi**

Kanuni ya 93 ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 inasema kuwa, kila Taasisi ya umma italazimika kumfanyia tathmini ya utendaji wa kazi mtumishi wake kila mwaka. Fomu ya tathmini itatolewa na Afisi kuu ya Utumishi wa Umma .

Kanuni ya 93(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 inasema kuwa, tathmini

hiyo itamuwezesha mtumishi kupatiwa nyongeza ya mwaka, kupandishwa daraja, barua ya pongezi na tunzo kwa utendaji mzuri.

Aidha tathmini hiyo pia itapelekea mtumishi kushushwa cheo, kupatiwa mafunzo, kupatiwa uhamisho pamoja na kubadilishwa katika nafasi yake.

Lengo la kutathmini utendaji ni kubainisha, kupima na kuweka kumbukumbu za uwezo na mapungufu ya kila mtumishi ili kuweza kuchukua hatua za kuboresha ufanisi katika utumishi wa umma kama lengo endelevu. Ukaguzi kuhusiana na ufuatiliaji wa kanuni Utumishi wa Umma umebaini kuwa watumishi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar hawakufanyiwa tathmini na kupima utendaji kama inavyotakiwa na Kanuni tajwa hapo juu.

Kushindwa kutathmini na kupima utendaji wa watumishi husababisha uongozi kushindwa kutambua mapungufu ya kiutendaji ya watumishi wake ili kutengeneza mikakati na namna bora ya kuyashughulikia.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kutekeleza matakwa ya kikanuni za utumishi kwa kupima na kutathimini utendaji wa watumishi kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 ili kuweza kubaini mapungufu ya watumishi na kuweza kutatua changamotozao.

**Majibu ya Chuo Kikuu Cha Taifa Zanzibar (SUZA)**

Uongozi unakiri kuweko kwa changamoto hii.

Hata hivyo, zoezi hili lilianza kuekelezwa tena mara tu Uongozi wa SUZA ulipopokea barua yenye kumb CAB.40/158/01/31 ya tarehe 11 Mei, 2020 iliyoelekeza upimaji wa utendaji kazi kwa watumishi wa Chuo. Katika kutekeleza agizo hilo, Uongozi kupitia kurugenzi ya rasilimali watu uliunda Kamati maalum ya kutekeleza zoezi hilo kuanzia tarehe 15 Juni, 2020. (Dokezo husika limeambatanishwa)

Kamati hiyo ilipewa jukumu la kuandaa majukumu ya wafanyakazi wote, kuandaa viashiria vya ufanisi na shabaha za utekelezaji.

Jumla ya watumishi 606, Wanaataluma 234 na Waendeshaji 372 walifanyiwa tathmini hiyo. Mchakato wa tathmini ya utendaji kazi uliwasilishwa katika mamlaka husika na kuidhinishwa na Baraza la Chuo kupitia Kikao chake cha Dharura cha tarehe 19/10/2021 kwa lengo la kuwasilishwa OR Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa hatua stahiki.

Kukamilika kwa mchakato huu kulipelekea watumishi kupatiwa stahiki ya nyongeza barua SUZA/70/20/VOLIV/14 ya tarehe 4 Novemba, 2021, CCB.73/158/06/18 ya tarehe 09 Novemba, 2021 na CCB. 213/149/01/20 ya tarehe 10 Mei, 2022 zilizoambatanishwa zinahusika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile uongozi wa Chuo umekiri kuwepo kwa dosari hiyo hata hivyo hatua zimeshachukuliwa kwa kutekeleza zoezi hilo.2

Kamati inaendelea kushauri uongozi wa Chuo kufuata Kanuni ya 93 ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 inayozitaka Taasisi za umma kufanya tathmini ya utendaji wa kazi kwa watumishi wake kila mwaka kwa lengo la kuwawezesha watumishi hao kupatiwa nyongeza ya mwaka, kupandishwa daraja, barua ya pongezi na tunzo kwa utendaji mzuri wa kazi.

### 5.4.8 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA (IPA)

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umebainisha taarifa ya michango ya vyanzo vya mapato vya Chuo cha Utawala wa Umma , utendaji wa mwaka kwa kila chanzo cha mapato katika Chuo cha Utawala wa Umma pamoja na kubainisha dosari za kiutendaji zilizojitokeza wakati wa ukaguzi na kubainisha njia za utatuzi wa dosari hizo.

**Taarifa ya Mapato**

Chuo cha Utawala wa Umma kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,383,935,000. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 1,434,100,000 ikiwa ni ruzuku na shilingi 1,949,835,000 ikiwa ni makusanyo kutoka vyanzo vya ndani.

#### 5.4.8.1 Dosari katika ujenzi wa ukuta shilingi 722,929,920

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika jumla ya shilingi 722,929,920 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa ukuta katika Chuo cha Utawala wa Umma na kumlipa mjenzi ambae ni duka la Chuo cha Mafunzo.

Kwa mujibu wa makubaliano ya uongozi wa Chuo cha Utumishi wa Umma ni kwamba mzabuni atakaepewa kazi lazima awe na vigezo vinavyotambulikana na kukubalika na Bodi ya Usajili ya Wakandarasi ili kuhakikisha ujenzi huo unasimamiwa katika hali ya ubora na wenye kuleta tija iliokusudiwa. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kuwa mzabuni aliyepewa kazi hiyo alikosa sifa zilizotarajiwa kupatikana kwa mujibu wa matakwa ya Chuo. Miongoni mwa dosari zilizobainika ni kama zifuatazo:-

Kukosekana kwa cheti cha usajili cha Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ambacho kitapelekea mzabuni huyo kufanya kazi kisheria na kuhakikisha kunapatikana kwa tozo ya kodi ambayo itapaswa kulipwa Serikalini.

- Kukosekana kwa utambulisho wa usajili kutoka Bodi ya Usajili wa Wakandarasi.
- Kukosekana kwa usajili wa mlipa kodi ambapo pamoja na uwepo wa taasisi ya Serikali kufanya kazi za Serikali lakini bado haijazuia taasisi hizo kulipa kodi.
- Pamoja na kuwa mchakato wa upatikanaji wa ujenzi wa ukuta haukuwa na ushindani wa wazi wa zabuni bado haujazuia taratibu za kisheria kufuatwa kwa mujibu Sheria ya Bodi ya Usajili wa Wakandarasi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Utawala wa Umma kuhakikisha kwamba pamoja na kutumia "force account" bado inatakiwa kuhakikisha wazabuni hao wana sifa na wamesajiliwa kwa mujibu wa sheria ili kuepusha kujitokeza kujenga ujenzi katika kiwango kisicho ridhisha na kupelekea kutokupatikana kwa tija iliyokusudiwa. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana na katika jadweli la hapo chini:-

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imebaini kuwa Chuo Cha Utawala wa Umma kutofuata sheria kuliko sababishwa na kujenga uaminifu na mazoea kwa taasisi ya kiserikali ambayo ni Chuo Cha Mafunzo kwa kumpa zabuni ya ujenzi wa ukuta huo pasi na kujiridhisha iwapo kampuni hiyo ina sifa za kisheria za kupewa zabuni hiyo zikiwemo usajili wa kampuni katika bodi ya wakandarasi, usajili katika Mamlaka ya Manunuzi na usajili wa Mlipa kodi.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Uongozi wa Chuo cha Utawala wa Umma umekiri kutofuata Sheria ya katika kutoa zabuni kwa Chuo Cha Mafunzo Kamati ya Laac inashauri yafuatayo

Kuacha kufanya kazi kwa mazoea badala yake yajikite katika kufuata misingi ya kisheria katika shughuli zao mbalimbali wanazofanya zikiwemo kutoa zabuni mbalimbali za ujenzi kwa kampuni zilizosajiliwa ili mapato ya Serikali yaweze kupatikana

Aidha Kamati inashauri utumiaji wa njia ya kutokuepo kwa ushindani wa zabuni (single source) uendesababa na kufuatwa kwa taratibu nyengine za kisheria kikamilifu na isiwe ni fursa ya kikiuka taratibu nyengine za kisheria

**5.4.8.2 Kutowasilishwa kwa mapato ya shilingi 105,505,488**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika chuo cha Utawala wa Umma kimefanya zuio la kodi ya ongezeko la thamani yenye thamani ya shilingi 105,505,488 kutokana na makato walioyafanya yanayotokana na mzabuni Duka la Chuo cha Mafunzo kutokana na huduma ya ujenzi wa uzio wa ukuta alioufanya katika eneo la chuo.

Dosari iliobainika katika ukaguzi ni kutokuwasilishwa fedha hizo kwenye mamlaka zinazohusika katika makusanyo ya mapato yanayotokana na makato ya wazabuni na watoa huduma mbalimbali kwa kubainika kuwa mzabuni aliepewa kazi hio hakusajiliwa kisheria na kupelekea kukosekana kwa namba ya utambulisho ya mlipa kodi jambo ambalo limepelekea fedha hizo kutokupokelewa kwa vile hazitajuilikana alifanya uhaulisho wa muamala huo.

Kutokana na kutokuwasilishwa fedha za mapato katika mamlaka husika kunapelekea kuikosesha Serikali mapato na hatimae malengo ya Serikali ya kukuza mapato ya ndani yanayotokana na watoa huduma mbali mbali kuweza kufikiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Utawala wa Umma kuhakikisha wanafuata misingi ya sheria ikiwemo kutoa zabuni kwa taasisi zilizosajiliwa kisheria ili kuepuka

kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma unaotokana na kutokuwasiliswa kwa mapato ya kodi ya thamani pamoja na kodi ya zuio katika mamlaka zinazohusika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Chuo Cha Utawala wa Umma (IPA) kimekiri kutowasilisha zuio la kodi ya ongezeko la thamani kwa Mamlaka husika kutokana na Makato waliyofanya ni ya Mzabuni ambae hajasajiliwa Mamlakaza za kodi hadi sasa na kusababisha kuikosesha Serikali mapato hata hivyo Kamati inaendelea kutoa ushauri kwa Chuo kufuata taratibu za kisheria zilizowekwa kwa lengo kuipatia Serikali mapato.

**5.4.8.3 Matumizi yasiyo na tija shilingi 25,496,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika mnamo tarehe 30 Juni, 2020 Chuo cha Utawala wa Umma kilisaini hati ya makubaliano (memorandum of understanding) na mkataba wa kitaaluma (Agreement on Academic Collaboration) na Chuo kikuu cha Dododma (UDOM) kwa lengo la kuwaendeleza watumishi wake kwa ngazi ya shahada ya uzamili (Master Degree) na ngazi ya uzamivu (PhD) kama ilivyoagizwa na Serikali kupitia mpango wa dharura wa kuimarisha Chuo cha utawala wa Umma ili kumudu vizuri kuendesha mafunzo ya shahada ya kwanza kupitia barua ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Katika Sheria na Utumishi wa Umma ya tarehe 4 Septemba 2018 yenye kumbukumbu namba CAB131/196/01/41.

Kupitia kifungu cha 3.1.7 cha mkataba wa kuwaendeleza watumishi baina ya IPA – UDOM, Chuo cha utawala wa Umma kilikuwa na jukumu la kuwatafutia nyumba ya makazi wakufunzi kutoka UDOM.

Katika utekelezaji wa matakwa ya kifungu 3.1.7 ukaguzi umebaini Chuo cha Utawala wa Umma kimefunga mkataba na Ndugu Mohamed Khamis Mohamed wa

ukodishwaji nyumba iliopo Tunguu kwa muda wa miaka miwili kwa thamani ya shilingi 14,000,000 ambapo sawa na shilingi 7,000,000 kwa mwaka.

Aidha, imebainika Chuo kimefanya malipo ya awali ya shilingi 7,000,000 kwa ajili ya malipo ya kodi ya mwaka wa mwanzo, malipo ya gharama za ununuzi wa fanicha pamoja na mahitaji mengineyo ya shilingi 11,496,000 ambapo hadi ukaguzi unakamilika chuo kimefanya malipo ya shilingi 18,496,000 kwa hatua ya awali. Dosari zilizobainika katika ukaguzi ni kama zifuatazo:-

Kutokupatikana kwa tija iliyokusudiwa ya upatikanaji wa huduma kwa walimu kutokana na mazingira yasiyoridhisha ya nyumba hiyo.

Thamani ya kodi ya shilingi 7,000,000 haiyendani na uhalisia wa mazingira ya nyumba ilivyo.

Kutokukubaliwa kwa nyumba iliyokodiwa kwa ajili ya wakufunzi wa chuo cha UDOM jambo ambalo limepelekea nyumba hiyo kutumiwa na askari wa UMAWA kinyume na malengo yaliyokusudiwa bila ya uwepo wa malipo yoyote.

Chuo kufanya matumizi ya shilingi 11,496,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbalimbali bila ya kushirikishwa kitengo cha manunuzi na hatimae manunuzi hayo yamefanywa na Afisa Sheria ambae ni Katibu wa Bodi ya Chuo.

Uwepo wa mazingira hatarishi wa eneo liliopo nyumba kwa mali zilizomo ndani ya nyumba pamoja na usalama wa wakaazi jambo ambalo limepelekea wakufunzi wa chuo cha UDOM kuikataa nyumba hio.

Kutokuzingatiwa kwa hadhi ya wakufunzi hao

Kutokana na dosari zilizobainika hapo juu na kwa vile ni muda wa mwaka mmoja tangu chuo kufanya malipo ya kodi ya mwanzo na hakuna tija iliyopatikana ya malipo hayo kinachojitokeza ni viashiria vya ufujaji wa fedha za umma kunakopelekea kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora kuliangalia kwa kina suala hili ili kunusuru bakaa ya fedha ya shilingi 7,000,000 ambayo haijalipwa kuendelea kupotea bila ya uwepo wa tija iliokusudiwa. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika uchunguzi wa hoja hii imebaini kutokamilika kwa kwa utekelezaji wa hati ya ya makubaliano (memorandum of understanding) na mkataba wa kitaaluma (Agreement on Academic Collaboration ) na Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) hali iyopelekea kuviza juhudi za kuwaendeleza kitaalamu watumishi wa chuo hicho kwa ngazi ya Shada ya Uzamili (Master Degree) na ngazi ya Uzamivu (PHD) kutokana na wakufunzi kutoka UDOM kukataa kuja Zanzibar kutokana na kutorizika na nyumba walizopangishiwa kwa kusingizio cha kukosa uhuru na faragha za starehe zao wakiwa katika mazingira ya nyumba hiyo ambapo ni tofauti na mazingira wanayohitaji ya kuishi hoteli au nyumba za kulala wageni ambazo Chuo wamekiri kutomudu gharama hizo.

Hata hivyo, Kamati imeelezwa kuwa bado jitihada zinaendelea ili kutafuta suluhu ya jambo hilo baina ya Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) na Chuo Kikuu Cha DODOMA (UDOM)

Aidha Kamati katika kujua ukweli wa hoja hii imeomba kuona nyumba hiyo iliyoandaliwa kwa ajili ya wakufunzi ili kuthibitisha dosari zilizoelezwa na mdhibiti, Kamati imeelezwa kuwa kwa sasa nyumba hiyo imerudishwa kwa mmiliki na kwa muda huo wa jioni ni vigumu kuweza kumpata muhusika kwa vile si mkaazi katika eneo hilo, hivyo Kamati imeshidwa Kuthibitisha thamani ya kodi ya Tsh 7,000,000 kulingana na ubora wa nyumba hiyo, hali halisi ya mazingira hatarishi na hadhi ya nyumba kulingana na wahadhiri hao

Vile vile Uongozi wa Chuo umekiri kufanyika kwa manunuzi ya vifaa mbalimbali na Afisa sheria ambae ni Katibu wa Bodi kwa kupewa amri ya kutekeleza shughuli hiyo badala ya kitengo cha manunuzi jambo ambalo ni kinyume na taratibu za sheria za manunuzi.

**Mandekezo ya Kamati**

Kwa vile mkataba huo hauko mbali kumalizika basi ni vyema Uongozi wa Chuo kuendelea na mkataba huo hadi ukomo wake na kufuatilia kwa karibu zaidi changamoto zilizojitokeza na kutafuta suluhu ya makubaliano hayo bila ya kuharibu uhusiano baina pande mbili za mkataba ili tija uliyokusudiwa iweze kupatikana kwa kipindi chote cha muda wa mkataba.

Aidha Kamati inashauri pindi mkataba huo ukiisha ni vyema uongozi wa chuo kuanzisha uhusiano na msaada wa kitaaluma katika vyuo vya ndani vya Zanzibar na ikibidi kutoka nje ya Zanzibar suala la kuanzisha uhusiano lizingatie sana kufanana kwa mazingira na tamaduni baina ya pande mbili za Mkataba, au kufanya mazungumzo ya awali kabla ya kufunga mkataba ili pande zote zikubaliane namna ya kuendesha makubaliono hayo ili kudhibiti upotevu wa fedha za Serikali na tija iliyokusudiwa iweze kufikiwa.

Vilevile Kamati inaomba uongozi wa chuo kuacha kuwapa majukumu watumishi ambao hawastahili kufanya kazi hizo kwa mujibu wa taaluma zao walizoajiriwa nazo kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya utumishi wa umma na kupelekea kazi hiyo kukosa ufanisi na kuwepo kwa matabaka miongoni mwa watendaji.

**5.4.8.4 Matumizi mabaya ya fedha za uendeshaji wa vikao vya Bodi shilingi 29,359,000**

Kwa mujibu wa utaratibu wa uendeshwaji wa vikao vya Bodi vya Baraza la chuo cha Utumishi wa Umma linatakiwa kufanya vikao vinne vya kawaida na vikao viwili vya

dharura ambapo jumla ya vikao sita kwa mwaka.

Aidha, Chuo cha Utumishi wa Umma kimepanga kutumia jumla ya shilingi 18,600,000 kwa ajili ya uendeshaji wa vikao vya Baraza la Chuo kwa mwaka, kwa mujibu wa miongozo ya utumishi pamoja na matakwa ya sheria kufanya vikao 6 tu kwa mwaka. Dosari iliobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa vikao 8 kinyume na utaratibu wa sheria na kupelekea kutumia jumla ya shilingi 29,359,000 ambapo kumejitokeza uwepo wa ziada ya matumizi yaliotumika nje ya mpango wa matumizi ya bajeti ya shilingi 10,759,000 sawa na asilimia 63 ya makadirio bila ya kuzingatia matakwa ya kisheria jambo ambalo limepelekea kujitokeza viashiria vya ukiukwaji wa sheria, miongozo ya utumishi wa umma pamoja na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Ummaya mwaka 2016.

Kufanya vikao vya baraza la chuo bila ya kuzingatia thamani halisi ya fedha, matakwa ya sheria na kanuni kunapelekea kujitokeza kwa matumizi mabaya ya fedha za Umma na kukosekana kwa udhibiti mzuri wa matumizi yasio ya lazima.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora kuhakikisha unakaa na uongozi wa Chuo cha IPA kutathmini ajenda za vikao vya lazima na vya dharura ili kupunguza gharama za matumizi yasio ya lazima yanayotokana na matumizi mabaya ya fedha za Umma. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Uongozi wa Chuo Umekiri kufanya vikao vya bodi nje utaratibu Kamati haikuona haja ya kuendelea na hoja hii badala yake imeomba kupatiwa muhtasari wa vikao hivyo viwili vya dharura na Kamati iliweza kupatiwa nyaraka hizo kwa ukaguzi na kubaini kuwa

nyaraka hizo hazikuwa za vikao vya dharura kwa mujibu kichwa cha habari (heading) na Agenda zilizomo, hivyo Kamati haikurizika na nyaraka hizo.

Hata hivyo Kamati inatoa ushauri kwa Uongozi wa Chuo cha Utawala wa Umma kufuata utaratibu na miongozo ya utumishi kwa kufanya vikao sita vya bodi kwa mwaka na kama kuna dharura ya jambo mahsusi ni vyema kutumia njia nyengine za vikao ikiwa idadi iliyopangwa kufanyika vikao vya bodi imeshatimia ili kujiepusha na ukiukwaji wa miongozo na taratibu za uendeshaji wa vikao vya bodi.

### 5.4.10 CHUO CHA KIISLAM ZANZIBAR

**Taarifa ya Mapato**

Chuo cha Kiislam Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 303,400,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Chuo kilikusanya jumla ya shilingi 315,041,976 sawa na asilimia 103 ya makadirio.

**Majibu ya Chuo**

Chuo cha Kiislamu hakikuandaa majibu mahsusi kuhusiana na Taarifa ya Mapato, hata hivyo, kilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

**Taarifa ya Matumizi**

Chuo cha Kiislam Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kiliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 933,372,000. Kati ya hizo shilingi 874,372,000 kwa ajili ya mshahara na shilingi 59,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shillingi 1,016,301,275 ziliingizwa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia 109 ya makadirio, Kati ya fedha hizo shilingi 959,697,103 zilitumika kwa ajili ya mshahara sawa na asilimia 110 ya makadirio na shilingi 56,604,172 zilitumika kwa ajili matumizi mengineyo sawa na asilimia 96 ya makadirio.

**Majibu ya Chuo**

Chuo cha Kiislamu hakikuandaa majibu mahsusi kuhusiana na Taarifa ya Matumizi, hata hivyo, kilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia Taarifa hizi Kamati ya LAAC ilibaini mapungufu kadhaa kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ikiwemo, baadhi ya "Note" kwa mfano "Note" 4, 5, 7 na kadhalika kukosa maelezo. Hali hii inaashiria Taasisi husika kuficha baadhi ya taarifa jambo ambalo ni kwenda kinyume na taratibu za ufungaji wa hesabu.

Kutokana na dosari hizo, Kamati ya LAAC ilimtaka Mhasibu wa Chuo kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya Mapato na Matumizi husika, hata hivyo, Mhasibu huyo aliieleza Kamati kuwa Chuo kiliajiri (hire) vijana kwa ajili ya kufunga hesabu ya mwaka husika. Hii ni kutokana na kuwa hana uelewa wa kutosha kuhusiana na ufungaji wa hesabu.

Kamati ya LAAC ilisikitishwa na kauli hiyo kwani fedha za umma zilizotumika kuwalipa vijana hao zimepotea bure kwa kuwa hakuna tija yoyote iliyopatikana.

Kwa kuwa Mhasibu alishindwa kuielezea Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka kutokana na sababu zilizoelezwa hapo kabla, Kamati ya LAAC ilishindwa kujadili kwa kina Taarifa ya Mapato na Matumizi.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kuweka katika Taasisi Wahasibu wenye sifa ili kuepusha dosari kama hizo.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

**5.4.10.1 Mapungufu yaliyojitokeza katika ufungaji wa hesabu**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Chuo cha Kiislamu hakikuweza kuzingatia matakwa ya ufungaji wa hesabu kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa na kupelekea hesabu za Chuo cha Kiislam kutokuonesha sura sahihi na halisi kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa.

Aidha, ukaguzi ulifanya mawasiliano ya mara kwa mara ikiwemo kuwataka wahusika wafanye marekebisho juu ya dosari zilizobainika ili kuepuka kujitokeza kwa wingi wa hoja za ukaguzi ambazo zitapelekea utolewaji wa hati isioridhisha jambo ambalo hawakuweza kutekeleza hadi ukaguzi unakamilika taarifa za hesabu za Chuo cha Kiislam zilikuwa na dosari zifuatazo:-

**a) Taarifa ambazo hazikuambatanishwa na hesabu za mwisho wa mwaka**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi zilikosa uchambuzi uliombatanishwa kwa lengo la kubainisha mchanganuo wa kila taarifa pamoja na thamani halisi ya fedha kwa kila muamala uliobainishwa jambo ambalo limepelekea kuwasilisha taarifa za ujumla ambazo hazioneshi uchambuzi wa taarifa za kujitosheleza ili kujuwa thamani halisi kwa kila kifungu kilichooneshwa.

Aidha, pamoja na dosari hiyo imebainika kukosekana kwa taarifa muhimu za mali za kudumu zinazomilikiwa na Chuo cha Kiislam kuoneshwa katika hesabu za mwisho wa mwaka jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa ugumu wa kuweza kupima ukwasi uliofikiwa pamoja na kushindwa kubaini madeni yanayodaiwa au wanayodai ambapo ukaguzi umeshindwa kufanya uchambuzi wa wastani (ratio analysis) ili kupima dhima za mpito pamoja na mali halisi za muda mfupi.

Vile vile, kumekosekana taarifa muhimu za hesabu za mapato zinazotumika kukusanya fedha za mapato kupitia vyanzo mbalimbali vilivyopo katika Chuo cha Kiislamu jambo ambalo limeshindwa kujulikana makadirio halisi ya fedha yanayokusnywa kwa kila chanzo cha mapato pamoja na mapato halisi yanayopatikana kwa chanzo hicho jambo ambalo limepelekea baadhi ya hesabu za mapato kutokuonekana katika kitabu cha taarifa za mapato na matumizi kilichowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kutokuonekana kwa taarifa hizo kunapelekea hesabu ya Chuo cha Kiislam kutokuonesha sura sahihi na halisi kutokana na kutokuzingatiwa viwango vya ufungaji wa hesabu kitaifa na kimataifa. Hata hivyo jitihada za kuwataka wafanye masawazisho (adjustment) kwa taarifa za fedha na kuwasilishwa Ofisi ya Mdhibiti kwa ajili ya

kutolewa maoni ya ukaguzi Chuo cha Kiislamu hawakutekeleza agizo hili. Mchanganuo wa baadhi ya taarifa zilizokosekana ni kama zinavyoonekana katika jadweli:-

| Nam. | Fedha zilizopokelewa kutoka WEMA | Chambuzi namba |
|---|---|---|
| 1. | Ruzuku (Exchequer issues) | 1 |
| 2. | Mapato ya chuo | 1 |

**Majibu ya Chuo**

Chuo cha Kiislamu kupitia Kitengo cha Uhasibu kiliweza kuambatanishwa na hesabu za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa miongozo ya kimataifa ya ufungaji wa hesabu inavyoelekeza. Kupitia ripoti ya fedha ya mwaka 2020/2021 Afisa Muhasibu wa Chuo cha Kiislamu aliweza kuziambatanisha chambuzi hizo kwa mujibu wa utaratibu wa usimamizi wa fedha.

Pamoja na ripoti hii naambatanisha na ripoti ya hesabu ya mwaka (financial statement) ambayo ndani yake inaonesha chambuzi (notes) na hesabu za mwisho wa mwaka kama miongozo ya kimataifa ya ufugaji wa hesabu inavyoelekeza. Ripoti hii pia iliwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali naambatanisha nayo nambari ya kumbukumbu pamoja na tarehe ya barua na kupokelewa kwake.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Chuo kwa kuwa Kamati iliyabaini pia mapungufu hayo, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 5.4.10.2 Ajira ya muda mfupi kinyume na taratibu za Utumishi wa Umma (Casual labour)

Ukaguzi umebaini kwamba Chuo kimetumia jumla ya shilingi 13,050,000 kwa kaujiri watumishi wa muda mfupi kwa ajili ya kufanya kazi za usafi bila ya kuomba kibali cha ajira kutoka Utumishi wa Umma kwa ajili ya wafanyakazi hao. Kwa mujibu wa kanuni za Utumishi wa Umma chini ya kifungu cha 37(4) cha sheria namba 2 ya mwaka 2011 ya Utumishi wa Umma, kifungu kidogo 135(1)(2) Taasisi ya Serikali hairuhusiwi kuajiri watumishi wa muda maalum/kutwa kwa kipindi kirefu.

Uwepo wa uajiri wa watumishi wa mkataba kwa muda mrefu bila ya kuthibitishwa kazi au kuajiriwa moja kwa moja kunaweza kupelekea kuwakosesha haki zao za msingi ikiwemo kupata mafunzo ya muda mrefu,kupata ufadhili wa mikopo,kupata haki zao za msingi katika mfuko wa hifadhi ya jamii jambo linaweza likapelekea kujitokeza kwa mogogoro isio ya lazima na kupelekea kukosekana kwa tija iliokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Kiislamu kuhakikisha ajira zote zinazofanyika zinazingatia misingi ya utumishi wa umma.

**Majibu ya Chuo**

Ni kweli wakati wa Ukaguzi wa hesabu za Chuo cha Kiislamu ilibainika Chuo kimetumia jumla ya shilingi 13,050,000 kwa kuajiri watumishi wa muda mfupi kwa ajili ya kufanya kazi za usafi bila ya kuomba kibali cha ajira kutoka Utumishi wa Umma kwa ajili ya wafanyakazi hao.

Chuo kiliweza kufuata taratibu za kiutumishi na kujiepusha na migogoro isiyokuwa na lazima ambapo iliweza kuwaondosha wafanyakazi hao ili kuweza kukiweka Chuo katika mikono salama. Kwa sasa usafi wa Chuo cha Kiislamu katika maeneo yake unafanywa na walimu wanafunzi kwa usimamizi wa wakufunzi wao.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati ya LAAC ilisikitishwa na majibu ya Chuo na hasa ikizingatiwa kuwa kwa ngazi ya Chuo wanafunzi wanaosoma Chuoni hapo hawastahiki tena kufanya usafi katika Chuo husika. Hivyo, kitendo cha Walimu Wanafunzi kufanya usafi katika Chuo hicho kinawashushia hadhi Walimu hao watarajiwa.

Kwa msingi huo, hoja hii imebaki kama ilivyo, ingawa Chuo kimeanza kupokea Maafisa mbali mbali akiwemo Afisa Utawala.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inakishauri Chuo kuajiri Kampuni ya Usafi na Walimu watarajiwa wahudhurie Chuoni hapo kwa ajili ya kupata elimu tu.

Vile vile, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kukipatia Chuo Wataalamu mbali mbali ili Chuo hicho kiendane na wakati.

**3.3 Kukosekana kwa mkataba wa huduma ya Mgahawa eneo la Chuo**

Ukaguzi umebaini kwamba hakuna mkataba wa kukodisha mgahawa unaomilikiwa na Chuo cha Kiislam Zanzibar ambao unatoa huduma ya chakula katika eneo la Chuo. Chuo kimekodisha mgahawa huo kwa mtu binafsi ambapo anatakiwa kulipa kodi kama walivyokubaliana. Kutokana na sababu zisizoeleweka hadi tunamaliza ukaguzi hatukuweza kupata mkataba huo wala kujua ni kiasi gani kinachotakiwa kulipwa.

Kukosekana kwa vielelezo hivyo kunaweza kukapelekea upotevu wa fedha za umma unaotokana na kutokuvianisha vyanzo vya mapato pamoja na kutokujulikana mapato halisi yanayokusanywa kutokana na vyanzo hivyo jambo ambalo litapelekea chuo kushindwa kufikia malengo waliojipangia.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Chuo kuhakikisha unasimamia vyema majukumu yao na kuandaa mkataba kwa mpangaji wa mkahawa huo.

**Majibu ya Chuo**

Ni kweli katika ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Chuo cha Kiislamu 2020/2021 kwamba hakuna mkataba wa kukodisha Mgahawa unaomilikiwa na Chuo cha Kiislamu Zanzibar ambao unatoa huduma ya chakula katika eneo la Chuo.

Mgahawa huu wa Chuo cha Kiislamu hapo awali ulikuwa unamilikiwa na Uongozi wa Serikali ya Wanafunzi ambao waliujenga kwa jitihada zao binafsi. Kutokana na maelekezo ya yaliotolewa na Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kwa Chuo kimeweza kuandaa mkataba wa kukodishia Mgahawa huo kwa wanaohitaji kutoa huduma za vyakula chuoni.

Pamoja na barua hii naambatanisha na kivuli (copy) ya mkataba wa kukodisha Mgahawa wa Chuo cha Kiislamu Zanzibar.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imeibakisha hoja hii kwa kuwa wakati wa ukaguzi kuliwa hakuna mkataba husika, ingawa Chuo kilikuwa hakimiliki mgahawa huo.

Kwa kuwa mgahawa upo katika eneo la Chuo, Kamati ya LAAC inakishauri Chuo kikiandaa mkataba ionekane kuwa Mkuu wa Chuo ni mlezi na Rais wa Serikali ya Wanafunzi awe ni shahidi.

Sambamba na hayo, katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Chuo cha Kiislamu kina Mkuu wa Chuo, isipokuwa kwamba, Mkuu wa Chuo huyo endapo atahitaji jambo lolote lazima jambo hilo lipitie kwanza kwa Mkurugenzi wa Idara ya Mafunzo ya Ualimu na baadae kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa maamuzi.

Hali hii inaleta urasimu mkubwa kiutendaji kwani endapo Mkurugenzi huyo hatokuwa na hamu “interest” na jambo husika basi ana haki ya kulikataa jambo hilo kabla ya kufika kwa Katibu Mkuu.

Kamati ya LAAC ilishtushwa na hali hiyo, hii ni kutokana na kuwa uendeshaji wa Chuo wa namna hiyo unachangia kwa asilimia kubwa uzoroteshaji wa  utendaji wa Chuo.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inaitaka Serikali kukirejeshea hadhi yake Chuo hicho kama ilivyokuwa hapo kabla ili Chuo kiweze kutekeleza shughuli zake kwa uhuru.

Vile vile, Kamati ya LAAC ilishangazwa na taarifa iliyopokea baada ya majadiliano ya kina na watendaji wa Chuo hicho kuwa Chuo kina tawi lake Pemba, na tawi hilo lipo chini ya Afisa Mdhamini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kitendo ambacho ni kinyume na utaratibu.

Kutokana na dosari hizo, Kamati ya LAAC inaitaka Serikali kuliangalia upya suala hilo na inapendekeza kufanyiwa marekebisho muundo wa Chuo na kuwekwa nafasi ya Msaidizi wa Mkuu wa Chuo ambaye atahusika moja kwa moja kutekeleza shughuli za Chuo kwa upande wa Pemba.

### 5.5.1 MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA MADAWA YA KULEVYA

**Taarifa ya Mapato**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 3,085,620,670 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 659,554,516 ziliingiziwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ambazo ni sawa na asilimia 21 ya makadirio.

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya hawakuandaa majibu mahsusi kuhusiana na Taarifa ya Mapato, hata hivyo, ilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya haina chanzo cha mapato, isipokuwa kwamba, katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilipata mapato kupitia mradi ilikuwa inatekeleza ambapo ilipokea jumla ya Tsh. 1,550,814,388 na mwaka wa fedha 2020/2021 ilipokea Tsh. 659,554,516, hivyo, kiwango hicho cha fedha kilipungua ukilinganisha mwaka wa fedha uliopita.

**Taarifa ya Matumizi**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 3,085,620,670. Kati ya fedha hizo shilingi 1,174,020,670 zilikadiriwa kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 1,911,600,000 zilikadiriwa kutumika kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 659,554,516 zimeingiziwa na kutumika kwa shughuli mbali mbali za ofisi sawa na asilimia 21 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 654,554,882 zilitumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 56 ya makadirio na shilingi 4,999,634 zilitumika kwa matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 0.26 za makadirio.

**Majibu ya Mamlaka**

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya hawakuandaa majibu mahsusi kuhusiana na Taarifa ya Matumizi, hata hivyo, ilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Katika mwaka huo wa fedha Mamlaka haikuwa na fedha za maendeleo kama ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu, isipokuwa kwamba, ilitumia fedha za Matumizi Mengineyo kwa ajili ya ununuzi wa mali za afisi.
2. Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka ina mapungufu kwa mfano: “Note” 9 imejumuisha matumizi ambayo hayakupaswa kuwekwa hapo jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya ufungaji wa hesabu.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inamshauri Mhasibu kuwa makini wakati anatekeleza shughuli zake ili kuepuka kasoro zisizo na msingi.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 5.5.1.1 Malipo Yaliyofanywa kwa Njia Taslim shilingi 18,000,000

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa jumla ya shilingi 18,000,000 zilizotumika kwa ajili ya kazi mbali mbali lakini malipo hayo yamefanyika kwa njia ya fedha taslim hali ambayo inaweza kupeleke kufanyika kwa matumizi yenye kutiliwa shaka ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Malipo yenyewe ni kama yanavyoonekana katika jadueli:-

<table>
<tr><th>Hati namba</th><th>Kiasi cha fedha kilichotumika (Tsh.)</th><th>Aliyelipwa</th><th>Maelezo</th></tr>
<tr><td>1/6</td><td>9,843,100</td><td>Mkurugenzi</td><td>Malipo ya kuteketeza Madawa ya kulevya Pemba</td></tr>
<tr><td>2/6</td><td>1,177,500</td><td>Mkurugenzi</td><td>Malipo ya fedha kwa ajili ya kikao cha Tume</td></tr>
<tr><td>3/6</td><td>763,000</td><td>Mkurugenzi</td><td rowspan="2">Malipo ya kuteketeza Madawa ya Kulevya Unguja</td></tr>
<tr><td>4/6</td><td>1,193,325</td><td>Mkurugenzi</td></tr>
<tr><td>5/6</td><td>131,810</td><td>Mkurugenzi</td><td>Mkurungenzi Malipo kwa ajili ya ununuzi wa feni na ufundi</td></tr>
<tr><td>6/6</td><td>100,000</td><td>Mkurugenzi</td><td>Malipo ya fedha kwa kazi maalum ya operation</td></tr>
<tr><td>7/6</td><td>100,000</td><td>Mkurugenzi</td><td>Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa</td></tr>
</table>

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | maksi |
| 8/6 | 10,000 | Mkurugenzi | Marejesho ya fedha kwa ajili ya kifaa cha gari SMZ 919A |
| 9/6 | 1,500,000 | Mkurugenzi | Malipo ya fedha ka ununuzi wa Umeme |
| 10/6 | 200,000 | Mkurugenzi | Mkurungenzi Malipo ya fedha kwa ajili ya viburudishaji |
| 11/6 | 250,000 | Mkurugenzi | Malipo ya fedha kwa ajili ya benk charges kwa mwaka |
| 12/6 | 35,000 | Mkurugenzi | Malipo ya fedha kwa ununuzi wa chakula |
| 13/6 | 49,000 | Mkurugenzi | Marejesho ya fedha ya ununuzi wa chakula |
| 14/6 | 97,400 | | |
| 15/6 | 2,500,000 | Mkurugenzi | Malipo kwa ajili ya mafunzo ya uchunguzi wa ukamataji wa dawa za kulevya |
| **Jumla** | **18,000,000** | | |

**Majibu ya Mamlaka**

Tume ilipokea fedha Tsh. 18,000,000 kwa matumizi ya dharura ya kawaida ambapo muda wa matumizi kwa kutumia mfumo wa 'Epicor' ushafikia mwisho kwa ajili ya kujitaarisha na ufungaji wa hesabu za Serikali lakini baada ya kujitokeza uhitaji mkubwa wa fedha hizi na muda wa kufanya matumizi kwa mtandao ulikuwa umefungwa ndipo Wizara ya Fedha ililazimika kutia fedha hizi kwa njia ya 'Dummy' na

matumizi yake kufanyika kupitia hesabu yetu iliopo PBZ kutokana na uhitaji uliojitokeza.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa barua kuhusiana na maombi ya fedha yaliyofanyika, hata hivyo, Mamlaka haikuwasilisha barua hiyo mbele ya Kamati kwa madai kuwa fedha hizo ziliingizwa baada ya majadiliano na Makamo wa Pili wa Rais.

Kamati ya LAAC haikukubaliana na maelezo ya Mamlaka hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC imeishauri Mamlaka kutekeleza shughuli zake kama taratibu zinavyoelekeza ili kuepusha dosari zisizo za lazima.

### 5.5.1.2 Kuchelewa kufika kwa Gari iliyonunuliwa shilingi 58,373,700

Katika ukauzi uliofanyika imebainika kuwa Tume ya Uratibu wa Kitaifa na Udhibiti wa dawa za Kulevya imefunga mkataba na Kampuni ya Safmi Development Ltd tarehe 18/8/2019 kwa ajili ya ununuzi wa gari aina ya Hilux Double Cabine kwa jumla shilingi 58,373,700 ambapo hadi ukaguzi unakamilika fedha zilizokusudiwa tayari zilishalipwa kwa kampuni iliyokusudiwa.

Kufanya hivyo kunapelekea shughuli zilizopangwa kutokutekelezwa kwa wakati na kusababisha upotevu wa fedha za Serikali kwa kutozingatia vipengele muhimu vya makubaliano ya mkataba ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Mamlaka**

Uongozi baada ya kuona hakuna mafanikio yoyote katika jitihada mbali mbali za kuifuatilia gari hiyo ikiwemo kufuatilia katika ubalozi, Mamlaka ilichukua hatua ya kuipeleka katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumu Zanzibar (ZAECA) kwa barua yenye kumbukumbu namba TKKUDK/V.01/VOL.2/25 ya tarehe 29/07/2021 kwa ajili ya kulishughulikia suala hili.

Hata hivyo, barua ya kukumbushia yenye kumbukumbu namba MKKDK/V.0l/Vol.2/46 ya tarehe 21/3/2023 tayari imeshapelekwa ZAECA.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa mkataba husika na kubaini kuwa mkataba huo una mapungufu kadhaa ikiwemo; kwa upande wa malipo, ilikubalika Mnunuzi kulipwa fedha zote (Tsh. 58,373,700) kwa awamu moja tu fedha ambazo ni nyingi.

Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC ilitaka kujua kama mkataba huo uliwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kama Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 inavyoelekeza. Hata hivyo, Kamati ya LAAC haikupata jibu la swali lake hilo kwa madai kuwa taratibu zote za ununuzi wa gari hiyo ulisimamiwa moja kwa moja na Mkurugenzi husika.

Kwa ujumla, Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Mamlaka na kutokana na kutoridhika kwake huko Kamati iliandaa kikao cha pamoja na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Madawa ya Kulevya na Mnunuzi wa gari hiyo tarehe 13 Aprili, 2023.

Hata hivyo, kikao hicho hakikuweza kufanyika baada ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar tarehe 30 Machi, 2023

kuiomba Kamati kutokufuatilia suala hilo kwa wakati ule kwa kuwa suala husika linafuatiliwa na Mamlaka hiyo na tayari Mnunuzi amekubali kulipa fedha hizo.
Kwa mnasaba huo, tarehe 07 Agosti, 2023 Kamati ya LAAC ilipokea barua yenye kumbukumbu namba MKKDK/B.02/VOL.2/30 kutoka kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuwa gari hiyo imeshafika na ipo Dar es Salaam na wanaendelea na taratibu za kuisafirisha kuja Zanzibar.

Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC inazitaka Taasisi za Umma kuwa makini wakati zinafunga mikataba mbali mbali ili kuepusha dosari kama hizo.

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2021**

### 5.1.1 BARAZA LA JIJI LA ZANZIBAR

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Jiji la Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 799,200,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Baraza la Jiji la Zanzibar lilipokea jumla ya shilingi 141,254,999 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 81 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Jiji la Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 799,200,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 Baraza la Jiji la Zanzibar limepokea na kutumia jumla ya shilingi 141,254,999 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 81 ya makadirio.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC ilipatiwa Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka ya mwaka wa fedha 2019/2020 badala ya mwaka wa fedha 2019/2020 kama ilivyoomba. Kwa msingi huo, Kamati ilishindwa kufuatilia Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Jiji.

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze katika siku zijazo, Kamati ya LAAC inalitaka Jiji kuwa makini wakati linatekeleza shughuli zake ili kuepusha usumbufu kwa Wadau wake.

**MATOKEO YA UCHUNGUZI**

### 5.1.1.1Malipo ya maposho yaliyolipwa bila ya kufuata utaratibu shilingi 1,350,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Jiji la Zanzibar limeanzisha utaratibu wa kutoa posho kwa wafanyakazi wake mbali mbali wa Baraza.

Ukaguzi umebaini posho hilo halikuidhinishwa na mamlaka husika ya utoaji posho kwa wafanyakazi, aidha utaratibu na miongozo ya utoaji posho kutoka Wizara ya Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia kitengo cha maslahi haukutolewa kwa Baraza ili kuweza kutoa maposho hayo.

Kufanya malipo ya posho ambayo hayakuidhinisha na taasisi husika inayoruhusu utoaji wa maposho nikwenda kinyume na sheria ya utumishi wa umma nambari 2 ya mwaka 2011 pamoja na kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Jiji la Zanzibar kuhakikisha kwamba inafuata taratibu za kisheria wa ulipaji wa posho hizo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Malipo ya maposho yaliyolipwa bila ya kufuata utaratibu**

| Hati ya malipo nambari | Kiasi cha fedha (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 6/7 | 450,000 | Baraza la jiji Zanzibar | Ikiwa ni malipo ya posho la simu kwa watendaji wa Baraza |
| 2/9 | 450,000 | | |
| 10/12 | 450,000 | | |
| **Jumla** | **1,350,000** | | |

**Majibu ya Baraza**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Jiji lilikuwa na utaratibu wa kuwalipa wafanyakazi wake posho za simu (muda wa mazungumzo) kwa ajili ya kuwawezesha kufanya mawasilsino na wajumbe wa Baraza la Madiwani na kuratibu ziara na vikao vyao na kazi nyengine kwa ujumla.

Msingi wa utekelezaji wa suala hilo unatokana na Maamuzi yaliyopitishwa na Kikao cha Baraza la Jiji Nam. 01/2020 cha 16/05/2020 kilichofanyika katika Ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdul Wakil – Kikwajuni ambapo kilielekeza kutumika kwa Ruzuku ya Bajeti kutoka Serikali Kuu kwa kulipia stahiki za Madiwani, kugharamia kazi za Kamati za Madiwani na katika kuratibu vikao na ziara za Madiwani ikiwemo kugharamia muda wa mawasiliano watakaotumia watendaji.

Hata hivyo, Baraza lilikatisha utaratibu wa ulipaji wa posho hizo kutokana na uhaba wa fedha na utata wa kiufafanuzi wa namna ya ulipaji wa posho hiyo na hakukua na uliapaji wa posho hizo kuanzia mwezi wa Januari 2021. Utata uliopo ni juu ya kutumika kwa Kanuni ya Kudumu ya Mamlaka ya Serikali za Mataa ya Zanzibar ambayo inaruhusu Baraza la Madiwani kuidhinisha matumizi ikiwemo posho kama hizo na kwa Maposho mengine yawe yameridhiwa na Mhe. Waziri anaehusika na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hali hiyo ni kinyume na Taasisi za Serikali Kuu ambazo ndizo zinalazimika kupata Idhini ya Wizara ya Katiba, Sheria Utumishi Umma na Utawala Bora.

Katika kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ya kutaka kuhakikisha tena na kujirishwa kufuatwa kwa taratibu na miongozo ya ulipwaji posho hizo, Baraza litapitia upya utaratibu huo ili uweze kuanza tena kwa kufuata taratibu husika kama inavyoelekezwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Nam 2 ya mwaka 2011.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hiyo isijitokeze tena Kamati ya LAAC, inalishauri Baraza kutekeleza majukumu yake kama Sheria zinavyoelekeza ili kuepuka kupata hoja zisizo na msingi.

**5.1.1.2 Dosari katika matumizi ya Mafuta**

Kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 pamoja na miongozo mbali mbali ya kiutumishi, viongozi wenye nafasi za uteuzi mafungu yao ya mafuta yanaingizwa katika mishahara yao ya kila mwezi.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Jiji la Zanzibar limetumia jumla ya lita 6,645 za mafuta ya Dizeli kwa viongozi mbali mbali wa Baraza na wale wasiokuwa wa Baraza ambapo ni kinyume na miongozo na taratibu za kiutumishi kwa kuwapatia viongozi hao mafuta ya utekelezaji wa shughuli za Baraza za kila siku.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na taratibu, miongozo pamoja na Sheria na Kanuni ya Utumishi wa Umma mwaka 2014. Mchanganuo wa matumizi ya mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Mafuta yaliyotumika bila ya kufuata utaratibu**

| **Muhusika** | **Mkurugenzi** | **Naibu Mkurugenzi** | **Meya wa Jiji** | **Naibu Meya wa Jiji** |
|---|---|---|---|---|
| | **Aina ya Mafuta** | **Aina ya Mafuta** | **Aina ya Mafuta** | **Aina ya Mafuta** |

| | Dizeli | Dizeli | Dizeli | Dizeli |
|---|---|---|---|---|
| **Mwezi** | | | | |
| Julai | - | - | - | - |
| Agosti | 120 | - | 70 | - |
| Septemba | 105 | 290 | 260 | |
| Oktoba | 175 | 130 | 150 | 60 |
| Novemba | 290 | 50 | 200 | 100 |
| Disemba | 180 | - | 10 | - |
| Januari | 410 | 70 | 280 | 20 |
| Februari | 335 | 20 | 50 | |
| Machi | 760 | - | 170 | - |
| Aprili | 500 | - | 340 | - |
| Mei | 460 | - | 300 | - |
| Juni | 520 | - | 220 | - |
| **Jumla** | **3,855** | **560** | **2,050** | **180** |

Kutumia mafuta ya kuendeshea kazi bila ya kufuata taratibu, miongozo, sheria na kanuni za utumishi wa umma kunapelekea shughuli zilizokusudiwa kutofanyika kwa wakati uliopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Jiji la Zanzibar kuhakikisha kwamba mafuta yote yanatumika kwa mujibu wa shughuli zilizokusudiwa.

**Majibu ya Baraza la Jiji**

Kimsingi hoja ya ukaguzi inalenga katika udhibiti wa utumiaji wa mafuta kwa shughuli za kikazi zilizokusudiwa kufanyika kwa wakati uliopangwa. Baraza la Jiji tokea kuundwa kwake limekuwa likikabiliwa na uchache wa vyombo vya usafiri.

Vyombo pekee viliopo ni Gari ya Mstahiki Meya na Gari ya Mkurugenzi ambavyo pia ndio gari zinatumika kwa kuendeshea shughuli za kiofisi, ufuatiliaji, operesheni za usafi na ziara. Aidha, Baraza hulazimika kuazima gari kutoka taasisi nyengine za Serikali pale inapobidi kufanya hivyo ili kutekeleza kazi zilizopangwa. Katika hali kama hiyo kulipelekea utoaji wa mafuta kwa jina la kiongozi au gari zinazotumiwa na viongozi hao; ingawaje matumizi ya mafuta hayo yalikuwa kwa kutekeleza kazi za taasisi zilizopangwa kwa mujibu wa mpango kazi wa Baraza na sio kiongozi au mtu binafsi.

Katika kuepusha kujirudia kwa hali hiyo, Baraza linaahidi kuzingatia mapendekezo ya ukaguzi ya kuhakikisha kwamba mafuta yote yanatumika kwa mujibu wa shughuli zilizokusudiwa.

Aidha, Baraza kupitia mpango wake wa bajeti 2021/2022 na 2022/2023 limeagiza gari kupitia Wizara Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango ili kupunguza tatizo la usafiri na utumiaji wa gari za viongozi na gari ya kazi za ofisi kwa utekelezaji wa kazi za Baraza, hata hivyo, hadi hivi sasa Baraza la Jiji halijapata gari yoyote.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilielezwa kuwa Baraza la Jiji hutoa barua kwa zile ziara za kawaida za viongozi na kwa zile ziara za kushitukiza Baraza huwa halitoi barua.

Kutokana na kauli hiyo Kamati iliomba kupatiwa nakala ya barua hizo ili kujiridhisha na kile kilichoelezwa, hata hivyo, Baraza lilishindwa kuwasilisha barua halisi zinazohusiana na mwaka husika wa fedha na badala yake liliwasilisha barua za mwaka 2023 barua ambazo Kamati haikuzizingatia kama ni uthibitisho wa kauli hiyo kwa kuwa hazihusiani moja kwa moja na mwaka husika.

Vile vile, katika kufuatilia zaidi hoja hii, Kamati ya LAAC ilikagua daftari la kumbukumbu za mafuta, hata hivyo, Kamati haikuridhika na ilichokibaini kwenye daftari hilo. Hii ni kutokana na kuwa katika daftari hilo imebainika kuwa mafuta yalitumika tarehe 16 Februari, 2021 na baadae kuendelea kutumika tarehe 4 Machi, 2021, na baadae tarehe zikarudi nyuma badala ya kwenda mbele kwani tarehe iliyofuata ni tarehe 17 Februari, 2021.

Kamati ya LAAC ilimhoji mhusika kwa nini imekuwa hivyo, hata hivyo, Kamati haikupata majibu ya kuridhisha.

Sambamba na hilo, Baraza liliijulisha Kamati kuwa idadi ya lita za mafuta zilizoandikwa na Mkaguzi Mkuu ni nyingi sana na Baraza halijawahi kufikia idadi hiyo. Kamati ya LAAC baada ya kupitia daftari la mafuta lilibaini kuwa kauli hiyo ya Baraza sio sahihi kwani baada ya Kamati kufanya hesabu za idadi za lita zilizotumika kwa baadhi ya miezi basi idadi ya lita za mafuta zinafikia idadi iliyoelezwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Kwa mnasaba huo, hoja hii imebaki kama ilivyo, na kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC inalishauri Baraza kutekeleza shughuli zake kama taratibu zinavyoelekeza ili dosari kama hizo zisijitokeze tena.

Aidha, Kamati ya LAAC inaiomba Serikali kulipatia usafiri Baraza ili liweze kutekeleza shughuli zake bila ya usumbufu wowote

### 5.1.2 BARAZA LA MANISPAA MJINI

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Manispaa ya Mjini kwa Mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 14,082,469,160 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, aidha Baraza la Manispaa ya Mjini lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 5,252,940,000 kutoka vyanzo vyake vya ndani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Baraza la Manispaa ya Mjini lilipokea jumla ya shilingi 12,726,894,194 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina saw ana asilimia 90.37 ya makadirio. Aidha Baraza la Manispaa ya Mjini lilikusanya jumla ya shilingi 4,626,293,115 kutoka vyanzo vyake vya ndani saw ana asilimia 88.10 ya makadirio.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baraza la Manispaa Mjini halikuandaa maelezo ya moja kwa moja juu ya taarifa ya mapato na badala yake lilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Manispaa ya Mjini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi 19,335,409,160. Kati ya fedha hizo shilingi 18,149,069,160 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 1,186,340,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Baraza la Manispaa ya Mjini lilitumia jumla ya shilingi 15,811,532,392.48 sawa na asilimia 81.78 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 15,277,204,622.48 ni kwa ajili yay a kazi za kawaida saw ana asilimia 84.18 ya makadirio na shilingi 534,327,770 kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 45.04.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baraza la Manispaa Mjini halikuandaa maelezo ya moja kwa moja juu ya taarifa ya mapato na badala yake lilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

**5.1.2.1 Kutokuwasilishwa nyaraka za makusanyo katika Baraza la Manispaa ya Mjini**

Kwa mujibu wa Kifungu nambari 31 cha makubaliano kupitia mkataba uliotiwa sahihi baina ya Baraza na Mzabuni kinaeleza kwamba "Mtoa huduma kila mwisho wa mwezi awasilishe stakabadhi za malipo, taarifa za Benki (Bank Statements) na taarifa za usimamizi wa maegesho ya mwezi".

Ukaguzi umebaini taarifa hizo haziwasilishwi Baraza la Manispaa ya Mjini kwa mujibu wa kifungu cha makubaliano hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha mkataba husika.

Kutofuatwa kwa makubaliano ya mkataba husika kupitia kifungu nambari 31 cha makataba kunapelekea Baraza kutojua mwenendo wa maegesho hayo juu ya utekelezaji wake na kusababisha upotevu wa mapato husika.

Aidha kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 26(1)(k) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha kwamba mikataba inayofungwa na kuzawadiwa mzabuni, makubaliano yaliyomo katika mkataba husika yanatekelezwa kwa mujibu wa mkataba.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Kampuni ya ECONEX wanawasilisha nyaraka zote za malipo wanayofanya Benki kwa kila mwezi na zipo tayari kwa ajili ya kukaguliwa

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

Kutokuwepo kwa kielelezo chochote kinachothibitisha kuwa Kampuni ya ECONEX ilikuwa ikiwasilisha stakabadhi za malipo ya kila mwisho wa mwezi kwa huduma za maegesho ya magari katika maeneo aliyokabidhiwa kuyasimamia katika Manispaa ya Mjini Benki.

Mtoa huduma (Mzabuni) kushindwa kutotekeleza masharti ya makubaliano yaliopo katika mkataba kama kifungu cha 31 cha mkataba huo kinavyoelekeza.

Baraza kutokuwa na usimamizi madhubuti katika ufuatiliaji wa mapato yanayokusanywa kupitia vyanzo vyao vya ndani.

Baraza la Manispaa ya Mjini kupokea taarifa za makusanyo ya maegesho kwa njia ya "Pay Slip" badala ya "Bank Statement".

Kukosekana kwa mkataba pale ambapo Kamati ilipohitaji kujiridhisha kuona.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na uchunguzi huo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

Uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuandaa Mpango Madhubuti wa kusimamia Mikataba wanayoingia na watoa huduma ili kuondokana na upotevu wa fedha za Serikali.

Baraza la Manispaa Mjini lianzishe daftari la mikataba (Contract Register), ili Baraza liweze kujua katika mwaka husika linafuatilia mikataba mingapi?

Baraza kuanzisha mfumo wa Kielektroniki katika uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu za Ofisi.

### 5.1.2.2 Kukosekana Mkataba wa Ukusanyaji wa mapato katika Maegesho ya Maeneo (4) ya Baraza la Manispaa ya Mjini

Baraza la Manispaa ya Mjini linamiliki sehemu mbali mbali za maegesho katika maeneo ya Mji ambayo hutumika kama ni vyanzo vyake vya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kila mwaka.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini kwamba kuna maeneo manne (4) yakiwemo Mwembeladu Stand, Darajani Stand ya Shamba, Vuga Culture na Mabluu Soko la Samaki. Maeneo haya ya maegesho hapo awali hayakuwemo katika makubaliano ya mkataba wa ukusanyaji wa mapato baina ya Baraza na Mzabuni wa ukusanyaji wa mapato kupitia maegesho.

Ukaguzi umebaini mzabuni huyokupewa kukusanya mapato katika maeneo hayo kinyume na mkataba husika. Aidha ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 30,069,000 zilikusanywa kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 2021 kupitia maegesho hayo.

Kufanya makusanyo katika maeneo ambayo haya kuwemo katika mikataba ya awali ni kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016 jambo ambalo linapelekea kutokujua kima halisi cha fedha kilichokusanywa na kile ambacho kinapaswa kuwasilishwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Baraza.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha kwamba mzabuni hakusanyi mapato ya Serikali bila ya kuwepo kwa makubaliano ya mkataba husika.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Maeneo yote ambayo yameainishwa katika hii yamo katika mkataba wa Nyongeza wa Maegesho.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imeshidwa kuthibitisha mkataba wa nyongeza (addendum) kwa kuwa haukuweza kuwasilishwa mbele ya Kamati.

Kukosekana kwa "Technical Team" ya ufuatiliaji na usimamizi wa mikataba katika Baraza la Manispaa ya Mjini.

Kuwepo kwa upotevu mkubwa wa fedha za Serikali kutokana na kukiukwa kwa masharti ya makataba uloingiwa baina ya mzabuni na Baraza la Manispaa Mjini kwa maeneo ya awali waliokubaliana.

Sambamba na hilo, Kamati wakati wa majadiliano walihitaji baadhi ya nyaraka kwa ajili ya kuzikagua pamoja na kujirizisha na wanachojibiwa hadi Kamati imekamilisha kazi yake nyaraka hizo hazikupatikana kwa ajili ya ukaguzi ikiwemo:

Barua ya agizo la kupunguza maeneo ya maegesho ya magari katika Manispaa ya Mjini.

Review ya Mkataba wa awali wa maengesho wa Kampuni ya ECONEX.

Minutes za vikao vya Baraza vilivyopitisha maamuzi ya kupunguza maeneo ya makusanyo pamoja na viwango vya makusanyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena katika siku zijazo, Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:

Baraza la Manispaa Mjini kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa taratibu zilizopo Kisheria na Kikanuni ili kuepuka hoja zisizo za lazima.

Baraza la Manispaa Mjini lihakikishe linaandaa utaratibu mzuri wa uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu kwa ajili ya uhifadhi wa taarifa za Serikali.

Baraza lihakikishe linaanda timu ya kitaalamu ya ufuatiliaji wa mikataba mbambali inayoingiwa baina Baraza na Kampuni za nje ili kufuatilia kwa karibu

utekelezaji wa mkataba husika.

Baraza kuhakikisha linakuwa na vielelezo husika wakati wa kujibu hoja za mdhibiti mbele ya Kamati ili kuthibitisha ukweli wa majibu wanayoyatoa.

**5.1.2.3 Hali ya ushukaji wa ukusanyaji wa mapato ya maegesho kupitia Kampuni ya ECONEX shilingi 172,876,914**

Baraza la Manispaa ya Mjini liliingia makubaliano na Kampuni ya ECONEX kuanzia mwaka 2019/2020 hadi mwaka 2020/2021 kwa ajili ya ukusanyaji mapato kupitia maeneo mbali mbali ya maegesho yaliomo ndani ya Baraza la Manispaa ya Mjini.

Ukaguzi umebaini kumekuwepo na ukusanyaji wa mapato yanayotokana katika vipindi tofauti kwa utekelezaji wa kazi zake, dosari iliyobainika ni kupungua kwa kiwango cha upatikanaji wa mapato yatokanayo na maegesho ya gari pamoja na vyombo vya moto kutoka shilingi 560,276,914 kwa mwaka 2019/2020 hadi shilingi 387,400,000 mwaka 2020/2021 kukiwa na upungufu wa mapato ya shilingi 172,876,914 sawa na asilimia 31 ya makusanyo ya awali jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya mkataba husika.

Kujitokeza kwa kitendo cha kushuka kwa ukusanyaji wa mapato kunatoa dira ya kwamba usimamizi usioridhisha wa ukusanyaji wa mapato hayo aua kutokuwa makini katika kuweka na mikakati na udhibiti wa ukusanyaji wa mapato kwa kila chomo kinachowekwa katika maegesho ya vyombo vya moto jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya mkataba huo.

Aidha ukaguzi umebaini Kampuni ya ECONEX haikuwa na uwezo wa ukusanyaji wa mapato ya maegesho jambo ambalo limeisababishia Baraza la Manispaa ya Mjini kupoteza zaidi ya shilingi 172,876,914 za mapato katika kipindi hicho cha mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha kwamba kabla ya kuingia makubaliano ya mkataba ba kampuni basi lazima ifanye utafiti wa kutosha na kujiridhisha juu ya kampuni ambayo inataka kuingia nayo makubaliano ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 15: Tofauti iliyobainika ya makusanyo ya mapato ya maegesho**

| **Tarehe ya Makusanyo 2019/2020** | **Makusanyo ya Mwaka 2019/2020 (Tshs)** | **Tarehe ya Makusanyo 2020/2021 (Tshs)** | **Makusanyo mwaka 2020/2021 (Tshs)** | **Tofauti upungufu wa makusanyo (Tshs)** |
|---|---|---|---|---|
| 07/10/2019 | 78,069,050 | 6/7/2020 | 25,000,000 | 53,069,050 |
| 06/11/2019 | 57,306,264 | 4/8/2020 | 27,000,000 | 30,306,264 |
| 05/12/2019 | 64,630,500 | 4/9/2020 | 30,000,000 | 34,630,500 |
| 02/01/2020 | 61,432,500 | 5/10/2020 | 30,000,000 | 31,432,500 |
| 03/02/2020 | 61,668,900 | 25/11/2020 | 25,000,000 | 36,668,900 |
| 04/03/2020 | 67,474,000 | 4/12/2020 | 31,000,000 | 36,474,000 |
| 03/04/2020 | 69,745,700 | 4/1/2021 | 36,300,000 | 33,445,700 |
| 04/05/2020 | 49,900,000 | 4/2/2021 | 37,000,000 | 12,900,000 |
| 04/06/2020 | 50,050,000 | 23/2/2021 | 4,400,000 | 45,650,000 |
| **Jumla ya fedha** | **560,276,914** | **Jumla ya fedha** | **245,700,000** | **314,576,914** |

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baraza la Manispaa Mjini liliingia mkataba wa maegesho na kampuni ya ECONEX mwaka 2019 ambapo taratibu zote za manunuzi zilifanyika ikiwa ni pamoja na kutangazwa zabuni na kupelekea kampuni ya ECONEX kushinda zabuni hiyo, Aidha, hoja ya kushuka kwa mapato imetokana na kushuka kwa bei ya Tshs. 5000 hadi 3000 kwa siku sambamba na kuondoshwa kwa maeneo ya maegesho ambayo yalikuwa yanaingiza kipato kikubwa, maeneo hayo ni pamoja na Barabara ya Mlandege hadi Mpirani, eneo la mbele ya Club ya Culture, Vuga Zantel, Mizingani, Mnadani Darajani na Forodha mchanga.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia kwa kina hoja hii imebaini yafuatayo:

Kampuni iliyopewa kazi ya makusanyo ya maegesho ndani ya maeneo ya Manispaa ya Mjini ilikuwa haina uwezo wa kiutendaji.

Baraza la Manispaa Mjini kutokuwa na kikosi kazi cha usimamizi na ufuatiliaji wa mkataba baada ya mzabuni kukabidhiwa kazi. Aidha, Kamati baada ya majadiliano ya kina iligundua kuwa mambo yote walimuachia mzabuni na wao kama Baraza lilikuwa halifuatilii lolote kuhusu uendeshwaji wa mkataba huu isipokuwa kusubiria kuletewa makusanyo kinyume na masharti waliokubaliana katika mkataba.

Kuchelewa kufanya “Contract Review” baada ya kutolewa agizo la kupunguza baadhi ya maeneo ya maegesho yaliomo katika mkataba wa awali ikiwemo kuondolewa kwa Eneo la Mlandege, Eneo la Mpirani na Eneo la Vuga.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inapendekeza Baraza la Manispaa ya Mjini kuwa makini katika usimamizi na ufuatiliaji wa mikataba wanayoingia na wazabuni ili kuondokana na kasoro zilizopelekea kuikosesha mapato Serikali.

Vile vile, Baraza Kufanya mapitio ya mikataba kwa wakati pindi inapotokezea mabadiliko katika mkataba wa awali.

Maagizo yote yanayotolewa na viongozi wa Serikali yanatakiwa yathibitishwe kwa njia ya maandishi pamoja na kuridhiwa na Baraza la Madiwani na si vyenginevyo.

**5.1.2.4 Dosari katika matumizi ya fedha za umma shilingi 48,570,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Baraza la Manispaa ya Mjini limefanya ununuzi wa vitu mbali mbali pamoja na upatikanaji wa huduma kwa thamani ya shilingi 31,920,000. Aidha, imebainika uwepo wa matumizi yenye thamani ya shilingi 16,650,000 kwa ajili ya upatikanaji wa huduma mbali mbali kwa Baraza la Manispaa ya Mjini ambapo stakbadhi za manunuzi ya bidhaa hizo hazikupatikana kwa ukaguzi.

Kutokuambatanishwa kwa vielelezo vya matumizi husika, pamoja na kukosekana kwa stakabadhi za manunuzi kunapelekea kujitokeza kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma jambo ambalo limepelekea kushindwa kujiridhisha juu ya thamani halisi ya fedha iliyotumika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mijni kuhakikisha matumizi yote yanayofanyika vielelezo vya matumizi hayo pamoja na stakabadhi za malipo vinapatikana na kuambatanishwa na hati za malipo husika ili kuweza kujiridhisha juu ya usahihi na uhalali wa matumizi hayo. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 16: Dosari katika matumizi ya fedha za umma**

| **Hati Namba** | **Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs)** | **Aliyelipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| **Malipo yaliyokuwa na Vielelezo Pungufu** | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 71/2 | 2,730,000 | Baraza la Manispaa Mjini | **Ikiwa ni malipo ya chakula** |
| 34/1 | 2,460,000 | | |
| 47/2 | 2,730,000 | | Ikiwa ni malipo ya Fedha kwa ajili ya kuendesha Mafunzo ya Ndani |
| 30/1 | 5,760,000 | | |
| 1/1 | 5,760,000 | | |
| 7/2 | 2,880,000 | | |
| 53/1 | 9,600,000 | | |
| **Jumla Ndogo** | **31,920,000** | | |
| **Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi** | | | |
| 33/4 | 13,150,000 | Baraza la Manispaa Mjini | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa Umeme |
| 7/6 | 3,500,000 | | |
| **Jumla Ndogo** | **16,650,000** | | |
| **Jumla Kuu** | **48,570,000** | | |

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli kwamba kipindi cha ukaguzi vielelezo vya matumizi ya fedha 48,570,000 havikuwepo hata hivyo vielelezo vilipatikana ila kwa sasa Baraza litashindwa kuviwasilisha vielelezo hivyo vimewasilishwa ZAECA kwa ajili ya kazi maalum. Aidha, Baraza limechukua juhudi ya kuviomba vielelezo hivyo ZAECA kwa barua ingawa hadi sasa havijawasilishwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja imeshindwa kufanya uchunguzi kwa kuwa Baraza limeshidwa kuwasilisha vielelezo hivyo kwa ajili ya ukaguzi kwa kuelezwa kuwa vielelezo hivyo vimewasilishwa ZAECA.

Hata hivyo, Kamati ilipohoji kwanini Baraza limeshidwa kuwa na vielelezo vya matumizi pamoja na Stakabadhi za malipo Baraza limeeleza kuwa baadhi ya matumi ya fedha hizo zilitumika kulipa vikosi kwa ajili ya posho la usafiri na chakula ambapo ilikuwa ni agizo kutoa kwa viongozi wa Serikali.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inazitaka taasisi za Serikali ikiwemo Baraza la Manispaa Mjini kuwa na utaratibu wa kuweka nakala laini (soft copy) za vielelezo vilivyopelekwa ZAECA kwa ajili ya kupatiwa taasisi nyengine za ukaguzi, aidha kuwepo na ushahidi wa maandishi wa makabidhiano ya vielelezo ambavyo huchukuliwa na ZAECA.

Kamati haipingani na maagizo yanayotolewa na viongozi wa Serikali isipokuwa maagizo hayo yatekelezwe kwa kufuata taratibu za kisheria ikiwemo sheria ya manunuzi na sheria ya fedha ya mwaka 2016.

### 5.1.2.5 Kutokuwepo kwa “Strong Room” ya kuhifadhia fedha za mapato Sokoni

Kwa mujibu wa kifungu nambari 121(1) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha ya Umma ya Mwaka 2021, kinaeleza kwamba “mapato yote yanayokusanywa na Serikal za Mitaa yatawekwa benki katika hesabu za benki kila siku”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika moja katika vyanzo vya ukusanyaji wa mapato vya Baraza la Manispaa ya Mjini ni mapato yatokanayo naukodishwaji wa vibaraza masokoni, mapato yatokanayo na wafanya biashara wadogo wadogo sokoni pamoja na mapato mengineyo yanayopatikana kutokana na huduma zinazotolewa masokoni.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa sehemu ya kuhifadhia fedha (Strong Room) kutokana na kutokutekelezeka kwa kifungu nambari 121(1) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha ya Umma ya Mwaka 2021 ambapo muda wa ukusanyaji wa mapato kwa wakati huo wa jioni benki zote huwa zimeshafungwa na huwalazimu wakusanyaji wa mapato kuondoka na mapato hayo majumbani mwao kwa kukosekana sehemu maalum ya kuhifadhia fedha hizo (strong room) jambp ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha unaotokanana dosari za kibinaadamu ambapo hulazimika mkusanyaji wa mapato hayo kulipa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuandaa utaratibu wa ukusanyaji wa mapato yote sehemu moja yanayotokana na makusanyo ya jioni ili kuepusha upotevu wa mapato hayo,

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli masoko yamekosa sehemu ya kuhifadhia mapato hususan wakati wa jioni, hata hivyo Baraza limeweka wakala wa Benki katika maeneo ya masoko ili kuepusha kuwa na fedha mkononi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya Baraza kukiri bado Kamati ya LAAC inapendekeza kwa Uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuyasimamia vyema mapato yake pamoja na kuhakikisha yanaingia Benki kwa wakati, aidha kuwa na "strong room" kwa ajili ya uhifadhi wa fedha zinazokusanywa wakati wa jioni ambapo benki zote huwa zimeshafungwa.

### 5.1.2.6 Kutokutekelezwa kwa Agizo la Baraza kuu la Madiwani la Mkopo wa shilingi 500,000,000

Kupitia kikao cha kwanza cha Baraza Kuu la Madiwani nambari 1/2021 kilichofanyika tarehe 7/2/2021 kiliazimia kumpata mtathmini wa Serikali kama agenda namba tatu (3) ya kupitisha azimio la mkopo la shilingi 500,000,000. Kikao kilikubaliana kuwa ili kuhakikisha fedha itatumika kama ilivyokusudiwa ni vyema kumtafuta mtathmini wa Serikali ili afanye tathmini ya ujenzi na kutoa mapendekezo ya fedha hiyo.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutekelezwa kwa agizo la kumtafuta mtathmini wa Serikali kwa lengo la kufanya tathmini ya ujenzi pamoja na kutoa mapendekezo yake ya matumizi mazuri ya fedha.

Hata hivyo, licha ya kukiukwa kwa agizo la ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa ya Mjini lilitengeneza mkataba wa nyongeza (addendum) wenye thamani ya shilingi 63,004,000 kwa ajili ya ujenzi wa maduka mengine sita (6) jambo ambalo lisingetarajiwa kujitokeza kwa mkataba wa nyongeza kama Baraza lingeweza kutekeleza maamuzi ya kumtafuta mtathmini wa Serikali kwa lengo la kufanya tathmini ya ujenzi pamoja na kutoa mapendekezo ya matumizi ya fedha.

Dosari iliyobaini katika ukaguzi ni kwamba matumizi ya shilingi 63,004,000 hayakupitishwa katika Kikao cha Madiwani ili yaweze kutolewa maamuzi sahihi ya matumizi hayo jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kufahamu uhalali wa

matumizi hayo kutokana na kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa matumizi hayo na kupelekea kutoa viashiria vya ukiukwaji wa makubaliano na utekelezaji wa maagizo ya Baraza Kuu la Madiwani.

Kutokutekelezwa kwa agizo na maamuzi ya kikao halali cha Baraza Kuu la Madiwani kunapelekea kujitokeza kwa viashiria vya ukiukwaji wa taratibu za uendeshaji wa Baraza la Madiwani na kutokuheshimu maamuzi halali agizo na maamuzi ya kikao halali na kusababisha matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Braza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha kwamba agizo na maamuzi ya vikao halali vya Madiwani vinavinafutwa kwa mujibu wa Sheria husika.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baraza la Manispaa ya Mjini limetekeleza agizo la kumtafuta Mitathmini wa Serikali ili afanye tathmini ya ujenzi na kutoa mapendekezo ya fedha za mkopo wa shilingi 500,000,000/-, Hata hivyo, Baraza halikupata mrejesho kutoka taasisi husika. Kwa upande wa shilingi 63,004,000/- hazikupita kwenye Baraza kwa sababu ni fedha za matumizi ya kawaida zinazotokana na makusanyo ya ndani ambazo tayari zilipitishwa katika bajeti ya Baraza la Manispaa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini mambo yafuatayo:

Kutowasilishwa barua ya kuomba kufanyiwa tathmini ya mradi wa ujenzi maduka yenye jumla ya Tsh 500,000,000 ili Kamati kuthibitisha kufanyika zoezi hilo kama Baraza la Madiwani lilivyoelekeza.

Kutokuwasilishwa kwa kumbukumbu za kikao cha Baraza la Madiwani liliidhinisha matumizi ya ziada (addendum) yenye jumla Tsh 63,004,000 kwa ajili ujenzi wa maduka mengine sita.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri Baraza la Manipaa Mjiji kuhakikisha linatekeleza kwa vitendo magizo na maamuzi ya kikao halali cha Baraza Kuu la Madiwani katika taratibu za uendeshaji wa Baraza na kuheshimu maamuzi na maagizo halali ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

**5.1.2.7 Kukosekana Mapato ya Ujenzi wa Maduka – Soko la Mboga Mombasa shilingi 13,590,000**

Baraza la Manispaa ya Mjini liliingia mkataba wa ujenzi wa maduka 23 kwa muda wa miaka nane (8) na kampuni ya Salem Construction limited katika Soko la Mombasa Zanzibar, mkataba huo ulitiwa Saini tarehe 27/01/2016 kwa thamani ya shilingi 204,518,831 kwa ajili ya ujenzi wa maduka hadi kukamilika kwake.

Kwa mujibu wa makubaliano maduka hayo yatakuwa chini ya usimamizi wa mkandarasi hadi atakapomaliza kujilipa gharama zake. Hadi kufikia Januari 2021 mkandarasi tayari alikuwa ameshakamilisha miaka mitano (5) umiliki wa maduka hayo. Kutokana na kutokufahamiana baina ya mkandarasi na Baraza la Manispaa ya Mjini, Baraza lilichukuwa maamuzi ya kumtaka kurejesha maduka kumi na moja (11) katika umiliki wa Baraza la Mjini ambapo mkandarasi alikabidhi maduka hayo mwezi wa Februari 2021.

Ukaguzi umebaini kwa mujibu wa makubaliano katika mapato ya shilingi 43,300,000 ambayo atayakusanya mkandarasi kwa mwaka atatakiwa kuchukua asilimia 70 ya mapato kwa ajili ya kujilipa gharama zake na asilimia 30 ya mapato hayo ambayo ni sawa na shilingi 13,590,000 kwa mwaka jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika fedha hiyo haikuonekana kupokelewa na Baraza la Manispaa ya Mjini. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 26(1)(k) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nambari 11 ya Mwaka 2016.

Kukosekana asilimia 30 ya mkataba kunapelekea kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba husika na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini kuhakikisha linasimamia makubaliano hayo ili mapato hayo yaweze kukusanywa na kuingizwa katika mikono ya Serikali.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baraza la Manispaa ya Mjini baada ya kubaini kukosekana kwa asilimia 30 limekubaliana na mkandarasi kugawana maduka 23 ambapo Baraza limebaki na maduka 11 na maduka 12 yapo chini ya mkandarasi hadi muda wa mkataba kukamilika Baraza limewasilisha nyongeza ya mkataba wa makubaliano hayo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Aidha, baada ya kugawana maduka hayo Manispaa tayari imekuwa ikipata mapato hayo.

**Uchunguzi wa Kamati.**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

Baraza la Manispaa limeshidwa kusimamia ipasavyo mkataba wake na mkandarasi wa kampuni ya Salem Construction limited katika Soko la Mombasa Zanzibar katika ukusanyaji wa mapato ya asilimia 30 kwa vile Baraza limeshidwa kuchukua hatua stahiki kwa muda wote wa miaka mitano kwa kukosa kukusanya mapato hayo hadi mkaguzi alipofanya ukaguzi wake.

kutokuwepo kwa usimamizi na ufuatiliaji mzuri wa mapato yatokanayo na maduka hayo kwa Baraza la Manispaa ya Mjini kama makataba unayoelekeza kwa vile Baraza halikuweza kujua deni halisi wanalomdai mkandarasi tokea tarehe waliofunga mkataba wa ujenzi wa maduka hayo hadi Kamati ilipofanya uchunguzi wake.

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hizo zisijitokeza tena Kamati ya LAAC inapendekeza yafuatayo:

Maafisa Mapato wa Baraza la Manispaa Mjini kusimamia vyema vyanzo vya mapato vya ndani vya Baraza kama Mikataba inavyoelekeza.

Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha linasimamia deni hilo ili fedha ya Serikali iweze kupatikana kutoka kwa mkandarasi kama makubaliano yaliongiwa mwaka 2016.

**5.1.2.8 Kukosekana Mapato ya Ujenzi wa Maduka Kumi (10) Soko la Saateni**

Kwa mujibu wa mkataba wa tarehe 13/08/2009 wa ujenzi wa maduka kumi (10) uliotiwa Saini baina ya Baraza la Manispaa ya Mjini na Nd. Mshenga Abdi Nasseb katika Soko la Saateni kwa muda wa miaka ishirini (20). Kwa mujibu wa mkataba mkandarasi atalipa gharama zake za ujenzi kupitia kodi itakayokusanywa kwa muda wa miaka ishirini (20), ambapo katika makusanyo hayo mkandarasi atachukuwa asilimia 80 na Baraza ataipatia asilimia 20 ya makusanyo hayo.

Ukaguzi umebaini hadi kukamilika kwa ukaguzi mkandarasi ameshindwa kutekeleza matakwa ya makubaliano ya mkataba husika. Aidha, ukaguzi umebaini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Baraza juu ya kupatiwa asilimia hiyo kutoka kwa mkandarasi husika jambo ambalo ukaguzi umeshindwa kubaini kiasi cha fedha atakachokikusanya na asilimia 20 ambayo anayotakiwa kukabidhi kwa Baraza la Manispaa Mjini kutokana na kukosekana kwa vielelezo vya ukusanyaji wa mapato kutoka kwa Mkandarasi na kupelekea Baraza kutokujua fedha halisi inayokusanywa na Mkandarasi huyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 30(1)(2)(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya Mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha kwamba makubaliano ya mkataba yanafuatwa kwa mujibu wa makubaliano husika.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baraza limechukua juhudi mbali mbali zikiwemo kufanya tathmini pamoja na kufanya vikao kwa lengo la kujadili na kusawazisha changamoto zilizojitokeza katika maduka hayo. Aidha, Baraza tayari limevunja mkataba na tayari maduka yote yapo chini ya umuliki wa Baraza la Manispaa Mjini.

**Uchunguzi wa Kamati**

Baraza la Manispaa ya Mjini halikuwa na majibu ya moja kwa moja kuhusiana na hoja hii. Hivyo, Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu yaliotolewa na kupelekea hoja kubakia kama ilivyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri uongozi Baraza kuwa makini katika ufungaji wa mikataba na kampuni mbalimbali za ujenzi wa maduka pamoja na usimamiaji wa makubaliano ya vifungu vya mkataba ikiwemo kukusanywa kwa asilimia za  mgawanyo wa mapato zinazopaswa kuingizwa katika Baraza jambo ambalo limekosekana katika mikataba yote ya ujenzi wa maduka.

Kamati inashauri Baraza kupitia maafisa mapato wake kuwa na usimamizi imara ya makusanyo ya vyanzo vyao ndani vya mapato kwa vile Kamati ilipohoji juu ya kiasi gani kilichotakiwa kukusanywa katika maduka hayo kumi, Mafisa mapato wa Baraza walishidwa kutoa jibu sahihi juu ya kiwango halisi kinachokusanywa na Mkandarasi.

**5.1.2.9 Kutokukabidhiwa kwa Baraza la Manispaaya Mjini maduka yaliopo katika Soko la Saateni**

Kwa mujibu wa mkataba wa tarehe 16/02/2010 wa ujenzi wa milango ya maduka uliotiwa Saini baina ya Baraza la Manispaa ya Mjini na Jumuiya ya wafanyabiashara wa Darajani katika Soko la Saateni kwa muda wa miaka kumi (10).

Kwa mujibu wa kifungu nambari saba (7) cha mkataba kinachoeleza masharti ya ukodishwaji, kinaeleza kwamba baada ya kunalizika muda wa mkataba huu kama ulivyotajwa na kifungu cha kwanza cha masharti ya ukodishaji, mkodishwajiatakabidhi rasmi maduka hayo kwa Baraza la Manispaa bila ya kutoa, kubomoa au kubadilisha kitu chochote ambacho kilikubalika katika ujenzi wa awali.

Pamoja na Jumuiya kujilipa gharama zake za ujenzi wa milango ya maduka wa shilingi 473,000,000 kwa muda wa miaka kumi (10), dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kumalizika kwa mkataba wa makubaliano ya ukodishwaji wa maduka ambapo mkandarasi kashindwa kukabidhi maduka hayo kwa Baraza la Manispaa ya Mjini bila ya kuwepo sababu za kufanya hivyo jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 7 cha makubaliano ya mkataba.

Kutokukabidhi milango ya maduka n Baraza la Manispaa Mjini kunapelekea kulikosesha Baraza mapato yatokanayo na ukodishwaji huo jambo ambalo linakosesha Baraza mapato yatokanayo na ukodishwaji huo jambo ambalo linaikosesha Serikali mapato.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha unasimamia misingi ya upatikanaji wa mapato yatokanayo na uhaulishwaji wa maduka hayo kwa vile muda wa makubaliano ymeshamalizika  kwa mujibu wa Sheria.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli mkataba ulimalizika muda na Jumuiya ilikuwa haijakabidhi milango ya maduka hayo kwa Baraza la Manispaa Mjini. Hata hivyo, Baraza tayari limekatisha mkataba na Jumuiya hiyo na kwamba maduka hayo yapo chini ya umiliki wa Manispaa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa Baraza limechelelewa kuchukua hatua stahiki katika kurejesha umiliki wa maduka hayo baada ya kumaliza kwa mkataba huo kutokana na sababu za kutokuwa na umakini na usimamizi wa mkataba huo.

Kutokana na kasoro hizo kamati haikuridhishwa na majibu na hivyo hoja hii inabakia kama ilivyo.

**5.1.2.10 Kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya mradi ya ujenzi wa Botanic** Garden na kuweka taa nyumba za kikwajuni shilingi 517,244,615

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Manispaa ya Mjini liliingia mkataba wa malipo nambari UMC/CW/01/2019wa tarehe 25/02/2020 na Kampuni ya SALEM CONSTRUCTION LIMITED kwa ajili ya ujenzi wa BOTANIC GARDEN na KUWEKA TAA NYUMBA ZA KIKWAJUNI ambapo fedha hizo zinatoka kutoka "ENGAGEMENT GLOBAL Gmbh – Service agency community for one World via State Capital of Postsdam from Germany" kuhusiana na gharama za kazi za malipo ya ujenzi wa maeneo hayo, malipo ya utekelezaji wa miradi hiyo itakuwa kama ifuatavyo:

Malipo ya kwanza yatakuwa asilimia 40% sawa na shilingi 206,900,726

Malipo ya pili yatakuwa asilimia 40% sawa na shilingi 206,900,726

Malipo ya tatu yatakuwa silimia 20% sawa na shilingi 103,443,163

Hadi ukaguzi unakamilika umendishwa kupata nyaraka pamoja na vielelezo mbali mbali vya matumizi ya kazi hizo, kama vile:

Mikataba ya ujenzi

Hati za malipo yaliofanyika

Aidha baada ya kufanya ziara katika maeneo husika ukaguzi umebaini ujenzi wa uwanja wa Baskeball pamoja na Bwawa la Kufugia Samaki haukufikia viwango vinavyokubalika na kusababisha miradi kutokutumika hadi tunakamilisha ukaguzi.

Kutoambatanishwa vielelezo kwenye hati za malipo kunapelekea kutokuwa na uthibitisho juu ya uhalali wa malipo hayo.

Ukaguzi unaishauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuambatanisha vielelezo husika katika hati za malipo ili kuweza kujiridhisha uhalali wa matumizi hayo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini yafuatayo.

Mkataba ulileletwa mbele ya Kamati hata hivyo ulikuwa na mapungufu mbalimbali ambapo Kamati imeshidwa kujirizisha vipengele vilivyokuwemo ndani ya mkataba huo.

Baraza kushidwa kuwasilisha vielelezo vya hati za malipo yaliyofanyika katika ujenzi wa Bustani ya BOTANIC GARDEN  na kuweka taa nyumba za kikwajuni.

Kukosekana kwa vielelezo husika katika hati za malipo ili kuweza Kamati kujiridhisha kumepelekea hoja hii kutokuwa na majibu sahihi na kubakia kama ilivyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri uongozi wa Baraza kuwa makini katika ufungaji na usimamizi wa mikataba ya miradi mbambali ili tija iliyokusudiwa iweze kufikiwa, aidha mikataba yote ni lazima uhifadhiwe ndani ya Baraza kupitia Afisi ya Mwanasheria kwa lengo la kupatika mikataba hiyo kwa wakati pale inapohitajika kwa ajili ya ukaguzi.

Kamati inaungana na ushauri uliotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali la kuitaka Baraza kuambatanisha vielelezo husika katika hati za malipo ili kuweza kujiridhisha uhalali wa matumizi hayo.

**5.1.2.11 Wafanyakazi wa Baraza kutorejesha mikopo kwa muda mrefu shilingi 73,000,000**

Baraza la Manispaa ya Mjinilimetoa mikopo ya fedha yenye thamani ya shilingi 73,000,000 kwa wafanyakazi wa Baraza hilo kwa lengo la kuweza kujikwamua katika

matatizo walionayo na kupelekea mikopo kurejeshwa kwa wakati na kupewa wafanyakazi wengine wenye kuhitaji, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kwamba uwepo wa madeni ya muda mrefu wa zaidi ya miaka mitano ambayo yanatokana na madeni hayo kutorejeshwa kwa wakati.

Kujitokeza kwa madeni kunapelekea kuwanyima fursa watumishi wengine kuweza kukopa na kwa lengo la kutatua matatizo yao kutokana na mikopo hiyo kutokurejeshwa kwa muda mrefu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha unachukuwa jitihada za makusudi kuwataka fedha kutoka katika mishahara yao na kuzirejesha fedha hizo ili ziweze kuwanufaisha wengine pamoja na kuandaa miongozo na sera Madhubuti zitakazosimamia mikopo inayotolewa na kuondokana na mikopo hiyo kutorejeshwa kwa muda mrefu.

Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Wafanyakazi wote waliopatiwa mkopo na Baraza la Manispaa tayari wamemaliza kulipa madeni ya mikopo waliopatiwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Licha ya Baraza kukiri kuwa madeni yote wameshalipwa na wafanyakazi wa Baraza hata hivyo Kamati imeshidwa kulithibitisha hilo kwa kuwa vielelezo vya marejesho ya mkopo havikuweza kuwasilisha mbele ya Kamati.

Aidha Kamati imebaini uongozo Baraza haukuwa na muongozo wowote wa utoaji wa mikopo kwa watendaji wake.

**Mapendekeza ya Kamati**

Kamati inashauri Baraza kuandaa muongozo wa utoaji wa mikopo kwa watendaji wake unaokwenda sambamba na muongo wa Serikali wa utoaji wa mikopo kwa lengo la kusimamia vyema urejeshwaji wa fedha za Serikali kwa wakati.

Baraza kuhakikisha linakuwa na vielelezo husika wakati wa kujibu hoja za mdhibiti mbele ya Kamati ili kuthibitisha ukweli wa majibu wanayoyatoa.

**5.1.2.12 Kukosekana uthibitisho wa malipo ya deni la shilingi 82,691,008**

Baraza la Manispaa ya Mjini katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 limemlipa VISIWANI GENERAL SUPPLIERS jumla ya shilingi 82,691,008 kwa ajili ya vifaa mbali mbali alivyowapatia Baraza la Manispaa ya Mjini katika kipindi husika.

Ukaguzi umebaini malipo hayo yamekosa vielelezo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo husika. Aidha ukaguzi unatia mashaka juu ya malipo kutokana na utaratibu wa ulipaji wa deni hilo ambapo hati za malipo nambari 12/5, 13/5 na 14/5/2021 zimelipwa kwa wakati mmoja na hati za malipo nambari 15/5 na 16/5 vile vile zimelipwa kwa wakati mmoja.

Vielelezo vilivyokosekana ni kama ifuatavyo:

- Mkataba baina ya Baraza na Mtoa huduma ambaye ni Visiwani General Traders.
- Ankara (invoices) zinazoonyesha vifaa husika.
- Hati ya kupokelea vifaa (Delivery note).
- Daftari la Madeni (Creditor ledger).
- Stakabadhi ya malipo husika.

kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 55(b) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2021.

Kufanya malipo bila ya kuwepo na kumbukumbu ni kwenda kinyume na Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2021 na kusababisha upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba malipo yote yanafanyika kukiwa na vielelezo sahihi. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli japo chini:

**Jadweli Nambari 18: Malipo yaliyofanyika bila ya kuonekana kwa uthibitisho wa malipo ya deni**

| Hati ya malipo | Thamani ya shilingi | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 12/5 | 8,996,145 | Visiwani General Supplier | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya vifaa ya magari Baraza la Manispaa Mjini |
| 13/5 | 8,044,522 | | |
| 14/5 | 18,904,627 | | |
| 15/5 | 25,444,830 | | |
| **16/5** | **21,299,884** | | |
| **Jumla** | **82,690,008** | | |

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Vielelezo vya malipo vipo na viko tayari kwa ajili ya kukaguliwa isipokuwa mkataba baina ya Baraza na Mtoa huduma ambae ni Visiwa General Trader haukuwepo kwa sababu ulitumika utaratibu wa Three Quatation na malipo hayo yaliyofanyika

yalikuwa ni madeni ambayo fedha zake zilitoka Wizara ya Fedha moja kwa moja kwa ajili ya kumlipa mtoa huduma huyo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu yaliyotolewa na Baraza hata hivyo Kamati inaishauri Baraza kufuata taratibu za Kisheria katika kwa kufanya malipo ya huduma na bidhaaa mbalimbali kwa kuzingatia kifungu 55(b) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2021.

**5.1.2.13 Dosari katika matumizi ya Mafuta**

Kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 pamoja na miongozo mbali mbali ya kiutumishi, viongozi wenye nafasi za uteuzi mafungu yao ya mafuta yanaingizwa katika mishahara yao ya kila mwezi.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Manispaa ya Mjini limetumia jumla ya 1,704 za mafuta ya Petroli kwa viongozi mbali mbali wa Baraza na wasiokuwa wa Baraza ambapo ni kinyume na miongozo na taratibu za kiutumishi kwa kuwapatia viongozi hao mafuta ya utekelezaji wa shughuli za Baraza za kila siku.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na taratibu, miongozi pamoja na Sheria na Kanuni ya Utumishi wa Umma mwaka 2014. Mchanganuo wa mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 19: Mafuta yaliotumika bila ya utaratibu**

| Mhusika | Gari ya Mkurugenzi Manispaa ya Mjini 557B | Gari ya Meya wa Mjini 860A | Gari la Polisi PT 1891 | Mkuu wa Wilaya (DC) Mjini Gari | Gari ya Mkuu wa Mkoa Mjini |
|---|---|---|---|---|---|

| | Aina ya Mafuta | Aina ya Mafuta | Aina ya Mafuta | Aina ya Mafuta | Aina ya Mafuta |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwezi** | **Petroli** | **Petroli** | **Petroli** | **Petroli** | **Petroli** |
| **Julai** | - | 45 | 100 | - | |
| **Agosti** | 150 | 135 | - | - | |
| **Septemba** | 98 | 199 | - | - | 25 |
| **Oktoba** | 25 | 60 | 80 | 80 | 40 |
| **Novemba** | 55 | 65 | - | 30 | |
| **Januari** | 60 | | - | - | - |
| **Februari** | 55 | | 20 | - | - |
| **Machi** | - | | 30 | - | - |
| **Aprili** | 97 | | - | - | - |
| **Mei** | - | | - | - | - |
| **Juni** | 25 | | - | - | - |
| **Jumla** | **565** | **504** | **230** | **110** | **65** |

Kutumia mafuta ya kuendeshea kazi bila ya kufuata utaratibu, miongozo, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma kunapelekea shughuli zilizokusudiwa kutofanyika kwa wakati uliopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha kwamba mafuta yote yanatumika kwa mujibu wa shughuli zilizokusudiwa.

| **Hati ya malipo** | **Nambari ya hundi** | **Ankara nambari** | **Kiasi cha fedha kilicholipwa** | **Aliyelipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | (Tshs) | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **12/3** | - | 0103 | 8,692,174 | Osaju Co. Ltd | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa remote controller pc 100, tix,sdh taa za solar Barabara ya Amani. Magomeni, Nyerere |
| **10/4** | TISS | 0102 | 9,702,000 | Osaju Co. Ltd | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa remote controller pc 100, tix, sdh taa za solar Barabara ya Amani. Magomeni, Nyerere |
| **33/4** | TISS | 0110,0202 | 20,413,828 | Osaju | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa betr za solar pamoja na chager control |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kwa ajili ya taa za barabara. |
| **Jumla** | | | **38,808,002** | | |

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

kawaida Baraza la Manispaa ya Mjini linatekeleza kazi zake mbali mbali ambazo zinahitaji ushiriki wa viongozi au matumizi ya magari kwa lengo la kufanikisha maazimio ya taasisi, hivyo magari ambayo yametajwa katika jadweli nambari 19 ambapo lita za mafuta 1,704 zilitumika kwa kufanya kazi za doria maalumu na ziara mbali mbali za viongozi.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati imebaini kuwa ni kweli Baraza limetumia mafuta kinyume na taratibu za Sheria kwa kutumia mafuta hayo katika shughuli za usafi kwa kuweka mafuta katika gari za viongozi mbalimbali ambao hawastahiki kutuliwa mafuta kwa vile viongozi wenye nafasi za uteuzi mafungu yao mafuta katika mishahara yao ya kila mwenzi kwa mujibu wa sharia na kanuni ya utumishi wa umma ya mwaka 2014.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri uongozi wa Baraza kutokiuka taratibu zilizopo katika Sheria na kanuni ya utumishi umma ya mwaka 2014 katika utoaji wa mafuta katika gari za viongozi badala yake mafuta hayo yatumike katika gari zinazotumika katika kufanyia shughuli za usafi tu na si venginevyo.

**5.1.2.14 Vifaa ambavyo haikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 38,808,002**

Katika ukaguzi uliofanyikanimebainika kuwa jumla ya shilingi 38,808,002 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa mbali mbali kwa matumizi ya Baraza la Manispaa ya Mjini lakini vifaa hivyo havikurikodiwa katika madaftari ya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Mwaka 2016. Mchanganuo wa bidhaa hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha kwamba vifaa vyote ambayo vinanunuliwa viingizwe katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani pamoja na vielelezo vinavyohusika na vifaa hivyo ili kuweza kuthibitisha mapokezi na matumizi ya vifaa hivyo.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baraza la Manispaa Mjini lilinunua Betri 100 kutoka Kampuni ya Osaju kwa Tshs 38,808,002 ambapo malipo hayo yalilipwa kwa awamu, tofauti za betri 200 ilivyoripotiwa katika kitabu cha mkaguzi. Vifaa hivyo vilifuata taratibu zote za manunuzi. Aidha hoja ya kutorikodiwa kwa vifaa hivyo katika Daftari la kutunza

Vifaa ghalani ilitokanana mtoa huduma (Osaju) kwenda moja kwa moja katika maeneo husika kwa kushirikiana na mafundi wa Baraza la Manispaa. Vielelezo husika Vimeambatanishwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Pamoja na majibu hayo Kamati imeshidwa kujiridhisha juu ya majibu yaliyotolewa na Baraza kwa vile vielelezo vya manunuzi ya vifaa hivyo havikuwasiliswa mbele ya Kamati kwa ajili ya ukaguzi.

Kuwasilisha vifaa ghalani ni moja kati ya utaratibu unaotakiwa kwa mujibu ya sheria ya manunuzi, hivyo ni wazi kuwa Baraza halikufuata taratibu za sheria ya manunuzi kinyume na majibu waliyoyatoa.

**Mapendekezo ya Kamati.**

Baraza kuhakikisha linakuwa na vielelezo husika wakati wa kujibu hoja za mdhibiti mbele ya Kamati ili kuthibitisha ukweli wa majibu wanayoyatoa.

Aidha Kamati inalishauri Baraza kurikodi vifaa vyote katika daftari la ghalani wakati wa manunuzi ili kuthibitisha uhalali wa manunuzi hayo hata kama kuna uharaka wa matumizi ya vifaa hivyo ili kwenda sambamba na masharti ya sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za umma ya Namba 11 ya mwaka 2016.

**5.1.2.15 Kutokutekelezwa miradi ya maendeleo ya wadi ya mwaka 2020/2021**

**Baraza la Manispaa ya Mjini lilipanga kutekeleza miradi kumi na moja (11) kupitia fedha za maendeleo ya wadi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021.**

Ukaguzi umebaini miradi hiyo haikutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 jambo ambalo linapelekea malengo yaliyokusudiwa kutofikiwa kwa wakati. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mpango wa utekelezaji wa miradi ya wadi husika.

**Jadweli Nambari 21: Kutokutekelezwa miradi ya maendeleo ya wadi**

| **Namba** | **Jina la Mradi** | **Wadi/Eneo** | **Thamani ya Mradi (Tshs)** |
|---|---|---|---|
| | Utiaji wat aa kumi 10 zinazotumia nguvu za jua | Mlandege | 7,500,000 |
| | Uwekaji wa Interllock Skuli ya | Malindi | 7,500,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Kajificheni | | |
| | Matengenezo ya vyoo Skuli ya M/makumbi | M/makumbi | 6,495,000 |
| | Ujenzi wa ukuta Skuli ya Mapinduzi | Kwamtipura | 7,477,600 |
| | Uchimbaji wa kisima na uwekaji wa tenki na ununuzi wa pampu Skuli ya Kidongochekundu | Urusi | 7,500,000 |
| | Uwekaji wa feni 16 Skuli ya Kiswandui, uchimbaji wa kisima na ujenzi wa banda la afya Kidutani | Kikwajuni | 7,500,000 |
| | | | |
| | Ukarabati wa Skuli ya Kilimahewa na uwekaji wa mageti | Kilima hewa | 6,500,000 |
| | Uwekaji wat aa za mitaani | Magomeni | 8,000,000 |
| | Ujenzi wa vyoo kituo cha Afya Sebbleni | Amani | 7,500,000 |
| | Ununuzi wa viti 100 Wadi ya Kwahani | Kwahani | 7,500,000 |
| | Ukarabati wa Skuli ya Msingi ya Shauri Moyo | Shauri Moyo | 7,500,000 |
| Jumla | | | 80,972,600 |

Kutokutekelezwa kwa miradi ya maendeleo kunapelekea malengo yaliyokusudiwa kutofikiwa kwa wakati na kusababisha wadi husika kutopata maendeleo yaliokusudia kwa wakati husika.

Ukaguzi unashauri uingozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha kwamba miradi yote inatekelezwa kama ilivyopangwa. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli kwamba Baraza la Manispaa Mjini halikutekeleza miradi ya wadi iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na badala yake mwaka wa fedha uliofuata imetekelezwa kwa wakati.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati imebaini katika mwaka wa fedha 2020/2021 lilikusanya Tzs 4,626,293,115 katika vyanzo vyake vya ndani sawa na asilimi 88.10 ya makadirio hivyo ni wazi kuwa kwa mujibu wa makusanyo hayo Baraza lilikuwa na uwezo wa kutenga asilimia 30 ya mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya wadi kama agizo la Mhe. Rais linavyoeleka.

**Mapendekezo ya Kamati.**

Kamati inashauri Baraza kuhakikisha linatekeleza majukumu yake ya mujibu wa malengo ya uanzishwaji wa Mabara na Halmashauri ya Miji ya kutoa huduma bora kwa wananchi ikiwa ni pamoja uendelezaji wa miradi ya Wadi kupitia fedha za makusanyo ya ndani kwa asilimia 30 ya makusanyo hayo.

### 5.1.3 BARAZA LA MANISPAA MAGHARIBI “A”

**Taarifa ya Mapato**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Manispaa ya Magharibi “A” lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 8,949,271,553 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na shilingi 1,150,000,000 kutokana na vyanzo vya ndani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Baraza la Manispaa Magharibi “A”limepokea jumla ya shilingi 8,769,326,724 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 98 ya makadirio na shilingi 1,217,907,585.91 kutoka katika vyanzo vya ndani sawa na asilimia 106 ya makadirio.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini mapugufu yafuatayo

1. Matumizi yasiyo sahihi ya vifungu kwa mfano mapato yote yaliyokusanywa yamewekwa katika kifungu cha mapato mengineyo other receipt badala ya “non tax revenue”
2. Makadirio madogo ya mapato kinyume na ukusanyaji halisi wa mapato hayo mfano ada ya matangazo imekusanya Zaidi ya kilichokadiriwa
3. Note moja kuwa na Zaidi ya namba moja katika taarifa zilizomo ndani ya “Financial Statement”

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri Baraza katika kufunga taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kuzingatia viwango stahiki vya kitaifa na Kimataifa katika taarifa hizo ili ziweze

kutoa sura halisi na sahihi katika mapato na matumizi ya Baraza kwa mwaka husika

**Taarifa ya Matumizi**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Manispaa Magharibi "A" lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 10,754,352,190, kati ya fedha hizo shilingi 10,464,773,190 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 289,579,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Baraza la Manispaa Magharibi "A" lilipokea na kutumia jumla ya shilingi 9,699,285,735.89 sawa na asilimia 90.19 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 9,590,359,192.89 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 92 ya makadirio na shilingi 108,926,543 zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 38 ya makadirio.

**5.1.3.1 Kukosekana vitabu 6 vya kukusanyia mapato kwa ukaguzi**

Baraza la Manispaa la Magharibi "A" linakusanya mapato kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa baadhi ya vitabu vya kukusanyia mapato kwa ajili ya ukaguzi ili kuweza kujiridhisha kima halisi cha fedha kilichokusanywa kwa mujibu wa stakabadhi za malipo hayo.

Aidha ukaguzi umebaini vitabu 6 vya stakabadhi za kukusanyia mapato vyenye risiti 100 kwa thamani ya shilingi 1,000 kwa kila stakabadhi moja kwa ajili ya kutolea huduma ya usafi kwa Baraza la Manispaa ya Magharibi "A", ambapo kwa idadi ya vitabu 6 vilivyokuwa havikupatikana vinafanya thamani ya shilingi 600,000 ambazo hazikuweza kupatikana na kujuulikana matumizi yake kwa kukosekana

kwa stakabadhi za kukusanyia mapato hayo jambo ambalo linaashiria ukiukwaji wa maadili na taratibu za fedha.

Kukosekana kwa taarifa za stakabadhi za kukusanyia mapato kwa ajili ya ukaguzi kunapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi "A" kuhakikisha unaanzisha Mpango Mkakati kwa wale wote watakaopewa dhamana ya ukusanyaji wa mapato kuwasilisha fedha pamoja na stakabadhi za kukusanyia fedha hizo ili kuepusha upotevu wa fedha za umma na hatua kali zichukuliwe kwa wale watakaobainika kujiingiza katika vitendo vya uhujumu wa uchumi. Mchanganuo wa vitabu hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 22: Vitabu vya kukusanyia mapato vilivyokosekana kwa ukaguzi

| **Tarehe** | **Mtiririko wa nambari za Stakabadhi** | **Jumla ya vitabuvya kukusanyiamapato** | **Aliyekabidhiwa kitabu cha risiti** |
|---|---|---|---|
| 2/7 | 26901-27000 | 2 | SAID JUMBE SAID |
| 21/10 | 33501-33600 | 2 | |
| 25/11 | 35101-35200 | 2 | |
| **Jumla** | | **6** | |

## Majibu ya Baraza

Baraza la Manispaa la Magharibi "A" linakusanya mapato kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 kwa kutumia stakabadhi za maandishi kwa njia ya mkono. Vitabu vilivyoainishwa hapo juu vilikuwa ni vitatu (3) badala ya sita (6) kama ilivyoainiskwa kwa mkaguzi kati ya vitabu hivyo vitabu viwili vilionekana na kimoja hakikupatikana

kutokana na kufariki kwa muhusika ambae alikuwa ni karani wa mapato. Hata hivyo kwa sasa suala la kutumia vitabu limeisha baraza linatumia mifumo ya malipo.

**Uchunguzi na Maendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini ni kweli vitabu vilivyoanishwa ni vitatu na sio vitabu sita kama ilivyoripotiwa na mkaguzi. Hata hivyo vitabu vitatu vilikosekana kwa ukaguzi kwa kuelezwa kuwa vitabu viwili vipo ZAECA na kimoja hakikupatikana kwa vile muhusika ambae ni karani mapato amefariki.

Hivyo basi, Kamati inaunga mkono ushauri uliotolewa na Mkaguzi wa kulitaka Baraza la Manispaa Magharibi "A" kuhakikisha unaanzisha Mpango Mkakati kwa wale wote watakaopewa dhamana ya ukusanyaji wa mapato kuwasilisha fedha pamoja na stakabadhi za kukusanyia fedha hizo ili kuepusha upotevu wa fedha za umma na hatua kali zichukuliwe kwa wale watakaobainika kujiingiza katika vitendo vya uhujumu wa uchumi.

**5.1.3.2 Tofauti iliyojitokeza baina ya taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka na Daftari la kutunzia fedha taslimu shilingi 1,526,123,819**

Ukaguzi ulipitia taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka (Financial Statement) pamoja na daftari la kutunzia fedha (Cash book) ili kuangalia uwiano kati ya taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka na daftari la kutunzia kumbu kumbu za mapato na matumizi ya Baraza la Manispaa ya Magharibi 'A'.

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 11,310,574,959 zimethibitishwa kutumika kupitia daftari la kutunzia fedha taslimu (cashbook) la hesabu za Baraza la Manispaa Magharibi "A" na kupitia taarifa ya upokeaji wa Ruzuku, aidha jumla

ya shilingi 9,784,451,140 zimeonyeshwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka, kukiwa na tofauti ya shilingi 1,526,123,819 ambazo hazikuonyeshwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka jambo ambalo limepelekea hesabu hizo kutoonyesha sura sahihi na halisi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na muongozo wa kitaifa na kimataifa wa utayarishaji, uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi “A” kusawazisha dosari hiyo ya tofauti kati ya daftari la kutunzia kumbu kumbu za mapato na matumizi na taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka za Baraza la Manispaa ya Magharibi “A” ili kuweka uwiano na usahihi wa taarifa za fedha na halisi kwa lengo la kuepuka taarifa za fedha kutokuonesha sura halisi na sahihi

**Majibu ya Baraza.**

Kwa mwaka wa fedha unaoishia June 2021 kulikuwa na jumla ya shilingi 9,987,234,309.91 ambazo zilithibitishwa kutumika kupitia daftari la kutunzia fedha taslimu (cashbook) la hesabu za Baraza la Manispaa Magharibi “A” na kupitia taarifa ya upokeaji wa Ruzuku, aidha jumla ya shilingi 8,769,326,724 zimeonyeshwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka, na jumla ya shilingi 1,217,907,585.9 zimekusanywa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imeomba kupatiwa cash book kwa ajili ya kulifanyia ukaguzi hata hivyo Daftari hilo halikuweza kupitiwa na kamati kwa vile halijawasilishwa mbele ya kamati kwa muda uliyotakiwa

Hivyo Kamati inaishauri Baraza kutayarisha vielelezo husika wakati wa ukaguzi ili Kamati ipate majibu sahihi na kuweza kutoa ushauri na mapendeko katika dosari zinazoibuliwa na mkaguzi.

**5.1.3.3 Kukosekana kwa Mikataba ya Walinzi wa Vituo vya Afya shilingi 5,000,000**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 60(1)(b) cha Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 kinaeleza kwamba " Mkataba wa muda mfupi au muda maalum wa utumishi ambao utakuwa kwa kipindi cha kurejewa rejewa baina ya miezi sita na miaka mitatu utafungwa baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi na idhini ya Tume ya Utumishi inayohusika… ". Dosari iliyobainika
katika ukaguzi ni kukiukwa matakwa ya kifungu kilichonakiliwa hapo juu kwa kuweka walinzi katika vituo vya afya bila ya uwepo wa mikataba ya kazi jambo ambalo linaweza likasababisha matatizo na kupelekea Serikali kuingia hasara pindipo tatizo lolote la kibinaadamu litakapotokezea dhidi ya walinzi hao.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 60(1)(b) cha Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi "A" kuhakikisha unafuata taratibu, kanuni na sheria za utumishi wa umma katika kuwapatia ajira watumishi wa mkataba ili kuweza kuepusha kuwakosesha waajiriwa hao stahiki zao za msingi kupitia Serikali kuu pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mchanganuo wa malipo ya walinzi hao wasio na mikataba ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 23 : Walinzi wasiokuwa na mikataba ya ajira katika kituo cha afya Magharibi "A"**

| Hati ya malipo nambari | Nambariya hundi | Kiasi cha fedha (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 8/8 | 000056 | 1,000,000 | Fedha za Ruzuku | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya walinzi wa vituo kumi vya Afya wilaya ya Magharib A. |
| 12/10 | 000079 | 1,000,000 | | |
| 10/12 | 000092 | 2,000,000 | | |
| 5/2 | - | 1,000,000 | | |
| **Jumla** | | **5,000,0000** | | |

**Majibu ya Baraza**

Mikataba ya Malipo ya fedhakwa ajili ya walinzi wa vituo kumi vya Afya wilaya ya Magharibi "A" kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020-2021 ilikuwepo lakini haikuwasilishwa kwa wakati wa ukaguzi kutokana ya kwamba katika kipindi hichi ukaguzi ulisitishwa na mikataba ya walinzi iliondoka na sekta ya afya lakini baada ya muda mikataba hiyo ilipatikana. Hata hivyo kwa sasa masuala yote ya ulinzi baraza limeingia mkataba na wakala wa ulinzi JKU.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja imeshidwa kujiridhisha juu ya majibu ya Baraza kwa vile Mikataba hiyo haikuweza kuwasilishwa mbele ya Kamati kwa kuelezwa kuwa imechukuliwa na Wizara ya afya baada ya kuondolewa kwa ugatuzi.

Kamati haikuridhika na majibu hayo kwa vile uwezo wa kupatikana mikataba hiyo kwa lengo la ukaguzi ulikuwepo hasa kwa vile Kamati inapotoa Barua zake wiki mbili kabla

ya kazi huomba vielelezo vyote vinavyohusiana na kujibu hoja za mkaguzi viwepo wakati wa kazi ya Ukaguzi.

Kamati inashauri uongozi wa Baraza kuwa makini wakati wanapojibu hoja za Mkaguzi kwa kuthibitisha majibu yao kwa kuambatanisha na vielelezo husika na sio maelezo matupu.

**5.1.3.4 Kukosekana ushindani katika utoaji huduma za usafi katika maeneo ya Baraza la Manispaa Magharibi 'A' shilingi 37,500,000.**

Baraza la Manispaa Magharibi 'A' limebinafsisha zoezi la ufanyaji usafi kwa baadhi ya barabara ziliomo katika Baraza la Manispaa Magharibi 'A' katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021.

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 37,500,000 zimetumika katika kipindi cha mwaka wa fedha husika kuvilipa vikundi vya usafi ambavyo havikuingia katika maombi ya ushindani wa zabuni wa utoaji huduma hizo kama sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma nambari 11 ya mwaka 2016 kama inavyoelekeza.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 38 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 24 : Malipo ya utoaji huduma za usafi yaliyokosa ushindani wa bei**

| Hati ya malipo nambari | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8/2 | 2,500,000 | Zan clean | Ikiwa ni malipo kwa kufanya usafi wa barabara kuanzia Mtoni hadi Bububu police |
| 18/7 | 2,500,000 | | |
| 5/9 | 2,500,000 | | |
| 14/4 | 2,500,000 | | |
| 5/6 | 5,000,000 | | |
| 62/6 | 2,500,000 | | |
| 19/7 | 2,000,000 | Hakuna mkamilifu | Ikiwa ni malipo kwa kufanya usfi barabaraya welezo,Aamani hadi Mkapa road |
| 6/9 | 2,000,000 | | |
| 2/2 | 2,000,000 | | |
| 4/3 | 2,000,000 | | |
| 8/4 | 6,000,000 | | |
| 4/6 | 4,000,000 | | |
| 53/6 | 2,000,000 | | |
| **Jumla** | **37,500,000** | | |

Kufanya malipo ya vikundi vya usafi ambavyo havikuingia katika maombi ya zabuni na bila ya kuwepo ushindani wa utoaji huduma za usafi kunapelekea kujitokeza kufanya malipo yenye gharama kubwa ukilinganisha na uhalisia jambo ambalo ni kwa kwenda kinyume na na kifungu namba 38 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba taratibu za kuwapata watoa huduma za usafi zinafuatwa kwa mujibu wa Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 ili kuondosha urasimu na kufika malengo yaliyokusudiwa.

**Majibu ya Baraza.**

Kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 Baraza la Manispaa Magharibi A lilipata agizo la mdomo kupitia vikao vya Uongozi wa Mkoa kwamba huduma zote za usafi zifanywe na Mabaraza ya Vijana ya Shehia. Na kwa kuwa Baraza la

Manispaa ni mlezi wa vijana katika shehia iliona ipo haja ya kushirikiana na vijana katika suala zima la usafi. Hatua hiyo ndiyo iliyopelekea mabaraza ya vijana ya shehia kufanya kazi za usafi wa barabara na majumbani bila ya ushindani.

**Uchunguzi wa Kamati.**

Kamati katika kufatilia hoja hii inaendelea kusisitiza katika Kutekeleza maagizo ya viongozi wa Serikali ni jambo jema hata hivyo masharti ya sheria zetu hazipaswi kuepukwa wakati wanapotekeleza maagizo hayo.

Kamati ilipotaka kupatiwa ushahidi wa maagizo hayo hayakuweza kupatikana kwa vile yalitolewa kwa njia ya mdomo tu.

**Mapendekezo ya Kamat**

Kamati inaishauri Baraza kufuata taratibu za Sheria wakati wa kutekeleza maagizo mbalimbali yanayotolewa na viongozi kutoka Serikalini.

Aidha Kamati inaendelea kuzishauri taasisi za Serikali wasiishie kwenye maagizo ya domo tu bali waombe kupatiwa barua ya agizo hilo kutoka kwa viongozi wa Serikali wakati wanapotoa maagizo hayo ili barua hizo zitumike kama ni vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa kutekeleza jambo hilo.

**5.1.3.5 Kutowekwa wazi kiwango cha ukusanyaji mapato baina ya Manispaa na Al-Jumura juu ya Minara mbali mbali iliyomo katika Manispaa ya Magharibi 'A'**

Katika makubaliano ya mapato ya tozo za minara ya makampuni ya simu, radio n.k waliokubaliana kati ya Baraza na Kampuni ya Al-Jumura kwa mujibu wa mkataba wa mwaka mmoja katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021

Ukaguzi umebaini katika mkataba husika haukubainisha tarehe ya kuanza na kumaliza kutoa huduma hiyo ya kushughulikia minara hiyo kwa Al-Jumura, aidha mkataba haukuonyesha kima cha fedha cha mkataba huo, hivyo Baraza kushindwa kukadiria mapato yanayotokana na makusanyo ya minara hiyo.

Kukosekana kwa kiasi cha fedha katika mkataba kumepelekea Al-Jumura kuwasilisha fedha zenye kubadilika badilika kwenye Baraza kwa kila anapowasilisha mapato hayo, hivyo kuomba kupatiwa malipo ya asilimia 40 ya malipo hayo ikiwa ni sehemu yake ya pato lake.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 25 : Mgawanyo wa mapato yatokanayo na ukodishwaji wa minara

| **Hati ya malipo nambari** | **Gawio la asilimia60 kwa Baraza (Tshs.)** | **Gawio la asilimia 40 kwa Aljumura(Tshs.)** | **Jumla ya Mapato yaliyogawanywa (Tshs.)** |
|---|---:|---:|---:|
| 24/7 | 3,100,000 | 1,900,000 | 5,000,000 |
| 18/8 | 1,500,000 | 1,000,000 | 2,500,000 |
| 30/10 | 3,000,000 | 2,000,000 | 5,000,000 |
| 13/11 | 18,985,790 | 12,657,060 | 31,642,850 |
| 14/11 | 37,200,000 | 22,800,000 | 60,000,000 |
| 17/12 | 18,600,000 | 11,400,000 | 30,000,000 |
| 1/3 | 9,480,000 | 5,520,000 | 15,000,000 |
| 19/4 | 27,300,000 | 18,200,000 | 45,500,000 |
| 28/5 | 27,300,000 | 18,200,000 | 45,500,000 |
| **Jumla** | **146,465,790** | **106,334,120** | **239,142,000** |

Kutokuwepo kwa utaratibu na uwazi wa makusanyo yanayokusanywa na Al-Jumura kwa kila mwezi kunapelekea kutowajibika katika kusimamia mapato yanayotokana na minara, radio n.k na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa kuhakikisha kwamba makusanyo yote yanawekwa wazi kwa mujibu wa sheria za fedha husika ili kuondoa mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali.

**Majibu ya Baraza**

Ni kweli chanzo cha mapato kinachotokana na tozo za minara ni miongoni mwa vyanzo vyenye makusanyo makubwa kwa Serikali za Mitaa ikiwemo Baraza la Manispaa Magharibi A. Kwa kipindi kirefu Mabaraza yalikuwa hayanufaiki kupitia chanzo hiki cha Minara kutokana na kutokuwa na wataalamu wa kutosha wakuweza kutambua idadi halisi ya minara iliyopo katika Mnara mmoja hali hiyo ilipelekea kuingia katika makubaliano na kampuni ya Al-jumura Company Limited kupitia maelekezo ya Wizara ya Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (TAMISEMI). Hivyo kutokana na umuhimu wa chanzo hiki cha Mapato imepelekea Manispaa kupata gawio la asilimia (60) na (40) kwa Kampuni ya Al-jumura jambo ambalo hapo awali Baraza halikunufaika nayo. Hivyo mkataba haukuonesha idadi ya fedha isipokuwa uliainisha asilimia ya makusanyo ambayo ni 60 kwa 40 na hasa kwa kuwa kulikuwa na madeni ya nyuma. Aidha, tarehe za kuanza na kumaliza zinaonekana kwenye mkataba tofauti na madai ya mkaguzi. Hadi sasa suala la minara linaratibiwa na Wizara

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imepatiwa mkataba huo kwa ukaguzi na kubaini kuwa mkataba ulikuwa na tarehe ya kuanza na kumalizika kwa mkataba huo ambao

unaishia tarehe 13/03/2021 hata hivyo mkataba huo ulishindwa kubainisha kiwango halisi kwa kila mwenzi kingelipaswa kulipwa na kuingizwa katika akaunti ya Baraza.

Hivyo Kamati inalishauri Baraza kuwa makini wakati wa kufunga mikataba mbalimbali ili kuepusha kuitia hasara Serikali

**5.1.3.6 Ucheleweshaji wa kuwasilisha fedha za mapato benki**

Katika ukaguzi uliofanyika katika Baraza la Manispaa Magharibi 'A' umebaini kwamba Baraza linakusanya fedha za mapato kupitia vyanzo mbali mbali vya ukusanyaji wa mapato dosari iliyobainika na ukaguzi ni ucheleweshwaji wa fedha kupelekwa benki jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu namba 30 (2) cha Sheria Nambari 12 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 26 : Fedha za mapato zilizocheleweshwa kupelekwa benki**

| Nambari ya Stakabadhi | Kiasi cha fedha kilichokusanywa (Tshs.) | Tarehe ya mapato yalipokusanywa | Tarehe ya Mapato yalipopelekwa benki | Siku zilizochelewa kwenda benki |
|---|---|---|---|---|
| 134458-134469 | 1,762,000 | 3/7/2020 | 6/7/2020 | 4 |
| 185701-185714 | 2,076,000 | 7/8/2020 | 10/8/2020 | 4 |
| 185732-185739 | 2,345,000 | 14/8/2020 | 17/8/2020 | 4 |
| 134401-134418 | 440,000 | 3/7/2020 | 6/7/2020 | 4 |
| 134419-134450 | 880,000 | 8/7/2020 | 10/7/2020 | 3 |
| 185821-185831 | 3,252,000 | 23/7/2020 | 25/7/2020 | 3 |
| 185756-185773 | 2,854,000 | 30/7/2020 | 3/8/2020 | 5 |
| 134396-134396 | 627,000 | 3/7/2020 | 6/7/2020 | 4 |
| 185502-185518 | 570,000 | 9/7/2020 | 13/7/2020 | 5 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 185519-185550 | 790,000 | 17/7/2020 | 20/7/2020 | 4 |
| 185601-185609 | 1,045,000 | 20/8/2020 | 24/8/2020 | 5 |
| 185610-185613 | 500,000 | 21/8/2020 | 24/8/2020 | 4 |
| 185623-185630 | 1,377,000 | 28/8/2020 | 31/8/2020 | 4 |
| 144637-144650 | 2,437,000 | 10/7/2020 | 13/7/2020 | 4 |

Kucheleweshwa fedha za mapato kupelekwa benki kunaweza kupelekea upotevu wa mapato ya Serikali na ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi ‘A’ kuhakikisha kwamba fedha za mapato zinawasilishwa benki kwa wakati ili kuondoa uwezekano wa upotevu wa mapato hayo.

**Majibu ya Baraza**

Ucheleweshwaji wa fedha za mapato kupelekwa benki ilitokana na matumizi ya vitabu vya risiti vya mkono ambavyo karani kulazimika kuhakikiwa makusanyo yake kabla ya kuwasilisha mapato husika benki hasa hasa kwa siku za mwisho wa wiki na za mapumziko lakini kwa sasa Baraza linatumia mfumo wa kielektroniki.

**Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati haikuona haja kuendelea na hoja hii kwa vile Baraza limekiri kuwepo kwa dosari hiyo na Kwasasa changamoto hiyo itadhibitiwa ipasavyo kwa vile mapato yote yanakusanywa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

**5.1.3.7 Malipo yaliyofanywa nje ya vifungu vya matumizi shilingi 116,448,175**

Baraza la Manispaa Magharibi ‘A’ katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 limefanya matumizi mbali mbali yenye thamani ya shilingi

116,448,175 katika kutekeleza majukumu yake ya kazi. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutumika kwa matumizi ya vifaa na vitu mbali mbali kinyume na vifungu husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na utaratibu wa matumizi ya kifungu nambari 50(1),(3) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Baraza**

Kutokana na upya wa utumiaji wa mfumo wa matumizi wa kielektroniki katika mabaraza ya Manispaa na halmashauri za Serikali za Mitaa ilipelekea changamoto katika uingizaji wa taarifa za vifungu vya matumizi katika mfumo na hivyo kusababisha utumiaji kimakosa katika vifungu husika.

Hata hivyo, Baraza la Manispaa Magharibi “A” lilifanikiwa kupitisha uhaulishaji wa vifungu vya matumizi katika mfumo lakini baadhi ya uhaulishaji wa vifungu hivyo hatukufanikiwa baada ya kuomba kufanya uhaulishaji huo katika mfumo wa IFMs nakupelekea matumizi mengi kutumika nje ya vifungu kutokana uharaka na umuhimu wake.

- Barua husika zinazoonesha uhaulishaji ambao ulikwama na uliopita katika Mfumo zipo tayari kwa ukaguzi.
- Mapendekezo ya mkaguzi tutayafanyia kazi na kuhakikisha matumizi yanafanywa kwa muhimu wa vifungu husika.

**Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

Baraza limekiri kuwepo kwa dosari hiyo iliyosababishwa na upya wa mfumo wa IFMS katika matumizi ya Baraza hata hivyo Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuuboresha mfumo wa IFMS kwa kuweka vifungu vya matumizi ambavyo vitakidhi haja ya kutumiwa katika taasisi sote za Serikali zinazotumia mfumo huo.

**5.1.3.8 Ujenzi uliofanyika chini ya kiwango shilingi 9,859,994**

Baraza la Manispaa Magharibi 'A' katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 limetekeleza miradi midogo midogo mbali mbali katika maeneo ya Daraja bovu ambapo wamejenga vyoo eneo la Chuini kwanyanya, Kituo cha Afya eneo la Kianga, shimo la kuchomea taka eneo la Kituo cha Daladala Mwera Mtofaani na Msikiti ulipo katika Afisi ya Baraza la Magharibi "A" kwa thamani ya shilingi 9,859,994, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba thamani halisi ya fedha hailingani na kiwango cha ujenzi huo jambo ambalo limeashiria ukiukwaji wa matumizi ya fedha na rasilimali za umma.

Kutekeleza miradi midogo midogo chini ya kiwango kunaweza kukasababisha maafa ya kuanguka au kuharibika kwa muda mchache kinyume na matarajio ya Serikali kuweka miradi hiyo ambayo ina lengo la kuondoshea usumbufu wananchi na kuwasogezea huduma bora.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na malengo ya Serikali ya kutatua matatizo ya wananchi.

**Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-**

| Hati Namba | Kiasi cha Fedha (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo | Matokeo ya mradi |
|---|---|---|---|---|
| 8/6 | 2,642,000 | Ashton store | Malipo kwa ajili ya ujenzi wa shimo kituo cha afya Kianga | Shimo hadi sasa halijatumika |
| 21/6 | 3,332,000 | Triple M general supplier | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi. | Ujenzi bado unaendelea |
| 22/6 | 3,885,594 | Triple M general supplier | Malipo ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo. | Hakuna miundo mbinu ya maji hadi sasa |
| **Jumla** | **9,859,994** | | | |

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba fedha za miradi zinazotumika zinaakisi matokeo mazuri ya miradi hiyo kwa lengo la kuwawezesha wananchi kufaidika na utekelezaji wa miradi hiyo.

**Majibu ya Baraza.**

Ujenzi wa vyoo katika eneo la Darajabovu na Chuini ulikuwa ni ujenzi wa muda kutokana na maeneo husika kuwa na pingamizi za ujenzi. Eneo la Chuini lilikuwa linasimamiwa na sheria ya PPP ambayo ilikataza eneo hilo kutofanya ujenzi wowote. Hata hivyo baada ya malalamiko ya wafanyabiashara wa eneo hilo mbele ya Makamo wa Pili kuhusina na vyoo Baraza lilipewa agizo la kujenga vyoo ndipo baraza lilijenga vyoo vya muda hadi kumalizika kwa soko kuu la chuini. Kuhusu eneo la Daraja bovu ni eneo lililopitiwa na miundombinu ya nyaya za umeme mkubwa hivyo nalo baraza lililazimika kujenga vyoo vya

muda mfupi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na majibu hayo kamati inashauri Baraza kuzingatia thamani ya fedha katika utekelezaji wa miradi yake kwani fedha hizo zinatokana na tozo za wananchi hivyo ni vyema miradi hiyo ijengwe katika kiwango stahiki.

**5.1.3.9 Kuwepo matumizi yasiyokuwa na tija shilingi 2,642,000**

Baraza la ManispaaMagharibi 'A' limejenga shimo la kuchomea taka za Hospitali katika Kituo cha Afya Kianga katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 kwa mujibu wa hati ya malipo nambari 8/6 yenye thamani ya shilingi 2,642,000 aliyelipwa Ashton Store kupitia ankara namba 614/051, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba shimo hilo lililojengwa limetumika kwa mwezi mmoja tu na baadae kutokutumika tena kwa uchomaji wa taka hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 27(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 ambapo kunapelekea malengo yaliyokusudiwa kutokufikiwa kwa sababu Baraza lilitumia fedha nyingi kwa ajili ya kuhifadhi taka za Hospitali ambazo zinahitaji uangalifu wa hali ya juu ili kuweza kuondoa tatizo la utupaji wa taka ovyo

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba shimo hilo linatumika kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuondokana na athari za taka hizo za Hospitali ambazo zinaweza kupelekea madhara makubwa kwa binaadamu na mazingira kwa ujumla.

**Majibu ya Baraza**

Kwa kipindi ambacho wakaguzi walipoenda kukagua eneo la ujenzi wa shimo la kuchomea taka lilikuwa bado halijaanza kutumika kutokana na kutofanyika kwa makabidhiano na sekta ya afya baada ya kusita kwa ugatuzi lakini baada ya makabidhiano shimo hilo lianza kutumika hadi sasa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Baraza limekiri kuwa shimo hilo limeshaanza kutumika ila Kamati imeshidwa kulithibitisha hilo kwakuwa imekosa muda wa kwenda kujionea hali halisi katika shimo hilo

Hata hivyo Kamati inalishauri Baraza kutekeleza miradi yake kwa ufanisi na kwa wakati uliopangwa ili tija uliyokusudiwa iweze kupatikana kwa wakati husika.

**5.1.3.10 Fedha za Mapato zilizotumika bila ya utaratibu shilingi 50,500,000**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 30(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Masuuli atachukuwa hatua zinazofaa kuhakikisha kwamba mapato yote yanayopokelewa yanawekwa vizuri au yanawekwa katika hesabu ya benki ya Mfuko Mkuu wa Hazina".

Baraza la Manispaa Magharibi "A" limekuwa na utaratibu wa kutumia fedha za mapato zinazotokana na makusanyo ya vyanzo vya mapato mbali mbali kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyakazi wa Baraza kutoka mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2020/2021. Ukaguzi ulipitia taarifa mbali mbali ili kuweza kubaini asili ya fedha hizo zinazotumika kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyakazi wa Baraza na kubaini fedha hizo zinatokana na makusanyo kutoka vyanzo mapato ya Baraza. Aidha ukaguzi ulishindwa kupata uthibitisho wa

utumiaji wa fedha hizo za mapato kabla ya kuwasilishwa benki kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Kwa hivyo, uongozi wa Baraza haukupata Baraka za utumiaji wa fedha hizo kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na kupelekea matumizi mabaya ya fedha za mapato.

Kutumia fedha za mapato kabla ya kupelekwa benki ni kwenda kinyume na Kifungu nambari 30(1)(2)(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 na kifungu nambari 29(3)(4) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi "A" kuhakikisha linafuata misingi na taratibu za fedha za mapato kuziwasilisha benki kabla ya kufanya matumizi au kupata idhini ya matumizi kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

**Majibu ya Baraza**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 hakukuwa na utaratibu wa kutumia fedha za mapato kabla ya kuwasilishwa benki na kupangiwa utaratibu maalum kwa ajili ya matumizi husika. Na kwa kipindi hichi kuna utaratibu maalum wa utoaji fedha za matumizi kupitia Wizara ya Fedha (IFMS).

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ilitaka kuthibitishiwa na Afisa aliyefuatana na Kamati kutoka Afisi ya Mkaguzi Mkuu sababu zilizowapelekea kusema kuwa fedha hizo hazikupitia benki, hata hivyo, Afisa huyo alishindwa kuthibitisha hilo.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ya LAAC inamshauri Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuandika taarifa ambazo amezithibitisha ili kuepuka usumbufu kwa

Wadau wake.

Vile vile, Kamati imeelezwa kuwa deni hilo limeshakamilishwa kulipwa na Watendaji hao, isipokuwa kwamba, kutokana na uwekaji mbovu wa kumbukumbu baadhi ya Watendaji wametakiwa kulipa upya kwa kuwa hakuna taarifa zao.

Kamati ya LAAC haikukubaliana na maamuzi hayo ya Baraza na imelitaka Baraza kuhakikisha kuwa haki inatendeka na kwale Watendaji ambao wamelipa basi wasitoleshwe fedha mara ya pili.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inalishauri Baraza kuwa na utaratibu mzuri wa kuweka kumbukumbu ili kuepusha lawama zisizo na msingi.

**5.1.3.11 Wafanyakazi wa Baraza kutokurejesha mikopo kwa muda mrefu shilingi 11,552,000**

Baraza la Manispaa Magharibi “A” limetoa mikopo ya fedha yenye thamani ya shilingi 11,552,000 kwa wafanyakazi wa Baraza hilo kwa lengo la kuweza kujikwamua katika matatizo waliyonayo na kupelekea mikopo hiyo kurejeshwa kwa wakati na kupewa wafanyakazi wengine wenye kuhitajia, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kwamba uwepo wa madeni ya muda mrefu wa zaidi ya miaka mitano ambayo yanatokana na madeni hayo kutokurejeshwa kwa wakati

Kujitokeza kwa madeni kunapelekea kuwanyima fursa watumishi wengine kuweza kukopa na kwa lengo la kutatua matatizo yao kutokana na mikopo hiyo kutokurejeshwa kwa muda mrefu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi "A" kuhakikisha unachukuwa jitihada za makusudi kuwakata fedha kutoka katika mishahara yao na kuzirejesha fedha hizo ili ziweze kuwanufaisha wengine pamoja na kuandaa miongozo na sera madhubuti zitakazosimamia mikopo inayotolewa na kuondokana na mikopo hiyo kutokurejeshwa kwa muda mrefu.

Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 29 : Wafanyakazi wa Baraza wanaodaiwa mikopo kwa muda mrefu**

| Mwaka wa fedha husika | Jina la Mkopaji | Kiasi cha fedha za mkopo alichokopa (Tshs) | Kiasi cha fedha za mkopo alizorejesha (Tshs.) | Kiasi cha fedha za mkopo anazodaiwa (Tshs.) |
|---|---|---:|---:|---:|
| 2016-2017 | Said Juma Ahmada | 3,000,000 | 1,920,000 | 1,080,000 |
| 2016-2017 | Yussuf M. yussuf | 500,000 | - | 500,000 |
| 2016/-2017 | Khadija Soud Mzee | 500,000 | 200,000 | 300,000 |
| 2017-2018 | Tatu Hussen Abdalla | 500,000 | 200,000 | 300,000 |
| 2017-2018 | MH:Fatma Ramadhan Masokwa | 300,000 | 200,000 | 100,000 |
| 20117-2018 | Salum Said | 550,000 | 490,000 | 60,000 |
| 2016-2017 | MST:Hamza Khamis Juma | 3,000,000 | 2,880,000 | 20,000 |
| 2016-2017 | Abdalla M Said | 1,000,000 | 625,000 | 375,000 |
| 2018-2019 | Kheri Shaaban Kheri | 1,000,000 | 450,000 | 550,000 |
| 2018-2019 | Tatu Hussen | 1,500,000 | 675,000 | 825,000 |
| 2018-2019 | Mbarouk Mrakib | 2,000,000 | 1,600,000 | 400,000 |
| 2018-2019 | Abdi Kombo Ameir | 1,000,000 | 800,000 | 200,000 |
| 2019-2020 | Hamza Haji Fadhil | 1,000,000 | 700,000 | 300,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2019-2020 | Nuru Suleiman Mohammed | 1,000,000 | 700,000 | 300,000 |
| 2019 -2020 | Maneno Suleiman Dau | 700,000 | 350,000 | 350,000 |
| 2019-2020 | Nasra Abeid Ali | 500,000 | 250,000 | 250,000 |
| 2019 -2020 | Kaimu/Amour Ali Abdalla | 4,000,000 | 758,000 | 3,242,000 |
| 2019-2020 | Mussa A khamis | 500,000 | 100,000 | 400,000 |
| 2020 -2021 | Aziza Seif Salum | 2,000,000 | - | 2,000,000 |
| **Jumla** | | | | **11,552,000** |

**Majibu ya Baraza**

Hadi kufikia sasa fedha zote za madai ya mikopo tayari zimesharejeshwa na kwa sasa Baraza limesitisha utoaji wa mikopo hiyo hadi utaratibu maalum wa kukopesha wafanyakazi wake utakapokamilika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Ili hoja kama hii isijitokeze tena kipindi kijacho, Kamati ya LAAC imelishauri Baraza kusimamia vyema marejesho ya mikopo ya Watendaji ili kutoa fursa na kwa Watendaji wengine.

### 5.1.3.12 Kuwepo na utofauti wa malipo ya deni analodai Ndugu Abdulsalami Building shilingi 4,151,000

Baraza la Manispaa Magharibi ‘A’ linadaiwa na Ndugu Abdulsalami Building kutokana huduma aliyoitoa kwa Baraza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Katika kitabu cha fedha cha mwaka 2019/2020 kinaonyesha kwamba Ndugu Abdulsalami analidai Baraza la Manispaa Magharibi ‘A’ jumla ya shilingi 4,130,000. Ukaguzi umebaini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Manispaa Magharibi ‘A’ limefanya malipo yenye thamani ya shilingi 8,281,000 kwa Ndugu Abdulsalami

ikiwa ni malipo ya mwisho ya madai ya kazi yake ya ujenzi, hivyo kupelekea tofauti ya malipo ya shilingi 4,151,000 ambapo yanapingana na deni analodai katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Aidha, ukaguzi umeshindwa kupata ufafanuzi na uthibitisho wa vielelezo vinavyooenesha na kuthbitisha uhalali wa ziada ya malipo ya shilingi 4,151,000 yaliyolipwa kwa mwaka 2020/2021 pasi na kujulikana kazi iliyofanyika kulipa madeni hayo.

Kutokuwepo kwa kumbukumbu sahihi zinazothibitisha uwepo wa deni la mdai kunapelekea kujitokeza kwa matumizi mabaya ya fedha ambayo yanaweza kupelekea hasara kwa Serikali. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu 47 (1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi 'A' kuhakikisha kwamba madeni yote yanawekwa katika daftari maalum la kuhifadhia kumbukumbu za madai ili kuweza kuyaombea madai hayo kulipwa kwa wakati kwa lengo la kuondoa kasoro na dosari zitakazojitokeza za kulipa deni ambalo halistahiki.

**Majibu ya Baraza**

Malipo ya ndg Abdulsalami ya shilingi **8,281,000** yalikuwa ni tofauti ya deni lililoainishwa katika ripoti ya mwaka 2019/2020 kama ilivyoelezwa katika hoja ya mkaguzi kuwa na tofati ya malipo ya shilingi **4,151,000**.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imeomba kupatiwa hati za malipo ya ndg Abdulsalami pamoja na Mkataba husika wa kazi hiyo ya ujenzi kwa lengo la Kamati

kujiridhisha utofauti huo.

Hata hivyo, Kamati imeshidwa kulithibitisha hilo kwa vile hati ya malipo pamoja na mkataba umeshidwa kuwasilishwa mbele ya Kamati kwa ajili ya ukaguzi.

**Mapendekezo ya Kamati**

Hoja hii inabaki kama ilivyo hata hivyo, Kamati inashauri Baraza kuwa na utunzaji mzuri wa mikataba pamoja nyaraka za kifedha ili ziweze kupatikana kwa ajili ya Ukaguzi.

**5.1.3.13 Malipo yaliyofanyika kinyume na vifungu shilingi 33,548,000**

Baraza la Manispaa Magharibi “A” katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 lilifanya malipo yenye thamani ya shilingi 33,548,000 kupitia vifungu mbali mbali vya malipo, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba malipo hayo yamefanyika kinyume na vifungu husika.

Kufanya malipo kinyume na vifungu husika kunapelekea kuathiri mwenendo wa makadirio ya mapato na matumizi ya fungu husika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi “A” kuhakikisha kwamba matumizi ya taasisi yafanyike kwa vifungu husika ili kuweza kutoa tathmini ya utekelezaji wa bajeti pamoja na kuangalia ufikiwaji wa malengo ya taasisi kwa mujibu wa bajeti husika. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 30 : Malipo yaliyolipwa kinyume na vifungu**

| Hati Namba | Kiasi cha Fedha kilicholipwa(Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo | Kifungu kilichotumika |
|---|---|---|---|---|
| 19/4 | 16,774,000 | Al-Jumura | Ikiwa ni malipo ya asilimia 40 ya matangazo ya Zanzibar Telecom | Purchase of survey instrument |
| 28/5 | 16,774,000 | | | |
| **Jumla** | **33,548,000** | | | |

## Majibu ya Baraza

Ni kweli matumizi haya yalifanyika kinyume na utaratibu wa kutumia vifungu husika kutokana na upya wa matumizi ya mfumo wa IFMs imepelekea kuwepo ugumu wa kutumia vifungu kama vilivyopangwa licha ya kuandika barua za uhaulishaji (realocation) wa matumizi wa vifungu husika lakini zilichelewa kujibiwa . Hivyo ilitulazimu kumlipa mtoa huduma kutokana na makubaliano ya kimkataba.

## Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kwa vile Baraza limekiri kutokea kwa dosari hiyo inayotokana upya wa matumizi ya mfumo wa IFMS kwa Baraza Kamati inashauri uongozi wa Wizara ya nchi, Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuboresha mfumo wake kwa kuingiza vifungu mbalimbali vya

matumizi kulingana na mahitaji ya taasisi husika ili dosari kama hizi zisijekujitokeza tena.

#### 5.1.3.14 Dosari katika matumizi ya Mafuta

Kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 pamoja na miongozo mbali mbali ya kiutumishi, viongozi wenye nafasi za uteuzi mafungu yao ya mafuta yanaingizwa katika mishahara yao ya kila mwezi.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Manispaa Magharibi "A" limetumia jumla ya 6,922 za mafuta ya Petroli na lita 4,400 za mafuta ya Dizeli kwa viongozi mbali mbali wa Baraza na wale wasiokuwa wa Baraza ambapo ni kinyume na miongozo na taratibu za kiutumishi kwa kuwapatia viongozi hao mafuta ya utekelezaji wa shughuli za Baraza za kila siku.

**Majibu ya Baraza**

Baraza la Manispaa Magharibi A halina vyombo vya kutosha vya kuhudumia kazi za ofisi kama zinavyopangwa, hivyo Baraza hulazimika kutumia vyombo vya usafiri vya Viongozi pamoja na wafanyakazi wake kwa kuhudumia kazi mbali mbali za ofisi pamoja na kazi za kamati ya ulinzi na usalama, zikiwemo kazi za ukaguzi, (wafanyabiashara, leseni, baa na ujenzi holela wa nyumba za makazi pamoja na maghala ya biashara) utembeleaji wa ujenzi wa miradi mbali mbali na ziara za viongozi wakuu wa Serikali. Hivyo mafuta yaliyoanishwa kwenye jaduweli hapo juu yalikuwa ni mafuta kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya baraza, kutokana na upungufu wa magari ndipo hulazimika kuazima gari ya mkurugenzi au Msatahiki Meya na kuipatia mafuta.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa barua inayothibitisha kuombwa kutumika gari hizo, hata hivyo, Baraza lilishindwa kuwasilisha barua hizo kwa madai kuwa gari hizo ziliombwa kwa mdomo tu.

Kwa msingi huo, hoja hii imebaki kama ilivyo na ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena Kamati ya LAAC inalitaka Baraza kufanya mawasiliano yake kwa maandishi ili kuwa na kumbukumbu na kile kinachofanyika kama kanuni ya 48(2) ya Kanuni za Sheria ya Utumishi zinavyoelekeza.

### 5.1.4 BARAZA LA MANISPAA YA MAGHARIBI "B"

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Manispaa Magharibi 'B' kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 11,334,020,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na jumla ya shilingi 2,150,000,000 kutoka vyanzo vyake vya ndani.

Hadi kufi kia tarehe 30 Juni, 2021 Baraza la Manispaa Magharibi 'B' lilipokea jumla ya shilingi 10,505,720,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 93 ya makadirio na kukusanya jumla ya shilingi 2,108,028,000 kutoka vyanzo vyake vya ndani sawa na asilimia 98 ya makadirio.

**Majibu ya Baraza**

Baraza la Manispaa Magharibi "B" halikuandaa maelezo ya moja kwa moja kuhusiana na Taarifa ya Mapato, hata hivyo, ilitoa ufafanuzi kwa mujibu wa maswali ya Kamati.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka katika mwaka husika Kamati ya LAAC ilibaini kuwa Baraza lilikusanya asilimia mia kinyume na ilivyoelezwa kwenye Ripoti ya Mkaguzi Mkuu.

Kwa msingi huo, Kamati ilitaka kujua siri ya mafanikio iliyofikiwa hadi Baraza likakusanya kwa asilimia hiyo, hata hivyo, Baraza lilishindwa kueleza sababu zilizopelekea mafanikio hayo.

Vile vile, Kamati ilibaini baadhi ya mapungufu kwenye Taarifa ya Hesabu ya Mwisho wa Mwaka kama vile;

i. Kwenye ukurasa wa 20 wa Taarifa hiyo, kifungu cha “Other Receipt” hakioneshi kama kimekusanya, ingawa, ukurasa wa 27 ambayo ni “Note” 6 kifungu hicho inaonesha kuwa kimekusanya jumla ya Tsh. 2,108,028,000.
ii. “Note” moja ina jina zaidi ya moja, kwa mfano; kwenye ukurasa wa 20 “Note” 6 imesomeka kuwa ni “Non Tax Revenue” lakini pia “Note” hiyo inasomeka kuwa ni “Other Receipt”.

Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC inawashauri Wahasibu wa Baraza kuwa makini wanavyotekeleza majukumu yao ili kuepusha utata kwa watumiaji wa Taarifa zao.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Manispaa Magharibi ‘B’ kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 13,484,020,000, kati ya fedha hizo shilingi 13,183,684,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 300,336,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Baraza la Manispaa Magharibi ‘B’ lilipokea na kutumia jumla ya shilingi 12,018,797,000 sawa na asilimia 89.13 ya makadirio, kati ya fedha hizo shilingi 11,907,511,000 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 90 ya makadirio na shilingi 111,284,000 zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 37 ya makadirio.

**Majibu ya Baraza**

Baraza la Manispaa Magharibi “B” halikuandaa maelezo ya moja kwa moja kuhusiana na Taarifa ya Matumizi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikujadili Taarifa ya Matumizi kutokana na ufinyu wa muda.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

**5.1.4.1 Kukosekana Idadi Halisi ya vyanzo vya Mapato vinavyotokana na Mabango ya Kibiashara, Minara ya Simu na Redio**

Baraza la Manispaa Magharibi "B" linafanya makusanyo ya mapato kupitia vyanzo mbali mbali ikiwemo mapato yatokanayo na Mabango ya kibiashara, Minara ya Simu na Redio ambayo imewekwa sehemu mbali mbali za Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" katika kipindi cha mwaka wafedha 2020/2021.

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini Baraza la Manispaa Magharibi "B" halina mambo yafuatayo:-

1. Idadi kamili ya mabango ya biashara yaliyomo ndani ya eneo lake kama vile Uwanja wa Ndege, Barabarani, Vijijini na katika Sheli za Mafuta, n.k.

2. Bajeti ya Ukusanyaji Mapato ya mwaka wa fedha 2020/2021.

3. Idadi ya fedha kamili zilizokusanywa kupitia mabango yaliyomo ndani ya Baraza hilo.

4. Idadi kamili ya Mabango ambayo yanafanyakazi na yale ambayo hayafanyi kazi hadi sasa.

5. Idadi kamili ya Minara ya Simu na Redio iliyomo katika eneo la Baraza la Manispaa Magharibi “B”.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na uongozi wa Baraza juu ya kutokuwepo kwa takwimu sahihi ya mabango ya biashara na minara ya simu na redio ambayo yaliyowekwa ndani ya maeneo ya Baraza la Magharibi “B”, uongozi ulishindwa kutoa ufafanuzi na takwimu za Mabango ya Biashara na Minara ya Simu na Redio iliyomo katika eneo la Baraza hilo jambo ambalo linapelekea upotevu wa mapato ya Serikali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 118(3) na 122(1)(2) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021. Baraza la Manispaa la Magharibi “B” kutokuwa na idadi kamili ya vyanzo vya mapato kunapelekea kutotoa taarifa kamili za mapato na kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi “B” kuhakikisha kwamba takwimu na idadi kamili ya mapato yanayotokana na mabango ya biashara na minara ya simu na redio iliyomo ndani ya eneo la Baraza la Manispaa inapatikana kwa ajili ya ukaguzi.

**Majibu ya Baraza**

Ofisi imepokea mapendekezo ya Mkaguzi hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Manispaa Magharib “B” kupitia wakala (ALJUMRA) ilikusanya mapato yatokanyo na Minara na mabango. Hivyo, jumla ya minara 36 ambayo 21 -Zantel, mmoja -Ttcl, mmoja -Airtel, tisa - Halotel, miwili -Zanlink na miwili – Htt ilitambuliuwa na kufatiliwa mapato yake. Jumla ya shilling 237,898,258 zilikusanywa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC ilitaka kujua sababu zilizopelekea baadhi ya maeneo kutokusanywa mapato na Baraza hilo ambapo, kwa upande wa Viwanja vya Ndege, Kamati ilielezwa kuwa Baraza halikukusanya mapato kwa kuwa Sheria za Viwanja vya Ndege zimetoa mamlaka kwa Mamlaka husika kukusanya mapato hayo.

Kamati ya LAAC haikukubaliana na maelezo hayo, kwa kuwa Sheria inayohusiana na Serikali za Mitaa inazipa mamlaka Serikali za Mitaa kukusanya mapato kwa wale wote watakaowekeza kwenye Manispaa husika.

Pamoja na hayo, hoja hii imebaki kama ilivyo, na Kamati ya LAAC imelitaka Baraza kusimamia vyema Sheria yake ili liweze kukusanya mapato kila panapostahiki kwa dhamira ya kuliongezea mapato Baraza.

**5.1.4.2 Malipo yaliyofanyika kinyume na vifungu shilingi 57,700,052.43**

Baraza la Manispaa Magharibi "B" katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 lilifanya malipo yenye thamani ya shilingi 57,700,052 kupitia vifungu mbali mbali vya malipo. Ukaguzi umebaini malipo hayo yamefanyika kinyume na vifungu husika.

Kufanya matumizi kinyume na vifungu husika kunapelekea kuathiri malengo ya kibajeti yaliyowekwa na hatimae kutokufi kiwa kwa malengo hayo. Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba matumizi ya taasisi yafanyike kwa vifungu husika na ikitokezea umuhimu wa kufanya hivyo ni vyema taratibu za uhaulishaji zifuatwe kwa mujibu wa maelekezo ya Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Malipo yaliofanyika kinyume na vifungu**

| Hati ya Malipo | Kifungu kilichotumika kutolea fedha | Kifungu kilichostahiki kulipa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 7/2 | Tuition fees | Salary Suspense | 31,399,800 |
| 6/2 | Tuition fees | Civil Servants | 7,920,000 |
| 9/2 | Stationary supplies | ZECO | 1,200,000 |
| 67/2 | Food and refreshment allowance | Stationary | 1,814,427.18 |
| 5/3 | Sitting allowance | ZECO | 1,250,000 |
| 8/3 | Transport allowance | Civil Servants | 10,800,000 |
| 70/2 | Food and refreshment allowance | Civil Servants | 3,315,825.25 |
| **Jumla** | | | **57,700,052.43** |

## Majibu ya Baraza

Ofisi imefanya Malipo hayo kwa kuzingatia taratibu na sheria za fedha zinavyoolekeza ila kutokana na changamoto ya upya wa mfumo mpya wa malipo wa IFMS na kuisha kwa vifungu vilipelekea Ofisi kutumia vifungu vingine ili kupeleka huduma kwa wananchi.

## Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Baraza na katika kufuatilia zaidi hoja hii Baraza lilieleza kuwa lililazimika kufanya hivyo, kutokana na upya wa watendaji pamoja na uharaka wa matumizi husika.

Walizidi kueleza kuwa baadhi ya Watendaji wa Baraza walihamishiwa katika ofisi nyengine jambo lililopelekea Baraza kutokufanya matumizi kwa takriban mwezi

mmoja, hivyo, walihisi endapo watafuata taratibu za uhaulishaji wangezidi kuchelewa kufanya matumizi hayo.

Pamoja na majibu yote hayo hoja hii imebaki kama ilivyo, na kwa msingi huo Kamati ya LAAC imelitaka Baraza kuhakikisha kuwa linafanya matumizi kama taratibu zinavyoelekeza ili kuepusha kupata hoja zisizo na msingi.

### 5.1.4.3 Dosari katika matumizi ya mafuta

Kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 pamoja na miongozo mbali mbali ya kiutumishi, viongozi wenye nafasi za uteuzi mafungu yao ya mafuta yanaingizwa katika mishahara yao ya kila mwezi.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" limetumia jumla ya lita 2,780 za mafuta ya Petroli na lita 4,400 za mafuta ya Dizeli kwa viongozi mbali mbali wa Baraza na wale wasiokuwa wa Baraza ambapo ni kinyume na miongozo na taratibu za kiutumishi kwa kuwapatia viongozi hao mafuta ya utekelezaji wa shughuli za Baraza za kila siku.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na taratibu, miongozo pamoja na Sheria na Kanuni ya Utumishi wa Umma mwaka 2014.

Kutumia mafuta ya kuendeshea kazi bila ya kufuata taratibu, miongozo, sheria na kanuni za utumishi wa umma kunapelekea shughuli zilizokusudiwa kutofanyika kwa wakati uliopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi "B" kuhakikisha kwamba mafuta yote yanatumika kwa mujibu wa shughuli zilizokusudiwa.

Mchanganuo wa matumizi ya mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

| **Mhusika** | **Gari ya Mkurugenzi Manispaa Magharibi "B"** | | **Gari ya Meya Wa Magharibi "B"** | | **Gari la Polisi** | | **Mkuu wa Wilaya (DC)** | | **Gari ya Meya wa Jiji** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Aina ya Mafuta** | | **Aina ya Mafuta** | | **Aina ya Mafuta** | | **Aina ya Mafuta** | | **Aina ya Mafuta** | |
| **Mwezi** | **Petrol** | **Dizeli** | **Petrol** | **Dizeli** | **Petrol** | **Dizeli** | **Petrol** | **Dizeli** | **Petrol** | **Dezeli** |
| Julai | - | 315 | 140 | 60 | 20 | 180 | - | - | 25 | 65 |
| Agosti | - | 180 | 150 | 40 | - | 60 | - | 30 | 25 | 50 |
| Septemba | - | 305 | 240 | 40 | - | 60 | - | 20 | 50 | 50 |
| Okotoba | 30 | 310 | 230 | - | - | 40 | 20 | - | 75 | 25 |
| Novemba | - | 280 | 150 | 50 | - | 90 | 30 | 40 | 50 | - |
| Decemba | 55 | 40 | 30 | 10 | - | 40 | - | - | - | - |
| Januari | - | 190 | 120 | - | - | 75 | - | - | - | - |
| Februari | 30 | 365 | 240 | - | 20 | 80 | - | - | - | - |
| Machi | 30 | 315 | 140 | - | - | 265 | - | - | - | - |
| Aprili | 20 | 320 | 290 | - | - | 60 | - | - | - | - |
| Mei | - | 150 | 240 | - | - | 60 | - | - | - | - |
| Juni | 120 | 70 | 210 | - | - | 70 | - | - | - | - |
| **Jumla** | **285** | **2840** | **2180** | **200** | **40** | **1080** | **50** | **90** | **225** | **190** |

**Majibu**

Kutokana na Ofisi kuwa na uchache wa gari zinazotumika kutolea huduma kwa Wananchi muda mwingi inapelekea Ofisi kutumia gari za viongozi ili watendaji waweze ili kufuatilia shughuli za Serikali kwa kusimamia na kuwafikishia huduma

wananchi kwa wakati na kuimarisha ustawi wa wananchi kiuchumi na kijamii, kwa mfano; Gari ya Mkurugenzi (Pick up) ndio iliyokuwa inatumika kufaanyia Ukaguzi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC iliomba kupatiwa barua inayothibitisha kuombwa kutumika gari hiyo, hata hivyo, Baraza lilishindwa kuwasilisha barua hiyo kwa madai kuwa gari hiyo iliombwa kwa mdomo tu.

Suala hili lilibainishwa pia na Mkaguzi wa Hesabu za Ndani za Baraza kupitia Taarifa yake ya ukaguzi na kutoa mapendekezo yake, isipokuwa kwamba, Baraza halikuyazingatia mapendekezo hayo jambo lililopelekea Mkaguzi wa nje kutoa dosari hiyo.

Kwa msingi huo, hoja hii imebaki kama ilivyo na ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena Kamati ya LAAC inalitaka Baraza kufanya mawasiliano yake kwa maandishi ili kuwa na kumbukumbu na kile kinachofanyika kama kanuni ya 48(2) ya Kanuni za Sheria ya Utumishi zinavyoelekeza.

Vile vile, Kamati inalitaka Baraza kuyafanyia kazi mapendekezo ya Mkaguzi wa Hesabu za Ndani ili kupunguza dosari zisizo na msingi.

**5.1.4.4 Wafanyakazi wa Baraza kutokupatiwa likizo kwa muda mrefu**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 58(1)(a) cha kanuni ya utumishi ya mwaka 2014 kinasema ‘mtumishi wa umma atastahiki kupewa likizo la siku ishirini na nane za kazi ndani ya miezi kumi na mbili na atastahiki posho la likizo kila baada ya miaka mitatu au kama itakavyofafanuliwa katika matoleo kutoka Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma.

Ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Magharibi "B" halikuwapatia likizo wafanyakazi wake kwa muda mrefu kwa mujibu wa utaratibu jambo ambalo ni kwenda kinyume na Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2014.

Kutowapatia wafanyakazi likizo zao za kila mwaka kunapelekea kudhoofisha utendaji na utekelezaji wa majukumu yao ya kazi ya kila siku na kunaweza kusababisha kutopatikana ufanisi katika kazi zao za kila siku.

Ukaguzi unashauri kwamba uongozi wa Manispaa Magharibi "B" kuhakikisha kwamba kila mfanyakazi anapatiwa likizo lake kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa.

Mchanganuo wa wafanyakazi hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo Chini:

**Watumishi ambao waliokuwa hawakwenda likizo kwa muda mrefu**

| Namba | Jina la mfanyakazi | Muda aliomaliza likizo | Miaka ambayo hajapatiwa likizo |
|---|---|---|---|
| 1. | Ali Omari Kaaby | 11/12/2017 | 4 |
| 2. | Abdul hakim Machano Haji | 7/3/2019 | 3 |
| 3. | Ameir Ali Haji | 9/4/2019 | 3 |
| 4. | Asha Rashid Mussa | 19/12/2019 | 3 |
| 5. | Aziza Ameir Mshenga | 5/7/2019 | 3 |
| 6. | Fatma Ali Khatib | 29/8/2019 | 3 |
| 7. | Hassan Abass Hassan | 18/6/2019 | 3 |
| 8. | Ibrahim Hassan Khamis | 6/3/2014 | 8 |
| 9. | Iddi Mbaraka Uledi | 14/6/2004 | 18 |
| 10. | Kazija Kaizar Omar | 24/7/2019 | 3 |
| 11. | Khadija Mohammed Khamis | 11/10/2019 | 3 |
| 12. | Khadija Mohammed Mwadini | 29/8/2019 | 3 |
| 13. | Khamis Mohammed Shekhe | 5/7/2019 | 3 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 14. | Khamis Said Mohammed | 20/5/2019 | 3 |
| 15. | Kombo Yasin Juma | 30/9/2019 | 3 |
| 16. | Nunuu Ali Abdalla | 30/1/2018 | 4 |
| 17. | Shaha Foum Haji | 9/10/2018 | 4 |
| 18. | Silima Ussi Haji | 15/4/2018 | 4 |
| 19. | Suleiman Juma Machano | 23/3/2017 | 4 |
| 20. | Vuai Makame Haji | 19/12/2018 | 4 |

**Majibu ya Baraza**

Wakati mkaguzi anatekeleza wajibu wake wa ukaguzi kuliwa tayari baadhi ya wafanyakazi wameshaenda likizo na wengine walifuata baadae kwa kupewa likizo zao pamoja na stahiki zao za posho ya likizo hivyo kwa sasa likizo kwa wafanyakazi zinaendelea kutolewa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja hii imebaki kama ilivyo, kwa kuwa ni miaka mitatu sasa hakuna hatua iliyochukuliwa na Baraza.

### 5.1.4.5 Fedha zilizolipwa kwa njia ya fedha taslimu kinyume na utaratibu shilling 44,590,800

Kwa mujibu wa kifungu nambari 55(3) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2021 "inaeleza kwamba malipo yote yalipwe kwa njia ya mfumo wa kimtandao na taasisi husika isipokuwa yale ambayo hayamo katika bajeti, na …….".

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, ukaguzi umebaini Baraza la Manispaa Magharibi "B" limefanya malipo jumla ya shilingi 44,590,800 kwa njia ya fedha taslimu

kwa wafanyakazi wake kinyume na utaratibu wa kifedha uliowekwa ambapo fedha zote zinatakiwa kulipwa kwa njia ya kimtandao na taasisi husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 55(3) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Manispaa kuhakikisha kwamba fedha zote zinalipwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.

**Malipo yaliyofanyika kwa fedha Taslim**

| Hati ya Malipo | Namba ya Hundi | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 19/7 | 63 | 18,818,000 | Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" | Ikiwa ni malipo ya mishahara na maposho |
| 15/8 | 77 | 1,010,000 | | |
| 23/11 | 205 | 9,177.000 | | |
| 11/12 | 221 | 8,770,000 | | |
| 26/9 | 128 | 6,815,800 | | |
| **Jumla** | | **44,590,800** | | |

## Majibu ya Baraza

Baraza la Manispaa Magharibi "B" limefanya malipo kwa kuzingatia taratibu na kanuni ya usimamizi wa fedha za umma ya mwaka 2021 zinavyoolekeza ambapo fedha hizo zimelipwa kwa njia taslim kutokana na kuwa mfumo wa malipo wa IFMS kuanza kutumika mwaka 2021 kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, hivyo baada ya kuanza kutumika kwa mfumo wa kielektroniki wa IFMS Ofisi inaendelea kufanya malipo yote kwa kutumia mfumo huo kama ilivyoelekezwa na Serikali.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini kuwa Mkaguzi amenukuu Sheria ya mwaka wa mbele ingawa dosari husika ilitokea miaka ya nyuma. Kitendo hicho ni kinyume na taratibu za kisheria, hivyo, Mkaguzi alipaswa kunukuu Sheria ya mwaka 2005.

Pamoja na kasoro hiyo, hoja hii imebaki kama ilivyo kwa kuwa kosa hilo lilikuwepo hapo kabla na kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC inamuomba Mkaguzi Mkuu kuwa makini wakati anaandaa Ripoti zake ili kuondosha usumbufu kwa Wadau wake.

**5.1.4.6 Kukosekana kwa muongozo wa ulipwaji wa maposho Tsh. 44,590,800**

Kwa mujibu wa utaratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekasimu majukumu kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora wa kuratibu na kupanga maslahi ya mishahara na maposho kwa watumishi wa umma kwa mujibu wa miongozo na miundo ya utumishi ya Serikalini. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Baraza la Manispaa Magharibi "B" liliidhinisha na kutumia jumla ya shilingi 44,590,800 kwa ajili ya maposho mbali mbali ya watumishi wake ikiwemo posho la mazingira magumu, posho la maziwa na posho la wadhifa kwa wafanyakazi wake.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa muongozo wa ilipwaji wa maposho hayo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa taratibu za ulipwaji wa maposho hayo.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu 87(1) cha Kanuni za Utumishi wa Umma ya Mwaka 2014 kinaeleza kwamba "Mtumishi wa Umma atakaepangiwa kazi katika mazingira hatarishi atalazimika kulipwa posho la mazingira hatarishi kama muongozo utakavyotolewa kutoka Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma".

Kifungu cha 87(2) kinaeleza "Kwa madhumuni ya kanuni ndogo (1) ya kanuni hii, watumishi watakaostahiki kulipwa posho la mazingira hatarishi miongoni mwao ni watumishi wa kada ya afya, madaktari wa Wanyama, wanaohusika na madawa ya mionzi, wanaohudumia wazee, wachimbaji wa mafuta na gesi asilia na watumishi wengine kama itakavyotolewa na Afisi Kuu ya Utumishi wa Umma". Kwa mnasaba wa vifungu hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa muongozo uliobainisha majukumu ya Baraza la Manispaa Magharibi "B" kuhusiana na uhalali wa malipo na posho hizo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi "B" kuhakikisha kwamba taratibu za uidhinishwaji na utoaji wa maposho mbali mbali kwa wafanyakazi wa Baraza la Manispaa Magharibi "B" unazingatia Sheria, Kanuni, utaratibu, matoleo na miongozo ya kiutumishi. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini*:*

**Malipo ya posho yanayolipwa bila ya muongozo kutoka Serikalini**

| **Hati ya Malipo** | **Nambari ya Hundi** | **Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs)** | **Aliyelipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|
| 19/7 | 63 | 18,818,000 | Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" | Ikiwa ni malipo mbali mbali ya mishahara na maposho kwa watendaji wa Baraza |
| 15/8 | 77 | 1,010,000 | Fedha za Ruzuku Magharibi "B" | |
| 23/11 | 205 | 9,177,000 | | |
| 11/12 | 221 | 8,770,000 | | |
| 26/9 | 128 | 6,815,800 | | |
| **Jumla** | | **44,590,800** | | |

**Majibu ya Baraza**

Baraza la Manispaa Magharibi “B” limewapatia watendaji maslahi yake kwa mujibu wa taratibu ambapo malipo hayo ni ya Mazingira magumu, Maziwa na wadhifa kama yalivyopitishwa na vikao vya Baraza la Madiwani.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati haikukubaliana na majibu ya Baraza, na katika kufuatilia hoja hii Kamati ilibaini kuwa katika mwezi wa Julai, 2020 Watendaji hao walilipwa viwango tofauti vya fedha kinyume na Toleo la Serikali. Hii ni kutokana na kuwa wapo baadhi ya Watendaji walilipwa juu ya kiwango kilichowekwa na Serikali kwa mfano wapo waliolipwa Tsh. 180,000, Tsh. 200,000 na wengine walilipwa chini ya kiwango kilichowekwa ambapo Watendaji hao wamelipwa Tsh. 50,000.

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena siku zijazo, Kamati ya LAAC imelishauri Baraza kuwalipa Watendaji wake kwa mujibu wa Matoleo ya Serikali yanavyoelekeza.

Vile vile, Kamati imelitaka Baraza la Manispaa Magharibi “B” kuhakikisha kuwa maagizo yanayotolewa na Baraza la Madiwani kuhusiana na maslahi ya Watendaji yanawasilishwa Afisi Kuu ya Utumishi kwa ajili ya kupata ridhaa kwa kuwa Baraza la Madiwani sio chombo cha mwisho juu ya masuala hayo.

### 5.1.4.7 Dosari ya utumiaji wa fedha za taasisi kinyume na utaratibu shilling 7,500,000/-

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Baraza la Manispaa Magharibi “B” katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 limefanya matumizi ya shilingi 7,500,000 katika kutekeleza majukumu yake ya kawaida ya uandaaji wa kitabu cha bajeti cha mwaka 2020/2021 na 2021/2022.

Kwa mujibu wa miongozo ya Utumishi wa Umma inakataza kulipa malipo ya posho kwa utekelezaji wa majukumu ya kawaida ya mtumishi husika unayoyafanyia kazi kila siku badala yake kulipwa posho la utekelezaji wa majukumu yake.

Mojawapo ya majukumu ya kitengo cha uhasibu ni kuhakikisha kinatengeneza bajeti ya matumizi ya taasisi pamoja na ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa utaratibu wa majukumu yao. Ukaguzi umebaini kitengo hicho hujilipa posho la utekelezaji wa majukumu yao jambo ambalo ni kosa kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi.

Kujilipa posho ambazo hazikuidhinishwa kisheria na wala hazijatolewa muongozo na Utumishi wa Umma kunapelekea natumizi mabaya ya fedha na upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi “B” Fedha za Umma ya Mwaka 2016. Mchanganuo kuhakikisha unatekeleza matakwa ya Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Malipo ya posho yanayolipwa kinyume na utaratibu**

| **Hati Namba** | **Nambari ya Hundi** | **Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.)** | **Aliyelipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|
| 32/9 | 314 | 4,260,000 | Fedha za Ruzuku Magharibi “B” | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya utekelezaji wa kitabu cha fedha cha mwaka 2020/2021 na mpango wa bajeti 2021/2022 |
| 30/6 | TISS | 3,240,000 | Salary Suspense | |
| **Jumla** | | **7,500,000** | | |

**Majibu ya Baraza**

Ofisi imefanya malipo kwa wafanyakazi kutokana na kazi hiyo ya utengenezaji wa bajeti, uingizaji katika mfumo wa serikali na ufungaji wa hesabu za ofisi (final accout), kazi hizo maalum zimefanyika baada ya saa za kazi hadi usiku kutokana na ukubwa na uzito wa kazi hizo na ikumbukwe kazi hizi zinafanywa mara moja kwa mwaka.

Aidha, kazi hizo zilitengewa kifungu maalum katika mpango wa bajeti uliopitishwa katika Baraza la Madiwani.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Baraza, hivyo, Hoja hii imebaki kama ilivyo.

**5.1.4.8 Ukiukwaji wa taratibu za mkataba**

Kwa mujibu wa mkataba makubaliano baina ya Manispaa Magharibi "B" na uongozi wa Jumuiya ya Wanawake na Mazingira uliotiwa Saini tarehe 01/05/2021 kuhusiana na shughuli za usafi katika maeneo ya Baraza la Manispaa Magharibi "B" katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021. Ukaguzi umebaini ukiukwaji wa kifungu nambari 4(f) cha makubaliano ya mkataba ambacho kinataka kuwasilishwa kwa maandishi ripoti ya kila mwezi ya utekelezaji jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika halikutekelezwa kwa mujibu wa mkataba husika.

Kutokufuatwa mkataba ya kazi husika ni kwenda kinyume na makubaliano hayo jambo ambalo huwenda likasababisha kutokutekelezwa kwa kazi walizokubaliana na kupelekea kutokukamilika kwa wakati.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba vipengele vya mikataba vilivyokubalika vinafutwa kwa mujibu wa mkataba husika na kazi zilizopangwa ziweze kukamilika kwa wakati.

**Majibu ya Baraza**

Vikundi vya usafi vinatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa makubaliano na ofisi na hii ndio lengo kuu la kuwepo kwa vikundi vya usafi. Vilevile, wanalipwa kwa mujibu wa makubaliano na ofisi na inaendelea kufuatilia ripoti ya utekelezaji wa shughuli zao kupitia wasimamizi wa vikundi na kuwasilishwa katika taarifa za utekelezaji.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Baraza, hii ni kutokana na kuwa Kamati iliomba kupatiwa Ripoti husika ili ijiridhishe na kile kilichoelezwa na Baraza, hata hivyo, Baraza lilishindwa kuwasilisha Ripoti hiyo, hivyo basi, Hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 5.1.4.9 Matengenezo ya gari la Polisi PT 3741 bila ya kufuata utaratibu Tshs 1,622,490

Kwa mujibu wa kifungu cha Sheria nambari 12(a)(f) cha Sheria Nambari 13 ya Government Motor Vehicles ya Mwaka 2004 kinaeleza kwamba “Afisa usafiri hatohusika na matengenezo ya vyombo vilivyo nje ya taasisi yake”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Baraza la Manispaa Magharibi “B” kulifanyia matengenezo gari la polisi lenye namba za usajili PT 3741 kwa mujibu wa hati ya malipo namba 18/10 iliyolipwa kwa Ankara namba 10501, 10350,10321 yenye thamani ya shilingi 1,622,490 aliyolipwa Ndugu ABRAHMAN ISMAIL VUAI.

Aidha, ukaguzi umebaini dosari katika malipo hayo ambapo malipo yaliyolipwa hayaendani na uhalisia wa matengenezo husika, kufanya matumizi ambayo hayakuwemo katika bajeti, kufanya matengenezo kinyume na sheria.

Kujitokeza kwa matumizi ya namna kama hiyo kunaweza kukapelekea kutokutekelezeka kwa kazi zilizopangwa jambo ambalo litasababisha kutokufikiwa kwa malengo waliojipangia kwa mwaka husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi "B" kuhakikisha unatekeleza mpango wa matumizi uliotayarishwa utekelezaji wake kwa mwaka husika ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Majibu ya Baraza**

Ofisi imefanya matengenezo ya gari lenye namba za usajili PT 3741 mali ya Jeshi la Polisi Tanzania inayotumika katiuka kituo cha mazizini, hii inatokana na maombi waliotuletea kuwasaidia kulifanyia matengenezo kwani Baraza la Manispaa Magharibi B linashirikiana na Jeshi la Polisi kwa kazi maalum ambazo Ofisi inalazimika kutumia Jeshi la Polisi ili kufanikisha kazi hizo ikiwemo operesheni maalum za usiku.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC imebaini kuwa Mkaguzi Mkuu hakufanya ukaguzi wa gari husika, hivyo, alishindwa kuithibitisha hoja yake. Kutokana na kasoro hiyo Kamati ya LAAC imeifuta sehemu ya hoja hii na kuibakisha hoja kuhusiana na Baraza kufanya matengenezo ya gari nje ya bajeti kitendo ambacho ni kinyume na utaratibu.

Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC inamshauri Mkaguzi Mkuu kuwa makini wakati anaandika hoja zake ili kuepusha usumbufu kwa Wadau wake.

Vile vile, Kamati ya LAAC inalitaka Baraza la Manispaa Magharibi "B" kutekeleza shughuli zake kama Sheria zinavyoelekeza.

**5.1.4.10 Fedha za Mapato zilitumika bila ya Utaratibu Tsh 66,320,000/=**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 30(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Mhasibu atachukuwa hatua zinazofaa kuhakikisha kwamba mapato yote yanayopokelewa yanawekwa vizuri au yanawekwa katika hesabu ya benki ya Mfuko Mkuu wa Hazina".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Baraza la Manispaa Magharibi "B" imekuwa na utaratibu wa kutumia fedha za mapato zinazotokana na makusanyo ya vyanzo vya mapato mbali mbali kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wafanyakazi wake.

Hata hivyo, ukaguzi ulishindwa kupata uthibitisho wa utumiaji wa fedha hizo za mapato kabla ya kuwasilishwa benki kwa mujibu wa taratibu, kufanya matumizi ya fedha za mapato kabla ya kuwasilishwa benki au kupatiwa idhini ya matumizi kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kunaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha za umma jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 30(1)(2)(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016 na kifungu nambari 29(3)(4) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2021.

Aidha, imebainika uwepo wa dosari za utumiwaji wa mkopo hiyo kutokana na kukosekana kwa sera inayoelekeza namna bora ya kukopa, kurejesha mikopo, kiwango cha fedha kinachopaswa kurejeshwa kwa kila mwezi jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa mikopo isiyorejeshwa kwa muda mrefu bila ya kuchukuliwa maamuzi yote jambo ambalo huwenda mikopo hiyo ikashindwa

kurejesheka kutokana na utaratibu wa watumishi kuzungushwa kutoka taasisi moja na kwenda taasisi nyengine.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi “B” kuhakikisha unatumia fedha za umma kwa mujibu wa utaratibu na kuacha kutumia fedha za makusanyo ya mapato kwa ajili ya kukopeshana jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa dosari ya kutokufikia malengo yaliyopangwa kutekelezwa na Baraza la Manispaa ya Magharibi “B” kwa mwaka husika.

**Majibu ya Baraza**

Kwa mujibu wa sheria namba 7 ya mwaka 2014 kifungu namba 70 mpaka kifungu namba 73 Mamlaka za Serikali za Mitaa imepewa dhamana ya kukusanya Mapato katika mipaka yake. Fedha hizo hukusanywa na kuingizwa katika nambari ya hesabu ya taasisi husika na kufanya matumizi kwa mujibu wa ruhusa kutoka Baraza la Madiwani baada ya matumizi hayo kuwasilishwa na kupitishwa kupitia Baraza la Madiwani kwa mujibu wa sheria. Hivyo matumizi yaliofanyika 66,320,000/= yamepitishwa na vikao halali vya Baraza la Madiwani ambacho ni chombo halali chenye mamlaka

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini kuwa mkopo huo haukutolewa mwaka 2020, isipokuwa kwamba, ni wa tokea mwaka 2017 na wakopeshwaji huo wamabakia na deni lifuatalo:

i. Ndg. Mwanaidi Harubu Mussa hadi tarehe 30 Septemba, 2022 amebakisha deni la Tsh. 150,000;

ii. Ndg. Mtwana Kheri Mtwana hadi tarehe 27 Oktoba, 2020 amebakisha deni la Tsh.800,000; na
iii. Ndg. Hidaya Tafa Faraji hadi tarehe 30 Septemba, 2022 amebakisha deni la Tsh.250,000.

Kwa kuwa fedha hizo ni mapato ya Baraza, hivyo, Kamati ya LAAC inawataka Watendaji hao kukamilisha deni hilo ndani ya kipindi kifupi ili hoja hiyo isijirejee tena katika miaka ijayo.

Vile vile, Kamati ya LAAC ilimtaka Mkaguzi aliyefuatana na Kamati kuithibitishia Kamati sababu zilizompelekea hata akasema kuwa mapato hayo hayakupelekwa benki, hata hivyo, Mkaguzi huyo alishindwa kuthibitisha hilo.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inamshauri Mkaguzi Mkuu kueleza kwa uwazi hoja zake ili aweze kueleweka na Wadau wake.

**5.1.4.11 Malipo yasiokuwa na stakabadhi Tsh. 35,770,666**

Katika ukaguzi uliofanyika imebanika Baraza la Manispaa Magharibi "B" limefanya malipo kwa ajili ya ununuzi na upatikanaji wa huduma za bidhaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya ofisi, dosari iliyobainika ni kutokupatikana kwa stakabadhi za malipo hayo jambo ambalo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanishwa kwa stakabadhi za malipo kunapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma zinazotokana na kuwepo kwa matumizi yasiyosahihi au kutokuwepo kwa matumizi hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi "B" kuhakikisha matumizi yote yanayoanyika yanaambatanishwa na vielelezo husika katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo kwa lengo la kuweza kupima

ufanisi wa matumizi hayo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Malipo yasiokuwa na stakabadhi**

| Hati ya Malipo | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 14/11 | TT | 1,600,000 | | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya mashine za ATM na CRDB |
| 15/11 | TT | 11,250,000 | | Ikiwa ni malipo ya Minara ya Telecomunication public |
| 2/12 | TT | 10,714,285 | Aljumra | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kupatiwa 40% ya Minara ya Zantel |
| 12/8 | TT | 952,381 | | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matangazo ya Halotel |
| 58/9 | TT | 11,254,000 | | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ulipaji wa Minara kwa Tanzania telecomunication |
| **Jumla** | | **35,770,666** | | |

### Majibu ya Baraza

Wakati mkaguzi anafanya ukaguzi ni kweli baadhi ya risiti zilikosekana na Baraza la Manispaa limefanya jitihada ya kuzifuatilia stakabadhi hizo na zimepatikana kwa ajili ya kumbukumbu za matumizi ya ofisi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Baraza, na katika kuijadili zaidi hoja hii Kamati ilielezwa na Baraza kuwa dosari hiyo imejitokeza kwa kuwa Wahasibu na Washika Fedha walikuwa wanabadilishwa mara kwa mara.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya LAAC haikukubaliana na maelezo yote yaliyotolewa Baraza hivyo, Hoja hii imebaki kama ilivyo.

Kwa mnasaba huo, Kamati ya LAAC inalitaka Baraza kutekeleza shughuli zake kama Sheria zinavyoelekeza ili kuepuka kupata hoja zisizo na msingi.

**5.1.4.12 Dosari katika udhibiti wa mafuta.**

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia daftari la kumbukumbu la kurikodia taarifa za matumizi limebainisha ya kwamba kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Manispaa Magharibi “B” limetumia jumla ya lita 3,245za mafuta kwa ajili ya matumizi mbali mbali kwa ajili ya shughuli za uendeshaji za kila siku.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuwa na mfumo mzuri wa udhibiti wa matumizi ya mafuta kwani imebainika hakuna taarifa zozote zilizorikodiwa ambazo zinaonesha mwenendo wa matumizi ya mafuta kwa vyombo vilivyotiwa mafuta hayo pamoja na kutokujulikana matumizi ya mafuta hayo jambo ambalo limepelekea kutia shaka juu ya uhalali wa matumizi ya mafuta hayo.

Kutokujulikana kwa matumizi ya mafuta kwa vyombo vinavyowekwa mafuta kunaweza kujitokeza viashiria vya upotevu wa mafuta au matumizi mabaya ya mafuta hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi “B” kuhakikisha unaweka mwenendo mzuri wa utumiaji wa mafuata ikiwemo kujulikana kwa vyombo

vinavyopewa mafuta na sababu za uwepo wa kupatiwa mafuat kulingana na kazi wanazozitekeleza ili kuepusha kujitokeza kwa viashiria vya ukiukwaji wa taratibu. Mchanganuo wa matumizi ya mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli japo chini:

**Mwenendo wa matumizi ya mafuta**

| Tarehe | Aliyepewa | Idadi ya lita zilizotolewa | Nambari Kuponi |
|---|---|---|---|
| 9/4/2021 | UUB | 500 | 274798 |
| 11/4/2021 | OPERESHENI | 350 | 274800 |
| 12/4/2021 | CCM MKOA | 40 | 274704 |
| 12/4/2021 | CCM WILAYA | 40 | 274705 |
| 12/4/2021 | KATIBU TAWALA | 30 | 274706 |
| 12/4/2021 | DC | 40 | 274707 |
| 16/4/2021 | UUB | 200 | 274722 |
| 2/4/2021 | OPERESHENI | 200 | 274731 |
| 2/4/2021 | UUB | 340 | 274735 |
| 12/5/2021 | OCD | 100 | 289779 |
| 12/5/2021 | WILAYANI | 200 | 289780 |
| 18/5/2021 | WILAYANI | 100 | 289559 |
| 18/5/2021 | UUB | 50 | 289562 |
| 18/5/2021 | MAWASILIANO | 60 | 289563 |
| 18/5/2021 | GARI YA KUKODI KIFUSI | 70 | 289564 |
| 20/5/2021 | MAWASILIANO | 50 | 289575 |
| 21/5/2021 | OPERESHENI | 100 | 289578 |
| 21/5/2021 | MAWASILIANO | 50 | 289581 |
| 21/5/2021 | WILAYA | 300 | 289584 |
| 21/5/2021 | UV CCM | 120 | 289587 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 21/5/2021 | GARI YA MIZIGO | 50 | 289592 |
| 22/5/2021 | MWENGE | 20 | 289593 |
| 22/5/2021 | MWENGE | 100 | 289594 |
| 22/5/2021 | MWENGE | 30 | 289595 |
| 23/5/2021 | MWENGE | 15 | 289597 |
| 23/5/2021 | MWENGE | 30 | 289598 |
| 24/5/2021 | MAWASILIANO | 50 | 290160 |
| 1/6/2021 | KAZI MAALUM | 40 | 290178 |
| **Jumla ya lita** | | **3,245** | |

**Majibu ya Baraza**

Changamoto hii inatokana na kuibuka kwa ziara na operation mbali mbali za serikali kuu na sherehe za kitaifa hali inayopelekea ofisi kutumia vyombo na mafuta ya ziada ili kufanikisha majukumu yake ya kila siku, ofisi imeshaweka mikakati ya udhibiti wa utumiaji wa mafuta kwa kumpatia afisa usafiri maelekezo ya uwekaji wa kumbukumbu vizuri kwa kuzingatia taratibu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC katika kufuatilia hoja hii ilishindwa kujua kiini cha hoja ya Mkaguzi Mkuu, hata hivyo, katika kufuatilia zaidi ilibaini kuwa katika mwaka husika Baraza halikuwa na "log book" jambo lililochangia kutokea kwa dosari hiyo.

Kwa msingi huo, Kamati ya LAAC haikukubaliana na majibu ya Baraza, hivyo basi, Hoja hii imebaki kama ilivyo.

Pamoja na kaosoro hizo, Kamati ya LAAC imelitaka Baraza kutekeleza shughuli zake kama Sheria zinavyoelekeza.

Vile vile, Kamati inamuomba Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuweka bayana hoja zake ili Taasisi husika iweze kujua kinachohitajika kwa lengo la kutoa majibu sahihi.

**5.1.4.13 Dosari katika ulipwaji wa maposho shilingi 2,000,000.**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 12(7) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma nambari 11 ya mwaka 2014 kinaeleza kwamba "Mtumishi wa kuazimwa atapaswa kulipwa mshahara ule wa sehemu anayotoka au anayolingana na wadhifa wa sehemu ile aliyoazimwa kama anakokwenda mshahara ni kubwa atalipwa tofauti ya mshahara bila ya maposho.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 2,000,000 zimetumika kwa kumlipa Ndugu Ferouz Kitwana Abdalla ambae ameazimwa kutoka Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba CCA/CCA/F.00826/C/23 ya tarehe 28/10/2019 kwa ajili ya kufanya kazi ya kuendesha kijiko katika Baraza la Manispaa Magharibi "B". Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni ukiukwaji wa kifungu nambari 12(7) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma Nambari 11 ya Mwaka 2014.

Kufanya malipo ya posho kinyume na muongozo na taratibu zilizowekwa na utumishi wa umma kunaweza kukapelekea kuitia hasara Serikali kwa kufanya matumizi yasiyo ya lazima na yasiyoleta tija kwa taasisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" kuhakikisha unafuata miongozo na taratibu zilizowekwa ili kuweza kufikia malengo waliojipangia.

**Majibu ya Baraza**

Changamoto hii inatokana na kuibuka kwa ziara na operation mbali mbali za Serikali Kuu na sherehe za kitaifa hali inayopelekea ofisi kutumia vyombo na mafuta ya ziada ili kufanikisha majukumu yake ya kila siku, ofisi imeshaweka mikakati ya udhibiti wa utumiaji wa mafuta kwa kumpatia afisa usafiri maelekezo ya uwekaji wa kumbukumbu vizuri kwa kuzingatia taratibu.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Hoja hii imebaki kama ilivyo, na hasa ikizingatiwa kuwa Baraza limekiri kasoro iliyokuwepo. Pamoja na hayo, Kamati ya LAAC imeilitaka Baraza kutekeleza shughuli zake kwa mujibu wa Sheria.

**5.1.4.13 Dosari katika ulipwaji wa maposho Tsh. 2,000,000**

| Hati ya Malipo | Hundi namba | Thamani ya Fedha (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 9/7 | 52 | 400,000 | Ferouz Kitwana Abdalla | Ikiwa ni malipo ya posho kwa ajili ya operator wa kijiko |
| 33/8 | 108 | 400,000 | | |
| 52/9 | 155 | 400,000 | | |
| 8/10 | 167 | 400,000 | | |
| 5/11 | 195 | 400,000 | | |
| **Jumla** | | **2,000,000** | | |

**Majibu ya Baraza**

Malipo yaliyofanyika kwa Ndugu Ferous Kitwana Abdalla yalilipwa kwa wamu tofauti kwa kipindi cha mwaka mmoja, kutokana na mazingira ya kazi alizokuwa akizifanya za uwendeshaji wa kijiko nje ya saa za kazi na mazingira hatarishi katika majaa yasiyo rasmi na yaliyoliyo rasmi, bila ya kua na msaidizi, jitihada zilizochukuliwa na ofisi ni

kumsomesha mtumishi mmoja mafunzo ya uwendeshaji wa kijiko ili aweze kusaidiana nae. Baraza la Manispaa Magharibi "B" limeshafanya jitihada za kumuombea uhamisho wa jumla kutoka Wizara ya Mawasiliano.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC haikuridhika na majibu ya Baraza, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

**5.1.4.14 Ukiukwaji wa taratibu za mkataba.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebaini Baraza la Manispaa Magharibi "B" ilifunga mkataba na kampuni ya Al – Jumra uliosainiwa tarehe 14/02/2020 kwa mujibu wa kifungu nambari 3 cha mkataba huo kinaitaka kampuni ya Al – Jumra kukusanya mapato yatokanayo na huduma ya mabango na minara ya simu, pamoja na redio kwa kipindi cha mara moja kwa mwaka kwa kampuni yoyote itakayopewa kazi hiyo ya utoaji wa huduma zilizokusudiwa na kutakiwa kukabidhi mapato hayo kwa msimamizi kwa njia ya maandishi.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 4 cha makubaliano ya mkataba kinaeleza kwamba pande zote mbili watakuwa na makubaliano ya kukabidhiana stakabadhi za malipo pale pale mapato hayo yanapokabidhiwa kwa msimamizi mkuu wa mapato.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutekelezwa kwa vifungu hivyo vya makubaliano ya mkataba jambo ambalo limepelekea kutokujiridhisha kwa usahihi wa makabidhiano ya mapato kwa kukosekana maandishi ya makabidhiano pamoja na stakabadhi zinazoonesha fedha halisi iliyokusanywa na iliyokabidhiwa.

Kutokuwepo kwa maandishi ya makabidhiano ya fedha pamoja na stakabadhi zinazothibitisha uhalali wa makabidhiano ya fedha hizo kunaweza kukajitokeza

viashiria vya ukiukwaji wa mikataba jambo ambalo litapelekea upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa Magharibi “B” kuhakikisha unatekeleza matakwa ya makubaliano hayo kwa lengo la kuwepo kwa uwazi na usawa wa fedha iliyokusanywa na kukabidhiwa kwa mujibu wa utaratibu.

**Majibu ya Baraza**

Kwa mujibu wa mkataba na makubaliano hakuna taratibu iliyokiukwa, mkataba upo, fedha zilizokusanywa zimeingizwa kwenye account husika na stakabadhi za fedha hizo zimewasilishwa kwa mtunza hazina.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa vocha ya tarehe 5 Agosti, 2020 yenye thamani ya Tsh. 952,381 imekatwa kodi ya asilimia tano (5%) kama taratibu zinavyoelekeza, isipokuwa kwamba, vocha ya tarehe 3 Novemba, 2020 yenye thamani ya Tsh. 11,250,000 haikukatwa kodi ya asilimia tano.

Kamati ya LAAC imeibakisha hoja hii kwa kuwa Baraza lilishindwa kuipatia Kamati vielelezo vinavyothibitisha kuwa viwango vilitajwa kwenye vocha hizo vilikuwa sahihi au kuna risiti nyengine.

Aidha, barua zilizopatiwa Kamati zilishindwa kuonesha makusanyo hayo ni ya miezi mingapi.

Ili kasoro kama hii isijitokeze tena Kamati ya LAAC inalitaka Baraza kuwa makini wakati linatekeleza majukumu yake.

**5.1.4.15 Dosari zilizojitokeza katika ununuzi wa mafuta ya miradi ya maendeleo ya Wadi shilling 15,000,000/=**

Katika ukaguzi uliofanyika umebainika Baraza la Manispaa la Magharibi "B" kufanya matumizi yenye thamani ya shilingi 15,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa lengo la kutekeleza usimamizi wa miradi ya maendeleo yaliyopo kwenye Wadi ya Magharibi "B". Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa ununuzi wa mafuta, uwekaji wa kumbukumbu za uingizaji na utoaji wa mafuta hayo, ugawaji wa mafuta hayo, matumizi ya fedha kutokulingana na uhalisia wa ununuzi wa mafuta hayo na utumiaji wake.

Kutokana na dosari zilizobainika zimeashiria uwepo wa udhibiti usiotosheleza wa ununuzi na utumiaji wa mafuta na usimamiaji wa miradi ya maendeleo jambo ambalo linaweza kupelekea kutokutekelezeka kwa miradi hiyo au kutokukamilika kwa wakati kutokana na kuwepo kwa matumizi ya mafuta yasiyoridhisha.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" kuhakikisha wanasimamia vizuri na kuweka udhibiti mzuri wa matumizi ya mafuta kwa lengo la kuweza kufikia malengo waliyokusudia. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Gharama za ununuzi wa mafuta ya usimamizi wa miradi ya maendeleo**

| **Nambari ya Hati ya Malipo** | **Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs)** | **Aliyelipwa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| 6/6 | 5,000,000 | Zanzibar Petroleum | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Limited | Mradi wa Madiwani |
| 50/6/2021 | 10,000,000 | | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya uchukuaji wa kifusi katika Idara ya Ujenzi katika Wadi ya Mombasa na Wadi ya Bweni |
| **Jumla** | **15,000,000** | | |

**Majibu ya Baraza**

Mafuta yalinunuliwa na kuingizwa ghalani kwa maana yalirikodiwa katika daftari la kuingia na kutoka ghalani kwani ipo saini ya mpokeaji wa mafuta hayo ambaye ni waheshimiwa madiwani waliochukua kwa niaba ya mamlaka ya ujenzi na utuzanji wa barabara (UUB), ambao ndio wakandarasi waliopewa kazi hiyo.

Aidha, kuhusu hoja ya fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta hazilingani na kazi zilizofanyika. Ieleweke kuwa gharama hizo zimetumika kwa uchukuaji wa kifusi kutoka shimo la Kibele na kukipeleka eneo husika kwa usambazaji na ushindiliaji wa kifusi kwa kutumia Doza na vitendea kazi vyengine vyenye gharama kubwa.

Mkaguzi katika maelezo yake ameweka wadi ya Mombasa hii wadi haijafanyiwa malipo ya ununuzi wa mafuta, hata hivyo, kuhusu kurikodiwa mafuta zipo nyaraka waliosani Waheshimiwa Madiwani na walipatiwa Wakaguzi wakati wa ukaguzi huo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilimtaka Mkaguzi kuthibitisha hoja hii kwa kuiweka Wadi ya Mombasa kama mnufaika. Kutokana na takwa hilo, Mkaguzi aliieleza Kamati kuwa taarifa hizo zimepatikana kupitia nyaraka za Baraza zilizowasilishwa kwa Mkaguzi wakati wa ukaguzi.

Kamati ya LAAC ilishindwa kulithibitisha hilo kutokana na ufinyu wa muda, hivyo, hoja hii imebaki kama ilivyo.

### 5.1.4.16 Dosari katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wadi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Baraza la Manispaa Magharibi “B” limefanya utekelezaji wa miradi 14 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yenye thamani ya shilingi 58,360,363 katika utekelezaji wa miradi hiyo dosari zifuatazo zimebainika kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Dosari katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Wadi**

| Nam. | Jina la Mradi | Eneo/Wadi | Makadirio ya fedha (Tshs.) | Fedha iliyopatikana (Tshs.) | Hatua ya Mradi ulivyotekelezwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ununuzi wa Viti 80 kikundi cha HANUNI MTU | Kijitoupele | 5,000,000 | 2,010,000 | Kutokuonekana kwa viti hivyo. |
| 2. | Ujenzi wa Kivuko | Kwarara - Kijitoupele | 2,990,000 | 2,990,000 | Mradi haukukamilika |
| 3. | Uwekaji wa Nguzo za umeme | Bweleo – Kipenyoni | 5,000,000 | 1,859,228 | Kukosekana kwa taarifa za utekelezaji wa mradi |
| 4. | Ujenzi wa Mtaro | Mombasa | 4,718,000 | 4,347,637 | Mradi umekamilika |
| 5. | Ukarabati wa njia za ndani | Mombasa | 5,000,000 | 5,000,000 | Mradi huu haukutekelezeka hadi ukaguzi unakamilika. |
| 6. | | Kinuni | 5,000,000 | 5,000,000 | Mradi haukukaguliwa. |
| 7. | | Fuoni Mambosasa | 5,000,000 | 5,000,000 | |
| **Jumla** | | | **58,360,363** | | |

Kwa mujibu wa jadweli linaonesha kwamba ipo miradi iliyotekelezeka kwa kiwango kisichoridhisha kutokana na uhaba wa upatikanaji wa fedha zilizokadiriwa kukamilisha miradi hiyo, na ipo miradi ambayo ilipatiwa fedha kamili kwa mujibu wa makadirio yao lakini utekelezaji wake hauridhishi kutokana na kutekelezeka kwa kiwango cha chini kulingana na thamani ya fedha iliyotumika. Aidha, ipo baadhi ya miradi pamoja na upatikanaji wa fedha zake kuwa mdogo lakini haikuweza kutekelezeka na kutokupatikana kwa sababu zilizopelekea kutokutekelezeka kwa miradi hiyo kwa kukosekana vielelezo vya matumizi ya fedha walizoingiziwa. Vile vile kuna baadhi ya miradi haikuweza kukaguliwa na kutolewa maomi ya utekelezaji wake.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Magharibi "B" kuhakikisha unabuni miradi michache ambayo itaweza kutekelezeka kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha kuliko kuwa na miradi mingi ambayo utekelezaji wake unakuwa mgumu kutokana na uchache wa upatikanaji wa fedha ambapo kunapelekea baadhi ya miradi kutokutekelezeka.

**Majibu ya Baraza**

**MIRADI YA MAENDELEO YA WADI**

1. Mradi wa viti 80 viti vimenunuliwa na vimepokelewa na Diwani husika na viti vipo kwenye hicho kikundi cha HANUNI MTU kwa lengo la ukodishwaji ili kiweze kujiendesha vile vile uhakiki na uchunguzi uliofanywa ZAECA kwa maafisa wao wamejiridhisha kwa kwenda kila kituo kilichokabidhiwa viti.

2. Mradi wa ujenzi wa kivuko katika shehia ya Kwarara ulikamilika na gharama iliyotumika inaendana na thamani ya fedha, ikumbukwe kuwa eneo hilo lilikuwa

na changamoto kubwa ya kutuwama kwa maji pia ardhi yake ina asili ya kutitia na kupelekea kivuko hicho kuonekana kipo chini. Na Mradi huo kwa sasa unatumika na umewaondolea shida Wananchi waliyokuwa wakiipata awali. Vile vile, uhakiki na uchunguzi uliofanywa ZAECA kwa maafisa wao wamejiridhisha kuwa kivuko kipo na kinatumika.

3. Mradi wa nguzo za umeme Eneo la Bweleo mkaguzi ameripoti kutopata taarifa sahihi kutoka kwa watendaji, Ofisi liliwapatia wakaguzi maafisa pamoja na Mh, Diwani husika wa wadi kwa ajili ya kwenda kufanya ukaguzi wa nguzo na kukuta nguzo tatu (3) kuhusu kuwepo nguzo mbili kwenye barua ya afisa manunuzi hii ilikuwa ni kosa la kiuwandishi (typing error) lakini kwenye invoice zipo nguzo tatu na hata barua ya maombi ya Mh. Diwani zipo nguzo tatu (3). na Malipo yamefanyika kwa gharama ya nguzo Tatu.

4. Mradi wa ujenzi wa mtaro kwenye Wadi ya Mombasa kwa ajili ya kupitishia maji ya mvua umekamilika na thamani ya fedha iliyotumika inaendana na kazi husika ikumbukwe hilo eneo lilikuwa na changamoto kubwa ya kutuama kwa maji.

5. Ofisi haikufanya malipo yoyote yenye gharama ya Shilingi 5,000,000 katika wadi ya Mombasa kwa ukarabati wa njia za ndani kama mkaguzi alivyoainisha kwenye hoja ya ukaguzi. Mradi huo haukuwepo kwenye bajeti ya mwaka husika na wala haukutekeleza.

6. Mradi wa ukarabati wa njia za ndani kwa wadi ya Kinuni katika hoja za mkaguzi ameeleza kwamba ameshindwa kutembelea katika eneo husika ili kuweza kuthibitisha. Ukweli ni kwamba wakaguzi walipelekwa eneo hilo mara mbili kwa siku tofauti. Vilevile, walipelekwa pamoja na mkuu wao wa ukaguzi (Supervisor).

**Uchunguzi na Mapendezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC imezifuta baadhi ya hoja baada ya Mkaguzi kama ifuatavyo:

i. Mradi wa ununuzi wa viti Kijito Upele, viti vimeonekana
ii. Mradi wa Ujenzi wa Kivuko - Kwarara – Kijitoupele haukukamilika wakati umekamilika na kilichotokea ni kuwa Mkaguzi huyo hakufanya utafiti zaidi.
iii. Mradi wa Ujenzi wa Mtaro – Mombasa, Mkaguzi kaeleza kuwa Mradi umekamilika, hivyo, Kamati ilishindwa kujua sababu iliyompelekea Mkaguzi kuandikwa hoja hiyo.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC imemtaka Mkaguzi Mkuu kuwa makini wakati anaandaa Ripoti yake ili kuondosha usumbufu kwa Wadau wake.

### 5.1.4 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

**Taarifa ya Mapato**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake ilikadiria kukusanya jumla ya Tzs 600,549,500/= kutoka katika vianzio vyake mbali mbali na hadi kufikia 30 June 2021 ilifanikiwa kukusanya jumla ya Tzs 657,042,962/= sawa na asilimia 109.4% ya makidirio.

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2020/2021 limefanikiwa kuzidi malengo ya makusanyo kwa sababu ya jitihada kubwa ya usimamizi na ufanisi wa watendaji wa Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake.

Mchanganuo wa vianzio hivyo ni kama unavoonekana katika jadweli hapo chini.

| Chanzo | Makadirio | Halisia | Asilimia(%) |
|---|---|---|---|
| Ada ya Madiko | 4,200,000 | 5,555,000 | 132.26 |
| Ada ya Masoko | 67,847,500 | 53,755,000 | 79.23 |
| Kodi ya Milango | 67,000,000 | 51,108,000 | 76.28 |
| Leseni za Biashara | 155,252,000 | 142,375,000 | 91.71 |
| Ada ya Ujenzi-DCU | 47,000,000 | 32,510,000 | 69.17 |
| Ada ya Maegesho | 31,500,000 | 26,648,400 | 84.60 |
| Ada ya Usafi | 34,200,000 | 55,108,000 | 161.13 |
| Malipo ya Kware | 57,000,000 | 22,152,000 | 38.86 |
| Uchinjaji na Uingizaji wa Wanyama | 5,700,000 | 7,162,000 | 125.65 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kodi ya ukumbi | 19,000,000 | 13,490,000 | 71.00 |
| Fomu za Leseni | - | 7,020,000 | |
| Minara & Matangazo | 80,000,000 | 187,744,000 | 234.68 |
| Ushuru wa Matangazo | - | 33,058,062 | |
| Fomu za Mchanga | 5,000,000 | 1,990,000 | 39.80 |
| Kodi ya gari | 21,500,00 | - | |
| Ada mbalimbali | 26,850,000 | 17,367,500 | 64.68 |
| JUMLA | 600,549,500 | 657,042,962 | 109.47 |

- Pia Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake ilikadiria kutumia jumla ya Tzs 8,182,619,000/= kwa matumizi ya kazi za kawaida lakini hadi kufikia 30 June 2021 ilitumia jumla ya Tzs 7,630,509,082/= sawa na asilimia 93.25% ya makadirio.

- Vilevile Baraza lilikadiria kutumia TZS 180,000,000/= kwa kazi za maendeleo lakini hadi kufikia 30 June 2021 lilitumia TZS 45,095,700/= sawa na asilimia 25.05% ya makadirio.

Makadirio na Halisia ya matumizi ya kazi za maendeleo ya Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yalikua kama ifuatavyo:-

| Jina la Mradi | **Makadirio** | **Matumizi Halisi** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| 1. Ukamilishaji wa Skuli ya Maandalizi Machomane | 25,000,000 | 21,929,446 | |
| 2. Ukamilishaji wa Skuli ya | 30,000,000 | 23,166,254 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Msingi Kwale | | | |
| 3 Ujenzi wa vyoo sita Skuli ya Uwandani | 25,000,000 | - | |
| 4. Ukarabati wa maduka Soko la Chake Chake. | 50,000,000 | - | |
| 5. Ujenzi wa msingi wa ghorofa Soko kongwe Machomane | 50,000,000 | - | |
| **JUMLA** | **180,000,000** | **45,095,700** | 25.05% |

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini kuwa mtandao Baraza la Mji Chake Chake linahitajika kutumia wataalam katika kukadiria vyanzo vyake vya mapato na sio kufanya kazi kimazoea hata hivyo Kamati imeridhika na ukusanyaji huo uliovuka malengo.

**MATOKEO YA UKAGUZI**

**5.1.5.1 Kutokufikiwa kwa ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya Maendeleo**

**Maelezo ya hoja.**

Ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba fedha zilizotumika kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo pamoja na uwezeshaji wa wajasirimali hazikuweza kufikia kiwango halisi kilichotakiwa kwa mujibu wa utaratibu na agizo lililotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa ziara za kutembelea miradi ya maendeleo katika Halmashauri na Mabaraza ni kwamba makusanyo yanapaswa yatumike kwa shughuli za miradi ya maendeleo kwa asilimia

30 na uwezesghaji wajasiriamlai ,vijana na wanawake na watu wenye ulemavu kwa asilimia 10 jambo ambalo ukaguzi umebaini matumizi ya miradi ya maendeleo yamefanyika kwa asilimia 6.86 ya makusanyo halisi na hakukubainika matumizi yoyote yaliyofanyika kwa uwezeshaji wa wajasiria mali vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa asilimia 10.

Aidha, ukaguzi umebaini matumizi ya asilimia 93.14 yametumika kwa huduma za uendeshaji wa Baraza jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Kutokana na Janga la Korona (Covid 19) kwa kipindi hicho utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ulikuwa mgumu kwani fedha nyingi zilielekezwa kwenye matumizi ya uendeshaji kwani kwa muda huo Baraza lilikuwa katika Ugatuzi.

**Uchunguzi wa Kamati**

Wakati Kamati ya LAAC inachunguza hoja hiyo imegundua kuwa bado Baraza la Mji Chake Chake halina mikakati Madhubuti ya kufanikisha mpango wa miradi ya maendeleo, hata hivyo Kamati imegundua kutokuwepo kwa ufanisi na mashirikiano Madhubuti ya kazi baina ya watendaji.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inapendekeza watendaji wote wa Serikali kuhakikisha wanatimiza malengo ya taasisi kwani kufanya hivyo ndo kunapelekea kutimia kwa malengo ya Serikali Kuu kwa ujumla, pia Kamati ya LAAC imelitaka Baraza La Mji Chake Chake kuzingatia uweledi katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

### 5.1.5.2 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma Shilingi 23,078,040.07

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Chake Chake Pemba limefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Watoa huduma hao walisajiliwa kisheria kwenye mamlaka ya manunuzi na uondoshaji wa mali za umma na sababu hiyo ndio iliyofanya kuweza kulipika katika mfumo wa malipo wa Wizara ya Fedha changamoto ni wafanyabiashara hao kutokutunza kumbukumbu za usajili (Certificate).

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

1. Baadhi ya mamlaka za serikali zinachelewesha kukamilisha majukumu yake kitu ambacho hupelekea ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuona kasoro katika taasisi zinazozikagua, ambapo Mamlaka ya Manunuzi imechelewa kuifanyia uhakiki orodha ya wafanyabiashara waliojisajili ndipo Mkaguzi akashindwa kuziona
2. Wafanya biashara kutokutunza vizuri vielelezo na hati za usajili wao kitu ambacho huleta taharuki wakati wa ukaguzi.
3. Baraza la Mji Chake Chake kutohakikisha usajili wa wafanya biashara kabla ya kufanya nao biashara na badala yake huhakiki wakati wa kuwalipa.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC imependekeza kwa Baraza kua na utaratibu wa kuhakiki uthibitisho wa uhalali wa wafanya biashara kabla ya uombaji wa huduma, pia kamati ya LAAC inazitaka malaka zote nchini kutimiza wajibu wao kuepusha usumbufu kwa taasisi amabazo zinategemea taarifa kutoka kwao.

Jadweli Nambari 43: Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

**5.1.5.3 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 16,360,204**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 16,360,204 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Baraza la Mji Chake Chake lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:- Jadweli Nambari 44 : Malipo yenye vielelezo pungufu**.**

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Vielelezo hivyo kwa wakati huo vilikosekana kutokana na muingiliano wa kaguzi za mara kwa mara na kupelekea kutokuonekana katika sehemu husika hata hivyo kwa sasa zipo kwenye hati za malipo (Vocha) husika.

**Uchunguzi na Mpaendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC imebaini Baraza linakabiliwa na changamoto ya ukaguzi wa kila mara kutoka Mamlaka tofauti jambo amabalo linampelekea kumkosesha Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kukagua baadhi ya hati za malipo.

Aidha, Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inazishauri Taasisi za uchunguzi kuhakikisha inaipisha ofisi ya Makaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kazi yake ya kikatiba kabala ya wao kufanya hivyo**.**

**5.1.5.4 Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 40,762,086**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 40,762,086 zimetumika kwa ununuzi wa bidhaa mbali mbali lakini bidhaa hizo hazikurikodiwa katika madaftari ya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Kwa wakati huo Baraza lilikuwa na mfumo wa Ugatuzi hivyo vifaa hivyo vilikosekana katika daftari la ghala kuu kutokana na mali /bidhaa hizo kurikodiwa na Vitengo husika Mfano. Elimu, Afya na Kilimo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Wakati Kamati inafuatilia hoja hii imegundua kuwa kasoro hii imetokana na uamuzi wa kuvigawa vifaa moja kwa moja kwa vitengo kabla ya kuvirikodi katika daftari kuu. Baraza la Mji CHake Chake limerekebisha kasoro hiyo baada ya kupata maoni ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, hata hivyo Kamati imelitaka Baraza kuhakikisha linatekeleza kazi zake kwa utaratibu na Sheria.

**5.1.5.5 Vifaa ambavyo havikuonekana kwa ukaguzi Shilingi 2,854,368**

Baraza la Mji Chake Chake limefanya matumizi kwa mujibu ya hati nambari 1/11 ya tarehe 30/10/2020 kwa hundi namba 004576 yenye thamani ya shilingi 2,854,368 aliyolipwa bwana Omar Said Haji kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya gari kwa kwa mujibu wa ankara nambari 172 na hati ya manununzi (LPO) namba 54795.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika vifaa hivyo havikuonekana kutumika, kupokelewa katika daftari la kumbukumbu la manunuzi, kutolewa kwa mujibu wa matumizi jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa matumizi hayo. Kufanya hivyo

ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Vifaa hivi vimepokelewa na kurikodiwa katika Daftari la kumbukumbu za manunuzi kiukamilifu kama taratibu zinavyotakiwa na tayari vilishatumika kwenye matengenezo ya gari hio, kujitokeza tena kwenye ripoti ya CAG tunaamini kua ni makosa ya kibinaadamu.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati ya LAAC imegundua kuwa wakati Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anakagua Ofisini hapo hakupatiwa daftari hilo kwa wakati jambo ambalo limempelekea mkaguzi kuiripoti hoja hii,

Hivyo, Kamati inazitaka sana Taasisi za Serikali kuwasilisha taafira, uthibitisho ama vielelezo vyote amabavyo mkaguzi atavihitaji wakati wa ukaguzi, kutopatiwa kwa vielelezo hivyo ni kwenda kinyume na taratibu za Sheria, Kanuni na Miongozo inayowapa wao kufanya kazi hiyo.

**5.1.5.6 Upotevu wa mapato ya ukodishwaji wa milango ya biashara Shilingi 10,800,000**

Baraza la Mji Chake Chake linamiliki milango ya maduka katika soko la matunda ambayo huikodisha kwa wafanyabiashara mbali mbali.

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini kuwepo kwa milango tisa (9) ya kufanyia biashara iliyokodishwa kwa wafanyabiashara mbali mbali hadi ukaguzi unakamilika tumeshindwa kujiridhisha thamani halisi ya bei ya ukodishwaji wa milango hiyo

kutokana na kukosekana kwa mikataba ya ukodishwaji na kujitokeza kwa kutofahamiana baina ya wafanyabiashara na mkodishaji ambaye alisita kutoa mikataba hiyo na kupelekea kutokutoa mikataba mikataba mipya ya ukodishaji na hatiamae wafanya biashara waliendelea kutumia milango hiyo bila uwepo wa uthibitisho wa kufanyika kwa malipo hayo.

Mchanganuo wa gharama za ukodishwaji wa milango hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:- Jadweli Nambari 46 : Gharama za ukodishwaji wa milango ya biashara.

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Kutokana na matengenezo na maboresho ya milango hiyo Baraza halikukodisha na halikutowa mikataba mipya ya ukodishwaji kwavile wafanyabiashara katika maduka hayo yaliotajwa walishapewa barua za kusitisha biashara ili kupisha Ujenzi.

**Uchunguzi wa Kamati**

Wakati Kamati ya LAAC inachunguza hoja hii ilibaini mambo yafuatayo.

1. Wapangaji hao wanatumia milango hiyo ya duka bila ya mikataba.
2. Malipo ya milango hiyo ya duka ni tofauti kitu ambacho kinadaiwa kuwa ni upendeleo kwa baadhi ya wapangishwaji.
3. Baraza La Mji Chake Chake licha ya kuwapa barua ya kuondoka wapangaji hao bado wapo wanafanya biashara.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kufuatia kasoro zilizojitokeza Kamati imelitaka Baraza la Mji Chake Chake kuhakikisha linafanya maamuzi yatayoongozwa na Sheria, ikiwa Baraza litaamini kuwabakisha

wapangaji hao kuna maslahi na taifa basi ifanye hivyo kwa kuwapa mikataba halali na kama litaendelea na ujenzi kama ulivyopanga basi ni liwaondoe kwa utaratibu ulio sahihi.

### 5.1.5.7 Dosari katika udhibiti wa Mapato

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa baadhi ya vianzio vya mapato ambavyo udhibiti wake hauridhishi hali inayopelekea kuwepo kwa dosari mbali mbali zinazosababisha ufanisi wa makusanyo kupitia vyanzo hivyo kutokufikiwa kama ilivyopangwa. Dosari hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:- Jadweli Nambari 47 : Dosari katika udhibiti wa mapato.

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

i) Utaratibu wa gari ya mizigo unaweka mafuta katika kituo chochote cha mafuta kilichokaribu na kazi husika, hii ni kutokana na wateja wa gari hiyo ni wananchi hawataki kufanya malipo kwa njia ya benki kwani ni usumbufu na ukilazimisha wanaamua kuacha gari ya serikali na kutumia gari binafsi za Mitaani.

ii) Kupitia Baraza la Madiwani (Kikao) walikubaliana Waheshimiwa Madiwani kulitafutia wateja gari hilo la mizigo ili liweze kuingiza mapato kutokana na Ushindani wa magari mengine ya mizigo ambayo yapo mitaani ilipelekea gari hili kukosa wateja hivyo Mwenyekiti alikuwa yuko Sahihi kutafuta wateja.

iii) Kupanga utaratibu maalum wa usafirishaji wa madagaa kutokana na mfumo wa usafirishaji nivigumu kwa sababu za kuhama hama kwa wavuvi kwenda dago. Aidha kuhusu ulipaji wa Ada kwa njia Taslim hilo halifanyiki badala yake fedha zote hulipwa kwa njia za kibenki.

#### 5.1.5.8 Ukusanyaji wa mapato kinyume na makadirio

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Chake Chake hukusanya mapato kupitia vyanzo mbali mbali lakini ukusanyaji wa mapato hayo hufanyika kinyume na makadirio yaliowekwa,aidha imebainika kutokuwepo kwa makadirio kwa baadhi ya vianzio vya mapato ukadiriaji mdogo kwa baadhi ya vianzio pamoja na kutokusanya mapato kwa baadhi ya vianzio kama ilivyopangwa.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa mapato ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(1) (2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Ofisi ya Baraza la Mji Chake Chake ni kawaida yake kila mwanzoni mwa mwaka wa fedha kuandaa makadirio kwa kila chanzo ambacho kinamilikiwa na Ofisi hio, utofauti ni ufafanuzi zaidi kwenye baadhi ya vianzio wakati tunawasilisha taarifa kwa Wah. Madiwani tukiwa tayari tulishavikadiria kwenye vyanzo vikuu vyake. Vilevile kama inavojuilikana kua mara nyingi makadirio yanapishana na uhalisia, hata hivyo kuonekana makadirio kuzidiwa sana na uhalisia kwenye chanzo cha Minara & Matangazo hii ni kutokana na Kampuni ya AL- JUMURA kuongeza malipo zaidi kutokana na makusanyo yake pia kuongezeka.

**Uchunguzi na Mapendekezo Kamati**

Kamati ya LAAC iliyakubali majibu ya Baraza baada ya kujiridhisha na makusanyo mazuri ya mapato yaliyopelekea kuvuka kwa lengo la makusanyo ya mwaka. Hata hivyo, Kamati ya LAAC ilishauri uongozi wa

barazala Mji Chake Chake kuzingatia wededi wakati wa kufanya makadirio ya mapato.

**5.1.5.9 Kukosekana kwa mapato yanayotokana na kutosajiliwa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato.**

Ukaguzi uliofanyika umebainika kujitokeza kwa uwezekano mkubwa wa kukosekana kwa mapato yanayotokana na kutokusajiliwa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato ambavyo havikusajiliwa na vina uwezo mkubwa wa kuchangia mapato kwa Baraza la Mji Chake Chake vikiwemo mahoteli, nyumba za kulala wageni, gereji,viwanda vya ufundi seremala na maduka ya ushonaji wa nguo.

Kufanya hivyo kunapelekea kulikosesha Baraza mapato yatokanayo na vyanzo hivyo ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 94 cha Sheria Nambari 7 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2014.

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Vyanzo hivi vya mapato (Hoteli na nyumba za kulala wageni bado kama ofisi ya baraza la Mji tunachangamoto ya muingiliano wa sheria na taasisi nyengine ikiwemo ZRA pamoja na Kamisheni ya Utalii hata hivyo ofisi bado inafuatilia kwenye kupata mapato yake Aidha kuhusu gereji, viwanda vya ufundi seremala na maduka ya ushonaji wa nguo taratibu za ukataji wa leseni zinafanyika

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika ufatiliaji wa hoja hii kamati ya LAAC iligundua yafuatayo.

1. Bado kuna sitonfahamu kubwa baina ya taasisi za serikali katika ukusanyaji wa baadhi ya kodi za ndani.

2. Uongozi wa Baraza la Mji Chake Chake hauna kasi katika ufanisi wa swala kusajili vyanzo vya mapato kama gereji, seremala na viwanda vyaufundi Pamoja na maduka ya ushonaji.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kufuatia kasoro hizo kamati ya LAAC inapendekeza taasisi zinazohusiana na ukusanyaji wa kodi kama ZRA, TRA, Kamisheni ya Utalii na Mabarza ya Mji yakaa kwa pamoja na kuunda utaratibu ulikua sahihi na usioleta kerokwa walipaji na wakusanyaji wa kodi hizo, kwani kutofanya hivyo kunapelekea kupotea kwa mapato hayo.

**5.1.5.10 Kukosekana kwa uwiyano wa taarifa za fedha Maelezo ya hoja.**

Katika ukaguzi uliofanyika umebaika kutowepo kwa uwiyano wa taarifa za fedha baina ya taarifa za benki 'Bank Statement' na taarifa za mwisho wa mwaka 'Final Account'.

Kufanya hivyo kunapelekea taarifa za ufungaji wa mahesabu kutokuwa na sura sahihi na halisi ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa dosari zilizobainika ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-Jadweli Nambari 49: Kukosekana kwa uwiyano wa taarifa za fedha

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Tatizo hili la kutokuwa na uwiyano wa taarifa za fedha ulisababishwa na upya wa utumiaji wa mfumo wa matumizi wa LGAs ambao ulianzishwa na kutumika katikati ya mwaka wa fedha 2020/2021. Hata hivyo, kwa mwaka mwengine unaofuata wa fedha tatizo hili halitojitokeza tena kwani tayari tumeshapewa mafunzo ya kutosha ya utumiaji wa mfumo huu.

**Uchunguzi na Mpaendekezo ya Kamati**

Kufuatia mabadiliko hayo ya mfumo yaliosababisha kasoro hizo Kamati haikuridhishwa na majibu hayo kwani uongozi ulikua na uwezo wa kurekebisha taarifa hizo kabla ya kuwasilisha ripoti hiyo ya fedha kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuwasilisha ripoti zisizo sahihi ni kitendo kinachoenda kinyume na taratibu za kihasibu.

Hivyo, Kamati imelitaka Baraza la Mji Chake Chake lihakikishe linafanya kazi kwa kuzingatia sheria na kufuata taratibu na kanuni na miongozi ya kihasibu.

**5.1.5.11 Kukosekana kwa matumizi na vielelezo vya Shilingi 20,000,000**

Baraza la Mji Chake Chake lilihaulisha jumla ya shilingi 65,701,335 kutoka Hesabu nambari 0717831001 yenye jina la Basket Fund ambayo ilikuwa ikitumika awali kwa ajili ya matumizi ya shughuli za uendeshaji wa Baraza kwenda Hesabu nambari 9928210104 yenye jina la Local Government Authorities Account (LGA's Account).

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 45,701,335 zilitumika kwa matumizi mbali mbali ya shughuli za uendeshaji na kupelekea kuwepo kwa bakaa ya shilingi 20,000,000 ambazo matumizi yake pamoja na vielelezo vya matumizi hayo havikuweza kupatikana kwa ukaguzi jambo ambalo limepelekea uwepo wa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Baraza la Mji Chake Chake**

Ni kweli lakini bakaa hii ya fedha ziliganda kwenye mfumo wa matumizi wa LGAs IFMS ikawa sisi hatupati kuzitumia, jitihada mbalimabli zilifanyika na kufanikiwa kurejeshwa fedha hizo kwenye mfumo huo katika account ya LGAs Reccurent Account mnamo mwezi Mei 2022.

**Uchunguzi na Mapendekeko Kamati**

Kamati ya LAAC imegundua kua kuanzishwa kwa mfumo mpya umeliweka katika wakati mgumu Baraza, hivyo unalitaka Baraza la Mji Chake Chake kuhakikisha mara tu inapoingia katika mfumo mwengine kuwapatia watendaji wake mafunzo ili kua weledi katika kutimiza majukum yao ya kila siku.

### 5.1.6 BARAZA LA MJI MKOANI

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Mji la Mkoani kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 374,720,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali . Hadi kufi kia tarehe 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 393,793,110 zilikusanywa na Baraza sawa na asilimia 105.09 ya makadirio.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini Kamati kubaini dosari kadhaa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka yaani **"Financial** Statement' ikiwemo kutofafanuliwa kwa vifungu "note" ya 10, 12, 18, 11, 13

Kamati inashauri uongozi wa Baraza kuwajengea uwezo watendaji wa kitengo cha uhasibu katika kufunga mahesabu hayo ikiwa ni pamoja na matumizi ya mifumo katika uandaaji wa taarifa hizo.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Mji Mkoani kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 6,452,337,890 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 286,137,890 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufi kia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 5,584,783,908.67 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 86.55 ya makadirio na shilingi 249,461,452 zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 87.18 ya makadirio.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini kuwa Baraza la Mji Mkoani limetumia fedha katika shughuli mbalimbali za miradi ya maendeleo hata hivyo halikuwasilisha ipasavyo fedha za

uwezeshaji wa a ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo pamoja na uwezeshwaji wa wajasiriamali kiuchumi, hivyo Kamati inaliomba Baraza katika kuzingatia suala hilo wakati wa kutekeleza bajeti ya mwaka husika kwa kuteka asilimia 40 ya mapato ya ndani kwa jili ya miradi ya maendeleo na kuwawezesha wananchi kiuchumi.

**5.1.6.1 Kutokufikiwa kwa ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.**

Baraza la Mji Mkoani limekusanya jumla ya shilingi 393,793,110 sawa na asilimia 105.09 ya makadirio kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 ambapo kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 63,323,862 zilitumika kwa ajili ya kazi za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 16.08 ya makusanyo halisi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba fedha zilizotumika kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo pamoja na uwezeshwaji wa wajasiriamali hazikuweza kufikia kiwango halisi kilichotakiwa, kwa mujibu wa utaratibu na agizo lililotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa ziara za kutembelea miradi ya maendeleo katika Halmashauri na Mabaraza ya Miji ni kwamba makusanyo yanapaswa yatumike kwa shughuli za miradi ya maendeleo kwa asilimia 30 na uwezeshaji wa wajasiria mali,vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa asilimia 10 jambo ambalo ukaguzi umebaini matumizi ya miradi ya maendeleo yamefanyika kwa asilimia 16.08 ya makusanyo halisi na hakukubainika matumizi yoyote yaliyofanyika kwa uwezeshaji wa wajasiria mali,vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa asilimia 10.

Aidha, ukaguzi umebaini matumizi ya asilimia 83.92 yametumika kwa huduma za uendeshaji wa Baraza jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

**Majibu ya Baraza la Mji Mkoani**

Baraza la Mji Mkoani limekuwa na utaratibu wa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia sehemu ya fedha zinazotokana na makusanyo ya ndani,

Ni kweli katika mwaka wa fedha 2020-2021 Baraza la Mji Mkoani lilitumia 16.08 ya fedha za makusanyo ya ndani kutekeleza miradi ya maendeleo na hivyo kupungua kwa ufanisi katika utekelezaji.

Baraza la Mji Mkoani kwa sasa limeshachukuwa hatua ya kutumia sehemu ya fedha za makusanyo ya ndani kwa kuzingatia maelekezo na miongozo inayotolewa.

Kuhusu asilimia 10 ya fedha za mahitaji maalum Baraza la Mji Mkoani linakiri

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imebaini kuwa Baraza limekwenda kinyume na agizo la Mhe Rais kwa vile wameshidwa kutenga asilimia 40 ya mapato ya makusanyo ya ndani licha ya kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa kisingizio kuwa agizo hilo limetolewa katikati ya mwaka wa utekelezaji wa Bajeti.

Kamati haikuridhika na sababu hizo kwa vile hata awamu iliyopita ya Mh. Dk Ali Mohd Shein ilikuwa inasisitiza juu ya mabaraza ya miji kuacha kutumia fedha nyingi katika shughuli za uendeshaji wa ofisi badala yake wajikite zaidi katika kutekeleza miradi ya jamii na kusaidia makundi maalum ya vijana,wanawake, walemavu na wajasiriamali mbalimbali hivyo maelekezo hayo sio mapya ila hayakuekwa katika mazingatio na Baraza hili.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya Laac inalishauri Baraza la Mji Mkoani wawe makini katika utekelezaji wa maagizo yanatolewa na viongozi wakuu wa nchi ambayo yanalenga kutoa huduma bora kwa jamii. Aidha Kamati inasisitiza juu ya utekelezaji wa Agizo la Mhe Rais katika Bajeti zijazo juu ya utoaji wa fedha kwa uwezeshaji wa wajasiriamali, vijana,wanawake na watu wenye ulemavu kwa asilimia 10 na Asilimia 30 kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili lengo kuanzishwa Mabaraza ya Miji na Manispaa liweze kufikiwa.

**5.1.6.2 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 13,089,111.**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi. Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Mkoani Pemba limefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Majibu ya Baraza la Mji Mkoani**

Baraza la Mji Mkoani katika kutekeleza majukumu yake ya manunuzi ya bidhaa na huduma, limekuwa likifanya manunuzi kwa wafanyabiashara ambao wamekidhi vigezo vilivyowekwa ikiwemo kusajiliwa katika Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa mali za umma.

Ni kweli Baraza la Mji Mkoani katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 lilifanya malipo kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa ka tika Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma.

Hii ilitokana na sababu kwamba malipo hayo yalikuwa ya malimbikizo ya madeni ya miaka ya nyuma ambayo wafanyabiashara waliokuwa wanatudai kwa wakati huo walikuwa hawakukidhi vigezo vinavotakiwa, ila Baraza likalazimika kuyalipa madeni hayo kwa lengo ya kuondoa uwezekano wa kutokea mgogoro baina ya Baraza na wafanya biashara hao.

Kwa sasa Baraza la Mji Mkoani limeshayafanyia kazi mafungufu haya na linafanya manunuzi kwa wafanyabiashara waliokithi vigezo vinavyotakiwa na Mamlaka ya manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kwa vile Baraza la Mji Mkoani limekiri kuwepo kwa dosari hii Kamati haikuona haja ya kuendelea na hoja hii hata hivyo Kamati haijaridhika na sababu zilizotolewa na baraza la Mji Mkoani kwenda kinyume na sheria ya manunuzi kwa kisingizio cha kuwa wafanyabiashara hao wamelipwa madeni wanayodai katika miaka ya nyuma ambapo sheria hii ya manunuzi ilikua bado haijaanzishwa, hivyo basi hawakuweza kuonekana katika mfumo.

Hata hivyo kamati imeomba kupatiwa uthibitisho wa madeni hayo iwapo ni kweli kulikuwa na madeni kwa wafanyabiashara kabla ya kuanzishwa sheria nambari 11 ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma ya mwaka 2016 Kamati imeshidwa kupatiwa vielelezo hivyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya Laac inaziomba taasisi za Serikali kuipatia majibu sahihi na ya uhakikia Kamati hii kwani haitosita kuchukua hatua kwa mtu au taasisi ambayo itakayotoa majibu ambayo sio sahihi kwa mujibu wa kanuni ya Baraza la Wawakilishi toleo la 2020

Aidha Kamati inashauri Baraza la Mji kufuata sheria kwa kufanya malipo kwa watoa huduma mbalimbali ambao tayari wameshasajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi ili Serikali iweze kupata mapato yake.

**5.1.6.3 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 91,315,235**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 91,315,235 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Baraza la Mji Mkoani lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Umma Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za ya mwaka 2016.

**Majibu ya Baraza la Mji Mkoani**

Baraza la Mji Mkoani limekuwa likiambatanisha vielelezo vyote muhimu vinavyotakiwa kuwekwa katika hati za malipo kila malipo yanapofanyika.

Kutokuonekana kwa vielelezo vilivyotaja katika hoja hii kulitokana na sababu kuwa katika robo ya mwisho ya mwaka wa fedha wa 2020-2021, hali iliyopelekea Baraza kushindwa kukamilisha kuweka baadhi ya vielelezo wakati ukaguzi ulipofanyika.

Baraza la Mji Mkoani kwa sasa linahakikisha vielelezo vyote vinavyotakiwa vinapatika kwa wakati kwa kila ukaguzi unapofanyika.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imebaini kuwa dosari hii inajitokeza mara kadhaa katika taasisi mbalimbali za Serikali hasa Mabaraza ya Miji na halmashauri kwa kisingizio cha kuwa vielelezo hivyo vinakosekana kutokana na baadhi ya taasisi za ukaguzi kama vile ZAECA huwa wanavichukua na kushidwa kuvirudisha kwa wakati hivyo wakati mdhibiti anapopita kufanya ukaguzi wake vielelezo hivyo huwa vinakosekana kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi.

Hata hivyo Kamati imeshidwa kulithibitisha hilo kwa vile imeomba kupatiwa barua na hati za makubaliano zinazoenesha kupeana vielelezo hivyo kwa ajili ya ukaguzi na taasisi hizo Kamati imeshidwa kupatiwa nyaraka hizo.

**Mapendekezo ya Kamati.**

Kamati ya laac haipingani na kaguzi zinazofanywa na taasisi mbalimbali ambazo zinafanya kazi yake kwa mujibu ya sheria ila ni vyema wanapoenda kufanya ukaguzi kuzingatia utoaji wa barua wa kuhitaji kufanya ukaguzi huo kwa taasisi husika, vile vile ikiwa kuna vielelezo ambavyo watahitaji kuondoka navyo basi ni vyema kupeana kwa makabidhiano ya maandishi ili vielelezo hivyo viweze kutambulikana idadi yake na muhusika aliyekabidhiwa ili vikihitajika kwa taasisi nyengine ya ukaguzi viweze kupatikana kwa wakati ili dosari hii isiweze kujitokeza tena kwa kisingizio hicho.

**5.1.6.4 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 38,387,935.**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 38,387,935 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Baraza la Mji Mkoani lakini hati za malipo hayo pamoja na vielelezo vyake hazikupatikana kwa ukaguzi jambo ambalo linapelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na

kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Baraza la Mji Mkoani**

Baraza la Mji Mkoani limekuwa likiziweka katika mafaili maalum hati zote za malipo yanayofanyika kwa kila siku.

Ni kweli wakati ukaguzi unafanyika baadhi ya hati za malipo zilikosekana kutokana na kuparaganyika kwa hati hizo kulikosababishwa na kaguzi mbali mbali zilizokuwa zikifanyika kwa mwaka huo na kupekekea baadhi ya hati hizo kuwepo ofisi nyengine za kiukaguzi.

Hivyo kwa sasa hati hizo zimetafutwa na kuwekwa katika mafaili husika

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Baraza la mji mkoani limekiri kuwepo kwa dosari hii hata hivyo Kamati ya laac imebaini Baraza la Mji Mkoani halikuwa na umakini katika utunzaji  wa kumbukumbu jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa hati hizo.

Kamati ya inalishauri Baraza la Mji Mkoani kuwa makini katika utunzaji wa kumbumbuku hasa nyaraka za kifedha ili kuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi mbalimbali yanayofanywa na Baraza hilo.

**5.1.6.5 Kutokuwepo kwa uwiyano wa kumbu kumbu za kifedha.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa uwiyano wa kumbu kumbu za kifedha baina ya taarifa za benki 'Bank Statement" na taarifa za mwisho wa mwaka"Final Account". Kufanya hivyo kunapelekea taarifa za ufungaji wa mahesabu kutokuwa sahihi ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016. Mchanganuo wa taarifa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Baraza la Mji Mkoani**

Baraza la Mji Mkoani limekuwa likifuata vigezo vyote vinavyohitajika wakati wa kuandaa hesabu za mwisho wa mwaka, ikwemo uwiyano wa taarifa za kibenki pamoja na zile za ripoti za hesabu za mwisho wa mwaka.

Kuwepo kwa utofauti wa hesabu katika taarifa za kibenki na zile za ripoti za hesabu za mwisho wa mwaka kulitokana na makosa ya kibinadamu ambapo kuna matumizi ya fedha za miradi hazikujumuishwa katika ripoti za fedha za mwaka, jambo lilipelekea uwepo wa utafauti huo.

Baraza la Mji Mkoani kwa sasa limeongeza umakini na linahakikisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka linawiana na taarifa za kibenki.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imebaini kuwa Baraza la Mji Mkoani limeshidwa kufanya usuluhishi wa taarifa za kifedha mara kwa mara baina ya taarifa za kibenki na taarifa za mwaka (final Account) vile vile uwezo wa watendaji katika kufunga mahesabu hayo pamoja na kutumia mifumo unaonekana ni mdogo jambo ambalo limepelekea Kamati kubaini dosari kadhaakatika taarifa za mwisho wa mwaka ya taasisi **"Financial** Statement' ikiwemo kutofafanuliwa kwa vifungu "note" ya 10, 12, 18, 11, 13

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuwa makini katika kufunga hesabu zake mwisho wa mwaka kwa mujibu wa miongozo kitaifa na Kimataifa ya IPSAS, aidha Kamati inaiomba Ofisi ya Rais fedha na Mipango kuendelea kutoa mafunzo kwa wahasibu kutoka taasisi mbalimbali ili kuwajengea uwezo juu ya namna ya ufungaji mzuri wa mahesabu wa mwisho wa mwaka kulingana na viwango "standand" inavyohitaji

**5.1.6.6 Kutokusajiliwa kwa baadhi ya vyanzo vya mapato**.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa baadhi ya vyanzo vya mapato ambavyo havijasajiliwa na Baraza kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato vikiwemo mahoteli, nyumba za kulala wageni, gereji, viwanda vya ufundi seremala na maduka ya ushonaji wa nguo. Kufanya hivyo kunapelekea kulikosesha Baraza mapato yatokanayo na vyanzo hivyo, aidha ni kwenda kinyume na Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Nam.7 ya mwaka 2014 kifungu nambari 94.

**Majubu ya Baraza la Mji Mkoani**

Baraza la Mji Mkoani limekuwa kila mwaka likiibua vianzio vipya vya mapato na kuviwasilisha katika mamlaka husika kwa ajili ya kusajiliwa.

Ni kweli katika ukaguzi uliofanyika ilibainika kuwepo kwa baadhi ya vianzio ambavyo havijasajiliwa kama vianzio rasmi vya mapato kama vile mahoteli ya kitalii na nyumba za kulala wageni.

Hali hii ilisababishwa na changamoto ya kuingiliana kwa taratibu za kutambua kama vianzio vinavyosimamiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa na mamlaka nyengine zinazosimamia masuala ya utalii.

Licha ya kuwepo kwa changamoto hii Baraza la Mji Mkoani limekuwa likiwaita katika vikao mbali mbali wamiliki wa mahoteli hayo pamoja na nyumba za kulala wageni kuwaelimisha juu ya ulazima wa kukata leseni za kuendeshea biashara zao.

Ama kuhusu viwanda vya ufundi useremala, gereji na maduka ya kushona nguo. Baraza la Mji Mkoani lilikuwa linawakatisha leseni za kuendeshea biashara wamiliki wa biashara kama kanuni ya huduma inavyoelekeza.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri uongozi wa Wizara kukaa pamoja na Mamlaka nyengine za Ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kulipatia ufumbuzi wa jambo hilo ili kila Mamlaka ipate haki yake hasa ukizingatia athari za kimazingira na mabadiliko ya tabia nchi zinazotakana uwekezaji unaofanywa katika maeneo ya wananchi unatakiwa kufidiwa kwa kurudisha kiasi cha mapato ili shughuli nyengine za kukarabati miundo mbinu na utunzaji wa mazingira zifanyike katika maeneo hayo

Aidha Kamati inashauri Baraza la Mji Mkoani wakati wa ukaguzi kutoa vielelezo vyote vinavyohitajika wakati wa kujibu hoja za mdhibiti ili kuepusha mdhibiti kutoa dosari ambazo hazipo katika Baraza la Mji Mkoani.

**5.1.6.7 Ukusanyaji wa mapato kinyume na makadirio.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Mji Mkoani hukusanya mapato kupitia vyanzo mbali mbali lakini ukusanyaji wa mapato hayo hufanyika kinyume na makadirio yaliyowekwa, aidha imebainka kutokuwepo kwa makadirio kwa baadhi ya vianzio vya mapato, ukadiriaji mdogo kwa baadhi ya vianzio, pamoja na kutokusanya mapato kwa baadhi ya vianzio kama ilivyopangwa.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa mapato ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(1) (2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majubu ya Baraza la Mji Mkoani**

Ni kweli katika ukaguzi ulifanyika imebainika kuwepo na changamoto ya ukusanyaji wa mapato kinyume na makadirio na kuwepo na ukadiriaji mdogo wa mapato kwa baadhi ya vianzio vya mapato vinavyosimamiwa na Baraza la Mji Mkoani.

Hii imetokana na Baraza la Mji Mkoani kwa wakati huo kutokuwepo kwa taarifa sahihi zinao onesha uhalisia wa idadi ya wafanyabiashara na biashara wanazoziendesha, hivyo kufanya makadirio ya mwaka kwa kukisia tu.

Baraza la Mji Mkoani ililifanyia kazi suala hili na kwa sasa linafanya makadirio ya mapato kwa usahihi, kwa kuwepo na idadi halisi ya wafanyabiashara na biashara wanazozifanya.

Jambo lililosaidia kuwepo kwa makusanya yanayoendana na uhalisia.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja inaungana na hoja ya mkaguzi kwani ni kweli kuna vyanzo vilikusanya zaidi ya mara mbili ya makisio yaliyopangwa kama vile ada ya matangazo, mapato mengineyo na baadhi ya vianzio vilikusanya chini ya makadario na vyengine havikukusanya kabisa, Kamati ya Laac inashauri Baraza la Mji Wete kuwa na mfumo sahihi ya kujua vyanzo vyote vya makusanyo katika maeneo ya Baraza la Mji na kuweka matarajio yanayolingana na ukusanyaji wa vyanzo hivyo kwa mwaka wa fedha uliopita.

### 5.1.7 BARAZA LA MJI WETE

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Mji Wete ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 395,500,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufi kia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 479,829,238 zilikusanywa na Baraza la Mji Wete sawa na asilimia 121.32 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Mji Wete lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 7,025,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 80,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufi kia tarehe 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 6,865,435,113 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 97.73 ya makadirio na shilingi 61,301,099 zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 69.5 ya makadirio

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imeshidwa kuijadili kwa kina taarifa ya mapato na matuzi kwa vile ilikua na dosari kadhaa kama vile taarifa hiyo kutokuwa na ufafanuzi wa vifungu "note" katika mwaka uliopita hivyo Kamati kushidwa kupima ufanisi wa utendaji kazi wa Baraza kwa kuweza kufanya mlinganisho wa vifungu vya mapato na matumizi kwa mwaka 2019/2020 na 2020/2021

Kamati inashauri Baraza kufunga hesabu za mwisho wa mwaka kwa kufuata viwango vya kitaifa na Kimataifa ili taarifa hiyo iweze kutoa sura halisi na sahihi.

#### 5.1.7.1 Kutokufikiwa kwa ufanisi wa utekelezaji wa miradi yamaendeleo

Baraza la Mji Mkoani limekusanya jumla ya shilingi 393,793,110 sawa na asilimia

105.09 ya makadirio kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni,2021 ambapo kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 63,323,862 zilitumika kwa ajili ya kazi za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 16.08 ya makusanyo halisi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba fedha zilizotumika kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo pamoja na uwezeshwaji wa wajasiriamali hazikuweza kufikia kiwango halisi kilichotakiwa, kwa mujibu wa utaratibu na agizo lililotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa ziara za kutembelea miradi ya maendeleo katika Halmashauri na Mabaraza ya Miji ni kwamba makusanyo yanapaswa yatumike kwa shughuli za miradi ya maendeleo kwa asilimia 30 na uwezeshaji wa wajasiria mali,vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa asilimia 10 jambo ambalo ukaguzi umebaini matumizi ya miradi ya maendeleo yamefanyika kwa asilimia 16.08 ya makusanyo halisi na hakukubainika matumizi yoyote yaliyofanyika kwa uwezeshaji wa wajasiria mali,vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa asilimia 10.

Aidha, ukaguzi umebaini matumizi ya asilimia 83.92 yametumika kwa huduma za uendeshaji wa Baraza jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

**Majibu ya Baraza la Mji Wete**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Baraza la Mji Wete lilitumia jumla ya Tsh 61,555,695 kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 76 ya makadirio ya matumizi ya miradi ya maendeleo amabayo ni Tsh 80,000,000.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kuchunguza hoja hii Baraza la Mji wete limeshidwa kutoa majibu sahihi ya hoja hii kwa vile Baraza hilo limeweza kukusanya mapato yake ya ndani kwa zaidi ya asilimia 100% lakini agizo la Mhe Rais halikuweza kutekelezwa ipasavyo kwa

visingizio mbalimbali vikiwemo agizo hilo kutolewa katikati ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2020/2021 ambapo Mhe. Rais alipoingia madarakani.

Kamati ya Laac haikuridhika na Majibu hayo kwa vile uwezo wa kutekeleza agizo hilo ulikuwepo licha ya kuwa limetolewa katikati ya utekelezaji wa Bajeti. aidha awamu iliyopita ya Mh. Dk Ali Mohd Shein ilikuwa inasisitiza juu ya Mabaraza ya Miji kuacha kutumia fedha nyingi katika shughuli za uendeshaji wa ofisi badala yake wajikite zaidi katika kutekeleza miradi ya jamii na kusaidia makundi maalum ya vijana,wanawake, walemavu na wajasiriamali mbalimbali hivyo maelekezo hayo sio mapya ila hayakuekwa katika mazingatio na Baraza hili.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya Laac inalishauri Baraza kuwa makini katika utekelezaji wa maagizo yanatolewa na viongozi wakuu wa nchi ambayo yanalenga kutoa huduma bora kwa jamii. Aidha Kamati inasisitiza juu ya utekelezaji wa Agizo la Mhe Rais katika Bajeti zijazo juu ya utoaji wa fedha kwa uwezeshaji wa wajasiriamali, vijana,wanawake na watu wenye ulemavu kwa asilimia 10 na Asilimia 30 kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili lengo kuanzishwa Mabaraza ya Miji na Manispaa liweze kufikiwa.

**5.1.7.2 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 37,020,895.**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 37,020,895 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Baraza la Mji Wete lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo, Kiambatisho Nambari 1 Kinahusika. Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Baraza la Mji Wete**

Nikweli kwamba wakati wa ukaguzi wa hesabu za mwaka 2020/2021 jumla ya malipo ya kiasi nilichokitaja hapo juu yalikosa vielelezo.

Hii ilisababishwa na baadhi ya vielelezo kutokufunganishwa katika nyaraka husika na baadhi yao kufunganishwa katika nyaraka nyengine.

Ofisi ya Baraza la Mji Wete imefanya juhudi ya kuweka vielelezo hivyo sehemu husika na kwa sasa baadhi ya vielelezo hivyo vipo tayari katika sehemu husika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika uchunguzi wa hoja hii Kamati haijaridhishwa na majibu yaliyotelewa na Baraza la Mji Wete hata hivyo hadi Kamati ilipopita kufanya kazi yake kupitia hoja za Mdhibiti bado kulikuwa na baadhi ya hati za malipo zenye vielelezo pungufu.

Kamati inalishauri Baraza la Mji Wete kuwa na Mfumo mzuri wa utunzaji wa taarifa za kifedha ili zinapohitajika kwa ajili ya ukaguzi ziweze kupatikana kwa wakati, aidha kukosekana vielelezo hivyo kunatia shaka juu ya uwazi na uwajibikaji wa fedha za umma

**5.1.7.3 Ukiukwaji wa taratibu za malipo ya kifuta jasho shilingi 3,000,000.**

Baraza la Mji Wete lina kawaida ya kulipana malipo maalum kwa ajili ya kifuta jasho kwa Madiwani waliomaliza muda wa utumishi katika Baraza la Mji Wete. Ukaguzi umebaini uwepo wa ukiukwaji wa taratibu za malipo kwani imebainika Mkurugenzi wa Baraza la Mji Wete ameingizwa katika orodha ya malipo na amelipwa kwa mujibu wa hati namba 26/8 ya tarehe 11 Agosti 2020 kwa hundi namba 670381 yenye

thamani ya shilingi 3,000,000 kwa ajili ya kifuta jasho jambo ambalo haikuwa stahiki yake kwani Mkurugenzi huyo hakuwa ni miongoni mwa madiwani waliomaliza muda.

Kujitokeza kwa malipo kwa mtumishi ambae hastahiki kufanyiwa malipo hayo kunapelekea viashiria vya upotevu wa fedha za umma, matumizi mabaya ya madaraka na ukiukwaji wa taratibu, kanuni na sheria za utumishi wa umma. Ukaguzi unapendekeza uongozi wa Baraza la Mji Wete kuchukuwa hatua stahiki ikiwemo kutoa maelezo yanayopelekea kupatikana kwa uhalali wa malipo hayo au fedha hiyo kurejeshwa kwa ajili ya matumizi ya Baraza la Mji Wete

**Majibu ya Baraza la Mji Wete**

Ni kweli malipo ya kifuta jasho yamelipwa kwa katibu wa baraza la madiwani, hata hivyo, ofisi inapokea ushauri unaohusu malipo haya kwa maslahi ya taifa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati ya Laac imesikitishwa na kadhia hii kwa vile Mkuu wa Taasisi ambae ni Mkurugenzi wa Baraza la Mji Wete ndie amekeuka taratibu, kanuni za sheria za utumishi wa ummah, hata hivyo kamati wakati inaendelea na majukumu yake katika Baraza hilo imebaini kuwa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na uongozi wa Baraza la Mji Wete kama ilivyopendekezwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inamshauri Mkurugenzi huyo kufanyakazi kwa uadilifu, kufuata sheria miongozo,  na kanuni mbalimbali zinazotumika katika uendeshaji wa tasisi na kuacha kutumia vibaya madaraka aliyopewa. Aidha Kamati inasisitiza uongozi wa Baraza la

Mji Wete kuchukua hatua stahiki kwa Mkurugenzi huyo kama ilivyoshauriwa na Mdhibiti ikiwemo kurudisha fedha hizo katika akaunti ya Baraza la Mji wete ili zitumike kwa ajili ya matumizi ya Baraza.

#### 5.1.7.4 Ucheleweshwaji wa fedha za mapato kupelekwa benki shilingi 3,525,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 3,525,000 ni mapato yanayotokana na ada ya leseni za biashara ambayo yamekusanywa lakini fedha hizo zimecheweshwa kupelekwa benki kwa wakati

Kuchelewa kuwasilisha fedha benki kwa wakati kunapelekea viashiria vya upotevu wa mapato, kutumia fedha za mapato kwa matumizi binafsi, kuzikopa au kuzikopesha kinyume na taratibu na sheria ya fedha na uondoshaji wa mali za umma na hatimae kutokujulikana kwa thamani halisi ya fedha iliyokusanywa na iliyowasilishwa benki.

**Majibu ya Baraza la Mji Wete**

Ni kweli kwamba, Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Ofisi ya Baraza la Mji Wete kumekuwepo kwa changamoto ya ucheleweshaji wa fedha za mapato kupelekwa benki

Hii mara nyingi ilisababishwa na mabadiliko ya ndani utaratibu wa ukusanyaji wa mapato pamoja na mabadiliko ya watendaji.

Hata hivyo ofisi imechukua hatua ya kuboresha mfumo wa kutokucheleweshwa kupelekwa kwa fedha hizo benki na kwasasa tayari mapato yote yanapelekwa benki kwa kutumia mfumo unaotoa control number (ZANMUTUM).

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza la Mji wete limekiri kutokea kwa dosari hii Kamati haikuona haja ya kuendelea na hoja hii, hata hivyo Kamati inalishauri Baraza la Mji Wete kuwa makini katika kutumia mifumo hii kwa kutoa taarifa kwa barua katika uongozi wa Wizara pindi kunapotekea hitilafu ya mfumo ili kuweza kupatiwa ufumbuzi wa haraka na kuepusha kutokea dosari hii ya kuonekana kuchelewesha kupeleka mapato benki bila ya kuwa visibitisho vyovyote vya dharura au kuwepo kwa hitilafu ya mfumo wa kukusanyia mapato.

**5.1.7.5 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na mauzo ya vitabu vya stakabadhi shilingi 6,800,000.**

Baraza la Mji Wete lina kawaida ya kufanya biashara ya kuwauzia masheha vitabu vya stakabadhi kwa ajili ya matumizi ya shughuli mbali mbali za kijamii. Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Mji Wete linawadai masheha mbali mbali madeni ya muda mrefu yenye jumla ya shilingi 6,800,000 kwa ajili ya utoaji wa vitabu vya vyeti vya mazao.

Uwepo wa malimbikizo ya madeni yatokanayo na uuzwaji wa vitabu vya stakabadhi kunapelekea kulikosesha Baraza mapato na hatimae kutokupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Wete kuchukuwa hatua za haraka kukusanya mapato yote yanayodaiwa kwa masheha hao pamoja na kuacha hatua za kuwakopesha vitabu vya mauzo jambo ambalo ni kulikosesha mapato Baraza na kutoa mwanya kwa masheha hao kutumia stakabadhi hizo kama ni sehemu ya kujipatia kipato binafsi kutokana na kununua stakabadhi kwa bei nafuu na kuzitumia

stakabadhi hizo kwa kutoa huduma kwa njia ya fedha na hatimae fedha hizo kuzitumia kwa maslahi binafsi.

**Majibu ya Baraza la Mji Wete**

Ni kweli kwamba, Kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, Ofisi ya Baraza la Mji Wete kulikua na malimbikizo ya madeni ya mapato ya kiasi kilichotajwa hapo juu.

Naomba nikujuulishe kuwa, kiutaratibu vyeti vya mazao vinakabidhiwa kwa Masheha kwa njia ya mkopo ili warudishe fedha baada ya kumalizika kwa vitabu hivyo.

Kwa utaratibu huo wakati mwengine tunashindwa kufahamu ni mda gani kitabu husika kimemalizika lakini ofisi inafatilia kwa karibu sana kumalizika kwa mauzo ya vitabu hivyo. Na kwa changamoto iliotokea baada ya kuona deni hilo ni la muda mrefu, Ofisi ya Baraza la Mji Wete ilichukua hatua ya kuandika barua kwenda kwa Mkuu wa Wilaya ya Wete Pemba ya tarehe 17/03/2021 na kwa sasa deni la vitabu hivyo tayari vimeshalipwa.

**Uchunguzi na Mapendezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza la Mji Wete limekiri kutokea kwa dosari hii na tayari madeni hayo yameshalipwa, Kamati haikuona haja ya Kuendelea na hoja hii na imejikita zaidi kulishauri Baraza la Mji kutafuta namna bora ya kuwauzia waheshimiwa masheha vitabu hivyo kwa bei nafuu zaidi ili kuwaepushia kuwabebesha mzigo wa madeni masheha hao na kulisababishia hasara baraza kwa kutofikia malengo ya makusanyo kwa mwaka husika.

### 5.1.7.6 Ukusanyaji wa mapato kinyume na makadirio.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Mji Wete hukusanya mapato kupitia vyanzo mbali mbali lakini ukusanyaji wa mapato hayo umefanywa kinyume na makadirio yaliyowekwa, aidha imebainka kutokuwepo kwa makadirio kwa baadhi ya vianzio vya mapato, ukadiriaji mdogo kwa baadhi ya vianzio, pamoja na kutokusanya mapato kwa baadhi ya vianzio kama ilivyopangwa. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa mapato, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(1) (2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Ofisi ya Baraza la Mji Wete inaendelea kukusanya mapato kwa mujibu wa sheria na taratibu. Hata hivyo kumekuwa na changamoto za taratibu za ukusanyaji wa makusanyo hayo. Aidha hii imesababishwa na ulipwaji wa madeni ya mapato ya minara na mabadiliko ya utaratibu na viwango vya ukusanyaji.

**Majibu ya Baraza la Mji Wete**

Ofisi ya Baraza la Mji Wete inaendelea kukusanya mapato kwa mujibu wa sheria na taratibu. Hata hivyo kumekuwa na changamoto za taratibu za ukusanyaji wa makusanyo hayo. Aidha hii imesababishwa na ulipwaji wa madeni ya mapato ya minara na mabadiliko ya utaratibu na viwango vya ukusanyaji.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja inaungana na hoja ya mkaguzi kwani ni kweli kuna vyanzo vilikusanya zaidi ya mara mbili ya makisio yaliyopangwa kama vile ada ya matangazo, mapato mengineyo na baadhi ya vianzio vilikusanya chini ya makadario na vyengine havikukusanya kabisa, Kamati ya Laac inashauri Baraza la Mji Wete kuwa

na mfumo sahihi ya  kujua vyanzo vyote vya makusanyo katika maeneo ya Baraza la Mji na kuweka matarajio yanayolingana na ukusanyaji wa vyanzo hivyo kwa mwaka wa fedha uliopita.

**5.1.7.7 Kukosekana kwa vielelezo vya uwasilishaji wa kodi Serikalini shilingi 3,333,815.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa zuio la kodi lenye thamani ya shilingi 3,333,815 linalotokana na makato ya huduma mbali mbali zinazotolewa na Baraza la Mji Wete.

Ukaguzi haukuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo kuwasilishwa katika Mamlaka husika kutokana na kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha mikato hiyo imewasilishwa katika Mamlaka hizo. Kushindwa kuwasilishwa vielelezo hivyo wakati wa ukaguzi kunatia shaka juu ya uhalali wa mikato hiyo ilivyotumika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya kodi. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Wete kuhakikisha inawasilisha uthibitisho na vielelezo vya kuwasilisha malipo hayo Serikalini kwa mujibu wa utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Majibu ya Baraza la Mji Wete**

Nikweli kwamba wakati wa ukaguzi wa hesabu za mwaka 2020/2021, Ofisi ilishindwa kumalizia taratibu za mwisho za malipo ya zuio la kodi kwa kiwango kilichotajwa hapo juu licha ya fedha hizo kutengwa kwa ajili ya malipo hayo.

Hii ilitokana na changamoto za mfumo wa malipo (ifms) ambapo mafungu ya zuio la kodi yalikosa fedha za kukamilisha malipo hayo.

Hata hivyo Ofisi iliwasiliana na Wizara ya fedha na mipango kwa ajili ya kutatua changamoto hio.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza la Wete limekiri kutokea kwa dosari hii Kamati ya laac inashauri uongozi wa Baraza kwa kushirikiana na uongozi wa Wizara kufuatilia fedha hizo ambazo zinaonekana kutolipwa kutoka na tatizo la Mfumo wa (ifms) ili taasisi hizo ziweze kuapatiwa stahiki zao kwa mujibu wa sheria

Vile Kamati ya Laac inaiomba Serikali katika kuboresha mfumo wa ifms unaomilikiwa na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango ili kuweza kutoa taarifa mbalimbali za uingiaji na utoaji wa fedha kwa tasisi za Serikali kwa vile mfumo huu umekua ukilalamikiwa sana na taasisi za Serikali kwa kutochakata vizuri taarifa za kifedha wakati wa ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka.

### 5.8.1 BARAZA LA MJI WILAYA YA KASKAZINI ‘A’ UNGUJA

Ukaguzi wa hesabu katika Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini “A” Unguja kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa kufuata sheria ,kanuni na taratibu za ukaguzi wa mahesabu. Matokeo ya kazi hii yanatokana na ukaguzi wa kumbukumbu za hesabu za shughuli za Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini “A” pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Baraza.

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini “A” Unguja ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 7,632,535,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na shilingi 1,000,900,000 ikiwa ni mapato kutoka katika vyanzo vyake vya ndani.

Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini “A” liliingiziwa jumla ya shilingi 7,272,474,232 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ikiwa sawa na asilimia 95.28 na shilingi 1,002,422,778 ni makusanyo kutoka katika vyanzo vyake vya ndani sawa na asilimia 100.152 ya makadirio.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati haikuweza kupitia taarifa ya mapato na matumizi kwa vile taarifa ya hesabu ya mwaka (Financial Statement) kuwa na mapungufuu kadhaa, Kamati inashauri uongozi wa Baraza kufunga hesabu za mwisho wa mwaka kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya ufungaji wa hesabu hizo ili ziweze kutoa sura halisi na sahihi ya matumizi ya fedha za Serikali kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,813,530,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na mapato yao ya ndani, kati ya hizo shilingi 8,557,395,000 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 256,135,000 kwa matumizi ya maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" liliingiziwa jumla ya shilingi 8,063,543,658.54 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 91.49. Kati ya fedha hizo shilingi 8,023,802,658.54 zilitumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 94 ya makadirio na shilingi 39,741,000 zilitumika kwa matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 16 ya makadirio.

**5.1.8.1 Kutofanyakazi kwa Mfumo Unaotumika Katika zoezi laukusanyaji wa Mapato**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Baraza la Mji Kaskazini "A" lina mfumo maalum unaotumika kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokufanya kazi kwa mfumo huo jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa mapato yatokanayo na kufanyika kwa makusanyo nje ya mfumo na kushindwa kujiridhisha juu ya uhalisia wa kima cha fedha kinachokusanywa kwa njia ya mikono (Manual). Kutofanya kazi kwa mfumo unaotumika kuwekea kumbukumbu halisi za ukasanyaji wa mapato kunaweza kupelekea kujitokeza baadhi ya dosari zifuatazo:-

- Kutopatikanwa kwa uhalisia wa fedha za mapato zinazokusanywa na kuwasilishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka wa

fedha 2020/2021.

- Kutokosekana kwa uhifadhi mzuri wa matumizi ya stakabadhi zinazotolewa kwenye mfumo jambo ambalo litapelekea kujitokeza kwa ugumu wa kufanya ufuluhisho wa miamala ya kifedha.
- Mfumo kutokutoa taarifa sahihi za mapato yaliyokusanywa na yaliyowasilishwa kwa kipindi husika.
- Kutojulikanwa kwa fedha halisi zilizokusanywa kupitia kwenye mfumo huo.
- Kutofanyika kwa uwiano wa fedha zilizorikodiwa kwenye stakabadhi za malipo pamoja na taarifa za kibenki,“bank statement” pamoja na fedhahalisi zilizomo kwenye mfumo.

Ukaguzi unashauri Uongozi kuhakikisha unachukua jitihada za makusudi kuhakikisha inaipatia ufumbuzi wa haraka changamoto hiyo kwa lengo la kupatika kwa tija iliyokusudiwa.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini ‘A’**

Kutopatikana kwa uhalisia wa fedha za mapato zinazokusanywa na kuwasilishwa katika hesabu ya mwisho ya mwaka wa fedha 2020/2021, hii imetokana na:-

i. Mfumo ulikuwa unarusha data (Data redundancy)

ii. Wafanyabiashara walikuwa hawana muamko mzuri wa kulipa kupitia mfumo na walikuwa wakilipia benki moja kwa moja.

iii. Kushindwa kuwasiliana baina ya Mfumo wa mapato na Mfumo wa Benki (Integration failure between MUTUM system and Bank System).

Kufuatia changamoto zilizojitokeza Ofisi ilikuwa ikifanya mawasiliano ya mara kwa mara na Wizara ili kuondoa changamoto hizo. Hivyo, Wizara walizichukuwa na kuzifanyia kazi mwaka uliofita changamo zimepungua kwa kiasi kikubwa.

Mfumo haukuwa na uwezo wa kutengeneza summary ya ripoti ya makusanyo kwa mkusanyaji na maeneo kwa kuzingatia kiwango cha makusanyo.

Mfumo ulikuwa na changamoto nyingi ikiwemo kutoa hisabu zaidi ya mara moja (Duplication), pia mfumo hakuweza kufanya miamala kwa wakati (timely transaction), vilevile mfumo ulishindwa kujiwekea taarifa za hakiba (backup). (Technical errors)

Mfumo ulikuwa na changamoto nyingi ikiwemo kutoa hisabu zaidi ya mara moja (Duplication) vilevile mfumo ulishindwa kujiwekea taarifa za hakiba (backup).

Kutofanyika kwa uwiano wa fedha zilizorikodiwa kwenye stakabadhi za malipo pamoja na taarifa za kibenki, “Bank statement” pamoja na fedha halisi zilizomo kwenye mfumo kwasababu:-

i. Mfumo haukuwa ukitoa taarifa sahihi za ukusanyaji mapato.

ii. Mfumo ulikuwa na changamoto ambayo Control number zinazotolewa zilikuwa hazikubali kufanya malipo benki hali ambayo imepelekea Taasisi kuamua kulipia moja kwa moja kupitia nambari ya Account.

**Uchunguzi wa Kamati.**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini ni kweli kulikuwa na changamoto kadhaa za mfumo wa kukusanyia mapato na kupelekea dosari mbalimbali ikiwemo kutofautiana taarifa za mapato baina mfumo taarifa za benki pamoja na vitabu vya kukusanyia mapato hayo.

Aidha Kamati imebaini kuwa mfumo huo ulikuwa unamilikiwa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango hivyo Baraza hawakuwa na uwezo wa ndani wa kurekebisha dosari hizo hadi wawasiliane na uongozi wa Mamlaka kwa kupata msaada wa kiufundi hali iliyopelekea mfumo huo kutofanyiwa marekebisho ndani ya wakati.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Wizara katika kuekeza mifumo ya Tehama katika Serikali za Mitaa hasa mifumo ya kukusanyia mapato ni vyema kushirikisha Mamlaka hizo katika hatua ya awali ya Mradi hadi kukamilika kwake kwa lengo la kujua mahitaji muhimu ya kuzingatia ndani ya mfumo, kubaini dosari mbalimbali na kuzipatia ufumbuzi kabla ya mfumo kukabidhiwa kwao kwa vile wao ndio watumiaji husika wa mfumo.

Aidha Kamati inashauri Wizara kutoa mafuzo elekezi kwa maafisa Tehama waliopo katika afisi za Mabaraza ya Miji na Halmashauri katika mifumo ya Ukusanyaji mapato kwa lengo la kutatua changamoto zinapojitokeza badala ya kutegemea maafisa Tehama waliopo Wizarani kwenda kutatua changamoto hizo.

### 5.1.8.2 Kukosekana kwa Vielelezo Vinavyohusiana na Maliposhilingi 10,064,896

Ukaguzi umekagua hati mbalimbali zilizotumika kwa ajili ya malipo yaliofanywa na Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini “A” na kubaini uwepo wa baadhi ya hati za malipo zenye thamani ya shilingi 10,064,896 ambazo zina mapungufu ya vielelezo vilivyothibitisha kufanyika kwa malipo hayo.

Kutokuambatanishwa kwa vielelezo sahihi vya malipo kwenye hati za malipo kunaweza kupelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Baraza kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaambatanisha na vielelezo vilivyokamilika ili kuweza kuthibitisha usahihi wa malipo yaliyofanyika. Mchanganuo wa Malipo yenyewe ni kama yanavyoonekana katika jadwali lifuatalo hapo chini:-

*Jadweli Nambari 59 : Malipo yaliyofanyika ambayo yamekosekana vielelezo*

| Hati namba | Alielipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 54/6 ya 25/6/2021 | ZSSF | 8,979,300 | Malipo ya deni la ZSSF |
| 19/7 ya 28/7/2020 | Absa Bank Tanzania Ltd | 1,085,596 | Malipo kwa ajili ya mikato ya mishahara ya wafanyakazi kwamwezi Julai 2020 |
| **Jumla** | | **10,064,896** | |

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini 'A'**

**Malipo yaliyofanyika ambayo yamekosa vielelezo**

| Hati namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo | Majibu ya hoja |
|---|---|---|---|---|
| 54/6 ya 25/06/2021 | ZSSF | 8,979,300 | Malipo ya deni la ZSSF | Vielelezo vimeambatanishwa katika vocha husika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 19/07 ya<br>28/07/2020 | ABSA Bank Tanzania LTD | 1,085,596 | Malipo kwa ajili ya mikato ya mishahara kwa | Vielelezo vimeambatanishwa katika vocha husika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **wafanyakazi kwa mwezi Julai 2020** | |
| **Jumla** | | **10,064,896** | | |

***Uchunguzi ya Kamati***

Baraza limekiri kuwa halikuwa na vielelezo vya malipo ya deni la ZSSF na ajili ya mikato ya mishahara ya wafanyakazi kwa mwezi Julai 2020 katika Benki ya ABSA hata hivyo wamefuatilia vielelezo hivyo katika taasisi husika na tayari vimeshawekwa katika vocha za malipo husika.

Kamati imeamua kuifuta hoja hii kwa vile haikuwa na mashiko kwa vile taasisi hizo zilizolipwa zipo kisheria hivyo mkaguzi alipaswa kwenda kujiridhisha iwapo ni kweli kulifanyika malipo hayo katika taasisi husika.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kujiridhisha ipasavyo katika dosari anazozibaini kwa kufanya uchunguzi wa kina na kufuatilia ipasavyo kabla kuziandika hoja zake katika kitabu.

**5.1.8.3 Kukosekana kwa ufanisi juu ya Utekelezaji wa Miradi yaMaendeleo**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kupitia hati za malipo zinazohusiana na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo iliyopo chini ya usimamizi wa Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "A" na kubaini kwamba jumla ya shilingi 97,980,700 zilikadiriwa kutumika katika kutekeleza miradi hiyo.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni Kukosekana kwa ufanisi juu ya utekelezajiwa miradi ya maendelea kuliko sababishwa na kutokuwepo kwa upunifu wa matumizi ya fedha na usimamizi wa matumizi ya fedha kwa mujibu wa

makadirio ya matumizi hayo, kwani imebainika hadi kufikia tarehe Juni 30 2021 baraza lilitumia jumla ya shilingi 39,577,500 katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 3.65 ya fedha zote za makusanyo jambo ambalo Baraza lilivuka lengo la makusanyo ya shilingi 1,084,340,236. Sawa na asilimia 108 ya makadirio.

Kukosekana kwa mipango imara ya matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo kunakopelekea kushindwa kutekeleza miradi hiyo kama walivyojipangia kunaweza kukwamisha jitihada za Serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi kwa kuwasogezea huduma karibu na maeneo yao. Kutokana na Uwepo wa dosari hiyo Ukaguzi haukuridhika na kiwango cha fedha kilichotengwa na kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Baraza.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Baraza kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kwa wakati na kwa ufanishi hasa ukizingatia fedhainayokusanywa inatosheleza kukidhi utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa.

Mchanganuo wa matumizi ya fedha na utekelezaji wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadual hapo chini:-

**Jadweli Nambari 60**: **Utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya kiwangoUjenzi wa Skuli ya Maandalizi Chaani Kikongeni**

| Jina la mradi | Mahali ulipo mradi | Fedha za makadirio zamradi (Tshs | Fedha halisi iliyotumik a katika |
|---|---|---|---|

| | | ) | **mradi (Tshs)** |
|---|---|---|---|
| | | | |
| Ujenzi wa skuli ya maandalizi | Chaani Kikongeni | 82,937,200 | 21,684,000 |
| Matengenezo ya uzio wa eneola ujenzi wa ofisi ya Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini A | Mto wa Pwani | 6,887,500 | 6,887,500 |
| Matengenezo ya vyoo | Fungu refu | 656,000 | 656,000 |
| Ujenzi wa vyoo soko la mamalishe | Kinyasini | 0 | 3,150,000 |
| Uwekaji wa kifusi njia ya Fungurefu | Fungu refu | 7,500,000 | 7,200,000 |
| **Jumla** | | **97,980,700** | **39,577,500** |

Ujenzi wa Skuli ya Chaani Kikongeni ulianza Mei 2021 kwa fedha ya Serikali kupitia Kamati ya Usimamizi wa udhibiti wa ujenzi (DCU) iliyopitishwa na kushirikiana na nguvu za Mheshimiwa Diwani, kamati ya sheha na wananchi ambapo ujenzi huo ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 82,937,200.

Namna ya utekelezaji wa ujenzi huo ulikua kama ifuatavyo:-

- Awamu ya kwanza ya ujenzi ulihusisha madarasa 4, ofisi mbili (2), ghala na matundu 6 ya vyoo, kushindilia kwa fusi, ujenzi wa kuta kozi 5, nguzo, ukanda wa kati, kuta kozi sita na ukanda wa juu ambapo gharama yake ilifikia jumla ya shlingi 21,684,000.

- Katika kutembelea utekelezaji wa mradi huo ukaguzi ulitembelea eneo la skuli

- hiyo na kuikuta iko katika hatua ya kuridhisha kulingana na fedha iliyotumika licha ya kuwa bado haijafikia kuezekwa na kutia sakafu ya chini na kupigwa plasta ya ndani na ya nje

- Ukaguzi pia ulipitia hati za malipo mbalimbali za Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini ‘A’ na kubaini uwepo wa hati ya malipo yenye namba 55/11 ya 15/11/2020 yenye thamani ya shilingi 1,663,000 ambayo yalilipwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa katika ujenzi wa skuli ya maandalizi Chaani Kikongeni kupitia risiti namba 0391 ya 11/11/2020 kutoka kwa Khamis Jumanne Mjaka.

- Katika ufuatiliaji wa taarifa hizo kiukaguzi wakaguzi wameshindwa kujiridhisha na matumizi ya shilingi 20,021,000 yaliotumika kwenye ujenzi

huo kutokana na kukosekanwa kwa vielelezo vilivyohusikana na matumizi hayo kwa ajiliya ukaguzi ambapo imebainika Thamani halisi ya fedha jumla ya shilingi 20,000,000 ziliingizwa katika hatua ya utekelezaji wa mradi huo kutoka Kamatiya kudhibiti ujenzi wa Mipango Miji na vijii (DCU).

- Awamu ya pili ya mradi itahusisha ujenzi wa gable, nguzo ziliopo kwenye koridoo, uchimbaji na ujengaji wa mashimo ya vyoo pamoja na ujenzi wapaa kwa gharama za shilingi 32,602,100.

Ukaguzi ulifanya mahojiano na watendaji mbalimbali wa Baraza hilo na kubaini kwamba jumla ya 30,000,000 ziliingizwa kutoka DCU kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutumika kwa fedha hizo kinyume na malengo yaliokusudiwa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na badala yake fedha hizo zilitumika kwa ajili ya ulipwaji wa mishahara kwa wafanyakazi wa Baraza alioajiriwa kwa Mkataba.

Hali ambayo ilipelekea kutokutekelezeka kwa hatua ya mradi huo kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa vielelezo halisi vya matumizi yaliyofanyika kutokana na uhaulishaji wa fedha hizo kutumika kinyume na miongozo.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini 'A'**

Katika mwaka 2020/2021 Baraza la Mji Kaskazini "A" lilitumia 39,577,500 katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 3.65 ya fedha zote za makusanyo jambo ambalo limepekea kukusekana ufanisi katika Miradi, hii imesababishwa na:-

- Upungufu wa fedha uliosababishwa na kupokea fungu dogo la ruzuku

(Ceiling) kutoka Serikali Kuu. Jambo hili limesababisha kutotekelezwa kwa baadhi ya miradi na kupelekea fedha kutumika kutoa huduma katika Afya, Elimu na Kilimo.

- Kuwepo kwa madeni katika Taasisi kama vile madeni ya fidia waliopisha ujenzi wa Soko la Kinyasini.

Ujenzi wa Skuli ya maandalizi Chaani Kikongeni Kukosekana kwa vielelezo vya malipo ya shilingi 20,021,000

- Vielelezo vya malipo vipo katika vocha husika.

Kutumika Shilingi 30,000,000 kinyume na malengo yaliyokusudiwa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na badala kutumika kulipia mishahara wafanyakazi wa Mkataba

- Jumla ya Shilingi 30,000,000 zilitumika kinyume na malengo yaliyokusidiwa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na badala yake kutumika kulipia mishahara ya wafanyakazi wa Mkataba kwasababu katika kipindi hicho Ofisi ilikuwa na uhaba wa fedha.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa ni kweli Baraza limetenga fedha chache kwa ajili ya miradi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kinyume na miongozo ya Serikali ya kutenga asilimia 30 ya mapato ya ndani kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo.

Aidha Kamati imesikitishwa na utekelezaji mdogo wa kiasi kilichotegwa kwa ajili ya shughuli za Mirada ambapo jumla ya Tzs 97,980,700 zimetengwa na kutumika 39,577,500 sawa na asilimia 40 kwa sababu zisizokuwa na msingi.

Aidha Kamati imebaini ni kweli matumizi ya fedha za DCU yenye Jumla ya Tsh 30,000,000 zilitumika kinyume na malengo yaliyokusidiwa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na badala yake kutumika kulipia mishahara ya wafanyakazi wa Mkataba bila ya uhaulishaji na kupata ridhaa kwa Baraza la Madiwani.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri Baraza kutenga asilimia 30 ya fedha za makusanyo ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kutii agizo la Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar wakati alipofanya ziara ya kutembelea Mabaraza ya Miji na Halmashauri.

Aidha Kamati inalishauri Baraza kutekeleza ipasavyo bajeti iliyotengwa ya miradi ya maendeleo kama ilivyopangwa kwa lengo la kupatika tija iliyokusudiwa ya kuanzishwa kwa Mabaraza na Halmashauri katika kuisaidia Serikali kutoa huduma bora kwa wananchi.

Vile vile Kamati inalishauri Baraza kutokwenda kinyume na makubaliano ya fedha za DCU pamoja na Fedha za mapato yatokanayo na minara zinazotolewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za miradi ya maendeleo katika jamiii kwa kuzihaulisha na kuzitumia katika shughuli za uendeshaji wa Afisi kinyume na malengo yaliyokusudiwa ya matumizi ya fedha hizo.

### 5.1.9 BARAZA LA MJI WILAYA YA KASKAZINI “B”

Ukaguzi wa hesabu katika Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini “B” kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za ukaguzi wa hesabu. Matokeo ya ukaguzi huo yanatokana na kukagua kumbukumbu za hesabu za shughuli za Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini “B” pamoja na mfumo wa tathmini ya udhibiti wa ndani ambao unahitaji uangalifu wa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini “B”.

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Mji Kaskazini ‘B’ kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 2,285,050,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 1,089,124,405.15 zilikusanywa na Baraza sawa na asilimia 47.66 ya makadirio.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini “B”**

Kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021 katika Baraza unatokana na sababu nyingi miongoni nazo ni kama ifuatavyo:-

a) Athari za mabadiliko ya kanuni ya Utoaji wa Huduma katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa hususan katika eneo la leseni za biashara
b) Kutopatiwa mgao stahiki wa rasilimali ya mchanga na mgao wa leseni za vileo kwa wakati kutoka Serikalini
c) Kutolipwa kwa wakati ada ya minara na tozo za matangazo kutoka kwa makampuni hususan makampuni ya mawasiliano (Zanzibar Telecom Plc , Viettel, Mic Tanzania, Vodacom)
d) Kupungua kwa mapato yatokanayo na kushusha na kuhifdhi wanyama katika eneo la Muanda, kwani eneo la bandari limekuwa ni sehemu ya

Wilaya ya Kaskazini A na uzio wa kuhifadhia wanyama "caranteen" umekuwa chini ya Idara ya Maendeleo ya Mifugo Zanzibar.

e) Ushindani mkubwa uliopo katika machinjio ya wanyama ya watu binafsi kwa Chinjio la Muanda, pamoja na kususiwa na wachinjaji kwa Chinjio la Mahonda kufuatia kutokuelewana katika umiliki kwa Chinjio hilo.

Vile vile kwa namna moja au nyengine, utalii kutoimarika ipasavyo kutokana na mdororo wa kiuchumi uliosababishwa na covid umechangia kuathiri kiasi fulani biashara za vinyango katika eneo la Kiwengwa na kupelekea kupungua idadi ya usajili wa Leseni za biashara.

**(kiambatanisho nambari 1 kinahusika)**

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini 'B' kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 9,042,433,818. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 8,714,278,714 zilikadiriwa kutumika kwa kazi za kawaida na shilingi 210,014,000 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 6,749,642,732.25 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa asilimia 77.45 ya makadirio, na shilingi 55,496,670 zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 26.43 ya makadirio.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B"**

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Baraza la Mji lilikadiria kutumia kiasi cha Tzs. 9,042,433,818.00 kwa ajili ya malipo ya mishahara na stahiki za watumishi, utekelezaji wa miradi, uendeshaji na utawala shughuli za Baraza pamoja na fedha za utekelezaji za Mfuko wa Mbunge wa Jimbo (CDCF).

Hadi tarehe 30 Juni, 2021 Baraza la Mji limetumia kiasi cha Tzs. 7,026,684,606.25 sawa na asilimia 77.71% ya makadirio, ikiwa ni fedha za:-

i) Mishahara Tzs. 5,981,515,783.00 sawa na asilimia 98.90% ya lengo.
ii) Matumizi ya sekta ya ugatuzi (Elimu, Afya na Kilimo) Tzs. 222,452,588.00 sawa na asilimia 27.07 ya lengo la matumizi.
iii) Matumizi ya Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Baraza ni Tzs. 545,674,361.25 sawa na asilimia 23.88% ya lengo.
iv) Utekelezaji wa miradi ya Wadi na uzalishaji ni Tzs. 158,900,766.00 sawa na asilimia 6.95% ya lengo.
v) Matumizi ya fedha za Basket Fund na Fedha za Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo (CDCF) Tzs. 118,141,108.00 sawa na asilimia 100%

(kiambatanisho nambari 2 kinahusika)

**5.1.9.1 Kutofanyakazi kwa mfumo wa ukusanyaji mapato**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa Mfumo wa kukusanyia mapato unaotumiwa na Baraza la Mji Kaskazini 'B' katika ukusanyaji wa mapato na uwekaji wa kumbu kumbu. Dosari iliyobainika ni kutokufanyakazi kwa Mfumo huo hali inayoweza kupelekea kuwepo kwa tofauti ya kumbu kumbu zinazohusiana na mapato baina ya Mfumo, Taarifa za Benki na Taarifa za mapato kuptia vitabu vya mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kwamba Mfumo wa Ukusanyaji Mapato unafanyakazi kiukamilifu.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B"**

Ni kweli Baraza la Mji ni mtumiaji wa mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za mapato (MUTM) ambao kiuhalisia umeanzishwa na kusimamiwa na (OR) Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Baraza lilikua linatumia mfumo wa (MUTM) ambapo mfumo huu ulifungwa matumizi yake na kuanza kutumika mfumo wa MUTM Zan-Malipo unaosimamiwa na Wakala wa Mkonga Zanzibar.

Kutokana na hoja ya Mkaguzi kutaka taarifa za mfumo tuliiomba (OR) Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kutufungulia mfumo ili kupata taarifa na kuziwasilisha kwa Mkaguzi kwa hatua za ukaguzi.

Kuhusu matumizi ya mfumo wa MUTM Zan-Malipo unakabiliwa na changamoto katika uendeshaji zinazojitokeza kutokana na hali ilivyo katika uendeshaji wa mfumo Mkaguzi akajenga hoja ya kutofanya kazi kwa mfumo wa malipo.

Kiuhalisia Baraza halina uwezo wa kufanya marekebisho ya aina yoyote katika mfumo, isipokuwa kuwajuilisha Kitengo cha Tehama Wizarani na kuwasilisha kwa Wakala kufanyia marekebisho yanayohitajika. Dosari zinazojitokeza katika matumizi ya mfumo ni kama ifuatavyo:-

Ankara za malipo "control number" kukataa katika mfumo wa malipo benki

Kujirejearejea kwa ankara za malipo "control number" zaidi ya mara tatu kwa pamoja

Kutotambua na kutotoa risiti kwa baadhi ya malipo yaliyopokelewa benki

Kutotafautiana katika ripoti za mfumo baina ya ripoti ya utengezaji wa ankara "created control number", ankara zilizokataa malipo "unpayable

control number", ankara zilizolipwa "paid control number"

**Uchunguzi wa Kamati.**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini ni kweli kulikuwa na changamoto kadhaa za mfumo wa kukusanyia mapato na kupelekea dosari mbalimbali ikiwemo kutofautiana taarifa za mapato baina mfumo taarifa za benki pamoja na vitabu vya kukusanyia mapato hayo.

Aidha Kamati imebaini kuwa mfumo huo ulikuwa unamilikiwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ hivyo Baraza hawakuwa na uwezo wa ndani wa kurekebisha dosari hizo hadi wawasiliane na uongozi wa Mamlaka kwa kupata msaada wa kiufundi hali iliyopelekea mfumo huo kutofanyiwa marekebisho ndani ya wakati.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inaishauri Wizara katika kuekeza mifumo ya Tehama katika Serikali za Mitaa hasa mifumo ya kukusanyia mapato ni vyema kushirikisha Mamlaka hizo katika hatua ya awali ya Mradi hadi kukamilika kwake kwa lengo la kujua mahitaji muhimu ya kuzingatia ndani ya mfumo, kubaini dosari mbalimbali na kuzipatia ufumbuzi kabla ya mfumo kukabidhiwa kwao kwa vile wao ndio watumiaji husika wa mfumo.

Aidha Kamati inashauri Wizara kutoa mafuzo elekezi kwa maafisa Tehama waliopo katika afisi za Mabaraza ya Miji na Halmashauri katika mifumo ya Ukusanyaji mapato kwa lengo la kutatua changamoto zinapojitokeza badala ya kutegemea maafisa Tehama waliopo Wizarani kwenda kutatua changamoto hizo.

### 5.1.9.2 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 60,353,105

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 60,353,105 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Baraza la Mji Kaskazini ‘B’ lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha sheria ya usimamizi wa fedha za Umma ya Zanzibar Nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 61 : Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Hati Namba | Alielipwa | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 32/7 ya 27/7/2020 | Mkurugenzi Halmashauri | 1,080,000 | Malipo kwa ajili ya ukaguzi wa mali asili |
| 10/8 ya 12/8/2020 | “ | 1,120,000 | Malipo kwa ajili ya kikao cha Mkuu wa Mkoa |
| 23/8 ya 12/8/2020 | “ | 3,660,000 | Malipo kwa ajili ya Sherehe ya Baraza la Eid al Hajji Kitaifa |
| 32/8 ya 12/8/2020 | Mohamed Haji Mtumwa | 2,470,000 | Malipo kwa ajili ya safari kikazi |
| 46 /8 ya 24/8/2020 | Postal bank | 6,946,775 | Malipo ya kwa ajili ya mikato ya wafanyakazi |
| 68/9 ya 7/9/2020 | Mkurugenzi Halmashauri | 1,000,000 | Malipo kwa ajili ya washiriki kwa kazi maalum |
| 71/9 ya 29/9/2020 | “ | 1,882,500 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa kitalu cha miche |
| 75/9 ya 30/9/2020 | “ | 1,350,000 | Malipo kwa ajili ya mafunzo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 79/9 ya 30/9/2020 | " | 1,080,000 | Malipo kwa ajili ya ya ukaguziwa ruti za magari |
| 81/9 ya 30/9/2020 | " | 3,060,000 | Malipo kwa ajili ya ufungaji wahesabu za mwaka |
| 68/9 ya 7/9/2020 | " | 1,000,000 | Malipo kwa washiriki wa kazi maalum ya uhakiki |
| 71/9 ya 29/9/2020 | " | 1,882,500 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa kitalu cha miche |
| 72/9 ya 30/9/2020 | " | 4,480,000 | Malipo kwa ajili ya ukaguzi wa maeneo ya ukusanyaji wa mapato |
| 75/9 ya 30/9/2020 | " | 1,350,000 | Malipo kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo |
| 79/9 ya 30/9/2020 | " | 1,080,000 | Malipo kwa ajili ya ruti za magari |
| 81/9 ya 30/9/2020 | " | 3,060,000 | Malipo kwa ajili ya ufungaji wa hesabu |
| 82/9 ya 30/9/2020 | Unguja Phamacy Limited | 13,035,830 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya usafi |
| PV206PV21000346 ya 9/6/2021 | Ridhwan Ali Kombo | 4,987,500 | Malipo kwa ajili ya kukodi gari |
| PV206PV21000352 ya 15/6/2021 | Salary Suspense | 2,553,000 | Malipo kwa ajili ya safari ya Dar es Salaam kikazi |
| PV206PV21000399 ya 25/6/2021 | Baraza la Mji Kaskazini B | 3,275,000 | Malipo kwa ajili ya tathmini kwa watoa huduma za afya |
| | **Jumla** | **60,353,105** | |

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini "B"**

Katika jaduweli nambari 61 katika kitabu cha Mdhibiti kuna hati za malipo zimejirudia na kufanya hoja nambari 5.1.9.2 inayosomeka "Malipo yasiyokuwa

na vielelezo shilingi 60,353,105.00” lakini uhalisia inatakiwa isomeke kuwa ni Tzs. 52,980,605.00 ikiwa ni ziada ya Tzs. 7,372,500.00

Hati za malipo zilizojirudia katika jaduweli ni kama ifuatavyo:-

| **Hati Namba** | **Aliyelipwa** | **Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs)** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| 71/9 ya 29/9/2020 | Mkurugenzi | 1,882,500.00 | |
| 75/9 ya 30/9/2020 | “ | 1,350,000.00 | |
| 79/9 ya 30/9/2020 | “ | 1,080,000.00 | |
| 81/9 ya 30/9/2020 | “ | 3,060,000.00 | |
| | **Jumla** | **7,372,500.00** | |

Ufafanuzi wa kila ya hati ya malipo iliyowekewa hoja na Mdhibiti kwa mwaka wa fedha ulioshia tarehe 30 Juni, 2021 kuwa malipo yasiyokuwa na vielelezo imefafanuliwa katika kiambatanisho nambari 3.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na majibu yaliyotolewa na Baraza Kamati imehoji juu ya kuwepo kwa malipo yasiokuwa na vielelezo yenye jumla ya Tzs.52,980,605.00 ambapo Kamati imeelezwa kuwa kwa kiasi kikubwa vielelezo vilivyokosekana ni mahudhurio ya wahusika walioshiriki katika vikao au kazi maalum.

Pamoja na majibu hayo Kamati imepata hofu juu ya ufanisi na utendaji kazi wa kitengo cha uhasibu kwa kufanya malipo kwa watendaji walihudhuria kwenye vikao au kazi fulani bila ya kuwa na fomu ya mahudhurio inayo halalisha malipo hayo.

## Mapendekezo ya Kamati

Kamati inashauri Baraza kupitia kitengo cha uhasibu kuacha kufanya kazi kwa mazoea badala yake kufuata taratibu za kisheria katika kufanya matumizi mbalimbali ya Baraza ikiwa ni pamoja na kuwa na vielelezo vyote vinavyohusika katika vocha za malipo

## Kiambatanisho nambari 1

**FUNGU 206-RUZUKU**

**RUZUKU YA MSHAHARA**

| MAELEZO | 2020/2021 | | 2019/2020 | |
|---|---|---|---|---|
| | MAKISIO | MAPATO | MAKISIO | MAPATO |
| **MSHAHARA** | 4,769,331,000.00 | 4,944,552,105.00 | 3,940,125,053.00 | 4,188,911,030.00 |
| **POSHO MAALUM** | 194,076,000.00 | 182,772,000.00 | 189,558,717.11 | 183,700,000.00 |
| 13% ZSSF | 854,135,710.00 | 637,154,625.00 | 512,216,256.89 | 543,715,298.00 |
| **JUMLA** | **5,817,542,710.00** | **5,764,478,730.00** | **4,641,900,027.00** | **4,916,326,328.00** |
| **RUZUKU YA MATUMIZI MENGINEYO** | | | | |
| **MAELEZO** | **2020/2021** | | **2019/2020** | |
| | **MAKISIO** | **MAPATO** | **MAKISIO** | **MAPATO** |
| ELIMU | 261,445,000.00 | 110,075,324.11 | 208,084,466.00 | 268,414,510.99 |
| AFYA | 260,879,400.00 | 77,488,196.10 | 367,949,041.00 | 188,952,032.91 |
| KILIMO | 99,375,600.00 | 34,889,067.79 | 47,657,666.00 | 85,075,671.10 |
| MIRADI YA MAENDELEO | 200,000,000.00 | - | 180,142,200.00 | 0.00 |
| **JUMLA** | **821,700,000.00** | **222,452,588.00** | **803,833,373.00** | **542,442,215.00** |
| **JUMLA YA FUNGU LA RUZUKU** | **6,639,242,710.00** | **5,986,931,318.00** | **5,445,733,400.00** | **5,458,768,543.00** |

**FUNGU 206-MAPATO YA NDANI YA BARAZA**

**ADA YA MAUZO YA HUDUMA**

| MAELEZO | 2020/2021 | | 2019/2020 | |
|---|---|---|---|---|
| | MAKISIO | MAPATO | MAKISIO | MAPATO |
| FOMU ZA LESENI | 16,850,000.00 | 210,000.00 | 35,000,000.00 | 24,522,000.00 |
| LESENI ZA BIASHARA | 95,357,000.00 | 120,445,000.00 | 145,000,000.00 | 130,010,500.00 |
| LESENI ZA VILEO | 155,000,000.00 | 67,670,000.00 | 50,000,000.00 | 48,500,000.00 |
| UJENZI | 147,250,000.00 | 46,499,124.00 | 70,000,000.00 | 49,216,000.00 |
| VYETI VYA MAZAO | 7,720,000.00 | 10,823,500.00 | 2,500,000.00 | 1,950,000.00 |
| UKAGUZI WA AFYA | 500,000.00 | 1,524,000.00 | 7,500,000.00 | 13,775,000.00 |
| KODI YA JENGO | 12,600,000.00 | 12,600,000.00 | 12,600,000.00 | 12,600,000.00 |
| KODI YA UKUMBI | 13,650,000.00 | 50,000.00 | 3,000,000.00 | 1,200,000.00 |
| **JUMLA** | **448,927,000.00** | **259,821,624.00** | **325,600,000.00** | **281,773,500.00** |
| **ADA ZA MALIPO YA TOZO** | | | | |
| CHINJIO | 76,150,000.00 | 37,394,500.00 | 224,473,000.00 | 45,993,000.00 |
| RUTI ZA MAGARI | 28,625,000.00 | 100,000.00 | 7,500,000.00 | 6,550,000.00 |
| ZABUNI | 300,000.00 | - | 500,000.00 | 384,000.00 |
| MBOGAMBOGA | 450,000.00 | - | 6,130,373.00 | 2,062,700.00 |
| MINARA NA MABANGO | 476,459,000.00 | 381,512,934.15 | 170,000,000.00 | 131,936,140.00 |
| ADHABU | 20,000,000.00 | 10,187,000.00 | 20,000,000.00 | 8,496,000.00 |
| **JUMLA** | **601,984,000.00** | **429,194,434.15** | **428,603,373.00** | **195,421,840.00** |
| **ADA ZA USAFIRISHAJI WA MALIASILI NA MAZINGIRA.** | | | | |
| MADAGAA | 101,000,000.00 | 15,413,000.00 | 20,000,000.00 | 16,129,011.00 |
| MALI ASILI | 7,340,800.00 | 1,362,700.00 | 36,000,000.00 | 5,383,000.00 |
| MAZINGIRA | 9,398,200.00 | 17,372,500.00 | 30,000,000.00 | 5,493,000.00 |
| MCHANGA | 1,116,400,000.00 | 365,960,147.00 | 1,250,730,000.00 | 584,703,577.05 |

| JUMLA | 1,234,139,000.00 | 400,108,347.00 | 1,336,730,000.00 | 611,708,588.05 |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| **MAREJESHO YA FEDHA** | | | | |

| MAELEZO | 2020/2021 | | 2019/2020 | |
|---|---|---|---|---|
| | MAKISIO | MAPATO | MAKISIO | MAPATO |
| MKOPO ZSSF | - | - | - | 14,194,925.95 |
| UTT INVESTMENT | - | - | - | 94,000,000.00 |
| **JUMLA** | **-** | **-** | **-** | **108,194,925.95** |
| **JUMLA YA MAPATO YA BARAZA** | **2,285,050,000.00** | **1,089,124,405.15** | **2,090,933,373.00** | **1,197,098,854.00** |

**FUNGU-CDCF FUND & BUSKET FUND**

**ADA YA MAUZO YA HUDUMA**

| MAELEZO | 2020/2021 | | 2019/2020 | |
|---|---|---|---|---|
| | MAKISIO | MAPATO | MAKISIO | MAPATO |
| AFYA BUSKET FUND | 30,000,000.00 | 30,000,000.00 | 30,000,000.00 | 30,000,000.00 |
| CATALIST DEVELOPMENT CATALIST | 88,141,108.00 | 88,141,108.00 | - | 66,291,058.95 |
| **JUMLA YA MAPATO** | **118,141,108.00** | **118,141,108.00** | **30,000,000.00** | **96,291,058.95** |
| **206-BARAZA LA MJI KASK. B** | **9,042,433,818.00** | **7,194,196,831.15** | **7,566,666,773.00** | **6,752,158,455.95** |

*Kiambatanisho Nambari 2*

## 206-MSHAHARA

| MAELEZO | 2020/2021 | | 2019/2020 | |
|---|---|---|---|---|
| | MAKISIO | MATUMIZI | MAKISIO | MATUMIZI |
| MSHAHARA (KUDUMU) | 5,817,542,710.00 | 5,764,478,730.00 | 4,641,900,027.00 | 4,916,326,328.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| MSHAHARA (MKATABA) | 230,000,000.00 | 217,037,053.00 | 150,000,000.00 | 149,651,743.38 |
| **JUMLA YA MATUMIZI** | **6,047,542,710.00** | **5,981,515,783.00** | **4,791,900,027.00** | **5,065,978,071.38** |

**MATUMIZI YA UENDESHAJI NA UTAWALA**

| MAELEZO | 2020/2021 | | 2019/2020 | |
|---|---|---|---|---|
| | MAKISIO | MATUMIZI | MAKISIO | MATUMIZI |
| UNUNUZI WA VITENDEA KAZI | 1,499,492,100.00 | 607,548,369.25 | 980,500,000.00 | 679,906,346.16 |
| MATENGENEZO VIFAA | 232,129,000.00 | 97,169,930.00 | 177,000,000.00 | 0.00 |
| HUDUMA ZA JAMII | 309,120,000.00 | 13,731,800.00 | 210,000,000.00 | 180,192,249.00 |
| HUDUMA NYENGINEZO | 105,654,000.00 | 49,676,850.00 | 148,000,000.00 | 32,511,781.52 |
| DENI ZSSF | 0.00 | 0.00 | 5,677,970.33 | 5,677,970.33 |
| **JUMLA** | **2,146,395,100.00** | **768,126,949.25** | **1,521,177,970.33** | **898,288,347.01** |

**UTEKELEZAJI WA MIRADI NA SAMANI**

| MAELEZO | 2020/2021 | | 2019/2020 | |
|---|---|---|---|---|
| | MAKISIO | MATUMIZI | MAKISIO | MATUMIZI |
| UNUNUZI WA SAMANI | 210,014,000.00 | 55,496,670.00 | 460,000,000.00 | 364,154,618.40 |
| UTEKELEZJI WA MIRADI | 520,340,900.00 | 103,404,096.00 | 675,000,000.00 | 185,238,841.35 |
| **JUMLA** | **730,354,900.00** | **158,900,766.00** | **1,135,000,000.00** | **549,393,459.75** |

**BUSKET FUND & CDCF**

| MAELEZO | 2020/2021 | | 2019/2020 | |
|---|---|---|---|---|
| | MAKISIO | MATUMIZI | MAKISIO | MATUMIZI |
| CONSTITUENCY CATALYST DEVELOPMENT | 88,141,108.00 | 88,141,108.00 | 88,588,775.67 | 305,000,252.67 |
| HEALTH BASKET FUND | 30,000,000.00 | 30,000,000.00 | 30,000,000.00 | 30,000,000.00 |

| JUMLA | 118,141,108.00 | 118,141,108.00 | 118,588,775.67 | 335,000,252.67 |
|---|---|---|---|---|
| JUMLA YA MATUMIZI | 9,042,433,818.00 | 7,026,684,606.25 | 7,566,666,773.00 | 6,848,660,130.81 |

**Kiambatanisho nambari**

| mba | Aliyelipwa | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Maelezo | Kilichokosekana |
|---|---|---|---|---|
| /7/2020 | Mkurugenzi Halmashauri | 1,080,000 | Malipo kwa ajili ya ukaguzi wa mali asili | • Mahudhurio ya washiril<br>• Ripoti ya kazi |
| /8/2020 | " | 1,120,000 | Malipo kwa ajili ya kikao cha Mkuu wa Mkoa | • Risiti ya Malipo |
| /8/2020 | " | 3,660,000 | Malipo kwa ajili ya Sherehe ya Baraza la Eid al Hajji Kitaifa | • Risiti ya Malipo |
| /8/2020 | Mohamed Haji Mtumwa | 2,470,000 | Malipo kwa ajili ya safari kikazi | • Mahudhurio ya washiril<br>• Ripoti ya kazi |
| /8/2020 | Postal bank | 6,946,775 | Malipo ya kwa ajili ya mikato ya wafanyakazi | • Tiketi za safari<br>• ZNZ-Arusha-ZNZ |
| )/2020 | Mkurugenzi Halmashauri | 1,000,000 | Malipo kwa ajili ya washiriki kwa kazi maalum | • Mahudhurio ya washiril<br>• Ripoti ya kazi |
| /9/2020 | " | 1,882,500 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa kitalu cha miche | • Risiti za malipo<br>• |
| /9/2020 | " | 4,480,000 | Malipo kwa ajili ya ukaguzi wa maeneo ya ukusanyaji wa mapato | • Mahudhurio ya washiril<br>• Ripoti ya kazi |
| /9/2020 | " | 1,350,000 | Malipo kwa ajili ya mafunzo | • Mahudhurio ya washiril<br>• Ripoti ya kazi |
| /9/2020 | " | 1,080,000 | Malipo kwa ajili ya ya ukaguziwa ruti za magari | • Mahudhurio ya washiril |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| /9/2020 | “ | 3,060,000 | Malipo kwa ajili ya ufungaji wahesabu za mwaka | • Mahudhurio ya washiril<br>• Ripoti ya kazi |
| /9/2020 | Unguja Phamacy Limited | 13,035,830 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya usafi | • Risiti ya malipo |
| 1000346 1 | Ridhwan Ali Kombo | 4,987,500 | Malipo kwa ajili ya kukodi gari | • Mkataba wa kazi |
| 1000352 21 | Salary Suspense | 2,553,000 | Malipo kwa ajili ya safari ya Dar es Salaam kikazi | • Tiketi za safari<br>• ZNZ-Dar-ZNZ |
| 1000399 21 | Baraza la Mji Kaskazini B | 3,275,000 | Malipo kwa ajili ya tathmini kwa watoa huduma za afya | • Ripoti ya kazi |
| | **Jumla** | **52,980,605** | | |

### 5.1.10 BARAZA LA MJI WILAYA YA KATI UNGUJA

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Mji la Wilaya ya Kati Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 11,391,105,400. Hadi kufi kia tarehe 30, Juni 2021 Baraza limekusanya jumla ya shilingi 12,041,209,801 sawa na asilimia 105.7 ya makadirio.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja halikuwa na maelezo ya moja kwa moja kuhusiana na taarifa za mapato, hivyo, Baraza lilijibu hoja za Kamati kama zilivyotolewa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati ya LAAC imeridhika na majibu mbali mbali yaliyotolewa na Watendaji wa Baraza hili.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 11,352,305,400 kwa ajili ya kazi za kawaida, na shilingi 38,800,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 jumla ya shilingi 11,851,001,756 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 105 ya makadirio na shilingi 184,119,005 kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 475 ya makadirio.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja pia halikuwa na maelezo ya moja kwa moja kuhusiana na taarifa za matumizi, hivyo, Baraza lilijibu hoja za Kamati kama zilivyotolewa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kuifuatilia taarifa hii ya Matumizi, Kamati ya LAAC imebaini kwamba taarifa ya Matumizi iliyoripotiwa na Mdhibiti na MKaguzi Mkuu wa Hesabu za

Serikali haiendani na Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka ya Baraza la Mji la Wilaya ya Kati Unguja.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inawashauri Maafisa Ukaguzi kutoka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Seikali kuwa makini wakati wa kuandika ripoti yake ili kuondosha lawama zisizo na msingi kwa Wakaguliwa.

**5.1.10.1 Hali ya ufanisi katika matumizi ya fedha za makusanyo kwa ajili ya kazi za maendeleo**

Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja limekusanya jumla ya shilingi 1,023,899,651 kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021 ambapo kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 32,653,000 zilitumika kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 3.19 ya makusanyo halisi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba fedha zilizotumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo pamoja na uwezeshwaji wa wajasiriamali hazikuweza kufikia kiwango halisi kinachotakiwa kwa mujibu wa sheria na kwa hali hiyo ufanisi katika matumizi ya fedha za makusanyo hauridhishi na kupelekea kutokupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 7 ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014, ambapo kwa mujibu wa sheria hiyo makusanyo ya Baraza yanapaswa yatumike kwa ajili ya shughuli za maendeleo na uwezeshwaji wa wajasiriamali katika kiwango kisichopungua asilimia 30 ya makusanyo halisi.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Ni kweli Baraza lilifanikiwa kukusanya kwa asilimia 85.32 na tunakiri kutumia kwa shughuli za kawaida kwa sababu tulishindwa kupata fedha za OC kutoka Serikali na ilipelekea baadhi ya shughuli za uendeshaji kukwama na kupelekea

kutumia fedha zilizo kusanywa ili kuhami mambo muhimu kwenye eneo la ugatuzi, baadhi ya shughuli zenyewe ni:

1. Huduma za lishe kwenye skuli za chekechea.
2. Huduma za mafuta kwa uendeshaji kwa vituo vya afya
3. Huduma za ukarabati kwa vyoo vya Skuli n.k.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati imebaini kutokutekelezwa miradi ya maendeleo kama ilivyopangwa katika bajeti husika na badala yake makusanyo hayo kwa kiasi kikubwa yametumika katika shughuli za uendeshaji wa Afisi.

Katika kuifuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC imebaini kwamba uhaulishaji uliofanyika katika baadhi ya vifungu bila ya kufuata utaratibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya Mwaka 2016.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inalishauri Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja wanapofanya uhaulishaji wa vifungu vya matumizi kufuata Sheria, Kanuni, pamoja na miongozo iliyopo.

Vile vile Kamati inashauri uongozi wa Baraza la mji kati kutekeleza kikamilifu Sheria Nambari 7 ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014, ambapo kwa mujibu wa sheria hiyo makusanyo ya Baraza yanapaswa yatumike kwa ajili ya shughuli za maendeleo na uwezeshwaji wa wajasiriamali katika kiwango kisichopungua asilimia 30 ya makusanyo halisi.

**5.1.10.2 Ucheleweshwaji wa mapato kupelekwa Benki shilingi 2,877,300**

Kwa mujibu wa kifungu Nambari 78(1), (2) na (3) cha Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005 kinaeleza kuwa “Makusanyo yote au fedha zozote za Serikali

lazima ziingizwe benki au hazina au ikishindikana angalau mapema iwezekanavyo".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa ucheleweshwaji wa upelekaji wa fedha za makusanyo Benki.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa uwezekano wa kutumika kwa fedha za makusanyo kinyume na malengo yaliyokusudiwa ambapo ni kwenda kinyume na kifungu kama nilivyokinakili hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja kuhakikisha unatumia mfumo katika ukusanyaji wa mapato ili kuepusha uwezekano wa ucheleweshwaji wa mapato kupelekwa Benki. Mchanganuo wa makusanyo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Baraza la Mji kati linakiri kuwepo kwa dosari ya kuchelewa kwa baadhi ya mapato kupelekwa benki, hali hii ilitokana kwa kuwepo mbali kwa benki, hakukuwepo kwa huduma za wakala ili kuwasilisha kwa wakati. Ila hali hii kwa sasa haipo kwa jitihada ya kuweka huduma ya wakala karibu na ofisi, pia uwanzishwaji wa mfumo wa ukusanyaji mapato wa eletroniki (MUTM) ambapo kwa pamoja imesaidia kuondosha tatizo hilo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kuifuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC imebaini kwamba Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja lilikuwa wanatumia mfumo ambao haupo chini Udhibiti wa Serikali za Mitaa hali inayopelekea kushindwa kufanya ufuatiliaji wa haraka pale inapotokezea hitilafu za kimfumo katika shughuli za ukusanyaji wa mapato.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri uongozi Wizara kuwashirikisha kikamilifu Mabaraza ya Miji na Halmashauri pale inapoanzisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kulengo la kuibua changamoto za kiutendaji za mfumo na kuweza kuzitatua kupitia wataalamu wake wa ndani pasi na kutegemea msaada wa kila jambo kutoka Wizara katika kutatua changamoto hizo za mfumo.

Aidha Kamati inashauri uongozi wa Baraza kutoa taarifa mapema pale inapotokezea hitilafu za kimfumo kwa njia ya maandishi ya barua kupitia Wizara na sio kwa njia yam domo kwa vile maandishi ni kielelezo tosha cha kuonesha uwajibakaji wa jambo husika

Wizara kutoa mafunzo kwa maafisa mapato wote pamoja na watenda wa Baraza juu ya matumizi sahihi ya mfumo na kuweza kufanya maboresho pale inapotokezea changamoto ndogo ndogo za kimfumo.

**5.1.10.3 Kutokutayarishwa kwa Usuluhisho wa Kibenki**

Kifungu nambari 162(1) cha Kanuni za fedha za mwaka 2005 kinaeleza kuwa "Bakaa ya kila hesabu ya benki kama inavyoonesha katika taarifa ya benki lazima uionekane usuluhisho wa pamoja na bakaa ya daftari la fedha taslim ukosefu kwa kila mwezi, taarifa ya usuluhisho hiyo itawekwa kwenye kumbukumbu au itarikodiwa katika daftari la fedha taslim.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja linakusanya mapato kupitia vyanzo mbalimbali inavyovimiliki na kuingiza mapato hayo katika Hesabu husika za mapato, dosari iliyobainika ni kutokutayarishwa kwa Usuluhisho wa kibenki ili kuweza kulinganisha Taarifa za Mapato baina Daftari la Mapato la Fedha Taslim na Taarifa za Benki.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kukosekana kwa mlingano wa taarifa za kifedha baina ya Daftari la Mapato la Fedha Taslim na Taarifa ya mapato ya

benki ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu cha Kanuni kama kilivyobainishwa hapo juu.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Ni kweli baraza la mji kati halikuweza kutaarisha taarifa za usuluhishi wa kibenki (benk reconciliation), na sababu kubwa kukosa uwelewa kwa watendaji wetu kwa kipindi hicho lakini kwa sasa baraza linaandaa taarifa zake kikamilifu na taarifa za kuweka usuluhishi wa kibenki kila mwisho wa mwaka tukifunga hesabu na kuandaa financial statement.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa kuwa Uongozi wa Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja wamekiri kuwepo kwa dosari hiyo iliyotokana na kutokuwepo kwa wataalamu wa kuandaa taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu wa kuwapatia mafunzo wahasibu waliopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuwawezesha kuandaa taarifa hizo kwa viwango vinavyohitajika Kitaifa na Kimataifa.

**5.1.10.4 Kutofautiana kwa taarifa za mapato katika baadhi ya vyanzo vya Mapato shilingi 1,379,150**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa tofauti ya taarifa za mapato kwa baadhi ya vyanzo vya mapato yenye jumla ya shilingi 1,379,150 iliyojitokeza baina ya Ripoti za Mapato na Mfumo wa kukusanyia mapato wa Baraza (MUTM) hali ambayo inaweza kupelekea kutokujulikana kwa mapato halisi yaliyokusanywa na Baraza kupitia vyanzo hivyo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria, Kanuni na Miongozo ya ukusanyaji wa mapato iliyopo Kitaifa na Kimataifa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha Sheria, Kanuni na Mongozo ya ukusanyaji mapato iliyopo Kitaifa na Kimataifa inafuatwa kiukamilifu.

Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Hoja ya kutokuwepo Kwa uwiano wa kumbukumbu za Mapato kupitia mfumo, Baraza bado linaendelea kupokea Ushauri wa Mkaguzi lkn pia Baraza halikuona msingi wa kwenda kinyume na miongozo, Kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma, ni Vyema Baraza anapopita CAG akubainishia ili tuendelee kujifunza na kutoendelea na makosa ya namna hii.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kuifuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:

Risiti mmoja kutolewa zaidi ya mara moja kutokana na kuganda kwa mfumo.

Kuwepo kwa uelewa mdogo wa matumizi ya mifumo kwa wahusika/watendaji.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri Wizara kuchukua jitihada za kurekebisha mfumo wa makusanyo wa mapato pindi wanapota taarifa ya kuharibika kwa mfumo kutoka kwa Mabaraza ya Miji na Halmashauri ili kunusuru upotevu wa fedha za Serikali wakati mfumo huo unapokuwa na hitilafu kwa muda mrefu

Aidha, Kamati inaishauri Serikali inapoanzisha mifumo katika ukusanyaji wa mapato ni vyema kuaandaa mafunzo kwa watendaji wanaohusika ili kuepusha upotevu wa fedha za Serikali.

**5.1.10.5 Dosari katika Vitabu vinavyotumika kusanyia Mapato**

Kifungu nambari 67(1) cha kanuni ya fedha ya mwaka 2005 kinawataka "Maafisa wanaokusanya nje kurejesha katika ofisi zao stakabadhi zote za risiti kabla ya kumaliza siku ya kazi ili risiti na makusanyo yao yaweze kuhifadhiwa chini ya ulinzi salama na vitolewe pale tu vinapohitajika kutumika".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja limetoa vitabu vya risiti kuwapa masheha mbali mbali kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato ya ada ya mazao kwa wananchi wanaosafirisha kwenda kuuza mazao yao, ambapo dosari mbali mbali zimebainika kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa Nakla katika vitabu vya mapato (duplicate copy).
- Kutokuandikwa kwa ada ya mazao iliyolipwa katika baadhi ya vishina vya stakabadhi
- Kutokujulikana kwa nambari za baadhi ya vitabu vilivyotumika katika ukusanyaji wa mapato vinavyotaka kwa Masheha.
- Kuchanganywa kwa mapato ya vyanzo tofauti katika Slip moja ya Benki.
- Kutokubainishwa kwa tarehe za makusanyo na tarehe za kuwasilishwa mapato benki.
- Kutokuainishwa nambari za Risiti zilizotumika katika ukusanyaji wa mapato.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa mapato ya Serikali, ambapo ni kwenda kinyume na kifungu cha Kanuni kama kilivyonakiliwa hapo juu.

Kutokuweka kumbukumbu za fedha kwa usahihi kunaweza kupelekea uvujaji wa fedha za umma, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 67(1) na 78 vya Kanuni ya fedha ya mwaka 2005.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Baraza linakiri kuwepo Kwa vitabu vilivyokuwa vinatumika Kwa kuweka usalama wa usafirishaji wa mazao, ambavyo havikuwa na nakala ( Duplicate ) hii inatoka na kuelekeza mawazo yetu kwenye msingi wa kukamilisha huduma zaidi na sio kianzio Cha mapato ya Baraza Kwa vile tulizingatia kurejesha zaidi gharama za uchapishaji wa Vitabu na sio Ada yenye kuzaa mapato ya Baraza.

Hii ilipelekea Baraza kutofanya ufuatiliaji wa Mara Kwa mara na kuweza kujitokea yaliobainika baada ya ukaguzi. Kwa sasa Baraza limefikiria kuandaa utaratibu mzuri wa kuviwekea muongozo mzuri wa kuwatoza kabisa Masheha gharama za uchapishaji Vitabu vya mazao na kutoa muongozo wa tozo/Ada Kwa wale wanaotaka huduma ya Kusafirisha mazao ili kuwe na mfafanano utozaji wa Ada/tozo kwa masheha wote.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya kukiri kuwepo kwa mapungufu ya kiutendaji katika suala hili na tayari hatua za kuboresha dosari hii zimeshachuliwa na Baraza, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali kupitia Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja katika utekelezaji wa majukumu yao kuhakikisha wanafuata masharti ya kifungu nambari 67(1) na 78 vya Kanuni ya fedha ya mwaka 2005 ili kuweka udhibiti wa makusanyo ya mapato kupitia masheha.

**5.1.10.6 Kukosekana kwa vitabu vya mapato kwa ajili ya Ukaguzi**

Kifungu nambari 66(3) na (4) cha Kanuni ya Fedha ya Umma ya mwaka 2005 kinaeleza "66 (3) Maafi sa wanaofanya makusanyo ya nje watarejesha katika ofi si zao stakabadhi zote za risiti kabla ya kufungwa kwa biashara ili risiti na makusanyo yao yaweze kuwekwa chini ya ulinzi salama, afi sa hawezi kuweka stakabadhi hizo kwenye majengo ya kibinafsi kwa usiku mmoja" na kifungu 66(4) kinaeleza kwamba Nyaraka zote za risiti zinazotumika zitafungwa mwisho wa kila siku na afi sa anayezisimamia.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa vitabu vya kukusanyia mapato vilivyopokelewa na kutolewa na Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja kwa ajili ukusanyaji wa mapato lakini baadhi ya vitabu hivyo havikupatikana kwa Ukaguzi ili kuweza kujiridhisha juu ya usahihi na uhalali wa taarifa za

mapato ya Baraza ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha unawasilishwa vitabu vilivyopokelewa na kutumika kwa ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya kukaguliwa. Mchanganuo wa vitabu hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Baraza la Mji Kati, Kwa kuwa imeshaweka utaratibu mzuri kupitia majibu ya Hoja namba 5 tutaendelea na utoaji wa huduma hii na kuendelea Utaratibu tuliojiwekea ili kuondoka Hali hii kutojitokeza tena, Kwa Vile tukiendeleza kuwatoza masheha kabisa ile gharama ya uchapishaji wa vitabu tutakuwa sisi na wao tushamalizana na hakutakuwa na marejesho yatakayochelewa kupitia utoaji wa huduma hii.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza limekiri kuwepo kwa dosari hiyo hata hivyo wameshachukua jitihada ya kulipatia ufumbuzi suala hilo kwa kuamua kuuza vitabu hivyo moja kwa moja kwa masheha ili kuondokana na usumbufu wa ucheleweshaji wa urudishwaji wa vitabu hivyo.

Hata hivyo Kamati inashauri Kusimamia vyema marejesho ya vitabu hivyo ili viweze kutumika kwa ajili ya ukaguzi.

**5.1.10.7 Dosari katika usimamizi na utekelezaji wa mradi wa maendeleo**

Baraza la Mji Wilaya ya Kati kwa mwaka 2020/2021 limetekeleza Mradi wa vijana Hanyegwa Mchana uliohusisha shamba kitalu (Greenhouse) pamoja na Ufugaji wa Kuku na Sungura. Mradi huu wenye jumla ya jumla ya shilingi 114,941,500 umefadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Mtaji wa Taifa (UNCDF) ambapo kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 92,255,143.52 zimetumika na

kuwepo kwa bakaa ya shilingi 40,919,114. Dosari zilizobaikika katika ukaguzi wa Mradi huu ni kama zifuatazo:-

- Kucheleweshwa kuanza kwa utekelezaji wa mradi kwa zaidi ya miezi 7 licha fedha Mradi kutolewa kwa wakati.
- Kutokukamilika kwa mradi kwa wakati pamoja na kuendelea kubakiza fedha za mradi huo katika Hesabu bila kutumika kinyume na mkataba
- Kutokujengwa kwa Banda la Kuku kama ilivyoolekezwa katika Mkataba na badala yake kubainika kufanyika kwa ukarabati wa banda moja ambalo lilikuwepo tangu awali.

Kufanya kwa dosari hizi kunaweza kunapelekea kuwepo kwa upotevu wa fedha za Serikali ambapo ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba pamoja na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Ofisi ya Baraza la Mji Kati inakiri kuchelewa kutekeleza Mradi wa Shamba (Green House), ufugaji wa Sungura na Kuku kutokana na sababu zifuatazo:-

i. Udogo wa eneo la Mradi: eneo lililopendekezwa awali (Umbuji) lilikuwa halitoshelezi na Ofisi ililazimika kutafuta eneo jengine litakalo kidhi vigezo vilivyohitajika, na tukafanikiwa kupata eneo la Hanyegwa Mchana kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi huo.
ii. Ofisi inakiri kutonyoosha maelezo juu ya mabanda yaliyojengwa na yaliyokarabatiwa, majengo yaliyopo kwenye mradi wa kuku na sungura moja lilijengwa na moja lilikarabatiwa. Jengo lilikarabatiwa liliamuliwa na maamuzi ya kikao cha Tenda bodi baada ya kuangalia Gharama za makisio za kujenga upya ni kubwa badala yake Bodi ikaona ni vyema kulikarabati jengo liliopo kwa kupunguza Gharama ambapo kumbukumbu za nyaraka hizo za Bodi zipo ZAECA.

iii. Baraza linaendelea na kupokea ushauri wa Mkaguzi na Kwa sasa miradi yote tukitekeleza tutazingatia maoni na ushauri tuliopatiwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati ya LAAC katika kufuatilia hoja hii imebaini yafuatayo:

- Kukosekana kwa Mikabata wa ujenzi miradi ya vijana.
- Kukosekana kwa "Minutes" za Maamuzi ya vikao vya Baraza la Madiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo iliyotekelezwa kinyume na mkataba wa awali.
- Kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya fedha hizo pamoja ni minutes za vikao vya Bodi ya Zabuni iliyoridhia kufanya mabadiliko ya utekelezaji wa mradi kwa kuelezwa kuwa vielelezo hivyo vimewasilishwa ZAECA kwa ukaguzi.
- Kukosekana kwa ridhaa ya maamuzi ya

**Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro hizo, Kamati ya LAAC inapendekeza yafuatayo:-

1. Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja kuhakikisha linasimamia vyema vipengele vya mikataba na kama kuna mabadiliko yoyote ni vyema kupitia upya mkataba wa awali ili kuufanyia marekebesho.
2. Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja linapofanya mabadiliko yoyote katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo lazima liwashirikishe ipasavyo Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupataa ridhaa.

**5.1.10.8 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 96,571,383**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 96,571,383 zimelipwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja lakini baadhi ya vielelezo vya malipo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo ambapo ni kwenda

kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa hati hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Baraza la Mji Wilaya ya Kati linakiri kujitokeza kwa dosari hio iliyotokana na kuchanganyika kwa mafaaili wakati wa ukarabati wa ofisi, na kwasasa vielelezo vyote vilivyokosekana vimeshafunganishwa na vocha husika kwa ukaguzi, pia tutanaahidi kurekebisha dosari hiyo isitokee tena kipindi kijacho cha fedha.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na Uongozi wa Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja kukubali kuwepo kwa kasoro hizo. Kamati inalishauri Baraza kuanzisha mfumo wa kielektroniki katika masuala ya uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu za Serikali ili kuondokana na upotevu wa vielelezo wakati wa ukaguzi unapofika na hatimae kupelekea kuwepo kwa hoja zisizo na ulazima.

**5.1.10.9 Malipo yaliyokosekana kwa ukaguzi shilingi 16,915,700**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 16,915,700 zimelipwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati Unguja lakini baadhi ya vielelezo vya kukamilisha malipo kupitia hati za malipo havikuambatanishwa na hati husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo kamili ya hati yaliyofanyika.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Baraza la Mji Wilaya ya Kati**

Uongozi wa Baraza la Mji Wilaya ya Kati linakiri kujitokeza kwa dosari hio na kwamba vielelezo vyote vilivyopungua vimeshakamilika na kuwekwa kwenye vocha husika kwa ukaguzi, pia tunaahidi kurekebisha dosari hiyo isitokee tena kipindi kijacho cha fedha.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya kukiri kuwepo kwa dosari hizo katika Baraza kulikosababishwa kutokuwa makini kwa watendaji wa kitengo cha uhasibu, hata hivyo Kati Unguja na hatua zimeshachukuliwa za kurekebisha dosari hiyo.

Kamati inalishauri Baraza kuwa na utaratibu mzuri wa uhifadhi wa nyaraka na kumbumbuku za Serikali ili kuepusha kasoro kama hizi zisijirudie tena katika utekelezaji wa majukumu yao.

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KUSINI UNGUJA

### Taarifa ya Mapato

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 550,612,000 kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 jumla ya shilingi 569,243,480 zilikusanywa sawa na asilimia 103 ya makadirio.

### Uchunguzi wa Kamati

Kamati ya LAAC ilitaka kujua sababu zilizopelekea Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kukusanya mapato zaidi ya asilimia 100, ambapo Watendaji wa Halmashauri walieleza sababu zifuatazo:

- Kuongezeka kwa ufuatiliaji wa mapato
- Kuongezeka kwa vyanzo vipya vya mapato
- Kuvifikia vyanzo vilivyokuwepo

### Taarifa ya Matumizi

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,941,304,334. Kati ya hizo jumla shilingi 4,724,651,764 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 216,652,570 kwaajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufi kia tarehe 30, Juni 2021 jumla ya shilingi 4,113,821,100.12 ziliingizwa na kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 87 ya makadirio na shilingi 113,602,967 ziliingizwa na kutumika kwa matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 52 ya makadirio.

### Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati

Katika kufuatilia taarifa ya matumizi Kamati ya LAAC imebaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini ilihamisha fedha Tshs. 95,000,000.00 kwa ajili ya Kamapuni ya Uvuvi kwa mujibu wa maelezo yao wakati kamati ilipohoji na

kutaka kupatiwa ufafanuzi wa kina juu ya matumizi halisi pamoja na uingizwaji wa fedha hiyo,

Vile vile, Kamati ilipohitaji kupatiwa maelezo zaidi juu ya Fedha hiyo ambayo haina hata “Note” katika Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa mwaka 2020/2021 majibu yalikosekana.

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inamshauri Mhasibu wa Wilaya ya Kusini na Mkaguzi wa Ndani kuwa makini wakati wa kuandaa Taarifa ya mwisho ya hesabu za Mwaka ili kuhakikisha taarifa zote muhimu ziweze kuingizwa kwenye Taarifa hiyo na kuondokana na kasoro zisizo na majibu sahihi wakati wa ukaguzi.

**5.1.11.1 Ucheleweshwaji wa mapato kupelekwa Benki shilingi 10,147,250**

Kwa mujibu wa kifungu Nambari 78(1), (2) na (3) cha Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005 kinaeleza kuwa “Makusanyo yote au fedha zozote za Serikali lazima ziingizwe benki au hazina au ikishindikana angalau mapema iwezekanavyo”.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa ucheleweshwaji wa upelekaji wa fedha za makusanyo Benki. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa uwezekano wa kutumika kwa fedha za makusanyo kinyume na malengo yaliyokusudiwa ambapo ni kwenda kinyume na kifungu kama nilivyokinakili hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri kuhakikisha unatumia mfumo katika ukusanyaji wa mapato ili kuepusha uwezekano wa ucheleweshwaji wa mapato kupelekwa Benki. Mchanganuo wa makusanyo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Halmashauri Wilaya ya Kusini**

Halmashauri imekuwa ikitumia mfumo wa kielektroniki “Mutum” kwa kuhusisha matumizi ya (POS) katika mwaka husika. Katika kipindi hiki kulikuwa

na changamoto mbali mbali ambazo ndizo zilipelekea kuonekana ucheleweshaji wa kuwasilisha malipo Benki. Changamoto hizo ni pamoja na kwa mtandao mara kwa mara katika vituo vyetu vya kukusanyia mapato. Pia, kumekuwa na kukosekana matatizo ya kiteknolojia ambapo mashine zinaleta "error" wakati wa kurikodi makusanyo ya siku, na pale linapoondoka tatizo ripoti inayotoka inaonesha makusanyo yote yamekusanywa kwa tarehe ya siku moja.

Matatizo haya ndio yamepelekea kuonekana kuwa fedha za siku nyingi zimepelekwa Benki tarehe moja.

Tatizo hili limeshapungua kutokana na kuboreshwa kwa mfumo ambapo hivi sasa kuna matumizi ya "Control Number" na mawakala wanaowezesha kufanya malipo kwa wakati.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC, ilibaini yafuatayo:

- Kuwepo kwa dosari ya mfumo wa kukusanyia mapato
- Watendaji kutokuwa na uelewa juu ya matumizi ya mashine za kielektroniki.
- Kuwepo kwa ufuatiliaji mdogo wa fedha zinazokusanywa kuingizwa benki.
- Kutokufuatwa ushauri unaotolewa na Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri.

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hizo zisijitokeze tena katika siku zijazo Kamati ya LAAC ilipendekeza yafuatayo:-

1. Halmashauri ya Wilaya ya Kusini ihakikishe kuwa inatoa taarifa haraka iwezekanavyo kwa njia ya maandishi pale inapotokezea changamaoto katika mfumo wa makusanyo ili marekebisho yaweze kufanyika kwa

wakati.

2. Halmashauri ifanyie kazi ushauri unaotolewa na Mkaguzi wa Ndani kwa wakati ili kuepusha hoja zisizo na msingi.
3. Halmashauri iandae mpango mkakati wa kuwapatia mafunzo Maafisa Mapato wa ndani ili kuepusha ucheleweshwaji wa mapato Benki na upotevu wa mapato ya Serikali

**5.1.11.2 Kutokuwepo kwa mkataba wa usambazaji wa mafuta Shilingi 65,516,366**

Kifungu nambari 162(1) cha kanuni ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma ya mwaka 2021 kinaeleza kuwa "kitengo cha ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kitatumia fomu maalum ya mkataba iliotolewa na Mamlaka yenye mabadiliko madogo katika kushughulikia masuala mahsusi".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa usambazaji wa mafuta ya petrol wenye jumla ya shilingi 65,516,366 uliofanywa na Zanzibar Petroleum Limited kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja. Doari iliyobainika ni kutokuwepo kwa Mkataba wa Uzambazaji wa mafuta hayo ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu kama kilivyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri kuhakikisha kwamba Sheria, Kanuni na Miongozo mbali mbali inafuatwa kiukamilifu ikiwemo kutumia mikataba katika kufanya malipo pale inapohitajika.

**Majibu ya Halmashauri Wilaya ya Kusini**

Halmashauri tayari imeandaa mkataba wa mafuta na msambazaji Zanzibar Petroleum

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kuifuatilia hoja hii, Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:-

1. Kukiukwa kwa utaratibu wa Zabuni katika upatikanaji wa Zanzibar Petroleum kuwa mzambazaji wa mafuta kwa Halmashauri ya Kusini.

2. Kutumia njia ya “Single Source” kutokana na ukaribu wa mzabuni huyo katika kupata huduma hiyo kwa karibu

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inaishauri uongozi wa Halmashauri kufuata Sheria ya manunuzi juu ya upatikanaji wa zabuni mbalimbali aidha kuwafungisha mikataba kwa watoa wa huduma hiyo ili kuthibitisha uhalali wa matumizi ya fedha za Serikali.

**5.1.11.3 Kutokulingana kwa taarifa za matumizi ya mafuta zilizopo Halmashauri na Kituo cha Mafuta shilingi 4,462,990**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 4,462,990 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa ajili matumizi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kusini. Dosari iliyobainika ni kutokulingana kwa taarifa za mafuta yaliyotumika baina ya Kituo cha Mafuta (Zanzibar Petroleum LTD) na taarifa zilizopo katika Ofi si za Halmashauri. 128 Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2021

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa utumiaji usioridhisha wa rasilimali ya mafuta katika Halmashauri ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri kuhakikisha kunakuwepo na utaratibu mzuri wa utumiaji wa rasilimali ya mafuta ikiwemo kulingana kwa taarifa za matumizi ya mafuta baina ya Halmashauri na Kituoni. Mchanganuo wa tofauti ya matumizi ya mafuta ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Halmashauri Wilaya ya Kusini**

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini imechukua ushauri. Baada ya kupokea ushauri kutoka kwa Ofisi ya Mkaguzi wa Serikali Ofisi ya Halmashauri imeanza

kuchukua hatua ya kuhakikisha kila atakaechukua risiti ya mafuta arejeshe risiti kwa ajili ya kuhakikisha utumizi wake wote wa mafuta pia tunafanya usuluhishi baina ya "Store Ledger" za Ofisi na Statement za kituo cha mafuta.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii imebaini kutokuwepo kwa ufuatiliaji na usimamizi imara wa ofisi katika matumizi ya mafuta.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri Uongozi wa Halmashauri kuwa makini katika matumizi ya mafuta kwa kufanya usulihishi wa matumizi ya mafuta kwa kila mwenzi ili kubaini dosari mbalimbali za matumizi hayo.

**5.1.11.4 Dosari katika utumiaji wa rasilimali ya mafuta**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Kusini hutoa vibali vya mafuta kwa wafanyakazi kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kupitia vyombo mbali mbali vya usafi ri vikiwemo gari na vespa. Dosari iliyobainika ni kuwepo kwa idadi kubwa ya mafuta inayotolewa kwa wafanyakazi. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021 129 kinyume na uwezo wa vyombo vilivyotumika kuingiza mafuta hayo. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo matumizi yasiyoridhisha ya rasilimali ya mafuta hayo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri kuhakikisha unaandaa utaratibu mzuri wa utoaji wa rasilimali ya mafuta kwa wafanyakazii ili mafuta hayo yaweze kutumika kama ilivyokusudiwa. Mchanganuo wa matumizi ya mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kutoa vibali vya mafuta kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kupitia vyombo mbali mbali vya usafiri vikiwemo gari na vespa. Dosari iliyotokea ni kuwepo kwa tofauti kubwa ya mafuta kinyume na uwezo wa vyombo hivyo hii kutokana na Halmashauri ilikuwa inaazima gari kwa aji ya kufanya ukaguzi wa sehemu mbali mbali. Halmashauri ilikuwa ikisaidia kufanikisha shughuli mbali mbali za Kiserikali, hii imepelekea kutumia risiti moja tu kwa gari ya kwetu.

**Uchunguzi wa Kamati**

- Mafuta kutolewa kinyume na taratibu za kiofisi.
- Matumizi mabaya ya mafuta kinyume na uhalisi wa vyombo husika.

**Mapendekezo ya Kamati**

Ili kasoro kama hizo zisijitokeza katika siku zijazo Kamati ya LAAC ilipendekeza Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kufuata taratibu za Sheria ya katika matumizi ya mafuta.

Aidha kwa vyombo vinatumiwa na Halmashauri vya binafsi kwa ajili ya shughuli za usafi ni vyema kuviandikia dokezo la utumiaji wa mafuta kwa vyombo hivyo badala ya kutumia namba ya usajili wa vyombo vya Serikali ambavyo havina uhalisia wa idadi ya lita zilizoorodheshwa katika vyombo hivyo.

### 5.1.11 HALMASHAURI YA WILAYA YA MICHEWENI

**Taarifa ya Mapato**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 300,000,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 337,819,04.00 sawa na asilimia 112.61 ya makadirio kama ifuatavyo:

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Michewni**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni haikuandaa maelezo ya moja kwa moja juu ya taarifa ya mapato na badala yake lilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilibaini yafuatayo:

Kuongezeka kwa mapato kulitokana na ada ya huduma Kifungu 1800 ikijumuisha makusanyo ya minara amabapo hapo awali haikuingizwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021.

**Taarifa ya Matumizi**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,775,860,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 297,160,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufi kia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 4,478,700,000 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 93.78 ya makadirio na shilingi 276,413,429.92 zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 93.02 ya makadirio 2021, hii iltokana na kutokupatikana fedha kamazilivyopangwa katika bajeti lakini hata hivyo miradi ya maendeleo imekamilika kwa kiwango kikubwa licha ya kutofikiwa kwa asilimia 100.

Aidha, zipo baadhi ya fedha za miradi ya maendeleo ambazo hazikutumika kutokana na changamoto ya Mfumo wa Malipo (IFMS)ikiwemo uendelezaji wa ujenzi wa Skuli ya Maandalizi Mapofu.

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Michewni**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni pia haikuandaa maelezo yoyote juu ya taarifa ya matumizi na badala yake lilijibu hoja za Kamati kama zilivyoulizwa

**5.1.12.1 Kutokufi kiwa kwa ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imekusanya jumla ya shilingi 337,819,041 sawa na asilimia 112.61 ya makadirio kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 ambapo kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 40,872,523.60 zilitumika kwa ajili ya kazi za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 12 ya makusanyo halisi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba fedha zilizotumika kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo pamoja na uwezeshwaji wa wajasiriamali hazikuweza kufi kia kiwango halisi kilichotakiwa, kwa mujibu wa utaratibu na agizo lililotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa ziara za kutembelea miradi ya maendeleo katika Halmashauri na Mabaraza ya Miji ni kwamba makusanyo yanapaswa yatumike kwa shughuli za miradi ya maendeleo kwa asilimia 30 na uwezeshaji wa wajasiria mali,vijana, Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2021 131 wanawake na watu wenye ulemavu kwa asilimia 10 jambo ambalo ukaguzi umebaini matumizi ya miradi ya maendeleo yamefanyika kwa asilimia 12 ya makusanyo halisi na hakukubainika matumizi yoyote yaliyofanyika kwa uwezeshaji wa wajasiria mali,vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwaasilimia 10.

Aidha, ukaguzi umebaini matumizi ya asilimia 88 yametumika kwa huduma za

uendeshaji wa Halmashauri jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa tija iliyokusudiwa.

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Michewni**

Katika ukaguzi uliofanywa na Ofisi ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serekali imeripotiwa Kutokufikiwa kwa ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo 2020/2021, hii ilitokana na changamoto za Mfumo wa malipo (IFMS) kuonesha kuwa fedha za makusanyo ya Halmashauri zimemalizika na kupelekea kuzuia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo uendelezaji wa ujenzi wa Skuli ya maandalizi Mapofu. Baada ya wizara ya fedha na mipango kuhakiki na kufunga hesabu ilibainika kwamba Jumla ya Tzs 63,282,377.80 zilikuwemo kwenye mfumo na kuingizwa katika vitabu (Cash book) kama ni bakaa iliobakia katika mwezi June, 2021

Aidha Jumla ya Tzs 15,698,650 zilitumika kwa kuwanunulia vifaaa wajasiriamali wa wilaya ya Micheweni ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa ziara ya kuzitembelea Halmashauri na Mabaraza ya Miji kwa kuwasaidia vijana, wanawake, na watu wenye ulemavu. Jumla ya vikundi kumi (10) vya wajasiria mali vilisaidiwa kati hivyo vikundi vinne (4) ni vya wananwake, vitano (5) vya vijana na kimoja cha wenye ulemavu kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Uchunguzi wa Kamati**

Katika kuifuatilia hoja hii kwa kina Kamati ya LAAC imebaini yafuatayo:-

1. Fedha za Miradi ya Maendeleo zilikuwa zinatumika kinyume na muongozo wa matumizi ya Serikali asilimia 10 ya makusanyo kwenda katika (LGAs) na badala yake kutumika asilimia 5 tu kwa makundi hayo matatu (Wanawake, Wajasiriamali na Watu Wenye Ulemavu).
2. Kutokana na kasoro hizo Kamati ilishindwa kujiridhisha kukosekana kwa vielelezo vilivyowapatia wao mamlaka ya kutumia asilimia 5 na sio

asilimia 10 kwa (LGAs) na kupelekea hoja hii kubakia kama ilivyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ikahakikishe kuwa linafanya utafiti wa kutosha juu ya jambo lolote kabla ya kuchukua hatua ili kuepusha hasara isiyo na lazima kwa Serikali.

**5.1.12.2 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 22,445,806**

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 22,445,806 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

Jumla ya Shilingi 22,445,806 zimeripotiwa na Ofisi ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 zimelipwa zikiwa na vielelezo pungufu kwenye malipo hayo, hata hivyo zipo baadhi ya hati zenye jumla ya Tzs 7,588,000 kama vile hati namba 19/10, 12/10, 16/10, 47/10, 45/10 na 39/10 ambazo zimelipwa na vielelzo vyake vimekamilika

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kufuatilia hoja hii Kamati ya LAAC ilishindwa kuifanyia kazi hoja hi kwa kutokupatika kwa vielelezo wakati wa ukaguzi wa Kamati. Hivyo, hoja hii inabakia kama ilivyo.

**5.1.12.3 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 24,879,864**

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au

taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni 2021 133 Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar. Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

Jumla ya Shilingi 24,879,864 zimeripotiwa na Ofisi ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serekali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 zimelipwa kwa watowa huduma ambao hawakusasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016,

hata hivyo ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni inakataa idadi ya fedha hizo zilizotajwa na mkaguzi kuwa watowa huduma hao wote hawajasajiliwa kwani hati namba 1/10, 1/11, 20/11 na 3/1 zenye ya jumla ya shillingi 10,690,716 zimelipwa kwa mtowa huduma Imania Petrol Station, hati namba 24/11 yenye thamani ya shilingi 653,127 imelipwa kwa mtowa huduma Omar Breik Omar na hati namba 26/11 yenye jumla ya shilingi 152,000 ambayo imelipwa kwa Yaks na kufanya jumla ya shilingi 12,095,843 kuwa wamesajiliwa katika mwaka huo

Na hati namba 3/10, 2/10, 26/10, 44/10, 42/10, na 56/10 zenye jumla ya 12,384,021 ndio watowa huduma ambao hawakusajili, hata hivyo kwa sasa watowa huduma hao wameshasajili ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imetowa mchango mkubwa kuwashajihisha wafanya biashara hao kuweza kujisajili

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati kutokana na muda mdogo waliokuwa nao wa kazi haikuweza kuvipata na kuvipitia kwa wakati vielelezo vyote hivyo. Sambamba, na hilo, Kamati inaishauri Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni katika utekelezaji wa majukumu yao kuhakikisha inafuata kikamilifu Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Mwaka 2016 ili kuepusha upotevu wa fedha za Serikali.

**5.1.12.4 Kutokuwepo kwa uwiyano wa kumbu kumbu za kifedha**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa uwiyano wa kumbu kumbu za kifedha baina ya taarifa za benki "Bank Statement" na taarifa za mwisho wa mwaka"Final Account". Kufanya hivyo kunapelekea taarifa za ufungaji wa mahesabu kutokuwa sahihi ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa uwiano wa kumbu kumbu hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

Katika ukaguzi uliofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeripotiwa Kutokuwepo kwa uwiyano wa kumbu kumbu za kifedha 2020/2021, hii ilitokana na changamoto za Mfumo wa malipo (IFMS) kuonesha kuwa fedha za makusanyo ya Halmashauri zimemalizika na kupelekea kufutwa kwa matumizi yaliyofanyika. Baada ya Wizara ya Fedha na Mipango kuhakiki na kufunga hesabu ilibainika kwamba Jumla ya Tzs 63,282,377.80 zilikuwemo

kwenye mfumo na kuingizwa katika vitabu (Cash book) kama ni bakaa iliobakia katika mwezi June, 2021 na kusababisha tofauti ya hesabu hizo

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kutokana na kasoro hiyo, Kamati ya LAAC inaishauri Serikali inapoanzisha matumizi ya mifumo ya makusanyo katika Halmashauri zetu ni vyema kuaanda mafunzo kwa Maafisa Mapato pamoja na wahasibu Wakuui li mapungufu kama haya yasije kujitokeza tena katika ripoti zijazo.

**5.1.12.5 Ukusanyaji wa mapato kinyume na makadirio**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni hukusanya kupitia vyanzo mbali mbali lakini ukusanyaji wa mapato hayo umefanya kinyume na makadirioyaliyowekwa,Aidha imebainika kutokuwepo kwa makadirio kwa baadhi ya vianzio vya mapato,ukadiriaji mdogo kwa baadhi ya vianzio, pamoja na kutokusanya mapato kwa baadhi ya vianzio kama ilivyopangwa.

Kufanya hivyo kunaweza kuepelekea upotevu wa mapato,aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari32(1)(2)cha sheria nambari 12 ya Usimamaizi wa Fedha za umma ya mwaka 2016.Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.

**jadweli Nambari 73: Ukusanyaji wa mapato kinyume na makadirio**

| Chanzo cha mapato | Makadirio ya makusanyo(Tshs) | Makusanyo halisi (Tshs) | Tofauti | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Fedha (Tshs) | Asilimia (%) |
| Ada ya mauzo | 25,800,000 | 12,759,200 | (13,040,800) | (50.55) |
| Lesseni za | 86,460,000 | 57,396,000 | (29,064,000) | (33.62) |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Biashara | | | | |
| Ada ya Huduma | 106,080,000 | 193,674,341 | (87,594,341) | (82.57) |
| M/fii | 10,000,000 | 1,721,000 | (8,279,000) | (82.79) |
| | | | | |

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

Katika ukaguzi uliofanywa na Ofisi ya mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serekali imegunduwa kuwepo na ukusanyaji wa mapato kinyume na makadirio yaliyowekwa, hii ni kutokana na sababu zifuatazo:-

Kuhusu chanzo cha ada ya mauzo kutokufikia malengo, hii ilitokana na kupata mapato ya minada yasiyoridhisha katika soko la samaki Tumbe kulikosababishwa na kukabidhiwa soko hilo kwa kamati ya uvuvi ambayo haina taaluma ya kutosha ya ukusanyaji wa mapato jambo limepelekea kutopatikana asilimia 20 ya makusanyanyo kama ilivyoelekezwa katika mkataba.

Kuhusu chanzo cha leseni za biashara kutokufikia malengo kulisababishwa na uwepo wa maradhi ya mripuko ya COVID 19 kulikopelekea athari za kiuchumi na mzunguko mdogo wa kibiashara.

Aidha kuhusu kuvuuka malengo kwa chanzo cha Ada ya huduma, hii ilitokana na kuingiziwa jumla ya Tsz 30,000,000 za mgao kutoka kamati ya udhibiti wa ujenzi (DCU) ambazo hapo awali hazikupangwa katika bajet ya 2020/2021pamoja na kulipwa malimbikizo ya Ada za matangazo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Katika kuifuatilia hoja hii Kamati ya LAAC haijaridhika na majibu yaliotolewa wakati wa majadiliano na kupelekea hoja hii kubakia kama ilivyo.

## UKAGUZI MAALUM WA MAPATO YATOKANAYO NA MINADA YA SAMAKI NA MAZAO YA BAHARINI "MADIKO" PEMBA

### 5.1.1 BARAZA LA MJI CHAKE CHAKE

#### 10.1.1.1 Kutokuwepo kwa udhibiti na usimamizi mzuri wa madiko

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa maeneo mbali mbali yanayofanywa minada ya samaki na mazao ya baharini katika Wilaya ya Chake Chake ambayo yanasimamiwa na Baraza la Mji Chake Chake lakini udhibiti na usimamizi wa maeneo hayo hauridhishi kutokana na kutokuzingatiwa kwa Sheria, kanuni na miongozo mbali mbali inayopaswa kutumika katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali zinazofanyika katika maeneo ya minada hiyo hali iliyopelekea kuwepo kwa dosari mbali mbali kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa huduma za choo kwa baadhi ya madiko, jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa uharibifu wa mazingira na hatimae kusababisha kutokea maradhi mbali mbali ya mripuko. Madiko yasiokuwa na huduma za choo ni Kichuwani, Vitongoji Kibokoni, Mkumbuu, Pujini, Furaha, Mjini Ole na Ndagoni.
- Kuwepo kwa makadirio madogo ya mapato yenye jumla ya shilingi 4,239,000 ambayo hayalingani na makusanyo halisi yenye jumla ya shilingi 5,555,000 sawa na asilimia 132.26 ya makadirio, hali iliopelekea kuwepo kwa ongezeko la fedha za makusanyo yenye jumla ya shilingi 1,316,000 sawa na asilimia 32.26 ya makusanyo ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(1)(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.
- Kutokuwepo kwa uwiyano baina ya taarifa za hesabu na taarifa za makusanyo zinazohusu mapato ya madiko ambapo imebainika kuripotiwa kwa mapato

yenye jumla ya shilingi 5,555,000 katika taarifa za hesabu lakini jumla ya Shilingi 3,677,000 zimeripotiwa katika taarifa za mapato, hali iliyopelekea kuwepo kwa tofauti ya shilingi 1,878,500 sawa na asilimia 33.9 ya makusanyo halisi, ambapo ni kwenda kinyume na sheria, miongozo na taratibu za hesabu za kitaifa na kimataifa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Chake Chake Pemba kuhakikisha kwamba udhibiti na usimamizi wa maeneo ya ukusanyaji wa mapato yanaimarishwa kwa lengo la kuengeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

**Majibu ya Baraza Mji Chake Chake**

Ni kweli baadhi ya madiko hayana huduma ya choo kutokana na sababu ya kwamba baadhi ya madiko hayo yalikuwa hayajarasimishwa kuwa sehemu au maeneo ya kufanya shughuli za kivuvi. Mfano wa madiko hayo ni kama ifuatavyo:

- Diko la Furaha
- Diko la Vitongoji
- Diko la Mkumbuu
- Diko la Miini Ole

Kukosekana kwa uwiano baina ya taarifa za kibenki na daftari la hesabu imetokana na kutokuwepo kwa muingiliano baina ya taarifa za kibenki na daftari ambapo kulisababishwa na mfumo wa ulipaji kwa wakati huo ambao ulikuwa hautumi Control Number hivyo ulisababisha kuwepo tofauti kati ya taarifa za mapato na kibenki.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC katika ufuatiliaji hoja hizi imebaini yafuatayo:

1. Katika baadhi ya madiko yaliotajwa na mkaguzi kama vile diko la furaha, vitongoji, mjini ole na mkumbuu shughuli za uvuvi hazifanyiki kila siku hivyo madiko hajafikia vigezo vya kurasimishwa.

2. Kiwango kidogo cha mapato yanayokusanywa katika baadhi ya madiko yamepelekea baraza la mji kutorasimisha na kuweka miundombinu ya vyoo katika madiko hayo mfano halisi, Diko la Furaha mapato yanayokusanywa kwa mwaka ni shilingi 350,000, Diko la Vitongoji mapato yanayokusanywa kwa mwaka ni shilingi 1,5000, Diko la Mkumbuu/Ndagoni mapato yanayokusanywa kwa mwaka ni 650,000 na Diko la Mji Ole mapato yanayokusanywa kwa mwaka ni 250,000

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja kamati inapendekeza mambo yafuatayo.

Kamati inashauri Baraza lifanye tathmini ya madiko yake ili kubaini ukusanyaji halisi wa mapato yanayotokana na madiko na kuweza kuchukua hatua ya kuyarasimisha kwa kuweka miundombinu ya huduma za vyoo ili kuongeza ufanisi wa makusanyo katika maeneo hayo

Kwa yale madiko ambayo yapo karibu katika eneo moja na hayajarisamishwa kutokana na uchache wa shughuli za uvuvi ni vyema kuzungumza na viongozi wa madiko hayo kwa lengo la kuyaunganisha kwa kufanya diko moja tu ili kuweza kurasimisha na kupeleka huduma za vyoo katika diko hilo.

**10.1.1.2 Kutokurasimishwa kwa maeneo ya Minada ya Samaki na mazao ya baharini**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa maeneo mbalimbali yanayotumika kwa ajili yaminada ya samaki na mazao ya baharini (Madiko) lakini maeneo hayo hayakuweza kurasimishwa kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato, hali inayopelekea uwepo wa viashiria vya uvujaji wa mapato ya Serikali yanayotokana na vianzio hivyo ambapo baadhi ya maeneo yaliyobainika kutokurasimishwa ni pamoja na Vitongoji Kibokoni, Mkumbuu, Pujini, Furaha, Mjini Ole, na Ndagoni. Kufanya hivyo kunapelekea kupunguza ufanisi wa Baraza la Mji Chake Chake katika ukusanyaji wa mapato pamoja na utowaji wa

huduma bora kwa jamii, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 70(b) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2014.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Chake Chake Pemba kuhakikisha kwamba maeneo yote ya minada yanarasimishwa kwa lengo la kuengeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

**Majibu ya Baraza Mji Chake Chake**

Kutokurasimishwa kwa baadhi ya maeneo ya minada ya Samaki kwamba maeneo hayo hayakuwa na shughuli rasmi za uvuvi na jamii ilikuwa haina uelewa juu ya jambo hilo hivyo ilipelekea kukosekana kwa mapato hayo kutokana na kutumia gharama kubwa kuliko mapato halisi yaliokuwa yanapatikana katika maeneo hayo. Kwa jitihada za Ofisi ya Baraza kwa mwaka 2021/2022 iliamua kulirasimisha eneo la Ndagoni baada ya kuona kwamba shughuli za uvuvi zinafanyika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inalishauri Baraza la Mji Chake Chake kabla ya kuyarasimisha maeneo ya madiko ya Samaki yaliopo katika maeneo mbali mbali ni vyema kufanyika tathmini ya kina juu ya mapato yatakayopatikana kabla ya uwekezaji wa majengo ya minada katika maeneo hayo ili kuepusha hasara ya kuekeza fedha nyingi kwa kujenga majengo katika maeneo hayo na kumlipa mfanyakazi wa kukusanya mapato ilhal ukusanyaji katika maeneo hayo hauwezi kurudisha gharama za uendeshaji

**10.1.1.3 Kukosekana kwa taarifa za ukusanyaji wa mapato**

Baraza la Mji Chake Chake Pemba lina wajibu wa kusimamia, kudhibiti na kukusanya mapato kupitia mfumo maalum wa ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kuongeza ufanisi katika makusanyo, ambapo katika ukaguzi uliofanyika imebainika mapato yatokanayo na maeneo yanayotumika kwa ajili ya minada ya samaki na mazao ya baharini (madiko) hayakuweza kuthibishwa kutokana na

kutokuwepo kwa taarifa zinazotokana na makusanyo hayo kupitia katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato (MUTM).

Kufanya hivyo kunapelekea kupunguza ufanisi wa Baraza la Mji Chake Chake katika ukusanyaji wa mapato pamoja na utowaji wa huduma bora kwa jamii, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 70(b) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2014.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Chake Chake Pemba kuhakikisha kwamba mfumo wa ukusanyaji wa mapato unaimarishwa kwa lengo la kuhakikisha kwamba taarifa sahihi za mapato zinapatikana kwa wakati

**Majibu ya Baraza Mji Chake Chake**

Ni kweli kwa wakati huo Baraza la Mji Chake Chake liliona hakuna haja ya kusajili maeneo ya minada ya Samaki na mauzo ya baharini katika mfumo wa makusanyo ya mapato (MUTM)kama vyanzo vya mapato kutokana na kutorasimishwa kwa maeneo hayo kama madiko rasmi kwa shughuli hizo lakini kwa sasa mfumo unatambua vyanzo hivyo.

**Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza limekiri kuwepo kwa changamoto hiyo ya mfumo hata hivyo dosari hiyo imesharekebishwa, Kamati inaishauri Baraza kuhakikisha linaisimamia na kuimarisha ipasavyo mifumo ya ukusanyaji mapato ili kuwa na taarifa sahihi za makusanyo hayo.

### 10.1.4. HALMASHAURI WILAYA YA MICHEWENI

#### 10.1.4.1 Kutokuwepo kwa udhibiti na usimamizi mzuri wa Madiko

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa maeneo mbalimbali yanayofanywa minada ya samaki na mazao ya baharini katika Wilaya ya Micheweni ambayo yanasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni lakini udhibiti na usimamizi wa maeneo hayo hauridhishi kutokana na kutokufuatwa kikamilifu kwa sheria, kanuni na miongozo mbali mbali inayopaswa kutumika katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazofanyika katika maeneo ya minada hiyo hali iliyopelekea kuwepo kwa dosari mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa huduma za choo kwa baadhi ya madiko, jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa uharibifu wa mazingira na hatimae kusababisha kutokea maradhi mbali mbali ya mripuko. Madiko yasiokuwa na huduma za choo ni Msuka, Kiuyu Mbuyuni, Shumba, Wingwi na Vuma Wimbi.
- Kutokuwepo kwa uwiyano baina ya taarifa za hesabu na taarifa za makusanyo zinazohusu mapato ya madiko ambapo imebainika kuripotiwa kwa mapato yenye jumla ya shilingi 12,759,200 katika taarifa za hesabu lakini jumla ya shilingi 9,969,500 zimeripotiwa katika taarifa za mapato, hali iliyopelekea kuwepo kwa tofauti ya shilingi 2,789,700, ambapo ni kwenda kinyume na sheria, miongozo na taratibu za hesabu za kitaifa na kimataifa.
- Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba kuhakikisha kwamba udhibiti na usimamizi wa maeneo ya ukusanyaji wa mapato yanaimarishwa kwa lengo la kuengeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

Mhe. Mwenyekiti maeneo rasmi yanayofanyika minada ya samaki katika Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ni Msuka, Tumbe, Shumba na Kiuyu. Katika maeneo hayo ya madiko huduma ya choo inapatikana kwa diko la Tumbe na Shumba Mjini. Ni kweli katika diko la Msuka na Kiuyu kwa sasa huduma hiyo haipo. Juhudi zilizochukuliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni katika kuboresha huduma hizo ni pamoja na kujenga soko jipya na la kisasa lenye huduma zote muhimu ikiwemo za vyoo vya kisasa kwa upande wa diko la Shumba Mjini kupitia Mradi wa Big-Z na kwa upande wa diko la Msuka Halmashauri imefanya mazungumzo na Kamati ya Soko na Kamati ya Uvuvi na kuwataka watupatie eneo kwa ajili ya ujenzi wa vyoo.

Pia ukaguzi uliofanyika ulibaini Kutokuwepo kwa uwiyano baina ya taarifa za hesabu na taarifa za makusanyo zinazohusu mapato ya madiko ambapo imebainika kuripotiwa kwa mapato yenye jumla ya shilingi 12,759,200 katika taarifa za hesabu lakini jumla ya shilingi 9,969,500 zimeripotiwa katika taarifa za mapato, hali iliyopelekea kuwepo kwa tofauti ya shilingi 2,789,700, hii ilitokana na wanaotunza kumbukumbu za mapato kurikodi taarifa za mgao wa Soko la Tumbe katika ada ya huduma na kusababisha tofauti hiyo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini uongozi wa Halmashauri imeshachukua jitihada za kujenga vyoo kwa baadhi ya madiko yake kama vile diko la Tumbe pamoja kuendelea kuyaboresha madiko mengine ambayo hayana vyoo kama vile diko la Msuka

Kamati inashauri uongozi wa Halmashauri kuongeza juhudi izo ili kukamilisha ujenzi wa vyoo katika madiko yote wanayoyasimamia kwa lengo

la kuweka mazingira safi na salama kwa watumiaji wa madiko hayo.

Aidha Kamati inashauri kupitia watendaji wa mapato wa Halmashauri kuwa na umakini na weledi katika ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Halmashauri kwa kuweka taarifa sahihi za mapato katika chanzo husika.

**10.1.4.2 Kutokurasimishwa kwa maeneo ya minada ya samaki na mazao ya baharini**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa maeneo mbalimbali yanayotumika kwa ajili ya minada ya samaki na mazao ya baharini (madiko) lakini maeneo hayo hayakuweza kurasimishwa kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato, hali inayopelekea uwepo wa viashiria vya uvujaji wa mapato ya Serikali yanayotokana na vianzio hivyo ambapo baadhi ya maeneo yaliyobainika kutokurasimishwa ni Wingwi na Vuma Wimbi

Kufanya hivyo kunapelekea kupunguza ufanisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni katika ukusanyaji wa mapato pamoja na utowaji wa huduma bora kwa jamii, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 70(b) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2014.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba kuhakikisha kwamba maeneo yote ya minada yanarasimishwa kwa lengo la kuengeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

Mhe. Mwenyekiti ni kweli kwamba baadhi ya wavuvi wa maeneo ya Wingwi na Makangale huyatumia maeno ya Wingwi (Kwa Mbwana) na Vuma Wimbi kwa ajili ya kuuza samaki wao kwa baadhi tu ya nyakati na baadhi ya msimu hususani pale wanapokuwa na samaki kidogo. Hata hivyo wavuvi wa maeneo ya Vumawimbi kwa sasa wanauzia samaki hao Bandari ya Msuka au

Tumbe ambapo kote kuna minada rasmi. Kutokana na uchache wa minada inayofanyika kwenye eneo la Vuma Wimbi na Wingwi; kupeleka watumishi kukusanya mapato kwenye maeneo hayo kunaweza kupelekea hasara kubwa zaidi kuliko tija itakayopatikana. Jambo ambalo ni kuliongezea mzigo Halmashauri na Serikali kiujumla.

Hata hivyo ushauri uliotolewa na ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serekali kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba kurasimisha maeneo ambayo yana ufanisi wa upatikanaji wa mapato umechukuliwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC inalishauri Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kabla ya kuyarasimisha maeneo ya madiko ya Samaki yaliopo katika maeneo mbali mbali ni vyema kufanyika tathmini ya kina juu ya mapato yatakayopatikana kabla ya uwekezaji wa majengo ya minada katika maeneo hayo ili kuepusha hasara ya kuekeza fedha nyingi kwa kujenga majengo katika maeneo hayo na kumlipa mfanyakazi wa kukusanya mapato ilhal ukusanyaji katika maeneo hayo hauna tija.

**10.1.4. 3 Makadirio ya ukusanyaji wa mapato kinyume na uhalisia shilingi 25,800,000**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa makadirio ya makusanyo yenye jumla ya shilingi 25,800,000 yaliyopangwa kukusanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo makadirio hayo ni madogo ukilinganisha na makusanyo halisi yenye jumla ya shilingi 12,759,200 yaliyokusanywa na kupelekea kuwepo kwa upungufu wa shilingi 13,040,800 sawa na asilimia 50.55 ya makadirio ambapo ni kwenda kinyume na Kifungu Nambari 32(1) (2) cha

Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016

Ukaguzi unashauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba kuhakikisha kwamba udhibiti na usimamizi wa maeneo ya ukusanyaji wa mapato yanaimarishwa kwa lengo la kuengeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.**

Mhe. Mwenyekiti makusanyo ya mapato ya ada ya mauzo yamekua kidogo kuliko makadirio hii ni kutokana na kupata mapato ya minada yasiyoridhisha katika soko la samaki Tumbe kulikosababishwa na kukabidhiwa soko hilo kwa kamati ya uvuvi ambayo haina taaluma ya kutosha ya ukusanyaji wa mapato jambo hili limepelekea kupatikana kiwango kidogo cha asilimia 20 ya makusanyo kama ilivyoelekezwa katika muongozo uliotolewa na Serikali wakati wa kulikabidhi soko kwa Kamati ya Uvuvi ya Tumbe. Vile vile mripuko wa maradhi ya COVID 19 kulikopelekea kupigwa marufuku mikusanyiko ya watu kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo maeneo ya minada ilipelekea kushuka kwa upatikanaji wa mapato ya minada kwa kiasi kikubwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imekiri kutokea kwa dosari hiyo hata hivyo Kamati inashauri uongozi wa Halmashauri kuongeza wiko wa ukusanyaji mapato yatokanayo na Madiko kutokana na kupungua kwa ugojwa wa UVIKO 19 na Serikali kuruhusu mikusanyiko katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

**10.1.4.4 Kukosekana kwa taarifa za ukusanyaji wa mapato**

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba ina wajibu wa kusimamia, kudhibiti na kukusanya mapato kupitia mfumo maalum wa ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kuongeza ufanisi katika makusanyo, ambapo katika

ukaguzi uliofanyika imebainika mapato yatokanayo na maeneo yanayotumika kwa ajili ya minada ya samaki na mazao ya baharini (madiko) hayakuweza kuthibishwa kutokana na kutokuwepo kwa taarifa zinazotokana na makusanyo hayo kupitia katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato (MUTM).

**Majibu ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni**

Ofisi inakiri kwamba mfumo wa ukusanyaji mapato wa MUTM una changamoto mbali mbali ikiwemo ukosekanaji wa ripoti ya makusanyo. Kutokana na kasoro hizo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambaye ndiye Msimamizi mkuu wa mfumo imeshachukua hatua za kuufanyia marekebisho mfumo huo ili kuondosha mapungufu yaliyojitokeza. Mafunzo maalum ya utumiaji wa mfumo huu yameshatolewa kwa maafisa wetu wa mapato pamoja na kuviingiza vyanzo vyote vya mapato vikiwemo vya madiko kwenye mfumo mpya wa Zan-MUTM kwa mujibu wa tangazo la Gazeti Maalum la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na jitihada nzuri zilizochukuliwa na uongozi wa Halmashauri ya kurekebisha dosari mbalimbali katika mfumo wa MUTM kwa lengo la kutoa taarifa sahihi za mapato hata hivyo Kamati inashauri mafunzo kwa watendaji yazidi kutolewa na kutoa taarifa kwa haraka Wizarani wakati mfumo unapokabiliwa na Changamoto ili dosari kama hizo zisijekujitokeza tena.

## 3.6 MRADI WA UJENZI WA DAHALIA YA WANAUME KATIKA SKULI YA SEKONDARI MOH'D JUMA PINDUA - PEMBA

Mradi wa ujenzi wa dahalia ya wanaume katika Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua ambao umetekelezwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Ubalozi wa Japan kwa lengo la kuondosha changamoto ya kutokuwepo kwa Dahalia rasmi ya wanafunzi wa kiume ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiishi katika mazingira yasioridhisha kutokana na tatizo la kutokuwepo kwa makaazi rasmi ya wanafunzi hao katika maeneo ya skuli hiyo.

### 3.6.1 TAARIFA YA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI

**Taarifa ya Mapato na Matumzi**

Baraza la Mji Mkoani limeingia Mkataba wa ujenzi na Kampuni ya Ujenzi ya M & J wenye nambari ya kumbukumbu BMM/U.H/82/VOL.1/3 kwa thamani ya shilingi 353,535,658.02 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za mradi huo ambapo kiasi cha shilingi 56,660,000 zimechangiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kiasi cha shilingi 294,571,138.81 zimechangiwa na Ubalozi wa Japan nchini Tanzania.

**MATOKEO YA UCHUNGUZI**

#### 3.6.1.1 Kutokuwasilishwa kwa makato ya kodi ya zuio la kodishilingi 52,838,925

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 52,838,925 ni fedha za makato ya zuio la kodi ambayo hayakuwasilishwa na Baraza la Mji

Mkoani katika mamlaka za kodi husika ZRB yaliyotokana na kazi za ujenzi wa Dakhalia kwa mujibu wa hati za malipo husika.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba malipo ya fedha zinazotokana na utekelezaji wa miradi yanafanyika kulingana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbalimbali iliyopo.

**Mchanganuo wa malipo ya makato ya kodi ni kama inavyoonekana katika jadweli**

| **Tarehe** | **Maelezo** | **Kiasi cha fedha kilicholipwa kabla ya kodi (Tshs)** | **Kodi iliyokatwa (VAT 18% to ZRB)** | **Kiasi cha fedha kilicholipwa baada ya kodi (Tshs)** |
|---|---|---|---|---|
| 04/03/2020 | Malipo ya fedha kwa Kampuni ya M & J kwa ajili ya Ujenzi wa Dahalia ya wanaume katika Skuli ya Sekondari ya Moh'd | 17,319,458.85 | 2,641,951.35 | 14,207,827.26 |
| 25/06/2019 | | 79,985,524.15 | 12,201,181.65 | 65,615,243.54 |
| 09/04/2019 | | 54,144,477 | 8,259,327 | 45,885,150 |
| 1/10/2019 | | 42,231,138 | 6,442,038 | 34,643,848 |
| 26/11/2019 | | 28,884,807 | 4,406,157 | 23,695,333 |
| 21/08/2019 | | 47,242,952 | 7,206,552 | 38,755,235 |
| 24/05/2019 | | 24,240,000 | 3,697,650 | 20,131,650 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 21/05/2019 | Juma Pindua | 52,340,000 | 7,984,068 | 43,468,813 |
| **Jumla** | | **346,388,357** | **52,838,925** | **286,403,099.8** |

**Majibu ya Baraza**

Kwa mujibu wa mkataba uliosainiwa kati ya Baraza la Mji Mkoani na Ubalozi wa Japan, ulikuwa unazuia kutumia fedha za ufadhili huu kulipia kodi ya aina yoyote ya Serikali ambayo itagharimu za mfadhili kwa ajili ya ujenzi huo. Kifungu (7) kinaeleza: "not to use grant fund for the items which are not mentioned in the annexure to the grant contract or for the payment of the othercharges such as bank charges and taxes including value added tax VAT".

Kwa maana hiyo Baraza likachukua hatua ya kuandika barua kwenda kwa Mkuu wa Mkoa yenye kumbukumbu namba SMZ/BMM/08/MK/VOL.I/55/151 ya tarehe 24 Febuari, 2019 ambao ndio walikuwa wasimamizi wa Mabaraza ya Miji kwa ajili ya kuombewa msamaha wa kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) kutoka kwa taasisi ya ZRB.

Lakini kutokana na muda wa makubaliano ya fedha hizo za ujenzi kuwa ni mfupi ukilinganisha na urasimu wa kuomba na kupata msamaha wa kodi kutoka ZRB, Baraza la Mji Mkoani lilishauriwa na Serikali kuu kutekeleza mradi huo kuliko kuzirudisha fedha kwa mfadhili wakati wanafunzi wana mahitaji ya Bweni la kulala.kwa hiyo Baraza liliendelea na utekelezaji wa mradi huo.

Hata hivyo, kodi nyengine zote ambazo zilikuwa haziathiri fedha za Mfadhili kama vile zuio la kodi ya mapato (Income Tax) ambayo inamruhusu mkandarasi

pekee ilizuiwa na kuwasilishwa TRA kwa mujibu wa utaratibu na vielelezo vyake vipo.

### 3.6.1.2 Kutokutayarisha na kuwasilisha taarifa za hesabu za miradi.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha sheria nambari 12 ya usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016 inawataka wakuu wa Taasisi kutayarisha taarifa za mapato na matumizi na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilikakwa matumizi.

Ukaguzi umebaini Baraza la Mji Mkoani limetekeleza Mradi wa ujenzi wa Dakhalia ya wanafunzi wa kiume katika Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua katika eneo la Mkanyegeni Wilaya ya Mkoani ambapo kwa mujibu wa taarifa za matumizi zinazohusiana na utekelezaji wa mradi huo kwa lengo la kukaguliwa na kutolewa ushauri wa kitaalamu, hadi ukaguzi unakamilika taarifa hizo hazikuwasilishwa jambo ambalo limenyima fursa ya kuweza kufahamu fedha halisi iliyopatikana na kutumika katika shughuli za uendeshaji na utekelezaji wa mradi huo.

**Majibu ya Baraza**

Baraza la Mji Mkoani lilikuwa linatayarisha taarifa zake za miradi kila baada ya miezi mitatu, miezi sita na za mwaka na kuziwasilisha ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Wizarani kama bango kitita na kutayarisha taarifa zote za hesabu za mwaka na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyo utaratibu.

Hata hivyo, Baraza la Mji Mkoani linakubaliana na mapendekezo ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu WA Hesabu za Serikali kuwasilisha taarifa za kila miezi mitatu katika Ofisi yake.

**3.6.1.3 Ujenzi wa Dakhalia kinyume na Mkataba**

Baraza la Mji Mkoani limeingia Mkataba wa Ujenzi wa Dahalia iliyojengwa katika Skuli ya Sekondari ya Moh'd Juma Pindua iliyopo Wilaya ya Mkoani Pemba lakini baadhi ya vipengele katika BOQ haviendani na uhalisia wa ujenzi uliyofanyika.

Kufanyika ujenzi usioendana na BOQ ya mkataba kunaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama za ujenzi, ambapo ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba pamoja na sheria nambari 11 ya ununuzi na uondoshsji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Braza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba miradi yote inapaswa kusimamiwa kwa mashirikiano ya karibu na Mkandarasi wa ujenzi ili utekelezaji wa mradai huo uende sambamba na makubaliano ya mkataba wa ujenzi.

**Mchanganuo wa kazi za ujenzi zilizofanyika kinyume na BOQ ni kama zinavyonekana katika jadweli**

| **Nam.** | **Kazi iliyofanywa** | **Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs)** | **Baadhi ya dosari zilizobainika** |
|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa paa na Silingi<br>(Roofing and Ceiling) | 32,877,500 | Bati zisizozidi 350 zimetumika kuezekea dahalia hiyo ambapo hazifikii idadi ya bati 540 zilizostahiki kununuliwa na kutumika kwa mujibu wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | B.O.Q |
| 2. | Utiaji wa madirisha na Milango (Doors and Windows) | 25,670,000 | Madirisha yametengenezwa kwa vyuma badala ya mbao ambapo ni kinyume na B.O.Q ya ujenzi huo. |
| 3. | Kazi za Umeme (Electrical works) | 21,098,000 | Taa aina ya Florescent light 16 pcs ambazo zimeingizwa kwenye B.O.Q hazikuonekana katika jengo husika |
| 4. | Mfumo wa maji safi na maji taka (Plumbing and Drainage) | 14,175,000 | Thamani ya ununuzi wa tankila kuhifadhia maji la lita 2000 lenye thamani ya shilingi 4,700,000 kwa mujibu wa B.O.Q ni kubwa ukilinganisha nabei husika za tanki hizo |
| 5. | Malipo ya Kodi (Tax Payments) (18%VAT) | 58,186,350 | Hati za malipo ya kodi pamoja na baadhi ya vielelezo vya ulipaji kodi hizo vimekosekana kwa ukaguzi |
| 6. | Malipo ambayo yalistahiki kubakia bila kulipwa kwa muda ulioelekezwa kisheria (Retention money) | 35,353,565 | Malipo yote ya Mkandarasi yamelipwa kabla ya kipindi chamajaribio kukamilika. |

**Majibu ya Baraza**

Baraza la Mji Mkoani liliingia Mkataba wa Ujenzi wa Dahalia iliyojengwa katika Skuli ya sekondari ya Mohd Juma Pindua iliyopo Mkanyageni Mkoani Pemba, ambapo Baraza kwa upande wake lilikuwa linasimamiwa na mshauri elekezi kutoka Wizarani Eng. Khamis Mtara ambae aliteuliwa na Ubalozi wa Japan kulingana na uwezo wake ambao wafadhili hao wanautambua kwa uzoefu wa kazi mbali mbali alizozifanya.

Kwa hiyo malipo yote ambayo yalikuwa yalikuwa yanafanyika yalikuwa yanaendana na certificate ambazo zilikuwa zinatayarishwa kwa mujibu wa BOQ ya kazi husika, kutoka awali kazi inaanza mpaka kukamilika kwake.

Kwa mantiki hiyo hakuna ujenzi wowote uliofanyika kinyume na makubaliano ya mkataba. Aidha mabadiliko madogo madogo katika ujenzi wa kisasa kama wa ukumbi wa umoja ni nguvu yanaweza kufanywa kwa ajili ya maboresho ya kazi na sio kwenda kinyume na mkataba.

Hata hivyo, hoja kwamba malipo ya mwisho ambayo yalitakiwa kulipwa baada ya muda wa majaribio yalilipwa kabla ya kipindi hicho kumalizika haikuwa sahihi.

Fedha za mwisho zililipwa baada ya miezi sita baada ya kazi kukamilika na kufunguliwa na Ubalozi wa Japani kwa ajili ya matumizi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati ya LAAC katika kufuatilia hoja za Ripoti hii haikupata majibu ya kuridhisha kutoka kwa Baraza la Mji Mkoani kwa madai kuwa Watendaji waliokuwepo katika Baraza hilo kwa kipindi ambacho Kamati inafanya uchunguzi wake ni wapya hivyo, Watendaji hao hawakuwa na majibu ya kutosheleza.

Kwa msingi huo, hoja zote za Ripoti hii zimabaki kama zilivyokuwa kwa kuwa Kamati haikupata muda wa ziada wa kuwaita Watendaji wote waliohusika na hoja hizo.

**MRADI WA UJENZI WA UKUMBI WA MIKUTANO WA UMOJA NI NGUVU PEMBA.**

Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu ni mradi ambao umesimamiwa na Baraza la Mji Mkoani na umetekelezwa kutokana na agizo la Rais mstaafu wa Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Moh'd Shein kuhakikisha kwamba Baraza la Mji Mkoani linajenga ukumbi wa mikutano ambao utaweza kuondosha changamoto zinazojitokeza katika kipindi cha kufanya mikutano na kuepuka kuingia gharama za kukodi ukumbi katika maeneo yasiokuwa rasmi.

**MLENGO YA MRADI**

Lengo la kuanzishwa kwa mradi huu ni pamoja na kupunguza changamoto za upatikanaji wa ukumbi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mikutano zinazohitaji matumizi ya ukumbi wenye ubora na uwepo wa nafasi yenye kujitosheleza pia kukamilika kwa ukumbi uliokusudiwa ni moja ya chanzo cha upatikanaji wa mapato ya Baraza la Mji Mkoani, kutokana na ukodishwaji wa ukumbi huo kwa ajili ya shughuli mbali mbali za kijamii.

**TAARIFA ZA FEDHA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MRADI**

**Taarifa ya Mapato na Matumizi**

Mradi huu umetekelezwa kwa kutumia wakandarasi wawili katika awamu mbili tofauti kama ifuatavyo:-

- Zenji Building ambaye alisaini mkataba wenye namba ya kumbu kumbu SMZ/BMM/Q/2018-2019/002 kwa jumla ya shilingi 286,604,890 pamoja na VAT ambapo katika mkataba huo mkandarasi alitakiwa kuanza ujenzi kwa hatua za awali hadi katika hatua za uwezekaji.

- Chuo cha Mafunzo ambaye alisaini mkataba wenye namba ya kumbu kumbu SMZ/BMM/DP/2018-2019-02 kwa jumla ya shilingi 386,137,890 pamoja na VAT ambapo katika mkataba huo mkandarasi alitakiwa kuanza ujenzi kwa hatua za umaliziaji hadi kukamilika kwa kazi za ujenzi na kukabidhi ukumbi kwa ajili ya matumizi.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 4.3.2.1 Mambo yaliyobainika katika ujenzi wa ukumbi wa Umoja ni Nguvu

Kazi za ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu zilitekelezwa na wakandarasi ambao ni Zenji Building pamoja na Chuo cha Mafunzo katika vipindi vya awamu mbili tofauti ambapo katika hatua za ujenzi huo mambo mbali mbali yalibainika kama ifuatavyo:-

Kutokufuatwa kwa utaratibu wa utowaji wa zabuni ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa ukumbi.

Kutokufuatwa kwa utaratibu wa utoaji wa zabuni ya kuwapata wakandarasi katika ujenzi wa uzio.

Kutokuwepo kwa vipengele vya adhabu ndani ya mikataba ya ujenzi.

Kutokufuatwa kwa utaratibu katika hatua za kumpata mshauri elekezi.

Kutokuwepo kwa uthibitisho wa makubaliano ya nyongeza ya kazi.

Kukosekana kwa vyeti vya malipo (certificate of completion).

**Majibu ya Baraza**

Baraza la Mji Mkoani lilifuata taratibu zote wa kumpata mkandasi Zenji Building Construction kwa hatua ya mwanzo wa ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu ikiwemo utoaji wa zabuni za kazi hiyo.

Kuhusu mkandarasi wa pili wa ujenzi huu alipatikana kufuatia uharaka wa uhitaji wa ukumbi kwa ajili ya kuendelesha shughuli za kiserikali na kwa dhamira ya kupunguza gharama Uongozi wa Baraza ukawatafuta Magereza kwa kigezo cha direct procurement ili afanikishe dhamira ya serikali ya kupatikana kwa ukumbi huo.

Kuhusu kutofutatwa kwa taratibu za kuwapata wakandarasi wa uzui ni kweli kwamba hakukuwa na makubaliano yoyote ya kimkataba yaliyoingiwa na Baraza la Mji Mkoani kazi ya Ujenzi wa uzuio.

Hatua hii ilikuja baada ya ziara mbali mbali za viongozi walizokuwa wakizifanya wakati ujenzi huu unaendelea na kushauri umuhimu wa kujengwa kwa uzio huo kwa maslahi mapana ya kuihifadhi ukumbi huu na changamoto mbali mbali za kiusalama.

Hivyo Baraza likashauriana na Magereza kuifanya kazi hiyo. Katika ujenzi huu Baraza la Mji Mkoani lilimtumia wakala wa Serikali wa majengo ZBA kuwa mshauri wa mradi huo

### 4.3.2.2 Kutokukamilika kwa kazi za ujenzi wa ukumbi

Barara la Mji Mkoani limeingia mikataba ya ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano yenye jumla ya shilingi 672,742,780 na Wakandarasi ambao ni Zenji Buildingna Chuo cha Mafunzo kwa awamu mbili tofauti kwa mkataba nambari SMZ/ BMM/Q/2018-2019/002 wenye jumla ya shilingi 286,604,890 pamoja na kodi na mkataba nambari SMZ/BMM/DP/2018-2019/02 wenye jumla ya shilingi

386,137,890 pamoja na kodi.

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Chuo cha Mafunzo ambae ni mkandarasi wa awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi alipaswa kukamilisha kazi aliyopangiwa ndani ya tarehe 13/12/2019 lakini hadi ukaguzi unakamilika mkandarasi huyo ameshindwa kukamilisha ujenzi na hivyo kupelekea mradi huo kutokamilika kwa wakati, ambapo imebainika kwamba baadhi ya kazi zenye thamani ya shilingi 100,000,000 zimeshindwa kukamilishwa licha ya mkandarasi huyo kulipwa fedha zote zilizoainishwa katika mkataba hali ambayo imesababisha kutokupatikana kwa tija inayotokana na malengo ya kuanzishwa kwa ujenzi huo.

Aidha, ukaguzi umeshindwa kuona vielelezo vya kuomba na kukubaliwa kuongezewa muda wa utekelezaji wa mkataba wa mradi huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba miradi yote wanayopaswa kuisimamia wanashirikiana kwa pamoja na wakandarasi iliutekelezaji wa miradi hiyo uende sambamba na mikataba ya ujenzi.

**Majibu ya Baraza**

Ni kweli kwamba mkandarasi wa pili wa ujenzi wa umoja ni nguvu ambae ni Chuo cha mafunzo Zanzibar hajakamilisha kazi ya ujenzi wa ukumbi wa umoja ni nguvu kama ilivyokubaliwa katika mkataba, ukweli wa hoja hii ilitokana na sababu zifuatazo:

i. Kuwepo kwa mripuko wa ugonjwa wa uviko19: katika kipindi cha utekelezaji wa kazi hiyo kulitokea mripuko wa ugonjwa hatari wa kuambukiza COVID 19 hapa nchini mnamo mwezi wa Machi 2020 na kuchukua zaidi ya miezi minne (4) iliyosababisha baadhi ya shughuli

zenye mkusanyiko kupigwa marufuku jambo lililopelekea kusita kwa kazi kwa kipindi

ii. Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar Oktoba 2020: harakati za uchaguzi ambazo iliwalazimu kwa sababu wao ni walinzi wa Taifa, walilazimika kushiriki katika shughuli za ulinzi katika kipindi cha uchaguzi na hivyo kushindwa kumalizia kwa wakati kama ilivyotarajiwa katika ujenzi huo.

iii. Aidha pamoja na maelezo hayo ofisi ya Baraza la Mji Mkoani inayachukua na kuyazingatia mapendekezo na ushauri wa Ofisi ya Mdhibitii na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali wa kusimamia mikataba kwa umakini.

**4.3.2.3 Ujenzi wa Ukumbi kinyume na makubaliano ya mkataba**

Baraza la Mji Mkoani limeingia mkataba wa ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu uliojengwa katika Wilaya ya Mkoani Pemba lakini baadhi ya vipengele katika BOQ haviendani na uhalisia wa ujenzi ulivyofanyika.

Kufanya ujenzi usioendana na B.O.Q ya Mkataba kunaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama za ujenzi, ambapo ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba pamoja na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba miradi yote wanayopaswa kuisimamia wanashirikiana kwa pamoja na wakandarasi ili utekelezaji wa miradi hiyo uende sambamba na makubaliano ya mikataba ya ujenzi.

Mchanganuo wa kazi za ujenzi zilizofanyika kinyume na BOQ ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

| Na | Maelezo ya kazi za ujenzi | Kazi zilizoainishwa katika mkataba | Kazi halisi zilizotekelezwa | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ununuzi wa Milango Mikubwa (Zanzibar Doors) | Mlango 1 | Milango 10 | Milango 9 |
| 2. | Urefu na upana wa ukumbi | Urefu mita 34<br>upana mita 15 | Urefu mita 38<br>Upana mita 19.4 | Urefu mita 4 na upana<br>mita 4.4 |
| 3. | Ununuzi wa Jipsumboard | 550pcs | 300pcs | 250pcs |
| 4. | Ununuzi wa Cornices | 420pcs | 250pcs | 170pcs |
| 5. | Ujenzi wa Uzio wa thamani ya shilingi 87,775,475 | Haumo | Umejengwa | Kujengwa |

**Majibu ya Baraza**

Katika ujenzi mkubwa kama ule wa ukumbi na kuboresha ujenzi wa majengo makubwa ya kisasa mabadiliko huwa ni vitu ambavyo haviwezi kuepukika na yanatakiwa kufanyika kwa sababu mbili kubwa. Moja kuboresha kazi inayoendelea na ya pili mabadiliko hayo yasiathiri lengo la msingi la kazi husika, ndio maana katika kazi nyingi za ujenzi pamoja na mikataba na BOQ inayotumika vilevile maelezo ya mteja katika kuboresha kazi hiyo

yanazingatiwa.

Hata hivyo, kwa miradi ya serikali ziara mbali mbali za viongozi wa serikali zinaacha mapendekezo ambayo kwa namna moja ama nyengine lazima kuyatekeleza. Kwa msingi huo ndio maana kwa mfano milango mikubwa ya Zanzibar doors imekuwa kumi (10) badala ya mmoja au kumekua na uzio badala ya kutokua na uzio kama ilivyo kwenye BOQ.

**4.3.2.4 Kutokukatwa kwa kodi ya zuio shilingi 19,333,234.56**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 19,333,234.56 ni fedha za kodi ambazo hazikukatwa na Baraza la Mji Mkoani kwa ajili ya kazi za ujenzi wa ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu kulingana na mikataba ya ujenzi huo ambapo kupitia mikataba hiyo jumla ya makato ya kodi ya zuio yaliyostahiki kukatwa wakandarasi ni shilingi 138,796,470.36 lakini makato halisi yaliyofanyika kupitia hati za malipo ni shilingi 119,463,236.2 na kupelekea uwepo wa tofauti ya makato ya kodi ya zuio kama ilivyobainishwa hapo juu.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba malipo ya fedha zinazotokana na utekelezaji wa miradi yanafanyika kulingana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

**Majibu ya Baraza**

Kwa mijibu wa malipo yaliyofanywa na Baraza la Mji Mkoani kwa kazi za ujenzi wa ukumbi wa Umoja ni Nguvu zinaonesha kuwa hati zote za malipo zimekatwa kodi za zuio kwa kufuata utaratibu wa kodi hiyo, kwa hiyo

hakuna kodi ya Shilingi 19,333,234.56 ambayo haikukatwa.

### 4.3.2.5 Kutokuwasilishwa kwa makato ya kodi ya zuio shilingi 21,272,771.62

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 21,272,771.62 ni fedha za makato ya kodi ya zuio ambayo hayakuwasilishwa na Baraza la Mji Mkoani katika mamlaka za kodi husika yaliyotokana na kazi za ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu.

Kwa mujibu wa hati za malipo husika, fedha walizokatwa wakandarasi wa ujenzi huo ni jumla ya shilingi 119,463,236.2 ambazo zilitakiwa kuwasilishwa katika mamlaka husika za kodi, lakini kodi halisi iliyowasilishwa ni shilingi 98,190,464.58 na kupelekea uwepo wa tofauti ya makato ya kodi ya zuio ambayo hayakuwasilishwa.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba malipo ya fedha zinazotokana na utekelezaji wa miradi yanafanyika kulingana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

**Majibu ya Baraza**

Kodi zote za zuio zilizokatwa wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Ukumbi wa Umoja ni Nguvu Mkoani ziliwasilishwa kwa Mamlaka husika kama zilivyoanishwa katika hati za malipo ya kodi hizo. Kwa maana hiyo hakuna kodi ya shilingi 21,272,771.62 ambazo hazikuwasilishwa kwa mamlaka husika.

#### 4.3.2.6 Uwepo wa malipo ya ziada kwa mkandarasi shilingi 8,212,936.32

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 8,212,936.32 ni fedha za malipo ya ziada aliyolipwa mkandarasi wa ujenzi Zenji Construction Co. Ltd kwa ajili ya ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu. Kwa mujibu wa mkataba mkandarasi huyo alistahiki kulipwa jumla ya shilingi 227,445,497.68 baada ya kodi, lakini fedha halisi alizolipwa ni shilingi 235,658,434 na kupelekea uwepo wa tofauti ya malipo ya ziada kama yalivyobainishwa hapo juu.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba malipo ya fedha zinazotokana na utekelezaji wa miradi yanafanyika kulingana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

**Majibu ya Baraza**

Hakuna malipo ya ziada ya TZS 8,213,329.32 yaliyolipwa kwa zenj building kama ilivyoanishwa katika taarifa ya ukaguzi, hii inatokana na ukweli kwamba kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi uliofungwa kati ya Baraza la mji Mkoani na Zenj building contractors wa TZS 286,604,890.00, mchanganua wa malipo hati za malipo ilikuwa kama ifuatavyo:

| Hati Namba | Tarehe | Malipo |
|---|---|---|
| 2/6 | 03/06/2019 | Tsh 143,302,445.00 |

| | | |
|---|---|---|
| 84/7 | 26/07/2019 | Tsh 94,911,136.35 |
| 33/9 | 02/09/2019 | Tsh 47,200,000.00 |

#### 4.3.2.7 Kutokufanyika kwa malipo yatokanayo na ujenzi shilingi 23,911,583.56

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 23,911,583.56 ni fedha ambazo zilizopaswa kulipwa kwa ajili ya kazi za ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Umoja ni Nguvu katika Wilaya ya Mkoani Pemba. Kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi mkandarasi ambaye ni Chuo cha Mafunzo alistahiki kulipwa jumla ya shilingi 306,500,811.56 malipo baada ya kodi, lakini fedha halisi alizolipwa ni shilingi 295,934,228 na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 10,566,583.56.

Aidha, malipo ya Mshauri Elekezi kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi ni shilingi 18,000,000 lakini fedha halisi alizolipwa ni shilingi 4,655,000 na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 13,345,000 hali ambayo inaweza kusababisha kukosekana kwa ufanisi katika usimamizi na ufuatiliaji wa kazi za ujenzi, pamoja na kwamba katika ufuatiliaji wa mwenendo wa utekelezaji wa mradi na ufanisi wa uingizwaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi pamoja na malipo stahiki kwa mshauri elekezi imebainika kwamba fedha zote zilizostahiki kwa ajili ya ujenzi huo zimeingizwa na kutumika kwa asilimia 100 na kwa kuzingatia wakati uliopangwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kwamba malipo ya fedha zinazotokana na utekelezaji wa miradi yanafanyika kulingana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

**Majibu ya Baraza**

Hakuna malipo pungufu yaliyofanywa kwa Magereza ya TZS 23,911,583.56 hii inatokana na ukweli kwamba kwa mujibu wa BOQ na mkataba wa ujenzi uliofungwa kati ya Baraza la mji Mkoani na Chuo cha mfunzo wa TZS 386,137,890.00(pamoja na VAT) ulikuwa na sehemu mbili, TZS 364,897,890.00 kwa Chuo cha mafunzo kwa ajili ya ujenzi na TZS 21,240,000.00 kwa bodi ya ushauri wa majengo ya serikali (ZBA).

Mchanganuo wa malipo kwa chuo cha mafunzo ulifanyika kama ifuatavyo:

| **Hati Namba** | **Tarehe** | **Kiwango** |
|---|---|---|
| 68/2 | 24/02/2020 | Tsh. 227,821,355.10 |
| 21/7 | 22/07/2020 | Tsh. 137,076,534.90 |
| **JUMLA** | | **TSH. 364,897,890.00** |

### 4.3.2.8 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 4,655,000

Katika ukaguzi uliyofanyika imebainika kuwepo kwa malipo yenye jumla ya shilingi 4,655,000 zilizolipwa na Baraza la Mji Mkoani kwa Mshauri Elekezi wa Ujenzi wa ukumbi wa Umoja ni Nguvu uliopo katika Wilaya Mkoani Pemba ambapo malipo hayo yamefanyika kwa kupitia hati ya malipo nambari 1/8 ya tarehe 22/7/2020 lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha malipo yote yanayofanyika ni lazima yaambatanishwa na vielelezo husika ili kuendana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

**Majibu ya Baraza**

Vielelezo kwa ajili ya malipo hayo yaliyotajwa ya Sh 4,655,000 yaliyolipwa kwa ZBA vipo na vimeambatanishwa na vocha husika.

### 4.3.2.9 Kukosekana kwa hati za malipo kwa ajili ya ukaguzi shilingi 38,394,260.17

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Barara la Mji Mkoani limeingiziwa jumla ya shilingi 672,742,780 kwa ajili ya Ujenzi wa Ukumbi wa Umoja ni Nguvu kutoka Wizara ya Nchi, (OR), Fedha na Mipango Pemba ambapo katika ufuatiliaji wa fedha hizo imebainika fedha halisi zilizoandaliwa hati za malipo na kukaguliwa ni shilingi 634,348,519.83 hivyo kupelekea uwepo wa tofauti ya fedha jumla ya shilingi 38,394,260.17 ambazo hati za malipo pamoja na vielelezo vinavyothibitisha kufanyika kwa malipo hayo zimekosekana kwa ajili ya ukaguzi na kupelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha malipo yote yanayofanyika ni lazima yaambatanishwe na vielelezo husika ili kuendana na matakwa ya sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo.

**Malipo ya fedha yaliokosekana kwa ukaguzi**

| Maelezo | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|
| **Fedha zilizoingizwa (A)** | **672,742,780** |
| **Fedha zilizotumika** | |
| Zenji Building Construction Limited | 235,568,827 |
| Chuo cha Mafunzo | 295,934,228.25 |
| Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) | 92,012,258.34 |
| Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) | 6,178,206.24 |
| Wakala wa Majengo (ZBA) | 4,655,000 |
| **Jumla ya fedha zilizotumika (B)** | **634,348,519.83** |
| **Fedha zilizokosekana kwa ukaguzi (A-B)** | **38,394,260.17** |

**Majibu ya Baraza**

Baraza la Mji Mkoani lilipokea jumla ya TZS 631,441,640.00 kutoka Wizara ya fedha na Mipango kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi wa umoja ni nguvu mkoani na sio TZS 672,742,780 kama inavyodaiwa katika taarifa ya ukaguzi. Naomba ikumbukwe kwamba TZS 672,742,780 ni thamani tu ya mikataba yote miwili ya ujenzi yaani TZS 286,604,890.00 kwa Zenj Building Contractors na TZS 386,137,890.00 kwa Magereza.

Mchanganuo wa fedha hizo kutoka Wizara ya Fedha ilikuwa kama ifuatavyo:

| NAM. | MWEZI NA MWAKA WA MAPOKEZI YA FEDHA | KIWANGO CHA FEDHA (TZS) |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | MEI, 2019 | 245,303,750.00 |
| 2. | JANUARI, 2020 | 200,000,000.00 |
| 3. | JULAI, 2020 | 186,137,890.00 |
| **JUMLA YA FEDHA** | | **631,441,640.00** |

Kwa hiyo ili kukamilisha fedha zote za mkataba wa awali uliofungwa na kati ya Zenj Buiding contractors wa TZS 286,604,890.00 Baraza lilipokea TZS 245,303,750 tu kutoka wizara ya fedha na hivyo basi Baraza lilitakiwa kuchangia kiasi kilichobaki kwa ajili ya ujenzi huo katika kikao kilichofanyika kati ya Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani na Maafisa wa Wizara ya Fedha Unguja na baraza lilifanya hivyo. Kwa sababu vocha zote za malipo walizolipwa wakandarasi wote wawili zilionekana wakati wa ukaguzi kama zilivyoanishwa na Mkaguzi katika majadweli yaliyopita ya taarifa yake, kwa hiyo hakuna fedha ambayo imekosekana kwa ajili ya ukaguzi.

Hata hivyo Baraza la Mji Mkoani linapokea mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati.**

Kwa ujumla Kamati ya LAAC wakati inafuatilia hoja za Ripoti hii haikupata majibu ya kuridhisha kutoka kwa Baraza la Mkoani kwa hoja namba 1, 2 na hoja namba 3 kwa madai kuwa Watendaji waliokuwepo katika Baraza hilo kwa kipindi ambacho Kamati inafanya uchunguzi wake ni wapya, hivyo, Watendaji hao hawakuwa na majibu ya kutosheleza.

Kwa kuwa Ripoti hii inatarajiwa kuwasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Baraza unaotarajiwa kuanza tarehe 13 Septemba, 2023, hivyo, Kamati haikupata muda wa ziada wa kuwaita Watendaji wote waliohusika na hoja

hizo.

Kwa msingi huo, Kamati ilishindwa kuendelea kufuatilia hoja hizo, hivyo, hoja zote zinazohusiana na Ujenzi wa Ukumbi wa Umoja ni Nguvu zimebaki kama zilivyo.

## 4.6 MFUMO WA ECONEX KATIKA BARAZA LA MANISPAA MJINI

### MATOKEO YA UKAGUZI

### 4.6.1 Dosari katika Mikataba iliyofungwa baina ya Baraza la Manispaa ya Mjini na kampuni ya ECONEX.

Baraza la Manispaa Mjini limefunga mkataba na ECONEX COMPANY LTD tarehe 9/8/2019 wa muda wa miaka mitatu kwa ajili ya kuitaka kampuni ya ECONEX kukusanya mapato ya maegesho ya vyombo vya moto kwa niaba ya Baraza katika maeneo ya Manispaa ya Mjini Unguja kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

Mkataba huu uliitaka kampuni ya ECONEX kukusanya kiasi kisichopungua shilingi 321,120,000 kwa kila mwezi ambapo kati ya fedha hizo, kwa mwaka wa kwanza Baraza lilipanga kuchukuwa mgao wa asilimia 45 na ECONEX kuchukuwa asilimia 65. Kwa mwaka wa Pili na wa Tatu Baraza lilipanga kuchukuwa mgao wa asilimia 60 na ECONEX kuchukuwa asilimia 40. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari mbali mbali katika mkataba huo kama zifuatazo:-

#### 4.6.1.1 Kutoainishwa kwa Nambari ya Hesabu ya Benki ya Mapato ya Baraza.

Ukaguzi umebaini kwamba Mkataba wa awali uliofungwa baina ya Baraza na ECONEX haukuainisha Nambari ya Hesabu ya Benki ya Mapato (Revenue Bank Account Number) ya Manispaa Mjini iliyotarajiwa kutumika kukusanyia mapato ya maegesho ya vyombo vya moto. Hali hii imeweza kupelekea mwanya wa kupotea kwa mapato ya Serikali kwa kuingizwa mapato ya maegesho katika nambari za hesabu za benki (Bank Account Number) zisizokusudiwa kwa ajili ya

Mapato ya Baraza la Manispaa ya Mjini na hatimae kuisababishia hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri kuainishwa kwenye Mkataba na kutumika hesabu ya mapato ya Baraza kwa ajili ya kuweka makusanyo yote ya tozo za maegesho ya vyombo vya moto kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya Serikali kwa lengo la kuepusha fedha za mapato kupotea na kuisababishia hasara Serikali.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli mkataba wa awali haukuwa na nambari ya akaunti hata hivyo, mapato yalikuwa yakiingia katika akaunti ya mapato ya Baraza la Manispaa 0404007000. Hii ilitokana na makubaliano baina ya Kampuni ya ECONEX na Baraza la Manispaa

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa akaunti iliyokuwa inatumiwa na Manispaa ya Mjini ambayo iliyooneshwa hapo juu haikuunganishwa moja kwa moja na mfumo wa kukusanyia mapato na hivyo mapato yote ya maegesho yalikuwa yakiingiingia kwenye akaunti ya ECONEX na kwa mujibu wa makubaliano yao ifikapo mwisho wa mwezi wanapokea gawio tu la asilimia walizokubaliana ambazo ndizo huingizwa katika akaunti ya Baraza la Manispaa Mjini yenye namba 0404007000

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Baraza la Manispaa Mjini kwa vile Mkataba na Kampuni ya ECONEX umekwisha basi ni vyema katika mikataba mengine yanayoingia kuhakikisha akaunti ya mapato ya Baraza inaunganishwa moja kwa moja na mfumo na makusanyo ya mapato kuingizwa katika akaunti ya Baraza na wao ndio wanaopaswa kutoa gawio kwenda kwa mmiliki wa mfumo na si vyenginevyo.

Kufanya hivyo kutapelekea Baraza kujua kiwango sahihi cha makusanyo kwa kila mwezi na kupata gawio lililosahihi, Aidha kutapelekea Baraza kupata baadhi ya maslahi ya kibenki ambayo Kampuni ya ECONEX huyapata kwa kutunza fedha za maegesho kwa kila mwezi katika akaunti yao.

**4.6.1.2 Kutoshirikishwa kwa watumiaji wa mfumo wa Baraza la Manispaa ya Mjini katika kutoa maoni na mahitaji yao wanayotaka yawemo ndani ya mfumo " User Requirements".**

Kwa mujibu wa viwango bora (Best Practise) vinaelekeza kwamba Taasisi inapotaka kubadilisha utoaji wa huduma kutoka njia ya kawaida (Manual) na kwenda kwa njia ya kielektroniki kupitia mifumo (Automate) inapaswa kushirikisha wadau wote watakaohusika na matumizi ya mfumo husika ili kuelewa mahitaji yao na kuyazingatia katika kutengeneza, kununua au kuanzisha mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kuhakikisha mahitaji yote ya utendaji kazi katika mfumo yanapatikana na kuboreshwa kwa lengo la kurahisisha kazi, kuongeza tija na kuleta ufanisi.

Ukaguzi umebaini utaratibu mzima wa kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki ndani ya Baraza la Manispaa Mjini haukua shirikishi kwa wadau wake ambao ni wafanyakazi wanaotarajiwa kuutumia mfumo huo kwa kupata taarifa za mapato ya maegesho, ambapo wafanyakazi hao hawakushirikishwa katika kuandaa mahitaji ya mfumo ambayo yangezingatiwa na kuingizwa katika Mkataba wa utoaji wa huduma za makusanyo ya maegesho ya vyombo vya moto kwa njia ya kielektroniki kutoka Kampuni ya ECONEX , vile vile kutokupatiwa mafunzo ya kutosha katika matumizi ya mfumo husika (intensively user trainings).

Hali hii imepelekea kujitokeza kwa dosari mbali mbali za kiutendaji kwa upande wa watumiaji wa mfumo wa makusanyo ya maegesho katika Baraza

la Manispaa ya Mjini. Baadhi ya dosari ni kama zifuatazo: -

- Mtumiaji wa mfumo kutoka Baraza hawezi kuzitoa ripoti za mapato kutoka katika mfumo kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za makusanyo ya mapato kwa siku, kwa wiki au kwa mwezi kutokana na mahitaji ya Baraza.
- Taarifa za makusanyo ya mapato ya vyombo vya maringi mawili na matatu kama vile Boda boda, Bajaji n.k hazipatikani katika mfumo, hivyo afisa mapato wa Baraza hawezi kuona na kujua mapato halisi ya vyombo yanayokusanywa na ECONEX na mgao halisi wa Baraza kutokana na mapato hayo.
- Watumiaji wa mfumo katika kitengo cha TEHAMA cha Baraza wanashindwa kuhifadhi taarifa za makusanyo zilizomo katika mfumo wa SLOTTEX ZANZIBAR (Lack of data Backup Process) kutokana na kutopata elimu na ruhusa kutoka kwa ECONEX kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za mapato kwa mujibu wa mkataba, hivyo Baraza limeshindwa kuthibitisha usalama wa taarifa za makusanyo katika mfumo na miundombinu inayotumika ikiwa kuna uwezekano kwa njia yoyote taarifa kupotea, kuharibika, kubadilishwa au kutumika kinyume na makubaliano kwa upande wa ECONEX.
- Afisa Mapato wa Baraza anaetumia mfumo kutofahamu madeni wanayodai ECONEX kwa vyombo vilivyokuwa havijalipa tozo ya maegesho.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Baraza la Manispaa Mjini ufanye utaratibu wa kushirikisha wadau na watumiaji wa mfumo (system users) katika kubaini mahitaji yao yote ya mfumo na kuainishwa katika mikataba na kuyazingatia kwenye mfumo husika kwa lengo la kuleta urahisi wa kazi, kuongeza tija na ufanisi kwa sasa na kwa mifumo itakayoanzishwa.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli kwamba wakati wa utaarishaji wa mfumo wa maegesho na kampuni ya ECONEX Baraza halikushirikishwa. Hata hivyo, Baraza litautekeleza ushauri huu na kwamba litahakikisha linashiriki katika utaarishaji na matumizi ya mfumo kwa mikataba inayofuata.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza la Manispaa Mjini limekiri kuwepo kwa dosari hiyo Kamati inalishauri Baraza kua makini wakati wa kufunga mikataba ya matumizi ya mifumo mbalimbali ya TEHAMA kwa kuhakikisha kuwa watumiaji wa mfumo wanashirikishwa ipasavyo katika hatua za awali na za mwisho za uandaaji wa mfumo ili mahitaji yao yote yazingatiwe kwa lengo la kuleta tija ya matumizi ya mfumo husika.

**4.6.1.3 Kutoainishwa umiliki wa mfumo baada ya kumalizika kwa muda wa Mkataba**

Ukaguzi umebaini kwamba Mkataba uliofungwa baina ya Baraza na ECONEX wa makusanyo ya maegesho ya vyombo vya moto kwa kutumia mfumo wa kielektroniki haukuainisha umiliki wa mfumo kama utakua mali ya Baraza au ECONEX baada ya kumalizika muda wa mkataba unaoendelea sasa.

Kwa kuzingatia malipo anayoyapata mtoa huduma (asilimia 55 ya mapato ya maegesho kwa mwaka wa kwanza na asilimia 40 kwa miaka miwili ya mwisho) ilitarajiwa kwamba huduma (ECONEX) hupata gawio lake kama sehemu ya kurejesha gharama alizotumia kwa ajili ya kutengeneza mfumo na gharama nyingine za ziada alizotumia kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za ukusanyaji wa mapato ya maegesho ambapo mwisho wa mkataba mtoa huduma angemwachia Baraza mfumo ili aweze kuusimamia mwenyewe kwa mujibu wa taratibu zake.

Hata hivyo kutokana na mkataba uliofungwa kutoainisha kifungu hicho

muhimu ambacho kingeeleza kuwa mfumo utakua mali ya nani baada ya mtoa huduma kurejesha gharama zake, kuna uwezekano mkubwa kwamba mtoa huduma akaondoka na mfumo wake baada ya mkataba huo kumaliza muda.

Pindipo ikitokezea hivyo Serikali itakua imepata hasara kwa sababu inalipia gharama kubwa ya huduma ya mfumo tofauti na bei za huduma ya mifumo zilizopo sokoni kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa kwenye mikataba.

Ukaguzi unashauri kwamba, uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kwa upande wa Serikali na uongozi wa kampuni ya ECONEX kwa upande mwingine kukaa pamoja na kuweka utaratibu mzuri kwenye mkataba utakaozingatia maslahi ya Serikali katika umiliki wa mfumo huu ili kuepuka kuendelea kuisababishia hasara Serikali.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli kwamba mkataba uliofungwa baina ya Baraza la Manispaa na ECONEX kwa makusanyo ya maegesho haukuainisha mmiliki wa mfumo. Hata hivyo baada ya kumaliza kwa mkataba maegesho hayo yanasimamiwa na Baraza kwa kutumia mfumo wa Serikali wa MUTM.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Baraza limekiri kukosa kipengele cha umiliki wa mfumo baada ya Mkataba kuisha, hali hii ingesababisha Baraza kurudi katika utaratibu wake wa awali wa kukusanya mapato hayo kwa njia ya mkono, licha ya kuwa kwa sasa Baraza linatumia mfumo wa Serikali wa MUTM Kamati inalishauri Baraza kuzungumza na Uongozi wa Kampuni ya ECONEX katika kurejesha taarifa za Serikali ambazo zimo katika mfumo kwani taarifa hizo ni mali ya Serikali kitendo cha taarifa hizo kumilikiwa na Kampuni binafsi zinaweza kufanyiwa hujuma na kuleta madhara katika jamii.

#### 4.6.1.4 Kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya maegesho.

Ukaguzi umebaini kwamba Mikataba yote ya makusanyo ya mapato ya maegesho ya vyombo vya moto iliyofungwa baina ya Baraza la Manispaa ya Mjini na ECONEX haikuweza kufikia malengo ya makusanyo yaliyopangwa awali na haikuweza kubainisha vigezo sahihi vilivyotumika na kuonesha mchanganuo halisi wa makusanyo katika kufikia malengo yaliyopangwa.

Kwa mujibu wa mkataba wa awali wa makusanyo ya maegesho uliofungwa baina ya Baraza na ECONEX kifungu Nambari 10(a) kimeeleza kwamba kampuni ya ECONEX ilitakiwa kukusanya mapato yasiopungua shilingi 321,120,000 kwa mwezi. Baadae malengo hayo yakapunguzwa kwa asilimia 76 na kufikia shilingi 75,000,000 kupitia mkataba wa Nyongeza Nambari 1 na hatimae malengo haya yakaongezwa kwa zaidi ya asilimia 60, kutoka shilingi 75,000,000 na kuwa shilingi 189,625,000 kupitia mkataba wa Nyongeza Namba 2.

Kutokana na kutokuwa na vigezo sahihi katika upangaji wa malengo ya makusanyo ya mapato kumepelekea Baraza na ECONEX kutofikia malengo ya awali waliyokusudia kukusanya ambayo yalikuwa ni kuanzia shilingi 321,120,000 kwa kila mwezi.

Aidha hali hii imepelekea kusababisha usumbufu na hasara kwa Serikali kutokana na kuibuka kwa mikataba mingi isiyo na tija pamoja na kutolewa kwa barua nyingi za kubadilisha viwango vya makusanyo ambavyo viko nje ya utaratibu wa mikataba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kufanya tathmini ya maeneo ya maegesho ili kutambua athari za maeneo yasiyotozwa kwenye maeneo yanayotozwa na kufanya maamuzi sahihi kwa masilahi mapana ya Serikali, kuyaainisha maeneo yote kwenye mkataba pamoja na kuainisha vigezo vyote viliyotumika katika kufikia malengo ya makusanyo ya kila mwezi.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli kwamba mapato ya maegesho baina ya Baraza la Manispaa na Kampuni ya ECONEX hayakuweza kufikiwa kama ilivyoelezwa katika Mkataba , hii ilitokana na changamoto mbali mbali ikiwemo kuondoshwa kwa baadhi ya maeneo pamoja na kuishuka kwa bei kutoka shilingi 5,000/- hadi shilingi 3,000/- kwa siku kufuatia maelekezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ambayo yalitokana na Malalamiko ya wananchi yaliyopelekea kujadiliwa katika Baraza la wawikili na kumtaka Waziri huyo kurekebisho hali hiyo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika uchunguzi wa hoja hii imebaini kuwa Baraza halikuwa na tathmini halisi ya mapato kwa kila eneo la maegesho hali iliyopelekea kukadiria viwango vya makusanyo ambavyo si sahii katika mkataba na kupelekea kuleta changamoto kadhaa wakati wa utekelezaji na kusababisha kutokea marekebisho ya mara kwa mara ya mkataba katika kiwango cha makusanyo ya mwezi ambacho kilikadiriwa ni Tsh. 321,120,000 na hatimae kupungua hadi Tsh. 189,625,000.

Aidha Kamati imebaini kuwepo na maagizo mbalimbali ya viongozi wa Serikali juu ya mabadiliko ya bei za maegesho hata hivyo Kamati ilipohitaji vielelezo vya maagizo hayo havikuweza kupatikana kwa ukaguzi.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Baraza la Manispaa Mjini kupitia kitengo chake cha Mapato kufanya tathmini ya kila mwaka katika vyanzo vyake vyote vya mapato ili kuwa na taarifa sahihi ambazo zitaweza kusaidia wakati wa ukadiriaji wa mapato katika bajeti Aidha kuweza kukadiria makusanyo sahihi kwa mtoa huduma ambae watahitaji kufunga nae mkataba katika ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyao ili kuepusha mikataba hiyo kufanyiwa

marekebisho ya mara kwa mara.

Aidha maagizo yote yanayotolewa na viongozi wa Serikali juu ya uamuzi au mabadiliko ya jambo Fulani ambalo lipo kimkataba ni vyema yasiishie kwa njia mdomo tu badala yake kuwepo na uthibitisho wa kimaandishi ili kuhalalisha maagizo hayo.]

**4.6.1.5 Kukosekana kwa vifungu vinavyobainisha utaratibu wa kutoza na kukusanya fedha za faini kwa maeneo yasiyoruhusiwa kuegesha vyombo.**

Ukaguzi umebaini kwamba Mikataba iliyofunguwa baina ya Baraza na ECONEX haina vipengele vinavyozungumzia faini za maegesho pamoja na utaratibu wa ukusanyaji wa faini hizo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kuegesha vyombo.

Kutokuwepo kwa vipengele hivyo katika mikataba kunaweza kupelekea kupotea kwa mapato ya makusanyo ya faini husika kutokana na kukosa utaratibu na usimamizi mzuri wa makusanyo hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuchukua hatua zilizobora katika kulisawazisha jambo hili kupitia mkataba husika ili mapato yanayotokana na faini za maegesho yaweze kusimamiwa vizuri na kukusanywa kwa mujibu wa makubaliano ya pande zote mbili.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Mkataba uliofungwa baina ya Manispaa na Kampuni ya ECONEX haukuonyesha vipengele vinavyozungumzia faini za maegesho pamoja na utaratibu wa ukusanyaji wa faini hizo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa kuegesha vyombo, kwasababu utaratibu wa maeneo yasiyorasmi hawakuachiwa ECONEX kukusanya tozo badala yake tozo hizo zilikuwa zikikusanywa na Baraza kwa kutumia kanuni zake.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati ilidokezwa kuwa kukosekana kwa kipengele katika mkataba kimeisababishia Kampuni ya kuamua kujiingiza katika zoezi la kutoza faini katika maeneo yasio rasmi kinyume na makubaliano ya mkataba kutokana na watumiaji wa vyombo vya moto walishidwa kutozwa faini husika kwa mujibu wa kanuni ya Baraza na kuendelea kuegesha vyombo vya moto katika maeneo yasiyo rasmi na kuikosesha mapato Kampuni ya ECONEX, aidha kumepelekea kuibuka kwa vikundi vya kutoza faini katika maeneo ya Mjini ambavyo si wahusika wa Baraza la Manispaa ya Mjini wala Kampuni ya ECONEX.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Baraza kuhakikisha inazingatia vipengele muhimu katika mikataba ijayo ya maegesho ili kudhibiti changamoto mbalimbali ambazo zimejitokeza katika mkataba na Kampuni ya ECONEX ikiwemo kubainishwa kwa muhusika wa kutoza faini ambae atatekeleza majukumu yake ipasavyo kwa maslahi ya pande mbili za mkataba.

**4.6.1.6 Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa madeni ya makusanyo ya maegesho katika Mfumo wa SLOTTEX.**

Ukaguzi umebaini kwamba Mikataba ya makusanyo ya maegesho haikuzingatia utaratibu wa kufuatwa katika kufuatilia madeni kwa vyombo visivyolipa tozo ya makusanyo ya maegesho.

Hali hii imepelekea kampuni ya ECONEX kushindwa kufuatilita vizuri madeni kwa vyombo vinavyodaiwa tozo ya maegesho na hatimae kufuta au kubadilisha taarifa za madeni hayo kwenye mfumo bila ya kushirikisha Baraza la Manispaa ya Mjini.

Kutokuepo kwa utaratibu mzuri kunaweza kupelekea kupotea kwa taarifa muhimu za mapato ya maegesho kutokana na ufutwaji wa kiholela wa

madeni au ubadilishwaji wa taarifa za makusanyo katika mfumo na hatimae kusababisha hasara kwa mapato ya Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha mkataba unaonesha utaratibu wa kufuatwa katika kutunza, kubadilisha au kufuta taarifa yoyote kwenye Mfumo wa SLOTEX ZANZIBAR na kuweka utaratibu wa ushikirikishwaji wa Baraza katika kuidhinisha na kufanya mapitio ya taarifa za makusanyo katika mfumo kila mara (Regular System Review).

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baraza la Manispaa Mjini katika kufuatilia na kusimamia madeni lilikaa pamoja na Kampuni ya ECONEX kwa ajili ya kupanga utaratibu wa kuwalipisha wadaiwa wa madeni hayo, na hatimae maafisa wa Baraza kwa kushirikiana na ECONEX walifanya kazi ya kuwalipisha wadaiwa sugu ambao ni daladala na gari binafsi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya kuwa Uongozi wa Baraza na Kampuni ya ECONEX kufanya jitihada za kufuatilia madeni hayo lakini jitihada hizo hazikuweza kukamilisha ukusanyaji wa madeni kwa vile utaratibu huo ulikuwa ni mgumu kutokana na kufanya zoezi hilo kwa njia ya (manually)

Kamati inalishauri Baraza la Manispaa Mjini kushiriki ipasavyo wakati wa uandaaji wa mifumo ili kuweza kutoa mapendekezo juu ya namna mfumo utakovyoweza kutatua changamoto mbalimbali kama vile njia ya bora ufatiliaji wa madeni kwa wamiliki wa vyombo vya moto na badala yake zoezi hilo limefanywa kwa njia ya (manually) ambayo siyo fanisi kiutendaji na kuisababishia hasara Serikali.

#### 4.6.1.7 Kukosekana kwa usahihi wa taarifa katika vifungu vya Mkataba

Ukaguzi umebaini kwamba Kifungu Nambari 10(a) cha Mkataba wa makusanyo ya maegesho ya vyombo vya moto kinaeleza kwamba Mtoa huduma lazima awasilishe kiwango cha fedha za makusanyo ya ada za maegesho kwa kila mwezi kisichopungua shilingi Milioni Mia Tatu Ishirini na Moja Laki Moja na Ishirini Elfu (Tshs 321,120,000).

Kwa upande mwingine wa mkataba huo Kifungu Nambari 13 kinamtaka Mtoa huduma kuwasilisha fedha zote za ada ya maegesho kwa kila siku katika hesabu ya benki ya Baraza bila kuainisha kiwango.

Kutokana na maelezo yaliyopo hapo juu ukaguzi umeshindwa kufahamu utaratibu uliokusudiwa wa kuwasilisha mapato benki ikiwa mapato ya makusanyo ya maegesho yanatakiwa kuwasilishwa kila siku au kwa mwezi.

Hali hii inaweza kusababisha mtoa huduma kushindwa kuelewa utaratibu gani unaotakiwa wa kuwasilisha fedha za makusanyo benki ikiwa awasilishe fedha za makusanyo kila siku au kwa mwezi.

Aidha kifungu Nambari 14 kinaeleza kwamba iwapo mtoa huduma atachelewa kuwasilisha fedha za makusanyo ya siku, au unapomalizika mwezi husika kwa mujibu wa kalenda akawa hajawasilisha kiwango cha fedha za makusanyo ya ada za maegesho ya mwezi kwa kiwango kilichotajwa katika mkataba huu atakua na wajibu wa kulipa kiwango alichocheleweshwa kukiwasilisha na asilimia 2 ya kiwango alichochelewesha kwa kila siku ambayo atachelewesha kuwasilisha fedha hizo.

Ukaguzi unashauri kwamba uongozi wa Baraza la Manispaa na ECONEX upitie tena mkataba huo na kusawazisha dosari zote zilizojitokeza ili kuweza kuondoa changamoto iliyobainika katika uandaaji wa mikataba hiyo.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli kwamba kulikuwa na vifungu viwili vilivyokuwa vinagongana katika mkataba. Hata hivyo, Baada ya kuwepo kwa mgongano wa Vifungu hivyo viwili, Baraza la Manispaa Mjini limeielekeza Kampuni ya ECONEX kutumia Kifungu Nambari 10(a) cha Mkataba wa makusanyo ya maegesho ya vyombo vya moto kinaeleza kwamba Mtoa huduma lazima awasilishe kiwango cha fedha za makusanyo ya ada za maegesho kwa kila mwezi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Uongozi wa ECONEX imeeleza kuwa baada ya kuwepo kwa changamoto hiyo kulifanyika kikao cha makubaliano na kuamuliwa kupelekwa fedha hizo benki kila mwisho wa mwenzi kutokana ugumu wa  kuwasilisha fedha benki kila siku

Hata hivyo Kamati iliomba kupatika nyaraka ya muhtasari wa maamuzi ya kikao hicho haikuweza kupatiwa kwa ukaguzi, Kamati inashauri uongozi wa Baraza kuwa makini katika ufungaji wa mikataba kwa kuwa na msimamo wa jambo moja tu na si vyenginevyo ili kuepusha migongano isiyo ya lazima.

**4.6.1.8 Baraza la Manispaa kushindwa kukagua kazi inayofanywa na Kampuni ya ECONEX**

Kwa mujibu wa Kifungu Nambari 22 cha Mkataba wa awali wa makusanyo ya maegesho kinampa mamlaka Baraza la Manispaa ya Mjini kukagua kazi yote inayofanywa na mtoa huduma (ECONEX) kwa ajili ya kujiridhisha hali ya utendaji kazi wa kampuni ya ECONEX na kutoa maelekezo kwa ajili ya kuongeza tija na ufanisi wa kazi hizo.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa ya Mjini halifanyi ufuatiliaji wa kina kujiridhisha kwa huduma zinazotolewa na kampuni ya ECONEX ambapo hali hii imepelekea Baraza kutokua na taarifa sahihi kwa mujibu wa hali halisi ya utekelezaji wa mkataba.

Baadhi ya taarifa ambazo Baraza lilithibitisha kwamba hazina utambuzi nazo ni kama zifuatazo:-

- Uwepo wa vikundi vya watu wanaotoza faini kwa maegesho yasiyoruhusiwa na kukusanya fedha za faini kwa matumizi yao binafsi ambapo watu hao si wafanyakazi kutoka Baraza wala ECONEX.
- Kutowekwa Alama za mabango ya makatazo ya maegesho "No Parking" kwa baadhi ya maeneo ambayo hayaruhusiwi kuegeshwa vyombo vya moto.
- Tozo za maegesho ya Boda boda na Bajaji hazikusanywi kupitia mfumo hivyo kutoweza kujua kiwango halisi kinachokusanywa kupitia vyombo hivyo.
- Makusanyo ya mapato ya maegesho kwa maeneo maalum yaliyohifadhiwa (Reserved Parkings) hayaonekani kwenye mfumo.
- Kutokubainishwa kwa alama za michoro ya utambulisho wa maegesho ya vyombo vya moto barabarani na kupelekea uwepo wa maegesho ambayo hayana utambulisho.

Kutokana na hali hiyo, ukaguzi unaona kwamba kuna hatari ya kupotea kwa mapato ya Serikali kutokana na hali ya kwamba Baraza linashindwa kufatilia utendaji kazi wa ECONEX ili kujuwa baadhi ya taarifa muhimu za makusanyo.

Ukaguzi unashauri Baraza kuchukuwa jitihada za makusudi katika kufatilia kwa kina utendaji kazi wa kampuni ya ECONEX ili kuweza kusimamia vizuri utekelezaji wa kazi na kuondoa dosari zitakazojitokeza ikiwemo kuondosha mianya ya upotevu wa mapato.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli kwamba hakukuwa na mfumo rasmi wa ukaguzi kwa kampuni ya ECONEX. Hata hivyo, Baraza la Manispaa Mjini lilifanya vikao na ziara mbali

mbali za kikazi za kufanya tathmini juu ya kukagua kazi inayofanywa na Kampuni ya ECONEX kwa lengo la kutatua changamoto zilizojitokeza

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika uchunguzi wake imebaini kuwa hakukuwa na uwazi katika hatua za awali za Mkataba baina ya Kampuni ya ECONEX na Baraza la Manispaa Mjini na kupelekea kutokea dosari mbalimbali, hivyo basi Kamati inalishauri Baraza kuhakikisha wanashiriki ipasavyo katika hatua za awali za ufungaji wa mikataba na kutekeleza ipasavyo vifungu vyote vilivyomo ndani ya mkataba husika ili tija uliyokusudiwa iweze kupatikana

**4.6.1.9 Kutofanyika kwa vikao vya kila mwezi**

Kwa mujibu wa mkataba wa makusanyo ya maegesho Kifungu Nambari 30 kinaeleza kwamba Baraza na Mtoa huduma watakua na vikao vya kila mwisho wa mwezi vinavyohusu usimamizi na utekelezaji wa mkataba huo.

Ukaguzi umebaini kwamba vikao hivyo havifanyiki kama inavyoelekezwa katika kifungu hiki jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa ufanisi katika utekelezaji wa mkataba huu.

Kupitia vikao vya pamoja vya kila mwezi kungefanyika majadiliano mengi na baadhi ya mambo yangeweza kutekelezeka kwa ufanisi kama vile kuongezeka kwa maeneo mapya ya kukusanya tozo, kupata kujua namna sahihi na yenye tija ya kukusanya madeni, athari za kuwepo kwa maeneo yasiyolipiwa tozo za makusanyo n.k.

Kutofanyika kwa vikao hivi kumepelekea kuwepo kwa changamoto zinazokaa muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi na hatimae kuchelewasha ufanisi katika utendaji kazi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kufanya vikao na kampuni ya ECONEX kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba ili kutatua changamoto zilizopo katika utekelezaji wa kazi za makusanyo ya maegesho

na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baraza la Manispaa Mjini halikuwa na utaraibu wa kukutana kila mwezi badala yake lilikuwa likikutana iwapo kukitokeza changamoto ili kuzipatia ufumbuzi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza limekiri kuwepo kwa dosari hiyo Kamati haikuona haja kuendelea na hoja hii badala yake inatoa ushauri kwa Baraza kuzingatia utekelezaji wa vifungu mbalimbali ambavyo vinaingiwa katika mikataba mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na ufanisi wa mikataba hiyo kwa kubaini changamoto za utekelezaji wa mikataba na kuzipatia ufumbuzi wa haraka.

**4.6.1.10 Fedha za makusanyo ya maegesho kutoingizwa katika Hesabu ya Benki ya Baraza kila siku.**

Kifungu Nambari 13 cha Mkataba wa makusanyo ya mapato ya maegesho kinaeleza kwamba fedha yoyote ya ada ya maegesho ni mali ya Baraza, hivyo mtoa huduma anawajibu wa kuwasilisha fedha zote za ada ya maegesho kwa kila siku katika akaunti ya Baraza.

Aidha ukaguzi umebaini kuwa kifungu hiki hakijazingatiwa kwa upande wa kampuni ya ECONEX kwani wao hupeleka mapato ya kila siku katika akaunti ya ECONEX ya benki na ikifika mwisho wa mwezi ECONEX huhaulisha kiwango kinachohusika tu cha gawio la Baraza na kuingiza kiwango hicho katika akaunti ya Baraza na fedha nyingine ambazo ni gawio la ECONEX husalia kwenye akaunti yake.

Hali hii ni kwenda kinyume na kifungu hicho na kuingiza hasara kubwa kwa Serikali ambayo ni pamoja na kukosa fursa ya kupata riba za kila mwezi, kukosa fedha za matumizi kwenye mahitaji ya kila siku hali inayoweza

pelekea Serikali kukopa fedha benki na kulipa kwa riba.

Ukaguzi unashauri kwamba uongozi wa Baraza na wa ECONEX upitie tena mkataba huo na kusawazisha dosari zote zilizojitokeza katika eneo hili ili kuinusuru Serikali kuendelea kupata hasara.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli kwamba Fedha za Makusanyo ya maegesho hazikuwa na utaratibu wa kuingizwa katika hesabu za benki ya Baraza kwa kila siku na badala yake mapato yalionekana kuingizwa kila mwezi kupitia Hesabu ya Mapato ya Baraza.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa mapato yanayoingizwa kila mwezi kupitia hesabu ya Mapato ya Baraza ni gawio la asilimia 45 kutoka katika kampuni ya ECONEX ambapo mapato ya maegesho huingia moja kwa moja katika akaunti ya ECONEX na mwisho wa mwezi huchukua asilimia 65 na asilimia 45 ndio huingia katika akaunti ya mapato ya Baraza.

**Mapendekezo ya Kamati**

Utaratibu wa kupokea gawio kutoka kampuni ya ECONEX sio sahihi kutokana na mtoa huduma anaweza kuuchezea mfumo kwa kupunguza mapato yaliyokusanywa kwa mwenzi na kutoka gawio ambalo si sahihi, Kamati inalishauri Baraza katika mikataba mengine na Kampuni binafsi katika ukusanyaji wa mapato kuhakikisha mapato yote yanaingizwa katika Akaunti ya Baraza na wao ndio wahusika wa kutoa gawio kwa mujibu makubaliano na si vyenginevyo.

**4.6.1.11 Hasara iliyotokana na dosari katika utekelezaji wa kanuni za maegesho**

Kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Mabaraza ya Manispaa ya mwaka 2017, inazungumzia faini zinazohusisha maegesho ya vyombo vya moto

kwenye maeneo yasiyoruhusiwa ambapo imeweka kiwango cha shilingi Elfu Hamsini (Tshs 50,000) kama kiwango cha chini na shilingi Laki Moja (Tshs 100,000) kama kiwango cha juu cha faini.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari mbali mbali katika utekelezaji wa kanuni hizo ambapo kwa mujibu wa ripoti ya makusanyo ya faini za maegesho iliyoandaliwa na Baraza kwa kipindi cha miezi sita kuanzia mwezi wa Januari 2021 hadi Juni 2021 imebainika faini zinazotozwa ni pungufu ukilinganisha na viwango halisi vilivyoidhinishwa kulipwa kwa mujibu wa kanuni za mwaka 2017, ambapo zaidi ya asilimia 50 za mapato ya faini hupotea kwa njia hii.

Hali hii inaonesha kwamba Serikali hupoteza mapato mengi kutokana na usimamizi mbaya uliopo kwa Baraza katika kutoza faini za maegesho.

Aidha, kulipa faini kinyume na viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa kanuni zilizopo kunaweza kupelekea kujitokeza kwa uchocheaji wa rushwa jambo ambalo litasababisha kujitokeza kwa upotevu wa mapato na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuzingatia na kutekeleza kanuni zinazosimamia faini za maegesho katika utekelezaji wa majukumu ili kuepusha uwezekano wa kuvuja kwa mapato kwa Serikali.

**Jadweli Nambari 29 : Mapato yanayotokana na faini yaliyokusanywa kwa miezi sitakuanzia Januari 2021 hadi Juni 2021**

| Namba | Kiwangocha fainikwa mujibu wa kanuni (Tshs) | Kiwango kilichotozwa Kuanzia Januari hadiJuni 2021 (Tshs) | Idadi ya Vyombo | Jumla ya mapato halisi yaliyokusanywakwa mujibu wa faini iliyotozwa Kuanzia Januarihadi Juni 2021 (Tshs) | Jumla ya mapato yaliyopaswa kupatikana kwa mujibu wa kanuni Kuanzia Januari hadi Juni 2021 (Tshs) | Mapato yaliyopotea kuanzia Januari hadi Juni 2021 (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 50,000 | 10,000 | 2 | 20,000 | 100,000 | 80,000 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2. | 50,000 | 15,000 | 3 | 45,000 | 150,000 | 105,000 |
| 3. | 50,000 | 20,000 | 29 | 580,000 | 1,450,000 | 870,000 |
| 4. | 50,000 | 30,000 | 29 | 870,000 | 1,450,000 | 580,000 |
| 5. | 50,000 | 40,000 | 3 | 120,000 | 150,000 | 30,000 |
| **Jumla Kuu** | | | | **1,635,000** | **3,300,000** | **1,665,000** |

## Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini

Baraza la Manispaa Mjini linatumia Kanuni ya Huduma zinazotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 2017 kwa ajili ya kusimamia na kuendesha maegesho ambapo Baraza la Manispaa linatoza kima stahiki kwa mujibu wa kanuni hiyo.

## Uchunguzi wa Mapendekezo ya Kamati

Kamati katika kufuatilia hoja hii imeelezwa Kuwa Baraza linatumia mahakama yake ya ndani katika kutoza faini kwa mujibu wa kanuni zake na asilimia ya fedha hizo huchukuliwa na mahakama na kiasi kilichobaki huingizwa katika akaunti ya mapato ya Baraza hata hivyo Baraza limeshidwa kuthibitisha ukweli ya maelezo hayo kwa vile hawakuwasilisha nyaraka zinazothibitisha hilo

Kamati inalishauri Baraza wakati wanapojibu hoja za Mkaguzi kuwa na uhakika wa majibu wanayoyatoa na kuambatanisha vielelezo husika vinavyotoa uthibitisho wa majibu wanayowasilisha mbele ya Kamati.

## 4.6.2 Dosari katika Usimamizi wa Mfumo wa SLOTTEX ZANZIBAR

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika kusimamizi wa mfumo wa kielektroniki wa makusanyo ya mapato ya maegesho ya vyombo vya moto. Baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

#### 4.6.2.1Kutokamilika kwa usajili wa mashine za POS na wanaokusanya tozo.

Utaratibu wa kukusanya mapato ya maegesho kwa kutumia mfumo wa kielektroniki unajumuisha mambo mbali mbali kama ifuatavyo:-

• Wafanyakazi ambao watakusanya mapato ya maegesho katika maeneo husika.

• Mashine za (POS) zitakazotumiwa na wafanyakazi kwa ajili ya kutolea ankara za malipo mwanzoni mwa huduma ya maegesho na kutoa stakabadhi baada ya kufanyika malipo kulingana na muda wa maegesho uliotumika.

• Maeneo ambayo yatatumika kwa ajili ya kuegeshewa vyombo na kulipiwa tozo ya maegesho.

• Mfumo wa kielektroniki utakaoweka kumbukumbu za makusanyo ya mapato na wafanyakazi wanaokusanya mapato hayo kupitia mashine za POS.

Ili kuliwezesha Baraza na Kampuni ya ECONEX kufuatilia na kupata taarifa sahihi za makusanyo ya maegesho kwa kila siku, ECONEX haina budi kuunganisha mashine za POS, watu wanaotumia mashine husika, na maeneo wanayokusanya mapato husika katika mfumo wa SLOTEX. Lengo la kuunganisha vitu vyote hivyo kwa pamoja katika mfumo ni kupata taarifa sahihi za makusanyo kwa kumtambua mtu anayetumia mashine, eneo anapokusanyia na mashine husika, wakati na kiwango alichokusanya.

Ukaguzi umebaini kwamba kampuni ya ECONEX haijaunganisha katika mfumo kwa pamoja mashine za POS, watumiaji wa mashine pamoja na maeneo husika ya maegesho, badala yake wakusanyaji mapato hukusanya kupitia POS bila ya kujulikana maeneo wanakokusanyia. Kwa hivyo, kuna uwezekano wa makusanyo kupatikana kwa kiwango kidogo kuliko uhalisia

wa eneo husika linalotumika kukusanyia mapato ya maegesho.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha vitendea kazi vyote, wakusanyaji wote na maeneo yao wanasajiliwa kwa pamoja na waonekane katika maeneo yao halisi waliopo ili iwe rahisi kwa Baraza kufuatilia na kupata taarifa sahihi za mapato yaliyokusanywa na kampuni.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Mashine ya POS zimeunganishwa moja kwa moja katika maeneo husika kwa ID na jina la mfanyakazi, eneo analofanyia kazi na muda analofanyia kazi (jina la Operetor, Mizingani, Forodhani). Hivyo ni dhahiri kwamba mashine inamtambua mfanyakazi na eneo analofanyia kazi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini Baraza la Manispaa Mjini limetoa majibu mawili tofauti baina ya Mkaguzi na Kamati kwani Baraza la Manispaa walikiri kuwepo kwa dosari hii katika majibu waliyompatia Mkaguzi kwenye "Management Letter" na kwa upande wa majibu ya Kamati yanaonesha kuwa hakukuwa na dosari hiyo.

Kamati inaliomba Baraza la Manispaa mjini kutoa majibu ya ukweli na ya uhakika kwa vile Kamati ina mamlaka ya kuchukua hatua kwa yoyote ambae atatoa taarifa zisizo sahihi mbele ya Kamati

**4.6.2.2 Uingizwaji wa mapato kwa njia ya mkono "manually" katika mfumo kinyume na utaratibu**

Ukaguzi umebaini kwamba Mfumo wa SLOTTEX ZANZIBAR unaruhusu mtumiaji wa kampuni ya ECONEX kuweza kuingiza taarifa za mapato kwa njia ya kawaida (manually) pamoja na kuzibadilisha taarifa hizo endapo

ikihitajika kubadilishwa.

Aidha ukaguzi umebaini taarifa hizo zinaweza kubadilishwa au kuingizwa katika mfumo kwa mkono na watendaji wa kampuni ya ECONEX bila ya kuwepo na utaratibu na idhini maalum kutoka kwa uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini.

Kuingiza taarifa za mapato kwa mkono na kuweza kubadilisha bila ya idhini ya Baraza kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya kufanyika kwa udanganyifu katika taarifa za makusanyo na kupelekea kupotea kwa mapato na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kupitia vifaa vya kukusanyia mapato vilivyopo na vilivyokwisha sajiliwa (POS na mobile apps) na kuweka usimamizi na udhibiti mzuri kwa kampuni ya ECONEX kuhakikisha kwamba makusanyo hayaingizwi ndani ya mfumo kwa njia ya mkono (manually).

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Dashboard ya mfumo wa SLOTTEX unasehemu kuu tano na ziada ya sita (Sehemu ya jina n a anuwani, Baraza la Manispaa Mjini limeshavunja mkataba wake na Kampuni ya ECONEX, hivyo Baraza linatumia mfumo wa MUTM kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato yake. Aidha hakuna mapato yanayoingizwa kwa njia ya mkono (manually).

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati haikubaliani na majibu yaliyotolewa na Baraza kwa vile wameshidwa kujibu hoja ipasavyo kama ilivyotolewa na Mkaguzi, Kamati inalishauri Baraza kujibu hoja za mkaguzi ipasavyo kama walivyojibu katika "Manegment letter" wakati wanapowasilisha kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu

za Serikali kwani Kamati imehisia kuna viashiria vya utoaji wa majibu ambayo sio sahihi katika hoja hii

**4.6.2.3 Madeni ya maegesho ambayo yamefutwa katika Mfumo kwa makusudi zaidi ya shilingi 398,536,000**

Kwa mujibu wa Kifungu nambari 28 cha Sheria nambari 11 ya mwaka 2003 ya Uanzishwaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanyia tathmini hesabu za mapato na kujiridhisha kwamba kiwango kinachotakiwa kukusanywa kwa mujibu wa sheria, kanuni na vyombo vyengine vinavyosimamia ukusanyaji wa mapato kimekusanywa na kwamba hatua stahiki zimechukuliwa kwa mapato ambayo hayajaweza kukusanywa.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa Mjini halijachukuwa hatua stahiki za kukusanya mapato ya madeni ya maegesho kwa kipindi cha mwaka 2019 na 2020. Hali hii imethibitika kutokana na kwamba kampuni ya ECONEX iliyopewa dhamana ya kukusanya mapato ya maegesho kuyafuta madeni ya maegesho katika mfumo yenye thamani zaidi ya **shilingi Milioni Miatatu Tisini na Nane Laki Tano Thalathini na Sita Elfu (Tshs 398,536,000)** kwa makusudi bila ya Baraza kutambua.

Hali hii inaashiria kutokuwepo kwa mpango imara wa ufatiliaji wa malipo ya madeni ya maegesho ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusiana na ada za maegesho na kushirikisha vyombo vya sheria ili kusaidia utekelezaji wa zoezi la ulipaji wa madeni ya maegesho kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kushirikiana na ECONEX kuweka utaratibu mzuri wa kufatilia madeni ya makusanyo ya maegesho yaliyopo katika mfumo kwa wahusika ili kuepuka kuingiza hasara Serikali. Baadhi ya

madeni yaliyofutwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Madeni ya maegesho ni utaratibu Mpya ambao haukuwepo awali. Katika mkataba wa Manispaa na Econex hakukuwa na suala la madeni. Mfumo wa SLOTTEX uliweza kuonesha watu waliokimbia kulipa na hivyo Kampuniya ECONEX ilileta mawazo juu ya namna ya kuweza kuwakamata wale wote wanaodaiwa na kwakuwa swala la kukamata magari lilihitaji uwepo wa Polisi wa usalama barabarani ili kurahisisha kazi hiyo, kwakuwa madeni mengine yalikuwa yanazidi ya miaka miwili na hakukuwa na elimu yoyote kwa wamiliki wa magari, vile vile mda wa miaka miwili gari linaweza kuwa na wamiliki zaidi ya mmoja na kupelekea kufutwa na kubakisha ya miezi sita na kuendelea na zoezi la kudai madeni ambapo matangazo yalitolewa kwa ushirikiano wa Manispaa, Econex na Jeshi la Polisi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza limeonesha kuwepo kwa madeni ya maegesho ya Zaidi ya miaka miwili na Baadhi yao yamefutwa kinyume na utaratibu Kamati inalishauri Baraza katika kutafuta njia mbadala ya kudhibiti madereva wa vyombo vya moto ambao wanakwepa kulipa ada ya maegesho badala ya kutumia njia ya kuwatafuta barabarani kitendo abacho hakina ufanisi kiutendaji na kinapoteza muda.

**4.6.2.4 Dosari katika mipaka ya matumizi ya Mfumo**

Utaratibu uliobora katika matumizi ya mfumo unaeleza kwamba Mfumo wa kielektroniki unatakiwa kuwa na mipaka kwa watumiaji ili taarifa zilizomo ndani yake zibakie katika hali ya usiri na usalama kwa muda wote. Hii inamaanisha kwamba kila mtumiaji awe na mipaka katika matumizi ya mfumo

na aruhusiwe kuzifikia taarifa kwa mujibu wa mipaka yake.

Aidha aina za akaunti za matumizi na mipaka katika mfumo ielezwe kwa uwazi kupitia nyaraka rasmi za mipaka ya matumizi ya mfumo (User Matrix Document) ili kuweza kudhibiti kila mtumiaji kuona au kufanya kila kitu katika mfumo.

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya ECONEX haina nyaraka nyenye kuonesha mipaka ya matumizi ya mfumo (User Matrix Document). Vile vile ukaguzi umebaini Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya ECONEX hutumia akaunti ya "Super Admin" kwa kufanyia kazi za uhasibu katika mfumo wa SLOTTEX ZANZIBAR ambapo akaunti hiyo ya Super Admin hutumiwa na "System Developer" wa kampuni kwa ajili ya utoaji wa msaada wa kiufundi katika mfumo.

Kutumika akaunti ya Super Admin kwa shughuli za kihasibu katika mfumo sio sahihi na kunaweza kupelekea athari ya kukosekana kwa taarifa muhimu zitakazosaidia kupatikana ushahidi endapo matukio ya kihalifu yakifanyika katika mfumo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kuchukuwa jitihada za makusudi katika kuwaelimisha ECONEX kutayarisha nyaraka zinazoonesha mipaka ya matumizi katika mfumo na watumiaji kuwa na akaunti zenye utambulisho kwa mujibu wa kazi zao ndani ya mfumo.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baada ya kubaininika Mkurugenzi wa ECONEX kutumia Account ya Super Admin kwa kufanya kazi za uhasibu, Baraza la Manispaa Mjini limeifanyia kazi suala hilo kwa kuitaka Kampuni ya ECONEX kufanya mabadiliko ambapo Mhasibu kutumia Accounti hiyo (super admin) badala ya Mkurugenzi.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa Uongozi wa Baraza haukuwa na uwezo wowote wa kuona taarifa za makusanyo na nyenginezo katika mfumo wa ECONEX mpaka waombe taarifa hizo kupitia kampuni na kwa vile Mkurugenzi wa Kampuni ya ECONEX alikuwa anatumia akaunti ya 'Super Admin' hivyo ni wazi kuwa alikuwa na uwezo wa kubadilisha taarifa za makusanyo na hasa ukizingatia mfumo huo ulikuwa na uwezo wa kufuta na kuingiza taarifa za makusanyo kwa njia ya mkono "manually', hali hii inaweza kusababisha mapato ya Serikali kupotea kwa kufanya udanganyifu kwa kutoa taarifa za makusanyo ya mapato ambayo hayana uhalisia.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza limekiri kutokea kwa dosari hiyo na kuweza kuirekebisha Kamati inashauri uongozi wa Baraza kuhakikisha kuwa wanakuwa na umiliki wa pamoja wa mifumo ili kupata taarifa sahihi zilizomo ndani ya mifumo na kuweza kuzifanyia kazi kwa pamoja kwani kukosa umiliki kunaweza kusababisha kupewa taarifa za udanganyifu za makusanyo ya mapato na kuisababishia hasara Serikali.

**4.6.2.5 Mfumo kutoweza kutoa ripoti za makusanyo ya mapato ya maegesho.**

Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa SLOTEX ZANZIBAR haujawekwa uwezo wa kutoa ripoti za aina yoyote za makusanyo ya mapato ya maegesho (export report) ambapo ripoti hizo kama zingepatikana zingeweza kuwekwa katika kumbu kumbu za mafaili ya makusanyo ya maegesho kwa upande wa Baraza. Hivyo Baraza hupata changamoto kubwa katika kuweka rikodi za makusanyo hayo ya maegesho kutoka ndani ya mfumo kwa vile mfumo hauna uwezo wa kutoa ripoti na badala yake taarifa za makusanyo huonekana tu kupitia "screen dash board" katika kompyuta ambapo maafisa mapato wa Baraza

hurikodi taarifa hizo katika madaftari kwa njia ya mkono, na wakati mwengine hupiga “screenshot” kwa simu au kompyuta.

Hali hii hupelekea kutokea kwa changamoto kubwa katika kuweka kumbu kumbu na kufanya maamuzi sahihi kwa wakati kwani taarifa zinazohitajika huwa hazipatikani kirahisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Manispaa ya Mjini kufanya mawasiliano na mtoa huduma kwa ajili ya kutengeneza moduli maalum itakayoweza kutoa ripoti za aina zote zitakazohitajika na Baraza ili kuweza kupatikana taarifa muhimu kwa urahisi ikiwemo taarifa za makusanyo ya siku, wiki, mwezi na mwaka kwa maeneo husika na kwa wakusanyaji husika, vyombo vya moto vinavyodaiwa, muda wa madeni husika kwenye maeneo husika na wakusanyaji husika.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Ni kweli Mfumo wa maegesho awali haukuwa na uwezo wa kutoa ripoti yoyote. Hata hivyo suala hilo limefanyiwa marekebisho na kwamba mfumo uliweza kutoa taarifa za makusanyo za siku, wiki na mwezi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile baraza limekiri kuwepo kwa dosari hiyo na waliweza kufanya jitihada za kurekebisha hata hivyo Kamati imeshidwa kulithibitisha hilo kwa vile Mfumo huo hautumiki tena katika Baraza kutokana na kumalizika kwa mkataba huo

Kamati inashauri uongozi wa Baraza kuwa makini wakati wanapoingia mkataba na Kampuni mbalimbali zinazotoa huduma za mifumo ya Tehama kwa kuhakikisha kuwa mifumo yao inazingatia mambo yote muhimu ya utendaji kazi ikiwemo mifumo kutoa taarifa zote muhimu zinazohitajika kwa

ajili ya matumizi mbalimbali ya Ofisi.

### 4.6.3 Mapato ya maegesho yanayokusanywa nje ya Mfumo

Kwa mujibu wa mkataba wa makusanyo ya maegesho Kifungu Nambari 16 kinamtaka mtoa huduma kukusanya tozo za maegesho zote kwa njia ya elektroniki. Ukaguzi umebaini kwamba kuna baadhi ya tozo zinakusanywa nje ya mfumo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu hicho cha mkataba wa makubaliano wa mapato yatokanayo na makusanyo ya maegesho. Mapato ya maegesho yanayokusanywa nje ya mfumo ni kama yafuatayo:-

#### 4.6.3.1Makusanyo ya maeneo maalum yaliyohifadhiwa ya maegesho (Reserved Parking)

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya ECONEX kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imekusanya jumla ya shilingi 7,965,000 ikiwa ni fedha kwa ajili ya mapato ya maegesho ya Boda boda na Bajaji.

Aidha imebainika kuwa mapato hayo hukusanywa kwa njia ya kawaida bila ya kutumia mashine za POS zilizounganishwa kwenye mfumo na vile vile baadhi ya mapato hukusanywa kwa mkono bila ya kutolewa stakabadhi za malipo. Baadhi ya malipo ya mapato yanayokusanywa ni kama yafuatayo: -

***Jadweli Nambari 31: Baadhi ya malipo yasiyotolewa stakabadhi (Receipts)***

| Nambari | Aina ya Chombo | Eneo la Maegesho | Muda wa Malipo | Kiasi cha Malipo kwa wiki (Tshs) | Kiasi cha Malipo kwamwaka (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Makundi ya Bodaboda | Darajani | Wiki | 6,000 | 312,000 |
| 2. | Makundi ya Bajaji | Darajani | Wiki | 6,000 | 312,000 |
| 3. | Makundi ya Carry | Darajani | Mwezi | 30,000 | 360,000 |

**Jadweli Nambari 32: Baadhi ya malipo yanayotolewa stakabadhi za mkono**

| Nambari | Aina ya Malipo | Eneo la Maegesho | Muda wa Malipo | Kiasi cha Malipo | Kiasi cha Malipokwa mwaka |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | (Tshs) | (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Maegesho kwa wakaazi | Mji mkongwe | Mwezi | 30,000 | 360,000 |
| 2. | Maegesho kwa wenye maduka | Maeneo ya mjini | Mwezi | 75,000 | 900,000 |
| 3. | Maegesho maalum kwawenye Taxi | Ngome kongwe | Mwezi | 450,000 | 5,400,000 |

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Mapato ya Maegesho maeneo maalumu (reserved parcking) awali yalikuwa yakikusanywa na Baraza la Manispaa wenyewe. Aidha mfumo wa SOLETTEX ulikuwa umeandaliwa kwa ajili ya makusanyo ya siku tu wakati makusanyo hayo yalikusanywa kwa mwezi. na Makusanyo reserved parcking baadae yakapelekwa katika Kampuni ya ECONEX ambapo mfumo huo haukuwa na kipengele cha kutoa stakadhi ya malipo hayo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Pamoja na majibu hayo Kamati inalishauri Baraza kufuatilia kwa karibu uwezo wa mifumo kiutendaji kabla ya kufunga mikataba ili kubaini mifumo kuwa inaweza kufanya mabadiliko mbalimbali kwa mujibu wa mahitaji pindi yanapotokea.

### 4.6.3.2 Faini za maegesho ya maeneo yasiyoruhusiwa

Ukaguzi umebaini kampuni ya ECONEX inakusanya mapato yanayotokana na faini za maegesho kwa maeneo yasiyoruhusiwa. Hata hivyo imebainika kwamba mapato hayo hayakusanywi kwa kutumia mfumo uliopo wa SLOTEX ZANZIBAR na hakuna utaratibu wowote unaotumika katika kuweka kumbu kumbu za mapato hayo baada ya kukusanywa.

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Kampuni ya ECONEX ilikuwa ikikusanya mapato kwa maeneo yaliyoanishwa katika mkataba na kwamba faini za maegesho kwa maeneo yasiyoruhusiwa yalikusanywa na Baraza la Manispaa kwa mujibu wa kanuni zilizopo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya Baraza kutokiri kuwepo kwa dosari hii Kamati imearifiwa na Mkaguzi kuwa katika kulithibitisha hili walikuwa wanafanya uchunguzi na kubaini kuwa baadhi ya wafanyakazi wa Kampuni ya ECONEX walikuwa wakitoza faini hizo. Adha kulikuwa na vikundi katika maeneo ya Mjini ambao si wafanyakazi wa Baraza wakishuhulika na jambo hilo.

Kamati inalishauri Baraza kufanya ufuatiliaji wa karibu katika maeneo mbalimbali ya mjini ili kubaini  vikundi vya watu wanaotoza faini ambao si watendaji wa Barza na kuwachukulia hatua stahiki.

**4.6.4 Maeneo yasiyolipiwa Tozo za Maegesho**

Ukaguzi umebaini kwamba kuna baadhi ya maeneo yaliyopo katika Manispaa ya Mjini ambayo hayamo katika orodha ya maeneo yote yanayolipiwa maegesho na kusimamiwa na ECONEX, lakini maeneo hayo yana uwezo mkubwa wa kongeza mapato kwa Serikali kama yakitumika rasmi kwa ajili ya shughuli za kukusanya mapato ya maegesho.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba endapo maeneo hayo yakitumika kwa shughuli za makusanyo ya maegesho Serikali inaweza kuingiza zaidi ya shilingi 471,024,000 kwa kipindi cha miaka miwili.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza kufuatilia maeneo hayo na kuandaa utaratibu mzuri wa kuyatumia kwa shughuli za maegesho ili kuongeza

ufanisi, tija pamoja na kuongeza mapato kwa Serikali. Orodha ya Maeneo yasiyotumika kwa maegesho ya vyombo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 17.**

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Baraza limechukua hatua ya kuyapitia kwa kuyatathmini maeneo hayo na kwamba tayari yanafanya kazi kwa ajili ya maegesho.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Baraza limekiri kuwepo kwa maeneo hayo na tayari wameshaanza kuchukua hatua ya kuyatumia kwa maegesho kamati ingependa kushauri uongozi wa baraza kwa kuendelea kutathmini maeneo mengine ili kuweza kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Baraza

**4.6.3.1 Kujitokeza kwa tofauti ya shilingi 131,537,197 katika uwasilishaji wa taarifa za mapato ya maegesho kwa Baraza la Manispaa ya Mjini kwa mwaka wa fedha 2020/2021.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Manispaa ya Mjini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 limeingiziwa jumla ya shilingi 446,861,620 ikiwa ni fedha za gawio la mapato ya maegesho ya Baraza kutoka kwa kampuni ya ECONEX, fedha hizo zimeingizwa katika akaunti ya mapato ya Baraza na zimeonekana kupitia Bank statement ya Baraza.

Kwa upande wa uwasilishaji wa taarifa, ukaguzi ulihitaji Baraza kuwasilisha taarifa za mapato ya maegesho ya mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo Baraza liliwasilisha jumla ya shilingi 578,398,817 na mapato hayo yamewasilishwa kupitia ripoti za mapato.

Kutokana na mapato yaliyoorodheshwa hapo juu ukaguzi umebaini kujitokeza kwa utofauti wa shilingi 131,537,197 baina ya mapato halisi ya

maegesho yanayoingia benki na mapato yaliyowasilishwa kwa ukaguzi kutoka Baraza.

Hali hii ya utofauti inaashiria kwamba kujitokeza kwa udhaifu wa uwekaji wa kumbu kumbu za taarifa za mapato ya maegesho ya vyombo yanayotokana na Baraza la Manispaa ya Mjini. Ukaguzi unashauri Baraza kuanzisha utaratibu mzuri wa utunzaji wa kumbukumbu za mapato ili ziwe sahihi na kuweza kupatikana kwa urahisi pale zinapohitajika.

Hata hivyo ni vyema kwa mkaguzi wa ndani kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa kuangalia mwenendo wa makusanyo ya maegesho ya vyombo na Baraza na kufanya mapitio ya taarifa za makusanyo ya maegesho kila mara ili kuhakikisha mapato ya Serikali yanalindwa

**Majibu ya Baraza la Manispaa Mjini**

Taarifa sahihi za makusanyo ni zile zilizotokana na Bank Statement, hata hivyo tofauti iliyojitokeza inatokana na uwasilishwaji wa taarifa. Aidha katika kutatua changamoto hiyo Baraza limeamua kufanya bank reconciliation kuondoa changamoto hizo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini baraza lilikuwa halifanyi usuluhisho wa mapato kwa kila mwenzi baina ya taarifa za benki na taarifa zilizopo baraza hali iliyosababisha kutokea tofauti hiyo.

Hata hivyo baraza lilianza kuchukua jitihada za kurekebisha dosari hiyo kwa kufanya usuluhisho kwa kila mwezi

Kamati inalishauri baraza kuwa na muendelezo wa kufanya hivyo katika mfumo mpya wa Serikali wa MUTM ambao unatumika sasa hivi ili taarifa za mapato ziwe sawa baina hesabu za mapato na taarifa za benki

## 13.0 UKAGUZI WA MIFUMO BODI YA MAPATO ZANZIBAR

### 13.1.1.1 Kukosekana kwa nyaraka za Mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapatowa "Virtual Fiscal Management System – VFMS"

Katika ukaguzi uliofanyika kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ilibainika kuwa ZRB imeanzisha mfumo mpya wa ukusanyaji wa mapato unaojulikana kama "Virtual Fiscal Management System - VFMS". Mfumo huo umetengenezwa kupitia wataalam wa ndani wa Idara yake ya Tehama ambapo kwa kiasi kikubwa mfumo umeweza kufanikisha malengo yake ya utendaji kazi na kuanzakutumika kuanzia Julai, 2021.

Aidha mfumo huo umeunganishwa moja kwa moja na mashine za kelektroniki "EFD" kwa ajili ya kutolea risiti za malipo kwa wafanya biashara mbali mbali waliopo Unguja na Pemba. Takriban asilimia kubwa ya walipa kodi wakubwa ikiwemo mahoteli na walipakodi wadogo wamesajiliwa na kuanza kuutumia mfumo huo.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa nyaraka muhimu zinazohusiana na matumizi ya mfumo pamoja na mipangilio mbali mbali iliyopo katika mfumo huo ambayo ingeweza kuonesha na kuweka kumbu kumbu za mfumo ulivyotengenezwa na matumizi yake kwa ujumla.

Nyaraka hizo zilizokosekana ni pamoja na nyaraka za usanidi "system configuration documents", miongozo ya kuwasaidia watumiaji wa mfumo "user support manuals", nyaraka zenye kubainisha usalama wa mfumo "security configuration documents", nyaraka za mahitaji ya utendaji wa mfumo "system requirements specification - (SRS) documents " , nyaraka zinazoonesha uwepo wa muingiliano na mifumo mengine kama vile mifumo ya malipo ya kibenki "API Support documents" n.k.

Kukosekana kwa nyaraka muhimu za usimamizi na uendeshaji wa mfumo mpya wa VFMS kunaweza kupelekea Idara ya TEHAMA ya ZRB kushindwa kuusimamia, kuulinda na kuuendeleza mfumo ipasavyo hasa ikitokea wafanyakazi waliotengeneza mfumo huo kuondoka ZRB kwa njia yoyote ikiwa kupata uhamisho wa kikazi katika taasisi nyengine, kwenda likizo za muda mrefu kama vile masomoni, na vyenginevyo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kupitia idara ya TEHAMA ya ZRB kufanya yafuatayo:-

- Kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) kuandaa nyaraka zote zinazohusiana na usimamizi, utendaji kazi pamoja na usalama wa mfumo wa VFMS, mfano wa nyaraka hizo ni “system configuration documents”, “user support manuals”, “security configuration documents”, “system requirements specification documents ” , “API Support documents” n.k. ambapo baada ya kukamilika nyaraka hizo zitathibitishwa na uongozi wa ZRB ili ziwe rasmi.
- Kutunza kumbu kumbu na kuzilinda wakati wote “source codes” zilizotumika kutengenezea mfumo huo pamoja na kuweka kumbu kumbu za matokeo ya majaribio ya utendaji kazi na kuangalia ukubalikaji wa mfumo kwa watumiaji, kuwepo kwa kumbukumbu hizo kutaweza kurahisisha kufanyika kwa zoezi la kuimarisha mfumo wa VFMS “system update processes” wakati itakapohitajika.
- Mabadiliko yoyote yanayofanywa na yatakayofanyika baadae katika mifumo yatapaswa kujaribiwa na kuwashirikisha watumiaji wa mifumo ili kuweza kupatikana ithibati na uhalisia wa matokeo ya utendaji kazi wa mfumo baada ya kufanyika kwa mabadiliko hayo.

- Idara ya TEHAMA kutoa msaada wa kiufundi na mafunzo endelevu kwa watumiaji wa mfumo kwa lengo la kuweza kutumika vizuri mfumo huo na hatimae kupatikana kwa tija na ufanisi wa ukusanyaji wa mapato kwa kupitia mfumo huo kulingana na thamani yake.

**13.1.1.2 Majibu ya Bodi ya Mapato Zanzibar**

Wakati wa ukaguzi huu, Mamlaka ilikuwa inaendelea kutengeneza mfumo hivyo nyaraka zilizokuwa zimekamilika kwa kipindi hicho ni ya Mahitaji (SRS) na 'Architectural design'.

Nyaraka za usanidi "system configuration documents", miongozo ya kuwasaidia watumiaji wa mfumo "user support manuals", nyaraka zenye kubainisha usalama wa mfumo "security configuration documents", nyaraka za mahitaji ya utendaji wa mfumo "system requirements specification - (SRS) documents", nyaraka zinazoonesha uwepo wa muingiliano na mifumo mengine "API Support documents" zilikamilika baada ya kukamilika kwa mfumo na zimeambatanishwa na ripoti hii.

Kwa upande wa mahitaji mapya ya TEHAMA baada ya kutengenezwa ndani ya Mamlaka tunawasilisha Serikali Mtandao kupata ridhaa.

Mfano wa mahitaji ambayo yamewasilishwa Serikali Mtandao ni pamoja na "Term of reference"(TOR), nyaraka za mahitaji ya utendaji wa mfumo (SRS)", "concept note" na "system design documents" (SDD) Kwa mfumo wa Funguka.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati haipingani na majibu yaliyotolewa na Mamlaka hata hivyo utaratibu uliobora kwa upande wa mifumo ya Tehama ni kukamilisha nyaraka zote

muhimu kabla ya kuanza matumizi yake kama vile nyaraza za Mahitaji (SRS), nyaraka za 'Architectural design'. , nyaraka za usanidi "system configuration documents", n.k. hivyo Kamati inaishauri Mamlaka kuzingatia jambo hilo wakati wanapotengeneza mifumo kwa kutumia wataalamu wao ndani ili mifumo hiyo kuwa na viwango vinavyotakiwa kwa mujibu wa miongozo ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ)

**13.1.1.2 Mapitio ya Mifumo ya ZRB**

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa ujumla wa utendaji kazi wa mifumo ya ZRB kwa kulinganisha na thamani iliyotumika kutengeneza mifumo hiyo ambapo imebainika baadhi ya mifumo iliyonunuliwa haifanyi kazi na kuwa imelala "dormant" licha ya kwamba fedha nyingi zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mifumo hiyo, baadhi yao haifanyi kazi ipasavyo kama ilivyotarajiwa ikiwemo Mfumo Mkuu wa Makusanyo ya Mapato (ZITAS) na mengine michache ndio inayotumika kwa kuendeshea shughuli za ZRB ambapo haina dhamana kubwa ya utendaji kazi katika siku zijazo kutokana na dosari mbali mbali zinazoendelea kujitokeza.

Hali hii imesababishwa kutokana na mifumo mingi ya ZRB kuwa na dosari za kiujumla kama zifuatazo:-

- Kukosekana kwa huduma za kuimarishwa mifumo hiyo kutoka kwa watengenezaji (lack of software updates and security patches from Vendors).
- Kukosekana kwa kiwango kikubwa cha msaada wa kiufundi (technical updates) kutoka kwa watengenezaji wa mifumo hiyo (vendors).
- Wataalam wa ndani wa Tehama wa ZRB kuwa na uwezo

mdogo wa kuendesha na kuikwamua kitaalam mifumo wakati inapokuwa na changamoto za kiufundi, hali hii imetokana na ZRB kununua mifumo mingi kutoka kwa Vendors walio nchi za nje ambao hutumia teknolojia zisizokuwa rafiki na maarufu kwa mazingira ya nchi za kwetu katika kutengenezea mifumo hiyo, vile vile ZRB kutopatiwa "Source Codes" zinazotumika kutengenezea mifumo hiyo kutoka kwa Vendors ambazo zingeliweza ZRB kupata uelewa wa namna ya mifumo yao ilivyotengenezwa na kuzisimamia Codes hizo kwa lengo la kuimarisha mifumo yao kwa baadae.

- Kukosekana kwa mafunzo ya kina (advanced courses – "Certifications") kwa watendaji wa ZRB wanaosimamia mifumo ili kuwajengea uwezo wa kuelewa na kufahamu kwa upana teknolojia zinazotumika kuhusiana na mifumo iliyopo ZRB pamoja na kupata mafunzo endelevu ya kiufundi na kusimamia mifumo kwa ujumla.
- Kukosekana kwa nyaraka muhimu za kusimamia utendaji kazi wa mifumo.
- Watumiaji wa mifumo (ZRB system users) kukataa kutumia mifumo ya ZRB kutokana na sababu tofauti ikiwemo kutoamini utendaji kazi wa mifumo yao kutokana na mifumo kutoa matokeo tofauti na inavyotarajiwa (unexpected results), uelewa mdogo wa utumiaji wa mifumo unaopelekea mifumo hiyo kutumika kwa kiwango kidogo na sehemu kubwa ya mifumo kutotumika ipasavyo na hatimae kusababisha watumiaji kufanya kazi nje ya mfumo "manually".

Aidha ukaguzi ulipitia baadhi ya mikataba ya mifumo iliyofungwa baina ya ZRB na watengenezaji wa Mifumo (Vendors) na kuifanyia tathmini na kubaini

kwamba mikataba mingi haikuwa vizuri katika maswala ya kisheria baina ya wauzaji wa mifumo na ZRB hivyo kusababisha watengenezaji hao kushindwa kuwatengenezea ZRB mifumo kwa mujibu wa mahitaji halisi yaliyotakiwa na ZRB

vile vile kukosekana kwa upembuzi yakinifu wa kina na kutokushirikishwa kwa watumiaji katika hatua za awali za uanzishwaji wa mfumo ambapo hali hiyo imepelekea kutengeneza mifumo ambayo haijakidhi matakwa ya watumiaji (user requirements) na kupelekea wakati mwingine kutokufanya kazi ipasavyo au kutoa matokeo tofauti na ilivyotarajiwa hususan katika vipengele vya kukokotoa mahesabu ya kodi na mapato jambo ambalo limepelekea kuingiza hasara Serikali.

Aidha, baadhi ya dosari za kimkataba zilizobainika kwa baadhi ya mikataba ni kukosekana kwa vifungu vitakavyowabana (bondi ya mkataba) watengenezaji hao kisheria jambo ambalo limepelekea watengenezaji hao kutotoa msaada ipasavyo au kutoonekana eneo la kazi pindipo wanapohitajika kwa ajili ya kutoa huduma za msaada wa kiufundi katika mifumo ya ZRB na bila ya kuchukuliwa hatua zozote za kisheria kwa mujibu wa mkataba. Jadweli lifuatalo linaonesha hali halisi ya kiwango cha utendaji kazi wa mifumo ya ZRB pamoja thamani ya fedha zilizotumika kutengenezea mifumo hiyo.

***Jadweli Nambari 43 : Hali halisi ya Utendaji kazi wa mifumo ya ZRB***

| Namba | Aina ya Mfumo | Muda ulionunuliwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (USD/Tshs.) | Hali halisiya Mfumo hadi ukaguzi unakamilika |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Web-portal | 31 Januari, 2018 | USD 366,405.70 | Haufanyi kazi /Umelala |
| 2 | e-Tax (Hotel Tax Collection Management System (HTCMS) | 2017 | Uligharamiwa na Wizaraya Fedha/Mkataba umekosekana kwa ukaguzi | Haufanyi kazi /Umelala |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Tax Block Management System (TBMS) | Mei, 2019 | Tshs. 210,545,544 | Haufanyi kazi ipasavyo/Umelala |
| 4 | Enterprise Resource Planning (ERP) | Juni, 2016 | Tshs. 464,916,000 | Mfumo unatumika kwa chini ya asilimia30. |
| 5 | Virtual Fiscal Device Management System (VFDMS) | 24 Aprili, 2019 | Gharama zilizotumika **USD 473,417.7**<br>Gharama zilizobaki **USD 879,204.3**<br>Jumla ya Gharama **USD 1,352,622** | Haufanyi kazi /umelala. |
| 6 | ZITAS (Zanzibar Integrated Tax Administration System) | 01/11/2010 | USD 80,000 | Moduli 3 zinafanya kazi kati ya moduli 10zilizopo |
| 7 | Pastel Accountin gPackage | Taarifa hazijapatikana | Mkataba wa manunuzi umekosekana kwa ukaguzi | Unafanya kazi |
| 8 | Revenue Forecast Module | 2018/2019 | USD 133,693 | Unafanya kazi |
| 9 | Call Centre | Umetenenezwa 2018/2019 (Umeanza kazi 2021) | Tshs. 280,674,173 | Unafanya kazi |
| 10 | Forensic | 2017/2018 | Mkataba wa manunuzi umekosekana kwa ukaguzi | Unafanya kazi |

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) kufanya mambo yafuatayo ili kuweza kuimarisha mifumo yake pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo hiyo:-

- Kuweka kipaombele cha kuwajengea uwezo wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA cha ZRB hususan katika eneo la utengenezaji wa mifumo (System Development) kwa lengo la kuwafanya waweze kusimamia na kuimarisha mifumo iliyopo kwa ufanisi mkubwa pasi na kutumia wataalamu kutoka nchi za nje, jambo ambalo litapelekea wataalamu wa ndani kupunguza gharama za uendeshaji na kutoa

msaada wa kifundi kwa wakati katika mifumo hiyo.

- Kuhakikisha unazingatia na kutekeleza matakwa na mahitaji yanayotolewa na watumiaji wa mifumo wa ZRB na kuwashirikisha ipasavyo kuanzia hatua za awali za utengenezaji hadi kukamilika kwa mfumo.
- Kuandaa sera madhubuti za kuhakikisha mifumo yote inayotengenezwa kwa ajili ya matumizi ya ZRB inafuata taratibu zilizobora, misingi imara pamoja na miongozo sahihi kutoka ZRB, eGov na miongozo ya kimataifa inayotumika katika utengenezaji wa mifumo (System Development Life Cycle - SDLC) kama vile kukusanya mahitaji ya watumiaji wa mifumo "user requirements", kufanya upembuzi yakinifu "system analysis" , kufanya ubunifu wa kutengeneza mifumo "system design and implementation" pamoja na kufanya majaribio mbali mbali ya utendaji wa mifumo kabla ya kuanza kutumika moja kwa moja "system testing". Hali hii itaweza kupunguza dosari kubwa za kiutendaji katika mfumo na kupelekea kupatikana kwa tija na ufanisi katika matumizi ya mifumo hiyo.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar**

Mamlaka ya Mapato kwa kipindii hicho cha ukaguzi ikijuilikana kwa jina la Bodi ya Mapato Zanzibar, ni kweli kulikuwa kuna uhaba wa uwelewa wa matakwa ya uwendeshaji kielektroniki hasa kwa upande wa kukimbizana na ukuwaji wa Teknolojia na uwekezaji katika miradi ya Tehama na ndio sababu kubwa iliyopelekea uwepo wa dosari zilizoibuliwa na Mkaguzi. Kwa sasa Mamlaka baada ya kubadilisha muundo kutoka ZRB kuja ZRA, imejikita katika kuwekeza kwenye tekeknojia za Tehama ili kuweza kutanua wigo wa utoaji huduma. Hivyo, imeanza kuekeza kwa kuongeza idadi ya wataalamu na watendaji kumi

na sita (16) wa Tehama pamoja na vitendea kazi vyao kuanzia mwezi wa Septemba 2022, sambamba na kuwajengea uwezo watendaji hao. Hivyo Kwa sasa Idara ina watendaji 34 pamoja na Mkurugenzi wa Idara ya Tehama.

Mamlaka imepanga kutumia wataalamu wake wa ndani (developer) kupitia mifumo yote ili kuangalia upi unaweza kurekebishwa na kutumika ndani ya Mamlaka ili kufidia gharama zilizotumika.

Mamlaka katika uwekezaji wake kwa sasa unazingatia mahitaji yote ya uwekezaji wa miradi ya Tehama ili kuimarisha utiifu wa kisheria za uwekezaji ya miradi ya Tehama kwa kuzingatia mahitaji ya kila hatua ya mradi.

Jadweli Nambari 1 : Hali halisi ya Utendaji kazi wa mifumo ya ZRA kwa sasa

| Namba | Aina ya Mfumo | Muda ulionunuliwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (USD/ Tshs.) | Hali halisi ya Mfumo hadi ukaguzi unakamilika | Hali ya sasa ya mifumo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Web-portal | 31 Januari, 2018 | USD 366,405.70 | Haufanyi kazi / Umelala | Ni kweli hautumiki kutokana na teknologia yake kupitwa na muda ambapo Kwa sasa tumepata mfumo mwengine unaitwa ZIDRAS wenye teknolojia ya kisasa. |
| 2 | e-Tax (Hotel Tax Collection Management System (HTCMS) | 2017 | Uligharamiwa na Wizara ya Fedha/Mkataba umekosekana kwa ukaguzi | Haufanyi kazi / Umelala | Mfumo huu haukukidhi mahitaji ya Mamlaka Kwa kua ulikua na technologia ya nyuma na haukutengenezwa kutoa huduma Kwa walipakodi wote.<br>Hata hivyo ZRA imeshatengeneza mfumo wa VFMS kupitia wataalamu wake wa ndani ambao ni mbadala wa mfumo huo. |
| 3 | Tax Block Managem ent System (TBMS) | Mei, 2019 | Tshs. 210,545,544 | Haufanyi kazi ipasavyo/Umelala | ZRA inaupitia mfumo huu kupitia wataalamu wake wa ndani pamoja na kufanya majadiliano na mkandarasi kwa ajili ya kuendelea na mfumo huo. |
| 4 | Enterprise Resource | Juni, 2016 | Tshs. 464,916,000 | Mfumo unatumika kwa | ERP ni mfumo ulioundwa na “module” 12. Kati ya hizo module |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Planning (ERP) | | | chini ya asilimia 30. | nne ndizo zinafanyakazi (Finance, Store, Payroll na procurement), hata hivyo ZRA inaupitia mfumo huu kupitia wataalamu wake wa ndani pamoja na kufanya majadiliano ya mahitaji Kwa module zilizobakia na watendaji wa ZRA kwa ajili ya kuendelea kutumia mfumo huo. |
| 5 | Virtual Fiscal Device Managem ent System (VFDMS) | 24 Aprili, 2019 | Gharama zilizotumika USD 473,417.7<br>Gharama zilizobaki USD 879,204.3<br>Jumla ya Gharama USD 1,352,622 | Haufanyi kazi / umelala. | Malipo yaliyofanyika ni Kwa mujibu wa mkataba. Nayo ni asilimia 20% baada ya kuwasilisha inception report na asilimia 15% baada ya kuwasilisha 'system design'. Hivyo kutengeneza jumla ya asilimia 35% ya mkataba, saw ana USD 473,417.70.<br><br>Baada ya kumaliza kutengenezwa na kuanza kujaribiwa tukabaini haujakidhi mahitaji hivyo tukazuiya malipo hadi mfumo utakapofanyiwa marekebisho.<br>Baada kuona muda umekuwa mrefu na marekebisho hayajafanyika, kupitia wataalamu wetu wa ndani tukatengeneza mfumo unaofanana na huo unaitwa VFMS ambao Kwa sasa ndio unaotumika.<br><br>Kwa upate wa kampuni iliyotengeneza mfumo wa VFDMS tunaendelea kufanya nao mazungumzo ili kupata muafaka wa jambo hili. Kwa sasa kesi hii iko Mahakamani. |
| 6 | ZITAS (Zanzibar Integrated Tax Administra tion System) | 01/11/2010 | USD 80,000 | Moduli 3 zinafanya kazi kati ya moduli 10 zilizopo | Mfumo wa ZITAS unamoduli tisa (9) ambazo zinafanya kazi kati ya moduli kumi na mbili (12).<br>moduli zinazofanya kazi ni<br>i. Utawala (management portal)<br>ii. Usajili wa vyombo vya moto (MVRS)<br>iii. Utowaji wa leseni za udereva (CDLS)<br>iv. Malipo (payment) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | v. Uingizaji wa ritani (filling)<br>vi. Usajili wa walipakodi (registration<br>vii. Account (wahasibu)<br>viii. Washika fedha (cashier) na<br>ix. Ripoti<br><br>Kutokana na mapungufu ya mfumo huo kuwa na viashiria vya upotevu wa mapato ZRA imeanzisha mfumo mpya wa ZIDRAS ambao ni mbadala wa ZITAS. |
| 7 | Pastel Accountin g Package | Taarifa hazijapatikana | Mkataba wa manunuzi umekosekana kwa ukaguzi | Unafanya kazi | Mfumo huu umenunuliwa na Mamlaka ukiwa ni mfumo ambao tayari umeshatengenezwa kwa ajili ya matumizi ya account (off the shelf), hivyo haukuwa na mkataba wa manunuzi. Mfumo huu umenunuliwa Kwa gharama ya TZS. 5,036,810.00 mwaka 2008. |
| 8 | Revenue Forecast Module | 2018/2019 | USD 133,693 | Unafanya kazi | Unafanya kazi |
| 9 | Call Centre | Umetenenezwa 2018/2019 (Umeanza kazi 2021) | Tshs. 280,674,173 | Unafanya kazi | Unafanya kazi |
| 10 | Forensic | 2017/2018 | Mkataba wa manunuzi umekosekana kwa ukaguzi | Unafanya kazi | Unafanya kazi na Mkataba wa manunuzi umeambatanishwa |

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini yafuatayo.

Uwezo mdogo wa Mamlaka kwa wakati huo katika kusimamia miradi ya Tehama ambapo kwa kiasi kikubwa umepelekea baadhi ya miradi ya mifumo kushidwa kukamilika licha ya kutumia fedha nyingi na mifumo mengine kuwa na moduli zisizoweza kufanya kazi kwa mahitaji ya ofisi

Kutoshirikishwa Wakala wa Serikali Mtandao katika hatua za awali za utayarishaji wa manunuzi ya Mifumo hadi kufungwa kwake jambo ambalo

limepelekea kukosa msaada wa kitaalamu na ushauri ambao ungeliweza kuisaidia Mamlaka katika kupata mifumo iliyokuwa bora na yenywe tija.

**Mapendekezo na Ushauri wa Kamati**

Pamoja na Mamlaka kuanza kuchukua hatua ya kuboresha kitengo cha TEHAMA hata hivyo Kamati inasisitiza watendaji hao waliongezeka ni vyema wakapatiwa mafunzo zaidi kwa ajili ya kuisaidia taasisi katika kusimamia masuala mazima ya Tehama aidha kwa idadi hiyo iliyopo kwa sasa ya watendaji wa TEHAMA katika Mamlaka Kamati inashauri kumalizwa kwa dosari zote zilizopo kwenye mifumo hiyo zikiwemo kuboresha kwa moduli ambazo hazifanyi kazi na kuunda mfumo mmoja tu utakaoweza kufanya shughuli zote za ukusanyaji wa mapato pamoja na uendeshaji wa Mamlaka ili kuondoa utitiri wa mifumo iliyopo sasa hivi ambapo baadhi yao haina tija zaidi ya kuongeza gharama tu.

Vile vile Kamati inaishauri Mamlaka kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao katika utekelezaji wa mambo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kufuata miongozo mbambali inayotolewa na Wakala huyo ili kuepusha Mamlaka kutekeleza miradi ya Tehama isiyokuwa na tija na kuisababishia hasara Serikali

**13.1.1.3 Uwepo wa Uhaba wa Bajeti katika Idara ya TEHAMA ya ZRB**

Taratibu zilizo bora kuhusiana na bajeti za TEHAMA zinaeleza kwamba, katika hali ya kawaida, Bajeti ya TEHAMA iliyoandaliwa vizuri inapotekelezwa kikamilifu huweza kuisaidia Taasisi katika kuleta maendeleo ya haraka ikiwemo kuweka mifumo madhubuti na miundombinu imara ya kurahisisha utendaji kazi na hatimae kuweza kufanikisha dira na malengo ya kimkakati yaliyopangwa na taasisi kwa ufanisi na uwiano mkubwa.

Katika ukaguzi uliofanyika wa Bodi ya Mapato Zanzibar imebainika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 makadirio ya matumizi ya Idara ya Tehama

yalikuwa ni shilingi bilioni 1.4 .Hadi kufikia tarehe 30 Juni,2021 jumla ya shilingi Milioni 800 ziliingizwa na kutumika kwa matumizi ya Idara ya TEHAMA ambazo ni sawa na asilimia 57.14 ya makadirio. Kati ya shilingi Milioni 800 zilizoingizwa kiasi cha shilingi Milioni 400 zilitumika kwa ajili ya kulipia gharama za vifurushi vya INTERNET pamoja na gharama za huduma za muunganisho wa mtandao wa ZRB (VPN Connection Services) katika ofisi zake za Unguja na Pemba ikiwemo matawi yake yanayotoa huduma za makusanyo ya mapato na huduma za leseni kwa niaba ya taasisi, na shilingi milioni 400 zimetumika kwa ajili ya kusaidia na kuimarisha miundombinu ya vifaa pamoja na mifumo ya TEHAMA ya ZRB inayotumika kwa ajili ya kufanyia kazi mbali mbali ikiwemo kazi za usimamizi wa makusanyo ya mapato na kodi, usimamizi wa malipo ya mishahara, usimamizi wa mali za Bodi pamoja na usimamizi wa rasimiali watu.

Ukaguzi baada ya kufanya mahojiano na watendaji pamoja na wasimamizi wa Idara ya TEHAMA kuhusiana na upatikanaji wa bajeti hiyo, umebaini kwamba kiasi hicho cha shilingi milioni 400 kilichoingizwa kwa ajili ya kusaidia na kuimarisha miundombinu ya vifaa pamoja na mifumo ya TEHAMA ya ZRB ni hafifu ukilinganisha na mipango mikakati ya kimaendeleo iliyopangwa na Idara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo mikakati hiyo inajumuisha usimamizi na uboreshaji wa miundombinu yote ya TEHAMA ya ZRB ikiwemo kompyuta, programu na mifumo, vifaa vya mawasiliano na ulinzi, mafunzo mbali mbali kwa watumiaji wa mifumo na watendaji wa Idara ya TEHAMA n.k jambo ambalo limepelekea kutotekelezeka ipasavyo kwa mpango huo kutokana na ufinyu wa bajeti iliyopatikana.

Kuwepo kwa ufinyu wa bajeti katika Idara ya TEHAMA kunaweza kupelekea Idara kushindwa kufanikisha kwa ufanisi malengo waliyojipangia kwa ujumla

ambayo yangeweza kuisaidia taasisi katika kufanikisha malengo makuu ya kimkakati yaliyopangwa na taasisi hiyo.

Vile vile kuwepo kwa ufinyu katika bajeti ya TEHAMA kunaweza kupelekea kutokezea mambo

yafuatayo:-

- Kufanyika kwa manunuzi ya vifaa vya TEHAMA vilivyo chini ya viwango na ubora wa kazi jambo ambalo litapelekea kuhatarisha usalama wa taarifa zitakazokuwa zinaingizwa, kutumika na kuhifadhiwa ndani ya vifaa hivyo.
- Kukosekana kwa mafunzo ya mara kwa mara kwa watumiaji wa mifumo (system users) pindipo yanapotokezea mabadiliko ya uboreshaji na uimarishaji wa mifumo.
- ZRB kushindwa kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani wa kitengo cha TEHAMA ili kuweza kusimamia na kuimarisha mifumo ya taasisi kwa kupitia wataalamu wa ndani na sio kutegemea makampuni ya nje ambayo yanaongeza hasara kwa Serikali katika mtazamo mwengine.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kutoa kipaombele cha utekekelezaji wa bajeti ya TEHAMA kwa kuzingatia sera ya Bodi ya Mapato Zanzibar inayohitaji kuimarisha udhibiti ili kuondoa upotevu wa mapato na kuongeza makusanyo ya mapato kupitia mifumo na miundombinu ya TEHAMA jambo ambalo linapelekea kuongezeka kwa gawio la Serikali na hatimae kupatikana huduma bora za kimaendeleo nchini kutokana thamani ya fedha inayotolewa kwa walipa kodi.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar (ZRA)**

Bajeti ya matumizi ya ZRA hupangwa kwa kutegemea upatikanaji wa mgao wa fedha za matumizi chini ya utaratibu wa ukomo wa bajeti "budget ceiling" kutoka hazina pamoja na mapato mengineyo. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, bajeti ya mapato na matumizi ya ZRA ilikadiriwa kuwa jumla ya TZS. 33.120 bilioni kwa shughuli za kawaida na shughuli za maendeleo ambapo TZS. 21.90 bilioni zilitarajiwa kutoka hazina, na fedha halisi iliyopatikana kutoka hazina ni TZS. 12.71 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 58.

Aidha, matumizi halisi katika mwaka 2020/2021 yalikuwa ni jumla ya TZS. 20.971 bilioni ambayo ni sawa na asilimia 63 ya makadirio ya bajeti jambo ambalo limepelekea athari katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali zilizopangwa ikiwemo miradi ya TEHAMA. Miongoni mwa athari zilizopatikana katika idara ya TEHAMA ni pamoja na kutokutekelezeka Kwa mradi wa kuboresha miundombinu ya TEHAMA yenye thamani ya TZS. 561,000,000.00 na mradi wa kuboresha usalama wa taarifa za Mamlaka zinazohifadhiwa katika mifumo ya TEHAMA na hati ngumu yenye thamani ya TZS. 118,000,000.00

Hali hii ndiyo iliyopelekea matumizi ya TEHAMA katika mwaka 2020/2021 kufikia asilimia 57.14. Hali ya upatikanaji wa fedha katika ZRA inategemea hali halisi ya upatikanaji wa fedha katika Serikali kuu.

Katika kupambana na changamoto hiyo, ZRA imeanzisha mahusiano na Mamlaka nyengine za Mapato za wadau wa maendeleo ikiwemo Mamlaka ya Mapato ya Norway (NTA) kwa ajili ya kupata msaada wa miundombinu ya TEHAMA na kuongezewa ujuzi watumishi wake wakiwemo watumishi kutoka Idara ya TEHAMA.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Mamlaka imekiri kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kufanya matumizi kwa asilimia ndogo katika utekelezaji wa Tehama hata hivyo Kamati inaendelea kuishauri Mamlaka kuweka kipao mbele katika matumizi ya Tehama kwa kuweka Bajeti toshelevu kwa vile matumizi ya mifumo ya Tehama kwa wakati huu ndio nyenzo kuu ya kurahisisha utoaji wa huduma kwa taasisi na kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato.

Aidha Kamati Kamati inaishauri Mamlaka kusimamia vyema mahusiano yaliyopo na Mamlaka ya Mapato ya Norway (NTA) kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujengeana uwezo ili Mamlaka iweze kufikia malengo waliyojiwekea.

**13.1.1.4 Kukosekana kwa njia imara za kuhifadhi taarifa na nyaraka muhimu zilizopo katika mifumo ya ZRB**

Katika ukaguzi uliofanyika wa Bodi ya Mapato Zanzibar imebainika kuwa ZRB haijaweka njia imara na salama kwa ajili kuzilinda, kuzidhibiti na kuzihifadhi taarifa zake zilizokuwa muhimu na zenye usiri wa hali ya juu (classified information) kwa taasisi.

Kwa mfano, hapakuwa na utumiaji wa programu maalum za kufichia taarifa nyeti zilizokuwa ndani ya mifumo (data encryptions software) ambazo programu hizo zingeweza kutumika kwa kudhibiti na kuzilinda taarifa nyeti zilizokuwa ndani ya mifumo. Vile vile hapakuwa na vifaa au zana maalum kwa ajili ya kufichia taarifa na nyaraka nyeti zilizokuwa 'hard copy' jambo ambalo lingeweza kusaidia Bodi kuzilinda taarifa zake zilizokua muhimu na nyeti.

Kukosekana kwa njia imara za kudhibiti, kuzilinda na kuziwekea kinga taarifa zilizokuwa muhimu na za zenye unyeti mkubwa kunaweza kupelekea taarifa hizo kuonekana na wasiohusika na hatimae kuweza kuzisoma, kuzifahamu,

kuzichukuwa na kuzibadilisha (kuzichezea) pamoja na kuzitumia kinyume na matakwa ya taasisi jambo ambalo kwa njia moja au nyengine linaweza kusababisha kutokezea kwa upotevu wa taarifa, ubadhirifu wa fedha au upotevu wa mapato na kupelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuandaa na kufuata sera,taratibu na miongozo madhubuti ya kudhibiti, kuzilinda na kuzihifadhi taarifa zake zilizomo ndani ya mifumo 'softcopy' na nje ya mifumo 'hardcopy ', ili kuweza kuzinusuru taarifa hizo kutokana na kutumiwa na wasiohusika na kusabisha kutokezea kwa upotevu wa taarifa, ubadhirifu wa fedha au upotevu wa mapato na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB kuongeza jitihada za kuwajengea uwezo Wasimamizi wa mifumo waliopo ZRB ili kuongeza ufahamu juu ya jukumu lao la kulinda na kusimamia mifumo pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria kwa watakaobainika kujihusisha na vitendo vya kuchezea na kubadilisha taarifa kinyume na matakwa ya ZRB kwa lengo la kuepuka kuitia hasara Serikali.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Kwa kipindi cha ukaguzi huu ni kweli hatukuwa tumeboresha uhifadhi imara wa taarifa zilizohifadhiwa ndani ya mifumo na hati ngumu.

Njia imara za kiusalama za kuhifadhia taarifa kwenye mifumo ya TEHAMA na hati ngumu Kwa upande wa ZRA zimegawika katika sehemu kuu mbili.

Njia ya kwanza ya kiusalama ni katika ngazi ya mtandao, ambapo tumeboresha usalam wa miundombinu ya mtandao Kwa kuweka "firewalls" ambazo zinahifadhi taarifa zinazotoka na zinazoingia katika mtandao wa ZRA kwa kutumia algorithm ya MD5, 3-DES na AES256.

Njia ya pili ni katika ngazi ya mifumo, ambapo tunatumia “secure standards” zifuatazo:-

i. “Authentication Framework for REST/APIs” Kwa kutumia “AOuth”.
ii. “API gateway”
iii. “Input validation”

Kwa upande wa uhifadhi wa taarifa za hati ngumu, ZRA imeboresha usalama wa hifadhi data (data center) Kwa kuongeza CCTV cameras na kuweka “access door” ili kuongeza udhibiti na uwajibikaji katika usimamizi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Mamlaka imekiri kutokuwa na uhifadhi salama wa mifumo yake kwa wakati huo wa ukaguzi, ila kwa sasa wameshachukua jitihada za kuboresha mifumo yao kwa kuweka uhifadhi wa soft na hardcopy kama walivyoeleza katika majibu yao hata hivyo Kamati inaishauri Mamlaka kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mifumo hiyo ili kubaini dosari za kiusalama na kuiongezea mifumo ulinzi zaidi kwani taarifa zilizomo ndani ya mfumo zikiweza kupenya na kutumiwa na wahalifu wa mtandao zinaweza kusababisha ubadhirifu wa fedha au upotevu wa mapato na hatimae kuingiza hasara Serikali.

Aidha Kamati inaungana ushauri uliotolewa na mkaguzi wa kuitaka uongozi wa ZRA kuongeza jitihada za kuwajengea uwezo Wasimamizi wa mifumo waliopo ZRB ili kuongeza ufahamu juu ya jukumu lao la kulinda na kusimamia mifumo pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria kwa watakaobainika kujihusisha na vitendo vya kuchezea na kubadilisha taarifa kinyume na matakwa ya ZRA kwa lengo la kuepuka kuitia hasara Serikali.

#### 13.1.1.5 Kutokuwepo kwa Mkaguzi wa Ndani wa TEHAMA wa kusimamia na kukagua mifumo na miundombinu ya TEHAMA

Ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar pamoja na kuwa imefunga na kutumia mifumo na miundombinu mbali mbali ya TEHAMA ikiwemo application programs, komputa, seva, network, firewalls n.k, lakini imebainika kuwa katika kitengo cha Ukaguzi wa Ndani hakuna mkaguzi wa mifumo ya miundombinu ya TEHAMA. Aidha ukaguzi ulifanya mahojiano na maafisa wanaohusika na Idara na kubaini kuwa kitengo hicho hakina utaalamu au wataalam wa TEHAMA ambao wangeweza kufanya uhakiki wa hali ya juu wa mifumo ya kukusanyia mapato na kodi, mifumo ya mishahara, mifumo ya rasilimali watu, kompyuta, vifaa vya mawasiliano pamoja na mtandao wa ZRB kwa ujumla na kuweza kutoa ripoti mbali mbali za kushauri uongozi wa ZRB namna bora ya kuimarisha mifumo pamoja na miundombinu ya mawasiliano iliyopo na kupelekea kuweza kudhibiti upotevu wa mapato kupitia mifumo.

Kutokuwepo kwa wakaguzi wa ndani wenye elimu ya TEHAMA na uwezo wa kukagua mifumo pamoja na taarifa zake zinazozalishwa kupitia mifumo hiyo kunaweza kupelekea uongozi wa ZRB kuchelewa kubaini na kuchukuwa hatua za kudhibiti changamoto zinazojitokeza katika mifumo hususan kwa mifumo inayotumika kukusanyia mapato na kodi katika taasisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kufanya jitihada za uwepo wa mkaguzi wa ndani wa mifumo ya TEHAMA (Internal Information System Auditor) ili kuweza kuishauri taasisi kuhusiana na mwenendo mzima wa mifumo ya ZRB ikiwemo kutoa ushauri katika michakato ya manunuzi ya mifumo pamoja na kuishauri taasisi kutokana na changamoto na dosari zinazojitokeza katika utendaji wa mifumo hiyo na miundombinu ya tehama ya kwa ujumla, hali hii itaweza kupelekea dosari nyingi za mifumo kuweza kurekebishwa mapema katika hatua za awali kwa lengo la kuongeza ufanisi na

tija katika ukusanyaji wa mapato na kupelekea kuongezeka kwa udhibiti na kuondoa mainya ya upotevu wa mapato.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Kwa kipindi cha ukaguzi huu ni kweli Mamlaka haikuwa imeajiri mkaguzi wa ndani wa TEHAMA. Kwa kuona umuhimu wake, kuanzia mwezi Septemba 2022 Mamlaka imeajiri mkaguzi wa ndani wa TEHAMA ambae anaendelea na majukumu yake, vilevile Mamlaka imepanga kuongeza wakaguzi wa ndani wa TEHAMA wawili(2) ndani ya mwaka 2023 - 2024 .

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hiyo na tayari wameshachukua hatua ya kuajiri mkaguzi huyo ambae kwa sasa anaendelea na majukumu yake hata hivyo Kamati inaishauri Mamlaka kuhakikisha inakamilisha uajiri wa wakaguzi wawili wa mifumo kama ilivyojipangia kwa lengo la kubaini dosari mbalimbali za mfumo na kuweza kuchukua hatua za haraka kadri iwezekanavyo.

**13.1.1.6 Kukosekana kwa Mfumo rasmi wenye leseni ya kuchunguza, kufuatilia,kudhibiti na kusimamia mtandao katika miundombinu ya ZRB (Licensed Network Monitoring System).**

Mfumo wa kuchunguza, kufuatilia na kusimamia matumizi ya mtandao (Network Monitoring System - NMS) ni moja kati ya zana muhimu za kiusalama ambazo taasisi kubwa zenye kutumia mifumo na miundombinu ya tehama hupaswa kutumia zana hizo kwa lengo la kupima, kudhibiti pamoja na kufanya tathmini ya viwango vya matumizi ya mtandao na miundombinu ya tehama iliyopo katika taasisi.

Tathmini hiyo hufanyika katika kipindi cha muda mfupi kwa njia ya kielektroniki kupitia mifumo ya aina hiyo ambapo hupima kasi ya mtandao, trafiki, matumizi ya data, huchunguza uwepo wa usalama na hali ya mtandao (network status & security updates), hudhibiti mashambulizi yanayotokana na udukuzi (cyber attacks) pamoja na kuweza kufanya utambuzi wa aina gani ya kifaa cha tehama au chanzo kinachopelekea kutokea kwa hitilafu katika mtandao wa Taasisi. Aidha, baada ya kumalizika kufanyika kwa tathmini mfumo huwasilisha ripoti ya matokeo kwa maafisa wasimamizi wa Mtandao (network administrators) kwa njia ya kielektroniki kupitia barua pepe au ujumbe mfupi "sms" kulingana na maafisa watakavyouseti mfumo namna ya kuwasilisha taarifa za matokeo.

Kwa ujumla mfumo wa Network Monitoring System huwasaidia na kuwarahisishia kazi Maafisa wanaosimamia Mtandao katika Taasisi kwa kuweza kugundua haraka chanzo cha hitilafu wakati inapotokezea tatizo katika mtandao wa taasisi ambapo bila ya uwepo wa mifumo hiyo maafisa wangekuwa wanafanya kazi kubwa ya kukagua vifaa na miundombinu ya tehama iliyopo kwenye taasisi kwa njia ya kawaida "manually" ili kubaini chanzo cha hitilafu jambo ambalo lingepelekea kupoteza muda, nguvu na usumbufu ikiwa miundombinu ya taasisi ni mikubwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Bodi ya Mapato Zanzibar imeweka mtandao mkubwa wa mawasiliano kwa lengo la kuwezesha upatikanaji mzuri wa mifumo yake ya makusanyo ya mapato katika ofisi zake zote ikiwemo na matawi na vituo vyake vya makusanyo ya mapato vilivyopo Unguja na Pemba. Hata hivyo dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwepo kwa mfumo ulio rasmi wenye leseni maalum ya matumizi (Lisenced Network Monitoring System) kwa ajili ya kuchunguza usalama wa mtandao wa ZRB, kufuatilia na kusimamia matumizi ya mtandao na mifumo , kudhibiti mashambulizi yanayotokana na

uhalifu wa udukuzi wa mtandao na mifumo ya ZRB pamoja na kufanya tathmini ya mwenendo wa utendaji kazi wa vifaa na miundombinuya tehama inayotumika ZRB kwa lengo la kuendelea kuimarisha na kurahisisha mawasiliano ili kuweza kupatikana huduma bora za makusanyo ya mapato kutoka kwa walipa kodi.

Aidha ukaguzi ulibaini Bodi ya Mapato walikuwa wakitumia zana (software tools) zilizokuwa na uwezo mdogo, zisizo salama na hazikuwa halali zenye leseni ya matumizi, ambazo zilipatikana bure kwenye Internet " free downloaded software/pirated software" na kutumika kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya mtandao wa ZRB jambo ambalo ni kinyume na sera na utarabu wa Bodi ya Mapato na Serikali kwa ujumla.

Kukosekana kwa Mfumo rasmi wenye leseni ya kuchunguza, kufuatilia, kudhibiti na kusimamia mtandao katika miundombinu ya ZRB kunaweza kupelekea ZRB kushindwa kulinda mtandao na mifumo yake dhidi ya uhalifu unaoweza kutokezea ikiwemo mifumo kufanyiwa udukuzi, kushambuliwa na virusi, kuchezewa kwa makusudi na hatimae kuweza kujitokeza kwa upotevu wa mapato jambo ambalo litapelekea kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuhakikisha unafanya jitihada za kununua na kumiliki mfumo madhubuti wenye leseni ya matumizi na uwezo mkubwa wa kusimamia, kuchunguza,kudhibiti, kufanya tathmini na kuongeza ulinzi katika mtandao, vifaa pamoja na miundombinu ya tehama iliyofungwa katika ofisi na matawi yote ya ZRB yaliyopo Unguja na Pemba ili kuweza kuhakikisha kwamba usalama wa matumizi ya mtandao na mifumo unaimarika kwa kiwango kikubwa pamoja na kurahisisha kazi ya ukusanyaji wa mapato kutoka kwa walipa kodi.

Aidha ukaguzi unashauri kwa ujumla taasisi za Serikali kutotumia zana

zilizokuwa hazina leseni ambazo hupatikana bure kutoka mitandaoni (free software tools) kwani zana hizo zinakuwa na uwezo mdogo wa kufanya kazi husika kwa mujibu wa namna zinavyotengenezwa ambapo mara nyingi hutengenezwa kwa majaribio au matangazo tu.

Vile vile kupitia zana hizo kunaweza kusababisha mifumo ya kuendeshea kompyuta (Operating Systems) kushambuliwa na virusi kwa urahisi na kupelekea kuharibika kwa taarifa zilizomo ndani ya kompyuta kutokana kuwa baadhi ya zana hizo pia hufanya na kazi nyengine ya kutumika kama ni programu maalum kwa ajili ya kuchunguza taarifa zilizohifadhiwa ndani ya mifumo ya kompyuta na kuzipeleka kunakohusika (malwares and spywares).

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Ni kweli, wakati wa ukaguzi huu Mamlaka haikuwa na mfumo wa "Network Mornitoring Tool". Kwa sasa Mamlaka imeshachakata manunuzi na mzabuni amepatikana, kwa kupitia zabuni nambari SMZ/FO111/G/CQ/2022~23/11 ya tarehe 22 Machi, 2023 na mkataba umefungwa tarehe 10 Agosti, 2023 ambapo matarajio kupatikana vifaa hivyo ndani ya siku thelathini kutokea tarehe iliyofungwa mkataba.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Mamlaka imekiri kuwepo kwa dosari hiyo na wameshaanza kuchukua hatua Kamati inaishauri Mamlaka kuwa makini katika kusimamia miundombinu pamoja na vifaa vya Tehama vilivyopo kwa kutumia program za kisasa pamoja na mifumo ya ufuatiliaji na kuachana kabisa na utumiaji wa zana ambazo hasina leseni ambazo zinapatika bure mtandaoni.

#### 13.1.1.7 Uwezo mdogo wa kifaa cha kurikodia matokeo katika kamera za CCTV (NVR)

Moja kati ya njia bora za kudhibiti na kuongeza usalama wa uhifadhi wa taarifa pamoja na mali za ofisi ni kufunga vifaa maalum vya ulinzi na usalama ambavyo vitasaidia kuonesha kumbukumu za matukio yote yanayofanyika katika mazingira ya ofisi na kubainisha muda uliofanyika wa matukio hayo kukiwa na lengo kusaidia kupatikana ushahidi kwa waliohusika kufanya matukio. Baadhi ya vifaa hivyo ni "CCTV Cameras" n.k.

Katika ukaguzi uliofanyika imbainika Bodi ya Mapato Zanzibar imefunga takribani kamera 110 katika jengo lake la Makao Makuu Unguja kwa ajili ya kurikodi matukio mbali mbali yanayofanyika katika nje na ndani ya ofisi hiyo ambapo taarifa hizo huhifadhiwa katika mtambo maalum wa kuhifadhia kumbu kumbu za matukio ya video (Network Video Camera - NVR) ambapo mtambo huo umeunganishwa moja kwa moja na CCTV cameras za Bodi.

Hata hivyo dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba mtambo huo wa kuhifadhia kumbu kumbu za matukio yanayorikodiwa moja kwa moja kupitia kamera una ujazo mdogo wa 8TB ukilinganisha na idadi kubwa ya kamera zilizofungwa na kurikodi katika maeneo yote ya nje na ndani ya ofisi ambazo ni takriban 110. Hali hii imepelekea mtambo kuwa na uwezo wa kuhifadhi kumbu kumbu za matukio kwa kipindi cha muda wa siku 45 pekee na baadae kuzifuta moja kwa moja ili kupatikana nafasi ya kuweka kumbu kumbu nyengine za matukio jambo ambalo linapelekea kutokupatikana kwa ushahidi wa matukio yaliyofanyika katika kipindi cha muda mrefu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Mapato kuhakikisha unaboresha uwezo wa mtambo wa kuhifadhia kumbukumbu za matukio yanayorikodwa kutoka katika kamera za CCTV ili kupata nafasi kubwa ya ujazo wa kuhifadhi

kumbu kumbu angalau kwa matukio yaliyofanyika katika kipindi cha miezi sita mfululizo ya nyuma kabla ya kufutika.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa ZRB kuhakikisha picha na video za matukio ya kihalifu zinazorikodiwa na CCTV zinatakiwa kuhifadhiwa kwa umakini na kuhakikisha zinafanyiwa nakala (backup) kumbu kumbu hizo katika sehemu nyingine nje ya mtambo ili kuepusha kumbu kumbu hizo kufutika wenyewe au kufutwa kwa makusudi na kupelekea kupoteza kwa ushahidi wa matukio yaliyofanyika.

**Majibu ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA)**

Uongozi unakubaliana na hoja ya mkaguzi, Kuanzia mwezi wa Oktoba 2022 Mamlaka imefanya maboresho katika kuongezea uwezo wa mtambo wa kuhifadhia kumbukumbu za matukio yanayorikodiwa kutoka katika kamera za CCTV ambao una ujazo 32TB kwa kila kifaa cha kurikodia (NVR) na kufanya jumla ya ujazo wa 64TB kwa vifaa viwili (2) vilivyopo, ambavyo vina uwezo wa kuhifadhi taarifa kwa muda wa miezi sita (6) na vimetenganishwa katika utendaji kazi wake. Hata hivyo, ZRA ina andaa hifadhi nyingine ya taarifa za CCTV cameras ambayo itawekwa katika ofisi ya ZRA Pemba itakayofanya kazi ya kuhifadhi taarifa za zamani.

Kwa sasa ZRA inaendelea na mchakato wa kutengeneza sera itakayosimamia matumizi ya mfumo wa CCTV cameras.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati imebaini kuwa Mamlaka imeshachukua hatua kwa kurekebisha dosari iliyopo hata hivyo Kamati inaishauri Mamlaka kukamilisha mchakato wa kutengeneza sera ya usimamizi wa mifumo ya CCTV camera pamoja na uandaaji wa hifadhi nyengine ya taarifa za CCTV cameras katika Afisi ya

Mamlaka Pemba ili kuwa na udhibiti imara wa matukio yanayorikodiwa na kuweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu.

## 14.0 UKAGUZI WA MIFUMO BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

### 14.2.1.1 Dosari katika utawala na Utawala wa Tehama (IT Governance)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) inatumia mifumo ya kielektroniki katika kuendesha shughuli mbalimbali muhimu za kiutendaji hususan katika utoaji wa huduma za kifedha kwa wananchi.Hata hivyo katika kusimamia Utawala wa Tehama dosari mbali mbali za kiutendaji zimebainika kama zifuatazo:-

- Kutokuwepo kwa mpango wa mkakati wa Tehama (IT Strategic Plan).
- Kukosekana kwa mpango wa uongozi wa usimamizi wa Tehama (IT Capacity Management Plan).
- Uwepo kwa sera za Tehama zisizokidhi haja kutokana na kutokufanyiwa mapitio na maboresho (updates) ambapo imebainika PBZ kwa mara ya mwisho ilifanya mapitio ya sera hizo mwaka 2018.
- Kutokuwepo kwa sera ya matumizi ya miradi ya Tehama pamoja na miongozo ya huduma zaTehama.
- Kukosekana kwa vipengele muhimu katika daftari linalotumika kuweka kumbukumbu za matokeo hatarishi na ya kuchukuwa tahadhari (IT Risk register).
- Kutokufanyika mafunzo kwa muda mrefu ya udhibiti na usalama katika mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa watumiaji na wasimamizi wa TEHAMA wa Benki.

Kutokana na kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kupelekea kukosekana kwa ufanisi katika utendaji kazi wa mifumo ikiwa ni pamoja na kuchelewesha

upatikanaji wa huduma za msingi na kwa wakati jambo ambalo linaweza kuisababishia hasara Taasisi kutokana na kuweza kujitokeza uharibifu au upotevu wa fedha unaoweza kusababishwa na kutokuwepo kwa umakini katika kusimamia masuala mazima ya utawala na uongozi wa mifumo ya Tehama.

Ukaguzi unashauri uongozi wa PBZ kuhakikisha unasimamia upatikanaji wa nyaraka muhimu za Tehama pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wake katika usimamizi na matumizi ya mifumo na kufanya tathmini ya viashiria hatarishi pamoja na kufanya majaribio ya kupenya kwa lengo la kubaini udhaifu uliopo katika mifumo na miundombinu ya Tehama ili kuweza kudhibiti na kulinda mifumo dhidi ya mashambulizi na udukuzi wa taarifa.**Majibu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

- Uongozi umekamilisha kuandaa mpango mkakati wa Tehama (ICT Strategic Plan 2023 - 2026) na unategemewa kwenda kupitishwa na kikao cha bodi cha robo ya tatu (3) 2023. Mpango huu umeandana na mabadiliko ya Tehama na mpango mkakati wa benki 2022-2026. Kukawia kukamilika kwa mpango huu kwa wakati kulitokana na kutegemea kukamilika mpango mkakati wa benki 2022-2026 na pia kukamilika kwa ripoti ya washauri elekezi kutoka kampuni ya Deloitte.
- Uongozi unatumia Mpango wa uongozi wa usimamizi wa Tehama (IT Capacity Management Plan) kupitia bajeti ya Tehama (ICT Budget) na kwa kawaida pia hutuma mahitaji pendekezwa kwa watoa huduma (vendors) wa mifumo husika katika kuandaa mahitaji ya mifumo kama "mahitaji ya hardware & software, mahitaji ya bandwidth, na makisio ya ukuwaji wa mahitaji.

- Uongozi umekamilisha kufanyia marekebisho ya sera za Tehama (ICT Policy & Procedure) na tayari imepitiswa na kikao cha bodi mwaka 2022. Sera hii imeandana na mabadiliko ya Tehama na mpango mkakati wa benki 2022-2026. Kukawia kukamilika kwa sera hii kwa wakati kulitokana na kutegemea kukamilika kwa mpango mkakati wa benki 2022-2026 na pia kukamilika kwa ripoti ya washauri elekezi kutoka kampuni ya Deloitte.
- Sera ya matumizi ya miradi ya Tehama pamoja na miongozo ya huduma za Tehama hizi zimeorodheshwa katika ICT Policy & Procedure iliyokamilishwa na kupitiwa mwaka 2022 ambayo imeendana na mapoendekezo ya mkaguzi wa serikali na mkaguzi maalum Delloite..
- Uongozi wa benki umeanza kuaandaa kumbukumbu za matokeo hatarishi na ya kuchukuwa tahadhari (IT Risk register), na kuwasilisha Idara ya kudhibiti vihatarishi (Risk Department) kila mwezi tangu mwaka 2022. Uongozi pia unaendelea kuboresha daftari hili kila mara panapotakiwa kuongeza kihatarishi. Hili zoezi endelevu kila tunapobioresha au kuongeza mifumo basi tunabudi kuongeza vihatarishi katika daftari hilo.
- Uongozi wa benki uliendesha mafunzo ya udhibiti na usalama katika mifumo na miundombinu ya Tehama kwa wafanyakazi mwaka 2022 na pia inatarajia kuendesha mafunzo haya ndani ya robo ya tatu (3) ya mwaka 2023 kwa wafanyakazi wote wa makao makuu na matawini. Vile vile, benki iliendesha mafunzo mbali mbali kwa wasimamamizi wa Tehama kwa mwaka 2022 na 2023 kama vile usimamizi wa mfumo wa uangalizi (monitoring system), usimamizi wa mfumo wa ulinzi (threat defence firewall), usimamizi wa mitandao (CCNA), ITIL n,k na pia kuwapeleka "attachment" kwenye benki nyenginezo ili kupata

uewelewa na uzoefu zaidi.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini Benki ya Watu wa Zanzibar imeshachukua hatua kwa baadhi ya dosari na dosari nyengine zinasubiri kuidhinishwa na bodi ili kuanza utekelezaji wake kama vile Mpango Mkakati wa Tehama ambao unatarajiwa kuidhinisha pamoja na Mpango Mkakati wa Benki wa mwaka 2022-2026

Aidha Kamati imebaini kuwa Sera ya  ya Tehama (ICT Policy) ya Benki imeshafanyiwa marekebisho na kupitishwa na Bodi hata hivyo Sera hiyo haijapelekwa kwa Wakala wa Serikali wa Mtandao E-Government kwa ajili ya kupatiwa Miongozo mbalimbali ya uundaji wa Sera hiyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri Benki ya Watu wa Zanzibar kukamilisha mchakato wa kuidhinisha Mpango Mkakati wa Tehama kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake ukizingatia kuwa mpango huo ndio dira ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Tehama kwa upande wa Benki.

Aidha Kamati inashauri Benki ya Watu Zanzibar kuwasilisha Sera ya Tehama ya Benki katika afisi za Wakala wa Miundombinu ya Tehama kwa ajili ya kupitiwa na kutolewa mapendekezo kwa mujibu ya miongozo ya Tehama ya kitaifa na kimataifa.

**14.2.1.2 Dosari katika Mpango wa Kuendeleza na Kusimamia Huduma za Biashara (Business Continuity Management Plan)**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 4.4.1.2(d) cha Sera ya Serikali Mtandao ya mwaka 2012 kinazitaka Taasisi za Serikali zenye kutumia mifumo kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao kuanzisha Mipango wa Kuendeleza na

Kusimamia Huduma za Mifumo na Miundombinu (BCP) pamoja na kuanzisha Mpango wa kupona maafa (DRP) endapo yakitokezea majanga dhidi ya miundombinu na mifumo katika taasisi.

Mpango huo unatarajiwa kuelezea utaratibu gani utatumika katika kuendeleza utoaji wa huduma wakati janga au dharura itakapotokezea katika taasisi, na hatua gani za kuchukuliwa kabla na baada ya janga kutokezea ili kuweza kudhibiti na kupunguza athari zinazoweza kutokezea pamoja na kurudisha huduma zinazotolewa na taasisi kwa wakati. Majanga yanayoweza kutokezea katika mifumo na miundombinu ya Tehama ni kama vile moto, mafuriko, udukuzi,virusi,wizi n.k

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba PBZ haikujiandaa ipasavyo katika kukabiliana na majanga pamoja na maafa yanayoweza kutokezea dhidi ya mifumo na miundombinu ya Tehama iliyopo, hali hii imebainika kutokana na kutokufanyiwa majaribio na kutokuimarishwa kwa Mpango uliopo wa Kuendeleza na Kusimamia Huduma za Biashara (BCP) endapo janga au dharura itakapotokezea, vile vile kutokufanyiwa mafunzo kwa wafanyakazi pamoja na wasimamizi wa mifumo na miundombinu ya Tehama ya Taasisi.

Kutukufanyiwa majaribio na kutokuimarishwa kwa mpango huo kunaweza kusababisha benki kuwa katika hali ya mazingira hatarishi na kutokezea athari zifuatazo:-

- Kushindwa kurejesha utoaji wa huduma za biashara kwa wakati jambo ambalo linaweza kupelekea kupoteza wateja kutokana na kukosa huduma na kusababisha hasara kwa Serikali.

- Kujitokeza kwa uharibifu na upotevu wa taarifa za benki, nyaraka mbali mbali , mali na miundombinu ya benki, fedha taslimu pamoja na maisha ya watu
- Kuingia hasara kwa kulipa fidia kutokana na aina ya janga lililotokea katika benki, kwa mfano kulipa fidia ya kukomboa dhidi ya shambulizi la mtandao linaloweza kufanyika katika mifumo ya benki (Ransomware), kulipa fi dia kwa wateja n.k.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kufanya maboresho ya Mpango huo kwa mujibu wa miongozo na sera za Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na kuzingatia miongozo na taratibu zinazokubalika kimataifa, aidha PBZ inashauriwa kujiwekea utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kufanya majaribio angalau mara moja kwa mwaka katika mipango yote inayolenga kulinda taarifa na kuendeleza huduma za biashara ambayo imegharimu fedha za Serikali, muda pamoja na jitihada kubwa katika utayarishaji wa mipango hiyo.

**Majibu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

Uongozi wa benki ulifanya majaribio ya kituo cha akiba cha kutunza data (Disaster Recovery site) mnamo mwezi Agosti 2022 na ina mkakati wa kufanyika jaribio jengine mwaka 2023 baada ya kukamilika uboreshaji wa mfumo mkuu wa kibenki ambao umemalizika mwezi Agosti 2023. Jaribio hili linatarajiwa kumalizika kabla ya kumalizika robo ya tatu (3) ya mwaka. 2023 Uongozi pia umeweka mikakati kufanya majaribio kila mwaka na kila pale panapotokea maboresho makubwa katika miundombinu au mifumo ya kibenki. Vile vile uongozi unategemea kukamilisha maboresho ya mpango uliopo wa kuendeleza na kusimamia huduma za Biashara (BCP) sambamba na kutoa mafuzo kwa wafanyakazi kabla ya kumalizika robo nne (4 ya waka 2023)

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa baada ya Mkaguzi kuibua daosari hii Benki imeanza kuchukua hatua ya majaribio ya kukabiliana na majanga pamoja na maafa yanayoweza kutokezea dhidi ya mifumo na miundombinu ya Tehama hata hivyo mchakato huu umefanyika bila ya kuwashirikisha Wakala wa Serikali Mtandao (E-Government).

Aidha Kamati imebaini Benki ya Watu wa Zanzibar haijakamilisha utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kukamilisha mpango wa kusimamia huduma za biashara (BCP) kama walivyoshauriwa na Mkaguzi jambo ambalo linaweza kuleta hasara kwa benki na Serikali pindi maafa yakitokezea katika mifumo kwa vile kurejesha huduma za mifumo baada ya maafa inahitaji gharama kubwa.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inashauri Benki ya Watu wa Zanzibar kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (E-Government) katika masuala mbalimbali ya Utekelezaji wa Shughuli za Tehama kwa vile wao ndio wenye Mamlaka kisheria wa Kusimamia utekelezaji wa Shughuli za Tehama Serikalini.

Aidha Kamati inashauri Benki kukamilisha kwa wakati kama ilivyojipangia kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kukamilisha mpango wa kusimamia huduma za biashara (BCP) ili kudhibiti kutokea maafa katika mifumo.

**14.2.1.3 Dosari katika usimamizi na udhibiti na matumizi ya Tehama (IT General Controls and Application Controls)**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba PBZ inatumia mifumo mbalimbali ya kielektroniki katika kuendesha shughuli muhimu za kiutendaji zinazowawezesha kutoa huduma kwa ubora na kwa wakati. Ukaguzi uliangalia maeneo mabalimbali ya kiutendaji ikiwemo programu za kuendeshea mifumo

(operating System), utaratibu na usimamizi katika mabadiliko ya mifumo ya Tehama (System Change Management) udhibiti wa upatikanaji wa taarifa kwa watumiaji (User Access Controls & Management) pamoja na utendaji kazi wa Tehama (IT operations). Dosari zilizobainika katika usimamizi na udhibiti wa matumizi ya Tehama ni kama ifuatavyo: -

- Kutokufanyika kwa tathmini ya Vihatarishi katika mifumo kwa muda mrefu (Vulnerability Assesment).
- Kutowahi kufanyika kwa majaribio ya kupenya katika mifumo kwa lengo la kupima udhibiti, uimara na usalama uliowekwa katika miundombinu ya Tehama (PenTest).
- Kukosekana kwa kumbukumbu za matokeo ya maboresho ya mfumo.

Aidha ukaguzi umebaini kukosekana kwa kumbukumbu za matokeo ya maboresho yaliyofanyika katika mifumo iliyokaguliwa ili kuthibitisha kuwa maboresho hayo yalifuatiliwa na kufanyiwa kazi baada ya kuombwa kufanyika.

Miongoni mwa maboresho ambayo ushahidi wake haukupokelewa yalikuwa ni Ombi la kufanyika kwa maboresho mapya katika mfumo wa "Internet Banking". (Change Request for applying new update on Internet Banking).

Kutokuwepo kwa usimamizi na udhibiti mzuri katika matumizi ya Tehama kunaweza kupelekea kukosekana kwa ufanisi katika matumizi ya mifumo ya kielektroniki ambapo Taasisi inaweza kuingia hasara inayotokana na matumizi mabaya na usimamizi usioridhisha wa mifumo na vifaa vya Tehama.

**Majibu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

- Uongozi wa benki umefanya tathmini ya ndani ya Vihatarishi (Internal Vulnerability Assessment) kwa kushirikiana na wakaguzi wan je katika ukaguzi wa mwaka 2021. Uongozi pia ulifanya tathmini hii kupitia kwa

mkaguzi wa nje (external auditor) kwa mwaka unaoishia 2022 ambapo dosari chache zilionekana kulinganisha mwaka 2021 na 2022 na dosari zimefanyiwa kazi na kuna nyingine zimetengewa bajeti kukamilishwa.

- Uongozi wa benki pia umefanya majaribio ya kupenya (Penetration Testing) mwaka 2022 kwa kupitia kwa mgaguzi wa nje (external auditor) ambapo dosari chache zilioonekana kulinganisha mwaka 2021 na 2022, pia dosari zimefanyiwa kazi.
- Uongozi wa benki pia umefanyia kazi dosari ya kukosekana kwa kumbukumbu za matokeo ya maboresho ya mfumo (change request) na kwa sasa unatumia mfumo maalumu wa kutunza taarifa za maboresho ya mifumo na miundombinu na taarifa muhimu zinatunzwa katika mfumo huo. Uongozi unaendelea kuweka mikakati matumizi ya mfumo huo na kukusanya taarifa na maboresho yanayofanywa na kuweka kumbukumbu pale itapokapohitajika kurejea na kufahamu maboesho yaliyofanyika kwenye mifumo na miundombinu ya benki.

**Uchunguzi na Mapendekeo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa Benki imeshachukua hatua katika dosari zilizobainishwa na Mkaguzi katika usimamizi na udhibiti wa Tehama hata hivyo Kamati inashauri Benki kuendelea na usimamizi na udhibiti wa mifumo ya Tehama kwa lengo la kuepusha benki kuingia hasara inayotokana na matumizi mabaya na usimamizi usioridhisha wa mifumo na vifaa vya Tehama.

**14.2.1.4 Dosari katika usimamizi wa matukio (Inadequate Incident Management Process)**

Ukaguzi umebaini kwamba PBZ wameanzisha mfumo wa Dawati la Usaidizi (Helpdesk System) ambao unatumiwa na wafanyakazi wa PBZ kwa ajili ya

kuripoti changamoto na dosari zinazojitokeza katika mifumo ya biashara ya benki kwa lengo la kuzitambua, kuzipatia ufumbuzi na kuzitatua kwa wakati.

Hata hivyo imebainika kwamba PBZ haina utaratibu mzuri wa kufanya mchakato wa kuyaripoti na kusimamia matukio kuanzia yanapotokezea, hatua ya ufuatiliaji hadi kukamilika na kupatiwa ufumbuzi. Aidha imebainika kutokuwepo kwa mkataba wa utoaji wa huduma (SLA) baina ya kitengo cha Tehama (IT Unit) na kitengo cha Biashara (Business Unit) jambo ambalo linaweza kupelekea kutokuwepo kwa maelewano ya utoaji na upatikanaji wa huduma za kibiashara baina ya vitengo hivyo

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ uanzishe utaratibu wa kina wa usimamizi wa matukio na kuhakikisha matukio yote yanaainishwa kulingana na vipaumbele vyake. Zaidi ya hayo, makubaliano ya kiwango cha huduma (SLA) kati ya vitengo vya IT na Biashara yanapaswa kutekelezwa ili kudumisha uwajibikaji na utatuzi wa matukio kwa wakati

**Majibu ya Benki ya Watu wa Zanzibar**

Uongozi wa benki unatumia mfumo wa Helpdesk kupokea matukio na kufanyia kazi maombi ya kutumia mifumo. Wafanyakazi wanapohitaji au wanapokuwa na shida ya mfumo wanatuma katika mfumo wa Helpdesk na maombi hufanyiwa kazi. Mfumo pia unarekodi muda uliotumika kufanyia kazi tukio au maombi au matukio yote huanishwa kulingana na vipaumbele vyake kama ya juu (High), ya kati (Medium) au ya chini (Low).

Uongozi wa benki pia umejumuisha vipengele vya mkataba wa utoaji wa huduma (SLA) baina ya kitengo cha Tehama and kitengo cha Biashara kupitia usimamizi miongozo ya matukio (incident management procedure) inayopatikana ndani ya Sera na Miongozo ya Tehama (ICT Policy and Procedures)

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa Benki imesharekebisha dosari hii baada ya Mkaguzi kupita hata hivyo Kamati inaendelea kushauri Benki kuimarisha mfumo wa "helpdesk" kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na ufanisi wa Shughuli za kibenki kwa kushughulikia kwa wakati changamoto za mifumo zinazoripotiwa na wafanyakazi kwa njia ya "Helpdesk"

**14.2.1.5 Kutokufanyiwa mapitio ya mara kwa mara shughuli za watumiaji na matukio ya mfumo (User activities and system events).**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa dosari mbali mbali za taarifa za watumiaji wa mfumo pamoja na taarifa za mfumo husika ambapo baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutokukaguliwa kwa shughuli za wasimamizi wa mfumo, mifumo ya uendeshaji na hifadhidata (database).
- Kutokufanyika kwa uhakiki na uchunguzi wa kumbukumbu za matukio yanayofanyika ndani ya mifumo pamoja na kompyuta za benki (Centralized Log Managment).
- Kukosekana kwa kifaa cha kufuatilia na kuchuja taarifa zinazoingia na kutoka pamoja na kusimamia matukio yanayofanyika ndani ya mfumo (Firewall)

Kutokukaguliwa kwa shughuli za Msimamizi wa mfumo (System Adminstrator) ambae mwenye uwezo mkubwa wa kuzifikia taarifa zote za mfumo, huduma, usalama, na uwezo wa kubadilisha utendaji kazi pamoja na mipaka ya matumizi katika mfumo kunaweza kupelekea kufanyika mabadiliko yoyote kinyume cha sheria kwenye mifumo bila ya kutambuliwa na kupelekea kuingiza hasara Serikali

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kuhakikisha kwamba shughuli zote za msimamizi wa mfumo pamoja na vipengele vya usalama zinapaswa kurekodiwa na kuchunguzwa. Aidha, marekebisho yote yatakayofanyika yanapaswa kuchunguzwa na kuthibitisha uhalali wake ambapo Afisa muhusika wa usalama wa mifumo (System Security Officer) ndie pekee anayepaswa kufikia taarifa za ndani za mfumo (System log).

**Majibu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

Uongozi wa benki kwa sasa hukagua shughuli (activity) za wasimamizi wa mifumo (IT Admins) kutumia wakaguzi wa ndani (Internal Audit) kwa kupitia mifumo kawaida (manually) kila robo ya mwaka.

Uongozi wa benki pia upo katika mikakati kununua mfumo wa kusimamia shughuli za wasimamizi wa mifumo (Privilege Access Management System). Mfumo huu utawezesha uongozi kusimamia kwa kina shughuli zote zinazofanyika katika mifumo pamoja na kuweka kumbukumbu ya kila shughuli inayofanywa ambapo Afisa muhusika wa usalama wa mifumo (System Security Officer) au wakaguzi wa ndani wataweza kufikia kumbukumbu hizo kwa ukaguzi. Mfumo huu unategemewa kukamilika kabla ya robo ya nne (4) ya mwaka 2023.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa Benki ya Watu wa Zanzibar bado ipo katika Mchakato wa kununua mfumo wa kusimamia shughuli zinazofanyika ndani ya mfumo (Privilege Access Management System).

Hivyo basi Kamati inashauri kumalizika kwa mchakato wa manunuzi wa wa mfumo huo kwa mwaka 2023 kama ilivyopangwa ili kudhibiti vitendo vinavyoashiria hujuma ndani ya mtandao kwa watumiaji wa ndani na nje ya

mfumo, aidha kuwashirikisha ipasavyo Wakala wa Serikali Mtandao katika utekelezaji wa Shughuli hii kwa lengo la kupata miongozo kupitia wakala huyo.

### 14.2.1.6 Dosari ya utumiaji wa akaunti za asili za Mifumo na Kanzidata (Default System Account – Administator Account)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa matumizi ya akaunti za asili katika mifumo ya mbalimbali inayotumika kwa kundeshea shughuli za biashara za PBZ. Miongoni mwa mifumo inayotumia akaunti za asili ni pamoja na Mfumo wa "Cheque Point(SQL Server 2014) unaofanya kazi katika Windows Server 2012 pamoja na akaunti asili ya Active directory." Aidha imebainika kuwa Akaunti ya asili "sa" haijazuiliwa kutumika katika kanzidata ya CTS (MS SQL Server 2008).

Kuendelea kutumika kwa akaunti hizo kunaweza kupelekea kutoa nafasi kwa wahalifu na wadukuzi wa mitandao kuweza kufanya mashambulio ya kimtandao (Cyber Attack) ambapo kunaweza kuisababishia upotevu wa taarifa na kupelekea kuingiza hasara Serikali

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kutokuendelea kuzitumia akaunti hizo ikiwa hakuna sababu ya msingi au kuzibadili majina ili kudhibiti na kuziba mianya ya uwezekano wa kutokezea uhalifu katika mifumo ya Benki.

**Majibu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

Uongozi wa benki umesitisha na umeacha kuzitumia akaunti za asili ya "sa" kwenye mfumo wa "Cheque Point" baada ya kufanyika maboresho ya mfumo huu ndani ya robo ya pili (2) ya mwaka 2023 ambapo kwa sasa unatumia kanzi data ya SQL Server 2019 unaofanya kazi katika Window Server 2019 ili kudhibiti na kuziba mianya ya uwezekano wa kutokezea uhalifu katika mifumo ya benki.

Uongozi pia umesitisha kuendelea kutumika kwa account za asili za Active Directory ambazo hazihitajiki kwa matumizi ya kila siku pia kubadilisha majina kwa account zinazohitajika kuendelea kutumika kama ilivyoshauriwa. Zoezi hili lilikamilika ndani ya robo ya kwanza (1) ya mwaka 2023.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Benki ya Watu wa Zanzibar imekiri kuwepo kwa dosari hiyo hata hivyo hatua zimeshachukuliwa  na kwasasa akaunti hizo hazitumiki tena, Kamati inashauri Benki ya Watu wa Zanzibar kuwa makini matumizi ambazo si salama kwa vile ndio chanzo cha kuleta matukio ya kihalifu ndani ya mtandao.

**14.2.1.7 Dosari katika usajili na ufuatiliaji wa akaunti zinazotumika katika Mifumo na Kanzidata**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa PBZ haina program maalum za kuchunguza na kusimamia akaunti zinazotumika katika uendeshaji wa mifumo ya PBZ (service accounts), aidha imebainika kuwa akaunti hizo hazifanyiwi usajili kwa lengo la kuzitambua na kuzifatilia matumizi na huduma zinazofanya katika mifumo na kanzidata za benki. Baadhi ya akaunti zilizobainika ambazo hazijafanyiwa usajili katika System Account Register na hazifuatiliwi na kuboreshwa matumizi yake ni kama zifuatazo:-

Akaunti za ujumla (generic account) katika "Active Directory" ambapo majina yake yamebainishwa kama ifuatavyo:-

- Cert Publishers
- DefaultAccount
- Administrator
- DnsAdmins
- DnsUpdateProxy
- echannels3

- Electronic Channels
- Electronic channels 2
- Guest
- Sheha
- temp1
- sqlstart Epic
- IUSR_BRSERVER
- BANKING OP. OPERATION

Kutokana na kuwepo kwa akaunti za ujumla zisizosajiliwa na kusimamiwa katika utendaji wake kunaweza kupelekea uwezekanao wa matumizi mabaya ya mfumo yanayoweza kufanywa na watendaji wasio waaminifu ambao mara nyingi huzitumia akaunti hizi kwa maslahi binafsi kwa vile hazina majina mahsusi ya watumiaji ambapo kutapelekea kujitokeza vitendo vya ubadhirifu wa fedha na kuingiza hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kuhakikisha kwamba kila mtumiaji anapewa akaunti kwa mujibu wa miongozo na taratibu za kibenki na kuhakikisha anawekewa mipaka ya matumizi katika mfumo, aidha kuhakikisha kwamba hakuna utengenezaji na utumiaji wa akaunti za jumla kukiwa hakuna umuhimu wa matumizi yake, na kama zikihitajika kutumiwa zinatakiwa kusajiliwa na kupewa idhini ya matumizi kwa watu maalum katika mfumo

**Majibu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

Uongozi wa benki umefanya maboresho kwenye akaunti zinazotumika kuendesha mifumo, ambapo akauti zisizotumika ziliondolewa na nyegine zilifungiwa (disabled) ndani ya robo ya kwanza (1) ya mwaka 2022.

Uongozi pia umechukua hatua ikiwemo kubadilishwa, kuhifadhiwa na kupewa watu maalum wanaohusika na usimamizi wa mifumo kwa account

zinazoendelea kutumika kuendeshea mifumo na kanzidata baada ya kufanyika kwa moboresho ya mifumo ambapo zoezi hili lilikamilika ndani ya robo ya kwanza (1) ya mwaka 2023.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile uongozi wa Benki umeshachukua hatua ya kuboresha dosari hii Kamati inasisitiza uongozi wa Benki kufuatilia kwa karibu mifumo mbalimbali wanaoyoimiliki na kuiboresha zaidi kiusalama kwa kuendelea kuweka programu za ufuatiliaji wa mifumo kulingana na mabadiliko ya teknolijia yanavyotaka.

**14.2.1.8 Udhibiti usiofaa wa Akaunti za Watumiaji kwenye "Active Directory"**

Katika ukaguzi uliofanyika imabainika kuwepo kwa orodha ya watumiaji wa "Active Directory" 78 ambao wamepewa dhima (Priviledge) ya kuwa wasimamizi wa mfumo (System Admin) hali ya kuwa wao ni watumiaji wa kawaida, pamoja na dosari hiyo ukaguzi umebaini uwepo wa akaunti zenye kujirudia mara mbili kwa watuamiaji wa mifumo hiyo. Kiambatisho Namba 26 kinahusika.

Kuwepo kwa idadi kubwa ya wasimamizi katika mifumo ambao hawakupaswa kuwa na ulazima wa kupewa dhima ya usimamizi katika akaunti zao za mifumo (Admin priviledges) kunapelekea kupewa haki zisizostahiki katika matumizi ya mfumo jambo ambalo linaweza kusababisha hatari ya kufanyika kwa vitendo vya kihalifu na ubadhirifu wa fedha katika mifumo ya benki.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kufanya uhakiki wa kina kwenye akaunti za watumiaji waliomo kwenye "Active Directory " pamoja na kanzidata za mifumo ya kibiashara inayotumika katika benki na kuhakikisha kuwa kila mtumiaji anamiliki akaunti moja katika mfumo na kwamba haki za usimamizi wa mifumo

zinatolewa kwa wanaohusika tu kwa lengo la kuongeza udhibiti na usalama katika usimamizi wa mfumo.

**Majibu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

Uongozi wa benki umemfanya uhakiki wa kina kwenye akaunti za watumiaji waliomo kwenye "Active Directory" na kuondoa akauti za watumiaji waliopewa dhima kimakosa hali ya kua ni watumiaji wa kawaida na pia kufanya uhakiki wa watumiaji kuhakikisha kuwa kuwa kila mtumiaji anamiliki akaunti moja katika mfumo na kwamba haki za usimamizi (access rights) wa mifumo zinatolewa kwa wanaohusika tu kwa lengo la kuongeza udhibiti na usalama katika usimamizi wa mfumo. Uongozi pia umeekueka mpangilio wa akaunti kujifunga yenyewe kama mtumiaji hajatumia akaunti ndani ya siku 30. Zoezi hili lilkamilika ndani ya robo ya pili y mwaka 2022

Uongozi pia umeweka mkakati wa kupitia watumiaji wa mifumo kila baada miezi 3 kwa kutumia kwa wakaguzi wa ndani.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Benki ya Watu wa Zanzibar imeshachukua jitihada ya kuondosha dosari hiyo kwa kuondoa akauti za watumiaji waliopewa dhima kimakosa hali ya kua ni watumiaji wa kawaida na badala yake haki za usimamizi (access rights) wa mifumo zinatolewa kwa wanaohusika tu.

Kamati inaendelea kushauri Benki ya Watu wa Zanzibar kulisimamia hili ipasavyo kwani akaunti za watumiaji zisizohusika zinaweza kupewa haki zisizostahiki katika matumizi ya mfumo jambo ambalo linaweza kusababisha hatari ya kufanyika kwa vitendo vya kihalifu na ubadhirifu wa fedha katika mifumo ya benki

#### 14.2.1.9 Dosari katika chumba maalum cha kuhifadhia taarifa (Physical Access to Data Centre)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba PBZ wanamiliki sehemu maalum kwa ajili ya uzalishaji wa taarifa pamoja na vituo vya uokozi wa taarifa (Production and Disaster recovery Center) ambapo dosari mbalimbali za kiukaguzi zimebainika katika maeneo hayo kama ifuatavyo:-

- Kutokuwepo kwa kamera za CCTV zinazosaidia kuimarisha ulinzi wa maeneo.
- Kuwepo kwa vitu vinavyoweza kushika moto kwa haraka na kuongeza kasi ya mripuko wa moto (maboksi) katika Kituo cha Uokozi wa Taarifa (DR Center).
- Kutokutunzwa kwa kumbukumbu za wageni wanaoingia na kutoka katika chumba cha Seva.

- Kukosekana ushahidi wa ukaguzi wa mara kwa mara katika kituo cha Uokozi wa Taarifa.

- Kukosekana kwa mafunzo ya kupambana na majanga ya moto kwa wafanyakazi wa TEHAMA.

Bila ya kuwepo kwa utaratibu mzuri ulioidhinishwa, uingiaji wa kiholela katika vyumba vya kuhifadhia taarifa hauwezi kugunduliwa kwa urahisi jambao ambalo linaweza kusababisha kutokea athari mbali mbali ikiwemo kupotea vifaa vilivyomo ndani ya chumba kwa kuchukuliwa kinyume na utaratibu, kupotea au kuharibiwa kwa taarifa pamoja na kupelekea kujitokeza kwa majanga yasiyotarajiwa kutokana na kutofahamika kwa sheria na miongozo ya Sehemu hizo.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa PBZ kuongeza usalama katika vituo hivyo ikiwa ni pamoja na kuweka miongozo na utaratibu ulio bora wa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vituo na kuweka kumbukumbu nzuri za wageni wanaoingia na kutoka katika maeneo hayo pamoja na kuweka vifaa maalum vya kudhibiti na kusimamia usalama kama vile CCTV Kamera na walinzi ili kuepusha kujitokeza kwa mambo ya kihalifu.

**Majibu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

- Uongozi wa benki umefunga kamera za CCTV zinazosaidia ulinzi na pia kuondoa vitu vyote vinavyoweza kushika moto katika kituo cha Uokozi wa Taarifa (DR center) ndani ya robo ya kwanza ya mwaka 2022
- Uongozi wa benki pia umeeka madaftari maalumu ya kutunza kumbukumbu za wageni wanaoingia na kutoka katika chumba seva ndani ya robo ya kwanza ya mwaka 2022
- Uongozi unafanya ukaguzi kila baada ya miezi mitatu kwa vituo vyote vya taarifa kutumia wakaguzi wa ndani na kupitia mifumo wa kibayometriki
- Uongozi uliendesha mafunzo ya kupambana na majanga ya moto kwa wafanyakazi wote wakiwemo wa Tehama mwaka 2022 na mafunzo haya hufanyika kila mwaka

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Benki ya Watu wa Zanzibar imeshachukua hatua ya kurekebisha dosari hii hata hivyo Kamati inashauri uongozi wa Benki kuendelea kutoa mafunzo ya kupambana na majanga ya moto kwa wafanyakazi wote wakiwemo wa Tehama kwa lengo la kuweza kuikabili hali hiyo pindi inapotokea ili kudhibiti uharibu wa vifaa pamoja na miundombinu ya Tehama iliyowekwa katika vituo vya kuhifadhia taarifa (Data Center) na katika maeneo ya kazi.

#### 14.2.1.10 Dosari katika matumizi ya programu zilizoisha muda (Unsupported Software Versions)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa programu mbambali zinazotumiwa katika kuendeshea mifumo ya kielektroniki. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuendelea kutumika programu ambazo muda wake wa matumizi umepitwa na wakati kutokana na viwango vya matumizi na matoleo mapya yanayotolewa na kuboreshwa na watengenezaji wa programu (software vendors),miongoni mwa prgramu zilizobainika kuisha muda wa matumizi (End Life Support) ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 44 : Programu zinazoendelea kutumika PBZ ambazo zimeisha mudawa matumizi**

| Namba | Programu Husika (Software) | Toleo (Version) | Muda wa Mwisho wa Matumizi (End of Life Support) |
|---|---|---|---|
| 1. | Microsoft SQL Server | 9 | 12 Aprili,2016 |
| 2. | Microsoft Windows Server | 2008,7 | 14 Januari,2020 |
| 3. | PHP | 5 | 01 Januari,2019 |
| 4. | Python | 3.6.8 | 12 Disemba,2021 |
| 5. | OpenSSL | 0.9.8x | 01 Januari,2016 |
| 6. | Microsoft IIS | 7.x | 14 Januari,2020 |
| 7. | Cisco IOS | 15.3 | 04 Juni,2020 |

Kendelea kutumia programu ambazo zimeshamaliza muda wa matumizi kunaweza kusababisha mifumo kutokuwa na kinga, usalama na ulinzi imara wa kuzilinda taarifa pamoja na kutoa huduma kwa ufanisi, jambo ambalo litapelekea mifumo kuweza kushambuliwa kwa urahisi dhidi ya virusi na wadukuzi wa mtandao na kusababisha kutokezea athari kubwa ya kuharibika na kupotea kwataarifa za benki na hatimae kuisababishia hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuimarisha mifumo na programu zake zote zinazotumika katika uendeshaji na utoaji wa huduma za biashara ili kuweza kuendelea kutoa huduma zenye kiwango bora, kwa wakati na kwa ufanisi pamoja na kuweza kujikinga na majanga yanayoweza kujitokeza katika utoaji wa huduma za benki.

**Majibu ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)**

Uongozi wa Benki umeimarisha mifumo na programu zake ndogo ndogo zilizoisha muda na ambazo zina mifumo inayotumika katika uendeshaji na utoaji wa huduma za biashara ili kuweza kuendelea kutoa huduma zenye kiwango bora, kwa wakati na kwa ufanisi pamoja na kuweza kujikinga na majanga yanayoweza kujitokeza katika utoaji wa huduma za benki. Zoezi hili lilikamilika ndani ya robo ya tatu ya mwaka 2022

Pia Uongozi wa benki mwanzo wa mwezi Agosti 2023 umefanikisha uboreshaji wa mfumo mkuu wa kibenki (Core Banking) kuongeza ufanisi wa utendaji na huduma kwa wateja.

Kwa mifumo ya zamani yenye taarifa zinazotumika kwa kumbukumbu kama mfumo wa zamani wa kibenki uongozi umeutenganisha na mifumo inayotumika kwa vile hautumiki kwa matumizi ya kawaida na haitowezekana kuimarisha kwa sasa

Uongozi wa benki utaendelea kuboresha mifumo na program zake kuendana na teknolojia na usalama wa mifumo ya Tehama.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Uongozi wa Benki umesharekebisha dosari iliyoibuliwa na Mkaguzi na kwasasa wanatumia program/software zinakwenda na wakati, hata hivyo Kamati inashauri Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kuendelea kutumia

program na vifaa vya Tehama kwa mujibu wa mabadiliko ya teknolojia na kuweza kuziboresha zaidi kulingana na mahitaji kwa wakati husika (update) kwa ajili ya kupata udhibiti mzuri wa kiulinzi na Usalama wa mifumo.

## 15.0 SHIRIKA LA UMEME ZECO

### 15.2.1.1 Kutokuwepo kwa wataalamu wa Mifumo (System Developers) katika muundo wa Idara ya Tehama.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kitengo cha Tehama, kina jumla ya watumishi saba (7) ambapo watumishi wawili kati yao walibainika kutokuwepo kazini kwa sababu tofauti, hali hiyo imepelekea kitengo kwa muda mrefu kuwa na watumishi watano tu waliopo kazini ambao ndio wanaotekeleza majukumu yote yanayohusiana na kazi za Tehama. Hali hii imepelekea kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu ya kusimamia mifumo na miundombinu ya Tehama jambo ambalo linaweza kusababisha kupungua kwa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na kupelekea kujitokeza kwa usumbufu ikiwemo ucheweshaji wa upatikanaji wa huduma za umeme zilizo bora na kwa wakati kwa wananchi.

Aidha ukaguzi umebaini licha ya kuwa Shirika limewekeza kwa kiasi kikubwa kwenye mifumo mbalimbali katika utendaji wake wa kazi za kila siku lakini bado lina uhaba katika fani ya watengenezaji wa mifumo pamoja na programu (system developers/programmers) jambo ambalo linalosababisha kuongezeka kwa ugumu katika kazi ya kusimamia mifumo, kubuni, kusasisha au kuboresha mifumo kupitia programu za kuboresha mfumo (system patches) na pia kupatikana ushauri wa kitaalamu juu ya ya uwepo wa aina gani za mifumo inayoendelea kuhitajika kwa Shirika ikiwa ni pamoja na miundombinu ya mtandao na Seva zinazotoa huduma hizo kupitia ofi si na vituo vyake vya kuuzia umeme ili kuweza kukidhi mahitaji ya utendaji kazi wa mifumo, kufahamu umuhimu na kumiliki misimbo (source codes) zinazotumika katika kutengeneza,kusimamia na kuimarisha utendaji kazi wa mifumo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZECO kuhakikisha unaweka kipaumbele katika mpangilio wake kuwajengea uwezo watendaji waliopo wa kitengo cha TEHAMA pamoja na mpangilio wa ajira zijazo kuongeza maafi sa tehama watakaokuwa na fani ya Utengenezaji na usanifu wa mifumo/ programu (system developers/programmers) ambao watakuwa na uwezo mkubwa katika kusanifu, kuboresha, kutengeneza na kusimamia mifumo yote ndani ya shirika ambapo wataalam hawa pia watasaidia kutoa muongozo wa namna ya kuwa na mfumo bora inayohitajika kwa Shirika ikiwa ni pamoja na kutunza na kusimamia 'source codes' , kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika utendaji kazi wa mifumo na vile vile kuweza kusaidia kutoa vigezo vinavyohitajika katika uingiaji wa mikataba ya manunuzi ya Mifumo kutoka kwa wauzaji wa mifumo (System Vendors) ili kuweza kuendelea kupatikana huduma bora zenye tija na ufanisi katika utoaji wa huduma za umeme kwa Shirika

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Kwa mwaka fedha 2022/2023 Shirika lilifanya jitihada ya kumtafuta mtaalamu huyo kutoka kwa watendaji wa ndani wenye sifa zilizotajatwa, hata hivyo hakupatikana mtu mwenye sifa hizo. Katika kuendeleza juhudi hizo za kupata mtaalamu huyo Shirika limepanga kuomba kupatiwa mtaalamu huyo kutoka katika taasisi za Serikali kupitia utaratibu wa utumishi wa umma kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024. Aidha, Shirika limefanya juhudi katika kutafuta watalaamu kutoka chuo kikuu cha Taifa (SUZA) kwa lengo la kuwapatia watendaji wake taaluma ya usimamizi wa mifumo ya TEHAMA ili kufikia lengo lililowekwa. Hatua iliyofikiwa hivi sasa ni kuendeleza mazungumzo kwa ajili kusainiwa kwa makubaliano ya awali kwa ajili ya kazi hiyo.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Shirika la umeme limekiri kukosa wataalamu wa kutengeneza mifumo katika muundo wa idara ya Tehama licha ya juhudi walizochukua katika kutafuta wataalamu hao lakini bado changamoto hiyo haijaweza kutatuka hadi Kamati ilipofanya ukaguzi wake.

Hata hivyo Kamati inalishauri Shirika kuharakisha mchakato wa makubaliano na Chuo Kikuu cha Taifa kwa ajili ya kupatiwa watalamu hao kusimamia mifumo ya Tehama pamoja na utengenezaji wa mifumo ya ndani, kwani kukosa wataalamu hao hadi sasa kunalisababishia shirika kutokuwa na usimamizi mzuri wa mifumo ya Shirika aidha kukosa utaalamu wa kujua ni aina gani ya mifumo inayohitajika kwa sasa ambayo italeta ufanisi katika utoaji wa huduma za umeme.

**15.2.1.2 Kutokuwepo kwa umiliki wa mifumo inayoitumiwa na ZECO.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa ZECO haina Mkataba wa kumiliki mifumo wa Programu (source code) kutoka kwa watengenezaji wa mifumo wanayoitumia kama vile mfumo wa Suprima, mfumo wa tukuza (Aquilium), mfumo wa SAP na mfumo wa Call Center.

Ukaguzi umebaini kwamba shirika lipo mbioni kuacha kutumia mfumo wa Aquillium (post-paid system) kwa sababu mfumo huo kwa sasa unakosa msaada wa matengenezo ambapo muuzaji wa mfumo huo anaonekana hayupo tena sokoni hali ambayo imepelekea shirika kupata taabu sana kuendelea na matumizi ya mfumo huo. Hali hii inatokana na kutokuwepo kwa umakini kwa ZECO ambapo kupitia makubaliano ya mkataba baina ya ZECO na muuzaji wa mfumo huo wa Aquilium,pia mfumo huu haujaboreshwa (system patch) tangu

mwaka 2012 pamoja na kuwepo na mabadiliko mengi na ya muda mrefu kuanzia mwaka 2012 hadi 2022 kutoka kwa watengenezaji aw mfumo.

Aidha shirika lilinunua mifumo inayoitumia bila kuzingatia matakwa ya mikataba na bila kupata ushauri mzuri wa kitaalamu kabla ya kununua au kukubaliana jinsi ya kumiliki mifumo endapo wauzaji hawatokuwapo tena sokoni.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Umeme kuhakikisha kwamba mifumo yote inayonunuliwa na kutumiwa na ZECO, inapaswa kuwa na mikataba ilio imara yenye vifungu vya kumbana kisheria muuzaji ,hali ambayo itasaidia endapo kutatokea sababu zisizotarajiwa kwa wauzaji wa mifumo hiyo kuacha biashara,kufilisika au kushindwa kusimamia mifumo hiyo kutaliwezesha shirika kupata usaidizi kwa kushirikiana na mtoa huduma mwingine kuendesha mifumo endapo mtengenezaji wa mifumo wa awali ataacha kutoa msaada kwa watumiaji/wateja

**Majibu ya Shirika la Umeme (ZECO)**

Ni kweli kwamba shirika halina umiliki wa mifumo tajwa katika hoja kwa kuwa Shirika linatumia mifumo ambayo imeshatayarishwa kwa mahitaji maalum “offshelf” ya uuzaji na ununuaji wa umeme ambapo Shirika linalipia leseni pekee ya matumizi ya mfumo husika. Hata hivyo, Shirika la umeme limejipanga kuongeza kipengele kinachohusiana na mambo ya *escrow agreement* katika mikataba itakayofuata, kwa kuzingatia hilo kwasasa mkataba unaotarajiwa kuwekwa kipengele hicho ni mkataba na kampuni ya Hexing.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Shirika la Umeme Zanzibar limekiri kutokuwa na umiliki wa mifumo wanayoitumia iliyotajwa na Mkaguzi, hata hivyo kwa sasa wameshaanza

kuchukua hatua kwa mifumo inayokuja kuhakikisha wanafunga mikataba imara ya kuhakikisha wanapata umiliki halali wa mifumo ambayo wanainunua kwa watengenezaji ikiwa ni pamoja na kupatiwa (Source code) ya mifumo husika

Kamati inaungana na ushauri uliotolewa na Mdhibiti wa kulitaka shirika kuendelea kusimamia vyema mikataba wanayoingia na wauzaji wa mifumo kwa kupatiwa umiliki (source code) hii itaweza kusaidia kupata msaada wa kifundi na maboresho mengine ya mifumo ikiwa mtengenezaji wa mfumo atafilisika au kuacha kufanya biashara kabisa.

**15.2.1.3 Kukosekana ulinzi wa taarifa muhimu za mifumo.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) halijaweka udhibiti wa taarifa muhimu kama vile (password) na (security keys) za mifumo ambazo hutumika wakati wa kutuma na kuhifadhi taarifa muhimu za mifumo ili kuhakikisha kunakuwepo na usiri na uadilifu katika upatikanaji wa taarifa za mifumo hiyo.

Hali hii imepelekea kuwepo na udhaifu katika kulinda rasilimali muhimu za taarifa za mifumo na udhaifu wa udhibiti wa rasilimali ya taarifa muhimu za mfumo,mbapo udhibiti wa taarifa (data encription),upatikanaji na utumiaji (access control) wa taarifa muhimu za mifumo unaweza kuwafi kia mtumiaji ambae hakuruhusika kiutaratibu na hivyo kuweza kupelekea kupata uwezo ambao utamruhusu mtu huyo kukwepa vipengele vya usalama wa mifumo na taarifa na hivyo kuweza kusoma, kurekebisha, au kuharibu taarifa au rasilimali nyingine za mifumo kama seva na kompyuta.

Ukaguzi unashauri wasimamizi wa usalama wa mifumo na taarifa (IT Security) wa ZECO kuchukuwa juhudi za makusudi katika kulinda taarifa muhimu za mifumo ya Shirika dhidi ya uwezekano wa mashambulizi ya programu

zinazoathiri mifumo (ransom-ware),virusi vya mtandao (internet virus) pamoja na wizi wa taarifa za mifumo na mashambulizi ya kimtandao (Cyber attack) jambo ambalo linapotokea linaweza kupelekea shirika kuingia hasara kubwa kwa kulipa ada ya kugomboa taarifa(ransom).

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Shirika la Umeme kwa mwaka fedha 2020/2021 lilikuwa linatumia vifaa vya ulinzi wa mtandao ambavyo kulingana na matumizi halisi ya Shirika ilikuwa tayari vimezidiwa uwezo wa kufanya kazi. Kwa kuzingatia hilo, Shirika lilifanya maboresho kwa kununua vifaa maalumu vya kukinga mashambulizi ya kimtandao (firewall) ambapo vifaa hivyo tayari vimeshafungwa katika miundombinu ya Shirika la Umeme.

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa shirika lilikuwa na program za ulinzi wa mifumo lakini program hizo haziendani na mahitaji ya mifumo uliyopo kwa vile imeshapitwa na wakati na ni rahisi kushambuliwa na virusi na mashambulizi ya kimtandao (Cyber attack).

**Mapendekezo ya Kamati**

kwa vile Shirika limesharekebisha dosari hiyo kwa kununua vifaa vya ulinzi wa mifumo ya Tehama vya kisasa, hata hivyo Kamati inasisitiza juu ya umakini wa Shirika katika kuongeza Zaidi vifaa vya ulinzi dhidi ya mashambulizi ya Kimatandao ambayo yanaweza kuathiri shughuli mzima ya utoaji huduma za umeme Zanzibar na kupelekea hasara kwa Shirika na Serikali kwa ujumla.

#### 5.2.1.4 Kutokukidhi vigezo kwa eneo la kuokoa maafa (Data Recovery Center)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Umeme ZECO linamiliki eneo la kuokoa maafa (Data Recovery Center) ambapo kikawaida eneo hili hutumika kwa kuwekea vifaa vinavyo huhifadhi nakala za taarifa (Data Backup) kwa ajili ya matumizi ya baadae endapo kukitokea hitilafu au kuimarisha mifumo(Updates).

Aidha imebainika kwamba maeneo ambayo kipo kituo cha kuokoa maafa Saateni ni masafa ambayo ni mafupi kutoka zilipo Ofi si kuu ya Shirika Gulioni,jambo ambalo endapo kutatokea maafa kuna uwezekano mkubwa wa kuathiri hadi kituo cha kuokoa maafa.hali hii imepelekea kituo hicho kukosa sifa na vigezo vinavyokubalika kulingana na utendaji kazi bora na viwango vya kimataifa kama vile ISO Standard 7031 vinavyozingatia mahitaji ya teknolojia ya habari na mawasiliano (ITC) kwa ajili ya kuendelea na biashara na kujitayarisha kwa maafa.

Utendaji kazi bora unahitaji taasisi inayotumia mifumo ya TEHAMA kama nguzo katika uendeshaji wa shughuli muhimu za kiutendaji ni lazima iwe na Mpango wa Kuokoa Maafa (DRP) na Mpango wa Kuendeleza Biashara (BCP) ambao unahitaji kuwa na maelezo muhimu na yenye kujitosheleza juu ya uendeshaji ambayo yanaruhusu uhuwishaji wa shughuli za kazi kama ulivyoandaliwa, kwa utaratibu na kwa wakati.

Ukaguzi umebaini hati na miongozo ifuatayo haikuwepo kama vile maelezo ya mawasiliano ya dharura, timu za uokoaji, hifadhi rudufu ya data muhimu nje ya sehemu ya kuhifadhia data kwa ajili ya dharura, mbinu mbadala ya mawasiliano na awamu ya waokoaji kama fi re brigade, polisi na kadharika, ingawa baadhi ya hatua za usalama zilizopo sasa zinaweza kutumika kurejesha

huduma za Tehama, kuna uwezekano mkubwa kwamba iwapo maafa makubwa yatatokea kwenye chumba cha kompyuta, uendelezaji wa shughuli za Tehama unaweza kuathirika. Aidha taarifa (data) zinazohifadhia kwa ajili ya kujikinga na maafa hazijaribiwi kwa ajili ya urejeshaji na hakuna utaratibu wa mara kwa mara wa kufanya nakala rudufu (backups) kwa ajili ya urejeshaji na mpango wa mwendelezo wa biashara hali hii inaweza kupelekea taarifa (data) za shirika kuwa katika hatari kubwa ya kutopatikana ikiwa janga litatokea.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZECO kuhakikisha kwamba wasimamizi wa usalama wa Tehama kupitia Kamati ya Uongozi ya Tehama kutafuta mahali panapofaa kwa ajili ya eneo la pili la uokoaji ambalo litakidhi vigezo vya mafasa (mahali pa mbali na mazingira ya ZECO HQ) pamoja na kupitia upya na kusasisha mara kwa mara na kwa wakati (Business continuity and Disaster Recovery Plans) ikiwa ni pamoja na kuandikwa upya,kusambazwa pamoja na kuhifadhiwa nje ya sehemu ya uhifadhi wa taarifa (data) makao makuu.

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Kwa sasa Shirika la Umeme Zanzibar limeweka kituo chake cha kuokoa taarifa za kimfumo katika ofisi zake zilizopo Saateni ambapo kimasafa kutoka ofisi kuu Gulioni ni karibu. Kwa kuzingatia hilo Shirika tayari limeshafanya mazungumzo na Wakala wa Miundombinu ya Tehama kuangalia uwezekano wa kutumia data center yake katika kuhifadhi mifumo muhimu ambapo Wakala wa Miundombinu kupitia barua yake ya tarehe 29/03/2023 tayari wameshatoa upembuzi wa gharama zinazohitajika kutokana na Mahitaji ambayo Shirika la Umeme liliwasilisha. Hivyo kutokana na umuhimu wake Shirika limepanga kutekeleza jambo hili katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024. Hata hivyo Shirika linafikiria kuhamisha kituo cha kuokoa  taarifa muhimu za mifumo kutoka kituo cha Saateni kwenda Makunduchi.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limekiri kuwepo kwa dosari hiyo na tayari wameshaanza kuchukua hatua ya kuomba kutumia data center ya Wakala wa miundo mbinu ya Tehama, hata hivyo Kamati ya laac inalishauri Shirika kukamilisha mchakato wa kuhamisha kituo hicho kutoka Saateni kwenda makunduchi ili kukidhi vigezo vya masafa ya zaidi ya kilomita 50 kutoka makao makuu ya Afisi hadi kituo kilipo ili kwenda sambamba na taratibu bora na miongozo ya Disaster Recovery Site.)

**15.2.1.5 Kutokufanya majaribio ya kupima usalama (Penetration Test)**

Kwa mujibu wa viwango (ISO 27001 mfumo wa usimamizi wa usalama wa habari) unahitaji kwamba upimaji wa usalama (Penetration Test) ufanywe kwa kuangalia uimara wa mifumo dhidi ya wavamizi ambao hawajaidhinishwa kutumia taarifa za mifumo husika.

Hali hii inahitaji taasisi kufanya tathmini ya mara kwa mara ya tishio na udhaifu ili kugundua na kurekebisha mapungufu ya kiusalama kwenye Tehama na vifaa ili kuzuia ueneaji wa mashambulizi yoyote na matishio ya mara kwa mara kuhusu usalama wa Tehama.

Ukaguzi umebaini kwamba Uongozi wa Shirika la Umeme (ZECO) haukutayarisha miongozo kuhusiana na masuala ya kupima usalama wa mifumo ambapo hata Sera za sasa za Tehama za ZECO hazina vipengele vinavyosisitiza juu ya umuhimu wa kufanyika kwa upimaji wa usalama (Penetration Test) hali ambayo inatilia shaka ubora na uimara wa usalama wa mifumo ya Tehama ya Shirika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa shirika kuhakikisha kwamba Jaribio la upimaji wa usalama kwenye mifumo ya Tehma linafanywa mara kwa mara kwa

kuwatumia wataalama wa ndani na nje angalau mara mbili katika kila baada ya miaka miwili kama ilivyoelezwa katika viwango vya kimataifa na utendaji bora wa Tehama na ripoti za majaribio hayo zinapaswa kuandikwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kufanya tathmini ya ubora na uimara wa mifumo ya shirika.

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Kwa mwaka fedha 2020/2021 ni kweli Shirika la Umeme Zanzibar halikufanya majaribio ya kupima usalama wa mifumo (Penetration Test). Katika kutekeleza ushauri wa ukaguzi, Shirika kwa kushirikiana na Wakala Wa Serikali mtandao tayari imeanza kutekeleza agizo hilo katika mwaka wa fedha 2022/2023 na ripoti ya majaribio ya kiusalama (Penetration Test) na tayari imeshawasilishwa kwa Uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limekiri kutofanya majaribio ya kupima usalama (Penetration Test) hata hivyo Shirika tayari limeshaanza kuchukua hatua, hivyo Kamati inaendelea kulishauri Shirika kufanya majaribio ya mfumo kwa mujibu wa miongozo ya Tehama ili kubaini mapungufu na kuyafanyia maboresho ya haraka kabla hayajaleta athari itakayosababisha shirika kuingia katika hasara kubwa ya kukarabati mifumo hiyo pindi inapopata matishio ya ushambulizi au ueneaji wa virusi.

**15.2.1.6 Mapitio ya kanzidata ya mfumo (System Database).**

Utendaji bora unahitaji kwamba, kila baada ya miaka miwili hadi mitatu kanzidata (System Database) inapaswa kufanyiwa mapitio ili kubaki na taarifa (data) sahihi ambazo zitakuwa za kuaminika na zenye ubora kwa ajili ya kufanya maamuzi, pia vipengele vya ubora wa taarifa vinavyoamua ubora huhitaji uchunguzi wa sifa na vigezo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba shirika lilikuwa likiendelea kutumia taarifa (data) zisizo sahihi ambazo nyingi hazifai tena kuendelea kuwapo au zinahitaji maboresho ndani ya na kanzidata ya mfumo wa SAP (SAP system Database) tokea kuanzishwa mwaka 2014 ambapo wateja wote walipewa nambari za SAP, kabla ya wateja hao kuingizwa katika mfumo wa Suprima kwa kukosa nambari za akaunti za SAP.

Hali hii inaweza kupelekea watumiaji wa mifumo wa ZECO kutokuutumia mfumo na kutegemea kutengeneza Ripoti nje ya mfumo kwa kutumia 'Microsoft Excel' ambapo inaweza kupelekea thamani ya fedha iliyowekezwa kwenye mfumo kuweza kutokupatikana.

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Shirika la Umeme Zanzibar kwa kushirikiana na wataalamu wa mfumo wa SAP walifanya mafunzo pamoja na kufanya maboresho ya miongozo ya utendaji kazi wa mfumo.

Vile vile Shirika tayari linaendelea na marekebisho ya kanzidata ambapo tayari zoezi la kuhuisha taarifa za wateja limefanyika kwa ufanisi

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limekiri kuwepo kwa dosari hiyo katika mfumo wa SAP ila kwa sasa changamoto hiyo imeshachukuliwa hatua kwa kufanya marekebisho ya kanzidata katika mfumo wa SAP, Kamati inalisisitiza shirika katika kuendelea kufanya maboresho mbalimbali ya mifumo yake ili mifumo hiyo iweze kufanya kazi zake kwa usahihi na ufanisi wa hali ya juu.

### 15.2.1.7 Dosari zilizobainika katika mfumo wa ulipaji mishahara (Payroll)

Mfumo wa ulipaji, nyongeza na ukataji wa kodi kutoka kwenye mishahara uliotengenezwa kwa ajili ya shirika haukidhi mahitaji ya kimsingi kwa michakato ya malipo kama ifuatavyo:

- Mfumo wa malipo kuendela kuwatambua wafanyakazi ambao hawapo kazini wastaafu na walioachishwa kazi.
- Mfumo kukosa uwezo wa kuchakata taarifa katika ulipaji wa malipo na makato kama muda wa ziada.
- Mfumo hauna udhibiti (access control) ambapo imebainika watumiaji ambao hawajaidhinishwa wanaweza kufikia majedwali ya mishahara (payroll tables) ambayo huhifadhi taarifa (data) muhimu za malipo ambazo zinapaswa kufikiwa na wafanyikazi walioidhinishwa pekee.
- Mfumo hauwezi kujumuisha nambari za malipo na makato kwa madhumuni ya kutengeneza jarida la malipo (payroll journal).
- Kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu kati ya idara ya Utumishi na Idara ya Fedha katika usimamizi wa taarifa za wafanyakazi (creation and diactivation) na usimamizi wa mishahara.
- Kukosekana kwa ripoti ya udhibiti wa mfumo wa malipo inayoonyesha malipo na makato kwa muda.
- Kufanyika malipo kwa kutumia Ms excel na SAP ambapo tofauti ya taarifa za malipo kutoka kwa excel na SAP zinatilia shaka juu ya uhalisia wa ripoti za kifedha.

Kushindwa kutumia mfumo katika kushughulikia taarifa za wafanyaazi kunaweza kupelekea uwezekano wa wafanyakazi kupokea mshahara hata

baada ya kuondoka kwenye shirika jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vinavyoweza kuasabisha upotevu wa fedha.

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Shirika la Umeme Zanzibar kwa mwaka fedha 2020/2021 ni kweli mishahara ilikuwa inalipwa kwa kutumia excel hii ilitokana na mfumo wa SAP kutokuwa na moduli ya mshahara. Hata hivyo, kwa kuzingatia ushauri wa wakaguzi, Shirika kwa kushirikiana na wataalamu wa mfumo wa SAP tayari limefanya maboresho katika moduli ya mishahara (Payroll) ambapo machapisho yote ya Mshahara yanafanywa kwa kutumia mfumo wa SAP pamoja na ripoti zote zinazohitajika.

Vile vile Shirika limeweka utaratibu maalumu wa kuifikia moduli ya mishahara ambapo watendaji husika pekee ndo watakua na uwezo wa kuona moduli hiyo katika mfumo wa SAP.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limekiri kuwepo kwa dosari mbalimbali zilizobainika katika mfumo wa ulipaji mishahara (payroll) katika mfumo wa SAP ila kwa sasa changamoto hiyo imeshachukuliwa hatua na sasa shughuli zote zinazohusu ulipaji wa mishahara zinafanyika ndani ya mfumo wa SAP ambapo wahusika tu ndio wenye kuona moduli hiyo.

Kamati inalishauri Shirika katika kununua mifumo ambayo itakidhi mahitaji yote ya Shirika na kuifanyia majaribio kwa watumiaji kabla ya kukabidhiwa ili kubaini dosari za kiutendaji na kuweza kufanyiwa marekebesho kabla ya mfumo kukabidhiwa kwa wahusika.

#### 15.2.1.8 Dosari katika ripoti za mfumo wa SAP

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba ripoti zinazotayarishwa na mfumo wa SAP hazikuandaliwa na kubainishwa (customized) vya kutosha katika mfumo huo ambapo katika ripoti hizo kumekuwa na hali ya kukosekana kwa taarifa muhimu ambazo mfumo wa SAP unashindwa kuzitoa. Miongoni mwa taarifa muhimu zilizokosekana ni pamoja na taarifa za wadai, wadaiwa, ghala za vifaa ambapo uandaaji wa hesabu za mwaka bado zinafanywa kwa mfumo wa kawaida (Manual System) jambo ambalo hupelekea mchakato wa kuripoti kutengnenezwa kwa njia ya kawaida "mkono" ambapo kunaweza kunatumia muda mwingi na kusababisha taarifa kutokupatikana kwa urahisi na uhakika kwa wafanyakazi walioidhinishwa.

Aidha ukaguzi umebaini kwamba watumiaji wa mifumo wa shirika hawana mafunzo ya kutosha ya utendakazi wa ripoti za SAP na hivyo kushindwa kurekebisha au kufanya mabadiliko katika vipengele vya kuripoti ili kukidhi mahitaji yanayotakiwa. Kushindwa kwa mfumo wa SAP kutoa taarifa muhimu kulinganana na mahitaji ya Shirika, na kuandaa taarifa hizo za mwongozo, kutasababisha watumiaji wa mfumo huo kutokuwa na imani nao jambo linalosababisha kuwepo kwa mifumo miwili yaani mmoja usio wa kieletroniki (manual) na mfumo wa SAP kwa wakati mmoja.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZECO kuwasiliana na mtengenezaji wa mfumo wa SAP ili kurekebisha dosari zilizobainika na kuwezesha upatikanaji wa ripoti zote kwenye mfumo.

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 katika mfumo wa SAP kuligundulikana baadhi ya ripoti ambazo zilikuwa haziendani na mahitaji hali ya shirika la umeme. Kwa

kuzingatia hilo Shirika la umeme kwa kushirikiana na wataalamu wa SAP lilianza maboresho kupitia mradi maalumu uliofadhiliwa na wahisani ambapo hadi kufikia mwaka wa fedha 2023/2024 mradi huo upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wake ambapo imejumuisha matengenezo ya ripoti zinazohitajika katika mfumo wa SAP, mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba 2023.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamatibiti**

licha ya Shirika kukiri kuwepo kwa dosari hiyo hadi sasa hata hivyo Shirika la umeme ZECO limeshaanza kuchukua hatua za kuwasiliana na mtengenezaji wa mfumo kwa kurekebisha dosari hizo, Kamati inalishauri shirika kusimamia vyema marekebisho hayo ili yaweze kumalizika katika muda uliopangwa na hatimae mfumo uweze kufanya kazi zake zote kwa usahihi na ufanisi mkubwa.

**15.2.1.9 Dosari katika matengenezo na upatikanaji wa mikataba na changamoto za Tehama.**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba shirika lina utaratibu uliojiwekea wa utunzaji wa mikataba yote kupitia ofisi ya mwanasheria wa shirika.

Ukaguzi umebaini kukosekana kwa utaratibu mzuri wa kuhifadhi mikataba katika ofisi ya mwanasheria, vile vile ukaguzi umebaini kwamba mikataba hiyo inahifadhiwa kwa njia ya nakala ngumu (hard copy) pekee ambazo zimehifadhiwa katika ofisi ya mwanasheria tu hali iliopelekea kuwepo kwa changamoto katika kupata mikataba ya mifumo inapohitajika kwa nakala za kielektroniki.

Kutokuwepo au kutopatikana kwa mikataba ya Tehama inayohusiana na ununuzi na mikataba ya uwezeshaji wa mifumo kuwa salama (Service Level

Agreement) kunapelekea kutilia shaka uhalali wa makubaliano kati ya shirika na mtoa huduma jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya upotevu wa fedha na mikataba isiyo na tija

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Kwa muda mrefu mikataba ya TEHAMA ya Shirika la Umeme Zanzibar ilikuwa ikihifadhi kwa njia ya nakala ngumu kutokana na kutokuwepo na uhifadhi kwa njia ya nakala laini. Hata hivyo, kufuatia mahitaji ya uwekaji wa mikataba hiyo kwa njia ya nakala laini (softcopy), Shirika kupitia Idara ya Tehama tayari imeandaa mfumo unaotumika katika kuweka kumbukumbu za mikataba yote ya Shirika ambayo inasimamiwa na ofisi ya Mwanasheria.

Utaratibu wa Uwekaji wa taarifa hizo katika mfumo tajwa hapo juu tayari umeshafanyika.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kamati katika kupitia hoja hii imeomba kupatiwa mikataba ya mifumo ya "Aquilium" na "Supreme" hata hiyo Kamati imeshidwa kupatiwa mikataba hiyo.

Kamati inalishauri Shirika kuwa na utunzaji mzuri wa mikataba na inapohitajika kwa ukaguzi iweze kupatikana kwa urahisi

**15.2.1.10 Kukosekana kwa programu ya Ufuatiliaji wa lesseni zilizokwisha muda wake wa matumizi vifaa vya Tehama,program/software na mifumo ya Tehama.**

Usimamizi wa leseni ya programu ni sehemu ya usimamizi wa tathmini ya programu nani mchakato ambao lengo lake kuu ni kupunguza na kudhibiti gharama za Tehama kwa ujumla. Kwa urahisi ni mpango wa matengenezo wa

kudhibiti leseni zote za programu za shirika na kupunguza hatari na kuokoa matumizi ya Tehama kama ifuatavyo:-

• Kupata picha ya jumla ya programu zilizoidhinishwa kwa matumizi yaliyo sahihi na kubaini program zisizo na leseni.

• Kupunguza hatari za usimamizi wa leseni na kuendelea kufuatilia tarehe za mwisho wa leseni na kutoa taarifa mapema.

• Kuboresha ununuzi wa leseni kwa kuwa na mwonekano wa pamoja wa idadi ya leseni ambazo hazijatumika na ambazo hazitumiki sana.

• Kutambua ukiukaji wa leseni kwa njia ya kielektroniki (automatic) kwa kuratibu ukaguzi wa mara kwa mara wa vituo vya kazi na kupitia ukaguzi kwa urahisi.

Katika ukaguzi wa Tehama na uhalali wa leseni ya mfumo wa uendeshaji na programu, ukaguzi umebaini shirika lina zaidi ya kompyuta 250 na seva nane kwa mfano, Seva sita ziko katika ofi si ya makao makuu na seva mbili ziko ofi sini Pemba. Hata hivyo, imebainika kuwa baadhi ya kompyuta zilikuwa zikifanya kazi bila leseni sahihi au za kisheria kutoka kwa Microsoft Corporation pia seva za HP ProLiant 380 G8 5 ambazo zinatumiwa na shirika kwa mfano Seva 2 ambazo ziko Pemba ni kwa ajili ya Aquillium na bakup na seva 2 za kuhudumia mfumo wa Aquillium na Antivirus zilizopo Makao Makuu na seva 1 ya Aquillium iliyopo kwenye kituo cha kuhifadhi nakala za (backup) zimeisha rasmi muda wake tangu tarehe 30/06/2021 na hazijapata tena updates/viendeshi, usasishaji na uboreshaji tangu tarehe ilipotangazwa na hakukuwa na programu ya ufuatiliaji wa programu ili kutambua na kutahadharisha hali ya Shirika ya Leseni zilizopo kwa ajili ya kupanga kuepuka leseni zinazoisha muda wake na kuepuka faini mbalimbali kutoka kwa

Microsoft Corporation na mtandao wa ushirika kwa matumizi yasiyo salama ya programu na hardware zilizoisha muda wake. .

Mbinu bora inasema kwamba kufuatilia orodha ya programu, matoleo, na uwekaji halisi unaweza kutekelezwa na Taasisi za Umma ili kudhibiti programu/vifaa vilivyo na leseni na pia itafanya ukaguzi wa programu kwenye kompyuta ya mezani,seva na Local Area Network (LAN).

Ufuatiliaji wa utoaji leseni na utiifu wa programu huhakikisha kwamba michakato ya usimamizi wa programu inafanya kazi kwa ufanisi na kwamba programu zisizo na leseni halali hazitumiki.

Kuendelea kutumika kwa programu zisozokuwa na leseni ya matumizi ya Shirika kunaweza kujitokeza kwa athari zifuatazo:-

• Kuathiri usalama wa mtandao wa shirika.

• Kutokupatikana kwa usaidizi wa kiufundi na matumizi yake yanayoweza kusababisha upotevu wa tija ndani ya mtandao wa shirika

• Inaweza kuharibu taswira na sifa ya kitaaluma ya shirika.

Ili kuhakikisha kuwa shirika linatumia programu halisi na yenye leseni, ukaguzi unapendekeza yafuatayo:-

• Shirika kununua programu ya usimamizi wa Leseni inayoweza kufanya vipengele vyote vya mchakato wa ufuatiliaji, taarifa na ununuzi wa leseni kiotomatiki na kufuatilia leseni zote za programu za shirika kwa kuhalalisha, kuainisha na kutambua kiotomatiki aina za leseni, kufuatilia matumizi ya leseni ya programu na kudhibiti orodha ya leseni ya mifumo mbalimbali .

• Idara ya Tehama, kupitia program yenye leseni ilizohifadhiwa katika kitengo cha Tehama kuthibitisha/kutathmini programu inayotumiwa ili kuhakikisha kwamba programu ni ya kweli na ina hitaji la leseni inayolingana.

• Kuimarisha usimamizi kuhakikisha kuwa programu inatumika kwa mujibu wa masharti ya makubaliano ya leseni husika.

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Shirika la Umeme Zanzibar kupitia Idara ya TEHAMA tayari imeweka mfumo maalumu ambao unafuatilia programu zote zilizosakinishwa katika kifaa husika.

Vile vile Shirika tayari limeandaa mpango wa kubadilisha vifaa vyote ambavyo muda wake wa matumizi umeshapita, miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na seva ambazo kupitia bajeti ya mwaka 2021/2022 Shirika la Umeme liliweza kufanya Manunuzi ya Seva mpya tatu ambazo tayari zimeshatumika kuzibadilisha za zamani ambazo zilikua zinatumika katika kuendesha mifumo ya Shirika la Umeme.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

**Kamati imebaini** Shirika la Umeme ZECO halikuwa na mfumo utakaofatilia program zote zilizosanikishwa katika kifaa husika ili kubaini leseni zilizokwisha muda na kuweza kuziboresha (update) ila kwa sasa mfumo huo umeshawekwa na umeshaanza kutumika.

Kamati inalishauri Shirika kufuata sera na miongozo mbalimbali ya Tehama kwa kuendelea kununua mifumo ya ufuatiliaji ya Tehama ambayo itasaidia kulinda kusaidia usalama wa mfumo dhidi ya wahalifu na mashambulizi ya kimtandao.

### 15.2.1.11 Matumizi zilizokwisha muda wake ya programu.

Katika ukaguzi ulifanyika imebainika kwamba Shirika la Umeme (ZECO) linatumia vifaa ambavyo vimeisha muda wake wa matumizi na havipati msaada wa kinga toka kwa watengenezaji wake kama vile HP ProLiant DL350 G8 kupangisha programu muhimu ikiwa ni pamoja na mfumo mkuu wa biashara yaani Aquillium na seva ya backup ya mfumo huo wa Aquillium. Seva ya HP ProLiant DL350 ilifi kia mwisho wa mtumizi mnamo Novemba 30, 2014. Mwisho wa matumizi ya huduma ya seva aina ya IBM System x3650 M4 ambayo ina program ya Anti virus ni tarehe 31 Desemba 2021. Biashara zinazotegemea miundo mbinu ya zamani zinaweza kuishia kutofaulu katika usanifu wa mfumo wao, na pia huweka afya na usalama wa vifaa vyote vilivyounganishwa katika hatari kubwa. Utaratibu huu katika mitandao ya biashara unaweza kuathiri tija na uwezo wa shirika kuhudumia wateja wake wa ndani na nje.

Aidha ukaguzi umebaini kuwa shirika linatumia Mfumo wa Uendeshaji wa seva ya Windows 2003 ambao haukuwa na msaada tena,kutokana na wamiliki wa programu hiyo (Microsoft) kutangaza rasmi Julai 14, 2015 kusitisha kutoa msaada wa aina yoyote kwa programu hio.

Kuendelea kutumia Window Server 2003 kunaweza kupelekea athari kushambuliwa na virusi na kuharibiwa kwa mfumo wa EQULLIUM ulioingizwa ndani ya kompyuta hiyo ya zamani kutokana na kukosekana kwa udhibiti, ulinzi na usalama katika seva hiyo pamoja na kukosa msaada wa maboresho kutoka kwa wamiliki waliotendeneza program hiyo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZECO kuhakikisha unapata toleo jipya la mfumo wa uendeshaji unaotumika ambapo kwa sasa mfumo mpya wa uendeshaji wa kompyuta uliopo sokoni ni Windows Server 2019.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa ZECO kusitisha matumizi ya mfumo wa zamani na kuimarisha ikiwa huduma zinazoendeshwa kwenye mfumo wa Windows Server 2003 hazihitajiki tena, au zinaweza kuunganishwa kwenye seva zingine, ukaguzi unashauri kuondoa seva kutoka katika mtandao wa shirika (network) inayohatarisha na kukaribisha mashambulizi toka kwa wizi wa mtandao (Cyber-Attackers).

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Kwa mwaka fedha 2020/2021 Shirika la Umeme Zanzibar lililazimika kuendelea kutumia seva DL350 G8 kwa ajili ya program ambayo sifa zake zinaendana kwa mujibu wa mfumo uliopo. Aidha, Shirika likifanya jitihada zake za kutafuta suluhisho la matumizi ya programu husika kwa kufanya manunuzi ya seva ambazo zilihitajika kufanyiwa mabadiliko baada ya kumaliza muda wake wa matumizi. Kwa sasa Jumla ya Seva tatu tayari zimenunuliwa katika kufanya maboresho ya mifumo inayotumika ambapo kati ya hizo seva DL350 G8 tayari imeshabadilishwa kwa kuweka seva mpya.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Shirika la Umeme ZECO limekiri kuwepo kwa dosari hiyo hata hivyo Shirika limeshaanza kuchukua jitihada za kuanza kununua vifaa hivyo, Kamati katika kufuatilia hoja hiyo imeomba kupatiwa vielelezo vinavyothibitisha manunuzi ya vifaa hivyo vya Tehama kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na ufanisi katika mifumo wanayoitumia na nyaraka hizo zimeletwa mbele ya Kamati

Kamati inaliomba Shirika katika kuendelea kununua vifaa vya kisasa vya Tehama na program mbali mbali zinazokwenda na wakati ili kuwa na usalama wa taarifa mbalimbali ambazo zinahifadhiwa ndani ya mfumo kwani taarifa hizo zikipotea au kuvuja kwa wahalifu wa mitandao zinaweza kulisababishia Afisi hasara kubwa hadi kuweza kutatua changamoto hizo.

**15.2.1.12 Kukosekana nyaraka muhimu za makabidhiano ya mifumo.**

Uhamisho wa mfumo wa programu kutoka kwa mtaalam anayehusika na uundaji wake hadi kwa mnunuzi anayehusika na matengenezo yake hurejelewa kama makabidhiano ya mfumo wa programu au mpito. Kukabidhi ni mchakato muhimu katika mzunguko wa maisha wa programu na ni muhimu kwamba ufanyike kwa urahisi iwezekanavyo.

Lengo la makabidhiano ni mawasiliano sahihi ya kuaminika ya taarifa zinazohusiana na kazi iliyofanywa na mtengenezaji kwa mujibu wa makubaliano na mtumiaji au watumiaji wa mfumo na hivyo kuhakikisha uendelevu wa kufanya kazi kwa usalama na kwa ufanisi.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Umeme halina nyaraka muhimu zinazoonesha kuwepo kwa makabidhiano ya mifumo yao yote kutoka kwa watengenezaji mifumo ili kuthibitisha kuwa wamekabidhiana mfumo kwa kuzingatia masharti ya mikataba na kwamba mifumo hio inamilikiwa wa shirika.

Hali hii inapelekea shirika kutokuwa na umiliki halali kisheria kwa mifumo iliyopo kutokana na kukosa nyaraka za umiliki. Katika siku zijazo, uongozi unapaswa kuhakikisha kuwa:-

• Mfumo wa kukabidhi vyeti upo kama ushahidi wa umiliki. Makabidhiano ya mfumo ni wakati muhimu wa kuhakikisha mwendelezo wa utunzaji na usalama

wa shirika na kwamba ripoti inayotolewa wakati mtaalamu muuzaji wa mfumo anahamisha jukumu la mfumo kwa shirika na kuanishwa ni muhimu.
• Hati lazima ziandikwe kwa watumiaji wa mwisho (system user). Huenda ikahitaji seti tofauti za hati kwa watumiaji tofauti lakini ili uwekaji wa hati kusaidia uhamishaji wa maarifa unahitaji kuwa wa maana, utumike na unaofaa kwa watumiaji wa mwisho.

• Watumiaji (uongozi) kukubaliana na Watengenezaji au wauza mifumo, na kuhakikisha kwamba wahusika wote wana uwasilishaji ulio wazi, na kujua kile kinachotarajiwa kutoka kwao na kujitahidi kufi kia lengo tangu mwanzo wa mradi

**Majibu ya Shirika la Umeme ZECO**

Kwa mwaka fedha 2020/2021 Shirika la Umeme Zanzibar lililazimika kuendelea kutumia seva DL350 G8 kwa ajili ya program ambayo sifa zake zinaendana kwa mujibu wa mfumo uliopo. Aidha, Shirika likifanya jitihada zake za kutafuta suluhisho la matumizi ya programu husika kwa kufanya manunuzi ya seva ambazo zilihitajika kufanyiwa mabadiliko baada ya kumaliza muda wake wa matumizi. Kwa sasa Jumla ya Seva tatu tayari zimenunuliwa katika kufanya maboresho ya mifumo inayotumika ambapo kati ya hizo seva DL350 G8 tayari imeshabadilishwa kwa kuweka seva mpya.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Uongozi wa Shirika umekiri kutokuwa na umilikiwa mifumo yake yote ya Tehama ila kwasasa wameshaanza kuchukua hatua kwa kuanza kuzingatia suala hilo katika mfumo mpya wa Hexing ambao upo katika hatua ya majaribio.

Hata hivyo Kamati inalishauri shirika kuchukua hatua zaidi za kufatilia nyaraka za makabidhiano ya mifumo yote inayotumiwa na Shirika ili kupata umiliki

halali wa mifumo kwa vile ukosefu wa nyaraka za makadhiano na kukosa umiliki wa mfumo Shirika huenda likashidwa kufanya seti mbalimbali pindipo ikihitaji kufanya hizo aidha taarifa muhimu za kiusalama za shirika zitaendelea kuwepo kwa mmiliki wa mfumo jambo ambalo ni hatarishi kwa maslahi ya Shirika.

.

## 17.0 SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR

### 17.2.1.1 Dosari katika Mkataba wa matengenezo ya mfumo wa CIMIS shilingi 1,962,857,200

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) liliingia mkataba tarehe 13 Aprili 2019 wenye thamani ya jumla ya shilingi 1,546,980,000 na kampuni ya IMATIC Technology Company Ltd (ITL) iliyopo Dar es Salaam kwa ajili ya kutengenezewa Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa huduma za Bima "Core Insurance Management Information System (CIMIS)".

Aidha katika kutafuta njia za kuweza kufanikisha mchakato huo Shirika la Bima Zanzibar liliingia mkataba na kampuni nyengine inayojuulikana kwa jina la BITZ iliyopo Zanzibar wenye thamani ya shilingi 104,000,000 kwa ajili ya kuwa Mshauri Elekezi (Consultant) kwa upande wa Shirika ili kuweza kulisaidia Shirika katika kufanikisha mchakato huo wa utengenezwaji wa mfumo wa CIMIS ambapo kampuni ya BITZ ilikuwa inakusanya mahitaji kutoka katika Shirika na kuyawasilisha kwa Kampuni ya ITL inayotengeneza Mfumo kwa mujibu wa utaratibu waliokubaliana katika mkataba.

Hata hivyo katika ukaguzi uliofanyika dosari mbali mbali zimebainika katika utekelezaji wa mchakato huo wa utengenezwaji wa Mfumo wa CIMIS ambapo baadhi ya dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa awali baina ya Shirika na kampuni ya IMATIC (ITL), kampuni ilikubali kufanya kazi ya kutengeneza, kujaribu hadi kukamilisha na kuufunga mfumo wa CIMIS kwa ajili ya matumizi kwa kipindi cha muda wa miezi 24 kuanzia tarehe 13 April 2019 hadi to tarehe 13 April 2021. Ukaguzi ulibaini kwamba kampuni ilishindwa kutimiza masharti ya mkataba na kupitisha mda waliokubalina na kulazimika kuomba mda wa

ziada ambapo Shirika lilikubaliana na maombi hayo na kuongeza mda wa miezi 8 hadi tarehe 31 disemba 2021 ili kukamilisha kazi hiyo kwa ufanisi. Aidha, pamoja na nyongeza hiyo ya muda Kampuni haikukamilisha kazi kwa ufanisi jambo lililopelekea ZIC kuendelea kuutumia mfumo huo kinyume na matarajio yaliowekwa.

• Kuongezeka kwa gharama kutokana na kufanyika mikataba ya ziada yenye jumla ya shilingi 213,127,200 sawa na asilimia 13.78 ya ongezeko kutoka mkataba wa awali wenye jumla ya shilingi 1,546,980,000 na kupelekea jumla ya fedha zilizolipwa kwa Kampuni ya ITL kuongezeka na kufi kia shilingi 1,760,107,200 ambapo gharama hizo zilitokana na kampuni ya ITL kupitiliza mda wa kukamilisha kazi ya kutengeneza mfumo wa CIMIS.

• Kuongezeka kwa gharama za mshauri elekezi kwa thamani ya shilingi 98,750,000 kutoka mkataba wa awali wenye jumla ya shilingi 104,000,000 na kupelekea jumla ya fedha alizolipwa mshauri elekezi kufi kia shilingi 202,750,000 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 95.0. Kuwepo kwa ongezeko hilo bila ya kupata idhini kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa 280 Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya Tehama kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021 OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR Serikali kumejitokeza ukiukwaji wa Sheria ya Ununuzi ambapo kifungu nambari 49(4-5) cha kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba “ Iwapo malipo yatazidi bei ya mkataba kwa zaidi ya asilimia 15 yawasilishwe kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho au Baraza la Wawakilishi (Approval).”

Hadi ukaguzi unakamilika jumla ya gharama ziliozobainika kutumika katika utengenezaji wa mfumo mpya wa CIMIS ni shilingi 213,127,200 ambazo zimelipwa kwa Mshauri Elekezi (BITZ) na shilingi 1,760,107,200 zimelipwa kwa

Mtengenezaji Mfumo (System Vendor – ITL) na kupelekea jumla ya fedha zote zilizotumika kwa malipo ya Mfumo wa CIMIS ni shilingi 1,962,857,200.

**Majibu ya Shirika la Bima Zanzibar**

Uongozi unakubaliana na hoja ya mkaguzi juu ya kuongezeka Kwa muda wa mkataba, lakini ongezeko hili lilisababishwa na hali tofauti ambazo zilikuwa juu ya uwezo wa Shirika. Kwa mfano:- i. Mripuko wa maradhi ya uviko -19 ni sababu kubwa iliyopelekea kuongezeka Kwa muda wa mkataba, kwani kazi nyingi zilipelekea kusimama ili kukwepa uambukizwaji wa maradhi. ii. Hata hivyo, pia tulipokea agizo kwa barua kutoka Serika Kuu juu ya kusitisha michanganyiko na muingiliano wa watu jambo ambalo lilipelekea kubadilika kwa utaratibu mzima wa ufanyaji kazi, hatimae mambo mingi yalisimama utendaji wake. iii. Kuongezeka Kwa wigo wa mfumo, wakati tunaingia kwenye makataba wa kutengeneza mfumo huu wa CIMIS, kuna mambo mengi hayakuwepo hata kwenye sheria wala kwenye soko. Kwa mfano, Ukataji wa Bima kupitia Mabenki (Bancassurance). Huduma hii ilianza wakati Mkandarasi anaendelea kutengeneza mfumo, Hivyo ikapelekea wigo na majukumu ya mkandarasi kuongezeka Pamoja na Mshauri elekezi kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuingiza mahitaji ya Bancassurance kwenye mfumo wa CIMIS. Kadhalika wigo uliendelea kutanuka kwa kutokea hitaji la kutengeneza moduli ya Payroll. Ongezeko la mahitaji hayo tajwa lilipelekea Shirika kuingia Mkataba wa ziada (Addendum), kwenye mkataba huu wa nyongeza ulippelekea kuongezeka kwa Gharama za Mkandarasi Pamoja na Mshauri elekezi. Gharama za mshauri elekezi zilikua juu ya kiwango kinachokubalika kwa mikataba ya nyongeza kwa sababu Mshauri elekezi tulikubaliana nae kufanya kazi kwa kuzingatia muda, na kwa mujibu wa makubaliano yetu hatukua na namna ya kurudi kwenye mchakato wa kutangaza tenda kwa sababu tulikua tayari tupo

nje ya muda. Soko lilituhitaji tuwe na mfumo ili tuweze kuendesha biashara kwa ufanisi. iv. Pia wigo uliendelea kutanuka kwa kuzingatia matakwa ya TIRA baada ya kubadilisha mfumo wao na kuyataka Mashirika yote ya bima kuunganishwa kwenye mfumo wake wa TIRAMIS. v. Lakini pia, tulipokea agizo la Serikali kuu juu ya kuunganisha mfumo wetu na mfumo wa ZRA na TRA (VFMS). Sababu zote hizo zilijitokeza baada ya Shirika kuingia mkataba na mtengenezaji mfumo na mshauri elekezi, jambo lililopelekea si tu kuongeza muda na wigo wa kazi lakini pia kuongezeka kwa gharama za utengenezaji mfumo

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kutokufanyika kwa uchunguzi wa kina juu ya mlinganisho wa uwiano baina ya gharama na faida (Cost and benefit analysis) wa mfumo wa CIMIS, uchunguzi huu ungeweza kusaidia katika kufanya maamuzi sahihi ya kutumia mfumo wa CIMIS au kutafuta mfumo mwengine wenye kukidhi shughuli zote za Shirika la Bima kufanyika ndani ya mfumo kwa kutumia gharama ndogo tu katika ununuzi pamoja na gharama za kuuhudumia mfumo huo.

Kwani Kamati imebaini kuwa mfumo huo umetumia gharama kubwa inayotokana mkandarasi kutomaliza kazi kwa wakati na ongezeko la kazi za ziada ambazo hazikuwemo katika mkataba wa awali hata hivyo bado mfumo huo haujaweza kufanya kazi kwa ufanisi kulingana na shughuli zinazofanywa na Shirika.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inazishauri taasisi za Serikali kabla ya kuanza kununua mifumo ni vyema kuandaa andiko la mradi la mfumo kwa kujumuisha mahitaji yote muhimu

yanayohitaji kuwemo ndani ya mfumo na kuwasilisha andiko hilo katika ofisi za Serikali Mtandao E- Government kwa ajili ya kupatiwa msaada wa kitaaluma na miongozo mengine ili kujiepusha katika kununua mifumo isiyokuwa na tija na wakati mwengine gharama kuongezeka kutokana na kuongeza mahitaji ambayo hayakuwepo katika mkataba wa awali.

Aidha Kamati inazielekeza taasisi za Serikali kufuata sheria katika kazi za nyongeza "addendum" kwa zaidi ya asilimia 15 bila ya kupata idhini kwa mlipaji mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho au Baraza la Wawakilishi, kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 49(4-5) cha kanuni ya Ununuzi na uodoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2021.

**17.2.1.2 Kutokufikia malengo ya matumizi ya mfumo wa CIMIS**

Shirika la Bima Zanzibar liligharamika kutengenezesha mfumo wa CIMIS kwa ajili ya kufanya kazi za usimamizi wa Huduma za biashara za Bima pamoja na kufanya shughuli nyengine za uendeshaji wa Shirika kama vile shughuli za kusimamia ununuzi, masuala ya mishahara, Uekezaji, bajeti, kutunza taarifa za mali za ofisi, Malipo Janja "Smart Pay", Sera Janja "Smart Policy", n.k. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba CIMIS haikuweza kufi kia malengo yaliotarajiwa na shirika kutokana kuwepo kwa dosari mbalimbali zilizojitokeza kama inavyoonkana katika jadweli lituatalo:-

**Jadweli Nambari 45: Malengo ya mfumo wa CIMIS ambayo hayakuweza kufikiwa**

| Lengo Namba | Lengo lililotarajiwa | Matokeo baada ya kutengenezwa na kutumika mfumo wa CIMIS | Majibu ya Uongozi |
|---|---|---|---|
| **1** | Kuimarisha | Halikufanikiwa kutekelezwa | udhibiti na uwajibikaji ni |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | udhibiti wa usimamizi na kuboresha uwajibikaji kwa kufanya maamuzi katika shirika juu ya masuala yanayohusiana na bima, shughuli za fedha na uwekezaji. | kutokana na CIMIS hutoa ripoti tofauti ambazo na uhalisia na hivyo haziwezi kutegemewa kwa uamuzi juu ya masuala ya fedha, bima na uwekezaji pia na kwa watumiaji wengine wa ripoti hizo. | matokeo ya michakato ya kiusalama kwenye mifumo. Uzalishaji wa ripoti ni matokeo ya taarifa zilizoandikwa kwenye mfumo. Kwa hivyo muda huo wa ukaguzi bado tulikuwa tunapata mafunzo ya kina kwa ajili kuboresha uwezo wa watumiaji. Lakini kwa sasa mfumo wetu umeboreka kwenye udhibiti na uwajibikaji. Na taarifa zinazofanyiwa maamuzi ndani ya Shirika zote zinatoka au zinatengenezwa ndani ya mfumo wetu wa CIMIS |
| **2** | Kuliwezesha Shirika kufunga akaunti za hesabu za kifedha 31 Januari kila mwaka. | Lengo halikufi kiwa kutokana na Mfumo kutoa taarifa zisizo sahihi (key input) ambazo ni muhimu kwa ajili ya maandalizi ya taarifa za kifedha hali iliopelekea baadhi ya ripoti kuandaliwa na kufanyiwa mlingano(reconciliation)kwa njia ya kawaida (manual) mikono na taarifa yengine zilikosekana kabisa kwenye mfumo kwa mfano; taarifa | Maandalizi ya taarifa ya fedha inategemea kukamilika kwa mchakato wa biashara wa kipindi hicho malum. Kwa kipindi hicho ukaguzi nikweli mfumo wetu ulikuwa haujaanza kuchakata taarifa zilizokuwa sahihi kutokana na kuwa taarifa nyingi za zamani zilikuwa hazijaingizwa kwenyewe mfumo na pia watumiaji |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | za kibenki (Banc Assurance) pamoja na shughuli za mawakala (brokers transaction | walikuwa hawajakuwa na utaalamu wakutosha. Lakini kwa sasa matizo mengi yameshaondoka na taarifa zote zinatumika kufungiwa hesabu zinachukuliwa kwenye mfumo huu wa CIMIS. |
| **3** | Kuboresha mchakato wa ufuatiliaji wa madai kwa kujumuisha sera ya bima na moduli za reinsurence ili kumpa mtumiaji uthibitisho wa muda wa malipo kulingana na tarehe iliyoripotiwa madai au tokeo. | Ripoti za "Reinsurance" hutolewa na moduli ya smart policy kupitia "Smart ERP" ambayo hutoka taarifa zisizo sahihi hali ambayo hupelekea ripoti za "reinsurance" zinazozalishwa na CIMIS (ERP) kutokuwa za kutegemewa | Repoti za "Reinsurance" zinatengenezwa na taarifa zilizoandikishwa kwenye " smartpolicy" kusawazishwa (business reconsiliation) ili ziweze kusukumwa kwenda ERP. Ni miamala iliyosawazishwa pekee ndiyo inayosukumwa hadi kwenye Smart ERP kutoka kwa Smartpolicy. Hivyo, ikitokea kuna bima za reinsurance zimeandikishwa na hasijasawazishwa, bila ya shaka hizo hazitatumwa kwenye ERP na hatimae hazitaonekana kwenye ERP na kutengeneza tofauti baina ya ERP na Smart Policy |
| **4** | Kupangilia mikataba ya bima ya ZIC na | Mikataba na ripoti za uwezeshaji zinazotolewa na moduli ya "Smart Policy" | Mpangilio wa Mikataba ya bima (reinsurance treaties) na "fucultative" pekee |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | mipangilio ya uwezeshaji pamoja na kuunganisha kielektroniki mchakato wa "reinsurance" katika usimamizi wa sera na utaratibu mzima wa madai. | kupitia smart ERP hutoa taarifa zisizo sahihi na kupelekea taarifa za "reinsurance" zinazozalishwa na CIMIS (ERP) kutokutegemewa kwa maamuzi | inaweza kuelezewa katika mfumo wa CIMIS. Mikataba ya reinsurance na "faultative" ambayo imeshagawiwa(allocated) ndiyo inayounganishwa moja kwa moja (automatically. Kama haikufanyika hivyo reinsurance ripoti hazitakuwa sawa. Kwa hali ya sasa, waandikishaji wa bima mtawanyo(reinsurance) wanauweledi wa kutosha katika kuandikisha bima hizo ndani ya mfumo wa CIMIS na yale makosa ya zamani hayategemewi kujitokeza tena |

Kushindwa kutekelezeka ipasavyo kwa malengo hayo malengo ya kiufundi kunapelekea mfumo wa CIMIS kutokuwa na manufaa kwa kutokufi kia lengo lililokusudiwa na hivyo kuliingiza Shirika hasara ya upotevu wa fedha kwa kutokuwepo kwa uwiano wa faida na gharama ya fedha ambayo imetumika kutengenezea mfumo huo.

**Uchunguzi wa Kamati**

Licha ya Shirika kufanya maboresho ya dosari mbalimbali za kiutendaji wa mfumo ambazo zimeelezwa na mdhibiti hata hivyo Kamati imebaini Mkataba wa awali haukuweza kutoa mafaniko yanayotorajiwa kwa upande wa Shirika

licha ya kutoa jumla ya Tsh 1,650,980,000 kwa mkandarasi na Mshauri elekezi, kwa vile Mkataba wa awali wa Mfumo haukuweza kukidhi haja ya matumizi ya shughuli za Bima hivyo, shirika liliamua kuongeza Mkataba ambao umefanya mfumo huo kutumia jumla ya Tsh 1,962,857,200 ambazo hazina uwiano baina ya gharama na utendaji kazi wa mfumo huo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Shirika la Bima Zanzibar kwa Kushirikiana na mshauri elekezi na Mkandarasi kuendelea kuzitatua changamoto zilizobaki za mfumo ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kuleta tija kwa vile gharama kubwa imetumika katika kununua mfumo huo. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza juu Tasisi za Serikali katika kufanya uwiano faida na gharama za mfumo kabla ya kununua kwa lengo la kuepuka kuingiza Serikali hasarani kwa kununua mifumo isiyoweza kukamilisha ufanyaji kazi wa program za taasisi husika.

**17.2.1.3 Mfumo wa CIMIS kuanza kutumika "GO-LIVE" kabla ya kufanyiwa Majaribio ya kutosha kwa moduli zake.**

Kwa mujibu wa taratibu zilizobora (best practices) pamoja na muongozo kutoka Wakala wa Serikali Mtandao wenye Hati namba eGA/EXT/APA/005 toleo nambari 1.0 la Novemba 2018 kifungu cha 2.1.6 unaohusiana na kufanya majaribio ya mfumo "System Testing" kabla ya kuanza kutumika unaeleza kwamba majaribio ya mifumo yanapaswa kufanyika kulingana na mahitaji yaliyoainishwa na watumiaji wa mfumo. Hii ina maana ya kwamba katika kila kipengele cha mfumo (moduli) ni lazima kifanyiwe majaribio ya kutosha na kujiridhisha kabla ya kuanza kutumika ili kuweza kubaini usahihi wa utendaji kazi wa mfumo kama ilivyotarajiwa kutokana na mahitaji ya watumiaji wa mfumo. Aidha matokeo ya majaribio hayo ni lazima yawekwe katika kumbu

kumbu na kutolewa mapendekezo utayari wa mfumo kutokana na matokeo hayo.

Baadhi ya majaribio ambayo hufanyika katika utendaji kazi wa mfumo kwa mujibu wa mahitaji ya watumiaji wa mfumo ni kama vile Jaribio la application, Jaribio la utendaji kazi (performance test) , Jaribio la usalama (security test) , Jaribio la kukubalika kwa mfumo (User acceptance test) n.k.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Bima Zanzibar halijafanya majaribio ya kutosha katika kila kipengele cha mfumo wake wa CIMIS kuhusiana na utendaji wake wa kazi. Hali hii imebainika kutokana na kukosekana kwa nyaraka muhimu inayoonesha kuwa mfumo umejaribiwa na kukubalika kwa watumiaji wote (User Acceptance Test Document) na kwamba uko tayari kwa matumizi kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba kama ilivyoelezwa katika kifungu nambari 23 na 24 cha Mkataba huo. Aidha, nyaraka hiyo huthibitishwa rasmi na uongozi wa Shirika.

Kutokufanyika kwa majaribio ya kutosha na kujiridhisha katika uanzishaji au uboreshaji wa mfumo kunaweza kupelekea mfumo kuzalisha taarifa (ripoti) zisizokuwa sahihi. Vile vile mfumo unaweza kusababisha kutokezea mabadiliko kadhaa baadae na kupelekea Shirika kuingia hasara ya kulipia gharama zisizotarajiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kuhakikisha kuwa mfumo mpya unafanyiwa majaribio ya kutosha kuhusu utendaji wake kwa kila kipengele (moduli) ili kuweza kubaini kama unafanya kazi kama ilivyokusudiwa na kutoa matokeo bora.

**Majibu ya Shirika la Bima Zanzibar**

Kabla ya kuanza kutumika Kwa mfumo wa CIMIS watumiaji walipatiwa mafunzo, mafunzo hayo yalitolewa Kwa makundi na Kwa awamu tofauti na kumbukumbu ziliwasilishwa Kwa wakaguzi wakati wa ukaguzi huu.

Ni kweli hatukuweka kumbukumbu za kesi za majaribio "test case document" lakini kumbukumbu za mahudhurio zilikuwepo katika nyakati zote za mafunzo hayo, nazo ziliwasilishwa Kwa wakaguzi. Hata hivyo, kadiri siku zilivoongezeka tumeboresha uhifadhi wa kumbukumbu zote za majiribio kila tunapoongeza kitu kipya katika mfumo.

Tunakuwa na kesi maalumu za majaribio (test cases document) ambayo majaribio yote yanafanyika kwenye sava ya majaribio (test server) Kwa mujibu wa kesi hizo, na baada ya kumalizika Kwa majiribio hayo walioshiriki wote wanasaini na kuhifadhiwa. Kwa majaribio yanayofanyika Kwa njia ya mtandao, tunatumia "teams".

Huu ni mfumo maalumu Kwa ajili ya mikutano inayofanyika Kwa njia ya mtandao. Mfumo huu unahifadhi taarifa za watu wote waliohudhuria na kurikodi mkutano wote, hivyo ikitokea mtumiaji kuna sehemu hajafahamu anaweza kuridi kwenye mfumo huu wa teams Kwa ajili ya kusikiliza tena

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Licha ya Shirika kukiri kutokuwa "Test case document" Kamati inashauri Shirika la Bima kutunza kumbukumbu hizo kwa vile ndio msingi wa uthibitisho wa ufanisi wa mfumo katika kufanya kazi kwa mujibu mahitaji yaliyokusudiwa, hivyo kuwepo kwa nyaraka hizo zitawezesha kumbana mtengenezaji wa mfumo kurekebisha dosari hizo kabla kukabidhi kazi kwa Shirika.

Vile vile kuendelea kuwepo dosari za kimfumo kutapelekea watumiaji kukosa imani ya kutumia mfumo huo na kuamua kurudi katika utaratibu wa zamani wa kufanya kazi zao nje ya mfumo hali itakayopelekea mfumo kukosa tija iliyokusudiwa.

**17.2.1.4 Kukosekana kwa mazingira mazuri ya kufanyia majaribio ya Mifumo (Poor Test Environment)**. Utaratibu uliobora unaeleza kwamba, Taasisi inatakiwa kuandaa mazingira mazuri ya TEHAMA “Reliable Test Environment ” kwa ajili ya kufanya majaaribio ya utendaji kazi wa mifumo kabla ya kuanza kutumika katika mazingira halisi ya kazi “Go - Live”.

Mazingira mazuri ya kufanya majaribio ni pamoja na kuwepo kwa kompyuta zilizo salama na zenye uwezo mkubwa wa kufanya kazi (Test servers), miundombinu ya mtandao iliyo imara itakayoweza kusaidia zoezi la majaribio kufanyika kwa weledi na ufanisi na vile vile kushirikishwa kwa ngazi tofauti za watumiaji wa mfumo ili kuweza kuthibitisha matokeo kulingana na mahitaji yao ya kazi na hatimae kuandikwa nyaraka za kukubali mfumo (User Acceptance Report / Installation Certifi cates etc).

Katika ukaguzi uliofanyika wa mapitio ya mazingira ya majaribio “ Test Environment ” imebainika kuwa Shirika la Bima Zanzibar limeweka kompyuta ya kawaida yenye uwezo mdogo kwa ajili ya kufanya majaribio ya mifumo yake licha ya kwamba Shirika lina mifumo muhimu ambayo inatumika katika kuweka taarifa mbali mbali za biashara na Bima kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Aidha ukaguzi ulibaini kwamba mfumo Mkuu wa Kusimamia Masuala ya Bima (CIMIS) kabla ya kuanza kazi ulijaribiwa kupitia kompyuta maalum (Test Server) pamoja na miundombinu kutoka kwa Mtengezaji wa mfumo (ITL) kwa vile

Shirika halikuwa na Kompyuta aina ya Seva kwa ajili ya kufanya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo huo.

Kushindwa kuweka kompyuta yenye uwezo mkubwa wa kufanyia majaribio (Test Server) katika Shirika kunaweza kusababisha hatari ya mfumo kutofanya kazi vizuri baadae kama ilivyotarajiwa, kwa mfano kupungua kasi ya utendaji kazi (slow performance), kukosekana kwa usalama katika kanzidata ya mfumo, na vile vile mfumo kukosa ufanisi na tija kwa watumiaji kwa vile hawakushirikishwa kikamilifu katika kuthibitisha matokeo kutokana na mfumo kujaribiwa nje ya Shirika la Bima.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kuimaisha mazingira ya kufanyia majaribio "Test Environment" kwa kununua Seva itakayokuwa na uwezo mkubwa kwa ajili ya kuwezesha michakato ya kufanya majaribio ya utendaji kazi kwa mifumo itakayoanzishwa au kurekebishwa katika Shirika.

**Majibu ya Shirika la Bima Zanzibar**

Uongozi unakubaliana na hoja ya mkaguzi ya kutokuwa na sehemu ya majaribio ya mfumo ndani ya ofisi ya shirika la bima wakati wa ukaguzi. Hata hivyo, Pamoja na kutokuwa na seheme ya majaribia ya mfumo ya Shirika Kwa wakati huo, lakini Shirika liliingia katika makubaliano na mtengenezaji mfumo ya kutupatia sehememu ya majaribio (test environment) na Kwa bahati nzuri walitukubalia na kutupatia na ndio tuliotumia Kwa majaribio yote ya mfumo.

Hali hiyo ilitokea Kwa sababu ya kupunguza gharama za mfumo kwani Shirika Kwa huo lilitumia kiasi kikubwa Kwa ajili ya kununua mfumo, hivyo uongozi wa Shirika ulikubaliana kutumia sehemu ya majaribio ya mtengenezaji mfumo (vendor test environment) ili kupunguza gharama.

Kwa hali ya sasa Shirika limenunua Sehemu ya majaribio ya mifumo ya tehama (User Acceptance Test Servers) ili kila kitu kipya kinachoongezwa kwenye mfumo uliokuwepo yaani CIMIS na mifumo mengine mipya inafanyiwa majaribio humo. Hivyo tatizo hili limeshatatuliwa.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limekiri kutokea kwa dosari hii na kwasasa wameweza kuitatua kwa kuwa na sehemu maalum ya majaribio ya mifumo ya Tehama, Kamati Shirika juu ya kufuata utaratibu na miongozo mbalimbali ya Tehama inayotolewa na Wakala wa Serikali Mtandao E-Government ikiwa ni pamoja ufungaji wa mifumo katika eneo husika la mradi ili kuepusha changamoto za mfumo kutofanya kazi ipasavyo endapo utahamishwa katika eneo jengine kutokana na sababu za kimtandao.

**17.2.1.5 Kukosekana kwa Mkataba wa Msaada na Matengenezo katika mfumo wa CIMIS (Support and Maintanance Contract).**

Katika ukaguzi uliofanyika wa Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Bima (CIMIS) imebainika Shirika la Bima limeanza kuutumia mfumo huo kuanzia tarehe 01 Januari 2021 ambapo hadi sasa inakaribia miaka miwili (2) ya matumizi.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini hakukuwa na mkataba wa msaada na huduma za matengenezo ya kila mwaka uliofungwa baina ya Shirika na Mtengenezaji wa Mfumo ili kuweza kuendeleza huduma bora katika mfumo kwa kupitia msaada wa kiufundi na matengenezo yatakayotolewa na Mtengenezaji wa Mfumo.

Kutokuwepo na mkataba wa utoaji wa msaada na huduma za matengenezo kwa mfumo wa CIMIS kunaweza kupelekea kukosekana kwa maboresho ya mfumo na kutopatikana kwa ufanisi na tija katika utendaji kazi wa mfumo na

hatimae kusababisha Shirika kuingia hasara kwa kulipa gharama za ziada zisizotarajiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima kuhakikisha unachukuwa jitihada za makusudi za kuweka makubaliano ya mkataba kwa kila mwaka baina yake na Kampuni ya ITIL (Mtengenezaji wa Mfumo) kwa ajili ya upatikanaji wa huduma za msaada wa kiufundi na matengenezo ya mfumo ili kuweza kuimarisha utendaji kazi wa mfumo pamoja na kuongeza usalama wa taarifa za biashara za Bima zinazowekwa ndani ya mfumo.

**Majibu ya Shirika la Bima Zanzibar**

Tukumbuke ya kwamba, mkataba mama wa utengenezwaji wa mfumo huu umemalizika tarehe 31 Disemba, 2021. Hivyo hadi umekamilika ukaguzi huu bado shirika linatumia mkataba mama, hivyo hakukuwa na mahitaji ya kuingia kwenye mkataba mwengine wa sapoti. Kuanzia mwaka 2022, Shirika limeianza kuingia mkataba wa sapoti na kampuni ya ITL ili ikitokea kuna mahitaji ya kupata sapoti kutoka Kwao inakuwa rahisi. Lakini pia ni Kwa sababu ya uhaba wa wafanyakazi wa ICT katika Shirika, nayo ni sababu kubwa inayofanya tuingie kwenye mkataba wa sapoti

**Uchunguzi wa Kamati**

Kamati katika kufuatilia hoja hii imebaini kuwa licha ya Shirika kutumia mkataba mama ambao umewapa fursa ya kupata Msaada na Matengenezo Katika mfumo katika kipindi cha Miaka miwili lakini kulikuwa na umuhimu mkubwa wa kuwa na kifungu maalum kitakacho mtaka mkandarasi kutoa msaada wa kiufundi wakati mfumo ukiendelea kutumika katika kipindi cha majaribio, kukosekana kwa kifungu hicho kunampa mwanya mkandarasi

endapo hitilafu ikitokea asiweze kuwajibika ipasavyo katika kutoa msaada huo na hakuna hatua yoyote itakayoweza kuchukuliwa endapo asipofanya hivyo.

**Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limeshanza kuingia Mkataba wa makubaliano ya msaada wa kifundi na Kampuni ya ITL basi ni vyema pia kuimarisha kitengo cha ICT kwa kuwaajiri wafanyakazi wapya na kuwaongezea ujuzi waliopo ili kuweza kushirikiana na Kampuni katika kupata taaluma na hatimae Mfumo huo uweze kusimamiwa na kitengo husika badala ya Kampuni ya ITL ili kuweza kupunguza gharama za kuhudumia mfumo huo.

**17.2.1.6 Shirika kutumia programu za Microsoft ambazo zishapitwa na wakati na hazina usalama tena (Microsoft Windows 7 na Microsoft Office 2007)**

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Bima Zanzibar bado linaendelea kutumia programu za zamani kwenye baadhi ya kompyuta zake ambazo kwa sasa programu hizo zishapitwa na wakati na hazina usalama tena kutokana na kuwa muda wake wa matumizi umeisha.

Baadhi ya Programu hizo ni kama vile Microsoft Windows 7 Operating System ambayo imeisha muda wa matumizi tangu tarehe 14 Januari, 2020 pamoja na Microsoft Offi ce 2007 ambayo imeisha muda wa matumizi tangu tarehe 10 Oktoba, 2017. Aidha programu hizo hazipati tena maboresho ya kiusalama (security updates) kutoka kwa mtengenezaji wa programu hizo ambae ni Shirika la Microsoft la Marekani.

Kuendelea kutumia programu zilizokua zimeisha muda wa matumizi katika kompyuta za Shirika zitapelekea mfumo wa Bima kukosa usalama na kusababisha hatari (risk) ya kupotea au kuharibika kwa taarifa muhimu za

Shirika na hatimae mfumo kuweza kuvamiwa na kushambuliwa kwa urahisi na virusi, wahalifu wa mitandao (Cyber Attack) n.k.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima kwa kupitia Idara ya TEHAMA kuchukua hatua za kuingiza (install) programu za kisasa zilizokuwa salama, halisi na zenye leseni (secured, genuine and lisenced software) kama vile Microsoft Windows 10 Operating System na matoleo mapya ya Microsoft Offi ce ikiwemo Offi ce 2013, 2016, 2019 n.k

**Majibu ya Shirika la Bima Zanzibar**

Uongozi unakubaliana na hoja ya mkaguzi ya kuwa na baadhi ya computer zilizokuwa na programu za zamani kipindi hicho cha ukaguzi. Kwa wakati huo wa ukaguzi shirika lilikuwa limejikita zaidi kupata mfumo utakaotumika kuuzia bima masaa 24 popote pale duniani, pamoja na kufanya kazi nyingine za Shirika kama vile uhasibu, manunuzi, kutunza taarifa za ghala n.k. Lakini pia katika vile vilivyopewa kipaombele ni kubadilisha vitendea kazi (laptop na desktop).

Baada ya kukamilika kwa mfumo , kilichofuata ni kubadilisha vitendea kazi ili viendane na matakwa na mahitaji ya Shirika lakini pia na kasi ya ukuwaji wa technolojia ya habari na mawasiliano. Kwa hali ya sasa vitendea kazi vyetu vyote tulivonunua ni vya kileo na vimeingizwa programu mpya na za kisasa (windows 10 na 11) tena zimewekewa na leseni kwa kila mwaka. Hivyo tatizo hilo limeshatatuliwa

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limekiri kuwepo kwa dosari hiyo wakati mdhibiti alipokuwa akifanya ukaguzi wake ila kwa sasa wameshachukua hatua Kamati inaendelea kulishauri Shirika kuhakikisha wanatumia vifaa na program ambazo zinakwenda na wakati, Aidha kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kubaini

muda wa mwisho wa matumizi wa vifaa na program hizo kwa ajili ya kuviboresha zaidi (update) ili kunusu mfumo kutoshambuliwa na virusi pamoja na wahalifu wa mtandao (Cyber Attack)

**17.2.1.7 Kutofanyika kwa Tathmini ya Vihatarishi na Jaribio la kupenya katika Mtandao na Miundombinu ya Mawasiliano ya Shirika la Bima (Vulnerability Assessment and Penetration Test).** Kwa mujibu wa muongozo wa udhibiti wa viwango vya kimataifa (ISO/IEC 27000:2013 Control A.12.6.1) unahitaji Taasisi kufanya tathmini ya mara kwa mara ya kubaini vihatarishishi pamoja na kufanya majaribio ya kupenya katika mazingira ya mitandao yake ili kuweza kubaini dosari za kiusalama zilizopo katika mitandao ya shirika, miundombinu ya mawasiliano pamoja na mifumo ya Shirika na hatimae kurekebisha dosari hizo.

Ukaguzi uliangalia uwezo wa Shirika la Bima katika kukabiliana na hatari (Risk) zinazoweza kutokezea kwenye mfumo Mkuu wa Bima, mtandao pamoja na miundombinu yake ya mawasiliano.

Ukaguzi umebaini Shirika la Bima halijawahi kufanya tathmini ya kugundua vihatarishi vilivyopo vinavyoweza kuharibu mfumo wa Bima (Vulnerability Assesment) na vile vile halijawahi kufanya jaribio la kupenya (Penetration Testing) katika Mtandao na Miundombinu yake ya mawasiliano ili kubaini udhaifu uliopo na kuimarisha udhibiti wa usalama dhidi ya mashambulizi mbali mbali yanayoweza kufanyika kupitia virusi, wahalifu wa mtandao (cyber attack) n.k.

Kutokufanya tathmini ya vihatarishi vinavyoweza kuharibu mfumo na kutokufanya jaribio la kupenya katika mtandao na miundombinu iliyopo kutapelekea Shirika kushindwa kutambua hatari yoyote inayoweza kutokea

katika mfumo wa Bima na hatimae kuingia hasara kubwa ya kupoteza taarifa muhimu au kuharibiwa mfumo endapo virusi vikiingia au shambulio la mfumo likitokea.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima kupima kuandaa mpango na utaratibu maalum wa kufanya tathmini ya vihatarishi vinavyoweza kutokea katika mfumo mkuu wa bima (CIMIS) pamoja na kufanya jaribio la kupenya katika mtandao na miundombinu ya mawasiliano ili kubaini udhaifu uliopo na kuweza kudhibiti pamoja na kuimarisha maeneo yote ambayo udhaifu umejitokeza.

**Majibu ya Shirika la Bima Zanzibar**

Uongozi unakubaliana na hoja ya mkaguzi kwa kipindi hicho cha ukaguzi. Kwa hali ya sasa Shirika limeekeza kwenye miundombinu imara na ya kisasa (Sophos firewalls) Kwa ajili ya kudhibiti usalama wa mifumo ya TEHAMA na waharibifu Kwa njia za kidigitali (cyberattack).

Pia tumeanzisha utaratibu wa kila mwaka kukaguliwa Kwa kufanya majaribio ya kiusalama wa mifumo yetu ya tehama (vulnerability assessment and Penetration test ), hii inasaidi sana kuweza kuonyesha miyanya inayoweza kupelekea uharifu wa usalama wetu wa Tehama. Baada ya uchunguzi huo tunapatiwa ripoti ili kama kuna haja ya kufanya maboresho tunafanya Kwa haraka. Kwa hali ya sasa, tatizo alilolisemea Mkaguzi limeshatatuliwa na sasa hakuna tena tatizo hilo

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limekiri kuwepo kwa dosari hiyo na hatua tayari zimeshachukuliwa, Kamati inalishauri Shirika kuwa makini katika kuisimamia vyema mifumo kwa vile mifumo hiyo imebeba taarifa nyeti ambazo

zikishambuliwa au kudukuliwa na wahalifu wa Kimtandao zinaweza kupelekea hasara kwa Shirika na Serikali kwa ujumla.

**17.2.1.8 Kutokuwepo kwa Kamati Tendaji ya TEHAMA.**

Katika miaka ya karibuni, dunia imekuwa na ongezeko kubwa la kutokea kwa mabadiliko ya kimaendeleo katika mabara, nchi pamoja na miji mbali mbali ambapo mabadiliko hayo hutokezea kwa haraka kupitia Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na husababishwa kutokana na kukua kwa mahitaji mbali mbali katika taasisi zinazotoa huduma na zinazozalisha bidhaa.

TEHAMA imekuwa ni nyenzo muhimu, yenye nguvu na tija inayosaidia Taasisi katika kufanikisha mipango na malengo yake iliyojipangia ya kimkakati (strategic plans and objectives) ambapo katika hali hii Shirika/Taasisi hupaswa kutumia nyenzo ya TEHAMA kwa ufanisi mkubwa kwa lengo la kuimarisha mchakato mzima wa utendaji kazi wa taasisi pamoja na kusimamia na kudhibiti rasilimali zinazotumika katika kufanikisha malengo ya taasisi ili kuweza kufanyika kwa wakati, kwa urahisi na kwa gharama nafuu. Hivyo, matumizi ya TEHAMA katika taasisi yamekuwa ni chanzo kikubwa cha utoaji wa huduma bora, utawala bora na husababisha kupatikana kwa maendeleo endelevu kwa Serikali na wananchi kwa ujumla.

Taratibu zilizobora (best practises) zinaelekeza kwamba ni vyema Shirika/Taasisi ikaunda Kamati Tendaji ya usimamizi wa TEHAMA ili kuhakikisha mipango imara ya kimkakati ya matumizi ya TEHAMA inapangwa na njia bora zinafuatwa kwa mujibu wa sera, miongozo na sheria ili kuisaidia taasisi kufanikisha malengo makuu iliyojipangia.

Aidha, Kamati hiyo itajumuisha wajumbe mbali mbali kama vile watendaji wa ngazi za juu katika Taasisi husika, watendaji wakuu wa idara ya TEHAMA wa

taasisi pamoja na wajumbe wengine kutoka katika taasisi nyengine inapowezekana kuwepo ambapo wajumbe hao kwa pamoja wanapaswa kupatiwa Hadidu za Rejea (Terms of Reference) za vikao na kutengeneza Muongozo wa Uendeshaji wa TEHAMA kwa taasisi (ICT Steering Charter).

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Bima halina Kamati Tendaji ya TEHAMA (IT Steering Committee) ambayo ingeweza kusimamia masuala yote ya TEHAMA kwa lengo la kulisaidia Shirika katika kusimamia, kulinda na kuikuza biashara ya Bima ndani na nje ya nchi ya Tanzania kwa kutoa huduma bora kwa wateja ili kuweza kupata ongezeko la makusanyo ya fedha na hatimae Shirika kuongoza katika soko la Bima.

Kwa sasa Shirika la Bima Zanzibar lina Ofi si za mawakala (Intemediaries Agents) zenye jumla zaidi ya 175 kwa Tanzania nzima ambapo wakala hao wameunganishwa na Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Biashara za Bima (CIMIS) uliotengenezwa karibuni na hupata kutoa huduma za bima kwa wateja mbali mbali kupitia mfumo huo.

Aidha mfumo mpya wa Bima wa Shirika (CIMIS) umeunganishwa na mifumo mengine mbali mbali ikiwemo mifumo ya kibenki , mfumo wa TIRA, mifumo ya Kampuni za Simu n.k. ambapo lengo kuu la kuunganisha mifumo hiyo ni kurahisisha masuala ya malipo ya bima kwa wateja wake popote walipo. Hivyo mfumo mpya wa Usimamizi wa Bima unaonesha kwamba ni muhimu na unapaswa kusimamiwa ipasavyo.

Kutokuwepo kwa Kamati Tendaji ya TEHAMA (ICT Steering Committee) katika Shirika la Bima Zanzibar kunaweza kusababisha kuchelewa/kutotekelezwa kabisa kwa mipango mikakati ya maendeleo ya TEHAMA ya Shirika ambayo

mipango hiyo ingesaidia kukuza biashara ya Bima kupitia mfumo wake wa Usimamizi wa Bima unaotumika kwa Tanzania nzima.

Ukaguzi unashauri Shirika la Bima Zanzibar kuanzisha Kamati itakayosimamia masuala yote ya TEHAMA katika shirika (ICT Steering Committee) ili kuweza kusimamia utendaji wa mfumo mpya wa Bima na kufanikisha malengo ya Shirika yaliyojipangia.

**Majibu ya Shirika la Bima Zanzibar**

Ni kweli kabisa wakati wa ukaguzi huu Shirika halikuwa na kamati Tendaji ya Tehama. Baada ya kuona mapendekezo ya mkaguzi lakini pia kuona mahitaji katika soko la Tehama, Shirika limeunda kamati tendaji ya Tehama ikiongozwa na Mkurugenzi Muendeshaji wa Shirika la Bima la Zanzibar.

**Uchunguzi na Mapendekezo ya Kamati**

Kwa vile Shirika limeshaunda Kamati tendaji ya Tehama hata hivyo Kamati inatia shaka juu ya uundwaji wa Kamati hiyo kama umekidhi vigezo kwa vile muongozo kutoka kwa wakala wa Serikali mtandao wa kuunda Kamati hizo bado uko katika mchakato wa kutayarishwa. Hivyo basi Kamati inalishauri Shirika kuwasiliana na Wakala wa Serikali Mtandao kwa lengo la kupata msaada wa kitaalamu na namna bora ya uundaji wa Kamati Tendaji hata kama muungozo huo haujatoka rasmi.

### 17.2.1.9 Kutokuwepo kwa daftari la Kumbukumbu za Utendaji kazi wa Muuzaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Bima (absence of vendor performance logbook)

Taratibu zilizobora zinaelekeza kwamba usimamizi wa utendaji kazi wa mtengenezaji/muuzaji wa mifumo ni moja ya hatua muhimu za uchunguzi, ufuatiliaji na tathmini zinazopaswa kufanywa na mteja ili kuweza kubaini hali

halisi ya kiwango cha huduma kinachotolewa na muuzaji husika wa mfumo na kuweka katika kumbu kumbu kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Bima Zanzibar halina daftari lenye kutunza kumbu kumbu za utendaji kazi wa watengeneza mifumo (logbook). Kitabu hicho (logbook) hutunza kumbukumbu ya kila kazi na hatua anayofanya hatua ikijumisha uadilifu wake, utendaji wake, ubora wa huduma anayotoa, uzingatiaji wa muda, kiwango cha msaada wa kiufundi anachotoa pamoja na masuala mengine ya kimkataba.

Kushindwa kufuatilia utendaji wa watengeneza mifumo kama ilivyoelezwa hapo juu kunaweza kusababisha kufanyika kwa tathmini isiyo sahihi na kutoa mwanya wa kuendelea kuwapa mikataba watengeneza mifumo wanaotoa huduma kwa kiwango chini ambapo ni kinyume na matarajio ya Shirika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima Zanzibar kutekeleza utaratibu mzuri wa kukagua na kufuatilia kwa kina kiwango cha huduma kinachotolewa na wauzaji/ watengeneza mifumo ambacho kitaonyesha kwa kiasi gani wauzaji/watengeneza mifumo wamekuwa wakitekeleza wajibu wao kutokana na kupima viashiria vya utendaji muhimu (Key Performance Indicators-KPI) kwa mujibu wa viwango vya huduma (Service Level Agreement) vilivyoainishwa katika mkataba ambapo uongozi hatimae utaweza kufanya maamuzi sahihi ikiwa ni kuendelea na mtoa huduma husika au kusitisha huduma kutoka kwake baada ya kumalizika kwa mkataba kutokana na huduma aliyoitoa.

**Majibu ya Shirika la Bima Zanzibar**

Wakati wa utengenezaji wa mfumo wa CIMIS, Uongozi wa Shirika la Bima la Zanzibar katika kuhakikisha mradi wa utengenezaji mfumo wa CIMIS

unafanikiwa, uliunda kamati mbili (Project Steering committee na Project Execution committee). Project Execution committee:

Hii ni kamati ya utekelezaji wa mradi, na wajumbe wake ni watumiaji mfumo kutoka kila idara ya Shirika, Meneja wa mradi(Mshauri elekezi) baadhi ya wajumbe wa Kamati tendanji ya Shirika na wajumbe kutoka kampuni inayotengeneza mfumo.

Kamati hii ni Kwa ajili kupitia kipengele kimoja kimoja katika vipengele vilivokamilika ilikuona kama kuna tatizo lolote likafanyiwe kazi. Kamati hii vikao vyake ni kila mwezi na ripoti inawasilishwa kwenye kamati tendaji ya mradi(Project Steering Committee).

Project Steering Committee: hii ni kamati tendaji ya Mradi. Kila kilichoamuliwa kwenye kamati ya utekelezaji ya mradi ni lazima kiwasilishwe kwenye kati hii Kwa ajili ya kupata baraka za Uongozi wa Shirika.

Wajumbe wa kamati hii ni wajumbe wote wa kamati tendaji ya Shirika, Mshauri elekezi na Mjumbe kutoka Serikali mtandano. Wajumbe wote hao Kwa ujumla wao wanaangalia mafanikio ya mdadi wa kutengeneza mfumo wa kuuzia bima(CIMIS) na kumbukumbu zote za vikao zinatunzwa na Katibu wa Shirika.

Hivyo niwazi kuwa uongozi wa Shirika uliliangalia Kwa kina suala la mafanikio ya Mtengenezaji mfumo, Kwa namna nyengine tu, sio Kwa kutumia (vendor logs book).

**Uchunguzi wa Kamati**

Licha ya Shirika la Bima kukiri kutotumia utaratibu wa (absence of vendor performance logbook) katika kupima utendaji kazi wa muuzaji wa mfumo na badala yake kutumia kamati mbili ambazo ni (Project streering committee na

Project Execution Committee) hata hivyo Kamati hizo hazikuweza kufanya kazi ipasavyo kwa vile hakukuwepo na taarifa za utendaji kazi wa mkandarasi kwa kila hatua ya utengenezaji wa mfumo pamoja na kupima viashiria muhimu vya kupima ufanisi na uwajibikaji kwa muda uliopangwa, hali hiyo imepekelekea mradi huo kutomalizika kwa muda uliopangwa na baadhi ya moduli kutofanya kazi kwa usahihi kutokana na kukosa usimamizi mzuri

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati inalishauri Shirika licha ya kuunda Kamati mbili za Kusimamia utekelezaji wa mradi basi ni vyema pia kutumia daftari la Kumbukumbu za Utendaji kazi wa Muuzaji wa Mfumo (absence of vendor performance logbook) kwa vile ndio mfumo mzuri ambao unakuonesha kwa kiasi gani wauzaji wa mifumo wamekuwa wakitekeleza wajibu wao kutokana na kupima viashiria vya utendaji muhimu (Key Performance Indicators-KPI) kwa mujibu wa viwango vya huduma (Service Level Agreement) ambapo uongozi hatimae utaweza kufanya maamuzi sahihi ikiwa ni kuendelea na mtoa huduma husika au kusitisha baada ya kumalizika kwa mkataba kutokana na kiwango cha utendaji kazi wake.

**HITIMISHO**

Kamati ya LAAC ni miongoni mwa Kamati zinazosimamia masuala ya kifedha, hufanya kazi zake za ukaguzi kwa kupitia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuchunguza hoja mbali mbali zilizojitokeza katika Ripoti hizo, kufanya ziara za uchunguzi pamoja na kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika yanayojitegemea kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Toleo la 2020.

Katika kutekeleza majukumu mbalimbali kwa mujibu wa kanuni za Baraza, Kamati ya LAAC ilieleza mambo ambayo imeyabaini kupitia majibu ya Watendaji na kutoa Mapendekezo kwa Wahusika kwa lengo la kuimarisha utendaji wa Taasisi za Umma. Kwa mnasaba huo, Kamati hii inaliomba Baraza la Wawakilishi, kuipitia, kuijadili na hatimaye kuiridhia Ripoti hii kwa lengo la kufanyiwa kazi na Serikali.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati ya LAAC inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi Zinazojitegemea za SMZ na wananchi wote walioshiriki kwa namna moja au nyengine kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati hii wakati inatekeleza majukumu yake ya kikatiba. Shukurani pia ziwafikie Watendaji wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mashirikiano yao kwa Kamati hii.

Vile vile, tunatoa shukurani za pekee kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa kuiwezesha Kamati hii ili iweze kutekeleza shughuli zake kwa wepesi na kwa weledi mkubwa. Mwisho na sio mwisho kwa umuhimu, tunatoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza pamoja na Watendaji wote wa Afisi ya Baraza

hilo kwa mashirikiano yao ya dhati waliyoyaonesha katika muda wote ambao Kamati hii ilipokuwa ikiwajibika na kufanyakazi zake.